# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARIMIMIWA

## ***UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!***

# *Injili Kama Ilivyoandikwa na Paulo: Warumi*

NA DKT. BOB UTLEY,

PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI

(UTAFASILI WA BIBLIA)

*MFULULIZO WA MWONGOZO WA KUJIFUNZA FASIRI AGANO JIPYA, VOL. YA 5*

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
1998
Imepitiwa 2010

# ORODHA YA YALIYOMO


Vifupisho Vilivyotumika katika Fasiri hii ........ i

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ........ ii

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika........ iii

Fasiri:

Utangulizi wa Warumi 1........ 01

Warumi 1 ........ 06

Warumi 2 ........ 47

Warumi 3 ........ 62

Warumi 4 ........ 81

Warumi 5 ........ 93

Warumi 6 ........ 112

Warumi 7 ........ 126

Warumi 8 ........ 139

Warumi 9 ........ 169

Warumi 10 ........ 197

Warumi 11 ........ 209

Warumi 12 ........ 223

Warumi 13 ........ 241

Warumi 14 ........ 262

Warumi 15 ........ 275

Warumi 16 ........ 289

## Viambatisho

Kiambatisho cha Kwanza: Tafsiri Sahihi za Istilahi za Kisarufi za Kiyunani: .......... 304

Kiambatisho cha Pili:Uhakiki wa Kimaandiko .......... 313

Kiambatisho cha tatu:Faharasa .......... 317

Kiambatisho cha  nne: Kauli ya Kimafundisho: .......... 326

# ORODHA YA YALIYOMO: MADA MAALUM KATIKA WARUMI

Kupelekwa (*Apostellō*), 1:1 ........ 08
*Mafundisho* ya kanisa la kwanza, 1:2 ........ 10
Mwana wa Mungu, 1:3 ........ 11
Mwili (*sarx*), 1:3 ........ 13
Masihi, 1:4 ........ 14
Majina ya Uungu, 1:4 ........ 15
Amini, Tumaini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale, 1:5 ........ 19
Ubaguzi wa Bob wa ki-Uinjilisti, 1:5 ........ 22
Kuitwa, 1:6 ........ 24
Watakatifu, 1:7 ........ 25
Ubaba wa Mungu, 1:7 ........ 26
Roho (*Pneuma*) katika Agano Jipya, 1:8 ........ 28
Wokovu (Kipindi cha Agano la Kale), 1:16 ........ 31
Haki, 1:17 ........ 32
Mungu kuelezewa kama Mwanadamu (Lugha za Kibinadamu), 1:18 ........ 35
"Kweli" katika Maadiko ya Paulo, 1:18 ........ 37
Kujua, 1:19 ........ 38
Haribu, Angamiza, Vuruga (*Phtheirē*), 1:23 ........ 40
Moyo, 1:24 ........ 41
Milele (Lahaja za Kiyunani) 1:25 ........ 42
Amina, 1:25 ........ 42
Kujamiiana kwa Jinsia moja, 1:26,27 ........ 43
Uovu na Wema katika Agano Jipya, 1:29-31 ........ 45
Matumizi ya Paulo ya *Huper* ambatani, 1:30 ........ 45
Toba, 2:4 ........ 50
Ubaguzi wa ki-mbali, 2:11 ........ 53
Majivuno, 2:17 ........ 57
Lahaja za Kiyunani za "majaribio" na Vidokezo Vyake, 2:18 ........ 58
Ubatili na Utupu (*Katargeō*), 3:3 ........ 64
Utukufu, 3:23 ........ 71
Ushahidi wa Agano Jipya wa Wokovu wa Mtu, 3:24 ........ 71
Fidia /Komboa, 3:24 ........ 73
Fasihi za Ki-Mashariki, 3:27 ........ 76
Kuamini Mungu Mmoja, 3:30 ........ 78
Amini/Imani, 4:5 ........ 84
Muhuri/Lakiri, 4:11 ........ 87

Dhamana, 4:16 ........ 89
Amani, 5:1 ........ 96
Simama (*Histēmi*), 5:2 ........ 97
Uhakika, 5:2 ........ 98
Kwa nini Wakristo Huteseka?, 5:3 ........ 100
Taabu, 5:3 ........ 100
Ukuaji wa Mkristo 5:4 ........ 101
Kutawala katika Ufalme wa Mungu 5:17,18 ........ 109
Ubatizo, 6:3-4 ........ 115
Utakaso, 6:4 ........ 117
Muundo, (*Tupos*), 6:17 ........ 122
Sifa, Maombi na Shukrani za Paulo kwa Mungu, 7:25 ........ 137
Yesu na Roho, 8:9 ........ 145
Utatu, 8:11 ........ 147
Urithi wa Mwamini, 8:17 ........ 151
Mali Asili, 8:19 ........ 153
Tumaini, 8:25 ........ 157
Ustahimilivu, 8:25 ........ 157
Utu wa Roho, 8:27 ........ 160
Mzaliwa wa Kwanza, 8:29 ........ 163
Uchaguzi/Majaliwa na Hitaji la Uwiano wa Ki-thiolojia, 8:33 ........ 164
*Archē*, 8:38 ........ 167
Dhamiri, 9:1 ........ 172
Maombezi, 9:3 ........ 173
Laana (*Anathema*), 9:3 ........ 176
Israeli, 9:4 ........ 177
Agano, 9:4 ........ 179
Lugha za kibinadamu kumwelezea Mungu 9:13 ........ 183
Wema (*Hesed*), 9:15 ........ 185
Mabaki, Namna Tatu, 9:27-28 ........ 190
Majina ya Uungu, 9:29 ........ 191
Jiwe Kuu la Pembeni, 9:33 ........ 195
Kujua, 10:2 ........ 199
Kujitoa, 10:3 ........ 200
Njeo za Kiyunani Zilizotumika katika Wokovu, 10:4 ........ 201
Kutubu, 10:9 ........ 202
Jina la Bwana, 10:9 ........ 203

Nuru, 10:18 .......... 207
Ukanaji wa Imani, 11:21 .......... 217
Siri, 11:25 .......... 219
Takatifu, 12:1 .......... 225
Enzi Hii na Enzi Ijayo, 12:2 .......... 227
Kufanywa Upya, (*Anakainōsis*), 12:2 .......... 228
Mapenzi Ya Mungu (*Thelēma*), 12:2 .......... 228
Unabii wa Agano Jipya, 12:6 .......... 231
Wema, Uaminifu *(Haplotes*), 12:8 .......... 234
*Koinōnia, 12:13* .......... 237
Mamlaka, 13:1 .......... 243
Serikali za Ki-binadamu, 13:1 .......... 245
Mitizamo ya Paulo Juu ya Sheria za Musa, 13:9 .......... 250
Dokezo za Kutoka 20, 13:15,17 .......... 251
Udhaifu, 14:1 .......... 264
Je Wakristo waweza Kuhukumiana?, 14:13 .......... 269
Ufalme wa Mungu, 14:17 .......... 271
Kuadilisha, 15:2 .......... 277
Utele (*Perissevō*), 15:13 .......... 281
Njaa, 15:26 .......... 285
Wanawake katika Biblia, 16:1 .......... 291
Kanisa (*Ekklesia),* 16:1 .......... 293
Uovu Binafsi, 16:20 .......... 298
Umilele, 16:26 .......... 302

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

AB Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB Jerusalem Bible
JPSOA The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
MOF A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT Masoretic Hebrew Text
NAB New American Bible Text
NASB New American Standard Bible
NEB New English Bible
NET NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV New Revised Standard Bible
NIDOTTE New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV New International Version
NJB New Jerusalem Bible
OTPG Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB Revised English Bible
RSV Revised Standard Version
SEPT The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
TEV Today's English Version from United Bible Societies
YLT Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la ($UBS^4$). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama "Upokeaji wa Maandishi". Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
Juni 27, 1996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini niliyoupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa "uhakiki wa andiko"
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama "mwitikio wa msomaji" (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa vitu nyote lazima kweli hivi vitatu vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira

d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    1) Agano la kale
        a) Simulizi za waebrania
        b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
        c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
        d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
        a) Simulizi (Injili, matendo)
        b) Hadithi za mafumbo (Injili)
        c) Barua/nyaraka
        d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mzunguko pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mzunguko wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
    1) Mwandishi
    2) Tarehe
    3) Wapokeaji
    4) Kusudu mahsusi la uandishi
    5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
    6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafsiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mzunguko wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
    1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
    3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo

c) Itifaki
2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
1) Soma biblia
2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
3) Tangulizi za biblia
4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18

   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:

   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi
   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
   c. Habari za kisarufi
   d. Usomaji wa neno
   e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA WARUMI

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Warumi ni kitabu cha mafundisho ya Paulo chenye mantiki na kilichopangiliwa. Kiliathiriwa na matukio huko Roma, kwa hiyo, ni nyaraka za vipindi. Kuna kitu kilichotokea kusababisha Paulo kuandika waraka huu. Ingawa ni moja ya maandiko ya Paulo yasio na upendeleo, kwa njia hiyo ya Paulo ya kushughulika na tatizo (yumkini wenye wivu kati ya waumini wa Kiyahudi na viongozi wa watu wa mataifa, kama vile 14:1-15:3) ulikuwa ni uwasilishaji wa wazi wa injili na uhusishaji wa maisha ya kila siku.

B. Kitabu cha Warumi ni maendeleo ya kithiolojia ya Wagalatia. Kitabu cha Waefeso ni maendeleo ya Warumi ndani ya ufupisho wa mzunguko wa waraka. Injili ya Paulo haikubadilika lakini uwasilishaji wake ulibadilika.

C. Uwasilishaji wa injili ya Paulo katika Warumi uliathiri maisha ya kanisa kwa kila rika.
   1. Agustino aliyebadilika (okolewa) mwaka wa 386 B.K akiwa anasoma Warumi 13:13-14
   2. Uelewa wa Martin Luther kuhusu wokovu kimsingi ulibadilika mwaka wa 1513 B.K akilinganisha Zaburi 31:1 na Warumi 1:17 (kama vile Hab. 2:4)
   3. John Wesley, akitembea na mkutano wa Wamenonite jijini London mwaka wa 1738 B.K, alibadilika (okolewa) baada ya kusikia mahubiri ya Martin Luther juu ya utangulizi wa Warumi ukiwa unasomwa kwa sababu muhubiri aliyehusika hakujitokeza.

D. Kufahamu kitabu cha Warumi ni kuufahamu Ukristo. Nyaraka zilitengeza maisha na mafundisho ya Yesu kuwa kitu cha kweli ndani ya kanisa kwa rika zote. Martin Luther kakisemea "kama kiongozi cha vitabu katika Agano Jipya na injili iliyo safi.

E. Mara zote nahamasisha waumini wapya kuanza kusoma Biblia kila siku. Napendelea kuanza na vitabu vitatu katika Agano Jipya.
   1. Injili ya Yohana, kumjua Yesu.
   2. Kitabu cha Warumi, kujua mafundisho ya Yesu aliyoyatumia makanisani
   3. Yohana wa kwanza, kufahamu namna ya kuishi nje ya injili katika maisha yako ya kila siku.

## MWANDISHI

Paulo alikuwa haswa mwandishi. Salamu zake hasa zinapatikana katika 1:1. Kwa pamoja nakubali kuwa "mwiba katika mwili" wa Paulo ulitazamwa vibaya, kwa hiyo, yeye mwenyewe hakuandika waraka huu, lakini alitumia waandishi wa Tarso (kama vile 16:20)

## TAREHE

A. Yumkini tarehe ya uandishi wa kitabu cha Warumi kiliandikwa mwaka 56-58 B.K. Hiki ni moja ya vitabu vichache vya Agano Jipya ambavyo vyaweza kuwa kiusahihi. Hili limefanyika kwa kulinganisha Mdo. 20:2 na Rum. 15:17. Yumkini Warumi kiliandikwa huko Korintho ikiwa ni mwisho wa safari ya tatu ya Paulo, mara tu alipoondoka Yerusalemu.
B. Yumkini maandiko ya Paulo kuhusu matukio yakifuata F.F Bruce na Murry Harris yakiwa na marekebisho madogo

| Kitabu | Tarehe | Mahali Kilipoandikwa | Uhusiano na Mdo |
|---|---|---|---|
| 1. Wagalatia | 48 | Antiokia ya Ashuru | 14:28, 15:2 |
| 2. 1 Wathesalonike | 50 | Korintho | 18:5 |
| 3. 2 Wathesalonike | 50 | Korintho | |
| 4. 1 Wakorintho | 55 | Efeso | 19:20 |
| 5. 2 Wakorintho | 56 | Makedonia | 20:2 |
| 6. Warumi | 57 | Korintho | 20:3 |
| 7-10 Nyaraka magerezani. | | | |
| Wakolosai | mwanzoni miaka ya 60 | | |
| Waefeso | mwanzoni miaka ya 60 | | |
| Filemoni | mwanzoni miaka ya 60 | | |
| Wafilipi | mwishoni miaka ya 62-63 | | 28:30-31 |
| 11-13 safari ya nne Ya kimishionari | | | |
| 1 Timotheo | 63 (au baadaye | Makedonia | |
| Tito | 63 lakini kabla | Efeso(?) | |
| 2 Timotheo | 63 B.K 64 | Roma | |

## WAPOKEAJI

Waraka unaeleza ukomo wa safari ulikuwa kama Roma. Hatufahamu nani alikuwa mwanzilishi wa kanisa la Roma.

A. Inaweza kuwa ni baadhi ya watu waliokuwa wanatembelea Yerusalemu siku ya Pentekoste na kuzaliwa upya na kurudi nyumbani kuanzisha kanisa (kama vile Mdo. 2:10)

B. Yawezekana wakawa wanafunzi waliokimbia mateso huko Yerusalemu baada ya kifo cha Stephano (kama vile Mdo 8:4)

C. Yaweza kuwa ni wale waliozaliwa upya tokana na safari za Kimisionari za Paulo walipoitembelea Roma. Paulo kamwe hakutembelea kanisa hili, lakini alipata shauku ya kufika huko(kama vile Mdo. 19:21). Alikuwa na marafiki huko (kama vile Rum. 16)

Dhahiri mpango wake ulikuwa ni kuzuru Roma akiwa njiani kuelekea Hispania (kama vile 15:28) baada ya safari yake kwenda Yerusalem akiwa na "zawadi ya upendo". Paulo alihisi huduma yake Mashariki ya Mediterania imekwisha. Alichagua Nyanja mpya (kama vile 15:20-23,28). Mbabaji wa barua toka kwa Paulo kwenda Korinto na Roma alikuwa Phibi, shemesi, aliyekuwa akisafiri katika mwelekeo huo(kama vile Rum 16:1).

Kwa nini waraka huu, uliandikwa kwenye mitaa ya Korintho katika karne ya kwanza na mtengeneza hema wa Kiyahudi, kikiwa cha thamani Martin Luther alikiita "kitabu kikuu cha Agano Jipya na injili safi". Thamani ya kitabu hiki inapatikana katika ukweli kwamba kina maelezo ya ndani ya injili na wale waliozaliwa upya, Sauli wa Taso aliyeitwa kuwa Mtume wa watu wa mataifa. Mara nyingi nyaraka za Paulo zimerembwa kimadhubuti kabisa zikifunikwa na hali ya mahali husika, lakini sio Roma. Ni mpanglio wa uwasilishaji wa imani ya mtume.

Unatambua, wakristo wenzetu, kwamba maneno mengi ya kiufundi yanayotumika nyakati hizi kuelezea "imani"(udhihirisho, shutuma, kuasiri na utakaso) yalikuja toka Roma. Ni maendeleo ya Kithiolojia ya ukweli ya Wagalatia. Omba Mungu afungue kwako waraka huu wa ajabu tukitafuta pamoja mapenzi yake kwenye maisha yetu ya sasa.

## DHUMUNI

A. Kuomba msaada toka kanisa la Roma kwa safari yake ya Kimisionari akielekea Hispania.

B. Kuelezea tatizo katika kanisa la Roma kati ya waumini wa Kiyahudi na waumini wa watu wa mataifa. Hii yamkini ilikuwa ni matokeo ya ufukuzaji wa Wayahudi toka Roma na baadaye wakarudi. Wakati huo nafasi ya viongozi wa Kikristo wa Kiyahudi ilichukuliwa na viongozi wa Kikristo wa watu wa mataifa.

C. Kujitambulisha mwenyewe katika kanisa la Roma. Kulikuwa na upinzani mkubwa kwa Paulo toka kwa Wayahudi waaminifu waliobadilika tokea Yerusalem (kama vile baraza la Yerusalemu la Mdo. 15), na kwa Wayahudi wasio waaminifu (wasaliti toka kwenye kitabu cha Wagalatia na 2 Wakorintho 3, 10-13) na toka kwa watu wa mataifa (Wakolosai, waefeso) waliojaribu kuunganisha injili na nadharia zao pendwa au Philosofia.

D. Paulo alishutumiwa kuwa moja ya mvumbuzi hatari, akiongoza uzembe kwenye mafundisho ya Yesu. Kitabu cha Warumi ilikuwa ni njia yake mwenyewe kujitetea kimpangilio kwa kuonyesha ni jinsi gani injili ilikuwa kweli, akitumia Agano la Kale na mafundisho ya Yesu (Injili).

## MAELEZO MAFUPI

A. Utangulizi (1:1-17)
   1. Salamu (1:1-17)
      a. Mwandishi (1-5)
      b. Mahali (6-7a)
      c. Maamkizi (7b)
   2. Wakati (1:8-15)
   3. Dhamira (1:16-17)

B. Hitaji la haki ya Uungu (1:18-3:20)
   1. Kutetereka kwa ulimwengu wa watu wa mataifa (1:18-32))
   2. Unafiki wa Wayahudi au wahubiri wa kipagani (2:1-16)
   3. Hukumu ya Wayahudi (2:17-3:8)
   4. Laana ya watu wote (3:9-20)

C. Nini maana ya haki ya Uungu (3:21-8:39)
   1. Haki kwa imani pekee (3:21-31)
   2. Msingi wa haki: ahadi ya Mungu (4:1-23)
      a. Msimamo wa kweli wa Ibrahimu (4:1-5)
      b. Daudi (4:6-8)
      c. Uhusiano wa Ibrahimu na tohara (4:9-12)
      d. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu (4:13-25)
   3. Ufikiaji wa haki (5:1-21)
      a. Mtizamo dhahania: upendo usiostahili, furaha isiolinganifu (5:1-5)
      b. Msingi usio na upendeleo: upendo wa Mungu wa ajabu (5:6-11)
      c. Uainishi wa Adamu/Kristo: kosa la Adamu, utoaji wa Mungu (5:12-21)
   4. Haki ya Uungu lazima itoke kwenye haki binafsi (6:1-7:25)
      a. Kuwekwa huru toka dhambini (6:1-14)
         (1) Pingamizi lililokusudiwa (6:1-2)
         (2) Maana ya ubatizo (6:3-14)
      b. Utumwa wa shetani au utumwa wa Mungu: chaguo ni lako (6:15-23)
      c. Ndoa ya mtu katika sheria (7:1-6)
      d. Sheria ni nzuri, lakini dhambi inazuia mema (7:7-14)
      e. Mapambano ya kutenda mema na mabaya katika muumini (7:15-25)
   5. Matokeo ya kiuchunguzi ya haki za Uungu (8:1-39)
      a. Maisha katika Roho (8:1-17)

    b. Ukombozi wa uumbaji (8:18-25)
    c. Msaada endelevu wa Roho (8:26-30)
    d. Ushindi wa kimahakama wa udhihirisho kwa njia ya imani (8:31-39)

D. Kusudi la Uungu kwa watu wote (9:1-11:32)
  1. Uchaguzi wa Israeli (9:1-33)
    a. Warithi wa kweli wa imani (9:1-13)
    b. Mamlaka ya Mungu (9:14-26)
    c. Mpango wa Mungu kwa watu wote ukijuisha wapagani (9:27-33)
  2. Wokovu wa Israeli (10:1-21)
    a. Haki ya Mungu dhidi ya haki ya binadamu (10:1-13)
    b. Hitaji la huruma ya Mungu kwa wajumbe, wito wa ulimwengu (10:14-18)
    c. Mwendelezo wa Israeli kutoamini Kristo (10:19-21)
  3. Kushindwa kwa Israeli (11:1-36)
    a. Mabaki ya Wayahudi (11:1-10)
    b. Wivu wa Wayahudi (11:11-24)
    c. Upofu wa muda wa Israeli (11:25-32)
    d. Kuangua sifa kwa Paulo (11:33-36)

E. Matokeo ya zawadi ya haki ya Uungu (12:1-15:13)
  1. Wito wa kuwekwa wakfu (12:1-2)
  2. Utumiaji wa vipawa (12:3-8)
  3. Uhusiano wa waumini na waumini wengine (12:9-21)
  4. Uhusiano na serikali (13:1-7)
  5. Uhusiano na majirani (13:8-10)
  6. Uhusiano na Bwana wetu (13:11-14)
  7. Uhusiano na wajumbe wenza wa kanisa (14:1-12)
  8. Athari zetu kwa wengine (12:13-23)
  9. Uhusiano na mfanano wa Kristo 15:1-13)

F. Hitimisho (15:14-33)
  1. Mpango binafsi wa Paulo (15:14-29)
  2. Hitaji la maombi (15:30-33)

G. Taarifa za ziada (16:1-27)
  1. Salamu (16:1-24)
  2. Baraka (16:25-27)

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# WARUMI 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu | Salamu za kusalimiana | Salamu | Salaam | Mahubiri |
| 1:1-7 | 1:1-7 | 1:1-6 | 1:1 | 1:1-2 |
| | | | 1:2-6 | |
| | | | | 1:3-7 |
| | | 1:7a | 1:7a | |
| | | 1:7b | 1:7b | |
| Hamu ya Paulo Kutembelea Rumi | Hamu ya kutembelea Rumi | Shukrani | Maombi ya shukrani | Shukrani na Maombi |
| 1:8-15 | 1:8-15 | 1:8-15 | 1:8-12 | 1:8-15 |
| | | | 1:13-15 | |
| Nguvu ya Injili | Wenye haki wataishi Kwa imani | Kiini cha barua | nguvu ya injili | Dhamira yaelezewa |
| 1:16-17 | 1:16-17 | 1:16-17 | 1:16-17 | 1:16-17 |
| Kosa la mwanadamu | Ghadhabu ya Mungu | Hukumu ya Mungu Kwa wasio haki | Kosa la juu ya dhambi | Adhabu ya Mungu mwanadamu dhidi ya Wapagani |
| 1:18-23 | 1:18-32 | 1:18-23 | 1:18-23 | 1:18-23 |
| 1:24-32 | | 1:24-25 | 1:24-25 | 1:24-25 |
| | | 1:26-27 | 1:26-27 | 1:26-27 |
| | | 1:28-32 | 1:28-32 | 1:28-32 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

**Tambua kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho yameelezewa kikamilifu katika Kiambatisho cha kwanza, pili na tatu**

2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Mstari wa 1-7 unatengeneza utangulizi wa waraka. Ndio utangulizi mrefu wa nyaraka za Paulo. Alikuwa anajaribu kujitambulisha yeye mwenyewe na thiolojia yake katika makanisa ambayo hayakumjua yeye binafsi na habari za kinyume walizo zisikia kumuhusu.

B. Mstari wa 8-12 ni ufunguzi wa maombi ya shukrani. Hii ilikuwa ni tabia ya nyaraka za Kiyunani na maandishi husika ya Paulo

C. Mstari wa 16-17 ina maelezo ya dhamira ya kitabu

D. Mstari wa 18 mpaka 3:20 unatengeza fasihi ya kwanza na nukta ya kwanza ya injili ya Paulo; watu wote (makundi 3) wamepotea na wanahitaji kuokolewa(kama vile Mwa. 3)
   1. Wapagani wasio adilifu
   2. Wapagani waadilifu
   3. Wayahudi

E. Rum. 1:18-3:20 inaangazia mwanzo 3 (kwa mshangao waalimu hawalengi katika neno hili, lakini mwanzo 6, kama mwanzo wa dhambi). Binadamu aliumbwa kufanya ushirika na Mungu. kwa sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27). Ingawa, mwanadamu alichagua mwangaza na ahadi ya nguvu na uhuru. Hatimaye, mwanadamu badala ya kumwinua Mungu wakajiinua wao wenyewe (elimu ya kukana Mungu)

   Mungu aliruhusu mchafuko huu, kuwa katika sura ya Mungu ni kuhusika, kuwa na hamu ya kuwajibika, kuwa hiari kulidhia matokeo. Mungu anatenganisha watu wake kwa pamoja chaguo lake na (uhusiano wa agano). Anaruhusu kuchagua mwenyewe na madhara yake yote. Mungu anahuzunika (kama vile Mwa. 6:5-7), lakini binadamu ni mawakala adilifu wenye haki na majukumu yanayo waijia.Kurudiwa kwa kifungu cha neno "Mungu aliwapa juu ya" (kama vile 1:24,26,28) ni utambulisho wa uhuru huo, sio matakwa ya kukataliwa na Mungu. Hili halikuwa chaguo la Mungu, Hii sio dunia Mungu alioikusudia (kama vile Mwa. 3:22; 6:5-7,11-13)!

F. Ufupisho wa kithiolojia wa 1:18-3:20 unapatikana katika 3:21-31. Hii ni nukta ya kwanza ya kithiolojia ya "habari njema"ya injili-watu wote wametenda dhambi na wanahitaji msamaha wa Mungu. Mungu kwa neema anatoa njia ya ndani ya mahusiano (kama vile, uzoefu wa Edeni, linganisha mwanzo 1-2 na ufunuo 21-22)

G. Katika fasihi ya kwanza ya uwasilishaji wa injili ya Paulo inafurahisha kuona kuwa mwanadamu aliyeanguka amehusika na uasi wao na dhambi bila kuwa na marejeo kwa shetani au mapepo (kama vile Rum.1:18-3:20). Walakini kipengele hiki kinatizamisha theolojia ya mwanzo 3, lakini bila kuwa na mjaribu binafsi. Mungu hataruhusu mwanadamu aliyeanguka kumlaumu shetani tena (kama vile Mwa. 3:13) au Mungu mwenyewe (kama vile Mwa. 3:12). Wanadamu walitengenezwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa 1:26; 5:1,3; 9:6). Wana haki, nguvu na ulazima wa kuchagua. Wanawajibika katika chaguzi zao wote wakishilikishwa katika Adamu na mmoja mmoja katika dhambi binafsi (kama vile 3:23)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:1-6**
**[1]Paulo, mtumwa wa kristo yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri injili ya Mungu, [2]ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu; [3]yaani habari za mwanawe, alizaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, [4]na kuthihirishwa kwa uweza wa mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu; [5]ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake; [6]ambao katika hao ninyi mmekuwa wateule wa Yesu Kristo;**

**1:1 "Paulo"** wayahudi wengi katika zama za Paulo walikuwa na majina mawili ya mwanzo. Moja la Kiyahudi na moja la Kirumi (kama vile Mdo. 13:9). Jina la Kiyahudi la Paulo aliitwa Sauli. Yeye, kama mfalme wa zamani wa Israel, alikuwa wa kabila la Benjamini (kama vile Rum.11:1; Flp 3:5). Jina lake la kirumi ni Paulo katika Kiyunani ni (paulos), lilimaanisha "mdogo". Hili linarejewa katika

1. Urefu wa umbo lake ambao ulidokezwa katika karne ya pili kwenye vitabu vya sheria za kanisa, *matendo ya Paulo,* katika sura iliyohusu Wathesalonike waliitwa "Paulo na Tekla"
2. Uafahamu wake binafsi wa kujishusha kuwa mdogo kati ya watakatifu kwa sababu mwanzo kabisa alilitesa kanisa (kama vile 1 Kor 15:9; Efe 3:8; 1 Tim 1:15)
3. Kwa sababu ni jina alilopewa na wazazi wake wakati wa kuzaliwa.

Chaguo #3 inaelekea kuwa bora.

◙**"Mtumwa"** Tafasiri za NKJV, TEV na JB inasomeka "mtumishi." Wazo hili lilikuwa aidha ni

1. Kinyume na Yesu kama Bwana
2. Cheo cha heshima cha Agano la Kale (kama vile Musa katika Hesabu 12:7 na Yosh. 1:1; Yoshua katika Yosh. 24:29; na Daudi katika Zaburi (cheo), na Isaya 42:1, 19; 52:13)

◙
**NASB, TEV**
**NJB, REB "Kristo Yesu"**
**NKJV, NRSV "Yesu Kristo"**

"Kristo Yesu" ni zaidi ya ukawaida na kwa hiyo, yamkini ni mwanzo (kama vile MSS P[10], B). Toleo la USB[4] inatoa kiwango "B" (takribani kwa kiasi fulani).
Ingawa, kwa jinsi nyingine ina ushuhuda mzuri (kama vile MSS P[26], א, A, D, G na mababa wa makanisa ya mwanzo.
Angalia kiambatisho mbili juu ya dhana ya ukosoaji maandiko.Mara nyingi utofauti wa maandiko ni kama haya kwa mantiki kuwa hayaathiri msingi wa maana ya andiko la Kiyunani.

◙**"Kuitwa kuwa mtume"** Huu ulikuwa uchaguzi wa Mungu, na wala sio wa Paulo (kama vile Mdo. 9:15; Gal 1:15; Efe. 3:7). Kwa kifungu hiki cha maneno Paulo anaweka kando sifa zake za kiroho na mamlaka, kama alivyofanya katika Wakorintho wa kwanza 1:1; 2 Wakorintho 1:1; Wagalatia 1:1; Wafilipi 1:1; Wakolosai 1:1; 1 Tim 1:1; Tit 1:1) kwa makanisa ambayo hawakuwahi kuonana. Angalia katika maada maalumu: walioitwa kuwa 1:6.

Katika lugha ya Koine ya Kiyunani neno "mtume" katika tamaduni za Palestina ya uyahudi ilimaanisha "aliyepelekwa kama mwakilishi wa kiofisi" (kama vile 2 Kor 17:7-9). Katika Agano Jipya neno hili lilitumika katika maana mbili (1) kati ya wanafunzi maalumu kumi na wawili na Paulo na (2) katika karama za kiroho ambazo zinaendelea kanisani (kama vile 1 Kor 12:28-29; Efe. 4:11)

### MADA MAALUMU: KUPELEKWA *(apostellō)*

Hili ni neno la kiyunanila kawaida kwa "upelekwa" (yaani *apostellō*). Neno hili lina matumizi kadha ya

kithiolojia:

1. Katika kiyunani cha sasa na kwa Wayahudi waliokuwa na elimu na viongozi wa dini, neno hili hutumiwa kama moja inayoitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kiingereza chetu "Balozi". (kama vile. 2 Kor. 5:20).
2. Injili daima zinatumia kitenzi hiki kwa Yesu kutumwa na baba yake, katika Yohana, linasikika zaidi kama Masihi (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48 na hasa Yohana 5:36, 38; 6:29, 57; 7:26; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8, 18, 21,23 25; 20:21 (Yote "*apostellō*" na KISAWE CHAKE *pempō* inayotumika katika mst. 21). Inatumika kwa Yesu kutuma waumini (kama vile. Yn 17:18; 20:2121 [Yote "*apostellō* na KISAWE CHAKE ni "*pempō*" katika Yohana 20:21]).
3. Agano Jipya lilituma jina "Mtume" kwa wanafunzi
    a. Mitume kumi na wawili wa mwanzo kama mzunguko wa kwanza kati ya wanafunzi wake. (Marko 6:30; Luka 6;13; Matendo 1:2; 26)
    b. Kundi maalumu la msaada la Mitume na watumishi wenzie.
        1) Barnabasi (kama vile Matendo 14:4, 14)
        2) Andronicus na Junias (KJV, Junia , kama vile. Rum. 16:7)
        3) Appollo (kama vile. 1 Kor. 4:6-9)
        4) Yakobo ndugu wa Bwana (kama vile. Gal. 1:19)
        5) Silvanus na Timotheo (kama vile. 1 The. 2:6)
        6) Bila shaka Tito (kama vile 2 Kor. 8:23)
        7) Bila shaka Epafrodito (kama vile Waf. 2:25)
    c. Zawadi inayoendelea katika kanisa (kama vile. 1 Kor. 12:28-29; Efe 4:11)
4. Paulo anatumia cheo hiki kwa ajili yake katika barua zake nyingi kama njia ya kuonesha mamlaka yake aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo. (kama vile. Rum. 1:1 1 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; Tim. 1:1 2Tim. 1:1; Tito 1:1).
5. Tatizo tunalokumbana nalo kama waamini wa leo ni kwamba Agano Jipya halitafasiri hii zawadi inayoendelea inahusu nini au vipi inabainishwa kwa waamini. Bila shaka mtu apaswa kutofautisha kati kumi nambaili ya awali (# 3b) na matumizi ya baadaye (# 3b). Tazama Mada Maalumu: Msukumo na Mada Maalumu: Mwangaza. Kama mitume wa leo hawakusukumwa kuandika maandiko mengi matakatifu (yaani, kitabu cha Wayunani kanoni kimefungwa, kama vile. Yuda mst. 3; tazama. Mada Maalumu: kanuni ya kanisa) kisha kipi wanafanya tofauti na Manabii wa Agano Jipya na Wainjilisti (kama vile. Efe. 4:11) hapa kuna uwezekano wa mambo.
    a. Waanzilishi wa kanisa la wamisionari huanza katika maeneo yasiyo ya uinjilisti (kutumika kama vile katika *Doache*)
    b. Viongozi wa Wachungaji katika eneo Fulani au madhehebu.
    c. ?

    Napenda # 1.

◙"**Tengwa**" Hii ni KAULI TENDWA TIMILIFU YENYE HALI YA KUENDELEA ambayo inamaanisha kuwa aliyetengwa na Mungu zamani (kama vile Yer 1:15 na Gal 1:15) na hii inaendelea katika hali ya ubinadamu, yamkini huu ulikuwa ni mchezo juu ya neno la Kiaramaiki "farisayo". Waliokuwa wanatengwa na sheria za Kiyahudi (na Paulo pia [Flp 3:5] kabla ya safari yake ya kukutana na Yesu), lakini sasa alitengwa kwa ajili ya injili.

Linafanana na neno la Kiebrania "takatifu" (BDB 872), lililomaanisha "tengwa kwa ajili ya matumizi ya Kimungu" (kama vile Kut 19:6; 1 Pet 2:5). Neno "mtakatifu "takasa"na "tengwa" yote yalikuwa na mzizi wa aina moja wa lugha ya Kiyunani neno "takatifu" (*hagios*).

◙"**injili ya Mungu"** kiwakilishi *eis* katika andiko hili (na mstari 5) inaonyesha kusudi la Paulo "kuitwa" (mstari 1b) na "kutengwa (mstari 1c).

Injili ni mkusanyiko wa neno kutoka "njema" (*eu*) na "ujumbe" (*angellos*). Limekuwa ni neno ambalo linaelezea mafundisho yaliyothibitishwa katika agano jipya (kama vile Yer 31:31-34; Eze 36:21-32;) ikiendana na ahadi ya Mungu alioahidi Masihi (kama vile mistari ya 3-4) ni injili ya mwana wake (mstari 2).

Hii ni injili ya Mungu wala sio ya Paulo (kama vile 15:16; Marko 1:14; 2 Kor 11:7; 1 The. 2:2,8,9; 1 Pet 4:17). Paulo hakuwa mtu mvumbuzi au mtu wa kubadilika kitamaduni, lakini alikuwa mwenezi wa ukweli alioupokea (kama vile Mdo. 9; 1 Kor 1:18-25)

**1:2 "aliahidi kabla kupitia manabii wake katika maandiko matakatifu"** kitenzi hiki ni CHA WAKATI ELEKEZI ULIOPITA KATI USIO TIMILIFU (chenye ushahidi). Kinatumika pekee kwa maandishi ya Paulo (hapa na 2 Kor 9:5). Injili haikuwa kinyume na Mungu. Lakini umilele wake, mpango uliokusudiwa (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5; Isaya 53; Zab. 118; Marko 10:45; Luka 2:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; Tit. 1:2). Mahubiri ya mwanzo katika kitabu cha matendo (*kerygma*) kinamtambulisha Yesu kama mkamilishaji wa ahadi na nabii za kale.

Agano la Kale linatajwa katika agano jipya katika njia mbili za kawaida.

1. "Imeandikwa"(au maandishi kama vile 2 Tim 3:16, 2 Petr 3:16)
2. Maandiko

Vile vile inatajwa kuunganishwa na manabii, katika mawazo ya Wayahudi manabii ndio walioandika maandiko.

1. "Sheria au Manabii" Mt. 5:17-18 vile vile Kumbuka Luka 24:44
2. "Unabii" Luka 24:27
3. "Maandishi ya Manabii" Mt 26:56
4. "Maandishi ya Kinabii" Rum 16:26 (Rum 1:2 vile vile inataja "manabii")
5. "Unabii wa maandiko" 2 Pet 1:20

Kuna mifumo miwili ya vivumishi vya neno "takatifu" ambavyo vimeambatanishwa.

1. "Maandiko matakatifu" (ibara nzima pia inataja "manabii" Rum 1:2
2. "Maandishi matakatifu" 2Tim 3:15

## MADA MAALUMU: MAFUNDISHO YA KANISA LA MWANZO

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana "kufanana." Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti ?

Sawa, kuna njia mbili:

A. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini (kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.
B. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuviwa waliuelezea Ukristo kwenye makundi. "matamko" haya ya awali au "mafundisho" (ambacho kitabu cha matendo ni mhutasari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma.* Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:
    1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo. 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
    2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
    3. Miujiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo 2:22; 3:16; 10:38
    4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
    5. Kusurubishwa – Mdo. 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
    6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26;23
    7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo. 2:33-36; 3:13,21
    8. Atakuja tena mara ya pili – Mdo. 3:20-21
    9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo. 10:42; 17:31
    10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo. 2:17-18,33,38-39; 10:44-47

11. Mwokozi wa kila aaminiye- Mdo. 13:38-39
12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo. 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
4. Mpokee Roho – Mdo. 2:38; 10:47
5. Yote yatakujilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

**1:3 "kuhusiana na mwana wake"** Kiini cha ujumbe wa habari njema ni mtu, Yesu wa Nazareti, mwana wa Bikra Maria. Katika agano la kale, nchi, Mfalme, na Masiha waliitwa "mwana" (kama vile 2 Sam 7:14; Hos 11:1; Zab. 2:7; Mt. 2:15).

Katika agano la kale Mungu aliongea kupitia watumishi na manabii.. Yesu hakuwa mtumishi wa Mungu bali alikuwa mmoja wa familia ya Mungu (kama vile Ebr.1:1-2; 3:6; 5:8; 7:28). Cha kushangaza hii ni sehemu pekee kwenye kitabu ambapo Paulo anaangazia juu ya maisha ya Yesu. Kitabu cha Warumi hakiko katika mfumo mzima wa thiolojia.

## MADA MAALUMU: MWANA WA MUNGU

Hii ni moja kati ya nyadhifa kubwa alizopewa Yesu katika Agano Jipya. Ni wazi kabisa ina kidokezo cha Uungu. Inamjumuisha Yesu kama "Mwana" au "Mwana wangu," pia Mungu anaelezewa kama "Baba" (angalia Mada Maalumu: Ubaba wa Mungu). Linatokea mara 124 katika Agano Jipya. Hata usanifu wa Yesu mwenyewe kama "Mwana wa Adamu" ina kidokezo cha Uungu toka Dan. 7:13-14

Katika Agano la Kale usanifu wa neno "Mwana" ingalirejea kwenye makundi maalumu manne (angalia Mada Maalumu: "Wana wa……..")

A. Malaika (mara nyingi iko katika hali ya WINGI, kama vile Mwa. 6:2; Ay. 1:6; 2:1)
B. Mfalme wa Israel (kama vile2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:26-27)
C. Taifa la Israel kwa pamoja (kama vile Kut. 4:22-23; Kumb. 14:1; Hos. 11:1; Mal. 2:10)
D. Waamuzi wa Israel (kama vile Zab. 82:6)

Ni utumiaji wa mara ya pili ambao unahusianishwa na Yesu. kwa njia hii "Mwana wa Daudi" na "Mwana wa Mungu" semi zote zinahusianishwa na 2 Samwel 17; Zaburi 2 na 89. Katika Agano la Kale neno "Mwana wa Mungu" kamwe halitumiki hasa kwa Masihi, isipokuwa kama ni mfalme wa siku za kiama kama mmoja wa "wapakwa mafuta" wa Israel. Hata hivyo, katika magombo ya bahari ya chumvi wadhifa unaohusiana na Masihi ni wa kawaida (angalia nukuu maalumu katika *Dictionary of Jesus and the Gospels*, uk. 770). Pia "Mwana wa Mungu" ni wadhifa wa Kimasihi katika miingiliano miwili ya kazi za mafunuo ya Kiyahudi (kama vile II Esdras 7:28; 13:32,37,52; 14:9 na I Enoch 105:2)

Mazingira ya nyuma ya Agano Jipya kama inavyorejerea kwa Yesu kwa uzuri imefupishwa kwa namna mbali mbali.

1. Uwepo wake kabla (kama vile Yohana 1:15-30; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8)
2. Kuzaliwa kwake kwa njia ya pekee (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:23; Luk. 1:31-35)
3. Ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Mk 1:11; Luk. 3:22. Sauti ya Mungu toka mbinguni ikiunganisha

ufalme wa kifahali wa Zaburi 2 na mtumishi mwenye mateso wa Isaya

4. Majaribu ya shetani (kama vile Mt. 4:1-11; Mk 1:12,13; Luk 4:1-13. Anajaribiwa kuuwekea mashaka uwana wake au kutimiliza kusudi lake kwa njia tofauti na ile ya msalaba.
5. Uthibitisho wake na wale wakiri wasiokubalika
   a. Mapepo (kama vile Mk 1:23-25; Luk 4:31-37,41; Mk 3:11-12; 5:7; angalia Mada Maalumu: Pepo [roho wachafu])
   b. Wasioamini (kama vile Mt. 27:43; Mk 14:61; Yohana 19:7)
6. Uthibitisho wake kupitia wanafunzi wake
   a. Mt. 14:33; 16:16
   b. Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
7. Uthibitisho wake mwenyewe
   a. Mt. 11:25-27
   b. Yohana 10:36
8. Utumiaji wake wa stiari ya kawaida ya Mungu kama Baba
   a. Utumiaji wake wa neno *abba* kwa ajili ya Mungu
      1) Mk 14:36
      2) Rum 8:15
      3) Gal 4:6
   b. Utumiaji wake wa sasa wa jina Baba (*patēr*) kuelezea uhusiano wake na Uungu.

Kwa ufupi, wadhifa wa neno "Mwana wa Mungu" una maana kubwa ya kithiolojia kwa wale waliolifahamu Agano la Kale na ahadi zake, lakini waandishi wa Agano Jipya waliogopeshwa kuhusu utumiaji wao na watu wa mataifa kwa sababu ya mazingira ya nyuma ya wapagani ya "miungu" ikiwachukulia wanawake na matokea ya watoto kuwa "majitu."

◙**''Nani aliyezaliwa wa uzao wa Daudi''** Hii inahusisha utabiri wa 2 Samwel 7. Masihi alikuwa wa uzao mtukufu wa Daudi (Isa 9:7, 11:1, 10; Yer. 23:3; 30:9; 33:15) kutoka kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:4-12; Isa 65:9). Katika injili ya kitabu cha Mathayo, inakiri mara kadhaa kuwa Yesu ni wa uzao wa Daudi (kama vile 1:6; 9:27; 12:23; 15:22; 20:30; 31; 21:9; 15; 22:42), ambapo vinaonyesha matumaini ya Wayahudi kwa ujio wa Yesu kuwa ni ukombozi wa uzao wa Daudi.

Inashangaza kuwa ni kwa nini Paulo hakukazia kuhusu Yesu. Alimtaja tu hapa na katika 2 Timotheo 2:8; na yote yangeweza kuwa ni nukuu kutoka katika kanuni ya imani ya kanisa la kwanza. Juzuu toleo 3, uk.61 wa NIDNTT, linaorodhersha maandiko kadhaa ya mafundisho ya kidini ambayo yanaonyesha imani ya Kikristo/nyimbo liturujia (yaani Rum.1:3-4; 8:34; 1 Kor 15:3-4; Flp. 2:6-11; 1 Tim 3:16; 2 Tim 2:8; 1 Petro 3:18-20).

**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"kufuatana na mwili"**
**TEV** **"Kama ilivyo kwa utu wake"**
**NJB** **"Kufuatana na asili ya mwanadamu"**

Huu ulikuwa ni utimilifu na ushuhuda wa ubinadamu wa Yesu ambao daima ulikuwa unakanwa na wengi katika ulimwengu wa kidini kipindi cha karne ya kwanza (kama vile 1 Yoh1:1-4; 4:1-3). Kifungu hiki kinaonyesha wazi kuwa Paulo mara nyingi hakutumia neno hili "mwili" kwa fikra hasi. Hata hivyo kwa kawaida Paulo alitumia neno "mwili" kwa kufananisha na "roho" (kama vile 6:19; 7:5,18,25; 8:3-9,12,13; 1 Kor.5:5; 2 Kor 1:17; 11:18; Kol 2:11, 13,18,23)

Muundo huu sanifu *kata* (kufuatana na) pamoja na UHUSIKA WA KUSHUTUMU kinaenda sambamba katika kifungu no.4 . Yesu ni mwanadamu kutokana na mwili kifungu no.3 na ni Mungu kutokana na roho kifungu no 4 . Imani hii ya kuja kwa Mungu kupitia Yesu katika sura ya mwanadamu ni muhimu sana.(kama vile 1 Yoh 4:1-3 ). Inaweza pia kudhihirisha Yesu katika hali ya mwanadamu kama alivyochagua mwenyewe "mwana wa Mungu" (kama vile zab 8:4; Hez 2:1 [mtu) na Dan 7:3 [Mungu]

## MADA MAALUMU: MWILI (sarx)

Neno hili limetumiwa mara kwa mara na Paulo kwa Wagalatia na makuzi yake kithiolojia katika Warumi. Wasomi wana tofautiana juu ya namna gani dokezo la maana ya maneno haya ibainishwe. Kuna uhakika wa baadhi ya mipishano katika maana. Lifuatalo ni jaribio tu la kunukuu uwanja mpana wa maana ya neno.

A. mwili wa binadamu, Yohana 1:14; Rum. 2:28; 1 Kor. 5:5; 7:28; 2 Kor. 4:11; 7:5; 12:7; Gal. 1:16; 2:16,20; 4:13; Flp. 1:22; Kol. 1:22,24; 2:5; 1 Tim. 3:16
B. kushuka kibinadamu, Yohana 3:6; Rum. 1:3; 4:1; 9:3,5,8; 11:14; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:23,29
C. mwanadamu, Rum. 3:20; 7:5; 8:7-8; 1 Kor. 1:29; 2 Kor. 10:3; Gal. 2:16; 5:24
D. kuzungumza kibinadamu, Yohana 8:15; 1 Kor. 1:26; 2 Kor. 1:12; 5:16; 10:2; Gal. 6:12
E. udhaifu wa kibinadamu, Rum. 6:19; 7:18; 8:5-6,9; 2 Kor. 10:4; Gal. 3:3; 5:13,16,19-21; Kol. 2:18
F. ghasia ya wanadamu kumwelekea Mungu, inayohusiana na matokeo ya Anguko, Rum. 7:14; 13:14; 1 Kor. 3:1,3; Efe. 2:3; Kol. 2:18; 1 Petro. 2:11; 1 Yohana 2:16

Inasisitizwa ya kwamba "mwili" hautazamwi kama uovu katika Agano Jipya, ni katika fikira za Kiyunani. Kwa wanafalsafa wa Kiyunani "mwili" ulikuwa chanzo cha matatizo ya wanadamu; kifo kilimweka huru mtu kutoka kwenye matakwa yake. Lakini katika Agano Jipya, "mwili" ni uwanja wa mgogoro wa mapambano ya kiroho (kama vile. Efe. 6:10-18), tena usio na upande. Mwingine anaweza kutumia umbile lake la mwili kwa mazuri au mabaya.

**1:4**
**NASB, NKJV**
**NRSV, NIV “alitamka bayana”**
**TEV “alimwonyesha”**
**NJB, RSV “alimpa wadhifa”**
**NET “alimteua”**
**REB “alimtangaza”**

Hii ni KAULI TENDWA YA WAKATI ULIOPITA ENDELEVU. Mungu bila tashwishi, alimteua Yesu “mwana wa Mungu”. Hii haina maana kwamba, Bethlehemu ulikuwa mwanzo wa Yesu au yeye hana thamani kwa Babaye. Tazama mada maalumu, Utatu katika 8:11, Tazama aya ya tatu chini.

◙**“Kuwa mwana wa Mungu mwenye mamlaka”** Waandishi wa Agano Jipya hawakusema Yesu kwa nafasi yake kama “mwana wa Mungu” (kama vile Mathayo 4:3) kwa sababu ya kuhofia maana batili iliyotokana na hadithi za Wayunani (sawa na kuzaliwa kwake). Dhana ambayo huimalishwa kwa neno “pekee, wa aina yake” (kama vile Yoh. 1:8, 3:16, 18:1, 1 Yoh. 4:9). Hivyo maana yake ni “Yesu mwana wa kweli pekee wa Mungu” Tazama Mada Maalumu katika 1:13.

Agano Jipya lina nguzo mbili za kithiolojia zinazohusisha Mungu Baba, na Yesu Mwana.

1. Wote wawili ni sawa (kama vile Yoh. 1:1; 5:18; 10:30; 14:9; 20:28; 2 Kor 4:4; Efe. 2:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:3; lakini
2. Ni nafasi mbili tofauti (kama vile Marko 10:18; 14:36; 15:34)

Inawezekana Paulo alikuwa ananukuu imani ya kale ya Kikristo akirejea kwa namna tofauti, ufalme wa YHWH katika Zab 2:6,7 au 110:1 (kama vile Mdo. 2:34-36). Kwa kufanya hivyo alikuwa akikazia fungu zima “Mwana wa Mungu mwenye mamlaka” (NIDNTT uk. 79) iliyo tazama si tu kuzaliwa kwake au ubatizo bali kupaa kwake mbinguni. Ingawa, waandishi wa kuasili thiolojia za kikristo kuhusu Kristo (rejea farahasa), walichukulia mstari huu

na kuunukuu kwa malengo yao. Kwa njia ya kuhakiki tafsiri za kibiblia, yeyote aweza kufanya Biblia iseme chochote (tazama semina yangu juu ya tafsiri ya Biblia katika tovuti huru katika (www.freebiblecommentary.org)

◙**"Kwa ufufuo"** Mungu Baba anathibitisha maisha ya Yesu na ujumbe kwa kumtoa katika wafu (kama vile 4:24; 6:4; 9:8,11; Mdo. 2:31-33) Uungu (kama vile Yoh. 1:1-14; Kol. 1:15-19; Flp. 2:6-11; Ebr. 1:2-3) na ufufuo wa Yesu (kama vile 4:25; 10:9-13; 1Kor 15) ni mihimili pacha ya Ukristo.

◙Fungu hili daima lilitetea sheria ya kupinga kurithi, ambalo linadai Yesu alitunukiwa na kuinuliwa na Mungu kwa ajili ya maisha yake ya upole wa pekee. Wapinzani hawa wanasema, daima yeye hakuwepo ili aabudiwe bali aliabudiwa wakati alipofufuliwa toka katika wafu. Ingawa huu ulikuwa uongo mtupu, jambo ambalo linathitishwa na maandiko mengi kama vile Yoh. 1 na 17, kitu cha ajabu kilitunukiwa Yesu wakati wa ufufuo wake. Sio rahisi kufafanua jinsi Uuungu unaweza kuzawadiwa, hata hivyo ndivyo ilivyotokea. Ingawa Mungu aligawana utukufu wa milele na Baba yake, hadhi yake ilipanda kutokana na ukamilishaji wa hakika wa kazi yake ya ukombozi, ambayo kwayo alipewa kuitenda. Ufufuo wa Yesu ulikuwa ni kuimarisha maisha yake, mfano, mafundisho yake, kifo cha Yesu wa Nazareti kama kafara, Mungu wa Milele, mwanadamu kamili, mkombozi wa kweli, alizaliwa upya na kutolewa kama zawadi, mwana wa pekee. Tazama kiambatanisho cha tatu "kuasili"

◙

**NASB, NKJV** **"kufuatana na roho ya utakatifu"**
**NKJV** **"Kufuatana na roho ya utakatifu"**
**TEV** **"Kwa utakatifu wa Mungu"**
**NJB** **"Kwa mjibu wa roho, roho ya utakatifu"**

Tafsiri zingine huandika herufi kubwa "R" neno roho zikiwa na maana Roho Mtakatifu, na kwa herufi ndogo "r" zikimaanisha roho ya "utu" wa Yesu, kwa vile Mungu Baba ni Roho, kadhalika na Yesu pia. Maandiko ya kale ya Kiebrania na Kiyunani hayakuwa kwa herufi kubwa, wala alama, na wala sura au vifungu, kwa hiyo hizi zote zilikuwa hoja za kiasili au fasihi za wakalimani.
Kuna njia tatu za kuyatazama mafungu ya 3 na 4

1. Kama rejea kwa Yesu – asili mbili, mwanadamu na Mungu
2. Kama rejea kwa hatua mbili katika maisha yake ya kidunia, mwanadamu na Bwana aliyefufuka.
3. Kama usambamba wa "Yesu Kristo Bwana wetu"

◙**"Yesu"** Jina Yesu kwa lugha ya Kiarami ni sawa na jina Yoshua Kiebrania. Ni muungano wa maneno mawili ya Kiebrania, YHWH na Wokovu. Inaweza kumaanisha "YHWH anaokoa". "YHWH anatoa", au "YHWH ni wokovu". Nguvu ya maana ya neno hili inawezakujionyesha katika Mt. 1:21,25.

◙**"Kristo"**Hii ilikuwa ni tafasiri ya neno la Kiebrania Masihi (BDB 603), iliyomaanisha", mwenye upako". Katika Agano la Kale, makundi kadhaa ya viongozi (mitume, wachungaji na wafalme) walipakwa mafuta kama ishara ya chaguo la Mungu na uimarisho. Yesu alitimiza upako huu katika Nyanja zote tatu (kama vile Ebr. 1:2-3). Katika Agano la Kale walibashiri kuwa, Mungu angetuma mwenye upako kuongea katika enzi mpya ya utakatifu. Yesu alikuwa "mtumishi," "mwana," na "Masihi."

## MADA MAALUMU: MASIHI (toka Dan.9: 26)

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika katika kumwekea mtu mafuta maalumu kuonyesha wito wa Mungu na kumkabidhi majukumu ya uongozi.

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6, 10;2 Sam. 19:21; 23;1; Zab. 89:51; 132:10, 17; Wim. 4:20; Hab. 3:13; "Malkia mtiwa mafuta" katika Dan. 9:25)
2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani, "makuhani walitiwa mafuta," Kut. 29:7; mf. Law. 4:3, 5, 16; 6:15; 7:36; 8:12; bila shaka Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. Lilitumika kwa makasisi, na Manabii (kama vile Mwa. 26:7; 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15, iliyomaanisha watu wa Agano kwa pamoja; yumkini Hab. 3:13)
4. Lilitumika kwa manabii (kama vile. 1 Fal. 19:16; yumkini 1 Nya. 29:22)
5. Lilitumika juu ya Koreshi (kama vile. Isa. 45 :1)
6. # 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.
7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
    a. uzao wa Yuda (kama vile Mwa. 49:10)
    b. nyumba ya Yesse (kama vile 2 Sam 7)
    c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)
    d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile.Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne
2. kutambulishwa kwa "mwana Adamu" katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima kukiri kuwa hii ni mada nadra katika Agano la Kale, bila shaka Dan. 9:25. Lazima pia ifahamike kuwa Yesu haingii sana katika maelezo ya jumla kuhusu Masihi katika Agano la Kale

1. hakuwa kiongozi katika Israeli
2. hakutiwa mafuta rasmi na kuhani
3. sio kama mwokozi wa Israeli
4. sio tu "mwana wa Adamu" lakini kwa mshangao "Mwana wa Mungu"

◙**"Bwana"** katika Uyahudi jina la Agano la Mungu, YHWH, likatukuka kiasi kwamba viongozi wa dini wa Kiyahudi wakalibadili na kumwita "Bwana" (*Adoni)* wakati wanasoma maandiko ya Mungu kwa vile waliogopa wangeweza kutaja jina hilo ovyo, (kama vile Kut. 20:7; Kumb. 5:11) na hivyo kuvunja moja ya amri kumi za Mungu. Wakati waandishi wa Agano Jipya walipomwita Yesu "Bwana"(*kurios)* kitheolojia walikuwa wanathibitisha Uungu wake (kama vile Mdo. 2:36; Rum 10:9-13; Flp. 2:6-11)

## MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU.

A. *El* (BDB 42, KB 48)
    1. Maana halisi ya asili ya kale ya neno Uungu ni mashaka, ingawa wana zuoni wengi wanaamini linatokana na asili ya Akkadi "kuwa na nguvu" (Mwa 17:1; Hes 23:19; Kumb 7:21; Zab 50:1)
    2. Katika miungu ya watu wa Kanani, mungu wa juu ni *El* (kutokana na maandiko ya Ras Shamra)
    3. Katika Biblia, *El* kwa kawaida halilinganishwi na maneno mengine, muunganiko wa maneno haya ni njia ya kumwelezea Mungu.
        a. *El-Elyon* ("Mungu juu ya vyote") BDB 42 & 751 II) Mwa. 14:18-22; Kumb. 32:8, Isa 14:14
        b. *El-Roi ("*Mungu anayeona", au "Mungu anayejidhihirisha mwenyewe", BDB 424 & 909) Mwa 16:13
        c. *El-Shaddai* ("Mungu ni mkubwa" BDB 42 & 994) Mwa. 17:13; 5:11; 43:14; 49:25; Kut. 6:2)
        d. *El-Olam ("*Mungu wa milele" BDB 42 & 761), Mwa. 21:33; Neno hili kitheolojia linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, 2Sam 7:13,16
        e. *El- Berit "*Mungu wa Agano", BDB 42 & 136, Am 9:46

4. Neno *El* linalinganishwa na
    a. YHWH- katika Zab 85:8; Isa 42:5
    b. *Elohim* katika Mwa. 46:3; Ay 5:8; "mimi ndimi Mungu, Mungu wa Baba yako"
    c. *Shadai* katika Mwa. 49:25
    d. "Wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
    e. "Huruma" Kumb. 4:31; Neh. 9:31
    f. "Hofu kubwa" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan 9:4
    g. "Maarifa" katika 1Sam. 2:3
    h. "Mhifadhi" katika 2Sam 22:23
    i. "Mlipizi wangu" katika 2Sam 22:48
    j. "Mtakatifu" Isa 5:16
    k. "Mkuu" katika Isa. 10:21
    l. "Wokovu wangu" Isa 12:2
    m. "Mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
    n. Mwadhibu wa wakosefu"
5. Muunganikano wa majina yote makuu ya Mungu katika Agano la Kale yanapatikana katika Yoshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH* yamerudiwa

B. *Elyon: (BDB 751, KB 832)*
1. Maana yake ya msingi ni "juu" "ametukuzwa" au "ameinuliwa" (kama vile Mwa 40:17; 1Fal 9:8; 2Fal. 18:17; Nah. 3:25; Yer 20:2; 36:10; Zab 18:13
2. Linatumika sambamba na majina mengine ya Mungu.
    a. *Elohim* – Zab 49:1-2; 7; 3:11; 107:11
    b. *YHWH* – Mwa 14:22; 2Sam 22:14
    c. *El-Shadai,* Zab 91:1,9
    d. *El*—Hes. 24:16
    e. *Elah*- Limetumika mara nyingi katika Dan. 2-6 na Ezr 4-7, likilinganishwa na *illair* (kwa kiaramia "Mungu alioko juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Limetumika mara nyingi na wasio Waisrael
    a. *Melchizedek* – Mwa. 14:18-22
    b. *Balaam* – Hes. 24:16
    c. *Musa,* akizungumzia mataifa katika Kumb. 32:8
    d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiwaandikia watu wa mataifa, pia walitumia neno sawa la Kiyunani *Hupsistos (*kama vile 1:32, 35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja) lilitumika kimsingi katika mashairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la kale.
2. Neno hili laweza kumaanisha Mungu wa Israel, au miungu ya mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3), familia ya Abraham waliamini ya kuwa palikuwa na Mungu zaidi ya mmoja (kama vile Yosh. 24:2)
3. Inaweza kuwa na maana ya waamuzi wa Israel (kama vile Kut. 21:6; Zab 82:6)
4. Neno *Elohim* lilitumika pia kwa roho zingine (malaika, mapepo) kama katika Kumb. 32:8 (LXX) Zab 8:5; Ay. 1:6; 38:7
5. Katika Bibilia ni kichwa cha habari cha kwanza/ jina la Uungu, limetumika kipekee mpaka Mwa. 2:4 ambapo limeunganishwa na YHWH, kimsingi (kitheolojia), lina maana ya "Muumbaji" "Mdumishaji" mpaji wa maisha yote katika safari hii (kama vile Zab 104). Ni neno sawa na *El* (Kumb.32:15-19). Laweza kuwa sambamba na YHWH kama Zab 14 (*Elohim)* ni sawa kabisa kama Zab 53 (YHWH), isipokuwa katika mabadiliko ya majina ya Mungu.
6. Ingawa ni WINGI na limetumika kwa miungu mingine, neno hili daima humaanisha Mungu wa Israel, lakini kwa kawaida lina kitenzi cha umoja, kuonyesha matumizi ya Mungu mmoja.
7. Neno hili linapatikana katika midomo ya wasio Waisrael kama jina la uungu.
    a. *Melchizedek*- Mwa 14:18-22
    b. *Balaam* - Hes. 24:2

   c. *Musa,* alipozungumzia mataifa – Kumb. 32:8

8. Ni jambo lisilo la kawaida kwamba, jina la kawaida kwa Mungu wa pekee (Mungu mmoja) wa Israel limeandikwa katika wingi, ingawa hapana uhakika. Zifuatazo ni nadharia kadhaa
   a. Waebrania wana maneno mengi ya wingi ambayo daima huyatumia kwa kusisitiza jambo. Linalokaribiana na hili ni neno sanifu la Kiebrania liitwalo "wingi wa heshima", ambalo wingi umetumika kukuza dhana.
   b. Hii yaweza kurejea baraza la malaika ambalo Mungu hukutana nalo huko mbinguni kufanya mapatano (kama vile 1Fal 22:19-23; Ay 1:6; Zab 82:1; 89:5-7
   c. Inawezekana pia kwamba, hii inaonesha ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja ndani ya nafsi tatu. Katika Mwa. 1:1 Mungu aliumba, Mwa 1:2 Roho ikawa juu ya vilivyoumbwa, na kutokana na Agano Jipya Yesu ni Mungu na Baba wakala wa Babaye katika uumbaji (kama vile Yoh 1:3,10; Rum 11:36; 1Kor 8:6; Kol 1:15; Ebr 1:2; 2:10

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaonyesha uungu kama Mungu wa kufanya maagano. Mungu kama mwokozi, mkombozi. Binadamu huvunja maagano, lakini Mungu ni mwema kwa neno lake, ahadi na agano (kama vile Zab 103). Jina hili limetamkwa likiwa limeunganishwa na neno *Elohim* katika Mwa.2:4. Hakuna hoja mbili za uumbaji bali ni misisitizo miwili (1) Mungu kama muumba wa nchi (umbo) na (2) Mungu kama muumba pekee wa mwanadamu Mwa. 2:4-3:4 aanza ufunuo wa mtu, nafasi ya upendeleo na makusudi ya kumuumba mtu, kadhalika na tatizo la dhambi na uasi, iliyotokana na nafasi ya pekee aliyopewa mwanadamu.
2. Katika Mwa. 4:26 inasemekana wanadamu walianza kuita kwa jina la Bwana "YHWH". HATA HIVYO, Kut 6:3 inaonyesha watu wa kwanza walifanya maagano naye (makuhani na familia zao) walimjua Mungu kwa jina moja tu la *El- Shadai*. Jina YHWH limeelezwa mara moja tu katika Kut. 6:13-16, hasa juzuu ya 14. Hata hivyo, maandishi ya Musa daima yalitafasiri maneno kwa kuigiza na sio maneno asilia kufuatana na historian a maana zake (kama vile Mwa. 17:5; 27:36; 29:13-35), panakuwa na nadharia kadhaa kuhusiana na maana ya neno hili (imechukuliwa kutoka IDB, juzuu 2 uk. 409-11)
   a. Kutoka katika asili ya kiarabu- "kuonyesha upendo mkubwa"
   b. Kutoka katika asilli ya kiarabu- "kuvuma" (YHWH Mungu wa dhoruba)
   c. Kutoka katika asili ya wakaanani-"Kusema"
   d. Kutoka katika asili ya wafoeniki- chanzo cha utimilifu wa maana ambaye ni
   e. Mdumishaji au mwanzishaji.
   f. Kutoka katika mfumo wa waebrania wa *Qal* "yeye ambaye", "yeye aliyepo", "yeye atakayekuwepo" (wakati ujao)
   g. Kutoka katika *Hiphil* ya Kiebrania "yeye asababishae jambo liwepo"
   h. Kutoka katika chanzo cha Waebrania "kuishi" (mf. Mwa 3:20) ikimaanisha yeye aishie daima, aishie pekee.
   i. Kutoka katika rejea za kitabu cha Kut. 3:13-16, igizo kuhusu hali ya kutokamilika kutumika katika hali ya kukamilika "nitaendelea kuwa nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile nilivyowahi kuwa" (kama vile J. Wash Watts-*A Survey of Syntax in the Old Testament*, *uk.69)*. jina kamili la YHWH, daima huonyeshwa katikaufupisho au bila shaka katika asili yake.
      1) *Yah* (mf., Hallelu-yah, BDB 219, kama vile Kut 15:2; 17:16; Zab89:9; 104:35
      2) *Yahu* ("iah" umaliziaji wa majina, mf, Isaiah)
      3) *Yo ("*jo" mwanzo wa majina, mf, Yoshua au Yoeli)
3. katika Uyahudi baadaye jina hili la maagano likawa takatifu mno( jina la Kiebrania la Mungu lenye herufi nne mf. YHWH au JHVH) hivyo kwamba Wayahudi waliogopa kulisema wakihofu kuvunja amri ya Kut. 20:7; Kumb.5:11; 6:13. Kwa hivyo,wakatumia neno mbadala la Kiebrania "mmiliki" "Tajiri" "Mume" "Bwana"-*Adon* au *Adonai* (Bwana wangu). Walipokutana na neno YHWH katika kusoma maandiko ya Agano la Kale, walitamka "Bwana." Hii ndiyo maana ya YHWH inaandikwa"BWANA" katika tafasiri za Kiingereza.

4. Kama vile *El,* YHWH, daima huunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia mbalimbali za maagano ya Mungu wa Israeli. Wakati kuna miunganiko mingi ya maneno haya, hapa kuna baadhi tu:
    a. *YHWH-Yirey* (YHWH atatoa , BDB 217 & 219), Mwa. 22:14
    b. *YHWH-Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako, BDB 217 & 950, itimilifu wa *Qal)* Kut. 15:26
    c. *YHWH-Nissi* (YHWH ni Bendera yangu, BDB 217 &651), Kut. 17:16
    d. *YHWH-Meqadishkem* (YHWH yeye ambaye hutakasa, BDB 217 & 872 itimilifu wa *Piel*) Kut. 31:13
    e. *YHWH-Shalom* (YHWH ni amani, BDB 217 & 1022) Am. 6:24
    f. *YHWH-Sabbaoth* (YHWH ni wa Ukarimu, BDB 217 & 878), 1Sam.1:3,11; 4:4; 15:2; daima katika mitume.
    g. *YHWH-Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu, BDB 217 & 944 utimilifu wa *Qal),* Zab.23:1
    h. *YHWH-Sidqenu* (YHWH ni Haki yetu, BDB 217 &841, utimilifu wa *Qal),*Yer 23:6
    i. *YHWH-Shammah* (YHWH yeye yupo siku zote, BDB 217 & 1027) Hez.48:35.

**1:5 "Sisi"** Paulo hamtaji mtu yeyote katika utangulizi wake, kama vile afanyavyo daima katika nyaraka zake. Fungu hili la kwanza linarejea ubadili wa njia ya Damaskasi na uteule wake (kama vile Mdo. 9) ambavyo inamfanya mhariri kusoma kwa uhakika "sisi"

◙**"Tumepokea rehema na utume"** Paulo anathibitisha kuwa sio tu zawadi ya wokovu kupitia kwa Yesu, lakini pia kwa kuungana na hilo, nimepata wito kwa utumishi wa watu wa mataifa. Haya yote yalitokea wakati mmoja katika safari yake kwenda Damaskasi (kama vile Mdo. 9:1-22; 26:9-18). Sio tu kwa kuzawadiwa bali kwa rehema iliyokusudiwa.

Inawezekana kuwa rehema na utume vinaweza kuchukuliwa kama kitu kimoja, "zawadi ya utume"(NET angalia #13).Tafasiri zote mbalimbali zilizoorodheshwa katika *Agano Jipya katika tafasiri 26* (uk 646) inaonekana pia kama "muunganiko wa maneno mawili kuleta maana moja"

◙**"kusababisha"**Haya ni matumizi mengine ya *eis* kwa lengo la kusudi (kama vile juzuu 1). Injili inarudisha taswira ya Mungu kama mwanadamu wa imani kwa Yesu. Hii inaleta kusudi la awali la Mungu kujidhihirisha ambalo ni uhusiano wake wa karibu sana na watu konyesha alivyo (kama vile juzuu 7)

◙

**NASB, NJB "Utii wa imani**
**NKJV "Kwa ajili ya utii kwa imani**
**NSRV "kuleta utii wa imani**
**TEV "kuamini na kutii**

Haya ni matumizi ya kwanza ya neno linalotuongoza "imani" katika Kirumi (Angalia Mada Maalumu 4:5). Ilitumika katika njia kuu tatu katika sura hii na kitabu.

1. Kifungu cha 5- kinatumika kwa mambo ya ukweli na imani kuhusiana na maisha ya Kikristo kama vile Mdo. 6:7; 13:8; 14:22; 16:5; Rum. 14:1; 16:26; Gal. 1:23; 6:10; Yud. 3:20
2. Kifungu cha 8-kinatumika kwa maana ya imani binafsi kwa Yesu. Maneno ya Kiingereza "kuamini" "imani" na "amini" yote yanatafasiri neno moja la Kiyunani (*pistis/pisteuo)*. Injili ni dhana ya imani (mafundisho) pia ni kitu binafsi (kama vile juzuu 16; Yoh. 1:12;' 3:16) tazama Mada maalumu 4:5
3. Kifungu 17 kinatumika katika hali ya kuaminika na kutegemeana kufuatana na Agano la Kale. Hii ndio maana ya Hab. 2:4. katika Agano la Kale hapakuwepo na imani iliyokuwepo ya kuamini imani inayosemwa, bali mifano kwa mifano ya maisha ya imani (kama vile Ibrahimu katika Mwa. 15:6), sio imani halisi bali imani ya kutafuta (kama vile Ebr. 11). Matumaini ya wanadamu hayako katika uwezo wao wa kutenda au kuamini kwa usahihi, bali ni katika tabia ya Mungu alivyo. Ni Mungu tu ambaye ni mwaminifu (kama vile Mal. 3:6).

Kuna mlolongo wa matendo unaweza kuitwa matukio ya wokovu.

a. Toba (kama vile 2:4; Marko 1:15; Luka 13:3,5; Mdo. 3:16,19; 20:21

b. Imani (kama vile 1:16; Yoh. 1:12; 3:16; Mdo. 16:31. Ubatizo ni tamko rasmi hadharani la imani ya mtu.
c. Utii (kama vile 2:13; 2Kor 9:13; 10:5; 1 Pet. 1:2,22)
d. Uvumilivu (kama vile 2:27; Luka 18:1; 2Kor 4:1; 16; Gal 6:9; 2 The. 3:13)

Hata ndiyo masharti ya Agano Jipya. Lazima tupokee/ tuamini na tuendelee kupokea/kuamini haki zetu za Mungu kwa Yesu

## MADA MAALUMU: Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale (אמן)

I. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

A. Watu binafsi na jamii
B. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani., usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

A. Ibrahimu na uzao wake
B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

II. Asili kuu iliyotumika

A. אמן (BDB 52, KB 63)
   1. KITENZI
   a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani, 2 Fal. 10:1,5; Ester 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
   b. Shina la neno ni *phal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
      1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
      2) Kwa vitu, Isa. 22:23
      3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
   c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
      1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
      2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
      3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
      4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
      5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
      6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
   2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
   3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno "amina" katika agano la kale na agano jipya.
B. אמת (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
   1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
   2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
   3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16
C. אמונה (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu

1. Katika mikono, Kut. 17:12
2. Katika muda, Isa. 33:6
3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale

A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).

B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (אמן).

1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
   a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
   b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale

A. Petro anaunganisha

1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
3. Zab. 118:22 – 1 Petr. 2:7 (jiwe lililokataliwa)

B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka

1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
2. Isa. 61:6; 66:21
3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

Na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1 Petro. 2:5,9)

1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii

A. Utumiaji wake kwenye Agano Jpya

Neno “aaminiye" linatokana na neno la Kiyunani pisteuō ambalo pia laweza kutafasiliwa “ kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. eis inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
   a. ndani ya  jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
   b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
   c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
   d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
   e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
   f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)

g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)

2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mk 1:15; Mdo 5:14
3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti*, likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
   a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
   b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
   c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
   d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
   e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
   f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
   g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
   h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
   i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye "Mimi ndiye" (Yohana 8:24; 13:19)
   j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
   k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

V. Hitimisho

A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
   1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
   2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
   3. Utii
   4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)

B. Imani ya Kibiblia ni
   1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
   2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
   3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

   Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba "urafiki wa karibu." Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za "kifamilia" (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia "moyo mpya" na "roho mpya" inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!

   Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)

   Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

◙
**NASB "kwa jina la haki yake"**
**NKJV "kwa jina lake"**
**NRSV "kwa haki ya jina lake"**
**TEV "kwa haki ya Kristo"**
**NJB "kwa heshima ya jina lake"**

Tazama Mada Maalumu katika 10:9

◙**"utii wa imani"** Usemi sanifu wa Kiyunani ni "utii katika (*eis)*". Injili ina

1. utii wa mara moja na toba na imani
2. utii wa mtindo wa maisha wa hali ya ukristo na uvumilivu.

Injili ni zawadi ya neema lakini yenye matarajio ya matokeo. Agano Jipya ni mbadala wa Agano la Kale. Wote wanadai mwitikio wa imani na utii. Vyote vina manufaa, wajibu, na matarajio (yaani Efe. 1:4; 2:10). Hii sio haki ya kazi bali uthibitisho wa kazi zake Mungu (kama vile Yakobo, 1 Yohana). Maisha ya milele yana viashiria.

◙
**NASB, NRSV "Miongoni mwa watu wote wa mataifa"**
**NKJV "miongoni mwa mataifa yote"**
**TEV "Watu wa mataifa yote"**
**NJB "Kwa mataifa yote ya kipagani"**

Hii ni injili ya ulimwengu wote. Ahadi ya Mungu ya ukombozi katika Mwanzo 3:15 ilihusisha watu wote. Kifo chake mbadala wa kifo chetu kilijumuisha watoto wote wa Adamu walioanguka (kama vile 5:18; Yoh. 1:29; 3:16; 4:42; 6:33,51; 1 Kor. 15:22; 2 Kor. 5:19; Efe. 2:11-3:13; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tit 2:11; Ebr. 2:9; 2 Pet 3:9; 1 Yoh 2:2; 4:14). Paulo anaona wito wake maalumu wa Mungu kuwa ni kufundisha injili kwa watu wa mataifa wasio mjua Mungu (kama vile Mdo. 9:15; 22:21; 26:17; Rum. 11:13; 15:16; Gal. 1:16; 2:29; Efe. 3:2,8; 1Tim. 2:7; 2Tim. 4:17)

## MADA MAALUM: UPENDELEO WA KIINJILISTI WA BOB

Nalazimika kukubali kwako msomaji kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31), wale wote walioumbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maagano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lililojificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israeli, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaoanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israeli, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12

2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Ibrahimu ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israeli. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahimu, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israeli ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
   a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
   b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
   c. Mika 4:1-3
   d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihirishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya limejikita shabaha yake juu ya Yesu, na sio Israeli. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatima ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumaini utaendelea kuchukua muda kusoma Mada Maalum: Kwanini Ahadi za kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti sana na Ahadi za kiagano za Agano Jipya. Unaweza ukaipata mtandaoni katika wavuti www.freebiblecommentary.org.

**1:6 "Wewe pia"** Paulo alikuwa mfano madhubuti (mtesaji wa kanisa) wa neema ya Mungu, lakini wasomaji wake pia walikuwa walikuwa mifano ya wasiositahili, wasio na neema yaMungu.

**NASB, NKJV "Wenye wito wa Yesu Kristo"**
**NRSV "Wanaoitwa kuwa wa Yesu Kristo"**
**TEV "Ambaye Mungu amemwita kuwa wakeYesu Kristo"**
**NJB "Kwa wito wake amekuwa wake Yesu Kristo"**

Hii inaweza kuwa:

1. Igizo la neno "Kanisa", lililomaanisha "wale walioitwa" au "walikusanywa"
2. Rejea kwa uchaguzi wa Mungu (kama vile Rum. 8:29-30; 9:1; 1 na kuendelea; Efe. 1:4,11; 3:21; 4:1,4)
3. Chapisho la biblia la Kiingereza yenye tafasiri ya fungu "nyie mliosikia wito na kuwa wa Yesu Kristo"

Hii pia inaaksi uelewa wa tungo hii kama ilivyotafsiriwa katika matoleo ya NRSV, TEV, na JB. Angalia Mada Maalum chini

## MADA MAALUMU: KUITWA

Siku zote Mungu anachukua uwezo wa kuanzisha jambo katika mwito, uchaguzi, na akiwatafuta waumini waje kwake (kama vile. Yohana 6:44,65; 15:16; 1 Kor. 1:1-2; Efe. 1:4-5,11). Neno "kuitwa" limetumika kwa maana nyingi za kithiolojia.

A. Katika Agano la Kale "uitaji wa jina" mara nyingi ulikuwa katika mazingira ya kuabudu (kama vile. Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5).
B. Wenye dhambi wanaitwa kwenye wokovu kwa neema ya Mungu (yaani., Kut. 34:6-7) kupitia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kwa kusadikishwa na Roho ((yaani., *klētos*, kama vile Rum. 1:6-7; 9:24, ambayo kithiolojia inafanana na 1 Kor. 1:1-2 na 2 Tim. 1:9; 2 Petr. 1:10).
C. Wenye dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waokolewe (yaani., *epikaleō*, kama vile. Mdo. 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13). Maelezo haya ni nahahu ya Kiyahudi katika taratibu za kuabudu.
D. Waumini huliita jina lake nyakati za migogora na msongo wa mawazo (yaani., Mdo.7:59).
E. Waumini wameitwa kuishi maisha yanayomfanana Yesu i.e., *klēsis*, kama vile. 1 Kor. 1:26; 7:20; Efe. 4:1; Fil. 3:14; 2 The. 1:11; 2 Tim. 1:9).

Waumini wameitwa kwenye kazi ya huduma (kama vile. Mdo. 13:2; 1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:7**
**7 Kwa wote walioko Rumi, wapendwao na Mungu, walioitwa kuwa watakatifu. Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.**

**1:7 "wapendwa wa Mungu"** Usemi huu daima ulisemwa na Yesu (kama vile Mt. 3:17; 17:5). Na sasa ulikuwa unatumika na kanisa la Rumi. Hii inaonyesha undani wa upendo wa Mungu kwa wale waliomwamini mwanaye. Aina hii ya uhamisho waweza pia kuonekana katika Efe.1:20 (matendo ya Mungu kwa niaba ya Yesu) na Efe. 2:5-6 (matendo ya Yesu kwa niaba ya waaminio)

◙**"katika Rumi"** Yesu hakuanzisha kanisa hili. Hakuna ajuaye nani alianzisha (angalia utangulizi). Warumi, ilikuwa ni barua iliyomtambulisha yeye kwa kanisa lililokuwepo tayari. Kitabu cha Warumi, ni andiko la hali ya juu lililowasilishwa kuhusu mahubiri yake ya injili. Huathiliwa kidogo sana na hali ya mazingira yale ingawa palikuwa na vikwazo kidogo kati ya Wayahudi na watu wa mataifa, ambao anasema katika barua yake yote (hasa sura ya 9-11)

◙
**NASB** **"Kuitwa kama watakatifu"**
**NKJV, NRSV,**
**NJB,** **"Kuitwa kuwa watakatifu"**
**TEV,** **"Kuitwa kuwa watu wake"**

Neno "watakatifu" linarejewa kwa nafasi ya waaminio katika Kristo (Angalia Mada maalumu katika 6:4) na siyo hali yao ya kutokuwa wadhambi. Yapaswa pia lielezee hali yao endelevu ya kufanana na Kristo. Neno hili lilikuwa katika wengi isipokuwa katika Wafilipi 4:21.Hata hivyo hapa linaonekana kujumuishwa. Kuwa Mkristo ni kuwa mmjawapo wa wanajamii, familia na mwili.

Kifungu cha 1 kinaonyesha kuwa, Paulo aliitwa kuwa mtume. Waaminio ndiyo "waitwa wa Kristo" Katika kifungu cha 6. Waamini pia wanaitwa watakatifu katika kifungu cha 7. Kuitwa huku ndio njia ya Agano Jipya ya kusisitiza ukweli wa kuanzisha kipaumbele cha Mungu (tazama mada maalumu 1:6). Hakuna mwanadamu aliyeanguka katu, aliyejiita (kama vile 3:9-13; Isa.53:6; 1 Pet. 2:25). Mungu daima huchukua uamuzi (kama vile Yoh. 6:44,65; 15:16). Daima huleta maagano kwetu (Angalia Mada maalumu katika 9:4) huu ndio ukweli wa wokovu wetu. (haki au msimamo wetu halali). Lakini pia hali ya kuzawadiwa kwa utumishi wetu thabiti (kama vile Kor. 12:7,11), na maisha yetu ya ukristo (Angalia Mada Maalumu) ifuatayo:

## MADA MAALUM: WATAKATIFU (*hagios*)

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOMINO, BDB 871; KITENZI, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utatakatifu usioumbwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusianao wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)

Waamini ni "watakatifu" (*hagioi*) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vikle 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoa kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

◙**"Neema kwenu na amani kutoka kwa Mungu"** Hii ni namna ya Paulo ya ufunguzi wa Baraka. Ni neno la kuigiza toka kwa neno la asili la Kiyunani "salaamu" (*charein),* na pekee la Kikristo "neema" (*charis)*. Yawezekana, Paulo alikuwa akiunganisha ufunguzi huu Kiyunani na la salamu za asili za Kiebrania "shalom" au "amani". Hata hivyo hii ni hisia /mawazo tu.Tambua kwamba kitheolojia neema huja kabla ya amani.

◙**"kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo"** Paulo mara zote alitumia KIELEZI kimoja kwa majina yote mawili (kama vile 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:3; Gal 1:3 Efe. 1:2; Flp. 1:2; 2The. 1:2; 1 Tim 1:2; Tit 1:4). Hii ndio njia yake sanifu aliyoitumia kuunganisha watu hawa wawili katika utatu. Hii ingesisitiza hali ya Yesu ya kusujudiwa, na usawa wa Baba yake.

## MADA MAALUM: UBABA WA MUNGU

I. Agano la Kale
   A. kuna maana kuwa Mungu ni Baba kwa maana ya uumbaji.
      1. Mwa. 1:26-27
      2. Mal. 2:10
      3. Mdo. 17:28
   B. Baba ni ushabihiano uliotumika katika maana mbalimbali.
      1. baba wa Israeli (kwa kuchaguliwa)
         a. "Mwana" – Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 3:19; 31:9,20; Hosea 1:10; 11:1; Mal. 1:6
         b. "mzaliwa wa kwanza" – Yer. 31:9
      2. baba wa mfalme wa Israeli (kwa maana ya Kimasihi)
         a. 2 Sam. 7:11-16
         b. Zab. 2:7; Mdo. 13:33; Ebr. 1:5; 5:5
         c. Hosea 11:1; Mt. 2:15
      3. mshabihiano wa kuwapenda wazazi
         a. baba (stiari)
            1) abebavyo mwanae – Kumb. 1:31
            2) kumwadibisha – Kumb. 8:5; Mith. 3:12
            3) mtoaji (yaani., Kutoka) – Kumb. 32:6
            4) hatawasahau – Zab. 27:10
            5) huwapenda – Zab. 103:13
            6) rafiki/mlinzi – Yer. 3:4
            7) mponyaji/mwenye kusamehe – Yer. 3:22
            8) hukupa rehema – Yer. 31:20
            9) mfundishaji – Hosea 11:1-4
            10) mwana wa pekee – Mal. 3:17
         b. mama (stiari)
            1) hatawasahau – Zab. 27:10
            2) upendo wa mama aleaye – Isa. 49:15; 66:9-13 na Hosea 11:4 (pakiwepo na mpango wa marekebisho ya kimuktadha wa neno "nira" kwenda "mtoto mchanga")

II. Agano Jipya
   A. Utatu (maandiko yote matatu yametaja)
      1. Injili
         a. Mt. 3:16-17; 28:19
         b. Yohana 14:26
      2. Paulo
         a. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
         b. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
         c. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
         d. Gal. 4:4-6
         e. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4
         f. 1 The. 1:2-5
         g. 2 The. 2:13
         h. Tito 3:4-6
      3. Petro – 1 Pet. 1:2
      4. Yuda – Mistari ya 20-21
   B. Yesu
      1. Yesu kama "mwana apendezwaye nae" – Yohana 1:18; 3:16,18; 1 Yohana 4:9

2. Yesu kama "Mwana wa Mungu" – Mt. 4:3; 14:33; 16:16; Luka 1:32,35; Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
3. Yesu kama mpendwa – Mt. 3:17; 17:5
4. Matumizi ya Yesu ya neno *abba* kwa ajili ya Mungu – Marko 14:36
5. matumizi ya Yesu ya VIHISISHI kuonyesha vyote kuhusu Yeye na uhusiano wetu na Mungu
   a. "Baba Yangu," mf., Yohana 5:18; 10:30,33; 19:7; 20:17
   b. "Baba yako," mf., Mt. 5:16,45,48; 6:1,4,6,8,9,14,15,18,26,32; 7:11; 10:20,29; 18:14
   c. "Baba yetu," mf., Mt. 6:9,14,26

C. moja ya stiari nyingi za kifamilia kuelezea ushirika wa ndani kati ya Mungu na mwanadamu:
1. Mungu kama Baba
2. waamini kama
   a. wana wa Mungu
   b. watoto
   c. wamezaliwa na Mungu
   d. wamezaliwa mara ya pili
   e. wameasiliwa
   f. wamezaliwa
   g. familia ya Mungu

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:8-15**

8 **kwanza namshukuru Mungu wangu katika Yesu Kristo kwa ajili yenu nyote, kwa kuwa imani yenu inahubiliwa katika dunia nzima. 9 Kwa maana Mungu, nimuabuduye kwa roho yangu katika injili ya mwana wake, ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma. 10 Siku zote katika sala zangu, nikiomba nije kwenu hivi karibu, Mungu akipenda kuifanikisha safari yangu. 11 Kwa maana ninatamani sana kuwaona, nipate kuwapa karama ya rohoni, ili mfanywe imara. 12 Yaani, tufarijiane mimi na ninyi, kila mtu kwa imani ya mwenzake, yenu ya yangu. 13 lakini, ndugu zangu, sipendi msiwe na habari, ya kuwa mara nyingi nalikusudia kuja kwenu, nikazuiliwa hata sasa, ili nipate kuwa na matunda kwenu ninyi pia kama nilivyo nayo katika mataifa mengine. 14 Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima. 15 Kwa hiyo, kwa upande wangu, mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa Rumi.**

**1:8 "Kwanza"** katika upeo huu, neno "kwanza" lina maana "tangu hapo mwanzo" "lazima nianze" (J.B. Phillips)

◙**"Namshukuru Mungu wangu kupitia Yesu Kristo"** Paulo kwa kawaida alifanya maombi yake kwa Mungu kupitia kwa Yesu Kristo. Yesu ndio njia pekee ya kumfikia Mungu! Tazama mada maalumu: Maombi ya Paulo ya kumtukuza na kumshukuru Mungu katika 7:15.

◙**"kwa ajili yenu nyote"** Matumizi ya "nyote" kama mstari wa 7 inaonyesha wivu na mgogoro kati ya viongozi waumini na Wayahudi walioikimbia Roma kufuatia agizo la Nero na viongozi wa watu wa mataifa walioamini ambao walichukua nafasi ya uongozi wa Wayahudi baada ya miaka michache. Warumi 9-11 inaeleza suala hili hili. Inawezekana pia kwamba, jumuisho hili linawahusu "wanyonge" na "wenye nguvu" wa Rumi 14:1-15:13. Mungu anawapenda wote wa kanisa la Roma na anawapenda wote kwa usawa.

◙**"kwa vile imani yako inatangazwa ulimwenguni kote**" Warumi 16:19 inaonyesha kwa namna nyingine ukweli huo huo. Huu bila shaka ni usemi uliokuzwa (uliotiwa chumvi) kutoka ulimwengu wa Mashariki kwa uliomwengu wa Warumi (kama vile 1The. 1:8)

**1:9 "Mungu ni shahidi wangu"** Paulo alikuwa akila kiapo kwa jina la Mungu (kama vile 9:1; 2 Kor 1:23; 11:10-11,31; 12:19; Gal. 1:20; 1The. 2:5). Hii ndio ilikuwa njia ya Wayahudi kusema ukweli

◙
**NASB "Ni kwa vipi pasipo kukoma"**
**NKJV, NRSV "Bila kukoma"**
**NJB "Kuendelea kutaja"**
**NIV "Kwa kutobadilika"**

Dhamira ya Paulo ya maombi ya dharura yasiyobadilika (1The. 1:2; 2:13; 2 Tim 1:3), yapaswa kuwa mfano wa viongozi wa makanisa kumfuata kwa makini (kama vile 1 The. 5:17). Maombi yanafungua mlango wa nguvu ya kiroho, hatuna kwa vile hatuombi.

◙**"Katika roho yangu"** Huu ni mfano mzuri wa matumizi ya neno *hewa* kwa roho ya mwanadamu (kama vile 8:5, 10,16; 12:11) likitumika kwa maisha ya mwanadamu ( yaani "pumzi", Kiebrania *ruach,* BDB 924, kama vile Mwa. 6:17; 7:15,22)

## MADA MAALUMU: ROHO (*pneuma*) KATIKA AGANO JIPYA

Neno la Kiyunani "roho" limetumika katika njia mbali mbali kwenye Agano Jipya. Hapa kuna baadhi ya maelezo yenye upambanuzi na mifano.

A. Mungu wa Utatu (angalia Mada Maalumu: Utatu)
   1. wa Baba (kama vile Yohana 4:24)
   2. wa Mwana (kama vile Rum. 8:9-10; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11)
   3. wa Roho Mtakatifu (kama vile Marko 1:11; Mt. 3:16; 10:20; Yohana 3:5,6,8; 7:39; 14:17; Mdo. 2:4; 5:9; 8:29,35; Rum. 1:4; 8:11,16; 1 Kor. 2:4,10,11,13,14; 12:7)
B. wa nguvu ya maisha ya mwanadamu
   1. wa Yesu (kama vile Marko 8:12; Yohana 11:33,38; 13:21)
   2. wa mwanadamu (kama vile Mat. 22:43; Mdo. 7:59; 17:16; 20:22; Rum. 1:9; 8:16; 1 Kor. 2:11; 5:3-5; 7:34; 15:45; 16:18; 2 Kor. 2:13; 7:13; Flp 4:23; Kol. 2:5)
   3. mambo ambayo Roho huzalisha ndani na kupitia roho za wanadamu
      a. isio roho ya utumwa dhidi roho ya kuasili - Rum. 8:15
      b. roho ya unyenyekevu – 1 Kor. 4:21
      c. roho ya imani – 2 Kor. 4:13
      d. rohoa ya hekima na ufunuo katika maarifa Yake – Efe. 1:17
      e. isio roho ya woga dhidi ya nguvu, pendo, na heshima – 2 Tim. 1:7
      f. roho ya ukengeufu dhidi ya roho ya ukweli – 1 Yohana 4:6
C. wa ulimwengu wa kiroho
   1. viumbe vya kiroho
      a. walio wazuri (yaani, malaika, kama vile Matendo 23:8-9; Ebr. 1:14)
      b. walio waovu (yaani, pepo wabaya, kama vile Mt. 8:16; 10:1; 12:43,45; Matendo 5:16; 8:7; 16:16; 19:12-21; Efe. 6:12)
      c. pepo (kama vile Luka 24:37)
   2. roho ya utambuzi (kama vile Mt. 5:3; 26:41; Yohana 3:6; 4:23; Mdo. 18:25; 19:21; Rum. 2:29; 7:6; 8:4,10; 12:11; 1 Kor. 14:37)
   3. mambo ya kiroho (kama vile Yohana 6:63; Rum. 2:29; 8:2,5,9,15; 15:27; 1 Kor. 9:11; 14:12)
   4. karama za kiroho (kama vile 1 Kor. 12:1; 14:1)
   5. uvuvio wa Roho (kama vile Mt. 22:43; Luka 2:27; Efe. 1:17)
   6. Viungo ya kiroho (kama vile 1 Kor. 15:44-45)
D. uainishaji
   1. mtazamo wa ulimwengu (kama vile Rum. 8:15; 11:8; 1 Kor. 2:12)
   2. mchakato wanadamu wa kufikiri (kama vile Mdo 6:10; Rum. 8:6; 1 Kor. 4:2)

E. wa ulimwengu wa kimwili
    1. wingu (kama vie Mt. 7:25,27; Yohana 3:8; Mdo. 2:2)
    2. pumzi (kama vile Mdo. 17:25; 2 The. 2:8)

Ni dhahiri kwamba neno hili linapaswa kufasiriwa katika upande wa mazingira ya sasa. Kuna maana mbalimbali ya vivuli ambavyo vinaweza kurejerewa (1) ulimwengu wa kiroho; (2) ulimwengu usioonekana; (3) pamoja na watu wa ulimwengu huu wa kiroho au ulimwengu dhahiri.

Roho Mtakatifu ni sehemu ile ya Utatu ambaye ni mtendaji mkuu katika hatua hii ya historia. Enzi mpya za Roho zimekuja. Vyote vilivyo vizuri, vitakatifu, vya haki, na vinavyohusiana naye kweli kweli. Uwepo Wake, karama, na huduma ni muhimu katika ukuzaji wa injili na mafanikio ya Ufalme wa Mungu (kama vile Yohana 14 na 16). Havutii upande wake Mwenyewe, bali kwa Kristo (kama vile Yohana 16:13-14). Anasadikisha, hushawishi, hubatiza, anabatiza, na anawakomaza waamini wote (kama vile Yohana 16:8-11).

**1:10 "Wakati wote katika maombi nataja mahitaji yangu**".Paulo hakuanzisha kanisa hili lakini wakati wote aliwaombea (kama vile 2 Kor. 11:28), kama alivyofanya kwa makanisa yake yote.Tazama mada maalumu: Maombi ya upatanishi 9:3. Hata hivyo Paulo alikuwa na marafiki wengi na wafanyakazi wenzake katika makanisa ya Roma kama sura ya 6 inavyosema wazi.

◙**"kama"** Hii ni SENTESI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambayo inachukuliwa kuwa ni sahihi kufuatana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi yake kifasihi. Paulo alipanga kuitembelea Roma akiwa safarini kuelekea Hispania (kama vile 15:22-24). Huenda bila shaka hakupanga kukaa muda mrefu. Paulo wakati wote alitamani kuhudumia katika eneo jipya ambalo hakuna mwingine aliyewahi kufanya kazi hapo (kama vile. 15:20; 2 Kor. 10:15-16). Inawezekana moja ya makusudi ya barua ya Warumi iilikuwa ni kumpa fedha kwa ajili ya safari yake ya upelekwa huko Uhispania (kama vile 15:24)

◙**"kwa mapenzi ya Mungu naweza kufanikiwa kuja kwenu"** Hii inaenda sambamba katika mstari 13 na 15:32. Paulo hakujisikia kuwa maisha yake na mipango ya safari ilimhusu yeye, bali Mungu wake (kama vile Mdo. 18:21; 1 Kor. 4:19; 16:7). Tazama mada maalumu katika 12:2.

Pia, tazama kuwa mapenzi ya Mungu yaweza kuathiriwa na maombi ya waumini.

**1:11 "kwa kuwa nasubiri kuwaona"** Hii inaenda sambamba na 15:23. Kwa muda mrefu Paulo alitaka kuonana na waumini katika Rumi (kama vile Mdo. 19:21)

◙**"kwamba naweza kuwapa zawadi za kiroho"** Fungu "zawadi za kiroho"zilitimika kwa maana ya maono ya kiroho /au Baraka (11:29; 15:27). Paulo alijiona kama aliitwa pekee kuwa mtume kwa watu wa mataifa.

◙**"kwamba waweza kuenezwa"** Hiki ni KITENZIJINA TENDEWA CHA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU cha neno *histēmi.* Neno hili lina maana tatu

1. Kuanzisha, Rum. 1:11; 16:25; 1 The. 3:13; 2 Pet 1:12.
2. Imarisha, Lk. 22:32; 1The. 3:2; 2 The. 2:17; 3:3; Yak. 5:8; Ufu. 3:2
3. Nahau za Kisemiti za Kiebrania na Kiarabu kwa ajili ya kufanya maamuzi thabiti Luka 9:5

Angalia mada maalumu katika 5:2

**1:12.** Hili ni kusudi la ushirika wa Kikristo. Zawadi zinazolenga kuunganisha waumini katika huduma kwa jamii. Waumini wanazawadiwa kwa lengo zuri (kama vile 1Kor 12:7).Vipawa vyote vina maana. Vipawa vyote vinatolewa na Roho katika wokovu (cf.1Kor 12:11). Waumini wote wanaitwa, wanazawadiwa, wanahudumu muda wote (kama vile Efe. 4:11-12).Paulo anasema wazi sababu yake ya mamlaka ya utume, lakini pia kusaidiana katika jamii nzima. Waumini kila mmoja anahitaji mwenzake! Waumini ni mwili wa Kristo.

**1:13 "sitaki msijue habari za wapendwa"** Hii ni nahau anayoitumia Paulo daima katika kuleta taarifa muhimu (kama vile 11:25; 1 Kor. 10:1; 12:1; 2 Kor 1:8; 1The. 4:13). Ina maana sawa na Yesu kifasihi. "Amina, amina"

◙**"Na tumezuliwa mbali"** Hili ni tendo mpito.Fungu hili pia linatokea katika 1Thes 2:18 ambapo shetani kama wakala. Paulo aliamini maisha yake yaliongozwa na Mungu lakini yakaharibiwa na shetani. Kiasi Fulani yote ni kweli (kama vile Ayu. 1:2; Dan. 10). Matumizi ya neno hili katika 15:22 inamaanisha, kuzuiliwa kulikuwa ni kazi ya upelekwa ya Paulo Mashariki mwa eneo la Meditraniani, ambayo hadi sasa bado (lakini inakaribia).

◙**"kwamba nitapata matunda toka miongoni mwenu"** Katika mazingira haya, "tunda"linaweza kuwa sawa na watu waliobadilika, lakini katika Yoh. 15:1-8 na Gal. 5:22 ina maana ya ukomavu wa Kikristo. Mt. 7 inasema "kwa matunda yenu mtajulikana" lakini haikufafanua tunda ni nini. Fungu linaloendana vizuri pengine ni Flp. 1:22 ambapo Paulo anatumia neno hili la zao la kilimo.

**1:14 "mimi niko katika masharti"** Paulo anatumia neno hili mara kadhaa kwa Warumi.

1. Paulo ameamriwa kuhubiri injili kwa watu wote wa mataifa (hapa)
2. Paulo hajaamriwa kwa "mwili" (8:12).
3. Kanisa la watu wa mataifa limeagizwa kusaidia kanisa lao asili katika Yerusalemu (15:27).

◙**"kwa Wayunani"** Hii ina maana kwa watu waliostarabika, waadilifu wanaozunguka bahari ya Mediteraniani. Alexander mkuu na wafusi wake walikuwa wameeneza utamaduni wa Kiyunani katika ulimwengu uliojulikana. Warumi walikuwa tayari wamejifunza utamaduni wa Wayunani.

◙**"Kwa washenzi wasiostarabika"** Hili neno (*onomatopoeia)* lilimaanisha makundi ya watu wasio na elimu au wasio sitarabika, mara nyingi upande wa Kaskazini. Lilitumika kwa watu wasio zungumza Kiyunani. Kuzungumza kwao walitamka kwa sauti kama "bar bar bar" kwa Wayunani na Warumi.

◙**"kwa werevu na wapumbavu"** Inawezekana haya yalikuwa sawia/ sambamba na maandiko ya Kiyunani kwa "wasiositarabika", lakini sio lazima iwe hivyo. Inawezekana ilikuwa njia ya kuwasema watu wa makundi yote na watu binafsi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:16-17**
**[16]Kwa maana siionei injili haya; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. [17]Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.**

**1:16-17** Vifungu vya 16-17 ni dhima ya kitabu kizima. Dhima hii imekuwa na kufupishwa katika 3:21-31.

**1:16**
**NASB, NRSV "Mimi siionei haya injili"**
**NKJV "Mimi siionei haya injili ya Kristo"**
**TEV "Ninjiamini kabisa katika injili"**
**NJB "Mimi siionei haya habari njema"**

Paulo anamsema Yesu kwa aina mbalimbali katika Marko 8:38 na Luka 9:26. Haoni aibu kwa yale yaliyomo katika injili au matokeo ya kuteswa kwake (kama vile 2 Tim 1:12,16,18).

Katika 1Kor. 1:23, Wayahudi waliionea haya injili iliyohubiriwa kwa vile ilimuimalisha Masihi aliyeteswa na Wayunani kwa vile iliimarisha ufufuko wa mwili.

◙**"Wokovu"** Katika Agano la Kale, neno la Kiebrania (*yasho)* kimsingi lilimaanisha kukombolewa kwa mwili (kama vile Yak. 5:15). Lakini katika Agano Jipya neno la Kiyunani (*sōzō)* kimsingi lina maana ya kukombolewa kiroho (kama vile 1 Kor 1:18,21). Tazama Robert B. Girdleston, *Synonyms of the Old Testament,* uk. 124-126.

## MADA MAALUM: WOKOVU (Neno la AGANO LA KALE)

Neno hili (BDB 447, KB 446, zote NOMINO JINSI YA KIKE NA KIUME), ambazo kimsingi humaanisha "pana na yenye nafasi kubwa" au "kuwa huru," lina vidokezo mbalimbali.

1. usalama, 2 Sam. 22:3; Ayubu 5:11; Zab. 12:5
2. ustawi, mafanikio, Ayubu 30:15
3. wokovu wa Kiungu wenye kujumuisha wokovu wa kimwili na kiroho
   a. Mwa. 49:18
   b. Kumb. 32:15
   c. 2 Sam. 23:5
   d. Zab. 3:2,8; 22:1; 35:3; 62:2; 69:29; 70:5; 78:22; 80:3; 89:26; 91:16; 106:4; 140:7
   e. Isa. 12:2; 33:2; 51:6,8; 52:7,10; 56:1; 59:11; 60:18; 62:1,11
4. wazo la ukombozi wa kiroho na kimwili kwa wazi unaonekana katika Yona 2:9-10
5. ushindi, Kut. 14:30; 15:2; 1 Sam. 14:45; Zab. 20:6; 21:5; 44:4-5; 68:19-20; 118:14,15,21; Isa. 12:2; Hab. 3:8
6. mara nyingi neno "furahini" linahusiana na wokovu wa YHWH, 1 Sam. 2:1; Isa. 25:9; 26:1; Zab. 9:14; 13:5; 21:1; 35:9; 118:15,21

Wokovu unahusisha uanzishaji wa ushirika wa mwanzo wa YHWH uliokusudiwa na jamii ya wanadamu. Inajumuisha ujumla wa kibinafsi na kijamii!

◙

**NASB "Kwa yeyote aaminiye"**
**NKJV "Kwa ajili ya kila aaminiye"**
**NRSV "Kila mmoja aliye na imani"**
**TEV "Wote waaminio"**
**NJB "Wote wenye imani"**

Injili ni kwa wanadamu (ninapendaje maneno "kila mmoja ", "yeyote awaye", "wote" angalia dokezo katika 1:15 kipengele cha sita). Lakini kuamini ni moja ya masharti ya kupokelewa (kama vile Mdo. 16:30-31). Lingine ni toba (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16 na 19; 20:21). Mungu anashughulika na wanadamu kwa njia ya ahadi (tazama mada maalumu katika 9:14). Daima anachukua hatua na kuweka hoja (kama vile Yoh. 6:44,65). Lakini pana masharti kadhaa kati yao (angalia dokezo katika 1:15 kipengele cha 4)

Neno la Kiyunani lililotafasiriwa hapa "kuamini" laweza kutafasiriwa kwa lugha ya kiingreza"imani" au "kuamini". Neno la Kiyunani lina maana za nyongeza nyingi kuliko neno lolote lile la Kiingereza. Tazama, ni HALI YA KUENDELEA YA WAKATI ULIOPO. Huduma ya imani, ni imani enderevu (kama vile 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15; 1 The. 4:14, angalia Mada maalumu katika 10:4).

Awali, neno la Kiebrania lililohusika karibu na neno la Kiyunani "imani" lilimaanisha "kusimama imara bila kuyumba au kuyumbishwa". Kinyume cha sitiali ya Agano la Kale lingekuwa "miguu yangu ilikuwa kwenye tope jekundu" (Zab. 40:2) "miguu yangu karibu iteleze" (Zab. 73:2). Maneno yenye asili ya Kiebrania *'emun', emunah, aman* yalikuja kutumika kwa njia mbalimbali kuelezea mtu mwema, mwaminifu na anayetegemewa. Kuhudumia imani haina maana ya mwanadamu aliyeanguka kutokuwa na uwezo wa kuwa mwaminifu, lakini, Mungu ni mwaminifu. Matumaini ya waaminio hayamo ndani ya uwezo wao bali katika hali ya Mungu na ahadi zake. Angalia Mada maalumu katika 1:15

◙**"kwa Wayahudi kwanza"** Sababu ya hili limejadiliwa kwa ufupi katika 2:9-10 na 3:1-20 na kuendelezwa zaidi katika sura ya 9-11. Inafuatia maneno ya Yesu katika Mt. 10:6; 15:24; Marko 7:27; Yoh. 4:22.

Hii inaweza kuhusisha wivu kati ya Wayahudi waaminio na viongozi wa watu wa mataifa katika kanisa la Rumi.

**1:17 "uadilifu wa Mungu"** Usemi huu katika eneo hili linarejea (1) tabia ya Mungu na, (2) na kwa vipi anaitumia tabia hiyo kwa wanadamu wenye dhambi. Tafasiri ya Biblia ya Jerusalem Bible (JB) inasema "hii ndio inabainisha

haki ya Mungu". Wakati hii haihusishi mwenendo wa maisha ya binadamu kitabia, kimsingi inahusisha msimamo wake mbele ya hakimu wa haki. Kuhusishwa huku kwa haki ya Mungu na wanadamu walioanguka, wenye dhambi tangu matengenezo, imeweka bayana "haki kwa rehema kupitia imani" (kama vile 2Kor 5:21, Flp. 3:9). Huu ndio hasa mstari uliobadilisha maisha ya Martin Luther na theolojia.

Hatahivyo, lengo langu la kuhalalisha haki ni utakaso, ufanano na Kristo au tabia ya Mungu ya haki (kama vile Rum. 8:28-29, Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10; 4:13; 1The. 3:13, 4:3; 1 Pet 1:15). Haki, sio tu tamshi la kisheria, ni wito kwa maisha ya utakatifu. Taswira ya Mungu katika mwanadamu ni kule kubadilika kwake (kama vile 2 Kor. 5:21)

## MADA MAALUMU: HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana.Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsia ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsia ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii anatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wawili halisi walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21). Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya aagano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, mahakama ya haki)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kusingiziwa)
3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii wa mtindo wa maisha
4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, iliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa rabbi aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili

kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii) na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakatholiki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu wa Edeni. Biblia inaanza kati Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (cf. Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
    a. Warumi 3:26
    b. 2 Wathesalonike 1:5-6
    c. 2 Timotheo 4:8
    d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
    a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    b. Mathayo 27:19
    c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki. Mambo ya Walawi 19:2
    a. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
    a. Warumi 3:21-31
    b. Warumi 4
    c. Warumi 5:6-11
    d. Wagalatia 3:6-14
5. Iliyotolewa na Mungu
    a. Warumi 3:24; 6:23
    b. 1 Wakorintho 1:30
    c. Waefeso 2:8-9
6. Iliyopokelewa kwa imani
    a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
    b. 2 Wakorintho 5:7,21
7. kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11
8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23

c. Waefeso 1:4; 2:10
d. 1 Timotheo 6:11
e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
f. 1 Yohana3:7
g. 1 Petro 2:24

9. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
   a. Matendo 17:31
   b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

1. agizo la Mungu
2. zawadi ya Mungu
3. tendo la Kristo
4. maisha yapasayo kuyaishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana Naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na Barua Zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa na kipengele cha kuachiliwa. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
2. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

◙

**NASB, NKJV** **"kutoka imani hadi imani"**
**NRSV** **"Kupitia imani hadi imani"**
**TEV** **"Ni kupitia imani toka mwanzo hadi mwisho"**
**NJB** **"Inaonyesha ni kwa vipi imani inakuongoza kufikia imani"**

Kifungu hiki cha maneno kina VIELEZI viwili, *ek* na *eis*, ambavyo vinaonyesha mpito au maendeleo. Alitumia umbo lile lile katika 2 Kor 2:16 na *apo* na *eis* katika 2 Kor 3:18. Ukiristo ni zawadi amboyo inategemewa kuwa tabia na mpangilio wa maisha.

Kuna uwezekano wa aina mbalimbali wa kuweza kukitafasiri kifungu hiki. (agano jipya la Wiliam) linatafasiri ya kuwa "ni njia ya imani inayokuongoza kufikia imani kubwa". Wazo kuu la kithiolojia ni kuwa

1. Imani inatokana na Mungu (imefunuliwa)
2. Mwanadamu ni lazima aitike na aendelee kuitikia
3. Imani ni lazima itokane na maisha ya kimungu

Kwa yakini kitu kimoja dhahiri "imani katika Kristo ni muhimu" (kama vile 5:1; Flp. 3:9). Ahadi ya Mungu ya wokovu imefungamanishwa juu ya mwitiko wa imani (kama vile Marko 1:15, Yoh. 1:12, 3:16, Mdo. 3:16 na 19, 20:21) angalia Mada Maalumu katika 1:5; 4:5 na 10:4

◙

**NASB** **"lakini mtu mwenye haki ataishi kwa imani"**
**NKJV** **"wenye haki wataishi kwa imani"**

**NRSV** **"yeye aliye na haki ataishi kwa imani"**
**TEV** **"aliyewekwa kuume na Mungu kupitia imani ataishi"**
**NJB** **"mtu aliyesimama atapata maisha kupitia imani"**

Hii ilikuwa dondoo kutoka Hab. 2:4 na sio kutoka katika andiko la Kiebrania la karne ya 8 (MT) au toleo la Tafsiri ya Agano la kale la Kiyunani (LXX). Katika agano la kale "imani" ilikuwa na maana pana ya sitiari ya neno "mdhamini" "uaminifu" au "mtiifu" (angalia Mada maalumu katika 1:5). Kuitumikia imani kumesimama juu ya uaminifu wa Mungu (kama vile 3:5, 21,22,25,26). Ingawa, uaminifu wa mtu ni kielelezo ya kuwa mmoja ameamini katika utoaji wa Mungu. Andiko lile lile katika agano la kale limenukuliwa katika Gal. 3:11 na Ebr. 10:38, fasihi tanzu inayofuata Warumi 1:18-3:20, inaonyesha kinyume cha uaminifu kwa Mungu. Inaweza kukusudia kuonyesha ni kwa vipi watoa maoni mbali mbali wa kisasa wanaelewa sehemu ya mwisho ya kifungu hiki.

1. Vaughan: "anza katika imani na umalizie katika imani"
2. Hodge: "kwa imani pekee"
3. Barrett: "pasipo juu ya kitu chochote lakini imani"
4. Knox: "imani mwanzo na mwisho"
5. Stagg: "waliosimama nje ya imani wataishi"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:18-23**
**[18] kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa mwanadamu waipingao kweli kwa uovu.[19] kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia.[20] kwa sababu mambo yake yasioonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru; [21] kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. [22] wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; [23] wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo.**

**1:18 "Kwa ajili ya"** Tazama ni mara ngapi *"gar"* imetumika katika dhamira ya fungu katika mstari wa 16-17- mara tatu, na sasa inaleta wazo la injili ya Paulo (1:18-3:31), ambalo linatofautiana kwa nguvu ya Mungu katika wokovu.

◙**"Hasira ya Mungu"** Mstari 18-23 inatoa picha ya ulimwengu wa wapagani wa enzi za Paulo. Udhihirisho wa ulimwengu wa wapagani pia unapatikana katika fasihi za Kiyahudi (kama vile hekima za Sulemani 13:11 na barua ya Aristeas, 134-38) na hata maandiko ya Kiyunani na Kirumi. Biblia ile ile inayotuambia kuwa Mungu ni upendo vile vile inadhirisha ghadhabu yake (kama vile mistari ya 23-32; 2:5,8; 3:5; 4:15; 5:9; 9:22; 12:19; 13:4-5).

Ghadhabu na upendo ni maneno ya kibinadamu yanayotumika na Mungu. Yanaelezea ukweli kuwa Mungu anayo njia ya kuwataka waamini wote kujongea kwake na waishi. Matakwa ya mtu ya kukataa mapenzi ya Mungu (injili ya Kristo) itasababisha madhara ya muda, kama ilivyo katika kifungu hiki, na theolojia ya kifo na hukumu (kama vile 2:5). Hata hivyo, Mungu asiangaliwe kama mlipiza kisasi. Hukumu ni "kazi yake ngeni" (kama vile Isa 28:2 na kuendelea), upendo ni tabia yake, linganisha Kumb. 5:9 na 5:10; 7:9. Katika yeye, haki na rehema vinatawala. Bado watu wote watatoa hesabu zao kwa Mungu (kama vile Wimb. 12:13-14; Gal 6:7), hata Wakristo (kama vile 14:10-12; 2 Kor 5:10)**.**

## MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UUNGU

I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
   A. Viungo vya mwili
      1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
      2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
      3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15

4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22

B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6

C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19

D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
1. Baba
   a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
   b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
   c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!

B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)

C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)

D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible,* ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika The International Standard Bible Encyclopaedia, kurasa za. 152-154

◙**"anajidhihirisha"** Kwa vile injili ni ukweli ulio dhahiri (mstari wa 17) vivyo hivyo - hasira ya Mungu. Huu sio uvumbuzi wa mwanadamu wala busara yeyote ile.

◙**"wanaoficha ukweli"**- Hii inahusu kukataa kwa makundi, sio ujinga (kama vile Mistari ya 21, 32; Yoh. 3:17-21). Fungu hili laweza kumaanisha;

1. Wanaujua ukweli bali wanaukataa
2. Mwenendo wao wa maisha unaonyesha wanavyo ukataa ukweli

3. Maisha yao/ maneno yao yanawafanya wengine wasijue wala kupokea ukweli

## MADA MAALUM: "KWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO

Matumizi ya Paulo ya neno hili na muundo wake wenye uhusianao yanatokana na usawa wake wa Agano la Kale, neno *emet*, linamaanisha uaminifu au mwaminifu (BDB 53; tazama Mada Maalum: Amini, Sadiki, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale). Katika maandiko ya Kiyahudi ya Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya neno hili lilitumika kuzungumzia ukweli katika kutofautisha uongo. Labda ufanano wa karibu wa "Nyimbo za Shukrani" ilikuwa katika Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi ambapo ufanano huu unatumika katika mafundisho yaliyofunuliwa". Wana Jumuiya ya Essene wakawa "maishahidi wa ukweli huu."

Paulo anatumia neno hili kama njia ya kuirejelea injili ya Yesu Kristo.

1. Warumi 1:18,25; 2:8,20; 3:7; 15:8
2. 1 Wakorintho 13:6
3. 2 Wakorintho 4:2; 6:7; 11:10; 13:8
4. Wagalatia 2:5,14; 5:7
5. Waefeso 1:13; 6:14
6. Wakolosai 1:5,6
7. 2 Wakolosai 2:10,12,13
8. 1 Timotheo 2:4; 3:15; 4:3; 6:5
9. 2 Timotheo 2:15,18,25; 3:7,8; 4:4
10. Tito1:1,14

Pia Paulo analitumia neno hili kama njia ya kueleza kunena kwake kwa usahihi/uaminifu

1. Matendo ya Mitume 26:25
2. Warumi 9:1
3. 2 Wakorinto 7:14; 12:6
4. Waefeso 4:25
5. Wafilipi 1:18
6. 1 Timotheo 2:7

Huyu pia analitumia neno hili kuieleza shauku yake katika 1 Kor. 5:8 na maisha (pia kwa Wakristo wote) katika Efe. 4:24; 5:9; Flp. 4:8. Wakati mwingine analitumia neno hili kuzungumzia watu.

1. Mungu, Rum. 3:4 (kama vile Yohana 3:33; 17:17)
2. Yesu, Efe. 4:21 (sawa sawa na Yohana 14:6)
3. Ushahidi wa ki-Utume, Tito 1:13
4. Paulo, 2 Kor. 6:8

Paulo anatumia muundo pekee wa KITENZI (yaani, *alētheuō*) katika Gal. 4:16 na Efe. 4:15, ambapo linairejelea injili. Kwa usomaji zaidi fuatilia Colin Brown (ed.), *The New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu 3, kr. 784-902.

**1:19 "kinacho fahamika kuhusu Mungu kinashuhudiwa ndani yao, kwa vile Mungu alikithibitisha ndani yao"** Binadamu wote wanajua kitu kuhusu Mungu tangu uumbaji (kama vile mstari wa 20, Ayub. 12:7-10 na Zab. 19:1-6 katika hali ya asili). Katika thiolojia, hii inaitwa "ufunuo asilia". Hajakamilika, lakini ni msingi wa Mungu kuweza kuwajibisha wote ambao hawajawahi kuupata ufunuo maalumu wa mafundisho ya neno la Mungu (kama vile Zab. 19:7-14). Au, hatimaye, katika Yesu (kama vile Kol. 1:15; 2:9)

Neno "kujua" lilitumika katika maana mbili kwenye Agano Jipya (1) maana ya Agano la Kale ya mahusiano ya karibu sana ya mtu (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5) na (2) maana ya Kiyunani kuhusu ukweli wa mlengwa (kama vile mstari wa 21). Injili ni kwa upande mmoja na mtu mwenyewe anayekaribishwa na upande mwingine, ujumbe kuhusu mtu huyo anayepokelewa na kuamini. Katika mstari huu lilitumika tu kwa maana kama ilivyo katika #2

**MADA MAALUMU: KUJUA (hasa ikitumia zaidi Kumbukumbu la Torati kama kielelezo)**

1. Kutambua mazuri na mabaya- Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yona 4:11
2. Kutambua kwa kuelewa - Kumbu. 9:2,3,6; 18:21
3. Kutambua kwa uzoefu - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Jos. 23:14
4. Kufikiria - Kumbu. 4:39; 11:2; 29:16
5. Kutambua wewe mwenyewe
   a. Mtu - Mwa. 29:5; Kuto. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9; Yer. 1:5
   b. miungu - Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
   c. YHWH- Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
   d. Kijinsia - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
6. Ujuzi au maarifa ya kufundishwa - Isa. 29:11,12; Amos 5:16
7. Kuwa mwelevu- Kumb. 29:4; Mith. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. Maarifa ya Mungu
   a. Juu ya Musa-Kumb.34:10
   b. Juu ya Israeli-Kumb.31:21

Kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya Biblia ni ushirika wa ndani, unaokuwa, wa ndani pamoja na Mungu (angalia Mada Maalumu: Koinōnia). Sio kanuni za imani au maisha pekee ya kiadilifu. Ni uhusiano binafsi wa imani. Hii ndio sababu ya Paulo kuitumia nyumba ya mkristo katika Efe. 5:22-6:9 kuuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa

**1:20.** Mstari huu, una mitizamo mitatu ya Mungu.

1. Kukiri asili yake ya kutoonekana (tabia yake, kama vile Kol. 1:15; 1Tim 1:17; Ebr. 11:27
2. Nguvu yake ya milele (ikionekana katika uumbaji- kama vile Zab. 19:1-6)
3. Asili yake kama Mungu (ikionekana katika matendo na makusudio yake ya uumbaji (kama vile Mwa. 1-2)

◙**"Tangu kuumbwa kwa ulimwengu"** Kihusishi *"apo"* kinatumika kwa maana ya "muda mfupi". Kifungu sambamba na hiki kinapatikana katika Marko 10:16; 19; 2Pet 3:40. Mungu asiyeonekana sasa anaonekana katika:

1. Uumbaji kimatendo (mstari huu)
2. Mafundisho ya neno (Zab. 19, 119)
3. Hatimaye kwa Yesu (kama vile Yoh. 14:9

◙**"asili ya Uuungu"** Kutoka fasihi ya Kiyunani *thelotēs* ingeweza kutafasiriwa "ukuu wa Mungu." Hii inaonekana katika ukuu wa Yesu. Kipekee ni mfano wa Mungu (kama vile 2Kor 4:4; Ebr. 1:3). Yeye ni ufunuo kamili katika umbo la binadamu (Kol 1:19; 2:9). Ajabu ya ukweli wa injili ni kwamba, mwanadamu aliyeanguka kutokana na imani katika Kristo, atakuwa wa kufanana naye (kama vile Ebr. 12:10; 1 Yoh. 3:2). Sura ya Mungu katika binadamu (kama vile Mwa. 1:26-27) imerejeshwa (*theois*, kama vile 2 Pet 1:3-4).

◙

**NASB** **"Wameonekana wazi, wameeleweka kwa kile kilichofanyika"**
**NKJV** **"Wanaonekana, wameeleweka kwa vile vitu vilivyofanyika"**
**NRSV** **"Wameeleweka na kuonekana kutokana na vitu alivyotengeneza"**
**TEV** **"Wameonekana wazi wameeleweka kwa vitu alivyovitengeneza Mungu"**
**NJB** **"Wameonekana kwa uelewa wa kiakili kwa vitu vilivyoumbwa"**

Muunganiko wa *noeō* (kama vile Mt. 15:17) na *kathoraō* (ZOTE KAULI TENDWA ZA WAKATI ULIOPO) inaonyesha kueleweka upya. Mungu ameandika vitabu viwili (1) Asili (kama vile Zab. 19:1-6) na (2) Mafundisho

(kama vile Zab. 19:7-14). Vyote viko katika uwezo wa mwanadamu kuvielewa na vinahitaji kukubalika (kama vile *hekima* 13:1-9)

◙**"kwa hivyo wapo bila msamaha"** Hili kimantiki, "halina kinga kisheria". Neno hili la Kiyunani (la kuongeza *apologeomai)* linatumika tu hapa na katika 1:2 kwenye Agano la Kale. Kumbuka kusudi la kitheolojia la 1:18-3:20 ni kuonyesha kupotea kwa wanadamu wote kiroho. Binadamu wanawajibika kwa maarifa walionayo. Mungu anawajibisha binadamu kwa yale tu wanayoyajua au wangeyajua (kama vile 4:15; 15:13)

**1:21 "kwa vile hata hivyo walimjua Mungu"** Wanadamu hawaendelei kulijua neno la Mungu, bali wanaendelea katika uovu. Kwani katika Mwanzo 3 ubinadamu umekuwa ukiporomoka, giza linaongezeka.

◙**"hawakumheshimu kama Mungu au kumshukuru"** Hii ni bahati mbaya sana kwa wapagani kuabudu miungu – katika mist.23,24 (kama vile Yer. 2:9-15). Waumini humtukuza Mungu kwa kuishi kama Kristo aishivyo (kama vile Mt 5:16; Rum. 12:1-2; 1 Kor. 6:20; 10:31; Flp. 1:20; 1Pet 4:11). Mungu anataka watu wanaoonyesha/kudhihirisha tabia yake kwa ulimwengu kipofu, ulioanguka.

◙**"njozi zao hazikuzaa matunda, na mioyo yao ya kipumbavu ikatiwa giza"** *The New Testament: A New Translation* cha Olaf M. Morlie inasema "walijishughulisha zaidi na njozi zao za kipumbavu, kumhusu, na mawazo yao ya kipumbavu yakipapasa katika giza. Mfumo wa dini za kibinadamu ni mnara wa uasi wa kiroho na majivuno (kama vile mst. 22; Kol. 2:16-23)**.**

Neno lililotumika "kutozaa matunda" lilitumika katika LXX kumanisha "hakuna kitu", "hakipo" vinyago vya majirani wa Israel. Paulo alikuwa mwebrania mwenye fikra kubwa. Alijua sana matoleo ya kale ya Kiyunani. Matumizi ya maneno ya Kiyunani katika LXX ni mwongozo mzuri kwa mawazo ya waandishi wa Agano Jipya kuliko ya kamusi ya Kiyunani.

VITENZI viwili ni KAUI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Je kauli TENDWA inamaanisha kukosa kwao uelewa na mwitikio mzuri ulikuwa ni kwa sababu Mungu aliwanyima mioyo ya wema au kukataa kwao mwanga kuliwafanya wawe na mioyo migumu (kama vile 10:12-16; 2 Fal. 17:15; Yer. 2:5; Efe. 4:17-19). Hili ndilo swali la kithiolojia lililohusiana na Farao katika kitabu cha Kutoka.

| Mungu akamfanyia moyo mugumu | Farao akaufanya moyo wake kuwa mugumu |
|---|---|
| Kutoka 4:21 | Kutoka 8:15 |
| 9:12 | 8:32 |
| 10:20 | 9:34 |
| 11:10 | |
| 14:4 | |
| 14:8 | |
| 14:17 | |

Katika 9:35, ugumu ungeweza kumanisha Mungu au Farao. Huu ni muujiza wa ki-uungu na mapenzi ya bure ya kibinadamu.

◙**"moyo"** Hii ilitimika katika fikra za Agano la kale kwa mtu mzima. Hivyo ilikuwa ni njia daima ya kumanisha mchakato wa kufikiri au kuhisi. Tazama mada maalumu katika 1:24

◙

**1:22**

**NASB, NKJV "Waliojifanya kuwa werevu wakawa wajinga"**
**NRSV "Wakidai kuwa werevu wakawa wajinga"**
**TEV "Wanasema ni werevu kumbe ni wajinga"**
**NJB "Kadri walivyojiita wanafalsafa ndivyo walivyozidi kuwa wapumbavu"**

Kutokana na neno la Kiyunani "mjinga" tunapata neno la Kiingereza "punguani" (likiwa na maana mjinga zaidi). Tatizo liko katika majivuno na kujiamini kwa binadamu katika maarifa walionayo (kama vile 1 Kor 1:18-31; Kol 1:8-

23). Hili linarudi mpaka Mwanzo 3. Marifa yakaleta utengano na hukumu. Sio kuwa wakati wote maarifa ya binadamu hayako sawa, siyo hivyo hatimaye!

**1:23** kwa mapenzi wanadamu wapumbavu waliofanywa kwa mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6) walibadilisha Mungu kuwa mfano wa dunia kama vile:

1. Wanyama (Misri)
2. Nguvu za asili (Uajemi)
3. Umbo la binadamu (Uyunani/Roma)- vinyago. Hata watu waliokuwa wa Mungu walifanya hivyo (Kumb 4:15-24)

Baadhi ya aina hii ya dhambi ni kama:

1. Hali ya kimazingira (Dunia mama)
2. Wazo la Mashariki la enzi mpya (imani katika maombi, hali ya kiroho na kishirikina)
3. Fikra za kibinadamu kuwa Mungu hayupo (nadharia za Marx, kufikirika, dhana ya kimaendeleo, hatima ya imani kisiasa na elimu)
4. Elimu ya tiba (afya na kuishi)
5. Elimu.

◙"**Utukufu"** Tazama mada maalumu katika 3:23

◙**"binadamu mla rushwa"** Tazama Mada Maalumu ifuatayo

## MADA MAALUM: ANGAMIZA, HARIBU, CHAFUKA (*phtheirō*))

Maana ya msingi ya neno hili *phtheirō* ni kuangamiza, kuharibu, kuchafua, au kuvuruga. Linaweza tumika kwa:

1. maangamizi ya kifedha (yawezekana 2 Kor. 7:2)
2. uharibifu wa kimwili (kama vile 1 Kor. 3:17a)
3. upotoshaji wa kimaadili (kama vile Rum. 1:23; 8:21; 1 Kor. 15:33,42,50; Gal. 6:8; Ufu. 19:2)
4. utongozaji wa kingono (kama vile 2 Kor. 11:3)
5. uharibifu wa milele (kama vile 2 Pet. 2:12,19)
6. tamaduni za wanadamu zipoteazo (kama vile Kol. 2:22)

Mara nyingi neno hili limetumika katika muktadha uleule kama unavyokanusha pinzani yake (kama vile Rum. 1:23; 1 Kor. 9:25; 15:50,53). Angalia mvutano wa usambamba kati ya miili yetu ya duniani na miili yetu ya kimbingu isiyoharibika.

1. iharibikayo dhidi ya isiyoharibika, 1 Kor. 15:42,50
2. kukosa heshima dhidi ya utukufu, 1 Kor. 15:43
3. udhaifu dhidi ya nguvu, 1 Kor. 15:43
4. mwili wa asili dhidi ya mwili wa kiroho, 1 Kor. 15:44
5. adamu wa kwanza dhidi ya Adamu wa mwisho, 1 Kor. 15:45
6. taswira ya duniani dhidi ya taswira ya kimbingu, 1 Kor. 15:49

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:24-25**
**24 Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tama za mioyo yao, wafuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao. 25 Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele, Amina.**

**1:24, 26,28 "Mungu aliwaacha"** Hii ndiyo hukumu mbaya kuliko zote. Ni Mungu anasema "acheni binadamu walioanguka waende zao" kama vile Zab. 81:12; Hos. 4:17; Mdo. 7:42; Inanukuu mandiko kadhaa ya Agano la Kale kuhusu suala hili la kithiolojia. Mistari ya 23-32 inaeleza ukataaji wa Mungu (ghadhabu ya muda) juu ya

ulimwengu wa kipagani na dini zao! (na zetu). Ukahaba ulikuwa na matendo ya kikahaba na unyonyaji na hata sasa.

**1:24 “moyo”** Tazama mada maalumu inyofuata.

## MADA MAALUMU: MOYO (AGANO JIPYA)

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania lēb (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*,, 2nd ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
    a. Mungu anatujua mioyo (kama vile. Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
    b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani, uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa,kama vile.Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani,Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
    a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
    b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
    c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
    d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
    e. Ezek. 36:26, "moyo mpya” dhidi ya “moyo wa jiwe” (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

**1:25 “walibadilisha ukweli wa Mungu kuwa uongo”** Hii inaweza kueleweka kwa njia kadhaa

1. Mwanadamu kujiabudu mwenyewe (kama vile 2 The. 2:4,11)
2. Mwanadamu kuabudu kile alichokitengeneza - sanamu ( kama vile Isa. 40:20; Yer. 13:25; 16:19) badala ya YHWH aliyeumba kila kitu.
3. Mwanadamu hatimaye kuukataa ukweli wa injili (kama vile Yoh. 14:17; 1 Yoh. 2:21-27). Andiko #2 linafaa zaidi

◙**“waliabudiwa na kutumikiwa”** Mwanadamu daima atakuwa na miungu. Katika fikra zote za mwanadamu , kuna mtu, ukweli, au kitu chochote zaidi ya wao wenyewe.

◙**“nani anabarikiwa milele. Amina”** Paulo akaingia kwa ghafla kwenye Baraka za Kiyahudi, kama ilivyokuwa kawaida yake (kama vile Rum. 9:5; 2 Kor. 11:31). Daima Paulo anaomba wakati akiandika (kama vile 9:5; 11:36; 15:33; 16:27)

◙**“milele”** Tazama Mada Maalumu hapa chini

## MADA MAALUM: MILELE (LAHAJA YA KIYUNANI)

Moja ya tungo ya kiyunani "katika nyakati" (kama vile Luka 1:33; Rum. 1:25; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 1 Tim. 1:17), ambayo inaweza kuaksi 'olam. Angalia Robert B. Girdlestone, Synonyms of the Old Testament, kur. 319-321, na Mada Maalum: Milele ('Olam).
Tungo zingine zinazoweza kufanana "katika nyakati" (kama vile Mt. 21:19; Marko 11:14; Luka 1:55; Yohana 6:58; 8:35; 12:34; 13:8; 14:16; 2 Kor. 9:9) na "ya nyakati za nyakati" (kama vile Efe. 3:21). Kunaonekana kutokuwepo na utofauti kati ya lahaja hizi mbili za Kiyunani za "milele." Neno "nyakati" inaweza kuwa wingi katika namna ya kimafumbo ya tungo za kisarufi za kiualimu wa kiyahudi "wingi wa mfalme," au inaweza kurejerea dhana ya "nyakati" kadhaa katika namna ya Kiyunani ya "zama ya uovu," "enzi ijayo," au "zama ya haki" (angalia Mada Maalum: Enzi Hii na Enzi Ijayo).

◙**"Amina"** Tazama Mada Maalumu hapo chini

## MADA MAALUMU: AMINA

I. AGANO LA KALE
   A. Neno "Amina" linatokana na neno la Kiebrania
      1. "ukweli (*emeth,* DBD 49)
      2. "hali ya ukweli" (*emun, emunah,* DBD 53)
      3. "imani" au "uaminifu"
      4. "kuamini" (*dmn,* DBD 52)
   B. Mwanzo na maana ya neno hili ni uimara wa mtu kutoweza kuanguka. Kinyume chake ni mtu asiye imara, awezaye kuteleza (kama vile Kumb 28:64-67; 38:16; Zab 40:2; 73:18; Yer 23:12) au kuyumba (kama vile Zab 73:2). Kutokana na matumizi haya ya kifasihi, alitumia maana nyingine ya kuelezea mwaminifu, anayeaminika, mwema na anayetegemewa (kama vile Mwa 15:16; Hab 2:4)
   C. Matumizi maalumu
      1. Mhimili, 2Fal 18:16 (1Tim 3:15)
      2. Uhakika, Kut 17:12
      3. Isiyoyumba, Kut 17:12
      4. Imara, Isa 33:6; 34:5-7
      5. Ukweli, 1Fal 10:6; 17:24; 22:16; Mith 12:22
      6. Imara, 2Kor 20:20; Isa 7:9
      7. Anayetegemewa, (Torah) Zab 119:43,142,151,168
   D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yametumika kuonyesha imani thabiti.
      1. *Bathach* (BDB 105), kuamini
      2. *Yra (*BDB 431). Uoga, heshima, kuabudu (kama vile Mwa 22:12)
   E. Kutokana na maana ya "kuamini"au "kuaminika" ilizaa matumizi ya litulujia iliyotumika kuimarisha usemi wa kweli au wa kuaminika wa neno sambamba (kama vile Kumb 27:15-26; Neh 8:6; Zab 4:13; 70:19; 89:52; 106:48)
   F. Ufunguo wa kitheolojia kwa maneno haya sio imani ya mwanadamu bali ya YHWH (kama vile Kut 34:6; Kumb 32:4; Zab 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la pekee la binadamu aliyeanguka, ni agano la huruma na imani ya wema wa YHWH na ahadi zake. Wale wanaomjua YHWH watakuwa kama yeye (kama vile Hab 2:4). Biblia ni historia na kumbukumbu ya Mungu ya kurejesha mfano wake (kama vile Mwa 1:26-27) kwa wanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu hatimaye kuwa na ushirika na Mungu. Hii ndio sababu tuliumbwa.

II. AGANO JIPYA.
   A. Matumizi ya neno "amina" kama hitimisho la uthibitisho wa liturujia kwa maelezo ya kuaminika ya usemi huu ni kawaida katika Agano Jipya (kama vile 1Kor. 14:16; 2Kor 1:20; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12)

B. Matumizi ya neno hili kwa kufunga maombi ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile Rum 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal 1:5; 6:18; Ef 3:21; Fil 4:20; 2Thes 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2Tim 4:18)
C. Yesu, ndiye pekee aliyetumia neno hili (daima likifanywa mara dufu katika Yohana) kutoa maelezo muhimu (kama vile Lk. 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43)
D. Linatumika kama wadhifa wa Yesu katika ufunuo 3:14 (yamkini wadhifa wa YHWH kutoka Isa 65:16)
E. Dhana ya uaminifu au imani, kuaminika, au kuamini inaelezwa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis* ambalo linatafasiriwa kwa Kiingereza kama "kuamini", "imani", "kusadiki"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:26-27**
**[26]Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tama zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi yao ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; [27]wanaume nao vivyo hivyo waliacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tama, wanaume wakayatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao.**

**1:26,27.** Ushoga ni moja ya mifano ya maisha mbali kabisa za mapenzi dhahiri katika uumbaji (zaeni matunda). Ilikuwa ni dhambi, na tatizo kubwa katika mila

1. Katika Agano Jipya (kama vile Law. 18:22; 20:13; Kumb. 23:18)
2. Katika ulimwengu Warumi ( kama vile 1Kor. 6:9; 1Tim. 1:10)
3. Katika siku zetu

Ushoga bila shaka unaorodheshwa Kama mfano wa maisha yaliyoanguka kwa sababu ya hali halisi iliyomo katika muktadha mzima wa Mwanzo 1-3. Mwanadamu aliumbwa kwa mfano wake (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu alifanywa mme na mke (kama vile Mwa. 1:27). Agizo la Mungu lilikuwa wazae matunda (wazaliane) na kuongezeka (kama vile Mwa. 1:28; 9:1,7). Kuanguka kwa mwanadamu (kama vile Mwa. 3) kulivuruga mpango wa Mungu na mapenzi yake. Ushoga ni uasi dhahiri! Hata hivyo inabidi isemwe kwamba hii sio dhambi pekee iliyotajwa katika eneo hili (kama vile mistari ya 29-31). Dhambi zote zinaonyesha utengano wa mwanadamu toka kwa Mungu na adhabu waipasayo. Dhambi zote hasa dhambi za mwenendo wa kimaisha ni chukizo kwa Mungu.

## MADA MAALUM: KUJAMIIANA KWA JINSIA MOJA

Kuna shinikizo kubwa la destuli za kisasa kukubali kujamiiana kwa jinsia moja kama mtindo wa maisha sahihi na mbadala.
Biblia inalaani kitendo hiki kama mtindo wa maisha wenye uharibifu, nje ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya uumbaji wake.

1. inavunja amri ya Mwanzo 1 juu ya kuzaa na kuongezeka
2. Inaweka bayana tabia za ibada za kipagani na desturi (kama vile Mambo ya Walawi 18:22; 20:13; Rum. 1:26-27; na Yuda 7)
3. Inafunua uhuru wa kibinafsi kujitenga mbali na Mungu(kama vile 1 Kor. 6:9-10)

Hatahivyo kabla sijaachana na mada hii ngoja nielezee upendo wa Mungu na msamaha kwa wanadamu wote waasi. Wakristo hawana haki ya kuwa na chuki kuu wala kujivuna juu ya dhambi hii, haswa wakati I wazi kwamba sisi sote tunatenda dhambi. Maombi, kujaliana, ushuhuda na huruma vinafanya kazi zaidi katika eneo hili kuliko kushutumiana kwa ukali. Neno la Mungu na Roho wake watafanya kazi ya kulaani na kuhukumu ikiwa tutawaruhusu. Dhambi zote za zinaa, sio tu hii ni chukizo mbele za Mungu na zinatupeleka katika hukumu. Hali ya kutamani kujamiina ni zawadi na kipawa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ustawi wa mwanadamu, furaha na jamii imara. Lakini hamu hii yenye nguvu na iliyotolewa na Mungu mara kwa mara inageuzwa kuelekea katika ubinafsi na kujitaftia maslahi yake yenyewe, maisha ya "zaidi-kwa ajili yangu-kwa gharama yoyote" (kama vile Rum. 8:1-8; Gal. 6:7-8).

Mara kwa mara watu wanasema, "Mungu aliniumba hivi."Ni kweli kwamba bado hatujui chanzo cha usenge (yaani kijenetiki au kijamii) lakini vyovyote, Biblia lazima utuongoze juu ya chaguzi zetu; Chaguzi zina matokeo. Maandiko yana vipaumbele juu ya hisia au upendeleo binafsi. Sisi ni jamii ya kiimani tunaoongozwa kwa ufunuo wa kiungu na sio uhuru au haki za mtu mmoja mmoja.

Neno la kuhitimisha kama kiongozi wa kanisa sifahamu kwamba asilimia mashindano ya Wakristo juu ya suala hili. Tatizo sio ile hulka ila tendo. Baadhi ya wanafunzi wa kihuduma katika chuo changu wanahangaika na mambo mengine ya kingono (yana nguvu sana katika hatua hii ya maisha). Wale wanaochagua kuweka mipaka katika shauku zao (yaani kujizuia) katika eneo hili (yaani matamanio ya kingono) hakika ndio watu sahihi kwa ajili ya nafasi za huduma. Hili pia ni hivyo hivyo kweli kwa wale wanaohangaika na kujamiiana kwa jinsia moja. Suala la msingi hapa ni tendo na sio wazo. Kwanini baadhi wanavutwa kwa wengine wa jinsi moja bado ni fumbo. Kuna uchaguzi katika eneo hili (kama ilivyo katika maeneo mengine). Tunawajibika kwa chaguzi zetu! Mungu anawapenda watu na kutamani afya zao za kudumu na ustawi kwa wale wote waliofanywa kwa sura na mfano wake (Mwanzo 1:26-27; angalia Mada Maalumu: Kujamiiana kwa Jinsia moja). Yale mambo/matendo ambayo yanamuharibu afya ya mtu na furaha na pia jamii lazima yakemewe na kulaaniwa. Mungu anataka kutuona tukiwa katika ubora wetu! Sisi tunataka kutimizwa kwa matakwa yetu haraka haraka! Mungu aturehemu sisi sote.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:28-32**
**28 Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa,**
**wafanye yasiyowapasa. 29 Wamejawa na udharimu wa kila namna, uovu na tama na ubaya; wamejawa na**
**husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya, 30 wenye kusingizia, wenye**
**kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii**
**wazazi wao, 31wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema;**
**32ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti,**
**wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao.**

**1:28-31** Hii ni sentesi moja katika Kiyunani. Yenye kupelekea uasi, anguko, mwanadamu huru (kama vile Rum 13:13; 1 Kor. 5:11; 6:9; Gal. 5:19-21; Efe. 5:5; 1Tim. 1:10; Ufu. 21:8).

Dhambi ya wanadamu ilikuwa kwamba walichagua kuishi mbali na Mungu. Maisha yakawa hivyo kujitenga na kujitegemea, ikawa ni fadhaiko. Ahera, pakawa ni makazi ya kudumu. Mwanadamu anamhitaji Mungu, amepotea, hatoshi na hakamiliki akiwa mbali na Mungu. Kibaya zaidi kutoka ahera ya milele ni kukosa kabisa mahusiano na Mungu.

**1:29 "mawazo maovu"** Anachokiona mwanadamu aliyeanguka kuwa ni uhuru kwake ni kujiabudu. "Chochote kile na kila kitu ni kwa ajili yangu." Sauti hii ya KUTENDWA inasemwa kama Mungu katika 1:24, 26,28. Lakini katika mazingira haya ya mahusiano katika Mwanzo 1-3 ni chaguo la mwanadamu la maarifa na pekee lililoleta tatizo. Mungu aliruhusu uumbaji wake upate matatizo kutokana na chaguo lao wenyewe na uhuru wao wenyewe.

◙**"Kujazwa na"** Hii ni KAULI YA KUTENDWA TIMILIFU YA HALI ENDELEVU. Wanadamu hujazwa na kuwa katika hali ya jinsi wanavyoishi. Wakuu wa maswala ya dini wangesema kuwa, kwa kila moyo wa binadamu kuna mbwa mweusi na umbwa mweupe. Yule anayelishwa zaidi ndiye huwa mkubwa zaidi.

**1:29-31** Haya ni matokeo na dalili za maisha bila Mungu. Yanaashiria mtu na jamii ambayo huamua kumkataa Mungu wa Biblia. Hii ilikuwa mojawapo ya orodha ya dhambi Paulo alizooredhesha (kama vile 1 Kor. 5:11; 6:9; 2 Kor. 12:20; Gal. 5:19-21; Efe. 4:31; 5:3-4; Kol. 3:5-9)

## MADA MAALUM: UOVU NA WEMA KATIKA AGANO JIPYA

Orodha zote za mabaya na mema ni ya kawaida katika Agano Jipya. Mara nyingi yanaaksi orodha za sheria za Kiyahudi na kitamaduni. Orodha ya tabia kinzani ya Agano Jipya zinaweza onekana katika:

| | **Maovu** | **Wema** |
|---|---|---|
| 1. Paulo | Rum. 1:28-32 | --- |
| | Rum. 13:13 | Rum. 12:9-21 |
| | 1 Kor. 5:9-11 | --- |
| | 1 Kor. 6:10 | 1 Kor. 6:6-9 |
| | 2 Kor. 12:20 | 2 Kor. 6:4-10 |
| | Gal. 5:19-21 | Gal. 5:22-23 |
| | Efe. 4:25-32 | --- |
| | Efe. 5:3-5 | --- |
| | --- | Flp. 4:8-9 |
| | Kol. 3:5,8 | Kol. 3:12-14 |
| | 1 Tim. 1:9-10 | --- |
| | 1 Tim. 6:4-5 | --- |
| | 2 Tim. 2:22a, 23 | 2 Tim. 2:22b,24 |
| | Tito 1:7, 3:3 | Tit 1:8-9; 3:1-2 |
| 2. Yakobo | Yak. 3:15-16 | Yak. 3:17-18 |
| 3. Petro | 1 Pet. 4:3 | 1 Pet. 4:7-11 |
| | 2 Pet. 1:9 | 2 Pet. 1:5-8 |
| 4. Yohana | Uf. 21:8; 22:15 | --- |

**1:30 "majivuno"** Hii ni *hupērphanous* (Angalia C, 3 chini)

## MADA MAALUM: MATUMIZI YA PAULO YA NENO AMBATANI *"HUPER"*

Paulo alikuwa na upendeleo binafsi kwa ajili ya kuyaumba maneno mapya kwa kutumia KIWAKILISHI cha Kiyunani *huper*, ambacho kimsingi kinamaanisha "juu ya" ama "kuu." Hiki kilipotumika pamoja na KIMILIKISHI (CHA KUONDOA) kilimaanisha "badala ya" Pia kinaweza kumaanisha "karibia na" au "kuhusiana na" kama *peri* (kama vile 2 Kor. 8:23; 2 The. 2:18). Hiki kikitumika pamoja na HALI YA KUSHUTUMU kinamaanisha "kuzidisha wastani," "juu ya," au "zaidi ya" (kama vile A. T. Robertson, *A Grammar of the Greek New Testament in the Light of Historical Research*, kr. 625-633). Wakati Paulo alipotaka kutia mkazo alitumia KIWAKILISHI katika uambatani. Ifuatayo ni orodha ya matumizi maalum ya Paulo ya KIWAKILISHI hiki katika uambatani.

A. Hapax legomenon (kimetumika mara moja katia Agano Jipya pekee)
   1. *Huperakmos*, mmoja wa maisha kwanza yaliyopita, 1 Kor. 7:36
   2. *Huperauxanō*, kuongezeka sana, 2 The. 1:3
   3. *Huperbainō*, kupunja ama kukosa, 1The. 4:6
   4. *Huperkeina*, mbele ya, 2 Kor. 10:16
   5. *Huperekteina*, kupita kadri, 2 Kor. 10:14
   6. *Huperentugchanō*, kuomba kwa kuugua, Rum. 8:26
   7. *Hupernikaō,* tunashinda tena zaidi ya kushinda, Rum. 8:37
   8. *Huperpleonazō*, kuwa katika hali ya kuzidi sana, 1 Tim. 1:14
   9. *Huperupsoō*, kuadhimisha mno, Flp. 2:9

10. *Huperphroneō*, kunii yaliyo makuu, Rum. 12:3

B. Maneno yaliyotumika katika maandiko ya Paulo pekee.

1. *Huperairomai*, kujivuna kwa mtu mwenyewe, 2 Kor. 12:7; 2 The. 2:4
2. *Huperballontōs*, zaidi ya kipimo, kupita kiasi, 2 Kor. 11:2 (KIVUMISHI kiko hapa tu, lakini KITENZI ki katika 2 kor. 3:10; 9:14; Efe. 1:19; 2:7; 3:19)
3. *Huperbolē*, kuzidi zaidi, kujilinda kuliko pitiliza, Rum. 7:13; 1 Kor. 12:31; 2 Kor. 1:8; 4:7,17; 12:7; Gal. 1:1
4. *Huperekperissou*, zaidi ya vipimo vyote, Efe. 3:20; 1 The. 3:10; 5:13
5. *Huperlian*, katika kiwango cha juu ama kuzidi wengine, 2 Kor. 11:5; 12:11
6. *Huperochē*, maarufu, bora, 1 K. 2:1; 1 Tim. 2:2
7. *Huperperisseuō*, kuzidi zaidi, Rum. 5:20 (KAULI YA KATI, nina ujasiri mwingi, kupita kiasi, 2 Kor. 7:4)

C. Maneno yaliyotumiwa na Paulo na yaliyo haba katika waandishi wengine wa Agano Jipya

1. *Huperanō*, juu sana, Efe. 1:21; 4:10; na Ebr. 9:5
2. *Huperechō*, maarufu, bora, Rum. 13:1; Flp. 2:3; 3:8; 4:7; 1 Pet. 2:13
3. *Huperēphanos*, kusingizia au majivuno, Rum. 1:30; 2 Tim. 3:2 na Luka 1:51; Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5.

Paulo alikuwa mtu wa hisia kali; wakati mambo au watu walipokuwa wema, walikuwa wazuri sana na walipokuwa wabaya walikuwa wabaya sana. KIWAKILISHI hiki kilimruhusu kueleza hisia zake zilizozidi kuihusu dhambi, mwenyewe, na Kristo na Injili.

**1:32 "wote wanaotenda mambo hayo wanastahili kifo"** Usemi huu unarejea usemi wa Musa. Imefupishwa katika Rum. 6:16,21,23; 8:6,13. Kifo ni kinyume cha mapenzi ya Mungu na maisha ya Mungu (kama vile Ezek. 18:32; 1 Tim. 2:4; II Pet. 3:9).

◙**"pia kuwapa thibitisho la moyoni kwa wale wote wanaoyatenda"** Ubahili hupenda kuwa pamoja. Mwanadamu aliyeanguka hutumia dhambi za wenziwe kama kisingizio. "Kila mtu anatenda dhambi." Tamaduni mbali mbali zinasababishwa hasa hasa na dhambi zao.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Kwa nini Paulo aliliandikia kanisa la Roma?
2. Kwa nini Waroma walikuwa suala muhimu la kithiolojia la Ukristo?
3. Eleza kwa kifupi 1:18-3:20 katika maneno yako mwenyewe
4. Je, itapasa wale ambao hawajasikia injili wakataliwe kwa vile hawamwamini Kristo?
5. Eleza kwa kina maisha ya mwanadamu bila Mungu.
6. Elezea maisha ya mwanadamu pasipo Mungu
7. Je mistari 24-27 inazungumzia kuhusu kujamiiiana kwa jinsia moja?

# WARUMI 2

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Hukumu ya Haki ya Mungu | Hukumu ya haki ya Mungu | Wayahudi chini ya hukumu | Hukumu ya Mungu | Wayahudi hawaondolewi kutoka katika adhabu ya Mungu |
| 2:1-16 | 2:1-16 | 2:1-11 | 2:1-16 | 2:1-11 |
| Wayahudi na sheria | Wayahudi hatiani kama wamataifa | Msingi wa hukumu | Wayahudi na sheria (2:17-3:8) | Sheria haitawaokoa |
| | | 2:12-16 | | 2:12-16 |
| 2:17-3:8 | 2:17-24 | 2:17-24 | 2:17-24 | 2:17-24 |
| | Tohara isiyo na tija | | | Tohara haitawaokoa |
| | 2:25-29 | 2:25-29 | 2:25-29 | 2:25-29 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA JUU YA WARUMI 2:1-3:20

A. Sura ya 2 na 3 zinahitimisha kipengele kilichoanza 1:18, sehemu hii inahusika na :
   1. Kupotea kwa wanadamu wote
   2. Hukumu ya Mungu juu ya dhambi
   3. Hitaji la haki la Mungu kupitia kwa Kristo kwa njia ya imani na toba

B. Katika sura ya pili kuna kanuni saba zinazohusu hukumu ya Mungu.
   1. Mstari wa 2, kufuatana na ukweli
   2. Mstari wa 5, hatia ya pamoja
   3. Mstari wa 6 na 7, kufuatana na kazi
   4. Mstari wa 11, hakuna heshima ya watu

5. Mstari wa 13, stadi ya maisha
6. Mstari wa 16, siri za rohoni za wanaume
7. Mstari wa 17-29, hakuna makundi maaalumu ya kitaifa

C. Kuna majadala mkubwa miongoni mwa watoa maoni kuhusu nani alikuwa anazungumuziwa katika sura 2:1-17. Ni wazi kwamba 2:12-29 inahusu Wayahudi. Mistari ya 1-17 inagusa makundi mawili ya kuzungumzia juu ya wapagani (desturi za jamii) na kwa taifa la Wayahudi (sheria za Musa)

D. Katika 1:18-21, Paulo alisisitiza kuwa wanadamu wanaweza kumjua Mungu kupitia uumbaji wake. Katika 2:14-15, Paulo anasisitiza pia wanadamu wana asili ya ndani ya utambuzi waliopewa na Mungu. Aina mbili hizi za ushuhuda; uumbaji na dhamiri, ndiyo msingi wa laana ya Mungu kwa wanadamu wote, hata wale ambao hawajawahi kusikia agano la kale au ujumbe wa injili. Wanadamu wanawajibika kwa sababu, hawajaishi kwa kiwango cha uelewa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:1-11**
**[1] Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umuhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale. [2] Nasi twajua ya kuwa hukumu ya Mungu ni ya kweli juu yao wafanyao hayo. [3] Wewe binadamu, uwahukumuye wale wafanyao hayo na kutenda hayo hayo mwenyewe, je! Wadhani ya kwamba utajiepusha na hukumu ya Mungu? [4] Au waudharau wingi wa wema wake na usitahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? [5] Bali kwa kadri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, [6] atakaye mlipa kila mtu kwa kadri ya matendo yake; [7] wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele; [8] na wale wenye fitina, wasioitii kweli, bali wakubalio dhuluma, watapata hasira na ghadhabu; [9] dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu, Myahudi kwanza na Myunani pia; [10] bali utukufu na heshima na amani kwa kila mtu atendaye mema, Myahudi kwanza na Myunani pia; [11] Kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu.**

◙
**2:1**
**NASB** **"Huna msamaha, kila mmoja wenu aliyepaswa kuipata hukumu"**
**NKJV** **"Husameheki, O! Ndugu, hata uwe Yule unayehukumu"**
**NSRV** **"Huna msamaha, hata uwe nani, unapowahukumu wengine"**
**TEV** **"Huna msamaha hata kidogo, hata uwe nani hata kama utahukumu wengine"**
**NJB** **"Kwa hiyo haijalishi wewe ni nani, kama unahukumiwa huna msamaha"**

Hili kimantiki "halina kinga kisheria" (kama vile 1:20). Kwa mara ya kwanza iliandikwa katika sentesi ya Kiyunani kuipa uzito. Mstari wa 1-16 inaonekana kuhusisha yote kwa haki binafsi ya wanasheria wa Kiyahudi na viongozi wa kimila wa Kiyunani. Kwa kuwahukumu wengine wanajilaani wenyewe.

Fungu hili hili limetumika katika 1:20, lakini KIWAKILISHI ni "wao"; hapa "wewe". Bila shaka, Paulo anazungumzia makundi mbalimbali ya watenda dhambi/waasi. Ambapo katika moja ya makundi hayo aliwahi kuwa mmoja wao dhabiti.

Kuna matatizo matatu:

1. Kukataa na kuchafua maarifa ya Mungu
2. Kuyageuza kuwa kanuni, kuwa ya kuhukumia na haki ya mtu

Pia, tazama kuwa "wao" ya sura ya 1 na kuwa "wewe" katika 2:1-8. Inajumuisha kutoka kwa Wayahudi na Wayunani kuwa "kila nafsi ya mtu" katika 2:9-11. Ingawa kuna makundi mbalimbali (mawili ama matatu), hatimaye haileti tofauti yeyote, wote wamo katika hukumu (kama vile 3:23)

**2:2** "**Tunajua**" kiwakilishi hiki bila shaka kinarejea Wayahudi wenzao au ingawa ingeweza kumaanisha Wakristo katika mstari wa 2-4, Paulo anarudia katika mbinu yake ya kawaida ya mfumo wa swali kwa jibu, iliyoitwa maneno ya kushambulia. (yaani, mistari 1-11, 17-19), ambayo ilikuwa ni uwakilishi wa ukweli kwa njia ya aliyepaswa kupinga. Ilitumiwa pia na Habakuki, malaki na viongozi wa kidini wa Wayahudi, na wanafalsafa wa Kiyunani (kama Socrates na Stoiks). Usemi "tunajua kuwa" unasemwa mara kadhaa na Warumi (kama vile 2:2; 3:19; 7:14; 8:22, 28). Paulo, anachukulia kuwa, wasikilizaji wake wana kiwango fulani cha uelewa tofauti na wapagani wasioamini wa sura ya 1.

◙ **"Hukumu ya Mungu"** Biblia iko wazi kwa ukweli huu. Kila mmoja atajieleza kwa Mungu kuhusu tunu ya maisha (kama vile mistari ya 5-9; Mathayo 25:31-46; Ufunuo 20:11-15). Hata Wakristo watasimama mbele ya Kristo (kama vile 14:10-12, 2 Kor. 5:10)

**2:3** Namna fasaha ya swali la Paulo akitegemea jibu la "hapana"

◙ **"Unadhani"** Hiki ni kitenzi cha Kiyunani *logizomai*. Paulo anakitumia daima (Warumi 2:3,26; 3:28; 4:3,4,5,6,8,9,10,11,22,23,24; 6:11; 8:18,36; 9:8;14:14; Wagalatia 3:6, mara kumi katika 1 Wakorintho na 2 Wakorintho na mara mbili katika Wafilipi). Tazama nukuu katika 4:3 na 8:18

◙ **"O ndugu"** hii inaendana na nahau katika mstari wa 1. Katika 9:20 inamaanisha Wayahudi.

**2:4** Hili pia ni swali katika Kiyunani.

◙
**NASB** **"Fikiri kirahisi"**
**NKJV, NRSV**
**TEV, REB** **"Dhalilisha"**
**NJB** **"Puuza"**
**NIV** **"Onyesha dharau"**
**NET** **"Kuwa na dharau kwa"**

Kwa kulinganisha tafsiri za Kiingereza wakarimani wanaguswa na upana wa kitenzi katika maana za maneno. Hili ni neno zito kwa kukataa kwa hiari. Tazama matumizi yake katika:

1. Maneno ya Yesu, Mt. 6:24; 18:10
2. Paulo, 1Kor. 11:22; 1Tim. 4:12;6:2
3. Waebrania (wa Yesu), 12:2
4. Petro, 2 Pet. 2:10
5. JINA katika Mdo. 13:41

◙ **"Utajiri wa wema wake, uvumilivu na subira"** wanadamu siku zote wanashindwa kuelewa neema ya Mungu, huruma na uvumilivu na wameyageuza haya kuwa fursa ya kutenda dhambi badala ya kutubu (kama vile 2Pet. 3:9). Paulo daima anaeleza kuwa mema ya Mungu ni kama "utajiri wa " (kama vile 9:23; 11:33; Kol. 1:27; Ef 1:7,18; 2:4,7; 3:8,18; Flp. 4:19). Jina "uvumilivu" limetumika mara mbili tu katika Agano Jipya, mara mbili na Paulo katika andiko lake (1:18-3:31), hapa na 3:26. Yote yakimaanisha uvumilivu wa Mungu kwa watenda dhambi.

◙ **"Hukupeleka katika toba"** Toba ni jambo nyeti kwa mahusiano ya agano la imani na Mungu (kama vile Mt. 3:2; 4:17; Marko 1:15; 6:12; Luka 13:3,5; Mdo. 2:38; 3:16,19; 20:21). Neno hili Kiebrania linamaanisha badiliko katika matendo, wakati Kiyunani linaaanisha badiliko katika mawazo. Toba ni utayari wa kubadilika kwa mtu kutoka katika maisha aliyonayo mtu kwenda kwa maisha ya kumjua Mungu kama anavyoyaelekeza Mungu mwenyewe. Ni wito kwa badiliko kutoka kipaumbele cha matendo ya mtu na kufungwa kwa mtu. Kimsingi ni mwelekeo mpya, mtazamo mpya wa ulimwengu, na bwana mpya. Toba ni nia ya Mungu kwa kila Mwana wa Adamu aliyeanguka, aliyeumbwa kwa sura yake (kama vile Hez.18:21,23, 32 na 2 Pet. 3:9). Habari katika Agano Jipya ambayo hasa inaonyesha maneno tofauti ya Kiyunani kwa toba ni 2 Kor. 7:8-11.

1. *Lupeō* , "fedheha" au "fadhaiko" katika mstari wa 8 (mara mbili), 9 (mara tatu), 10 (mara mbili),11
2. *Metamelomai "*jutia" au "huduma ifuatayo" mstari wa 9,10

Utofati ni toba bandia (*metamelomai)* (kama vile Yuda, Mathayo 27:3 na Esau, Ebr. 12:16-17) dhidi ya toba ya kweli (*metanoeō*). Toba ya kweli kitheolojia imeungana na:

1. Mahuburi ya Yesu katika masharti ya Agano Jipya (kama vile Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 13:3,5)
2. Kupelekwa wa habari ya dini katika Matendo (*kerygma,* kama vile Mdo. 3:16,19,20,21)
3. Zawadi huru ya Mungu (kama vile Mdo. 5:31; 11:18 na 2 Tim 2:25
4. Kuharibika (kama vile 2Pet. 3:9)

Toba sio hiari!

## MADA MAALUMU: TOBA

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la agano la kale (*Nacham,* BDB 636, mf 13:12; 32:12,14; *shuv,* BDB 996, mf 1Kor 8:47; Hez 14:6; 18:30) angalia Mada Maalum: Toba [agano la Kale] na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt 3:2; Marko 1:4; Luk 3:3,8)
2. Yesu (Mt 4:17; Marko 1:15; Lk. 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Mdo. 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Kor 2:9-10)
4. Paulo (Mdo. 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini toba ni nini? Je ni huzuni? Je ni mwisho wa dhambi? Sura bora zaidi katika Agano Jipya kwa kuelewa maana nyinginezo mbalimbali ya dhana hii ni 2Kor 7:8-11, ambapo maneno matatu ya Kiyunani yaliyokaribiana lakini kwa tofauti yanatumika.

5. "Huzuni" (*lupē,* kama vile mstari 8 (mara mbili), 9 (mara tatu), 10 (mara mbili),11). Inamaanisha fadhaiko au kero na lina maana ya kawaida kithiolojia.
6. "Toba" (*metanoeō*, kama vile mstari 9,10). Ni muungano wa maneno mawili "baada" na "fikra", likimaanisha "fikra mpya", njia mpya ya kufikiri, mwenendo mpya wa maisha na Mungu. Hii ndio toba ya kweli.
7. "Majuto" (*metamelomai,* kama vile mstari 8 (mara mbili), 10). Ni muungano wa maneno "baada" na "tunza". Limetumika kwa Yuda katika Mathayo 27:3 na Esau katika Waebrania 12:16-17. Inaonyesha huzuni kwa matokeo siyo juu ya matendo.

Toba na imani ni matendo yanayohitajika kwa agano (kama vile Marko 1:15; Mdo. 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko yanayosema kuwa Mungu hutoa toba (kama vile Mdo. 5:31; 11:18; 2 Tim 2:25). Lakini maandiko mengi huona haya kama ni mwitikio wa lazima wa wanadamu kwa agano la Mungu la kutoa wokovu bure.

Maelezo kwa kifupi kwa maneno yote ya Waebrania na Wayunani yanahitajika ili kupata maaana kamili ya toba. Waebrania wanadai "badiliko la vitendo" wakati Wayunani wanadai "badiliko la fikra". Mtu aliyehudumiwa hupokea fikra mpya na moyo mpya. Hufikiri tofauti na huishi tofauti. Badala ya "kuna nini ndani kwa ajili yangu". Swali sasa linakuwa "ni yapi mapenzi ya Mungu?." Toba siyo mchemko ambao unapotea tu baada ya muda mfupi au kutokuwepo dhambi kabisa, bali ni mahusiano mpya na Yule Mtakatifu, ambayo humbadilisha muumini polepole kuwa mtu mtakatifu. Si sana juu ya kile ambacho mtu ana acha kukitenda au anakiacha bali mwelekeo mpya katika maisha,au lengo jipya. Anguko linatufanya sisi sote kukabiliana na nafsi zetu lakini Injili inaturuhusu kukabiliana na Mungu. Toba ni mgeuko kutoka na Imani ni kugeukia.

**2:5-9** Mistari hii inaeleza (1) ukaidi wa mwanadamu aliyeanguka (2) hasira ya Mungu na hukumu.

**2:5 "Ukaidi"** Neno hili linapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Israeli inaelezwa kwa namna hii katika Kutoka 32:9,33:3,5; 34:9; Kumb. 9:6,13,27 (pia angalia Ebr. 3:8,15; 4:7)

◙ "**Moyo"** Tazama mada maalumu katika 1:24

◙**"Siku ya ghadhabu"** Hii iliitwa "siku ya Bwana" katika Agano la Kale (kama vile Yoeli, Amosi). Hii ni dhana ya siku ya hukumu, au kwa waumini ni "siku ya ufufuo". Mwanadamu lazima atoe ushuhuda kwa Mungu kwa zawadi yake ya maisha (kama vile Mt. 25:31-46; Ufu. 20:11-15).

Tazama ni wa dhambi wenyewe ("wewe" na "wewe mwenyewe") ambao mtaitunza hukumu. Mungu katika hatua Fulani, anairuhusu hukumu hii iwe dhahiri na kuendesha shitaka zima.

Hukumu kama maneno mengine ya binadamu yanayo mweleza Mungu, yanafananishwa na (tabia ya kibinadamu kumwelezea Mungu, tazama mada maalumu katika 1:18) yanatumika kwa miungu. Mungu ni wa milele, Mtakatifu na Roho. Wanadamu ni wa muda, wenye dhambi, na wa kimwili. Mungu hana hasira kama ilivyo ya kwetu, hasira kali. Biblia inamweleza Mungu kama mpenda wadhambi hali ikiwataka tu watubu, lakini pia akiwa na upinzani thabiti dhidi ya maasi ya wanadamu. Mungu ni nafsi, huchukua dhambi kipekee, nasi kipekee tunawajibika na dhambi zetu.

Wazo moja la nyongeza kuhusu ghadhabu ya Mungu. Katika Biblia iko katika nyakati mbili, wakati uliopo (wa muda, kama vile 1:24, 26, 28) na wakati wa mwisho (mambo ya siku za mwisho, kama vile 2:5-8). Siku ya Bwana (siku ya hukumu) ilikuwa kwa upande mmoja wa Mitume wa Agano la Kale waliionya Israel itubu kwa wakati huo ili maisha yao ya mbele yabarikiwe, na siyo kuhukumiwa (kama vile Kumb. 27-28). Mitime wa Agano la Kale walichukulia matatizo ya siku zao kama mwisho wa maisha yao ya mbele.

**2:6** Hii ni hukumu kutoka katika Zaburi 62:12 (kama vile Mt. 16:27). Ni kanuni (Angalia 2:1, aya ya pili) ya kuwa wanadamu wanahusika juu ya matendo yao na watatoa hesabu mbele za Mungu (kama vile Ayub. 34:11, Mithali 24:12, Wimb. 12:14, Yer 1:17, Ufu. 2:23, 20:12, 22:12). Hata waumini watatoa hesabu ya maisha yao na utumikaji wao kwa Kristo (kama vile 2Kor 5:10). Waumini hawaokolewi kwa juhudi ya kazi zao bali huokolewa ndani ya kazi (kama vile Efe. 2:8-10 [hasa 2:14-26]; Yakobo na Yohana). Maisha yaliyobadilika na kubadili maisha ya upendo, huduma, na utoubinafsi ni uthibitisho wa wokovu wa kweli.

**2:7 "Kwa wale ambao"** Kuna tofauti kati ya watu walioelezwa katika mstari wa 7 na wale wa mstari wa 8 ("lakini kwa wale ambao").

◙

**NASB "Kwa wale ambao kutokana na uvumilivu wao katika kutenda mema, wanatafuta utukufu na heshima, maisha ya milele"**

**NKJV "Maisha ya milele kwa wale ambao kwa uvumilivu unaoendelea kwa kufanya mema hutafuta utukufu, heshima na maisha marefu.**

**NRSV "Kwa wale ambao kwa kuvumilia kutenda mema hutafuta utukufu na heshima na maisha marefu, atawapa maisha ya milele.**

**TEV "Watu wengine huendelea kutenda mema, na kutafuta utukufu, heshima na maisha endelevu; kwa hao Mungu atawapa maisha ya milele.**

**NJB "Kwa ajili ya wale ambao walitafuta kujulikana na heshima na maisha marefu daima wakitenda mema patakuwa na maisha ya milele.**

Hii ilizungumzia watu kama Kornelio (kama vile Mdo. 10:34 -35). Habari hii inaweza kueleweka kama haki ya matendo (kupata haki kupitia juhudi za mtu). Lakini hii itakuwa kinyume na dhima kuu ya kitabu cha Warumi.

Kumbuka kuwa mistari ya 1-16 au 1-11 ni aya. Wazo la kithiolojia hapa lina maana kuwa, Mungu sio wa kuheshimu watu (mstari 11) na kwamba wote wametenda dhambi (mstari 12) na kama watu wanaishi kwa uelewa waliokuwa nao (ufunuo wa asili kwa mataifa, na ufunuo maalumu kwa Wayahudi, kama vile 10:5), hivyo basi wangekuwa vizuri na Mungu. Hata hivyo, majumuisho ya 3:9-18, 23 yanaonyesha ya kuwa hakuna hata mmoja anaweza au wataweza.

Maisha ya Ki-Mungu ya mwamini yaliyobadilika yanaonekana kuthibitika, kuthaminisha hatua za mwanzo za kupokea imani. Maisha yaliyobadilika ni ushahidi wa kuishi ndani kwa Roho wa Mungu (ona mistari ya 10,13; Mt. 7, Efe. 2:8-10, Yak. 2:14-26 na 1Yohana). Angalia mada maalumu: haja ya kuvumilia katika 8:25.

◙"**Maisha ya Milele"** Hii ni namna ya usemi katika maandiko ya Yohana na linatumika mara chache katika ufupisha wa injili. Inaonekana Paulo alitoa usemi huu katika Daniel 12:2 (kama vile Tit. 1:2; 3:7), ampapo inaonyesha maisha ya enzi mpya, maisha katika ushirika na Mungu, maisha ya ufufuo. Kwanza analitumia katika Wagalatia 6:8. Ni dhima muhimu katika sehemu ya imani ya Waroma (kama vile 2:7, 5:21,6:22,23) na pia inaonekana mara kadhaa katika nyaraka za kichungaji (kama vile 1Tim. 1:16, Tit. 1:2; 3:7)

◙

**2:8**
**NASB "Wale wenye uchu wa ubinafsi"**
**NKJV, NRSV "Wale ambao wanatafutia nafsi zao"**
**TEV "Watu wengine ni wabinafsi"**
**NJB "Wasioishi kwa wivu"**

Neno awali linamaanisha "kazi ya kukodi" (kama vile Tob. 2:11).

Louw na Nida, *Greek-English Lexicon,* juzuu ya 2, ukr. 104, inaorodhesha matumizi mawili ya neno hili.

1. "Uchu wa ubinafsi", kwa kutumia Warumi 2:8 inaonyesha "kutaka kuwa mtu bora kuliko wengine" ambalo linafaa kwa dhana hii.
2. "Ukatili", kwa kutumia Wafilipi 1:17 wakinukuu "mashindano" kama tafsiri ya nyongeza (angalia 2 Kor 12:20, Gal. 5:20; Flp. 2:3; Amo. 3:14,16)

◙ **"Na usitii ukweli",** Neno "ukweli" (*aletheia)* lilitumika katika maana ya Kiebrania (*emeth)* ukweli na kusadiki. Katika eneo hili, lilikuwa na mtazamo wa kidesturi zaidi, kuliko usomi, ama mtazamo. Tazama mada maalumu: Ukweli katika maandiko ya Paulo 1:18.

**2:9 "Kwa kila nafsi ya mtu",** Paulo alitumia neno la Kiyunani *pas* lililotafsiri "wote" au "kila" mara nyingi katika sura hizi za mwanzo katika Warumi kuonyesha maana ya jumla ya maneno "habari mbaya" (upotevu wa wanadamu na hukumu ya Mungu isiyopendelea) na "habari njema" (zawadi ya Mungu ya wokovu wa bure na msamaha kamili katika Kristo kwa wote wanaotubu na kuamini).
Haja hii kwa nguvu kabisa inaonyesha hukumu ya jumla na madhara yake. Ukweli huu unataka ufufuo wa wote wenye haki na wenye dhambi (Kumb. 12:6; Yoh. 5; 28-29, Mdo. 24:15). Kama mstari wa 6-11 ni alama mkato kwa hiyo, mistari ya 8-9 ni mistari muhimu ambayo inaonyesha hukumu au watenda maovu.

**2:9-10 "Wayahudi kwanza",** Hii inadaiwa kwa msisitizo. Wayahudi kwanza walikuwa na fursa kwa vile walikuwa na ufunuo wa Mungu (kama vile 1:16; Mt. 10:6; 15:24; Yoh. 4:22; Mdo. 3:26; 13:46), lakini pia kwanza katika hukumu (kama vile 9-11) kwa sababu walikuwa na ufunuo wa Mungu.

◙

**2:11**
**NASB, NKJV "Kwa vile hakuna upendeleo kwa Mungu"**
**NRSV "Kwa vile Mungu haonyeshi upendeleo"**

**TEV** "Kwa vile Mungu anahukumu watu kwa kiasi kilekile"
**NJB** "Hakuna upendeleo kwa Mungu"

Kimantiki hii ni "kuinua uso", ambao ulikuwa ni usemi kwa namna nyingine kutoka katika mfumo wa kisheria wa Agano la Kale (kama Law. 19:15; Kumb. 10:17; 2 Nya.19:7; Mdo. 10:34; Gal. 2:6; Efe. 6:9; Kol. 3:25; 1 Pet 1:7), kama mwamuzi aliona kuwa, wakati anatoa haki palikuwa na upenyo wa upendeleo, kwa hiyo hakutakiwa kuinua uso wa yeyote aliyesimama mbele yake.

## MADA MAALUM:UBAGUZI WA KIMBARI

I. Utangulizi
   A. Tabia hii ya kujikuza ni ya watu wote kwa wanadamu walioanguka katika jamii, huu ni ubinafsi wa mwanadamu ili kujilinda kwa wengine, ubaguzi wa mataifa kwa namna mbalimbali, na kauli ya sasa wakati utaifa (au ukabila) ni mtindo wa kizamani.
   B. Utaifa ulianzia Babeli (Mwanzo 11) na mwanzoni ulihusishwa na wana watatu wa Nuhu ambapo neno hili mataifa lilitokana kwalo (kama vile Mwanzo 1-3; Matendo 17:24-26).
   C. Ubaguzi wa mataifa ni mojawapo ya aina nyingi za uonevu
      1. Kutukuza elimu
      2. Ujivuni wa kijamii na kiuchumi
      3. Uhalalisho wa haki binafsi ya kidini
      4. Msimamo usiobadilika wa kuingiza dini katika siasa
II. Matini ya Biblia
   A. Agano la Kale
      1. Mwa. 1:27 –wanadamu jinsi ya kiume walifanywa kwa taswira na mfano wa Mungu, vitu vinavyomfanya awe wa pekee kuonesha pia uthamani wa mtu na hadhi/ utu (kama vile Yohana 3:18)
      2. Mwanzo 1:11-25- inaandika fungu, "… baada ya jinsi yao…" mara kumi. Hii imetumika kusaidia utenganisho wa mataifa. Hata hivyo ni wazi kutokana na mazingira, hii inamaanisha kwa wanyama na mimea na sio kwa watu.
      3. Mwa. 9:18-27- Hii imetumika kusaidia utawala wa mataifa. Ikumbukwe kwamba Mungu hakulaani kanani. Nuhu, ambaye ni baba yake, alimlaani kanani baada ya kuzinduka kutoka kwenye ulevi wa pombe. Biblia haioneshi kuwa Mungu alithibitisha kiapo/laana. Hata kama alifanya hivyo haiwaathiri watu weusi. Kaanani alikuwa ni baba wa wote wale waliokuwa wakiishi Palestina na kuta za Misri zilizokuwa zimechorwa zinaonyesha kuwa hawakuwa weusi.
      4. Yoshua 9:23- Hii imetumika kuhakiki kuwa taifa moja litatumikia lingine. Hata hivyo katika uhalisia wa Gibeoni ni wa asili moja na Wayahudi.
      5. Ezra 9-10 na Nehemia 13- Hivi vimetumika kwa maana ya mataifa, lakini kiuhalisia inaonesha kuwa ndoa zilikuwa zimekatazwa, sio kwa sababu ya mataifa (walitoka kwa kaka mmoja Nuhu Mwanzo 10) lakini kwa misingi ya kidini.
   B. Agano Jipya
      1. Injili
         a. Yesu alitumia hali hii ya chuki kati ya Wasamaria na Wayahudi katika mifano kadhaa ambayo ilionesha kuwa ubaguzi wa kimataifa haufai.
            1) Fumbo la Msamaria mwema (Luka 10:25-37)
            2) Mwanamke kisimani (Yohana 4)
            3) Mgonjwa wa ukoma aliyeshukuru (Luka 17:11-19)
         b. Injili ni kwa watu wote
            1) Yohana 3:18
            2) Luka 24:46-47

3) Waebrania 2:9
4) Ufunuo 14:6

c. Ufalme utawajumuisha wanadamu wote
1) Luka 13:29
2) Ufunuo 5

2. Matendo
   a. Matendo 10 ni habari kamili kuhusu upendo wa Mungu kwa ulimwengu wote na ujumbe wa injili kwa walimwengu wote.
   b. Petro alishambuliwa kwa vitendo vyake katika Matendo 11 na tatizo lake halikutatuliwa hadi baraza la Yerusalemu katika matendo 15 lilipokutana na kupata ufumbuzi. Mvutano kati ya Wayahudi wa Karne ya kwanza na wapagani ulikuwa umezidi.
3. Paulo
   a. Hakuna Vipingamizi/vizuizi katika Kristo.
      1) Gal. 3:26-28
      2) Efe. 2:11- 22
      3) Kor. 3:11
   b. Mungu haitii watu
      1) Rum. 2:11
      2) Efe. 6:9
4. Petro na Yakobo
   a. Mungu hatii watu (1 Petro 1:17)
   b. Kwasababu Mungu haoneshi upendeleo, vivyo hivyo watu wake Yakobo 2:1
5. Yohana
   a. Mojawapo ya maelezo marefu kuhusu uwajibikaji wa waamini yanaonekana katika 1 Yohana 4:20.

III. Hitimisho

A. Ubaguzi au kwa maana hiyo, uonevu wa aina yoyote haufai kabisa kwa watoto wa Mungu. Hapa kuna nukuu kutoka kwa Henlee Barnette aliyezungumza katika mkutano/kikao Glorieta New Mexico katika kamisheni ya maisha ya mkristo mwaka 1964. “Ubaguzi ni imani dhidi ya dini kwa sababu si wa kibiblia wala Kikristo wala wa kisayansi”.

B. Suala hili linawapa Wakristo fursa ya kuonesha upendo wao wa Kikristo msamaha na uelewa kuhusu ulimwengu uliopotea kuja kwa Kristo.

C. “Nifanye nini” (Sehemu hii inatolewa katika kamisheni ya maisha ya Mkristo iitwayo “mahusiano ya mataifa”)

“KATIKA KIWANGO CHA MTU”

★ Kubali kuwajibika binafsi katika kutatua matatizo yanayohusiana na taifa.
★ Kupitia maombi, kusoma biblia na kushirikiana na mataifa mengine na kupambana na maisha ya uonevu wa mataifa mengine.
★ Elezea msimamo wako kuhusu ushindani uliopo, hasa pale waliochochea ushindani wa chuki hawakupingwa

“KATIKA MAISHA YA FAMILIA”

★ Tambua umuhimu wa athari ya familia katika kueneza tabia kwa mataifa mengine.
★ Jaribu kuendeleza tabia za Kikristo kwa kuzungumza juu ya kile ambacho watoto na wazazi wanasikia kuhusu maswala ya mataifa nje ya nyumbani kwao.
★ Wazazi wanapaswa kuwa waangalifu kwa kuonesha mifano ya mienendo ya Kikristo kwa kuhusiana na watu wa mataifa mengine
★ Tafuta fursa kufanya urafiki wa kifamilia kwa watu wa mataifa yote.

"NDANI YA KANISA LAKO"

- ★ Kwa mahubiri na mafundisho ya ukweli wa Biblia kuhusiana na mataifa, mkutano unaweza kuhamasisha kuonesha mfano kwa jamii nzima.
- ★ Uwe na uhakika kuwa, ibada, ushirikiano na huduma kupitia kanisani viko wazi kwa wote hata vile ambavyo makanisa ya Agano Jipya yalivyoona kutokuwepo kwa vizuizi vya kimataifa (Efe. 2:11-22 Wagalatia 3:26-29)

KATIKA MAISHA YA KILA SIKU"

- ★ Saidia kuondoa ubaguzi wa kimataifa wa aina zote katika ulimwengu wa kazi.
- ★ Fanya kazi kupitia katika taasisi za kijamii za aina zote ili kupata haki sawa na fursa ukikumbuka kuwa ni tatizo la kimataifa linalotakiwa kushambuliwa, na sio watu, lengo ni kukuza uelewa na sio kuunda machungu.
- ★ Ikionekana inaunda kamati maalumu za wananchi walengwa kwa lengo la kufungua njia za mawasiliano katika jamii kwa ajili ya kuwaelimisha wote katika mambo na vitendo maalumu katika kuboresha mahusiano ya mataifa.
- ★ Saidia vyombo vya sheria na watunga sheria katika kupitisha sheria, kukuza haki za kimataifa na kupinga wale karibu haki kwa faida za kisasa.
- ★ Pendekeza mtumiaji wa maarifa wa sheria kuitumia bila upendeleo.
- ★ Epusha vurugu na hali ya kuheshimu sheria ili kufanya uwezekano wa mambo wa mambo kwenda sana kama raia Mkristo hakkikisha kuwa mfumo wa kisheria haitumiki kama vyombo vya kuwawezesha wanaojenga ubaguzi.

Onesha mfano wa roho na fikra za Kristo kwa mahusiano yote ya wanadamu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:12-16**
**12Kwa kuwa wote waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheria, na wote waliokosa, wenye sheria,**
**watahukumiwa kwa sheria. 13Kwa sababu sio wale waisikiao sheria walio wenye haki mbele za Mungu, bali**
**ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki. 14 Kwa maana watu wa mataifa wasio na sheria**
**wafanyapo kwa tabia zao yalio ndani ya torati, hao wasio na sheria wamekuwa sheria kwa nafsi zao**
**wenyewe. 15Hao waionyesha kazi ya torati iliyoandikwa mioyoni mwao, dhamiri yao ikiwashuhudia, na**
**mawazo yao, yenyewe kwa yenyewe, yakiwashitaki au kuwatetea; 16Katika siku ile Mungu**
**atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu.**

**2:12 "Kwa wale wote waliotenda dhambi pasipo sheria"** Mungu atawajibisha watu wote hata wale ambao bado hawajapata kusikia Agano la Kale au injili. Watu wote wana angalau ufahamu wa Mungu kutokana na uimbaji na ile maana ya asili ya kuzaliwa nayo (kama vile 2:14-15). Jambo hili zaidi ni kwamba wote wamehiari kuasi yale wanayoyafahamu (kama vile 1:21-23; 3:9,19, 23; 11:32; Gal. 3:22)

◙ **"Sheria"** Hakuna makala yenye neno "sheria." Muundo huu sanifu kwa kawaida unasisitiza sifa ya neno. Hata hivyo katika Warumi, Paulo anatumia neno "sheria" kumaanisha vitu kadha wa kadha.

1. Sheria ya Warumi
2. Sheria ya Musa
3. Dhana ya desturi za jamii kwa ujumla

Mtindo, na siyo makala, lazima udhihirishe ni ipi. Mtindo huu unasisitiza kuwa, binadamu wote wana ufahamu kiasi wa mafunuo ya asili ya Mungu mwenyewe katika roho zao (kama vile mstari 15).

**2:13 "Kwa vile siyo tu wasikiao sheria ambao wako mbele ya Mungu"** Neno "wasikiao" linaweza kumaanisha (1) Matumizi ya viongozi wa dini ya Kiyahudi lenye maana kwa wanafunzi wa masomo ya uongozi wa dini ya Torah, au (2) Waliosikia mafundisho katika masinagogi. Kumbuka waandishi wa Agano Jipya walikuwa Waebrania wenye

fikra kubwa walioandika huko Koine Ugiriki. Kwa hiyo, uchambuzi wa neno lazima uanze ngano za kale na sio misamiati ya Kiyunani.

Neno “haki” au “kufanywa haki” (*dikē* katika namna zake zote) ni neno muhimu katika theolojia ya Paulo (kama vile 3:4, 20,24,26,28,30; 4:2,5; 5:1,9; 6:7; 8:30,33). Maneno “haki”, “kuhesabiwa haki”, “hali ya kuwa katika haki” na “kuwa haki” yanatoka katika neno *dikaios.* Tazama mada maalumu: haki katika 1:17. Katika Kiebrania (*isadag,* BDB 843) awali lilimaanisha gome refu la mti lililonyooka (futi 15 hadi 20) lililotumika kupima vitu kama , ukuta au uzio, kwa timanzi. Likaja kutumika kama neno mbadala la Mungu kama kipimo cha uamuzi wa haki.
Katika maandiko ya Paulo neno hilo lilikuwa kwa mitizamo miwili. Kwanza, haki ya Mungu inapewa watenda dhambi kama zawadi huru kwa imani ya Kikristo. Hii daima huitwa haki ya mtu iliyohalalishwa. Hii inamaanisha kusimama mbele ya Mungu mwenye haki. Hii ndiyo asili ya utendaji wa Paulo kutokana na “haki ya neema kupitia imani”.

Pili, kitendo cha Mungu cha kumrejesha mwanadamu aliyetenda dhambi kwa sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27) au kuweka kwa namna nyingine, kurejesha hali kwa mfano wa Kristo. Mstari huu- kama Matayo 7:24; Luka 8:21 na 11:28; Yohana 13:17; Amosi 1:22-23,25 inawahimiza waumini wawe watendaji na sio wasikilizaji tu. Uhalalisho wa haki lazima ulete matokeo ya haki ya kuishi. Mungu husamehe na kubadilisha watenda dhambi. Matumizi ya Paulo yalikuwa halali na adilifu. Agano Jipya linampa binadamu haki ya kusimama, lakini pia linadai mwenendo wa maisha Kimungu ni bure, lakini pia linagharimu.

◙ **”Lakini watendaji wa sheria”** Mungu anahitaji mwenendo mpya wa maisha wenye utii (kama vile Ebr. 18:5; Mat 7:24-27; Luka 8:21; 11:28; Yoh 13:17; Yak. 1:22-25; 2:14-28). Kwa njia nyingi, dhana hii inafanana na neno la Kiebrania *shema* (BDB1033), lililomaanisha kusikia kwa nia ya kutenda (kama vile Kumb. 5:1; 6:4; 9:1; 20:3; 27:9-10).

◙

**2:14**

**NASB “Kwa vile pale watu wa mataifa ambao hawajapata kujua sheria, wanafanya mambo ya sheria, hawa, wasio na sheria, ni sheria wao wenyewe.**

**NKJV “Kwa vile watu wa mataifa ambao hawana sheria kwa asili ya kuzaliwa wanafanya mambo yaliyo ndani ya sheria, hawa, ingawa hawana sheria, wao ni sheria kwa wao wenyewe”**

**NSRV “Wakati watu wa mataifa ambao hawana sheria, hufanya kile ambacho. Sheria inahitaji, japo hawana sheria, wao ni sheria kwa wenyewe**

**TEV “Watu wa mataifa hawajui sheria, lakini wawapo huru wenyewe, hufanya sheria inachohitaji, wao ni sheria kwa wenyewe, hata kama wao hawana sheria.**

**NJB “Kwa mfano, wapagani ambao hawajapata kusikia sheria, lakini wanaongozwa, bila shaka ‘hawana sheria’, lakini wanaweza kusemwa kuwa wao ni sheria.**

Tamaduni zote zina sheria ndani mwao, desturi za jamii. Zinawajibika kwa hayo wanayoyaelewa (kama vile 1 Kor 9:21). Mstari huu haukukusudiwa kumaanisha kuwa wanaweza kuwa sawa na Mungu kama wataishi kwa uwelewa wa tamaduni zao, bali wanawajibika kwa Mungu kwa maarifa ya kuzaliwa.

**2:15 “Dhamiri zao zikiwashuhudia, na mawazo yao yakiwatuhumu au kuwalinda”** Kuna sauti ya kutoka ndani. Lakini ni maandiko pekee, yaliyoeleweshwa na Roho yanaweza kuaminiwa kikamilifu. Kuanguka kwetu kumeathiri dhamiri zetu. Hata hivyo uumbaji (1:8-20) na sheria adilifu ya ndani (2:14-15) vyote ni ufahamu wa Mungu ambao watu wengine wanao. Hapakuwepo na neno la Kiebrania lenye kufanana na neno la Kiyunani “dhamiri” (*syneidesis)*. Dhana ya Wayunani ya hali ya ndani ya utambuzi wa jema na baya daima ulijadiliwa na wanafalsafa wa Stoic. Paulo alikuwa na mazoea ya wanafalsafa wa Kiyunani (anamnukuu Cleanthe katika Mdo.17:28; Menanda

katika 1 Kor. 15:33; na Epimenida katika Tit. 1:12) kutoka katika elimu yake ya awali huko Tarshishi. Mji wa nyumbani kwao ulijulikana kwa mashule mazuri mno ya falsafa.

**2:16 "Katika siku"** Angalia dokezo katika 2:5.

◙ **"Kufuatana na injili yangu"** Katika maandiko haya yanaelezea mahubiri ya Paulo juu ya ufunuo wa Kristo Yesu. KIWAKILISHI "yangu" kinaelekeza uelewa wa Paulo wa utumishi wake wa injili ulioaminiwa juu yake (kama vile 16:25; 1Kor. 15:1; Gal. 1:11; 1Tim. 1:11; 2Tim. 2:8). Haikuwa yake pekee, lakini kama Mtume kwa watu wa mataifa alisikia hali ya huruma ya ndani ya uwajibikaji kwa kuieneza kweli kuhusu Yesu katika ulimwengu wa Warumi.

◙**"Mungu atazihukumu siri za wanadamu"** Mungu anajua mioyo wa watu wote (kama vile 1 Sam 2:7; 16:7; 1Fal 8:39; 1 Nyak. 28:9; 2 Nyak. 6:30; Zab. 7:9; 44:21; 139:1-6; Mith.15:11; 21:2; Yer. 11:20;17:10; 20:12; Luka 15:16; Mdo. 1:24; 15:8; Rum. 8:27; Ufu. 2:23). Baba, kupitia wakala wa mwanaye, ataleta sababu na matendo katika mapitio ya kisheria (kama vile Mt. 25: 31-46; Law. 20:11-15).

◙ **"Kupitia kwa Yesu Kristo"** Yesu hakuja kufanya kazi ya kuhukumu (kama vile Yoh. 3:17-21). Alikuja kumdhihirisha Baba yake, akafa kifo mbadala kwa ajili yetu, na kuwapa waumini mifano ya kufuata. Watu wanapomkana Yesu wanajihukumu wenyewe.
Hata hivyo, Agano Jipya halifundishi kuwa Yesu atafanya uakilishi wa Babaye kama hakimu (kama vile Yoh. 5:22,27; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Tim 4:1). Mvutano wa Yesu kama jaji au mwokozi unaonekana katika injili ya Yohana (kama vile 3:17-21 dhidi ya 9:39)

**ANDIKO NASB (LILILOBORESHWA): 2:17-24**
**[17]Lakini wewe, ukiwa unaitwa Myahudi na kuitegemea torati, na kujisifu katika Mungu, [18]na kuyajua mapenzi yake, na kuyakubali mambo yaliyo bora, nawe umeelimishwa katika torati, [19]na kujua hakika ya kuwa wewe mwenyewe u kiongozi wa vipofu, mwanga wao wlio gizani, [20]mkufunzi wa wajinga, mwalimu wa watoto wachanga, mwenye namna ya maarifa na ya kweli katika torati; [21]basi wewe umfundishaye mwingine, je! Hujifundishi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, waiba mwenyewe? [22]Wewe usemaye kwamba mtu asizini, wazini mwenyewe? Wewe uchukiaye sanamu wateka mahekalu? [23]Wewe ujisifuye katika torati, wamvunjia Mungu heshima kwa kuiasi torati? [24] kwa maana jina la Mungu latukanwa katika mataifa kwa ajili yenu, kama ilivyo andikwa.**

**2:17 "Kama"** Hii ni SENTESI YA MASHARTI YA DARAJA LA KWANZA, ambayo inasemekana kuwa ya kweli kutokana na maoni ya mwandishi au kwa makusudi ya maoni yake. Sharti hili linaendelea hadi mstari wa 20, lakini halina hitimisho, kwa hiyo TEV inalitafasiri kama ni udhihirisho wa kufikirika ungefanywa na Yesu. Wayahudi walikuwa wanaamini katika uzao, tamaduni, utendaji ili kuleta wokovu (kama vile Mt. 3:9; Yoh. 8:33,37,39)

◙ **"Kujivuna katika Mungu"** Wayahudi wengi walikuwa wanategemea (1) uzao wao wa taifa la Ibrahim, na (2) utendaji wao binafsi wa sheria ya Musa kama njia ya kukubaliwa na Mungu. Hata hivyo, haki ya uhalali wao uliwatenga kutoka kwa Mungu (kama vile Mt. 5:20; Gal. 3). Ni jambo la ajabu kiasi gani? Paulo anatazama wazo la kujivuna katika 1 Wakorintho. Paulo anakabiliana na Waisraeli na Wayunani wenye kujivuna kielimu. Mstari wa mwisho unaonyesha hakuna mwenye mwili atatukuka mbele za Mungu.

## MADA MAALUM: MAJIVUNO

Haya maneno ya Kiyunani, *kauchaomai, kauchēma*, na *kauchēsis*, yametumiwa na Paulo mara therathini na tano na mara mbili tu katika kitabu vya Agano Jipya (yote katika kitabu cha Yakobo). Matumizi yake yaliyozidi yanapatikana katika 1 na 2 Wakorintho.

Kuna kweli kuu mbili zilizohusishwa kwenye majivuno.

A. Hapana mwili utakao jisifu/kujivuna mbele za Mungu (kama vile. 1 Kor. 1:29; Efe. 2:9)
B. Waamini wanapaswa kujisifu katika Bwana (kama vile. 1 Kor. 1:31; 2 Kor. 10:17, ambalo ni dokezo kwa Yer. 9:23-24)

Kwa hiyo, kuna majivuno yenye kustahili na yasiyo stahili (yaani., kiburi)

A. Majivuno yanayo stahili
   1. Katika tumaini la utukufu (kama vile Rum. 4:2)
   2. Katika Mungu kupitia mwanaye Yesu Kristo (kama vile Rum. 5:11)
   3. Katika msalaba wa Bwana Yesu Kristo (yaaani., dhamira kuu ya Paulo, kama vile 1 Kor. 1:17-18; Gal. 6:14)
   4. Paulo anajivuna katika
      a. Huduma yake isiyo na fidia (kama vile 1 Kor.9:15,16)
      b. Mamlaka yake kutoka kwa Kristo (kama vile. 2 Kor. 10:8,12)
      c. kutojisifu kwake katika kazi ya wengine (kama baadhi huko walivyokuwa, kama vile 2 Kor. 10:15)
      d. urithi wa kijamii 2:Kor.(kama wengine walivyokuwa wakifanya huko Korintho , kama vile. 2 Kor. 11:17; 12:1,5,6)
      e. Makanisa yake
         1) Korintho (2 Kor. 7:4,14; 8:24; 9:2; 11:10)
         2) Thessalonika (kama vile. 2 The. 1:4)
         3) Kujiamini kwake katika faraja ya Mungu na ukombozi (kama vile. 2 Kor. 1:12)
B. Majivuno yasiyo stahili
   1. Katika kuhusiana na urithi wa Kiyahudi (kama vile. Rum. 2:17-23; 3:27; Gal. 6:13)
   2. Baadhi katika kanisa Korintho walikuwa wakijivuna
      a. Katika Watu (kama vile. 1 Kor. 3:21)
      b. Katika hekima (kama vile. 1 Kor. 4:7)
      c. Katika uhuru (kama vile. 1 Kor. 5:6)
   3. Walimu wa uongo walijaribu kujivuna ndani ya kanisa huko Korintho (kama vile. 2 Kor. 11:12)

**2:18 "Kuidhinisha"** Hiki ni KITENZI cha Kiyunani *dokima*zō KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO. Angalia mada maalumu ifuatayo juu ya kujaribiwa.

## MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO JARIBU NA VIDOKEZO VYAKE VINGINE

Kuna maneno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumjaribu mtu kwa kusudi fulani.

1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

   Neno hili ni neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale).

   Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya
   a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
   b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
   c. imani yetu – Yakobo 1:3
   d. hata Mungu –Ebr. 3:9

   Matokeo ya majaribu hayajafikiriwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7;

Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

a. kuwa wa thamani
b. kuwa wazuri
c. kuwa halisi
d. kuwa wa maana
e. kuwa wa kuheshimiwa

*2. Peirazō, Peirasmus*

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
c. Matumizi
    1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mt. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
    2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).
    3) Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

◙ **"Sheria"** Mstari 17 na kuendelea. Inashughulika na Wayahudi, hivyo neno 'sheria', litamaanisha sheria ya Musa. Hii inathibitishwa na mstari wa 25 unaoshughulika na tohara.

**2:18-20** Viongozi wa Kiyahudi waliamini njia yao (imani zao za Kiyahudi) ilikuwa njia sahihi, njia pekee kwenda kwa Mungu. Walijiaminisha kuwa wao ndio walimu wa kweli kuhusu mambo ya kidini (kama vile Mt. 15:14).
Masilahi husababisha uwajibikaji (kama Luka 12:48)
Tazama mafungu sambamba yanayohusiana na kujiamini kwao (kama vile Mt. 15:14; 23:16,24; Luka 6:39).

1. Mwongozo kwa kipofu, mstari 19
2. Mwanga kwa walio gizani, mstari 19
3. Sahihisho kwa wajinga, mstari wa 20
4. Mwalimu wa wasio pevuka, mstari wa 20
5. Kuweka katika sheria maarifa na ukweli wa kushikamanika, mstari wa 20

**2:21-24** Kama mtu anajiamini katika utii, basi utii huo sharti uwe timilifu (kama vile Mt. 5:20,48; Gal. 3:10, ambayo ni nukuu kutoka katika Kumb.27:26 na Yak. 2:10). Hili ni jambo lisilowezekana la mwandamu aliyeanguka. Paulo anawauliza maswali wasomaji/wasikilizaji wake wa Kiyahudi katika mstari wa 21-23.

**2:22** Ni vigumu kufahamu Paulo alikuwa analemga nani katika mistari ya 22-23. Kwa vile maelezo hayawalengi Wayahudi wa siku za Paulo, inawezekana dhambi hizi zinatumika kwa namna ya kiroho sawa na jinsi Yesu alivyotafasiri sheria katika Mathayo 5:20-48. George Ladd katika *A Theology of the New Testament,* anasema "Paulo alikuwa ana maana ya kumpora Mungu heshima yake, udanganyifu wa kiroho, kudharau kujitoa kwa Mungu pekee kwa kujikweza wao wenyewe kama hakimu na Bwana kwa viumbe wenzao Ukurasa wa 505.

**2:22 "Chukizo la sanamu"** Kugeukia mbali kutoka kwa kitu kutokana na harufu mbaya ndio maana ya msingi wa neno hili.

◙**"Je unapora Hekalu"** Hakuna uhakika kihistoria na kile kilichomaanishwa, lakini kwa kiasi fulani kulihusiana na kuabudu sanamu.

**2:23 "Kujivuna"** Angalia Mada maalumu majivuno katika 2:17

**2:24** Hii ni nukuu kutoka katika Isaya 52:5 katika vitabu vya (Ngano za kale). Baraka za Mungu kwa Israeli kwa ajili ya kutunza Agano (kama vile Kumb.27-28) ilikuwa na maana ya kuwa shahidi kwa ulimwengu. Hata hivyo, Israeli haikutunza agano hili, kwa hiyo, ulimwengu ukatizama tu hukumu ya Mungu (kama vile Ezek. 36:22-32). Israel ilitakiwa kuwa ufalme wa makuhani (kama vile Kut. 19:5-6), kufanya ulimwengu wote kuwa na imani katika YHWH (kama vile Mwa. 12:3; Efe. 2:11-3:13), angalia Mada Maalumu: Ubaguzi wa Bob wa Kiinjilisti katika 1:5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2:25-29**
**25 Kwa maana kutahiriwa kwafaa kama ukiwa mtendaji wa sheria, lakini ukiwa mvunjaji wa sheria kutahiriwa kwako kumekuwa kutotahiriwa. 26 Basi ikiwa yeye aliyetahiriwa huyashika maagizo ya torati, je! Kutokutahiriwa kwake hakutahesabiwa kuwa kutahiriwa? 27 na yeye asiyetahiriwa kwa asili, aishikaye torati, je! Hatakuhukumu wewe, uliye na kutahiriwa, ukaihalifu torati? 28 Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ye nje tu katika mwili; 29 bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani, na tohara ni ya moyo, katika roho, si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu.**

**2:25"Tohara"** Paulo bado anatumia lugha yake ya mashambulizi. Mtu atasema kuwa, angalau tumetahiriwa (kama vile 17:10-11). Tumo katika ukoo wa Ibrahimu. Paulo waziwazi anaharibu dai hili la Wayahudi (kama vile Mt. 3:7-10; Yoh. 8:31-39). Majirani wote wa Waisrael isipokuwa Wafilisti walitahiriwa. Halikuwa lenyewe tendo muhimu; ni imani endelevu ya aliyepokea (kama vile mistari ya 26-27; Kumb. 10:16; 30:6). Hivi ndivyo lilivyo kwa matambiko ya kidini. Watu wa dini daima huhitaji wapate Baraka za agano la Mungu lakini wao bila kuwajibika.

**2:25-26 "Kama…..kama…..kama"** Hizi ni SENTESI SHIRIKISHI INAYOONYESHA KITENDO KITAKACHOTOKEA BAADAYE ambazo hurejea uwezekano wa matendo yajayo. Utii (kama vile Kumb. 27-30) ni ufunguo katika hoja ya Paulo katika sura ya 2, lakini sio katika 3:21-31 (kama vile Gal. 3). Utii ni matokeo ya wokovu lakini neema ndiyo msingi (kama vile Efe. 2:8-10).

**2:26-27** Mistari hii inaleta matumaini kuwa baadhi ya watu wa mataifa wamepokea mwanga walio nao (lugha sanifu inatarajia jibu la "ndiyo" katika mstari wa 26). Mfano pekee wa biblia kwa hili ungekuwa Kornelia wa Matendo 10. Bado hakufaa vizuri katika mstari huu kwa vile alikuwa akimwogopa Mungu na aliabudu katika sinagogi la kwao. Mistari hii kusema kweli ni hoja inayopinga hoja ya Paulo kuhusu mahitaji ya wokovu kwa Wayahudi. Warumi 3:23 ni majumuisho ya kwamba, wanadamu wote bila Kristo wamepotea kiroho. Kama kuna watu wa mataifa wanaoishi kwa mwanga huu wa kumjua Mungu kutokana na uumbaji na utambuzi kutoka ndani mwao, Mungu atawapa fursa ya kumpokea Kristo-kwa vyovyote vile, kwa njia nyingine, kwa wakati fulani.

**2:28-29 "Kwa vile yeye si Myahudi………yeye ni Myahudi"** Huu ni mjadala muhimu sana kwa vile baadhi ya makundi ya wanathiolojia yanajaribu kutenga au kufunika watu wa Mungu wa agano la kale na agano jipya. Kuna agano moja tu na watu wamoja (kama vile Rum. 9:6; Gal. 3:7-9,29; 6:16; 1 Pet. 3:6). Agano jipya ni mwendelezo na utimilifu wa agano la kale. Watu wa Mungu wamekuwa hivyo kwa imani na sio koo zao. Ni "watu wa moyo" na sio wa matambiko na utaifa. Imani, na sio mzazi ndio ufunguo. Fikira za agano, na sio dalili za agano, ndio alama.

◙**"Mwili"** Angalia mada maalumu katika 1:3

**2:29** Alama ya agano la tohara (kama vile Mwa. 17:14) ilikuwa ni sitiari katika agano la kale la uwazi wa mtu wa Mungu. Ilijionyesha katika njia kadhaa

1. Tohara ya rohoni (kama vile Kumb. 10:16; Yer. 4:4; 9:24-25)
2. Tohara ya masikio (kama vile Yer. 6:10)
3. Tohara ya kinywa (kama vile Kut. 6:12,30)

Sheria haikukusudiwa kuwa tu kanuni za nje, bali zinazobadili maisha ya kila siku ya uhusiano na YHWH ambayo ilidhihirisha tabia ya Mungu na ahadi zake kwa watoto wote wa Adamu. Tazama Mada Maalumu kuhusu maoni ya Paulo juu ya sheria katika 13:9.

◙
**NASB "Kile ambacho ni cha moyo, kwa roho, na sio kwa walaka"**
**NKJV "Kile cha moyo, katika roho, na sio katika waraka"**
**NRSV "Ni suala la moyo….ni la kiroho na sio la kimaandiko"**
**TEV "Ambayo ni kazi ya roho wa Mungu, na sio sheria iliyoandikwa"**
**NJB "Katika moyo-na sio kitu cha waraka bali kitu cha roho"**

Fungu hili ni kubwa mno Kiyunani. Tafsiri zingine hufanya liwe la kiroho dhidi ya uandishi (kama vile NRSV, Agano Jipya la karne ya ishirini, tafsiri za Knox, tafsiri ya Lamsa ya Peshitta, tafsiri ya Williams na chapisho jipya la Berkley). Tafsiri zingine zinaona kama ni kupingana baina ya Roho Mtakatifu (kama vile 7:6; 2 Kor. 3:6; ambako muundo sawia unaonekana) na andiko lililoandikwa (kama vile NASB, NKJV, NEB, NIV na TEV) *The Jerome Biblical Commentary*, uk. 299, inatoa pendekezo ambalo linaegemea 2 Kor. 3:6 ambayo ilikuwa ni namna nyingine ya Paulo kurejea Agano la Kale na Agano Jipya; la kwanza lilikuwa na mambo ya nje na la pili ni fikra mpya za ndani na roho mpya iliyotolewa na Roho Mtakatifu katika enzi mpya ya Roho.

Paulo amekuwa akijadili ukweli kwamba baadhi ya watu wa mataifa yanaweza kutenda na kumpendeza Mungu mbali na sheria. Kama hii ni kweli, basi watoto wa Mungu walijumuishwa zaidi ya watu waliotahiriwa kimwili (kama vile Wagalatia). Familia ya Mungu ni pana zaidi ya taifa la Wayahudi. Hata makabila ya Efrahimu na Manase walikuwa nusu Wamisri (kama vile Mwa. 41:50-52)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa vipi kukosa imani kwa Wayahudi kunaathiri ahadi ya Mungu (3:3-4)
2. Kuna faida yeyote mbele ya Mungu kuwa Myahudi?
3. Lugha ya kushambulia ina maana gani?
4. Ni lipi lengo lililokusudiwa la lugha ya kushambulia?
5. Je, jinsi ya kuishi kwa mtu inajalisha katika kupata haki ya neema kupitia njia ya imani mbali na matendo (3:8)?
6. Ni nini dhana ya kitheolojia ya kuasi maadili kamili (3:10-18)?
7. Nini kusudi la sheria ya Musa au sheria ya ujumla (3:20; Gal. 3:24-25)?
8. Kwa nini shetani haikutajwa kabisa katika sura ya 1-3 ambazo zimejishughulisha na upotevu wa mwanadamu.
9. Je ahadi za agano la kale ni za masharti au la?
10. Nini kusudi la sheria za Musa katika maisha ya; (1) wasio Wayahudi na (2)Wayahudi
11. Andika kwa kifupi kwa maneno yako mwenyewe hoja za Paulo katika 1:18-3:20 aya kwa aya

# WARUMI 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Wayahudi na sheria 2:17-3:8 | Hukumu ya Mungu Inatetewa | Faida ya Wayahudi | Wayahudi na sheria (2:17-3:8) | Ahadi ya Mungu haitawaokoa |
| 3:1-8 | 3:1-8 | 3:1-8 | 3:1-4<br>3:5-6<br><br>3:7-8 | 3:1-8 |
| Hakuna mwenye Haki | wote wametenda dhambi | Wote wana hatia | Hakuna aliye safi | Wote wana hatia |
| 3:9-20 | 3:9-20 | 3:9-18<br><br>3:19-20 | 3:9-18<br><br>3:19-20 | 3:9-18<br><br>3:19-20 |
| Haki kupitia katika Imani | Haki ya Mungu kupitia katika imani | Haki ya kweli | Jinsi Mungu alivyowapa watu haki | Ufunuo wa hukumu ya Mungu |
| 3:21-26 | 3:21-26 | 3:21-26 | 3:21-26 | 3:21-26 |
| | | Majivuno kutengwa | Majivuno yanatengwa | Kile imani inachofanya |
| 3:27-31 | 3:27-31 | 3:27-31 | 3:27-31 | 3:27-31 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA MUKTADHA

A. Mistari 1-8 inahusianakimaudhui ,lakini ni vigumu kufuata mantiki ya Paulo kwasababu anatumia mbinu ya fasihi yenye makemeo (kama mpinzani vile)
B. Inaonekana kwamba Paulo anatarajia ni kwa vipi Wayahudi wataitikia kwa 2:17-29,kwa hiyo anajibu upinzani wao (corley, vaunghani, *Warumi* - uk.37-39).
    1. Swali la kwanza. Hivi kweli,hakuna faida zozote kwa Wayahudi (mstari wa 1-2)
    2. Swali la pili. Je, Neno la Mungu limeshindwa kwa vile baadhi ya Wayahudi sio waaminifu? (mstari 3-4)
    3. Swali la tatu. Kama Mungu alitumia Wayahudi kudhihirisha alivyo je! Wayahudi bado wanawajibika kisheria (mstari 5-8)
C. Hitimisho linarudia kwa 2:11. Hakuna upendeleo kwa Mungu. Binadamu wote wanawajibika kujitenga kutoka kwenye nuru walionao (ufunuo asilia na / au ufunuo wa kipekee).
D. Mistari 9-18 ina mtiririko wa nukuu za Angano la kale ambazo hutamka dhambi za Wayahudi
E. Mistari 19-20 inafanya majumuisho ya hali ya kiroho ya Israeli na kusudi la Agano la Kale (Wagalatia 3)
F. Mistari ya 21-31 ni ufupisho wa 1:18-3:20. Ni hoja za kwanza za thiolojia ya injili (angalia maelezo kwa kifupi uk.2)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 3:1-8**
**[1]Basi Myahudi ana ziada gani? Na kutahiriwa kwafaa nini? [2]Kwafaa sana kwa kila njia. Kwanza kwa kuwa wamekabidhiwa mausia ya Mungu. [3]Ni nini, basi, ikiwa baadhi yao hawakuamini? Je! Kutokuamini kwao kutaubatili uaminifu wa Mungu?[4] Hasha! Mungu aonekane kuwa amini na kila mtu mwongo; kama ilivyoandikwa, Ili ujulikane kuwa una haki katika maneno yako, Ukashinde uingiapo katika hukumu.[5] Lakini, ikiwa udharimu wetu waithibitisha haki ya Mungu, tuseme nini? Je! Mungu ni dharimu aletaye ghadhabu? (nasema kwa jinsi ya kibinadamu) [6] Hasha! Kwa maana hapo Mungu atawezaje kuuhukumu ulimwengu? [7] Lakini, ikiwa kweli ya Mungu imezidi kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa mwenye dhambi? [8] Kwa nini tusiseme (kama tulivyosingiziwa, na kama wengine wanavyokaza kusema ya kwamba twasema hivyo), na tufanye mabaya, ili yaje mema? Ambao kuhukumiwa kwao kuna haki.**

**3:1**“**Ni faida gani aliyonayo Myahudi**” Paulo anaendelea kutumia mbinu ya kifasihi ya kukaripia, au kamavile mpinzani, ili kufikisha ujumbe wake. Kwa kuorodhesha maslahi ya watu wa Uyahudi, angalia 3:2 na 9:4-5. Paulo anaendeleza aya hiii katika 9-11

**3:2** “**Awali ya yote**”- Paulo anatumia “kwanza” katika 1:8, lakini bila kipengele cha pili kutajwa. Anafanya vilevile tena hapa. Uandishi wa Paulo ulikuwa wa kina, pia wenye imla, ambao mara kwa mara muundo wake kisarufi haukamiliki.

◙“**Waliaminishwa na ushauri wa Mungu.”**Kupata ufunuo wa Mungu ni wajibu wenye heshima na bahati kubwa (9:4-5). Walikuwa watumishi wa karama ya Mungu (kama vile The. 2:4). Neno *‘logion*’ lilitumika katika maandiko yakalekumaanisha neno kutoka kwa Mungu (Hes. 24:4,16, Kumb. 33:9, Zaburi 107:11, Isa. 5:24, 28:13), linalomaanisha Agano la Kale linatumika vivyo hivyo katika Agano Jipya (Mdo. 7:38, Ebr. 5:12, 1 Pet. 4.11).

**3:3“kama**”Hii ni SENTENSI INAYOELEKEA KUWA KWELI ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi hili la kifasihi. Mistari 5 na 7 ni SENTENSI INAYOELEKEA KUWA KWELI. Sarufi ya mstariwa 3 hautarajii jibu la “hapana”.

◙
**NASB, NKJV “baadhi hawakuamini.’’**
**NRSV, NJB “Baadhi yao hawakuwa waaminifu’’**

**TEV** **"Ni vipi kama baadhi yao hawakuwa waaminifu.''**

Hii inaweza kumrejelea Mwisraeli binafsi, (1) Uaminifu au (2) Kukosa imani binafisi kwa YHWH. Nivigumu kiakili kuhusisha ahadi za Mungu zisizo na masharti (yaani ukombozi wa mwanadamu aliye anguka) na mamlaka yenye masharti ya mwanadamu kuzipokea. Tazama maada maalumu: ''Agano''katika 9:4. Bado hili ni fumbo la Kibiblia (3:4-5).Mungu ni mwaminifu hata kama watu wake sio waaminifu (kama vile Hosea 1:3, 2 Tim 2:13).

◙**''Batilisha"** Tazama mada maalumu hapa chini.

## MADA MAALUM: BATILI NA UTUPU (*katargeō*)

Hili neno (*katargeō*) lilikuwa ni moja ya maneno pendwa ya Paulo. Aliyatumia takribani mara ishirini na tano lakini lilikuwa na utofauti mpana.

A. Mzizi wa kiasili wa neno unatoka kwenye neno *argos* linalo maanisha
   1. Isio tendaji
   2. Isio na kazi
   3. Isiotumika
   4. Isiofaa
   5. Isiofanya kazi
B. Neno ambani likiwa na *kata* lilitumika kuelezea
   1. Isiofanya kazi
   2. Isiofaa kabisa
   3. Iliyo imebatilishwa
   4. Lililofanyikia mbali
   5. Ambalo lilikuwa halifanyi kazi kabisa
C. Limetumika mara moja tu katika Luka kuelezea lisilozaa matunda, kwa hiyo ni mti usiofaa(kama vile. Lk 13:7)
D. Paulo analitumia kwa maana ya kitamathari kwa njia mbili za msingi
   1. Mungu anafanya vitu visivyotumuka ambavyo havina faida kwa mwanadamu
      a. Asili ya dhambi ya mwanadamu-Rum. 6:6
      b. Sheria za Musa ukilinganisha na ahadi ya Mungu ya "mbegu"-Rum. 4:14; 3:17;5:4,11; Efe. 2:15
      c. Nguvu za kiroho-1 Kor. 15:24
      d. "Mtu asiye wa sheria"- 2The. 2:8
      e. Mauti ya mwili– 1 Kor. 15:26; 2 Tim. 1:10 (Ebr. 2:14)
   2. Mungu anaweka ktu kingine cha zamani (Agano, zama) kwa kipya
      a. Vitu vinavyohusiana na sheria za Musa – Rum. 3:3,31; 4:14; 2 Kor. 3:7,11,13,14
      b. Mshabihiano wa ndoa uliotumia sheria – Rum. 7:2,6
      c. Mambo ya zama hizi – 1 Kor. 13:8,10,11
      d. Mwili huu – 1 Kor. 6:13
      e. Viongozi wa zama hizi – 1 Kor. 1:28; 2:6

Neno hili linatafasiliwa kwa njia mbali mbali, lakini maana yake kuu ni kukifanya kitu kisichofaa, batili na utupu, kisichofanya kazi, kisicho na nguvu, lakini sio muhimu kuwa hakiishi, kilichoharibiwa au angamizwa

◙**"uaminifu wa mungu"** Ukweli huu (kama vile I Kor. 1:9;10:13; II Kor. 1.18) ni wa msingi kwa uaminifu wa mwanadamu kwa Mungu (Kumb. 7:9; Isa. 49:7)

1. Tabia isiyobadilika
2. Ahadi za milele

Amejidhihirisha mwenyewe katika uumbaji, ufunuo, agano na masihi. Hata katikati ya kutoaminika kwa mwanadamu, yeye anabaki mwaminifu tu (kama vile II Tim. 2:13)

**3:4**
**NASB "Inaweza isiwe"**
**NRSV "Hakika hapana"**
**NKJ, TEV "Hakuna njia"**
**NJB "ingekuwa ni ajabu"**

Haya ni matumizi nadra ya HALI YA KUCHAGUA iliyoonesha hitaji au ombi na fungu hili linapaswa kutafsiliwa ''Inaweza isiwe'.Linaweza kuashiria nahau ya Kiebrania.Fungu hili la ''mshangao wa kutoamini'' mara nyingi lilitumiwa na Paulo kwa sababu ya mbinu zake za kifasihi za kukemea (3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14;11:1; I Kor. 6;15;Gal. 2:17; 3:21; 6:14). Ilikuwa ni namna yake yamsisitizo wakukana utetezi wa haki uliokusudiwa.

Angalia njia za kifasihi Paulo anazozikataa za maswalina semi za kufikiriwa kwa upinzani

1. "Inaweza isiwe" mistari ya 4, 6
2. Mwache Mungu aonekane mkweli, japo kila mtu anaonekana muongo, mstari wa 4
3. "(Ninazungumza katika hali ya kibinadamu)" mstari wa 5
4. "(Kama tunavyosemwa na kama baadhi wanavyodai tusemavyo)," mstari wa 8

◙**"Hebu Mungu aonekane mkweli, japo kila mtu *aonekane* muongo"**. Hii ni KAULI INAYOONYESHA HALI YA KITU KUENDELEA KWA WAKATI ULIOPO. Usemi huu unalenga kuhusu hali inayoendelea ya somo; Munguni mwaminifu na mkweli (angalia mada maalum 1:18), wanadamu siyo waaminifu na waongo! Hii inadhibitishwa toka Zaburi 116:11, na ni sawia na alichokuwa Ayubu ajifunze katika 32:2, 40:8.

Tazama jambo hili la utendaji dhambi lilivyoenea ulimwenguni kote katika sura hii, lilivyowasilishwa na Paulo katika matumizi ya neno *pas* (wote, kila mmoja) katika mistari ya 4,9, 12, 19,20, 23, 24 lakini Mungu asifiwe, pia wokovu alioutoa kwa wote ulimwenguni (kama vile 3:22).

◙**"Kama ilivyoandikwa "**Hii imekuwa, na inaendelea kuandikwa. Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU INAYOELEKEZA. Ikawa ni nahau iliyotumika kusisitiza msukumo wa maandiko ya Mungu. Inaingiza nukuu kutoka Zaburi 51:4 kutoka katika vitabu vya kale (LXX).

**3:5-6.** Ubishi unaofanywa na Paulo katika mistari hii unahusiana na chaguo maalum la Mungu kwa Waisrael kama njia yake ya kuifikia ulimwengu. (Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6). Katika Agano la Kale "uchaguzi", unamaanisha kuhudumia, na siyo upendeleo maalum. Mungu alifanya Agano nao. Alikuwa mwaminifu wao hawakuwa waaminifu (Nehemia 9). Ukweli kwamba Mungu alihukumu Waisrael wasiokuwa waaminifuni ushahidi tosha wa haki aitendayo.

Israeli ilikusudiwa kuwa njia ya kuwafikia wapagani. Walishindwa (3:24)! Kusudi la Mungu la wokovu wa ulimwengu (Mwanzo 3:15) hauathiriwi na kushindwa kwa Israel. Ukwelini kwamba, uaminifu wa Mungu kwa agano lake la mwanzo unathibitishwa katika Warumi 9:11. Israel isioamini inakataliwa, lakini Israel inayoamini itaendea kukamilisha mpango wa Mungu wa ukombozi. Makemeo ya Paulo katika mistari 5-6 ni sambamba na mistari 7-8.

**3:5**"**Kama**" Hii ni KAULI INAYOSADIKIWA KUWA NI KWELI ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtizamo wa mwaandishi au kwa kusudi lake kifasihi. Mstari 3 na 7 pia ni KAULI ZINAZOSADIKIWA KUWA NI KWELI.

◙"**Kama kutokuwa na haki kwetu kunaonyesha haki ya Mungu**."KIWAKILISHI hiki "sisi" lazima kirejeree katika hali ya kuwaleta pamoja kwa Wayahudi wote. Tazama mada maalum katika 1:17

◙ "**Tusema nini basi"** Paulo bado anaendelea kutumia lugha yake ya kukemea (3:5; 7:7;8:31; 9:14,39) Paulo anafafanua bado uwasilishi wake kwa kutumia hali ya kudhaniwa mpinzani. (Mal. 1:2, 6, 7, 12,13; 2:14,17 [mara mbili] 3:7,13,14).

◙

**NASB "Ninazungumzakwa maneno ya kibinadamu"**
**NKJV "Ninazungumza kama binadamu"**

**NRSV "Ninazungumzakwa jinsi ya kibinadamu"**
**TEV "Ninazungumza hapa kamawatu wafanyavyo"**
**NJB "Kutumia ulinganisho wa binadamu"**

Paulo mara nyingi alitumia mantiki ya binadamu katika mabishano ya kithiolojia (6:19; 1 Kor. 9:8; Gal. 3:15). Hapa inafanya kazi kama njia ya kukataaa msimamo wa kudhaniwa mpinzani.

**3:7-8** Dhahiri kuna usambamba wa wazi kati ya mstari 5 na 7 (yote inaanza na *ei de*). Paulo huenda;

1. Anaendelea kutumia mbinu ya kifasihi ya kukemea, kudhaniwa mpinzani (3:5,7; 7:7; 8:31; 9:14,30).
2. Ajibu kubezwa kwake kwa kuhalalisha mafundisho kwa njia ya imani tu. (Mstari 8).

Paulo hakueleza au kujibu kosa kwa kina lakini kwa kulazimishwa analaani tuhuma. Inawezekana kuwa kupinga kutokubaliana kuhalalisha mafundisho kwa njia ya imani ilikuwa kwamba ingeweza kusababisha ukosefu wa sheria au hata utii. Paulo anaamini kuwa neema ya bure ingeleta hali ya kumfanana Kristo kupitia roho mpya na maisha ya furaha! Wayahudi, Wayunani waadlifu na Paulo walitaka kuishi kimaadili katika maisha mapya ya kuamini kwao! Lakini inatokea siyo katika usawa kwa kanuni ya sheria bali moyo mpya, mawazo mapya na roho mpya (Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-36)

**3:7"kama"** Hii ni KAULI INAYOSADIKIWA KUWA NI KWELI (Pia mstari 3 na 5) ambao unadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi lake Kifasihi.

◙**"Sheheni"** – tazama mada maalum katika 15 :13

◙**"Utukufu wake"** tazama dokezo katika 3:23.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 3:9-18**
**9 Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wayaunani ya kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi; 10 kama ilivyoandikwa, ya kwamba,"HAKUNA MWENYE HAKI HATA MMOJA. 11 HAKUNA AFAHAMUYE; HAKUNA AMTAFUTAYE MUNGU. 12 WOTE WAMEPOTOKA, WAMEOZA PIA; HAKUNA MTENDA MEMA; LA! HATA MMOJA. 13 KOO LAO NI KABURI WAZI, KWA NDIMI ZAO WAMETUMIA HILA. SUMU YA FILA I CHINI YA MIDOMO YAO. 14 VINYWA VYAO VIMEJAA LAANA NA UCHUNGU 15 MIGUU YAO INA MBIO KUMWAGA DAMU. 16 UHARIBIFU NA MASHAKA YAMO NJIANI MWAO. 17 WALA NJIA YA AMANI HAWAKUIJUA. 18 KUMUCHA MUNGU HAKUPO MACHONI PAO."**

**3:9 "Sisi ni bora kuzidi wao"**Sarufi katika hatua hii ni tata. Niwazi kuwa ukweli halisi katika ujumbe ni kuwa watu wote wanahitaji neema ya Mungu (3:9,19,23;11:32; Gal. 3:22). Ingawa, hakuna uhakika kuwa rejea hii mahususi ilikuwa kwa ajili ya wayahudi (Paulo na ukoo wake, kama vile TEV, NRSV) au Wakristo (Paulo na waumini wenzake,mbali na neema ya Mungu).Wayahudi walau walikuwa na manufaa (mst.1-2,9:4-5), lakini manufaa haya yaliwafanya wawajibike zaidi (Luka 12:48)

Neno "bora'', linafahamika kwa wasomi wachache kama KAULI YA KUTENDEWA badala ya KATI ("mwenye hadhi'') ikipelekea tafsiri kuzidi kwa ubora au kutonufaika nacho.

Mara nyingi Warumi hawasemi chochote kuhusu nyaraka za Paulo. Nyaraka nyingi za Paulo zilikuwa zikishungulikia mahitaji au matatizo Kama yalivyojitokeza (nyaraka zilizojitokeza mara kadhaa).Ingawa, wivu kati ya viongozi waamini wa Kiyahudi na viongozi waamini wa kipagani katika kanisa la Rumi inaweza ikatokana na sura ya 1-3 na 9-11

◙"**Kama tulivyokwisha dai ya kuwa wote Wayahudi na Wayunani wamo katika dhambi' '**KITENZI hiki "ELEKEZI''kinapatikana hapa katika Agano jipya. Paulo anarejea katika ubishi wake endelevu wa 1:18-2:29.

◙**"Chini ya dhambi''** Paulo anaichukulia "dhambi".*Jerome Biblical commentary,* uk. 300) Kama mtu mwenye wajibu juu ya binadamu aliyeanguka (kama vile 6:16-23).

**3:10-18"Kama ilivyoandikwa"** fungu hili pia linatokea katika mstari wa 4. Maneno yafuatayo ni mfuatano wa nukuu za Agano la kale akitumia sitiari ya mwili wa binadamu kusisitiza mtu aliyeanguka.

1. Mistari ya 10-12 Mhu. 7:20 au Zab. 14:1-3
2. Mstari wa 13, Zab. 5:9 na 140:3
3. Mstari wa 14, Zab. 10:7
4. Mistari ya 15-17 Isa. 59:7-8 na Mdo. 1:16
5. Mstari wa 18, Zab. 36:1

Inashangaza kuwa Paulo hakutumia Isa 5 3:6

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 3:19-20**
**[19]Basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu; [20]Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakaye hesabiwa haki mbele yake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi *huja* kwa njia ya sheria.**

**3:19 "Tunajua ya kuwa"** Tazama dokezo katika 2:2

◙**"Sheria"** Katika mtindo huu, ni lazima irejee katika Agano la kale zima (kama vile mstari 21) kwa sababu kurasa zisizitokana na Torati zilizonukuliwa katika mistari ya 10-18. Paulo anaifanya "sheria" kama alivyotenda "dhambi" katika mstari 9 (kama vile 6:16-23).

◙**"kwa wale walio chini ya sheria"** Hii inarejea pekee kwa Wayahudi na watu wa mataifa walioamini. Ingawa inaweza semekana ya kuwa nukuu nyingi za Agano la Kale zilizotumika zinawarejea watu wamataifa katika asili yao ya awali.Binadamu wote ni watenda dhambi (kama vile 3:23)

◙

**NASB "Kwamba kila kinywa chaweza kufungwa, na ulimwengu wote uwajibike mbele za Mungu"**
**NKJV "Kwamba kila kinywa kitaachishwa kusema,na ulimwengu wote utakuwa na hatia mbele za Mungu**
**NRSV "Hivyo kwamba kila mdomo unaweza kunyamazishwa na ulimwengu wote Kuwajibishwa kwa Mungu"**
**TEV "Ili kukomesha misamaha yote ya binadamu; na kuuleta ulimwengu wote mbele ya ukumu ya Mungu".**
**NJB "Lakini, imemainisha kunyamazishwa kila mmoja na kuuweka uliwengu wote wazi kwa hukumu ya Mungu**

Hii ndiyo dhima kuu ya sura 1:18-3:20 ambayo inajumuishwa katika 3:23.

◙"**Kila mdomo**" Kuna mafungu kadhaa katika mistari 19-20 ambayo inamaanisha binadamu wote.
1. "Kila mdomo" mstari 19
2. "ulimwengu wote" mstari 19
3. "Hakuna mfano/mwili" mstari 20.

**3:20"Kwa sababu, kwa kazi za sheria hakuna mwenye mwili atakayethibitishwa mbele yake"**Huu ni ukweli katika Zab.143:2 (pia angalia Ayu. 4:17;9:2;25:4; Zab.130:30; Mit. 20:9; Wim. 7:20; 1 Efe. 8:46, II Kor. 6:36),lakini pakiwa na nyongeza ya fungu la wazi. Huu ulikuwa mwelekeo mkuu wa injili ya Paulo (Gal. 2:16; 3:11). Kama mfarisayo aliyejitoa, alijua udhaifu wa shauku ya kidini na utendaji angalifu kuleta amani ya ndani.
Kwa"mwili "tazama mada maalum katika1:3.

◙

**NASB, NRSV "kupitia sheria unapatikana ufahamu ya dhambi"**
**NKJV "kwa vile, kwa sheria ni ufahamu wa dhambi"**
**TEV "sheria inachofanya ni kumfanya mtu ajue kwamba ametenda dhambi "**
**NJB "kile sheria ifanyacho ni kutuambia sisi kipi ni dhambi"**

Hili ndilo lilikuwa mojawapo ya makusudi ya Agano la kale.Tazama mada maalum katika13:9. Kamwe haikumaanisha kuleta wokovu kwa mwanadamu aliyeanguka. Kusudi lake lilikuwa kudhihirisha ile hali ya dhambi na kuwapeleka watu wote kwenye huruma ya YHWH (kama vile 4:15; 5:13,20; 7:7; Gal.3:19-22,23-29**)**

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa vipi kukosa imani kwa Wayahudi kwaweza kuathiri ahadi za Mungu (3:3-4)
2. Kuna faida yoyote na Mungu kuwa Myahudi (3:1-8)
3. Kuna maana gani kwa aliyedhaniwa kuwa mpinzani (Lugha ya kukemea) katika mistar 5-8?
4. Ni kwa vipi maisha ya mtu yana maana kama haki ni kwa neema kupitia imani mbali na kazi zitendwazo (3:8)?
5. Elelezea dhana ya kithiolojia (Calvin) ya mkengeuko mzima (3:10-18)
6. Nini kusudi la sheria ya Musa au sheria kwa ujumla (3:20; Gal. 3:24-25)?
7. Kwa nini shetani hakutajwa kabisa katika sura za 1-3 ambayo inashughulika na upotevu wa mwanadamu

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WARUMI 3:21-31

A. Warumi 3:21-31
   1. muhtasari wa mabadiliko katika 1:18-3:20
   2. Kuelezea zaidi kwa 1:16-17
   3. Utangulizi wa sura za 4-5 (hasa 3:28)

B. Mhutasari wa mabadiliko ya mafundisho ya udhihirisho kwa neema kupitia imani yalijulikana na watu walioongoka kama;
   1. Martini Luther-“kama kigezo kikuu na mahali muhimu waraka na Biblia nzima”.
   2. John Calvin-Bila shaka hakuna pahali katika Biblia nzima ambapo panaonyesha umuhimu mkubwa wa haki ya Mungu katika Kristo.

C. Huu ndiyo umuhimu wa kithiolojia wa ukiristo wa injili. Kuelewa muktadha huu ni kuelewa ukristo. Hii ni injili iliyofupishwa katika aya mbili, kama vile katika Yohana 3:6 neno la injili ndani ya mstari tu.Huu ndiyo moyo na nafsi wa uwasilisho wainjili ya Paulo.
   Maswali matatu muhimu ya tafsiri ni;-
   1. Neno “sheria” lina maana gani?
   2. Kifungu hiki “Haki ya Mungu” kina maana gani?
   3. Maneno “imani”na “kuamini” yana maana gani?

D. Namshukuru Mungu kwa neno “yote”katika mstari 22(kama vile mstari 29) na neno “karama”katika mstari wa 24 (kama vile 5:15, 17;6:23)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 3:21-26**
**[21]Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii; [22]ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti; [23]kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; [24]wamehesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi iliyo katika Kristo Yesu; [25]ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika**

**usitahimili wa Mungu dhambi zote zilizotanguliwa kufanywa; [26]apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu.**

**3:21 "Lakini sasa"**Paulo anatofautisha Agano la kale na Agano jipya. Enzi ya zamani ya uasi na enzi mpya ya haki. Hii itaenda sambamba na "wakati uliopo" (ya 26," lakini sasa kwa 6:22,7:6)

◙**"Sasa, mbali na sheri"** Ni aghalabu kuwa na hakika iwapo Paulo anazungumuzia sheria ya Musa (NASB) au sheria kwa ujumla (NSRV, TEV, NJB, NIV) katika sura hizi za utangulizi. Katika muktadha huu sheria za Kiyahudi zinaoana vyema kabisa na hoja za Paulo. Binadamu wote wamekiuka kila aina ya maadili, mwongozo wa kijamii ama wa ndani au wa nje. Matatizo yetu kama Mwanadamu aliyeanguka ni kuwa hatuhitaji kabisa muongozo isipokuwa binafsi wetu na matamanio (kama vile Mwanzo.3) ambayo yana uelekeo wa ubinafsi wa ulimwengu wa kisasa wa kimagharibi.

◙

**NASB** **"Haki ya Mungu"**
**NKJV, NSRV** **"Haki ya mungu"**
**TEV** **"Njia ya Mungu ya kuwaweka watu sawa na yeye".**
**NJB** **"Haki ya mungu ya kuwaokoa watu".**

Hakuna IRABU hasa kwa neno "haki".hii haimaanishi tabia ya Mungu, bali njia ya Mungu itoayo msamaha na ukubarifu kwa watu wenye dhambi.Fungu hili hili lilitumika katika dhima ya kithiolojia katika Roma 1:16-17. Mfumo uliowekwa wazi ni imani katika Yesu kristo aliyesulubiwa (kama vile mistari ya 22, 24-26)

Ukweli kwamba neno hili (*dikaiosonē*) na yale yatokanayo (tazama nukuu katika 2:13) yanatumika mara nyingi katika muktadha huu kuonyesha umuhimu (kama vile 1:17;3:5,21,22,25,26; 4:3,5,6,9,11,13,22; 5:17,21; 6:13,16,18,19,20; 8:10; 9:28,30,31; 10:3,4,5,6,10,17). Neno hili la Kiyunani linatokana na Istiari ya muundo wa Agano la Kale (*isadaka*) likimaanisha "kipimio" au "kamba ya kupimia itokanayo na gome la mti" (angalia Mada maalum katika 1:17). Kipimo ni Mungu mwenyewe. Neno hili linaashiria tabia ya Mungu inayotolewa bure kwa mwanadamu aliyeanguka kupitia kristo (kama vile sura 4; II Kor. 5:21). Kukiri hitaji lao na kupokea karama ya Mungu ilikuwa na inaendelea, kudhalilisha majivuno ya binadamu, mtu mwenye ubinafsi,na hasa binadamu mfuata sheria na mtu wa dini.

◙"**Imedhihirishwa**" fungu hili ni sawa na 1:17. Ingawa, hiki KITENZI ni tofauti. KITENZI hiki chaweza kutafsiriwa "amekuwa na ameendelea kuonyesha wazi" NI KAULI TENDEWA ELEKEZI Y WAKATI TIMILIFU wakati ukaribu wa maana katika 1:17 ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Mungu ameweka wazi injili yake ktk Agano la kale (kama vile sura 4) na kwa Yesu.

◙"**Tukishuhudiwa kwa sheria na manabii**" Hii ilimaanishwa katika sehemu mbili kati ya sehemu tatu za kitabu cha kanuni ya Waebraimia (sheria, manabii na maandiko).Sehemu hizi mbili zilitumika kuonyesha vyote (angalia nukuu katika 3:19, Mt. 5:17).Hii inaonyesha wazi kuwa injili ilikuwa katika mfumo wa awali wa Agano la kale (kama vile Luka 24:27;44' Mdo. 10:43). Halikuwa wazo la baadaye au "mpango B" au mpango wa dharura dakika za mwisho (kama vile 1:2)

**3:22 "Kupitia imani katika kristo Yesu"** Hiki ni kifasihi"kupitia imani katika Kristo Yesu." Hiki ni KIMILIKISHI chenye kuunda. Limerudiwa katika Gal. 2:16 na Flp. 3:9 kadhalika katika muundo uleule katika Rum. 3:26; Gal. 2:16,20; 3:22. Lingemaanisha

1. Imani au uaminifu wa Yesu (KIMILIKISHI DHAHANIA).
2. Yesu kama kitu cha imani yetu (KIMILIKISHI KISICHO NA UPENDELEO)

Muundo sawia wa kisarufi katika Gal.2:16 inafanya #2 kuwa changuo bora.

Hii inaonyesha swala la msingi la haki ya Mungu. Ni haki ya Mungu aliyofanya uwezo wa kutengeneza maisha ya mtu kutokana na kipawa cha bure cha Mungu kupitia kristo. (kama vile 4:5,6:23) ambacho sharti kikubalike kwa imani /kusadiki/kuamini (kama vile Efe.2:8:9) na ilidumu kwa maisha ya binadamu (Efe.1:4;2:10)

◙"**kwa wote**"Injili ni kwa wanadamu wote (kama vile mstari. 24; Isa. 53:6; Eze. 18:23,32) Yoh. 3:16-17; 4:42; I Tim. 2:4, 4:10; Tit. 2:11, II Pet.3:9; 1 Yn. 2:1:4:14). Ni ukweli ulioje! Hii inapaswa ilinganishe ukweli wa Kibiblia katika uchaguzi. Uchaguziwa Mungu usieleweke katika maana ya kiislamu ya mawaidha wala maana zaidi ya ile ya Calvin baadhi ya mambo dhidi yawengine, bali katika maana ya maagano. Uchaguzi wa Agano la kale ulikuwa kwa ajili ya huduma, na siyo upendeleo! Mungu aliahidi kuwakomboa binadamu walioanguka (kama vile Mwa. 3:15). Mungu aliita na kuchagua wanadamu wote kupitia Israel (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6). Mungu huchagua kupitia imani katika kristo.Mungu daima huchukua hatua katika wokovu (kama vile Yoh. 6:44,65). Waefeso 1 na Warumi 9 ni insha za Biblia zenye nguvu juu ya mafundisho kuwa kila kitu kinachotokea kimepangwa na Mungu na hakuna mwanadamu awezae kubadili fikra ambayo kithiolojia ilisisitizwa na Agostino na Calvin.Mungu aliwachangua waaminio siyo tu kwa wokovu (kuweka usawa) lakini pia kwa utakaso (kama vile Efe. 1:4, Kol. 1:12). Hii ingehusiana na:-

1. Nafasi yetu kwa kristo (kama vile II Kor. 5:21)
2. Nia ya Mungu kuendeleza katika kizazi tabia yake katika watoto wake (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19; Efe. 2:10).

Mapenzi ya Mungu kwa watoto wake ni mbinguni siku moja na hali ya kufanana na kristo wakati huu.Lengo la imani kuwa kila kinachotokea ni mpango wa Mungu ni utakatifu (kama vile Efe. 1:4),na siyo upendeleo! wito wa Mungu haukuwa kwa wachache kwa wana wa Adamu,bali wote ! Ulikuwa ni wito wa tabia yake Mungu (kama vile I The. 5:23; II The. 2:13). Kugeuza imani ya kuwa kila kinachotokea ni mpango wa Mungu kuingiza katika upangaji wa kithiolojia badala ya maisha matakatifu ni sikitiko la mfumo wa mwanadamu kithiolojia. Mara nyingi mkanganyiko wetu kithiolojia huharibu maandiko ya Biblia. Tazama mada maalum: Uteuzi /imani ya kitokeacho ni Mungu kapanga na hitaji la usawa wa kithiologia katika 8:33

◙"**Nani anasadiki"** Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote. Inawezekana watu wote kuokolewa. Ni mapokeo binafsi ya binadamu (KAULI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, angalia mada maalum katika 10:4) ambayo inafanya haki ya Yesu itumike maishani mwao"(kama vile 1:16; Yoh.1:12; 3:16; 20:31; Rum. 10:9-13; I Yoh. 5:13). Biblia inaonyesha misingi miwili ya sifa ya haki: imani na toba (Marko 1:15; Mdo. 3:16, 19;20:31 na angalia nukuu katika 1:15). Andiko hili kwa wazi kabisa linabainisha kutoa ahadi ya wokovu kwa watu wote lakini mkasa na ajabu ni kwamba sio wote watakao okolewa.

◙**"kwa vile hakuna utofauti"**kuna njia moja tu na mtu mmoja ambaye kwake wanadamu (Wayahudi na watu wa mataifa) waweza kuokolewa (kama vile Yoh. 10:1-2,7;11:25;14:16). Yeyote na kila mmoja aweza kuokolewa kwa imani katika kristo (kama vile 1:16; 4:11,10:4,12; Gal. 3:28; Kol. 3:11)

**3:23-26** Hii ni sentensi moja tu ya kiyunani.

◙
**3:23**
**NASB NKJV,**
**NRSV "wote wamendeza dhambi na kupungukiwa na"**
**TEV "Watu wote wametenda dhambi na wako mbali"**
**NJB "Wametenda dhambi na wamepotea"**

Huu ni muhtasari wa 1:18-3:20, kila mmoja anahitaji kuokolewa na kristo (kama vile 3:9, 19, 11:32; Gal. 3:22; Isa. 53:6) "Kutenda dhambi" KAULI TIMILIFU INAYOELEKEZA, Wakati "kuendelea kupungukiwa" KAULI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Yamkini kifungu hiki kilimaanisha kwa wote (1) anguko la pamoja la mwanadamu kwa Adamu (kama vile 5:12-21) na (2) kuendeleza matendo yake binafsi ya uasi. Hakuna tafsiri yoyote ya kisasa ya kiingereza inayoonyesha utofauti huu.

Mstari huu kithiolojia unahusiana na mstari wa 21 na siyo moja kwa moja na mstari wa 24

◙"**Utukufu wa Mungu**" Wanadamu waliumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27), suala ambalo si hivyo kwa kiumbe kingine kilichoumbwa. Wanadamu walipaswa kushirikiana na Mungu wa utukufu na kuonesha tabia yake! Dhambi iliharibu sura ya Mungu, lakini neema ya Mungu kupitia kifo cha kristo na imani ya waumini imerejesha sura (kama vile Kol. 3:10). Katika Agano la kale neno la kawaida kabisa la Kiebrania "utukufu" (*kbd)* mwanzoni kabisa lilikuwa ni neno la kibiashara (ambalo lilimaanisha jozi ya mizani) likimaanisha "kuwa nzito"taz.mada maalum hapa chini

## MADA MAALUMU: UTUKUFU (*doxa*)

Dhana ya Biblia ya "utukufu"ni ngumu kuielezea. Toleo la Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale (LXX) lilitumia *doxa* kufasiri zaidi ya maneno ya Kiebrania Ishirini. Linatumika mara nyingi katika Agano Jipya lote kwa namna tofauti tofauti. Linatumika kwa Mungu, Yesu, Wanadamu na Ufalme wa Kimasihi.
Katika Agano la kale neno la Kiebrania "utukufu" (*kabod*, BDB 458, KB 455-458) Lilikuwa awali neno la kibiashara lililohusisha jozi ya mizani ("kuwa mzito," KB 455). Kwamba kilichokuwa kizito kilithamanishwa. Mara nyingi. Dhana ya mng'ao iliongezwa kwenye hilo neno kuonesha ukuu wa Mungu (kama vile Kut. 19:16-18; 24:17;Isa. 60:1-2) yeye pekee ni wa thamani na kuheshimika (kama vile Zab 24:7-10; 66:2; 79:9). Yeye anag'ara zaidi kiasi kwamba mwanadamu aliyeanguka asiweze kumkabili (kama vile Kut. 33:17-23; Isa. 6:5). YHWH aweza kiukweli kufahamika kupitia kwa kristo (kama vile Yn.14:8-11; kol. 1:15; Ebr. 1:3, 1 Yn.4:12).

Kwa Mjadala kamili wa *kabod*, angalia Mada Maalum: Utukufu (Agano la Kale). Utukufu wa Waaminio ni kwamba waelewe injili na utukufu katika Mungu, sio katika wao wenyewe (kama vile 1 Kor. 1:29-31; Yer. 9:23-24). Kwa mjadala wa ndani, angalia NIDOTTE, vol. 2, kur. 577-587.

**3:24 "Kuhalalishwa kama zawadi kwa neema yake**"Huu ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hapa ndipo injili inaanzia neema ya Bwana atoae haki (kama vile 5:15-17;6:23; Efe. 2:8-9). Neno la Kiyunani "halalishwa" (*dekaioō*) lililotokana na msingi neno "haki" (*Dekaiosunē*, angalia mada maalum katika 1:7). Mungu wakati wote huchukua hatua (Yoh. 6:44-45).
Katika mistari ya 24-25 kuna maneno mbadala matatu yanayoelezea wokovu.

1. "Kuhalalishwa"ambalo lilikuwa neno la kisheria lililomaanisha "hakuna adhabu inayotolewa"au kutangaza mtu kutokuwa na hatia.
2. "Ukombozi" ambalo lilitoka katika soko la watumwa lililomaanisha "rudisha" au "kuweka huru"
3. "Heri"ambalo lilitokana na mfumo wa utoaji sadaka likimaanisha mahali pa upatanisho.

Likimaanisha mlango wa sanduku la Agano ambapo damu ya utakaso iliwekwa kwa ajili ya upatanisho (kama vile Law. 16:-Ebr. 9:5)

## MADA MAALUMU: USHAHIDI WA AGANO JIPYA KWA WOKOVU WA MTU

Msingi wake unatokana na Agano Jipya (kama vile Yer.31:31-34;Ezek 36:22-38) katika Kristo Yesu:

1. Tabia ya Baba (kama vile Yoh 3:16); kazi ya mwana (kama vile 2 Kor.5:21), na huduma wa Roho (kama vile Rum 8:14-16) na siyo kwa utendaji wa mwanadamu, na siyo ujira utokanao na utii, na siyo kanuni.
2. Ni zawadi (kama vile Rum 3:24,6:23; Waefeso 2:5, 8-9)
3. Ni maisha mapya, mtazamo mpya wa ulimwengu (kama vile Yakobo na I Yohana.)
4. Ni maarifa (injili), ushirika (imani ndani na katika Kristo Yesu), na mtindo mpya wa maisha (hali ya kufanana na Yesu kwa kuongozwa na roho ) zote tatu, na siyo tu mtu mmoja peke yake.
5. Angalia majaribu ya wokovu wa kweli katika muktadha wa uelewa kwa I Yohana. 2:3-3:3)

◙"**zawadi**"-Paulo anatumia dhana hii mara kadhaakwa kutumia maneno tofauti tofauti

1. *Dōrean,* KIVUMISHI-"bure"
2. *Dōrea*, NOMINO-"zawadi ya bure"

3. *Dōron,* NOMINO-"zawadi Efe. 2:8)
4. *Charisma*, NOMINO "deni la bure"au "upendeleo wa bure" (kama vile 1:11,5:15;16,6:23;11:29,12:6)
5. *Charisomai*, KITENZI –"kupewa kama upendeleo wa bure" (kama vile 8:32)
6. *Charis*, NOMINO "upendeleo wa bure"au zawadi ya bure" (kama vile 4:4,16,11:5,6, Efe. 2:5,8)

◙"**Kupitia katika ukombozi ambao uko ndani ya kristo Yesu**"njia ya ukombozi wetu ni kifo chake Yesu na ufufuo kilichochukuwa nafasi yetu. Mtazamo wa Kibiblia siyo ni kwa kiasi gani deni limelipwa au gharama ililipwa kwa nani(Agostino), lakini katika ukweli kwamba mwanadamu ameondolewa kutoka katika hatia ya dhambi na adhabu kwa njia mbadala ya mtu asiyekuwa na hatia (kama vile Yohana 1:29,36, II Kor. 5:21; I Pet.1:19).

Mstari pia unaonyesha gharama ya Mwa. 3:15. Yesu alibeba laana, (kama vile Gal. 3:13) na akafa (kama vile II kor. 5:21) badala ya mwanadamu aliyeanguka.Wokovu waweza kuwa bure, lakini kwa kweli sio rahisi kihivyo.

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

. AGANO LA KALE
- A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
  1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25, 27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
  2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
     a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
     b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
     c. YHWH ataikomboa Israeli kutoka katika dhambi na uasi wao (Zab. 130:7-8)
- B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
  1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
     a. Kimaumbile
     b. Kijamii
     c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
  2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
     a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
     b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
  3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (yaani, *go'el*, BDB 145).
  4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
     a. Baba
     b. Mme
     c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

. AGANO JIPYA
- A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
  1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisi ni wa Kristo.
  2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laana" utedaji uliojikita ndani

ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!

3. *Luō,* "kuweka huru"
    a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
    b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
        1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
        2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
        3) Kuwa uasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
    c. *Lutrōsis,* "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
        1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
        2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
        3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
4. *Apolytrōsis*
    a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
        1) Luka 21:28
        2) Warumi 8:23
        3) Waefeso 1:14; 4:30
        4) Waebrania 9:15
    b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
        1) Warumi 3:24
        2) 1 Wakorintho 1:30
        3) Waefeso 1:7
        4) Wakolosai 1:14
5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kithiolojia katika Agano Jipya.
1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18, 23; 6:23).
2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, thiolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa

ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

**3:25**
**NASB "Ambaye Mungu alijionyesha hadharani"**
**NKJV "Ambaye Mungu alimtanguliza"**
**NRSV "Ambaye Mungu alimwekambele"**
**TEV "Mungu aliyemtoa"**
**NJB "Aliyeteuliwa na Mungu"**

Hii ni KAULI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU *Protithemi* (katika Rum. 1:13 na Efe. 1:9 ikiwa na maana "kukusudia", kama NOMINO katika Rum. 8:28), ikiwa maana kuwa Mungu peke yake aliweka wazi roho yake na kusudi kwa kifo cha Yesu (kama vile Efe.1:9; Gal. 3:1). Mpango wa Mungu wa ukombozi wa milele (kama vile Matendo 2:23;3:18;4:28;13:29;26:22;na mada maalum katika 1:5) uliyohusu sadaka ya Yesu (kama vile 53:10,Ufu. 13:8). Angalia nukuu katika 9:11

◙"**Kuonyesha**" Neno hili la Kiyunani *"endeiknumai*" (*endeixis*, kama vile 3:25,26) linatumika mara kadhaa katika warumi (kama vile 2:15;17:23:LXX Kut. 9:16) maana yake kuu ni "kujidhihirisha" au "kujionyesha." Mungu alitaka wanadamu kuelewa wazi kusudi lake la ukombozi, mipango na "haki." Muktadha huu unaweka Biblia kwa mtazamo wa kiulimwengu.

1. Kuhusu tabia ya Mungu
2. Kuhusu kazi ya kristo
3. Kuhusu hitaji la wanadamu
4. Kuhusu kusudi la ukombozi

Mungu anataka tuelewe! Dhana hii ni nyeti kwa ajili ya kuelewa barabara ukristo. Baadhi ya maneno na mafungu yana mkanganyiko au yanaweza kueleweka kwa namna nyingine tofauti, lakini kwa ujumla wake yako wazi na yamenyooka. Muktadha huu ni dira ya thiolojia ya injili.

◙
**NASB "kama upendeleo katika damu yake**
**NKJV "kuwa upendeleo kwa damu yake**
**NRSV "Kama sadaka ya upatanisho kwa damu yake**
**TEV "hivyo kwamba kwa damu yake itakuwa ni njia ambayo kwa dhambi za watu zitasamehewa.**
**NJB "kutoa sadaka maisha yake ili kupata suluhu.**

Katika ulimwengu wa Warumi wa Uyunani neno hili lilibeba dhana ya kurejesha ushiriki na Uungu uliotenganishwa kwa gharama inayolipwa. Ingawa, haitumiki kwa maana hivyo katika kitabu cha kale. Ilitumika kale na katika Waebrania 9:5 kutafsiri "kiti cha neema"(kama vile Kut. 25:21-22; Walawi 16:12-15), ambalo lilikuwa kifuniko cha sanduku la agano lililowekwa mahali patakatifu pa patakatifu, sehemu ambapo upatanisho ulipatikana kwa niaba ya taifa siku ya upatanisho (kama vile Walawi 16). Ni dhahiri Paulo anatumia maneno ya utoaji toka katika mtindo wa Waisrael walivyotoa dhabihu (kama vile Walawi. 1-7), maneno haya (kama vile upendeleo, fidia, dhabihu) yanaeleweka kwa kuhusishwa na maneno toka agano la kale yaliyotoka kwa Mungu. Kwa hiyo Paulo yampasa aeleze umuhimu wao kwa wanadamu wote. YHWH alijidhihirisha yeye mwenyewe kwa IbrahImu/Israeli kujidhihirisha mwenyewe kwa wote; wote wako kwa mfano wake; wote wameasi;wote wanaweza kuokolewa kwa njia ya imani katika kristo Yesu (masia wa Wayahudi).

Neno hili lapaswa kushungulikiwa kwa namna isiyoweza kupunguza maudhi ya Mungu kwa dhambi, bali ithibitishe msimamo wake wa ukombozi wa wenye dhambi.Mjadala mzuri unapatikana katika kitabu cha James Stewart kiitwacho "*A man in Christ*, uk. 214-224.njia moja ya kukamilisha hili ni kutafsiri neno ili kwamba liweze kuonesha kazi ya Mungu katika kristo "sadaka ya upendeleo" au "yenye nguvu ya kupendelea."

"Katika ya damu yake" kuna njia ya kiebrania ya kurejelea sadaka mbadala ya mwanakondoo wa Mungu asiye na hatia (kama vile Yohana 1:29). Kuielewa kikamilifu dhana hii Walawi 1-7 ni muhimu sana kadhalika na siku ya

upatanisho katika sura ya 16. Damu inamaanisha maisha yasiokuwa na dhambi yaliyotolewa kwa niaba ya wenye hatia (kama vile Isa. 52:13-5 3:12) mmoja alikufa kwa ajili ya wote (kama vile 5:12-21).

◙"**kupitia imani**" Hapa pia pana namna(kama vile 1:17,3:22,25,26,27,28,30,)kwa yeyote na faida binafsi ya mtu yeyote iliyopo katika mbadala wa kifo cha Kristo. Fungu hili limeondolewa katika miswada ya kale kutoka karne ya tano (pia,andiko la Kiyunani lilotumika na Chrysostom), na karne ya 12, MS (2127), linajumuishwa katika miswaada mingineyo ya zamani ya kiyunani. Mengine ni KIFUNGU KILICHO WAZI (kama vile MSS P, B, $C^3$, $D^3$) yakiwa na "imani", mengine hayana (kama vile MSSℵ, C*,D*, F,G) hata hivyo, hii haiathiri maana. $UBS^3$ Inaunganisha yote pamoja kama D (bila mashaka)

◙"**kuonyesha haki yake**"-Mungu lazima afanane na tabia yake na neno lake (kama vile Mal.3:6). Katika Agano la Kale nafsi itendayo dhambi lazima ife (kama vile Mwa. 2:17; Ezek. 18:4,20). Mungu alisema hatamwachia huru mwenye hatia (kama vile Kut. 23:7). Upendo wa Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka ni mkubwa alikuwa tayari afanyike mtu, kutekeleza sheria, na kufa kwa niaba ya mwanadamu aliyeanguka (kama vile 5:12-21). Mapenzi ya Mungu na haki hukutana katika Yesu (kama vile mstari wa 26)

◙

**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"Alisahau dhambi zilizotendwa awali"**
**TEV** **"Enzi zile alivumilia, na kutojali dhabi za watu"**
**NJB** **"Enzi za nyuma, wakati dhambi hazikuadhibiwa**

Neno "Pasaka" ni *paresis*, ambalo linatumika hapa tu katika Agano la Jipya na kamwe si katika maandiko ya kale.Wahanga wa Kiyunani na wafasiri wa Jerome wakalichukua kama lilivyomaanisha katika fasihi za Kiyunani "msamaha wa deni" (kama vile moulton na milligan uk- 493). Ingawa "*pariēmi*", KITENZI mahali kilipochukuliwa kinamaanisha "kuruhusu kupita pembeni"au "kupumzika" (kama vile Luka 11:42)

Kwa hiyo swali ni kwamba je Mungu alisamehe dhambi hapo kale kwa kuangalia kazi ya baadaye ya kristo au aliziacha tu akijua kifo cha Kristo kilicho mbele kingeshughulika na tatizo la dhambi? Matokeo ni yale yale.Dhambi ya mwanadamu, ya wakati ulioyopita, uliyopo na ujayo inashughulikiwa na sadaka ya kristo.

Hili lilikuwa tendo lililopita la neema ya Mungu kwa kuangalia mbele kazi ya kristo (kama vile Mdo. 17:30, Rum. 4:15, 5:13) kadhalika tendo lililopo na lijalo(kama vile mstari wa 26).Mungu hakuchukulia na hatachukulia dhambi kirahisi,lakini anakubali sadaka ya Yesu kama suluhisho kamili na la mwisho kwa uasi wa mwanadamu. Hapana tena kizuizi kwa ushirika wa kweli na yeye, ambalo ndilo lilokuwa lengo lake la uumbaji (kama vile Mwa. 1:26-27).

**3:26** Neno "Haki" katika mstari wa 25 kwa maelezo ya asili unahusiana na "haki" na "mtenda haki" kwa mstari wa 26. Mungu anapenda tabia yake kudhihirishwa ndani ya maisha ya wamwaminio kupitia imani katika Kristo. Yesu anakuwa haki yetu (kama vile II Kor. 5:21), lakini waaminio lazima nao wanapaswa kuendana na "haki" yake, na kufanana naye (kama vile 8:29; Mt. 5:48; Law.19:2 (tazama mada maalum katika 1:17)

**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"Yule ambaye ana imani katika Yesu"**
**TEV** **"Kila mmoja anayemwamini Yesu"**
**NJB** **"Kila aliye na imani na Yesu"**
**NEB** **"Yeyote yule anayeweka imani yake kwa Yesu"**
**NET** **"Yule ambaye huishi kwa sababu ya uaminifu wa Yesu"**

Andiko la kiyunani linalo neno "Yule mwenye imani kwa Yesu". Ugumu unakuja katika wingi wa matumizi ya KIMILIKISHI (Angalia G.B; Caird "*the language and Imagery of the bible* [Lugha na taswira ya biblia] tafsiri nyingi za Kingereza zinaitazama kama kusadiki, imani, kuamini kwa mtu katika Yesu Kristo, Biblia ya NET inalichukulia kama linavyorejewa katika 3:22. Hata hivyo, mstari wa 22 una rejea zote mbili katika

1. "Uaminifu wa Yesu"

2. “Imani ya Waumini”

Wokovu ni matokeo ya uaminifu wa Yesu ambao sharti upokelewe (kama vile mstari wa 30

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 3:27-30**
**27 Ku wapi, basi, kujisifu? Kumefungiwa nje. Kwa sheria ya namna gani? Kwa sharia ya matendo? La! Bali kwa sharia ya imani. 28 Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sharia. 29 Au je! Mungu ni Mungu wa Wayahudi tu? Sie Mungu wa mataifa pia? Naam, ni Mungu wa mataifa pia; 30 Kama kwa kweli Mungu ni mmoja, atakayewahesabia haki wale waliotahiriwa katika imani, nao wale wasiotahiriwa kwa njia ya imani atawahesabia haki kwa njia ya imani hiyo hiyo.**

**3:27“Yako wapi sasa majigambo”** Kuwepokwa kwa KIFUNGU kinachoendana na neno “majigambo” kinaweza kuonyesha majivuno ya wayahudi (kama vile 2:17, 23). Injili ni ya upole. Mwanadamu aliyeanguka (Wayahudi na wamataifa) hawawezi kujisaidia wenyewe (kama vile Efe. 2:8-9) taz mada maalumu: majigambo katika 2:17.

Ni muhtasari mfupi unaofafanua maelezo yangu ya awali. Ingawa mwanadamu hawawezi stahili upendo na msamaha wa Mungu haina maana kwamba hawana sehemu katika suala la wokovu wao. Wanadamu sharti watambue dhambi zao/ hatiana kukubalia walichopewa na Mungu katika Kristo. Mungu anashughulika na aliyeanguka kwa njia ya “agano.” lazima tuitike na tuendelee kuitikia.

1. Toba
2. Imani
3. Utii
4. Uvumilivu

Tuna sehemu muhimu sana katika uhusiano wetu na Mungu. sisi ni waitikiaji! Lakini ni sharti tuitike! Hiari ya mtuni muhimu kama yalivyo mafundisho ya Biblia na Uungu. Biblia, kama kitabu cha mashariki, kilileta ukweli pale palipo na mvutano wa wawili.

## MADA MAALUM: FASIHI YA KIMASHARIKI (mafumbo ya kibiblia)

1. Utambuzi huu wa ndani (yaani, kwamba Biblia ni kitabu cha mashariki, si kitabu cha magharibi) umekuwa msaada zaidi kwangu binafsi kama mtu anayependa na kuiamini Biblia kama Neno la Mungu. Katika kujaribu kuichukulia Biblia kwa umakini inakuwa dhahiri kwamba maandiko tofauti tofauti yanaifunua kweli katika uteuzi, si katika namna za kimfumo. Andiko moja lililovuviwa haliwezi kufuta ama kushusha andiko lingine lililovuviwa! Kweli huja katika kuyafahamu Maandiko (Maandiko yote, si sehemu tu, iliyovuviwa, kama vile 2 Tim. 3:16-17), si kunukuu kifungu kimoja (kuhakiki maandiko)!
2. Kweli nyingi za kibiblia (fasihi ya mashariki) zinawasilishwa katika are presented in mtindo wa lahaja ufanano wa kimafumbo (kumbuka waandishi wa Agano Jipya, isipokuwa Luka, ni wanafikra wa Kiebrania, walioandika katika Kiebrania cha kawaida. Fasihi ya Hekima na Fasihi ya Ushahiri inawasilisha kweli katika mfuatano. Huu ufanano kinzani hutenda kazi kama fumbo. Huu uigaji wa ufanano hutenda kazi kama ufanano wa vifungu). Kwa kiasi fulani yote kwa ni ya kweli kwa usawa! Mafumbo haya ni ya kimaumivu kwa mapokeo ya kimadhehebu yaliyotunzwa kwa upendo mkubwa!
   a. Maamuzi ya kabla dhidi ya utashi huru wa mwanadamu
   b. Ulinzi wa mwamini dhidi ya hitaji la ustahimilivu(angalia Mada Maalum: Uatahimilivu)
   c. Dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
   d. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama Mwanadamu
   e. Yesu kuwa sawa na Baba dhidi ya Yesu aliyekuwa mtii kwa Baba
   f. Biblia kama neno la Mungu dhidi ya uandishi wa kibinadamu
   g. Kutotenda dhambi (ukamilifu, kama vile Warumi 6) dhidi ya kutenda dhambi kidogo
   h. Kuhesabiwa haki kwa mwanzo moja kwa moja dhidi ya utakaso endelevu (angalia Mada Maalum: Utakaso)
   i. Kuhesabiwa haki kwa imani (Warumi 4) dhidi ya kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo (kama vile

Yakobo 2:14-26)
j. Uhuru wa Mkristo (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33) dhidi ya wajibu wa Mkristo (kama vile Gal. 5:16-21; Efe. 4:1)
k. Mungu apitaye uwezo wa kibinadamu dhidi ya uwepo wake wa kila mahali
l. Hatimaye Mungu asiyejulikana dhidi ya Mungu ajulikanaye katika maandiko na ndani ya Kristo.
m. Sitiari nyingi za Paulo kwa ajili ya wokovu
    1) Uasilishaji (kupanga mtoto/kumtwaa)
    2) Utakaso
    3) kuhesabiwa haki
    4) Kukombolewa
    5) Kutukuza
    6) Majaaliwa
    7) Upatanisho
n. Ufalme wa Mungu uliopo dhidi ya ule utakaotimia mbeleni
o. Toba kama zawadi ya Mungu (kama vile Mdo.11:18; Rum. 2:4; 2 Tim. 2:25) dhidi ya toba kama mwitikio wa lazima kwa ajili ya wokovu (kama vile Marko 1:15; Mdo. 20:21)
p. Agano la Kale ni la kudumu dhidi ya Agano la Kale limekwisha kupita na ni batili na utupu (kama vile Mt. 3:17-19 dhidi ya Mt. 5:21-48; Warumi 7 dhidi ya Wagalatia 3)
q. Waamini ni watumishi/watumwa au wana/warithi

◙“**Imetengwa**”neno hili (*ek*-[nje] ukiongeza na *kleiō̄* [funga] linatumika tu hapa katika Gal. 4:17. kifasihi linamahanisha “kufungiwa nje”

◙“**Kwa sheria ya imani**” Agano jipya la Mungu la Yer. 31:31-34 (Ezek. 36:22-38) halipo kiutendaji bali kwa kuamini/imani/kusadiki (*pists*) katika tabia yake na ahadi. Agano la kale na Agano jipya yote yalikusudia kubadili mwanadamu aliyeanguka kuwa na tabia ya Mungu (mwenye haki yaani Walawi 19:2; Mt. 5:48; Rum. 8:29)

**3.28: “Tudumishe kuwa mtu huthibitishwa kwa imani mbali na matendo ya sheria!.”** Hu ni ufupisho wa 3:21-26 na ikionyesha dalili ya sura ya 4-8 (kama vile II Tim. 1:9; Tito 3:5). Wokovu ni zawadi ya bure kupitia katika imani kwa kazi ya kristo aliyoikamilisha (kama vile 3:24; 5:15, 17;6:23; Efe.2:8-9). Hata hivyo ukomavu ni “gharama kwa kila kitu”maisha ya utii, huduma na kuabudu (Gal. 5:6; Efe. 2:10; Flp. 2:12 na tazama nukuu katika 1:5)

**3:29** kusudi la Mungu siku zote limekuwa ni kukomboa wanadamu wote walioumbwa kwa mfano wake (Mark 1:26,27;5:1;9:6). Ahadi ya ukombozi ya mwanzo 3:15 ni kwa wana wote wa Adamu. Alimchagua Abraham ili kwamba achague ulimwengu (kama vile Mwa. 12:31; Kut. 19:4-6; Yohana 3:16).

Mstari huu, Kama 3:9, unambaini mvutano ndani ya kanisa la Roma kati ya uongozi wa Wayahudi walioamini, ambao huenda waliondoka Roma kufuata amri ya Mfalme Nero ya kuwakataza ibada za Wayahudi iliyopelekea kuamini uongozi wa watu wa mataifa, waliochukua nafasi yao. Sura 9-11 yanaweza pia kuonyesha mvutano huu.

◙
**3:30:**
**NASB “kwa vile hakika Mungu ni mmoja”**
**NKJV “kwa vile kuna Mungu mmoja tu”**
**NRSV “kwa vile Mungu ni mmoja tu”**
**TEV “Mungu ni mmoja”**
**NJB “kwa vile kuna Mungu mmoja tu”**

Hii ni SENTENSI DARAJA LA KWANZA YENYE MASHARTI ambayo inachukuliwa kama kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi la kazi yake ya kifasihi. Kama imani ya kuwepo Mungu mmoja ni kweli, basi ni lazima kwamba yeye ni Mungu wa wote.

## MADA MAALUM: IMANI KATIKA MUNGU MMOJA

Mwanadamu siku zote amekuwa akihisi kuna zaidi ya ukweli kuliko huu unaoonekana (yaani kuathiriwa na vitu nje ya uwezo, kama vile dhoruba, kupatwa kwa jua na mwezi, kuanguka kwa vimondo, hali ya hewa, matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa sayansi ya binadamu wanatwambia kuwa wanakutana na vitu katika makaburi ya wanyama wa kale waliowahi kuishi ambavyo yumkini ni viashiria ya maisha yajayo, ambayo yanaweza kuonekana kama mwendelezo wa maisha ya baadaye.

Tamaduni ya kwanza kuandikwa ilikuwa ni ya wakati wa kiangazi (Hedekeli Kusini, Mito Yufrati), ilianza miaka ya 10,000 - 8,000 K.K. Waliandika mashairi kuelezea mawazo yao kwa Mungu na namna wanavyojamiiana. Tena, zaidi kama wanadamu pamoja na madhaifu yao yote. Tamaduni zao zilikuwepo katika namna za midomo zamani hata kabla hazijaandikwa.

Kulikuwa na kukua kwa kithiolojia kutoka

1. kuabudu wanyama mpaka
2. kuabudu miungu wengi mpaka
3. mungu mkuu (kuabudu miungu wawili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (mmoja na mmoja tu binafsi Mungu mwenye maadili asiye na asili ya kike), si tu "mungu mkuu" ya miungu wengi au mungu mzuri kama miungu ye upili ya kiashuru (wafuasi wa Zoroaster), ni pekee kwa Israeli (Ibraham na Ayubu, 2000 K.K.). ni mmoja tu wa pekee asiye patikana patikana katika Misri (Amenhotep IV, pia akijulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 K.K., aliyeabudu *Aten*, mungu jua, kama mungu pekee). Angalia J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kurasa za 216-217.

Dhana hii inaelezea katika tungo kadhaa katika Agano la Kale

1. "hakuna kama YHWH wetu Elohim," Kutoka 8:10; 9:14; Kumbukumbu la Torati 33:26; 1 Wafalme 8:23
2. "Hakuna mwingine zaidi Yake," Kumbukumbu la Torati:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
3. "Hakuna kama wewe," 2 Samweli 7:22; Yeremia 10:6
4. "wewe pekee ndiwe Mungu," Zaburi 86:10; Isaya 37:16
5. "Kabla yangu hakukuwa na Mungu na baada yangu hatotokea," Isaya 43:10 adherence
6. "hakuna mwingine; zaidi yangu. . .hakuna mwingine," Isaya 45:5,6,22
7. "Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isaya 45:7 (kama vile Amosi 3:6)
8. "hakuna mwingine, hakuna Mungu mwingine," Isaya 45:14,18
9. "hakuna mwingine isipokuwa," Isaya 45:21
10. "hakuna kama mwingine;. . .hakuna kama mimi," Isaya 46:9

Lazima kukiri kuwa fundisho hili muhimu limefunuliwa katika maendeleo katika njia. Kauli ya mwanzo ingeweza kueleweka "utii kwa mungu mmoja kati ya wengi" au kuabudu mungu mmoja kwa kimatendo (kuna miungu mingine, yani Joshua 24:15; 1 Wafalme 18:21), lakini Mungu mmoja tu kwa ajili yetu (kama vile Kutoka 15:11; 20:2-5; Kumbukumbu la Torati 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Wafalme 8:23; Zaburi 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kuonesha umoja (Hali ya Kifalsafa ya Mungu mmoja) ni mapema (kama vile Kutoka 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumbukumbu la Torati 4:35,39; 33:26). Madai yaliyokamili na yashinda nayo yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Agano la Kale linapunguza miungu ya mataifa kama

1. Uumbaji wa kibinadamu – Kumbukumbu la Torati 4:28; 2 Wafalme 19:18; Zaburi 115:4-8; 135:15-18; Isaya 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Yeremia 10:3-5; Ufunuo 9:10
2. mapepo – Kumbukumbu la Torati 32:17; Zaburi 106:37; Isaya 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufunuo 9:20
3. ubatili, utupu – KumbuKumbu la Torati 32:21; 2 Wafalme 17:15; Zaburi 31:6; Isaya 2:18; 41:29; Yeremia 2:5; 10:8; 14:22; Yeremia 2:5; 8:19
4. hakuna miungu – Kumbukumbu la Torati 32:21; 2 Nyakati 13:9; Isaya 37:19; Yeremia 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufunuo 9:20

Agano Jipya linaelezea katika Kumbukumbu la Torati 6:4 katika Warumi 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu alinukuu kama amri ya kwanza katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Agano la Kale pia kama Agano Jipya, linaelezea ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (mapepo, malaika), lakini muumbaji mmoja tu/Mungu mkombozi (YHWH, Mwanzo 1:1).

hali ya kuwepo kwa Mungu mmoja kibiblia kunatabia zifuatazo

1. Mungu ni mmoja na wa pekee ((ontology) nadharia inayojishughulisha na asili ya uhai inadhaniwa, haijawekwa bayana)
2. Mungu ni wa binafsi (kama vile Mwanzo 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni mwadilifu (kama vile Mwanzo 34:6; Nehemia 9:17; Zaburi 103:8-10)
4. Mungu aliwaumba wanadamu katika sura yake (Mwanzo 1:26-27) kwa ajili ya ushirika (yaani #2). Ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kutoka 20:5-6)

Kutoka katika Agano Jipya

1. Mungu ana milele tatu, udhihirisho wa nafsi (angalia Mada Maalum: Utatu)
2. Mungu kwa ukamilifu wake amefunuliwa kikamilifu ndani ya Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:2-3)
3. Mpango wa milele wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni sadaka ya Mwanawe wa Pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Fil. 2:6-11; Waebrania)

◙**"Atahalalalisha wariotahiriwa kwa imani"** Neno la kiyunani "kuhalalisha"linatoka kwenye shina moja naneno "haki" taz mada maalum 1:17. Kuna njia moja tu ya kuwa sawa na Mungu (kama vile Rum. 9:30-32). Vigezo viwili vya wokovu ni imani na toba (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16, 19; 20:21; angalia nukuu katika 1:5). Hii ni kweli kwa wote Wayahudi na Wayunani

◙"**kwa imani -- kupitia katika imani**" Kuna usambamba wa wazi katika ibara hizi mbili. VIVUMISHI *ek* na *dia* vinatumika hapa kwa kufanana.Hakuna utofauti unaokusudiwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 3:31**
**31 Basi je! Twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sharia**

◙
**3:31**
**NASB "Basi je! Twaibatirisha sheria kwa imani hiyo?**
**NKJV "Basi je! Twaifanya sheria kuwa tupu kwa imani hiyo?**
**NRSV "Basi je! Tuitupe sheria kwa imani hii?"**
**TEV "Inamaanisha kuwa kwa imani hii, tuitupilie mbali sheria?**
**NJB "tuna maanisha kuwa, imani inaifanya sheria isifae?"**

Agano jipya linalielezea Agano la kale katika njia mbili

1. Limevuviwa, ni ufunuo alioutoa Mungu ambao utakuwepo daima (Mt. 5:17-19; Rum. 7:12,14,16)
2. Limechakaa na kupitwa na wakati (kama vile Ebr.8:13)

Paulo alitumia neno "batili" takribani mara ishirini na tano. Inatafsiriwa "kufanya ubatili na utupu" "kufanya kitu kutokuwa na athari" taz mada katika 3:3.kwa Paulo, sheria ilikuwa ni ulinzi (kama vile Gal.3:23) na mkufunzi (kama vile Gal. 3:24) lakini haikutoa uzima wa milele (kama vile Gal. 2:16; 19; 3:19). Haya ni mazingira ya hukumu ya wanadamu (Gal. 3:13; Kol. 2:14) sheria ya Musa ilifanya kazi kwa pamoja kama ufunuo na kipimo cha uadilifu kama ilivyofanya kwa "mti wa ujuzi wa mema na mabaya".
Kuna uwalakini kuhusu Paulo alichokimaanisha juu ya "sheria"

1. Mfumo wa kazi za haki za dini ya Kiyahudi.
2. Hatua ya waumini wa watu wa mataifa kuingia kwenye wokovu katika kristo (Wayahudi katika Wagalatia)
3. Kipimio/kiwango ambacho wanadamu wote hawakuweza kukifikia (kama vile Rum. 1:18-3:20; 7:7-25; Gal. 3:1-29).

◙"**tumeasisi sheria"** ukiangazia fungu lililopita,fungu hili linamaana ngani? Lingeweza kuonyesha kuwa

1. Sheria haikuwa njia ya wokovu bali mwongozo ulioendeleza maadili mema.

2. Ilishuhudiwa katika mafundisho ya “uthibitisho kwa njia ya imani “3:21; 4:3 (Mwa.15:6; Zab. 32:1-2, 10-11)
3. Udhaifu wa sheria (uasi wa mwanadamu kama vile Rum. 7; Gal.3) ulikamilishwa kabisa na kifo cha kristo (8:3-4)
4. Kusudi la ufunuo ni kurejesha taswira ya Mungu kwa mwanadamu.

Sheria, baada ya “haki ya kimahakama” inakuwa mwongozo wa Haki au ufanano wa kristo, angalia Mada maalum “mtazamo wa Paulo kuhusu sheria ya Musa 13:9.

Kitendawili kinachoshangaza ni kwamba sheria ilishindwa kuanzisha haki ya Mungu, lakini kutokana na kubatilishwa kwake, kwa njia ya neema ya karama ya Mungu kupitia imani, Mkristo anaishi maisha ya haki na Kimungu. Lengo la sheria limefikiwa, siyo kwa utendaji wa Mwanadamu, bali kwa zawadi huru ya neema ya Mungu katika kristo! Kwa “kuanzisha” tazama mada maalum: Simamia katika 5:2

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Eleza kwa kifupi Warumi 3:21-31 katika maneno yako mwenyewe
2. Kwa nini Mungu hakuzijali dhambi za mwanadamu za enzi ya nyuma (mstari wa 25)?
3. Ni vipi mwamini wa Agano la kale aliokolewa toka dhambini (3:25)?
4. Ni kwa vipi imani katika Kristo inaithibitisha sheria (3:31)?

# WARUMI 4

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mfano wa Abrahamu | Ibrahimu anathibitishwa kwa imani | Abrahamu alithibitishwa kwa imani | Mfano wa Ibrahimu | Ibrahimu alithibitishwa kwa imani |
| 4:1-12 | 4:1-4 | 4:1-8 | 4:1-8 | 4:1-8 |
| | Daudi anasherekea ukweli ule ule | | | Anathibitishwa mbele ya tohara |
| | 4:5-8 | | | |
| | Abrahamu anathibitishwa mbele ya tohara | | | |
| | 4:9-12 | 4:9-12 | 4:9-12 | 4:9-12 |
| Ahadi inabainishwa kwa imani | Ahadi inatolewa kupitia imani | Wazawa wa kweli wa Ibrahimu | Ahadi ya Mungu inapokelewa | Kutothibitishwa kwa utii wa sheria |
| 4:13-25 | 4:13-25 | 4:13-15 | 4:13-15 | 4:13-17 |
| | | 4:16-25 | 4:16-25 | Imani ya Ibrahimu kifani cha mkristo |
| | | | | 4:18-25 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Thiolojia ya kushitua ya Paulo iliyosemwa katika 3:21-31 inasisitiza kuwa mwanadamu aliyeanguka alikwisha tangazwa kuwa na haki kwa Mungu kama zawadi huru. Mbali kabisa na sheria ya Musa. Bila shaka Paulo alikuwa na upinzani wa Kiyahudi katika fikra zake. Paulo sasa anajaribu kuonyesha kuwa neno lake halikuwa la mwanzo, (kama vile 3:21b) kwa kutoa mifano ya agano la kale kutoka kwa Abrahamu pamoja Daudi (kama vile mistari 6-8)

B. Warumi 4 inatoa ushuhuda kutoka katika sheria ya Musa, Mwanzo hadi Kumbukumbu la torati, kwa mafundisho ya kuthibitishwa kwa neema kupitia imani. Hii inafupishwa katika 3:21-31. Kwa Myahudi, nukuu kutoka kwa maandiko ya Musa yalikuwa na uzito kithiolojia, hasa kuhusiana na Ibrahimu, aliyeonekana kama Baba wa taifa la Wayahudi. Daudi alionekana kama aina ya Masia ajaye (kama vile 2 Samweli 7)

C. Mvutano katika Rumi kati ya Wayahudi waaminio na watu wa mataifa waaminio ungeweza kuwa tukio la mjadala huu. Inawezekana viongozi wa wayahudi, wakristo walijisikia kulazimishwa na Nero (ambaye alifuatilia taratibu za Kiyahudi) kuondoka Roma. Kwa kipindi, nafasi yao ilichukuliwa na viongozi Wakristo wa Mataifa. Kurejea kwa kundi la kwanza kulizua mtafaruku wa nani awe katika nafasi ya uongozi

D. Warumi 4 inaonyesha kwamba mwanadamu aliyeanguka amekuwa daima akiokolewa kwa neema ya Mungu kupitia imani na toba kwa Mungu kwa mahusiano na mwanga wa kiroho walionao (Mwa. 15:6; Rum 4:3). Kwa njia nyingi Agano jipya (injili, kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) sio hasa hasa tofauti na Agano la Kale.

E. Njia hii ya haki kwa neema kupitia imani iko wazi kwa wote, na sio tu kwa viongozi wa dini ama watu wa taifa la Israel. Paulo hapa anaendeleza na kupanua hoja yake ya kithiolojia kwa kumtumia Abrahamu, hoja ambayo alisha ianzisha katika Wagalatia 3.

F. Lazima nikiri kwamba, kama uinjilisti Rum. 3:21-31; 4:1-25; 5:1-21 na Wagalatia 3 ni maandiko nyeti. Yanaelezea ukristo kwa namna ambayo naweza kuelewa. Tumaini langu liko kwa:-
   1. Neema ya Mungu
   2. Kazi ya Kristo
   3. Kuaminika kwa mafundisho ya neno la Mungu
   4. Maandiko yaliyo wazi ya Paulo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:1-8**
**[1]Basi, tusemeje juu ya Ibrahimu, baba yetu kwa jinsi ya mwili? [2]Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu. [3]Maana maandiko yasemaje? IBRAHIMU ALIMWAMINI MUNGU, IKAHESABIWA KWAKE KUWA HAKI. [4]Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni. [5]Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki. [6]Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo, [7]HERI WALIOSAMEHEWA MAKOSA YAO, NA WALIOSITIRIWA DHAMBI ZAO. [8]HERI MTU YULE AMBAYE MUNGU HAMHESABII DHAMBI.**

**4:1 "Tuseme nini basi, kwamba Ibrahimu, baba yetu"** Jina la Ibrahimu lina maanisha –"Baba wa watu wengi (kama vile mistari ya 16-18). Jina lake halisi, Abraham, lilimaanisha "Baba aliyeinuliwa." Mbinu ya kifasihi iliyotumika hapa inaitwa mbinu ya makemeo (kama vile 4:1; 6:1; 7:7; 8:31; 9:14, 30). Sababu ya kutumia Ibrahimu (Mwa. 11:27; 25:11) kama mfano ni kuwa kama :-
1. Sababu Wayahudi waliweka manufaa hayo kwa asili ya Taifa lao (Mt. 3:9; Yoh. 8:33-37,39)
2. Sababu imani yake binafsi inatoa mfano wa namna ya agano (Mwa. 15:6)

3. Imani yake ilitangulia kabla ya kumpa Musa sheria (kama vile Kut. 19:20).
4. Alitumia walimu bandia (Wayahudi, kama vile Wagalatia)

Kwa sababu hii alama za zama hizo zilitumika kati ya:-

1. Wahenga, MSS א*[2], A, C*
2. Baba, MSS א[1], C[3], D, E, G.

Bila shaka lilihusu suala la babu wa Abrahamu (yaani viongozi wa dini, Paulo anahutubia Wayahudi) wa taifa la Israeli dhidi ya Ibrahimu baba wa wote wanaoshughulikia imani kwa Mungu (Baba wa wote, Wayahudi na watu wa mataifa 2:28-29)

◙**"Mwili" –**Tazama mada maalum katika 1:3

**4:2 "Kama"** HII NI SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA (kama vile A.t Robertsm, *Word pictures*, juzuu ya 4 ukurasa wa 350) ambayo inafikiriwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kifasihi. Huu ni mfano mzuri wa SENTENSI DARAJA LA KWANZA YENYE MASHARTI ambayo si sahihi kiuhalisia, lakini inasaidia kutetea wazo la kithiolojia. (kama vile mstari wa 14).

Joseph A. Fitzmyer, *The Anchor Bible,* juzuu ya 3 uk. 372, anasema hii inaweza kuwa mchanganyiko wa SENTENSI SHURUTISHI na sehemu ya kwanza kuwa DARAJA LA PILI (Kinyume na ukweli "kama", Ibrahimu alihalalishwa kwa kazi ambapo ilikuwa sivyo…") na ya pili ikiwa ni DARAJA LA KWANZA.

◙**"Kuthibitishwa kwa kazi"** Hii ni kinyume cha kuthibitishwa kwa neema kupitia imani katika Kristo .Kama njia hii ya wokovu kwa juhudi za mwanadamu (4:4) zingewezekana, ingeifanya huduma ya Kristo iliyo muhimu kutokuwa na umuhimu. Uhalalisho kwa matendo ya sheria ndiyo hasa viongozi wa dini wakati huu walichotetea kuhusiana na Abrahamu (kama vile *hekima* – 10:5 kusanyiko la Kristo 44:20-21; I Mac. 2:52, Jubilei 6:19-20; 15:1-2) Paulo, kama mwanafunzi wa dini angelikuwa anatambua kabisa maandiko haya.

Hata hivyo, Agano la kale linaonyesha wazi kukosa uwezo kwa binadamu aliyeanguka katika kufanya agano la kazi ya Mungu. Kwa hiyo Agano la kale likawa ni laana na hukumu ya kifo (kama vile Gal. 3;13; Kol. 2:14). Wasomi wa Kiyahudi walijua Abrahamu alikuwepo kabla ya sheria ya Musa, lakini waliamini alitarajia sheria hii na kuitunza (kama vile Kusanyiko la Kristo 44:20 na Jubilee 6:19; 15:1-2).

◙**"alikuwa na sababu ya kujivunia"** Dhima hii daima huonekana katika maandiko ya Paulo. Na asili yake kama Mafarisayo ilimhamasisha kwa tatizo hili (kama vile 3:27; 1 Kor 7:29; Efe 2:8-9) Angalia Mada maalum: kujivunia.

◙

**4:3**

**NASB, NKJV,**

**NRSV, TEV** **"Ibrahimu alimwamini Mungu"**

**NJB** **"Ibrahimu aliweka imani yake kwa Mungu"**

Hii ni nukuu kutoka Mwa 15:6 Paulo anaitumia mara tatu katika sura hii (kama vile 4:3, 9,22), inachoonyesha umuhimu wake katika uelewa wa kithiolojia wa Paulo kuhusu wokovu. Neno "imani" katika Agano la Kale lilimaanisha "wema /wongofu" au hali ya kuaminika na ilikuwa ni kielelezo cha asili/alivyo Mungu, sio asili yetu. Ilitokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*) iliyomaanisha "kuwa na hakika au imara".

Kulinda/kutunza imani ni :-

1. Kufikiri ukweli kifikra
2. Uamuzi/ dhamira
3. Stadi/mfumo wa maisha
4. Kimsingi uhusiano (kumkubali/kumkaribisha mtu).

Tazama Mada Maalum: kukiri, kuamini, imani na uaminifu katika AGANO LA KALE katika 1:5.

Lazima isisitizwe kwamba, imani ya Abrahamu haikuwa kwa Masihi aliyetegemewa kuja, bali katika ahadi ya Mungu kwamba angepata mtoto na wazawa. (kama vile Mwa. 12:2; 15:2-5; 17:4-8; 18:14) Ibrahimu alikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu. Lakini bado alikuwa na mashaka na matatizo kuhusu ahadi hii. Kusema kweli

ilichukua miaka kumi na tatu kutekelezwa imani yake haba, ingawa bado ilikubaliwa na Mungu. Mungu yu tayari kufanya kazi na wanadamu waharifu wanaomwitikia na kumkubali ahadi zake katika imani, hata kama imani yao ni ndogo kama mbegu ya haradari (kama vile Mt. 17:20)

**4:3,4,5,6,8,9,10,22,23,24**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"Ilitabiriwa kwake"** |
| **NKJV** | **"Ilisemwa kumhusu"** |
| **TEV** | **"Kwa vile Mungu alimpokea"** |
| **NJB** | **"Imani yake ilifikiriwa"** |

Inarejelea imani ya Ibrahimu kwa ahadi za Mungu. "Ilitabiriwa" *(logizomia*, kama vile 3:28 na mara 11 katika sura ya 4), ni neno la kuelezea lililomaanisha "kusingiziwa" au " kuweka amana kwa ajili ya mwingine" (kama vile LXX Mwa. 15:6; Law. 7:18; 17:4). Ukweli huu unaelezwa vizuri katika II Kor. 5:21 na Gal. 3:6. Inawezekana kuwa Paulo aliunganisha Mwa. 15:6 na Zab. 32:2 kwa sababu yote inatumia neno la kuelezea "kutabiri". Uunganishaji huu wa maandiko ulikuwa ni kanuni iliyotumiwa na viongozi wa dini.

Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili katika maandiko ya kale sio neno la msingi sana la kutazamwa sana katika vitabu, bila shaka kwa kuhusishwa na vitabu vya Dan 7:10; 12:1.

Vitabu hivi viwili vyenye asili ya kufanana (kumbukumbu ya Mungu) ni:-

1. Kitabu cha Matendo na Kumbukumbu (kama vile Zab. 56:8; 139:16; Isa. 65:6; Mal. 3:16; Ufu. 20:12-13
2. Kitabu cha uzima (Kut. 32:32; Zab. 69:28; Isa 4:3; Dan. 12:1; Luka 10:20; Flp. 4:3; Ebr. 12:23; Ufu. 3:5; 13:8; 17:8; 20:15; 21:27)

Kitabu ambamo imani ya Abrahamu ilielezwa na Mungu kama mwenye haki kilikuwa ni "kitabu cha uzima".

**4:3, 5,6,9,10,1,13,22,25 "Kama mwenye haki"** Hii inarejea katika neno la Agano la kale "kamba ya kupimia" (*tsadak*). Ilikuwa muundo wa sitiari kuelezea namna fulani ya tabia ya Mungu. Mungu yuko sawa na wanadamu wamepinda. Katika Agano jipya lilitumika kwa mtazamo ya kinafasi, na kisheria ambalo kwa mwelekeo limo katika mfumo wa tabia za maisha ya kimiungu. Lengo la Mungu kwa kila mkristo ni tabia yake yeye kwao au kwa maneno mengine, ufanani wa mkristo (kama vile 8:28-29; Gal. 4:19) Tazama Mada Maalum"Haki" katika 1:17.

**4:5** Umuhimu wa imani ni kuitikia Mungu anaye jidhiirisha mwenyewe, bila hata kidogo kutegemea jitihada ya mwanadamu au sifa njema. Hii haina maana kwamba tukisha okolewa na kuwa na roho ndani mwetu, mfumo wa maisha sio wa muhumu. Kusudi la ukristo sio tu mbinguni tunapokufa, bali ufanani wa Kristo kwa sasa. Hatujaokolewa, kuhalalishwa au uzima thabiti kwa kazi zetu, bali tumeokolewa kwa kazi njema (kama vile Efe. 2:8-9 & 10; Yakobo na I Yohana). Maisha yaliyobadilika na yanayobadilika ni ushahidi kuwa mtu huyu ameokolewa. Uthibitisho lazima uzae utakaso!

◙ **"Kuamini"** Huu ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Tazama Mada Muhimu chini.

## MADA MAALUMU: KUSADIKI, KUAMINI, IMANI

A. Hili ni aina ya neno muhimu katika Biblia (kama vile. Ebr. 11:1,6). Lilikuwa ni somo la Yesu katika mahubiri ya awali (kama vile. Mk 1:15). Kiwastani kuna mahitaji mapya mawili ya agano: toba na imani (Mk 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21)
B. Asili na historia yake ya maneno haya
   1. Neno "imani" katika Agano la Kale lilimaanisha mtiifu, mwaminifu au mwaminifu wa kutumainiwa na yalikuwa ni maelezo ya asili ya Mungu na si yetu.
   2. Linatokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*, BDB 53, yaani., Hab. 2:4), ambalo mwanzo kabisa lilimaanisha "kuwa na uhakika au imara." Kuitumikia imani ni
      a. Kumkaribisha mtu (yaani., imani binafsi, sadiki, kama vile. E.1.hapo chini)
      b. Kuamini imani kuhusu mtu (yaani., maandiko, kama vile. E.5.hapo chini)
      c. Kuishi maisha kama ya mtu huyo (yaani., mfano wa Kristo)

C. Matumizi yake katika Agano la Kale
Lazima isisitiziwe kuwa imani ya Ibrahim ilikuwa si kwa ajili ya Masiha ajaye, lakini ni kwa ahadi ya Mungu ya kwamba atapata mototo na uzao (kama vile Mwa. 12:2-5; 17:4-8; Rum. 4:1-5). Ibrahim aliikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu (angalia Mada Maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) na neno lake. Bado anamashaka na kuhusika juu ya ahadi hii, ambayo ilimchukua miaka kumi na mitano kutimizwa. Imani yake isiyo kamili, hata hivyo, alikubaliwa na Mungu. Mungu anapenda kufanya kazi na mwanadamu mwenye mapungufu anayejongea kwake na katika ahadi zake kwa imani, hata kama kwa kipimo cha chembe ya haradari (kama vile. Mt. 17:20) au imani mchanganyiko (kama vile. Mark 9:22-24)

D. Matumizi yake katika Agano Jipya
Neno "kuamini" linatoka katika neno la Kiyunani *pisteuō* au nomino *pistis,* ambayo yanatafasiliwa kwa Kiingereza "kuamini" "amini" au "imani." Kwa mfano, nomino haijitokezi katika injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna uwalakini katika uhalisia wa uwajibikaji wa kundi kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha. Mifano mwingine wa matumizi ya kubabiya ya neno hili "kuamini" ni katika Yohana 8:31-59 na Matendo 8:13, 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi ya uwajibikaji wa awali. Lazima ifuatishwe na mchakato wa uwanafunzi (cf. Mt. 13:20-23, 31-32; 28:19-20)

E. Matumizi yake ikiwa na vivumishi
1. *eis* inamaanisha "ndani ya." Muundo huu wa kipekee unasisitizia waumini kuweka imani zao kwa Yesu
   a) ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
   b) ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45,48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo 10:43; Flp. 1:29; 1 Petr. 1:8)
   c) ndani yangu (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
   d) ndani ya mwanaye (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
   e) ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
   f) ndani ya nuru (Yohana 12:36)
   g) ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo 5:14
3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petro. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti* likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
   a) Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
   b) Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
   c) Yesu katika Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
   d) Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
   e) Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
   f) Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
   g) Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
   h) Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30
   i) Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye "Mimi ndiye" (Yohana 8:24; 13:19)
   j) Tutaishi naye (Rum. 6:8)
   k) Yesu alikufa na kufufuka tena (1 The. 4:14)

◘
**NASB, NKJV "imani yake"**
**NRSV "imani hiyo"**

**TEV, NJB "ni imani hii"**

Imani ya Ibrahimu ilihesabiwa kwake kama haki. Hii haikuzingatia matendo ya Ibrahimu, bali kukubali kwake. Matendo yake yalithibitisha imani (kama vile Yak. 2:14-26) Neno "kutabiriwa" linatumika pia na Finiasi katika LXX ya Zaburi 106:31 inayoendana na Hesabu 25:11-13. Kwa msingi huu kutabiriwa kulizingatia matendo ya Finiasi, lakini sio hivyo kwa Ibrahimu katika Mwanzo 15:61.

◙**"Lakini anaamini kwake yeye athibitishae wasio wa Mungu, imani yake inamhesabia kuwa haki"** Hili ni jambo la kushtua! Ni sawa kabisa na Ibrahimu katika mst. 3 (15:6). Haki ni zawadi ya Mungu (nukuu zaidi katika 3:24), siyo matokeo ya utendaji wa mwanadamu. Tazama Mada Maalum katika 1:17

◙**"Daudi"** Kama Ibrahimu hakuwa mtu mkamilifu, lakini bado alikuwa sawa mbele za Mungu kwa imani, vivyo hivyo Daudi mwenye dhambi. (kama vile Zab. 32 na 51). Mungu anapenda kufanya na mwanadamu aliyeanguka (Mwanzo 3) anayeonyesha imani kwake, Agano la kale na kwa mwanaye, yaani Agano Jipya.

**4:6 "mbali na kazi"** Paulo anasisitiza fungu hili kwa kuliweka kabla tu ya nukuu yake katika Agano la Kale (Zab. 32:1-2). Binadamu yu kwa Mungu kwa neema yake kupitia kwa Kristo kwa njia ya imani ya mtu pekee na siyo utendaji wao wa kidini (kama vile 3:21-31; Efe. 2:8-10).

**4:7-8** Hii ni nukuu kutoka Zab. 32:1-2 VITENZI vyote katika mstari wa 7, "wamesamehewa" na "wamefunikwa" NI KAULI TENDEWA TIMILIFU. Mungu ndiye wakala atajwaye. Mstari wa 8 una KANUSHO MARA MBILI lenye nguvu, "Kwa vyovyote vile hata" singiziwa, tabiriwa, kuhesabiwa. Tazama VITENZI vitatu katika nukuu hii; kuachilia vyote kuna maanisha "Kuwekwa huru kutokana na dhambi".

**4:7 "Ni dhambi za nani zimefunikwa"** Hii ni nukuu kutoka Zab. 32:1. Dhana ya "kuondoa" ilikuwa kiini cha utoaji wa dhabihu kwa Waisrael (Walawi 1-7) kwa Mungu kufunika dhambi (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU), Aliliondoa mbele ya macho yake (Isa. 38:17; Mika 7:19 Brown, Driver, Briggs Uk 491). Dhana hii hii, ingawa neno jingine kwa Kiebrania la neno "kufunika" *(caphar*), lilitumika siku ya upatanisho wa kusamehewa dhambi (kufunikwa), ambapo damu iliwekwa juu ya "kiti cha rehema" kuliondoa dhambi za Waisrael (yaani Walawi 16). Neno mbadala la kibiblia linalohusiana ni "kufuta" (kama vile Isa. 1:18; 43:25) au kutupilia mbali, (kama vile Mdo. 3:19, Kol 2:14; Ufu. 3:5) dhambi zao.

**4:8 "Aliyebarikiwa ni mtu yule ambaye Bwana hatamhesabia dhambi zake"** Hii ni nukuu kutoka katika Zaburi 32:2. Ni neno "tabiri," "singizia," "kuweka katika hesabu", yaliyotumiwa visivyo. Mungu hamwekei muumini dhambi asizonazo (KITENZI HASI CHENYE JOZI). Anamwekea haki. Hii inatokana na tabia ya neema ya Mungu, zawadi na tamko, siyo sifa nzuri ya mtu wala mafanikio /thamani!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:9-12**
**[9] Basi je?, uheri huo ni kwao waliotahiriwa, au kwa hao pia wasiotahiriwa? Kwa kuwa twanena ya kwamba kwake Ibrahimu imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki. [10]Alihesabiwaje basi? Alipokwisha kutahiriwa, au kabla hajatahiriwa? Si baada ya kutahiriwa; bali kabla ya kutahiriwa.[11]Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri ya ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa; apate kuwa baba yao wote waaminio, ijapokuwa hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki; [12]tena awe baba ya kutahiriwa, kwa wale ambao si waliotahiriwa tu, bali wanazifuasa nyayo za imani yake baba yetu Ibrahimu aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa.**

**4:9-12** Bila shaka Paulo alihusisha mjadala huu wa tohara kutokana na msisitizo wa Ki-Yuda juu ya ulazima wa tohara kwa wokovu (kama vile kitabu cha Wagalatia na baraza la Yerusalem la Matendo 15) Paulo aliyefunzwa kuwa kiongozi wa dini, aliyajua haya katika Mwanzo 15:6 na Zab. 32:2. KITENZI kile kile kianaonekana katika vyote (Andiko la Kiebrania) na kitabu cha kiyunani cha maandiko ya kale). Hivi vingeweza kuwa vimeunganishwa hivi kwa makusudi ya kithiolojia.

**4:9** Suala la mst. wa 9 linatarajia jibu la "hapana". Mungu anawakubali watu wote hata wa mataifa kwa imani, Mwanzo 15:6. Kitabu cha Mwanzo kinanukuliwa tena, Abrahamu Baba wa taifa la Wayahudi, alitabiriwa haki (kama vile Mwanzo 15) kabla ya sheria ya Musa (mst. 13) na kabla hajatahiriwa (kama vile Mwanzo 17).

**4:10-11 "Alama ya tohara, ni rakili ya haki ya imani"** Baada ya kuwa Ibrahimu ameitwa na kutabiriwa kama mwenye haki, Mungu akafanya tohara kama ishara ya agano (kama vile Mwa. 17:9-14). Watu wote wa kale karibu na mashariki isipokuwa Wafilisti waliokuwa wa asili ya Kiyunani kutoka katika visiwa vya Aegean. Tohara kwa wao ilikuwa ni utaratibu wa kutoka katika ujana kwenda katika utu-uzima. Kwa maisha ya Wayahudi ilikuwa ishara ya kidini ya agano la ushirika, iliyofanyika kwa watoto wa kiume siku ya nane baada ya kuzaliwa. Katika mstari huu, "alama" na "rakili" ni vitu sambamba na vyote vikimaanisha imani ya Ibrahimu. Tohara ilikuwa ni alama ya wazi inayoonekana kwa yule aliyekuwa na imani kwa Mungu. Kifungu MILIKISHI "ya haki ya imani", linajirudia katika mstari wa 13. Kielelezo cha kuwa sawa na Mungu Mtakatifu si tohara, bali kilikuwa ni imani.

**4:11 "Kwamba angekuwa baba wa wote waaminio pasipo tohara"** Kitabu cha Warumi kiliandikwa baada ya kitabu cha Wagalatia. Paulo alikuwa anajali sana mwenendo wa Wayahudi wa kuamini (1) mfumo wa uzao (Mathayo 3:9; Yohana 8:33,37,39) na (2) utekelezaji wa tafsiri za sasa za agano la Musa (utamaduni wa kusema au utamaduni wa wakubwa waliotangulia ambao baadaye uliandikwa na kuitwa Talmud). Kwa hiyo alimtumia Abrahamu kama kielelezo kwa wote wanaoamini kwa imani (baba wa kuamini watu wa mataifa yasiyotahiriwa, kama vile 2:28-29, Wagalatia 3:29).

◙Tazama Mada Maalum chini.

## MADA MAALUMU: MUHURI/LAKIRI

Muhuri au lakiri yaweza kuwa ni njia ya kale ya kuonyesha

1. Ukweli (kama vile Yohana 3:33)
2. Umiliki (kama vile Yohana 6:27; 2 Tim. 2:19; Ufu.. 7:2-3; 9:4)
3. Ulinzi (kama vile Mwa. 4:15; Mt. 27:66; Rum. 4:11; 15:28; 2 Kor. 1:22; Efe. 1:13; 4:30; Ufu. 20:3)
4. Yawezakuwa pia ni dalili za ukweli wa ahadi ya Mungu (kama vile Rum. 4:11 and 1 Kor. 9:2)

Kusudi la muhuri huu katika Ufunuo 7:2-4; 9:4 ni kuwatambua watu wa Mungu ili kwamba ghathabu ya Mungu isiwadhuru. Muhuri wa shetani pia huwatambua walio wake, wale walio chombo cha ghathabu ya Mungu. Katika kitabu cha Ufunuo "dhiki kuu" (yaani., *thlipsis)* mara zote inarejerea wasio waumini wakiwatesa waumini, wakati ghadhabu/hasira (yaani., *orgē* or *thumos*) mara zote huwa ni hukumu ya Mungu juu ya wale wasioamini ili kwamba wapate kutubu na kuirudia imani katika Kristo. Kusudi hili chanya la hukumu laweza kuonekana katika agano la laana/Baraka katika kitabu cha Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28;30; Zaburi 1

**4:12 "Zifuate nyayo"** Hili lilikuwa neno la kijeshi *(stoicheō)* kwa askari waliokuwa wakitembea katika mstari (kama vile Mdo. 21:24; Gal. 5:25; 6:16; Flp. 3:16) Paulo anazungumza katika mstari huu wa Wayahudi ("Baba wa tohara") anayeamini. Abrahamu ni Baba wa wote wanaoonyesha imani kwa Mungu na ahadi zake.

Kwa sababu ya KIFUNGU mara mbili (*tois*) inawezekana kuwa suala hili la pili ("kufuata hatua za") linaongeza dhana ya imani katika stadi za maisha (KAULI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO) na siyo imani ya mara moja tu. Wokovu ni uhusiano unaoendelea, sio uamuzi tu au wakati tu wa kutoa uamuzi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:13-15.**
**[13]Kwa maana kwa ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sheria bali kwa haki aliohesabiwa kwa imani. [14]Maana ikiwa wale wa sheria ndio warithi, imani imekuwa bure, na ahadi imebatilika. [15]Kwa sababu sheria ndiyo ifanyayo hasira; maana pasipo kuwapo sheria, hapana kosa.**

**4:13 "Ahadi ya Ibrahimu au kwa wazawa wake"** Mungu alifanya ahadi ya "ardhi/nchi na mbegu" kwa Abrahamu. (kama vile Mwa. 12:1-3; 15:1-6; 17:1-8; 22:17-18). Agano la kale lilizungumzia "nchi" (Palestina), lakini Agano Jipya lilizungumzia "mbegu" (Yesu Masihi) (kama vile Gal. 3:16, 19) lakini hapa "mbegu" ilimaanisha watu wenye imani. (Gal. 3:29). Ahadi za Mungu ndio msingi wa imani ya waumini wote (kama vile Gal. 3:14,17,18,19,21,22,29; 4:28; Ebr. 5:13-18)

◙**"Kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu"** Usemi huu wa ulimwengu mzima ni wa muhimu sana kwa mtazamo wa Mwanzo 12:3; 18:18; 22:18 na Kutoka 19:5-6. Mungu alimwita Ibrahimu aite watu wote (kama vile Mwa. 1:26-27; 3:15)! Ibrahim na uzao wake walikuwa wawe njia ya ufunuo kwa ulimwengu wote. Hii ni njia nyingine ya kuonyesha ufalme wa Mungu duniani (kama vile Mt. 6:10).

◙**"Siyo kwa kupitia katika sheria"** Sheria ya Musa ilikuwa bado haijadhihirika. Usemi huu ulisemwa kwanza katika sentensi ya Kiyunani kuonyesha umuhimu wake. Hii ilikuwa sehemu muhimu katika kusisitiza tofauti iliyopo kati ya jitihada ya mwanadamu na neema ya Kimungu (kama vile 3:21-31). Neema imeondoa sheria kama njia ya wokovu (Ebr. 8:7, 13). Tazama Mada Maalum: maoni ya Paulo kuhusu sheria ya Musa katika 13:19.

**4:14 "kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambayo ilichukuliwa kuwa kweli kwa mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi lake kifasili. Paulo alitumia usemi wa kufafanusha ili kufanikisha mantiki ya wazo lake. Huu ni mfano mzuri wa SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA uliotumika kusisitiza suala lisilotarajia jibu. Yeye hakuamini usemi huu kuwa kweli, ila alisema tu kuonyesha kasoro yake (kama vile mstari 2).

Taifa la Wayahudi na alama yao ya kuonekana ya tohara sio wao watakaurithi ulimwengu, bali wale wenye kuonyesha imani katika utashi wa Mungu na neno lake ndio warithi. Tohara ya kimwili sio alama ya kweli ya agano, bali imani (kama vile 2:28-29

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"Imani imefanywa utupu"** |
| **NRSV** | **"Imani ni bure"** |
| **TEV** | **"Imani ya mtu haina maana yoyote"** |
| **NJB** | **"Imani inakuwa haina lolote"** |

Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU ya *kenoō*, inayosisitiza hali ya kitenzi chenye nguvu cha Wayunani kumaanisha "kumaliza kabisa" "Kuonyesha kutokuwa na msingi," hata "kupotosha" (kama vile II Kor. 1:17). Neno hili pia lilitumiwa na Paulo, katika 1 Kor. 1:17; 9:15; II Kor 9:3 na Flp. 2:7.

◙

| | |
|---|---|
| **NSAB** | **"Ahadi inafutwa"** |
| **NKJV** | **"Ahadi inafanywa kutoathiri kitu"** |
| **NRSV** | **"Ahadi ni tupu"** |
| **TEV** | **"Ahadi ya Mungu haina thamani"** |
| **NJB** | **"Ahadi haina maana yoyote"** |

Hii pia ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU inayosisitiza hali ya KITENZI chenye nguvu cha Wayunani kinachomaanisha "kumaliza kabisa," "kutangua" "kufikia mwisho" "kuharibu au kuteketeza kabisa". Neno hili lilitumiwa pia na Paulo katika Warumi 3:3,31; 6:6; 7:2,6; 1 Kor. 2:6; 13:8; 15:24,26; Gal 5:4; II The. 2:8. Dhahiri kuna usambamba katika mstari huu. Hakuna njia mbili katika wokovu. Agano jipya kwa neema limefanya kazi ya agano la kale kuwa bure na tupu!
Tazama Mada Maalum. Bure na tupu katika 3:3.

**4:15 "sheria …sheria"** Tumizi la kwanza la neno hili lina neno la Kiyunani, wakati huo la pili halina. Ingawa ni hatari kuzingatia kuwepo au kutokuwepo kwa NENO hili la Kiyunani, inaonekana kwa hali hii inasaidia kuonyesha Paulo alitumia neno hili kwa namna mbili.

1. Sheria ya Musa yenye utamaduni wa kuelezwa kwa maneno ya midomo, ambayo baadhi ya Wayahudi waliamini kwa wokovu wao.
2. Dhana ya sheria kwa ujumla.

Maana hii pana ingejumuisha haki binafsi ya watu wa Mataifa walioendana nayo au kanuni ya kijadi au matambiko ya dini na wahisi kukubalika kwa miungu kutokana na utendaji wao.

◙ **"Sheria inasababisha ghadhabu"** Huu ni usemi wa kushtua, (kama vile 3:20; Gal. 3:10-13; Kol. 2:14). Shera ya Musa haikukusudiwa kuwa njia ya wokovu (kama vile Gal. 3:23-29). Hii ingelikuwa ukweli mgumu kwa Myahudi yeyote (au mwanasheria) kuelewa au kukubali, lakini ilikuwa ndio msingi wa hoja ya Paulo. Tazama Mada Maalum, katika 13:9.

◙**"Lakini pale pasipo na sheria, pia hapana kuvunja sheria"** Mungu anawawajibisha wanadamu kwa nuru walionayo. Watu wa mataifa hawatahukumiwa kwa sheria ya Musa ambayo hawakuwahi kuisikia. Waliwajibishwa kwa ufunuo asilia (kama vile 1:19-20; 2:14-15).

Ukweli huu unaendelezwa hatua moja mbele katika hoja ya Paulo.Kabla ya sheria ya Musa kuwekwa wazi Mungu, hakufuatilia maasi ya mwanadamu. (kama vile 3:20, 25; 4:15; 5:13,20; 7:5,7-8; Mdo. 14:16; 17:30; I Kor. 15:56.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:16-25**
**16 Kwa hiyo ilitoka katika imani, iwe kwa njia ya neema, ili kwamba ile ahadi iwe imara kwa wazao wote; si**
**kwa wale wa torati tu, ila na kwa wale wa imani ya Ibrahimu; aliye baba wa imani kwetu sisi sote; 17 (kama**
**ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu,**
**mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako. 18 Naye aliamini kwa**
**kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa, kama alivyonenwa, Ndivyo itakavyokuwa**
**uzao wako. 19 Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa**
**amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. 20 Lakini akiiona ahadi ya**
**Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu. 21 huku akijua hakika ya**
**kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi. 22 Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki. 23 Walakini**
**haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake; 24 bali na kwa ajili yetu sisi tutakaohesabiwa**
**vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu; 25 ambaye alitolewa kwa**
**ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki.**

**4:16** Huu ni ufupisho thabiti wa hoja ya Paulo mstari wa 14,

1. Wanadamu sharti wakubali kwa imani
2. Kwa ahadi ya neema ya Mungu
3. Hakika ahadi ilikuwa kwa wazawa wote, (wayahudi na watu wa mataifa) wa Ibrahimu aliye mwenye imani.
4. Ibrahimu alikuwa kielelezo cha wote wenye imani.

◙

**NASB, NRSV**
**TEV, NIV** **"kimedhaminiwa"**
**NKJV** **"hakika"**
**REB** **"kinafaa"**
**NET** **"hakika"**

Tazama Mada Maalum ifuatayo

## MADA MAALUM: DHAMANA

Hili ni neno la Kiyunani *bebaios,* lenye vidokezo vitatu

1. Kile ambacho ni hakika (kama vile Rum 4:16; II Kor 1:7; Ebr 2:20; 3:6,14; 6:19; II Pet 1:10,19

2. Mchakato ambao kitu chenye hali ya kuaminika kinaonyeshwa au kuwekwa wazi (kama vile Louw and Nida, *Greek-English Lexicon of the New Testament,* Uk 1, pp. 340,377,670).
3. Maandiko katika magombo yakawa ndiyo kifungu cha dhamana ya kisheria (kama vile Moulton na Milligan, *Vocabulary of the Greek New Testament,* kurasa*.107-80).*

Hii inawezekana kuwa kinyume na mstari wa 14. Ahadi za Mungu ni za kweli.

◙**"wote…..wote"** Hii inaanisha waumini wote (Wayahudi na wa Mataifa)

**4:17-23** Paulo pia anamtumia Ibrahimu kuonyesha kipaumbele cha (1) Mungu anaanzisha ahadi za neema (Agano) na (2) Hitaji la mwanadamu la imani ya awali na kukubali imani endelevu (agano, tazama nukuu katika1:5) Agano daima linahusu matendo ya pande mbili.

**4:17 "Kama ilivyoandikwa", 'BABA WA MATAIFA MENGI' "** Hii ni nukuu kutoka katika Mwanzo 17:5. Mtafasiri wa Kiyunani wa agano la kale (LXX) una "Watu wa Mataifa" Mungu daima amekuwa akitaka Ukombozi kwa watoto wote wa Adamu (kama vile Mwa. 3:15); na sio tu kwa watoto wa Ibrahimu. Jina jipya la Ibrahimu lina maana ya "Baba wa watu wengi". Sasa tumejua linajumuisha sio tu wazawa wa kimwili, bali pia wazawa wa imani.

◙**"Awapaye uhai waliokufa"** Katika mtindo huu, ana maana ya nguvu mpya ya kujamiiana ya Abrahamu na Sara (kama vile mstari 19).

◙**"Huvirejesha kuwa hai visivyokuwepo"** katika mtindo huu inamaanisha ujauzito wa Sara toka Isaka, lakini pia inaonyesha suala nyeti la imani (kama vile Ebr. 11:1).

◙
**4:18**
**NASB "Kwa matumaini aliamini pasipo matumaini"**
**NKJV "Ambaye, kinyume na tumaini, katika tumaini aliamini"**
**NRSV "Aliamini kutumainishwa dhidi ya tumaini"**
**TEV "Abrahamu aliamini na kutumaini, hata kama hapakuwa na sababu ya kuamini"**
**NJB "Japo hapakuonekana kuwepo na tumaini, alitumaini na kuamini"**

Mada maalum kuhusu "tumaini" inapatikana katika 12:12. Neno hili ni pana sana kwenye somo la maana ya maneno. Harold K. Moulton, *The analytical Greak Lexicon Revised,* ukurasa wa 133, inaonyesha matumizi kadhaa.
1. Maana ya msingi, tumaini (kama vile Rum. 5:4; Mdo. 24:15)
2. Kusudi la tumaini (Rum. 8:24; Gal. 5:5
3. Mwandishi au mwanzilishi (kama vile Kol. 1:27; I Tim. 1:1).
4. Kuamini, hali ya kujiamini (kama vile Mdo. 2:26, Rum. 8:20).
5. Pasipo na dhamana ya ulinzi

Katika eneo hili tumaini limetumika kwa maana halisi mbili. Tumaini katika uwezo na nguvu za mwanadamu (kama vile mistari ya 19-21) dhidi ya tumaini katika ahadi ya Mungu (kama vile mstari wa 17)

◙
**NASB, NKJV "wazawa wako watakuwa hivyo"**
**NRSV "wazawa wako watavyokuwa wengi"**
**TEV "wazawa wako watakuwa wengi"**
**NJB "wazawa wako watakuwa wengi kama nyota"**

Hii ni kutoka Mwanzo 15:5 inasisitiza uhakika wa ahadi ya Mungu kwa Abrahamu kuhusu mtoto wa kiume (kama vile mistari ya 19-22) Kumbuka kuwa Isaka alizaliwa.
1. Miaka 13 baada ya ahadi.
2. Baada ya Ibrahimu kutaka kumwacha Sara (mara mbili kama vile Mwa. 12:10-19; 20:1-7)

3. Baada ya Ibrahimu kupata mtoto wa kiume na Hajiri, mtumishi wa Sara kutoka Misri.
4. Baada ya wote Sara (kama vile Mwa. 18:12 ) na Ibrahimu (kama vile Mwa. 17:17) kucheka, kukebehi ahadi.

Abrahamu na Sara hawakuwa na imani madhubuti! Shukuru Mungu, wokovu hauhitaji imani madhubuti lakini ni kitu sahihi. (Mungu katika Agano la Kale na mwanae wa kiume katika Agano Jipya).

**4:19 "alitafakari"** Tafsiri hii inafuatia MSS **א,** A, B,C**.** lakini baadhi ya maandiko ya kale yanaongezeza KIAMBATA hasi, (*ou*) A, B, C. UBS[4] haina uwezo wa kufanya maamuzi (kiwango cha "C" ) lakini inapiga chapa andiko fupi, Biblia ya NET pia inaunga mkono andiko fupi.

**4:20** Awali, Ibrahimu hakufahamu ahadi kuwa mtoto angetoka kwa Sara. Hata imani ya IbrahImu haikuwa thabiti. Mungu hupokea na kushughulika na watu wenye imani haba kwa sababu anawapenda wasio wakamilifu.

◙**"Hakuyumbishwa na kutokuamini"** KITENZI kilekile *diakrinō* kinatumika na Yesu katika Mathayo 21:21; Marko 11:23. Ibrahimu alikuwa na sababu (kama vile mstari wa 19) kuhoji neno la Mungu (ahadi), lakini badala yake akawa imara zaidi. VITENZI viwili katika mst wa 20, yote kwa pamoja KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, kauli tendewa inaonyesha uwakala wa Mungu. Lakini Ibrahimu alibidi kuruhusu (agano) nguvu ya Mungu kumuimarisha.

◙**"Kumpa Mungu utukufu"** Tazama Mada Maalum katika 3:23.

◙
**4:21**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kuhakikishwa kikamilifu"** |
| **NKJV, NRSV** | **"kushawishiwa kikamilifu"** |
| **TEV** | **"alikuwa na hakika kabisa"** |
| **NJB** | **"kushawishika kikamilifu"** |

Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU ENDELEVU inaonyesha uhakika kamili wa kitu (Luka 1:1; Kol. 4:12) au mtu yeyote (kama vile Rum. 4:21; 14:5). NOMINO inatumika kwa uhakika zaidi katika Wakolosai 2:2 na 1 Wathesalonike 1:5 kujiamini huku katika matakwa ya Mungu, neno na nguvu kunawezesha wanadamu kutenda kwa imani.

◙**"Alichoahidi Mungu pia alikuwa na uwezo wa kukitekeleza"** Hii ni KAULI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU ikiwa na maana kuwa, tendo la nyuma limekamilishwa na jambo limekuwa kama ilivyobidi liwe. Asili ya imani ni kwamba mtu anaamini tabia na ahadi ya Mungu (kama vile 16:25; Efe. 3:20; Yuda 24) na siyo katika utendaji wa binadamu. Imani huamini Mungu wa ahadi.

**4:22** Hiki ni kidokezo cha Mwanzo 15:6 (kama vile mst 3), ambavyo ni kielelezo muhimu cha hoja ya kithiolojia ya Paulo jinsi Mungu anavyowapa wenye dhambi haki yake.

**4:23-25** Mistari hii ni sentensi moja katika Kiyunani. Angalia mwendelezo.

1. Kwa faida ya Ibrahimu mstari. 23
2. Kwa faida ya waumini mstari. 24
3. Kwa Mungu kumwinua Yesu mstari. 24
4. Yesu alitolewa kwa ajili ya dhambi zetu (kama vile Yohana 3:16) Yesu aliinuliwa kwa ajili ya dhambi zetu tusamehewe (uhalalisho) mstari 25

**4:24** Imani ya Ibrahimu ikawa ndio mfumo wa wazawa wake kufuata. Ibrahimu aliamini (Tazama Mada Maalum katika 4:5) Mungu kuhusu mwana aliyeahidiwa na wazawa wake. Waumini wa agano jipya wanaamini kuwa Yesu Masia ndiyo utimilifu wa ahadi zake kwa wanadamu walioanguka. Neno "mbegu" liko pote kwenye hali ya UMOJA na WINGI (mwana, watu).

◙ Kwa ajili ya "kuinuliwa" tazama nukuu katika 8:11

**4:25 “Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu”** lilikuwa neno la kisheria lililomaanisha “mtu kukabidhiwa kwa ajili ya adhabu” mstari wa 25 ni maneno ya ajabu ya Kristo yakionyesha mtafasiri wa Kiyunani wa agano la kale (LXX) la Isaya 53:11-12).

◙ **“Aliinuliwa kwa ajili ya kututhibitisha”** mafungu mawili ya mstari wa 25 yanaendana pamoja (VIHUSISHI vile vile pia vina KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, lakini kimaandishi tu sio kwa sababu ya za kithiolojia. (kama vile 5:9-10; 2 Kor 13:4). Fasili ya Frank Stagg (*New Testament Theology*, uk.97) “kutolewa kwa ajili ya makosa yetu na kuinuliwa kwa lengo la kutufanya kuwa na haki ”yanastahili kusifiwa”. Maana hii inahusu masuala mawili ya sababu ya Paulo kutumia neno “kuhalalisha” (1) ustadi wa kusimamia mambo ya mahakama (sharia) na (2) mambo ya kiuungu, maisha ya kufanana na Kristo! Tazama Mada Maalum katika 1:17.

Ufufuo wa Yesu ni kiini cha ukweli wa thiolojia kwa Paulo (kama vile 1:3-4; 4:24-25; 6:4,9; 7:4; 8:11,34; 10;9 ; II Kor. 6:14; 15;3-11,20-23; II Kor. 1:9; 4:14; 5:15; 13:4; Gal. 1:1; Efe. 2:20; Kol 2:12; II Thesal 1:10, II Tim 2:28) kaburi li wazi au ukristo ni uongo (kama vile II Kor 15:12-19)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini sehemu hii ya Warumi ni muhimu kiasi hicho?
2. Kwa nini Paulo alitumia Ibrahimu na Daudi kama mifano?
3. Fasili maeneo haya muhimu, kufuatana na matumizi yake kama Paulo alivyoyatumia (siyo fasili yako)
    a) “haki”
    b) “kutabiri”
    c) “imani”
    d) “ahadi”
4. Kwa nini tohara ilikuwa muhimu sana kwa Wayahudi (mst. 9-12)?
5. Neno “mbegu” linamaanisha akina nani katika mistari ya 13 na 16?

# WARUMI 5

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Matokeo Ya Kuhesabiwa Haki | Imani Inashinda Katika Matatizo | Matokeo ya Kuhesabiwa Haki | Kuenenda sawa na Mungu | Imani ni uthibitisho Wa Wokovu |
| 5:1-11 | 5:1-5 | 5:1-5 | 5:1-5 | 5:1-11 |
| | Kristo katika Nafasi Yetu | | | |
| | 5:6-11 | 5:6-11 | 5:6-11 | |
| Adamu na | Kifo katika Adamu, Uzima katika Kristo | Adamu na Kristo Ulinganifu na Utofautiano | Adamu na Kristo | Adamu na Yesu Kristo |
| 5:12-14 | 5;12-21 | 5:12-14 | 5:12-14b | 5:12-14 |
| 5:15-21 | | 5:15-17 | | 5:15-21 |
| | | 5:18-21 | 5:18-19 | |
| | | | 5:20-21 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Mistari 1-11 ni sentensi moja katika Kiyunani inaendeleza dhana elekezi ya "uhalalisho wa neema kupitia imani" (kama vile 3:21-4:25).

B. Vidokezo vinavyowezekana vya mistari ya 1-11

| Mistari 1-5 | Mistari 6-8 | Mistari 9-11 |
|---|---|---|
| 1. Manufaa ya Wokovu | 1. Msingi wa Wokovu | 1.Uhakika Ujao wa Wokovu |
| 2. Uzoefu utuhusuo uhalalisho | 2.Ukweli uhusuo wokovu | 2. Uhakika Ujao wa Wokovu |
| 3. Uhalalisho | 3. Utakaso unaendelea | 3. Kumpa Mungu utukufu |
| 4. Elimu juu ya asili ya mtu | 4. Thiolojia | 4. Thiolojia ya mambo yajayo |

C. Mistari 12-21 ni mjadala juu ya Yesu kama Adamu wa pili (kama vile I Kor. 15:21-22, 45-49, Flp. 2:6-8). Inatoa msisitizo kwa dhana ya kithiolojia ya dhambiya mtu binafsi na maovu yaliyomo. Mwendelezo wa Paulo juu ya anguko la mwanadamu (na uumbaji) Adamu alikuwa wa pekee na tofauti na viongozi wa kidini wa Kiyahudi (waliokuza imani yao juu ya dhambi kutoka Mwanzo 6), wakati maoni yao kuhusisha hayo ulikuwa unalandana na mafundisho ya viongozi hawa wa kidini. Ilionesha uwezo wa Paulo ndani ya uvuvio wa kutumia au kuongezea ukweli aliofundishwa akiwa mafunzoni huko Yerusalemu chini ya Gamalieli (kama vile  Mdo. 22:3).

Imani ya Kiinjili iliyorekebishwa ya dhambi ya awali kutoka Mwanzo 3 ilielezwa na Agostino na Calvin. Kimsingi inasema kuwa wanadamu wamezaliwa na dhambi (wakengeufu). Mara nyingi Zaburi 51:5; 58:3 na Ayubu 15:14;25:4inatumika kama uthibitisho wa Agano la Kale. Mtazamo mwingine wa kithiolijia kuwa mwanadamu kimaendeleo, kimaono na kiroho wanawajibika na uchaguzi wao wenyewe kuhusu mwisho wao ulileta na Pelagius na Arminius. Kuna ushahidi katika maneno yao katika Kumbukumbu la Torati 1:39; Isaya 7:15 na Yona 4:11; Yohana 9:41; 15:22; 24; Matendo17:30; Warumi 4:15. Msukumo wa nafasi hii ya kithiolojia ingekuwa kwamba,watoto hawana kosa, hadi hapowanapofikia umri wa kuwajibika kimaono (kwa viongozi wa kidini wa Kiyahudi) hii ilikuwa miaka 13 kwa wavulana na 12 kwa wasichana). Kuna wakati ulikuwa wakati wa mapatano ambapo uovu wa kuzaliwa na umri wa kuwajibika kimaono vyote vinakuwa kweli. Uovu sio tu umo ndani ya mtu bali, mwendelezo wa uovu wa mtu binafsi kwa dhambi (maisha hatua kwa hatua kuondoka kwa Mungu). Ukaidi wa binadamu sio suala (Mw. 6:5,11-12,13, Rum. 3:9-18,25), bali wakati upi wa kuzaliwaau baadaye katika maisha?

D. Pamekuwa na nadharia kuhusu matokeo ya mst. 12
   1. watu wote wanakufa kwa kuwa wamechagua kutenda dhambi  (Pelagius)
   2. dhambi ya Adamu iliathiri uumbaji wote na hivyo wote hufa (mst. 18-19)
   3. Kiukweli, inawezekana ni muungano wa adhabu ya Mwanzo, na ile ya kuamua kufanya.

E. Ulinganisho wa Paulo “kama vile” ulianza katika mst. 12 na haukuisha hadi mstari wa 18. Mistari ya 13-17 inaunda parandesi ambayo inabainisha kabisa maandiko ya Paulo.

F. Kumbuka uwasilishaji wa Paulo na injili, 1:18-8:39ni hoja moja iliyodumu. Lazima itazamwe yote ili kuweza kutafsiri na kutambua sehemu mbalimbali.

G. Martin Luther amesema katika sura 5, katika Biblia nzima ni si rahisi kupata sura ambayo ni sawa na andiko hili lililotukuka.

## USOMAJI WA NENO LA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:1-5**
**[1]Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. [2]Ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. [3]Wala si hivyo tu, ila na tufurahi katika dhiki pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; [4]na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; [5]tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.**

**5:1 "kwa hiyo"** neno hili daima liliashiria

1. muhtasari wa hoja ya kithiolojia hadi hapo ilipo
2. hitimisho lilizunguka uwasilisho wa kithiolojia
3. uwasilisho wa ukweli mpya (5:1; 8:1; 12:1)

◙**"kwa kuhalalishwa"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA; Mungu amewahalalisha walioamini. Hii imewekwa ya kwanza katika sentensi ya Kiyunani (mist. 1-2) kwa kusisitiza. Inaonekana kuwepo kwa utiririko wa muda katika mist.1-11.

1. Mist. 1-5, uzoefu wetu wa sasa wa neema
2. Mist .6-8, kazi ya Yesu iliyomalizika kwa niaba yetu
3. Mist. 9-11, matumizi yetu yajayo na uhakika wa wokovu

Tazama kidokezo, B. Katika mtazamo Halisi.

Asili ya Agano la Kale kumbuka mwandishi wa Agano Jipya ni Waebrania wenye fikra kubwa wakiandika kwa Kiyunani cha mitaani kwa neno "halalishwa" (*dikaioō*) ilikuwa "ukingoni ulionyooka"au "kamba maalum ya kupimia."Ilikuja kueleza Mungu mwenyewe alivyo.Tazama Mada maalum: haki katika 1:17 tabia Mungu, utimilifu, kilikuwa ndicho kipimo pekee cha hukumu ( kama vile Maandiko ya kale ya miaka ya 1970 ya Walawi 24:22; na kithiolojia katika Mathayo 5:48) Kwa sababu ya kifo cha Yesu kama sadaka, kwa niaba, (kama vile Isaya 53) waamini wana haki kisheria kusimama mbele ya Mungu (tazama nukuu katika 5:2). Hili halina maana ya muumini kutokuwa na hatia, la hasha, bali hili ni kama mahakama ya haki. Mtu mwingine anachukua adhabu (2 Kor 5:21). Waumini wametangaziwa kusamehewa (mist. 9,10).

◙**"kwa imani"** imani ni mkono unaopokea zawadi ya Mungu (kama vile mst. 2; Rum. 4:1 na kuendelea). Imani haikutazama hazina ya mwamini (kama vile Mt. 17:20), bali tabia na ahadi za Mungu(Efe. 2:8-9). Neno la Agano la KaleKwa neno "imani" kimsingi lilimaanisha mtu aliye simama imara/na wima kwa miguu yake. Baadaye likaja likatumika kwa njia nyingine kama mtu aliye muungwana, wa kutegemewa na mwaminifu. Imani haizingatii imani yetuau uaminifu wetu bali kwa Mungu. Tazama Mada Maalum : Imani katika 4:5.

◙**"tunayo amani"** kuna utofauti wa maandiko ya Kiyunani hapa. KITENZI hiki ama KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO (*echōmen*, MSS ℵ*, A, B*, C, D) au KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO (*echomen*, MSS $ℵ^1$, $B^2$, F, G).Utatawasarufi hii pia unapatikana katika mistari ya 1, 2 na 3.

1. Kama kitenzi hiki ni KAULI TEGEMEZI kingetafsiriwa kama "hebu tuendelee kufurahia amani" au "endelea kufurahia amani."
2. Kama kitenzi hiki ni KAULI ELEKEZI kingelitafasiriwa "tunayo amani."

Andiko la mist. 1-11 sio ushawishi, bali ni tamkojinsi waumini walivyo tayari na walichonacho kupitia Kristo. Kwa hiyo, yamkini KITENZI ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, "tunayo amani" Toleo la Biblia ya $USB^4$ linatoa uchaguzi "A" kwa vyo vyote (yamkini)

Maandiko yetu mengi ya Kiyunani ya zama hizo yalitolewa na mtu mmoja aliyesoma maandiko na mengineyo kuandika nakala. Maneno yanayotamkwa kwa kufanana daima yalichanganya. Hapo ndipo upana wa uandishi au wakati mwinginembinu ya uandishi na misamiati ya kawaida ya mwandishi inaposaidia kufanya uamuzi wa kutafsiri kuwa rahisi.

◙**"amani"**Tazama Mada Maalum chini

## MADA MAALUMU: AMANI (AGANO JIPYA)

Hili neno la asili la Kiyunani lilimaanisha "kuunganisha pamoja kile kilichokuwa kimevunjika" (kama vile Yohana 14:27; 16:33; Flp. 4:7). Zipo njia tatu ambazo Agano Jipya huzungumzia amani:

1. Kama kuhusu mtazamo wa amani yetu na Mungu kupitia kristo (kama vile. Kol. 1:20)
2. Kama dhahania ya mtazamo wa kupatanishwa na Mungu (kama vile. Yohana 14:27; 16:33; Flp. 4:7)
3. Kwamba Mungu ameunganishwa katika mwili mmoja mpya kwa njia ya Kristo, wote Wayahudi waaminio na Mataifa (kama vile Efe. 2:14-17; Kol. 3:15).

Newman na Nida, *A Translator's Handbook on Paul's Letter to the Romans*, p. 92, kina hoja nzuri kuhusu "amani."

"Katika Agano la Kale na katika Agano Jipya neno "amani" lina maana pana. Kimsingi unaelezea hali nzuri ya maisha ya mtu; uliasiliwa miongoni mwa Wayahudi kama kanuni ya salamu. Mtajo huu ulikuwa maana ya kina kiasi kwamba ungeweza kutumika na Wayahudi kama maelezo ya Wokovu wa kimasihi. Kwasababu ya ukweli huu ulikuwa na maana ya kina kiasi kwamba ungeweza kutumika na Wayahudi kama maelezo ya wokovu wa kimasihi. Kwasababu ya ukweli huu kuna nyakati inatumika karibu sawa na mtajo peleka "ili kuwa na uhusiano sahihi na Mungu" (uk. 92).

◙**"pamoja na Mungu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo"** Yesu ni wakala (*dia*, mist. 2,9,11,17,21; wa Roho katika mst.5) ambaye huleta amani na Mungu.Yesu ndiye njia pekee ya kupata amani na Mungu (kama vile Yohana 10:7-8; 14:6; Matendo 4:12; 1 Tim. 2:5).Kwa maneno katika kichwa cha habari "Bwana Yesu Kristo" tazama nukuu katika 1:4.

**5:2 "tumepata utambulisho wetu"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA; kinazungumzia mambo ya wakati uliopita ambayo yametimizwa na kupelekea katika hali ya kuwepo.
Neno "utambulisho" kifasihi linamaanisha "ufikikaji", au "haki ya kuingia" (*prosagōgē*, cf. Efe. 2:18; 3;12). Baadaye likaja kutumika kama neno mbadala kwa

1. kutambulishwa binafsi katika wema
2. Kuletwa salama hadi bandalini (kama vile I Pet. 3:18)

Fungu hili lina tofauti za maandiko ya Kiyunani. Baadhi ya maandikoya Kale yaliongezwa "kwa imani"(kama vile א*,2, C, kadhalika na baadhi ya Kilatini, Vulgate, Kishamu, na tafsiri ya Koptiki).Maandiko mengine huongeza KIHUSISHI kuwa "kwa imani" (kama vile א1, A, na toleo la Vulgate). Hata hivyo, maandiko ya B, D, F na G yote yanaachwa. Inaonekana kuwa waandishi kutanua usambamba wa 5:1 na 4:16 (mara mbili), 19, na 20. "Kwa imani" ni dhana ya Paulo inayojirudia!

◙**"katika hiineema"** neno hili (*charis*) lilimaanisha upendo wa Mungu usiostahili, usio na masharti, usio na mnunufaa (kama vile Efe. 2:4-9).Inaonekana wazi katika kifo cha Kristo kwa niaba ya wanadamu wenye dhambi(kama vile mst. 8).

◙**"ambamo kwamo tumesimama"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA; kifasihi,"tunasimama na tunaendelea kusimama."Hii inamaanisha nafasi ya waamini kithiolojia katika Kristona azma yao ya kubakia katika

imani ambayo inajumuisha fumbo la kithiolojia la ukuu wa Mungu (kama vile I Kor. 15:1) na utashi huru wa mwanadamu (kama vile Efe. 6:11,13,14). suala la muda ni mbeleni

## MADA MAALUM: KUSIMAMA (*histēmi*)

Neno hili lililozoeleka linatumika katika namna kadhaa ya kithiolojia katika Agano Jipya

1. kujieneza
   a. sheria ya Agano la Kale, Rum. 3:31
   b. haki yenu wenyewe, Rum. 10:3
   c. agano jipya, Ebr. 10:9
   d. mamlaka, 2 Kor. 13:1
   e. Kweli ya Mungu, 2 Tim. 2:19
2. kupinga kiroho
   a. shetani, Efe. 6:11
   b. katika siku ya hukumu, Ufunuo 6:17
3. kupinga kwa kusimama katika miguu yake mwenyewe
   a. sitiari za kijeshi, Efe. 6:14
   b. sitiari za kijamii, Rum. 14:4
4. nafasi ya kweli, Yohana 8:44
5. nafasi ya neema
   a. Rum. 5:2
   b. 1 Kor. 15:1
   c. 1 Petro 5:12
6. nafasi ya imani
   a. Rum. 11:20
   b. 1 Kor. 7:37
   c. 1 Kor. 15:1
   d. 2 Kor. 1:24
7. nafasi ya majivuno, 1 Kor. 10:12

Neno hili linaelezea vyote neema ya kiagano na rehema za Mungu mwenye nguvu na ukweli kwamba waamini wanaitaji kuitikia na kufuata kwa imani! Vyote ni kweli za Kibiblia. Lazima vishikiliwe kwa pamoja! Angalia Mada Maalum: Agano na Mada Maalum: Mgongano katika Maandiko

◙**"tunafurahia**" Muundohuu kisarufi unaweza kueleweka kama (1) KITENZI CHA KATI ELEKEZI (shahidi) CHA WAKATI ULIOPO, "tunafurahia" au (2) KITENZI CHA KATI TEGEMEZI (shahidi) CHA WAKATI ULIOPO "hebu tufurahie." Wasomi wamegawanyika kwa wazo hili. Kama mtu atachukulia "tuna" katika mst. 1 kama ELEKEZI kisha hiyo tafsiri lazima iwe thabiti katika mst. 3. Asili ya neno "furahia" ni kujivuna (NRSV, JB). Tazama Mada Maalum katika. 2:17. Waamini hawafurahii ndani mwao wenyewe (kama vile 3:27), bali katika lile Bwana alilowafanyia (kama vile Yer. 9:23-24). Asili hii hii ya Kiyunani umerudiwa katika mist. 3 na 11.

◙ **"katika matumaini ya"** Paulo daima alitumia neno hili kwa njia mbalimbali lakini zenye maana ile ile. Tazama nukuu katika 4:18. Daima ilihusiana na utimilifu wa imani ya mwamini. Hii inaweza kuelezewa kama utukufu, uzima wa milele, wokovu kamili, Ujio wa Pili, n.k. Utimilifu ni dhahiri, lakini dalili wakati zinakuja na hazijulikani. Daima ilihusishwa na "imani" na "upendo,"(kama vile 1 Kor. 13:13; Gal. 5:5-6; Efe. 4:2-5; 1The. 1:3; 5:8). Baadhi ya orodha ya matumizi ya maneno ya Paulo ni kama ifuatavyo.

1. Ujio waPili, Gal. 5:5; Efe.1:18; Tit. 2:13.
2. Yesu ndiye tumaini letu, 1 Tim. 1:1
3. Mwamini kuletwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 Thes. 2:19
4. Tumaini limewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Wokovu kamili, 1 The. 4;13

6. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2; 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
7. Hakikisho la wokovu, 1 The. 5:8-9
8. Uzima wa milele, Tit. 1:2; 3:7
9. Matokeo ya ukomavu wa Ukristo, Rum. 5:2-5
10. Ukombozi wa uumbaji wote, Rum.8:20-22
11. Wadhifa wa Mungu, 15:13
12. Utimilifu wa kuchukuliwa, Rum. 8:23-25
13. Agano la Kale kama mwongozo kwa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

## MADA MAALUMU: DHAMANA YA MKRISTO

A. Je! Wakristo wanaweza kutambua kwamba wameokolewa (kama vile 1 Yohana 5:13)? Yohana ana majaribio matatu au ushahidi.
   1. Kimafundisho (imani, 1 Yohana 1:1,5,10; 2:18-25; 4:1-6,14-16; 5:11-12)
   2. Mtindo wa maisha (utii, 1 Yohana 2:2-3; 2:3-6; 3:1-10; 5:18)
   3. Kijamii (upendo, 1 Yohana 1:2-3; 2:7-11; 3:11-18; 4:7-12, 16-21)
B. Dhamana imekuwa ni suala la kimadhehebu
   1. John Calvin alijikita katika uchaguzi wa Mungu. Amesema kuwa katika maisha haya kamwe hatuwezi kuwa na uhakika.
   2. John Wesley aliegemea juu ya dhamana ya uzoefu wa kidini. Aliamini kuwa tunao uwezo wa kuishi juu ya dhambi inayofahamika.
   3. Waamini wa Kanisa Katoriki na Kanisa la Kristo wanaegemea juu ya Kanisa la kimamlaka. Kundi alilomo mtu huyu ni jawabu la neno dhamana.
   4. Walokole wengi wameweka dhamana zao juu ya uhadi za Biblia, zilizoungamanishwa na tunda la Roho (kama vile Gal. 5:22-23) katika maisha ya mwamini (yaani, ufanano na Kristo wa kila siku).
C. Dhamana ya awali ya waaminio imeungamanishwa na sifa za Mungu wa Utatu
   1. Upendo wa Mungu Baba
      a. Yohana 3:16; 10:28-29
      b. Warumi 8:31-39
      c. Waefeso 2:5,8-9
      d. Wafilipi 1:6
      e. 1 Petro 1:3-5
      f. 1 Yohana 4:7-21
   2. Matendo ya Mungu mwana
      a. kifo badala yetu
         1) Matendo 2:23
         2) Warumi 5:6-11
         3) Wakorintho 5:21
         4) 1 Yohana 2:2; 4:9-10
      b. maombi ya kuhani mkuu (Yohana 17:12)
      c. maombi endeleu ya kusihi
         1) Warumi 8:34
         2) Waebrania 7:25
         3) 1 Yohana 2:1
   3. Huduma ya Roho wa Mungu
      a. wito (Yohana 6:44,65)
      b. kutia mhuri
         1) 2 Wakorintho 1:22; 5:5
         2) Waefeso 1:13-14; 4:3

c. hakikisha
    1) Warumi 8:16-17
    2) 1 Yohana 5:7-13

D. Lakini wanadamu yawapasa kukubali kujitolea kwa Mungu kupiitia agano lake (katika nafasi zote, ya awali na ile endelevu)
   1. waamini yawapasa kugeuka kutoka dhambini (toba) na kumwelekea Mungu kupitia Yesu (imani)
      a. Marko 1:15
      b. Matendo 3:16,19; 20:21
   2. waamini yawapasa kukupokea kujitolea kwa Mungu katika Kristo (tazama Mada Maalumu: Je! Kunamaanisha nini "kupokea," "Kuamini," "Kukiri/Kuungama," "Kusihi")
      a. Yohana 1:12; 3:16
      b. Warumi 5:1 (na kwa mfanano 10:9-13)
      c. Waefeso 2:5,8-9
   3. waamini yawapasa kuendelea katika imani (tazama Mada Maalumu: Ustahimilivu)
      a. Marko 13:13
      b. 1Wakorintho 15:2
      c. Wagalatia 6:9
      d. Waebrania 3:14
      e. 2 Petro 1:10
      f. Yuda 20-21
      g. Ufunuo 2:2-3,7,10,17,19,25-26; 3:5,10,11,21

E. Dhamana ni ngumu kwa sababu
   1. mara kwa mara waamini hutafuta uzoefu fulani ambao haukuhaidiwa katika Biblia
   2. mara kwa mara waamini hawaielewi injili kwa ukamilifu
   3. mara kwa mara waamini wanaendelea na dhambi kwa makusudi (kama vile Kor. 3:10-15; 9:27; 1 Tim. 1:19-20; 2 Tim. 4:10; 2 Pet. 1:8-11)
   4. aina ya mtu fulani (yaani, mtu aaminiye katika kushinda) asiyeweza kamwe kukubali upendo na ukubalifu usio na masharti wa Mungu
   5. katika Biblia kuna mifano ya maungamo ya uongo (kama vile Mat. 13:3-23; 7:21-23; Marko 4:14-20; 2 Pet. 2:19-20; 1 Yohana 2:18-19, tazama Mada Maalumu: Uasi)

Tazama Mada Maalumu: Dhamana ya Mkristo kwa maelezo ya mihitasari tofauti tofauti ya mafundisho haya.

◙**"utukufu wa Mungu"** fungu hili ni nahau ya Agano la Kale kwa uwepo binafsi wa Mungu. Hii ilimaanisha kusimama kwa mwamini mbele ya Mungu katika haki ya imani iliyotolewa na Yesu Siku ya Ufufuo (kama vile 2 Kor. 5:21). Mara nyingi inaitwa kwa neno la kithiolojia "kutukuza" (kama vile mist. 9-10; 8:30). Waamini watagawana ufanano wa Yesu (kama vile 1 Yohana 3:2; II Pet. 1:4). Tazama Mada Maalum: Tukufu 3:23.

**5:3**
**NASB "na siyo hii tu, lakini"**
**NKJV "na siyo hiyo tu, lakini"**
**NRSV "na siyo hiyo tu, lakini"**
**TEV -ondoa-**
**NJB "siyo hiyo tu"**

Pauloanatumia muungano huu wa maneno mara kadhaa (kama vile 5:3, 11; 8:23; 9:10, na 2 Kor. 8:19).

◙
**NASB "tunafurahi pia katika taabu zetu"**
**NKJV "tunajitukuza pia katika taabu zetu"**
**NRSV "tunajivuna pia katika mateso yetu"**
**TEV "tunajivuna pia katika shida zetu"**

**NJB “hebu tufurahi, vivyohivyo, katika shida zetu”**

Kama ulimwengu ulimchukia Yesu, utawachukia na wafuasi Wake (kama vile Mt. 10:22; 24:9; Yohana15:18-21). Yesu alikuwa amekomaa, akizungumza kibinadamu, kwa mambo alivyoteseka (kama vile Ebr. 5:8). Mateso huzaa kuaminiwa na ukomavu. Ufanano na Kristo ni mpango wa Mungu kwa kila aaminiye, mateso ni sehemu yake (kama vile 8:17-19; Matendo 14:22; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-19)!

## MADA MAALUM: KWANINI WAKRISTO WANATESEKA?

1. kwasababu ya dhambi binafsi (hukumu ya muda). Hii haimaanishi kwamba matatizo yote na mazingira magumu ni matokeo ya dhambi (kama vile Ayubu; Zaburi 73; Luka 14:1-5; Nehemia 9; Yohana 9; Mdo. 5:1-11; 1 Kor. 11:29-30; Gal. 6:7).
2. Kukuza hali ya kufanana na Kristo (Ebr. 5:8). Hata Yesu, ukizungumza kibinadamu alitakiwa akomae na ndivyo inavyowapasa wafuasi wake (kama vile Rum. 5:3-4, 8:28-29; 2 Kor. 12:7-10; Flp. 3:10; Ebr. 12:5-12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 1:7).
3. Kukuza ushuhuda wenye nguvu na wenye uhalisia (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-22; 1 Pet. 2:18-21, 3:13-17).
4. Kama ishara ya kuzaa kwa uchungu kwa Zama mpya (kama vile Mt. 24:6; Marko 13:8).
   Vitabu viwili ambavyo vimenisaidia mimi kushughulikia kutokuwepo na usawa na uovu wa ulimwengu ulioanguka ni Hannah Whithall Smith, The Christian's Secret of a Happy Life na John W. Wenham, The Goodness of God.

Mwamini lazima akumbuke kwamba matatizo na mateso sio kwamba ni ishara ya hasira ya Mungu au kukataliwa. Vitu vibaya hutokea kwa wafuasi waamiifu katika ulimwengu ulioanguka(kama vile. 1 Pet. 4:12-19). Ahadi za Mungu na kujitoa kwa Kristo ni ishara za upendo wa Mungu (kamavile Rum. 5:8). Maandiko lazima yachukue nafasi juu ya hali za muda!

◙**“kufahamu”** Huu ni KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA ENDELEVU, cha neno “*oida.*” Ni katika hali TIMILIFU, lakini kinafanyakazi kama NJEO YA WAKATI ULIOPO. Waamini, wakifahamu ukweli wa injili kama wanavyohusishana mateso inawafanya kukabili maisha kwa furaha na kujiamini ambayo haitegemei mazingira, hata wakati wa kuteswa (Efe. 4:4; 1 Thes. 5:16, 18). Waumini walifurahi“katika” matesona siyo “kwa sababu” yao.

**5:3 “taabu”** Tazama Mada Maalum ifuatayo**.**

## MADA MAALUM: TAABU (*thlipsis*)

Kunahitajika kuwepo na utofauti wa kithiolojia kati ya matumizi ya Paulo ya neno **(***thlipsis***)** na Yohana

A. Matumizi ya Paulo (ambayo yanaaksi matumizi ya Yesu)
   1. Matatizo, mateso, uovu uliohusishwa kwenye ulimwengu ulioanguka
      a. Mt. 13:21
      b. Rum. 5:3
      c. 1 Kor. 7:28
      d. 2 Kor. 7:4
      e. Efe. 3:13
   2. Matatizo, mateso, uovu uliosababishwa na wasio amini
      a. Rum. 5:3; 8:35; 12:12
      b. 2 Kor. 1:4,8; 6:4; 7:4; 8:2,13
      c. Efe. 3:13
      d. Flp. 4:14

e. 1 The. 1:6
f. 2 The. 1:4
3. Matatizo, mateso, uovu wa siku za mwisho
   a. Mt. 24:21,29
   b. Mark 13:19,24
   c. 2 The. 1:6-9

B. Matumizi ya Yohana
1. Yohana analeta utofauti maalum kati ya *thlipsis* na *orgē* au *thumos* (ghadhabu) katika ufunuo. *Thlipsis* ni kile waaminio hukifanya kwa wale wasio amini na *orgē* na *thumos* ni kile Mungu hukifanya kwa wale wasio amini.
   a. *thlipsis* – Uf. 1:9; 2:9-10,22; 7:14
   b. *orgē* – Uf. 6:16-17; 11:18; 16:19; 19:15
   c. *thumos* – Uf. 12:12; 14:8,10,19; 15:1,7; 16:1; 18:3
2. Yohana pia analitumia neno katika injili yake kuaksi matatizo yale waaminio hukabiliana nayo katika kila zama-Yohana 16:33

**5:3,4 "usitahimilivu"** Neno hili linamaanisha "kujitolea," "kuwa imara," "kuvumilia." Ni neno linalohusiana na uvumilivu kwa watu na mazingira. Tazama Mada Maalum katika 8:25.

◙

**5:4**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"tabiailiyothibtishwa"** |
| **NKJV, NRSV** | **"tabia"** |
| **TEV** | **"uthibitisho wa Mungu"** |
| **NJB** | **"tabia iliyojaribiwa"** |

Katika maandiko ya kale ya miaka ya 1970 katika Mwa.23:16; 1 Fal.10:18; 1 Nya.28:18neno hili lilitumika kujaribisha vyuma kwa ubora na uhalisia (kama vile 2 Kor. 2:9; 8:2; 9:13; 13:3; Flp. 2:22; 2 Tim. 2:15; Yakobo 1:12). Majaribu ya Mungu siku zote ni ya kuimarisha (kama vile Ebr. 12:10-11)! Tazama Mada Maalum: Kupimwa katika 2:18.

## MADA MAALUM: UKUAJI WA MKRISTO (tabia)

| Warumi 5:3-4 | Wagalatia 5:22-23 | Yakobo 1:3-4 | 2 Petro 1:5-7 |
|---|---|---|---|
| Dhiki inasababisha<br>* ustahimilivu<br>* tabia iliyothibitishwa<br>* tumaini (kama vile Mstari wa 2) | Tunda la Roho<br>* upendo<br>* furaha<br>* amani<br>* uvumilivu<br>* wema<br>* ukarimu<br>* uaminifu<br>* upole<br>* kiasi | Majaribu huzaa<br>* uvumilivu<br>* ukomavu<br>1. bidii<br>2.ukamilifu | Kufanyia kazi kwa bidii<br>* tabia njema<br>* maarifa<br>* kiasi<br>* ustahimilvu<br>* utauwa<br>* ukarimu wa kindugu (*philadelphia*)<br>* upendo wa kikristo (*agapē*) |

**5:5 "tumaini halikatishi tamaa"** Hiki kinaweza kuwa ni kidokezo kwenye nahau za Kiebrania (yaani, aibu kama vile Zab. 25:3,20; 31:1,17; 119:16; Isa. 28:16 [imenukuliwa kutoka Warumi 9:33]; Flp. 1:20).

◙**"kwa sababu upendo wa Mungu umemwagwa ndani ya mioyo yetu"** Hii inaonesha KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA; kifasihi, "upendo wa Mungu umemwagwa na unaendelea kumwagwa" KITENZI hiki daima kilitumika kwa Roho Mtakatifu (kama vile Matendo 2:17, 18,33; 10:45 na Tito. 3:6), ambacho kinaweza kuakisi Yoeli 2:28-29 (Isa. 32:15).

KIFUNGU MILIKISHI, "upendo wa Mungu kisarufi linaweza maanisha (1) upendo wetu kwa Mungu au (2) upendo wa Mungu kwetu" kama vile Yohana 3:16; 2 Kor. 5:14). Namba 2 ndio mtazamo pekee.

◙**"Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"** Ni KAULI TENDWA TIMILIFU YENYE HALI YA KUENDELEA. IRABU YA KUTENDWA daima inatumika kuelezea uwakala na Mungu. Hii ikiwa na maana kuwa, waaminio hawahitaji zaidi Roho. Ama wanae Roho tayari au sio Wakristo (kama vile 8:9). Kupewa Roho ilikuwa ni ishara kwa Enzi Mpya (kama vile Yoeli. 2:28-29), Agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-32).

◙Tazama uwepo wa nafsi tatu za Mungu yaani Utatu katika aya hii.

1. Mungu, mist. 1,2 ,5,8,10
2. Yesu, mist.1,6,8,9,10.
3. Roho, mst. 5

Tazama Mada Maalum: Utatu katika 8:11.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:6-11**
**6Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. 7Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. 8Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. 9Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.10Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake. 11Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho.**

**5:6**
**NASB "kwa wakati tulipokuwa tungali hatuna msaada"**
**NKJV "kwa wakati tulipokuwa bado hatuna nguvu"**
**NRSV "kwa wakati tulipokuwa tungali dhaifu"**
**TEV "kwa wakati tulipokuwa tungali hatuna msaada"**
**NJB "tulipokuwa tungali hatuna msaada"**

KITENZI hiki ni KAULI YA WAKATI ULIOPO YENYE HALI YA KUENDELEA. Kinamaanisha mwanadamu aliyeanguka wa asili ya Adamu. Wanadamu ni dhaifu dhidi ya dhambi. KIWAKILISHI"sisi" kinaelezea na kuonyesha usambamba wake na NOMINO katika mst. 6b "kisicho cha miungu" mst. 8 "watenda dhambi," namst. wa 10, "maadui," mist. 6 na 8 kithiolojia na kimuundo viko sambamba.

Usambamba wa nukuu:

| | ① | ② | ③ |
|---|---|---|---|
| mst.6 | hatukuwa na Msaada | Kristo alikufa kwa wasio wa Mungu | ----------- |
| mst. 8 | tulikuwa watenda dhambi | Kristo akafa kwa ajili yetu | ------------ |

| | | | |
|---|---|---|---|
| mst. 9 | ------ | kwa damu ake | akiwa sasa amehalalishwa |
| mst. 10 | tulikuwa maadui | kifo cha Mwanaye | tumepokea upatanisho |

Ukweli mkuu umerudiwa kwa kusisitiza

1. hitaji letu
2. kujitolea kwa Kristo
3. msimamo wetu mpya

◙

**NASB, NRSV "kwa wakati muafaka"**
**NKJV "kwa wakati sahihi"**
**TEV "kwa wakati ule Mungu alipochagua"**
**NJB "kwa wakati wake teule"**

Hii kihistoria ingerejea

1. amani ya Warumi (nabarabara) yaliyoruhusuusafirihuru
2. lugha ya Kiyunani iliyoruhusu kuvuka mawasilianoya kijadi
3. mwishowa miungu ya Wayunani na Warumi ukaleta matarajio, ulimengu wenye njaa kiroho (Marko. 1:15; Gal. 4:4; Efe. 1:10; Tito. 1:3)

Kithiolojia kuwa katika hali ya binadamu ulikuwa mpango, tukio la Mungu (kama vile Luka 22:22; Matendo 2:23; 3:18; 4:28; Waefeso 1:11)

**5:6,8,10 "alikufa kwa ajili ya waovu"**Hii ni KAULI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI.Inaonyesha maisha ya Yesu na kifo chake kama tukio lililounganishwa. Yesu alilipa deni. Hakudaiwa denibali sisi tulidaiwa deni ambalo hatungeweza kulilipa (kama vile Gal. 3:13; I Yohana. 4:10).

Kifo cha Yesu kilikuwa ni dhima iliyojirudia katika maandiko ya Paulo. Alitumia maneno kadha tofauti na mafungu kurejea kifo mbadala cha Yesu.

1. "damu" (kama vile 3:25; 5:9; 1 Kor. 11:25, 27; Efe. 1:7; 2:13; Kol. 1:20)
2. "alijitoa binafsi" (Efe. 5:2,25)
3. "alitolewa" (kama vile Rum. 4;25; 8:32)
4. "sadaka" (kama vile 1 Kor. 5:7)
5. "alikufa" (kama vile Rum. 5:6;8:34; 14:9,15; 1 Kor. 8:11; 15:3; 2 Kor. 5;15; Gal. 5:21; 1 The. 4:14; 5:10)
6. "msalaba" (kama vile 1 Kor. 1:17-18; Gal. 5:11; 6:12-14; Efe. 2:16; Flp. 2:8; Kol. 1:20;2:14)
7. "kusurubishwa" (kama vile 1 Kor. 1:23; 2:2; 2 Kor. 13:4; Gal. 3:1)

KIHUSISHI *huper* katika neno hili kina maana ya

1. uwakilisho, "kwa niaba yetu"
2. mbadala, "kwa nafasi yetu"

Kwa kawaida maana kuu ya *huper* kikiwa na HALI YA UMILIKISHI ni "kwa niaba ya" (Louw na Nida). Inaelezea faida kadhaa zinazotokana na watu (*The New Internation dictionary of the New Testament Theology,* vol. 3, ukur.1196). Hata hivyo, *huper* lina maana ya *ant*, likimaanisha "kwanafasi ya" hivyo kithiolojia linamaanisha upatanisho mbadala kwa ajili ya wengine (kama vile Marko 10:45; Yn. 11:50; 18:14; 2 Kor. 5:14; 1 Tim. 2:6). M.J. Harris (NIDNTT. Juzuu 3.uk.1197) anasema, lakini kwa nini Paulo hasemi kuwa Yesu Kristo alikufa "*anti hēmōn* (1 Tim. 2:6 na karibu anakuja-*antilutron huper pantōn*)? Labda ni kwa sababu kiwakilishi *huper,* tofauti na*anti,* kwa pamoja vingeonyesha uwakilisho na hali mbadala.

M. R. Vincent, *World Studies,* juzuu 2, anasema

> "Bado kunabishana kama *huper,* kwa niaba ya, ni sawa kabisa na *anti,* badalaya. Waandishi mahiri huonyesha mifano pale ambapo maana zinaonekana kubadilishana…Maana ya habari hii hata hivyo, haina uhakika kabisa kiasi kwamba haiwezi kuonekana Kama ushuhuda. Kihisishi kinaweza kuwa na maana isiyo rasmi, *juu ya* mfu.Hakuna habari yoyote kati ya hizi inaweza kuchukuliwaKama ya maamuzi. Kinachoweza

kusemwa zaidini kuwa*huper* inazingira juu ya neno *anti. Badala ya* linasihi Sana juu ya misingi ya imani. Sehemu kubwa yahabari iliyoandikwa maana iko wazikwa neno *"kwa niaba ya,"* "*kwa ajili ya*." Maelezo halisi yanaonyesha kuwa, katika habari hii kikanuni katika swali, zile, zilizotajwa, zinazojihusisha na kifo cha Kristo, kama ilivyo hapa ni Gal. 3:13; Rum. 14:15; 1 Pet. 3:18, *huper* inaonyesha kihusishi kisicho na hakika, yaani cha jumla tu–Kristo alikufa kwa niaba yetu–likawa limeacha neno badala ya pasipo kubainisha, hivyo kuendelea kutafutiwa maana katika habari nyingine. Maana ya *badala ya* inaweza kujumuisha humo, lakini kwa kuhitimisha tu." (uk. 692).

**5:7** Mstari huu unaonyesha upendo wa mwanadamu wakati mstari wa 8 unaonyesha upendo wa Mungu!

◙
**NASB, NKJV,**
**TEV "kwa binadamu mwenye haki"**
**NRSV "kwa mtu mwenye haki"**
**NJB "kwa mtu mwema"**

Usemi huu alitumiwa kwa maana ile ile kama Nuhu na Ayubu walikuwa watu wenye haki au wasiolaumiwa. Walitimiza matakwa ya kidini kwa siku zao. Haimanishi kuwa hawakuwa na dhambi. Tazama Mada Maalum katika 1:17.

**5:8 "Mungu anadhihirisha upendo Wake"** Hii inaonyesha KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO (kama vile 3:5). Baba alimtuma Mwanae (kama vile 8:3,32; 2 Kor. 5:19), upendo wa Mungu sio fuata upepo,bali hufuata matendo (kama vile Yn. 3:16; 1 Yn. 4:10) na hautetereki.

◙ **"ya kwamba wakati ambao tulikuwa bado watenda dhambi"** Inatushangaza kuona kwamba upendo wa Mungu ulionyeshwa kwa "watenda dhambi,"sio wasio tu wa Mungu, au watu wa asili ya Mataifa mengine bali waasi! Neema, sio manufaa, ni msingi wa ukweli! Mungu bado anahitaji ushirika na wanadamu. Ni tabia Yake isiyobadilika inayotupa amani na matumaini (Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8; 145:8).

**5:9 "zaidi na zaidi"** Haya yalikuwa mojawapo ya maelezo pendwa ya paulo (kama vile mist. 10, 15,17). Kama Mungu aliwapenda waaminio kiasi kile wakati wakiwa watenda dhambi, ni kwa kiasi gani hivi Yeye leoanawapenda kwamba wao ni watoto Wake (kama vile 5:10; 8:22).

◙**"akiwa sasa amethibitishwa"** Hii ni KAULI TENDWA TIMILIFU ENDELEVU, ambayo inasisitiza uthibitisho kama tendo timilifu lililohitimishwa na Mungu. Paulo anarudia ukweli wa mst. 1. Pia tazama usambamba uliopo kati ya maneno "kuhalalishwa"(mst.9) na "kuthibitishwa" (mist. 10-11).

◙**"kwadamu Yake"** Hii ilikuwa ni marejeo ya kifocha Kristo (kama vile 3:5; 4:25; Marko 10:45; II Kor. 5:21). Dhana hii ya sadaka, maisha yasiyo na hatia kutolewa kwa niaba ya maisha yenye hatia, inapatikana katika Walawi 1-7 na bila shaka Kutoka 12 (Pasaka ya mwana- kondoo), na kithiolojia ilitumika kwa Yesu katika Isa. 53:4-6. Na inaendelezwa katika mtizamo waKikristo katika kitabu cha Waebrania (kama vile sura 9-10). Waebrania inalinganisha Agano la Kale na Agano Jipya katika vipengele kadhaa.

◙**"tutaokolewa"**Hii inamanisha KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO (kama vile mst. 10). Hii inamaanisha wokovu wetu kamili, ambao unaitwa utukufu (kama vile mst. 2; 8:30; I Yohana 3:2).Agano la Jipya linaeleza wokovu katika nyakati za VITENZI vyote.

1. Tendo lililotendeka (WAKATI TIMILIFU), Matendo. 15:11; Rom. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito. 3:5
2. tendo lililopita lenye matokeo katika hali iliyopo (WAKATI ULIOPITA), Efe. 2:5,8
3. hatua ya kimaendeleo (WAKATI ULIOPO), 1Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15; 1 Thes. 4:14; 1 Pet. 3:21.
4. ukamilisho ujao (WAKATI UJAO), Rum. 5:9,10; 10:9.

Tazama Mada Maalum katika 10:4. Wokovu unaanza na maamuzi ya awali (kama vile 10:9-13; Yohana. 1:12; 3:16) lakini unakuwa ndani ya uhusiano hatua moja hadi nyinginehadi siku moja kukamilika. Dhana hii daima inaelezeka kwa maneno matatu ya kithiolojia.

1. uthibitisho, linalomaanisha “kukombolewa kutoka adhabu ya dhambi”.
2. utakaso, linalomaanisha “kukombolewa kutoka katika nguvu za dhambi”
3. utukufu, linalomaanisha “kukombolewa kutoka katika uwepo wa dhambi.”

Ni vyema kutambua kuwa kuthibitishwa na kutakaswa yoteni matendo ya neema ya Mungu, yalitolewa kwa aliyeamini kupitia imani katika Kristo. Hata hivyo Agano Jipya pia linazungumzia juu ya utakaso kama mchakato unaendelea wa kufanana na Kristo. Kwa maana hiyo, wanathiolojia wanazungumza kuhusu “utakaso wa mahali” na “utakaso unaoendelea.” Hii ni ajabu ya wokovu wa burekuunganishwa na maisha ya kimungu. Tazama Mada Maalum katika 6:4.

◙**“kutoka katika hasira *ya Mungu*”** huu ni muktadha wa mambo yajayo. Biblia inaelezea juu ya ukuu wa Mungu, usiostahili, upendo usio na manufaa, lakini pia inasema wazi upinzani wake wa dhambi na uasi. Mungu anatoa njia ya wokovu namsamaha kupitia kwa Kristo, lakini wale wanao mkataawako katika hasira Yake (kama vile 1:18-3:20). Hili ni fungu la maneno ya lugha za kidini kuhusu Mungu,(tazama Mada Maalum katika 1:18), lakini linaelezeaukweli. Tazama Mada Maalum katika 6:4.Ni jambo la kutisha kuangukia katika mikono ya Mungu mwenye hasira (Waeb. 10:31).

**5:10 “kama”** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZAambayo inachukuliwa kuwa kwelikutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi yake ya kifasihi. Ubinadamu, lengo kuu la Mungu la uumbaji (kama vile Mwa. 1:26-27), akawa adui! Mtu (kama vile Mwa. 3:5) akatamani kutawala, akatamani kuwa miungu.

◙**“tulisuluhishwana Mungu….tulipokwisha suluhishwa”** Ni zote mbili KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU na KAULI TENDWA TIMILIFU YENYE HALI YA KUENDELEA. KITENZI “suluhishwa” (kama vile I Kor. 7:11; II Kor. 5:18, 19, 20; pia nukuu Kol. 1:20) kwa asili kilimaaanisha “kubadilishana.” Mungu amebadilisha dhambi zetu na haki ya Yesu (kama vile Isa. 53:4-6). Imani imerejeshwa (kama vile mst.1)!

◙ **“kupitia katika kifo cha Mwanae”** Injili ya msamahaimejumuishwa katika

1. upendo wa Mungu (kama vile Yohana 3:16)
2. kazi ya Kristo (8:32; Gal. 1:4; 2:20)
3. ombi la Roho (Yohana 6:44;65),
4. mwitikio wa imani/toba ya mtu mwenyewe (Mk. 1:15; Yn 1:12, Mdo. 20:21

Hakuna njia nyingine ya kuwa sawana Mungu (kama vile 10:1-2, 7-8; Yohana 14:6; Mdo. 4:12; I Tim. 2:5). Uthibitisho wa wokovu uko katika tabia ya Mungu wa Utatu (kama vile Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8; 145:8), na siyo utendaji wa mwanadamu. Kitendawili ni kwamba, matendo ya mwanadamu baada ya wokovu ni ushuhuda wa wokovu wa bure (Yakobo na I Yohana).

◙**“tutakombolewa”** Agano Jipya linazungumzia wokovu kama wakati uliopita, uliopo, na ujao. Hapa ujao unaoneshwa na mwisho wetu, wokovu kamili kwa Ujio wa Pili (kama vile 1 Yohana 3:2) Tazama nukuu katika mst. 9 na Mada Maalum katika 10:13.

◙**“kwa maisha Yake”** Neno la Kiyunani lenye kumaanisha maisha ni *zoa*. Neno hili katika maandiko ya Yohana siku zote lilitumika katika maisha ya ufufuo, uzima wa milele au maisha ya ufalme. Paulo pia alitumia vivyo katika maana ya kithiolojia. Msukumo wa neno hili hapa ni kwamba tangu pale Mungu alilipa gharama kubwa kwa ajili ya msamaha wa waaminio, kwa ajili ya msamaha wao, hakika ataendeleza kuitenda.

“Maisha” yanaweza kumaanisha ama:

1. ufufuo wa Yesu (kama vile 8:34; 1 Kor. 15)
2. kazi ya Yesu ya kutuombea (kama vile 8:34; Ebr. 7:25; 1 Yohana 2:1)
3. Roho kumfanya Kristo ndani yetu (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19)

Paulo alitetea kuwa, maisha ya Yesu duniani na kifo chake pamoja na maisha yake kuinuliwa (kupaa mbinguni, Matendo 1) ndio misingi ya usuluhisho wetu.

**5:11 “Na siyo hili tu, lakini”** Tazama nukuu katika mst. 3

◙**"sisi pia tunafurahia"** Tazama nukuu katika 5:2. Hii ni mara ya tatu ya matumizi ya "kufurahi" (jivunia) katika eneo hili.

1. kufurahi katika tumaini la utukufu, mst. 2
2. kufurahi katika dhiki kuu,mst. 3
3. kufurahi katika suluhisho, mst. 11

◙**"sasa tumepata suluhisho"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, tendo lililokamilika. Patano la Waamini (kubadilishana) pia linajadiliwa hapa katika mst. 10 na 2 Kor 5:18-21; Efe. 2:16-22, Kol. 1:19-23. Katika Mazingira haya "suluhisho" kithiolojia ni ufupisho wa neno "uhalalisho"

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:12-14**
**[12]Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi; [13]maana kabla ya sheria dhambi likuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria; [14]walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, aliye mfano wake yeye atakayekuja.**

**5:12 "Kwa hiyo"**Warumi imeweka mikakati mingi "hivyo" (kama vile 5:1; 8:1; 12:1). Swali la kutafakari ni kwamba zinahusianaje. Zingeweza kuwa ni rejea kwa mjadala mzima wa Paulo. Kwa hakika hili linahusiana na Mwanzo na, kwa hiyo, yamkini rejea katika Rum. 1:18-32.

◙**"na kwa kupitia kwa mtu mmoja dhambi ikaingia"** VITENZI vyote vitatu katika mst. 12 ni NJEO TIMILIFU kuanguka kwa Adamu kulileta kifo (kama vile 1 Kor. 15:22). Biblia haisimami kwenye asili ya dhambi. Dhambi pia ilitokea katika ufalme wa malaika (Mwa. 3 na Ufu. 12:7-9). Kwa namna gani na lini hakuna uhakika (kama vile Isa. 14:12-27; Ezek. 28:12-19; Ayubu. 4:18; Mt. 25:41; Luka. 10:18; Yohana. 12:31; Ufu. 12:7-9).

Dhambi ya Adam ilihusu maeneo mawili (1) kutotii amri maalum (kama vile Mwa. 2:16-17), na (2) majivuno yake binafsi (kamavile Mwa. 3:5-6). Hili linaendelea kutajwa katika Mwanzo 3 likianzia Rum. 1:18-32. Ni thiolojia ya dhambi ambayo waziwazi inamtenga Paulo na wazo la kiongozi wa dini. Viongozi wa dini hawakutazama Mwanzo 3, badala yake walidai kuwa kuna "makusudio" mawili (*yetzers*) katika kila mtu. Semi zao maarufu za viongozi wao wa dini "Katika kila moyo wa mwanadamu kuna mbwa mweusi na mweupe. Anayemlisha sana ndiye anayenenepa zaidi". Paulo aliona dhambi kuwa ndio ilikuwa kikwazo kati ya Roho Mtakatifu na uumbaji wa Mungu. Paulo hakuwa Mwanathiolojia aliyekuwa na mipangilio sana (kama vile James Steward's *A man in Christ*). Alionyesha vyanzo kadhaa vya dhambi (1) Kuanguka kwa Adamu (2) majaribu ya kishetani, na (3) mwendelezo wa uasi wa binadamu (Efe. 2:2-3).

Katika kutofautiana na kushabihiana kithiolojia kati ya Adamu na Yesu mambo mawili muhimu yanajitokeza:

1. Adamu alikuwa mtu wa kihistoria wa kweli.
2. Yesu alikuwa mwanadamu wa kweli.

Kweli hizi mbili zinaikubali Biblia kuwa katika sura ya mafundisho ya uongo. Tazama kurudiakwatumizi ya neno "mtu mmoja" au "ambaye." Njia hizi mbili za kuwarejea Adamu na Yesu zinatumika mara kumi na moja katika sura hii.

◙**"mtu mmoja"** Asiliya fungu hili (kifasihi. *henos anthrōpou*) linatumika kumwakilisha Adamu (mist. 12,16,17,18,19) au Yesu (mist. 15 [mara mbili], 17 [mara mbili], 18,19). Kila moja linawakilisha kundi au jamii (yaani "wengi," kama vile mist. 15 [mara mbili], 19 [mara mbili]; "yote," kama vile mist. 12,13,18 [mara mbili].

◙**"kifo kupitia katika dhambi"** Kwanza Agostino alifuatilia neno "dhambi asilia." Linaelezea matokeo ya chaguzi za Adamu/Eva katika Mwanzo 3.Uasi wao umeathiri uumbaji wote. Wanadamu wanakabiliwa na:

1. mfumo wa ulimwengu ulioanguka
2. ushawishi binafsi
3. ajili iliyoanguka

Dhambi ya asili (mist.12-14, 16a,17) inaunda ubia na dhambi binafsi (mist. 12d, 16b) kuwafanya wanadamu wote kuwa watenda dhambi. Dhambi matokeo yake ni "mauti" (kama vile 1:32, 6:13,16,21,23; 7:5,9,10,11,13,24; 8:13).

Maoni yaKibiblia ya Jerome (uk. 308) inataja utamaduni wa viongozi wa kidini kuwa kulikuwa na vipindi vitatu vya historia.

1. Adamu – Musa
2. Musa – Masia
3. Masia – Thiolojia ya mambo yajayo

Kama Paulo alikuwa anafikiri mgawanyo huu basi

1. Adamu – Musa (dhambi asili, hakuna sheria bali kifo)
2. Musa – Masia (dhambi binafsi, uasi wa sheria
3. Masia – (uhuru kutoka katika Sheria/sheria kupitia neema)

◙**"kifo kilienea kwa watu wote"** Msukumo mkubwa katika aya hii ni ule mwenendo wa dhambi ulimwenguni kote (kama vile mist. 16-19; 1 Kor. 15:22; Gal. 1:10), ambayo ni kifo.

1. kifo cha kiroho – Mwa. 2:17; 3:1-24; Isa. 59:2; Rum. 7:10-11; Efe. 2:1; Kol. 2:13; Yakobo 1:15
2. kifo cha mwili – Mwa. 3:4-5; 5:1-32
3. kifo cha milele – Ufu.2:11; 20:6, 14; 21:8

◙**"kwa sababu wote walitenda dhambi"**Wanadamu wote wanatenda dhambi kutokana na ushirika na Adamu (yaani, walirithi hali ya dhambi na tabia ya kuwa wenye dhambi.) Kwa sababu hii , kila nafsi inachagua kutenda dhambi kibinafsi na kwa kurudiarudia. Biblia inasisitiza kuwawanadamu wote ni watenda dhambi kwa ushirika na binafsi (kama vile 1 Falm. 8:46; 2 Kor. 6:36; Zab. 14:1-2; 130:3; 143:2; Mithali 20:9; Mhu. 7:20; Isa. 9:17;53:6; Rum. 3:9-18;23; 5:18; 11:32; Gal. 3:22; 1 Yohana. 1:8-10).Bado katika hili inasisitizwa (kama vile mist. 15-19) kuwa tendo moja linasababisha kifo (Adamu) na tendo moja linasababisha uzima (Yesu). Hata hivyo, Munguameunda kikamilifu uhusiano Wakena mwanadamu hivyo kwamba uamuzi wa mwanadamu nisuala nyeti la "upotevu" na "uthihirisho". Wanadamukwa maamuzi yao wanahusika na hatima yao ya mbele. Wanaendelea kuchagua dhambi au Kristo. Hawawezi kuathiri chaguzi hizi mbili, bali kwa uamuzi wao huamua upande gani wawe.

Tafsiri ya "kwa sababu"ni ya kawaida, lakini maana yake daima ina mjadala. Paulo alitumia *eph' hō* katika 2 Kor. 5:4; Flp. 3:12 na 4:10 kwa maana ya "kwa sababu." Kwa hiyo kilamwanadamu binafsi ana ushirika katika dhambi na uasi kwa Mungu. Baadhi kwa kukataa ufunuo maalum, lakini wengi kwa kukataa ufunuo asilia (kama vile 1:18-3:20).

**5:13-14** Ukweli huu unafundishwa katika Warumi 3:20; 4:15 na Matendo 17:30. Mungu hapendelei. Wanadamu wanawajibika tu na kile ambacho ni chao. Mstari huuunazungumzia tu ufunuo maalum (Agano la Kale, Yesu, Agano Jipya), na sio ufunuo alisia (kama vile Zab. 19:1-6; Rum. 1:18-23; 2:11-16). Nukuu kuwa NKJV inaona ulinganisho huu wa mst.12 kama umetenganishwa na mabano marefu (mist. 13-17) kutoka katika hitimisho lake katika mist.ya18-21.

**5:14**
**NASB, NKJV,**
**NJB** **"kifo kilitawala"**
**NRSV** **"kifo kilifanya himaya"**
**TEV** **"kifo kilitawala"**

Kifo kilitawala kama mfalme (kama vile mist. 17 na 21). Hali hii ya kifo kuwa kama mtu na dhambi kuwa kama mtawala inanaendelea kujadiliwa katika sura hii na sura ya sita 6. Uzoefu wa kifo ulimwenguni unadhihirisha dhambi ya mwanadamu ulimwenguni.Katika mistari ya 17 na 21, neema inaonekana kama mtu, neema inatawala. Wanadamu wana uchaguzi (njia mbili za Agano la Kale yaani; "kifo" au "uzima" kama vile Rum. 11:26; 30:1,19), kifo au uzima. Nani anatawala katika maisha yako?

◙**"hata juu ya wale ambao hawakutenda dhambi mithili ya uasi wa Adamu"** Adamu aliasi amri halali ya Mungu ( yaani Mwa. 2:15-17), hata Hawa hakutenda dhambi kwa njia hii. Alisikia kutoka kwa Adamu kuhusu mti, siyo moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Wanadamu kutokea kwa Adamu hadi kwa Musa waliathiriwa na uasi wa Adamu. Hawakukaidi amri maalum toka kwa Mungu, lakini 1:18-32, ambayo kwa hakika ni sehemu ya kithiolojia ya suala

hili, inaeleza ukweli kuwa walikaidi nuru waliokuwa nayo tangu uumbajina hivyo basi kuwajibika kwa Mungu kwa uasi/dhambi. Hulka ya Adamu ya kutenda dhambi ikaenea hadi kwa watoto wakewote.

◙

**NASB, NKJV**
**NRSV** **"ni nani ambaye ni wa aina Yake aliyekuwa aje?"**
**TEV** **"Adamu alikuwa na umbo lake ambaye alikuwa aje"**
**NJB** **"Adamu alitengenezwa umbo la Yule ajae"**

Hii inaelezea njia thabiti ya uainishi waAdamu – Kristo (kama vile 2 Kor. 15:21-22; 45-49; Flp. 2:6-8). Wote wawili wanaonekana kuwa wa kwanza katika mfuatano, mwanzo wa mbio (kama vile 1 Kor. 15:45-49). Adamu ni mtu pekee kutoka katika Agano la Kale aliyeitwa kipekee "aina" katika Agano Jipya ( kwa "Israel" tazama, 1 Kor. 10:16). Tazama Mada Maalum: Namna (*Tupos*) katika 6:17.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:15-17**
**[15]Lakini karama ile haikuwa kama lile kosa; kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi. [16]Wala kadiri ya yule mtu mmoja aliyefanya dhambi si kadiri ya kile kipawa; kwa maana hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu; bali karama ya neema ilikuja kwa ajili ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki. [17]Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo.**

**5:15-19** Huu ni mjadala unaoendelea kwa kutumia mafungu yaliyosambamba. NASB, NRSV, na TEV wanaigawa aya katika mst. 18. Ambapo UBS[4], NKJ na JB, wanaitafasiri kama kifungu. Kumbuka kitu muhimu kwenye utafasiriwa kusudi la mwandishi wa kwanza ndiyo hoja kubwa ya ukweli kwa kila aya.Tazama kuwa kila neno "wengi," mist. 15na 19 ni sawa na neno "wote" katika mist. ya 12 na 18. Hili pia ni sawa katika Isa. 53:11-12 na mst.6. Hakuna mipaka ya kithiolojia (chaguo la Calvin mst.dhidi ya ile isiyochaguliwa) lazima ifanyike kwa msingi wa maneno haya.

**5:15 "kipawa cha bure"** Kuna maneno mawili tofauti ya Kiyunani kwa "karama" yanayo tumika katika mazingira haya-*charisma*, mist. 15, 16 (6:23) na *dorea/dorama*, mist. 15,16,17. (tazama nukuu katika 3:24)–lakini yanafanana. Hii hakika ni habari njema kuhusu wokovu. Ni karama ya bure kutoka kwa Mungu kupitia kwa Yesu Kristo (kama vile 3:24; 6:23; Efe. 2:8, 9) kwa wote wanaomwamini Yesu Kristo.

◙**"kama"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudio lake la kifasihi. Dhambi ya Adamu ilileta mauti kwa watu wote. Hii ni sambamba na mst.wa 17.

◙**"kama wingi,"** Tazama Mada Maalum katika 15:13.

**5:16 "laana …uhalalisho"** Yote ni maneno yanayotumika katika uchunguzi wa kitaalamuna kisheria. Daima Agano la Kale liliwasilisha ujumbe wamtume kama maelezo. Paulo anatumia namna hii (kama vile Rum. 8:1, 31-34).

**5:17 "kama"** Hii tena ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudi lake la kifasihi. Kosa la Adamu lilileteleza kifo kwa wanadamu wote.

◙**"watakao pokea wapata zaidi"** Mistari 18 na 19 kithiolojia haina mlinganyo mzuri. Fungu hili haliwezi kuondolewa kutokana na mazingira ya Warumi 1-8 na kuthibitisha kwa walimwengu (kwamba wote wataokolewa). Wanadamu wote lazima wapokee (mst. 17b) kujitolea kwa Mungu katika Kristo. Wokovu unapatikana kwa wote, lakini sharti upokelewe kwa mtu binafsi (kama vile Yn. 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13).Tendo moja la Adamu la uasi limepelekea wanadamu wote kuwa waasi kabisa.Tendo moja la dhambi limekuzwa! Lakini katika Kristo, sadaka moja ya haki imekuzwa kuenea kwa kuondoa dhambi ya mtu mmoja mmoja na ile dhambi ya

ushirika kutokana na Adamu. “ile nyingi zaidi” ya tendo la Kristo imesisitizwa (kama vile mst. 9,10,15,17). Neema kwa wingi!

**5:17,18 “zawadi ya hakiitatawalauzimani….uthibitisho wa uzima”**Yesu ni zawadi ya Mungu na toleo kwa wanadamu wote walioanguka katika hitaji la kiroho (kama vile 1 Kor. 1:30). Ayahizi zilizosambamba zinazoweza kumaanisha

1. mwanadamu aliyetenda dhambi amepewa haki ya kusimama na Mungu kupitia kazi ya Kristo aliyoimaliza iliyoleta matokeo ya “maisha ya kimungu.”
2. aya hii ina maana sawa na “kuishi milele”.

Mtazamo huu unaunga mkono maoni ya kwanza. Kwa neno la kujifunza juu ya haki tazama mada maalum katika 1:17.

KITENZI “kutawala” kinatumika mara kadhaa katika muundo huu.

1. “kifo kilitawala tangu Adamu hadi Musa,” mst. 14 (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU)
2. “Kifo kilitawala kupitia kwa mmoja,” mst. 17 (KAULI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI)
3. “zaidisana wapate wale wanaopokea wingi wa neema, na zawadi ya haki itatawala katika maisha yao,” mst. 17 KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI UJAO)
4. “Dhambi ilitawala katika mauti,”mst. 21 (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU)
5. “neema ingetawala,” (KAULI TENDAJI TIMILIFU YA HALI YA UTEGEMEZI)
6. “Tusiruhusu dhambi kutawala,” mst. 16:12 (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO)

Nafsi ya Paulo katika dhambi na mauti dhidi yakarama ya neema ni njia madhubuti kuelezea ukweli wa thiolojia!

## MADA MAALUM: KUTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU

Dhana ya kutawala tukiwa na Kristo ni sehemu ya namna kubwa ya kithiolojia inayitwa “ufalme wa Mungu.” Huu ni mwito toka dhana ya Agano la Kale la Mungu Yeye kama Mfalme wa kweli wa Israel (kama vile 1 Sam.8:7). Kiishara anatawala (1 Sam. 8:7; 10:17-19) kupitia kizazi cha kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10) na familia ya Yese (kama vile 2 Samwel 7).

Yesu ni ahadi ya utimilifu wa unabii wa Agano la kale kuhusiana na Masihi. Aliuanzisha Ufalme wa Mungu akiwa na mwili wa kibinadamu pale Bethlehemu. Ufalme wa Mungu ukaja kuwa ni nguzo kuu ya mafundisho ya Yesu. ufalme wa Mungu ukawa kamili ndani yake (kama vile Mt. 10:7; 11:12; 12:28; Mark 1:15; Lk 10:9,11; 11:20; 16:16; 17:20-21).

Hata hivyo, ufalme ulikuwa wa wakati ujao (matukio ya siku za mwisho). Ulikuwepo lakini ukawa haujatimilizwa (kama vile. Mt. 6:10; 8:11; 16:28; 22:1-14; 26:29; Lk 9:27; 11:2; 13:29; 14:10-24; 22:16,18). Kwa mara ya kwanza Yesu akaja kama mtumwa mwenye mateso (kama vile. Isa. 52:13-53:12); mwenye kunyenyekea (kama vile. Zak. 9:9), bali atarudi kama Mfalme wa Wafalme (kama vile. Mt. 2:2; 21:5; 27:11-14). Dhana ya “kutawala” kwa uhakika ni sehemu ya “Ufalme” wa thiolojia. Mungu amekwisha kuwapatia ufalme wafuasi wa Kristo (angalia Lk 12:32).

Dhana ya kutawala pamoja na Kristo ina mitizamo mbali mbali pamoja na maswali

1. Je sura zile zinazodai kuwa Mungu amewapa waamini “ufalme” kupitia Kristo zinarejea juu ya “kutawala” (kama vile Mt. 5:3,10; Lk 12:32)?
2. Je maneno ya Yesu kwa wanafunzi wa mwanzo kwenye karne ya kwanza katika mazingira ya Kiyahudi yanarejea kwa waamini wote (kama vile. Mt. 19:28; Lk 22:28-30)?
3. Je misisitizo ya Paulo juu ya kutawala katika maisha haya ya sasa yanakinzana au yanawiana na maandiko ya hapo juu (kama vile. Rum. 5:17; 1 Kor. 4:8)?
4. Ni kwa namna gani mateso na utawala vinahusiana (kama vile. Rum. 8:17; 2 Tim. 2:11-12; 1 Pet. 4:13; Uf. 1:9)?
5. Dhana ya kujirudia ya ufunuo unachangia pamoja utawala wa Yesu uliotukuzwa, lakini huo utawala wa
    a. Kidunia, Uf. 5:10
    b. Utawala wa miaka 1000, Uf. 20:4-6
    c. Milele, Uf. 2:26; 3:21; 22:5 na Dan. 7:14,18,27
        a.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:18-21**
**[18]Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadharika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. [19]Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wameingizwa katika hali ya wenye haki. [20]Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi; [21]ili kwamba, kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, vivyo hivyo kwa njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu.**

**5:18**
**NASB “hata hivyo kupitia kwa tendo moja la haki pakatokea udhihirisho wa maisha kwa watu wote”**
**NKJV “hata hivyo kupitia tendo la haki la mtu mmoja, zawadi huru ikaja kwa watu wote”**
**NRSV “kwa hiyo tendo moja la mtu la haki likapelekea kufanyika udhihirisho na maisha kwa wote.”**
**TEV “kwa njia hiyo hiyo tendo moja la haki likawaweka watu huru na kuwapa maisha?”**
**NJB “kwa hiyo, tendo moja jema la mtu mmoja maishani nakufanya wadhihirishwe.”**

Hii si kusema kwamba kila mmoja ataokolewa (ulimwengu wote). Mstari huu hauwezi kutafasiriwa mbali na ujumbe nzima toka kitabu cha Warumi na mazingira yaliyopo. Hii inamaanisha thamani ya wokovu kwa watu wote kupitia maisha ya Yesu/kifo/na ufufuo. Wanadamu wanapaswa kujongea kwenye zawadi ya Injili kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19 20:21). Siku zote Mungu anaangalia ari (kama vile Yohana. 6:44,65), lakini amechagua ya kwamba kila mtu lazima ajongee kwake binafsi (kama vile Mt. 11:28-29, Yohana 1:12, 3:16 na Rum. 10:9-13). Zawadi yake ni ya ulimwengu (kama vile 1 Tim. 2:4,6; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2), lakini ajabu ya uovu ni kwamba wengi wanasema “hapana.” “Tendo la haki” ni kama

1. Maisha yote ya Yesu ya utii na kufundisha kikamilifu kulibainisha Baba
2. Kifo chake hasa, kwa niaba ya wanadamu wote watenda dhambi.

Kwa vile maisha ya mtu mmoja yaliathiri wote (ushiriki wa Wayahudi kama vile Yos. 7),vivyo hivyo, maisha ya mmoja asiye na hatia yaliathiri wote (Law 1:7,16). Matendo haya mawili yako sambamba, lakini sio sawa. Wote wameathiriwa na dhambi ya Adamu, lakini kiuthamani wote wameathiriwa na maisha ya Yesu, na waumini pekee ambao wamepokea zawadi ya uhalalisho. Tendo la Yesu pia linaathiri dhambi za watu wote. Kwa wale wanaoamini na kupokea wakati uliopita, uliopo na ujao.

**5:18-19 “laana kwa watu wote….uhalalisho wa maisha kwa watu wote…..wengi walifanywa wadhambi….wengi walifanywa kuwa wenye haki”** Haya ni mafungu sambamba yanayoonyesha neno “wengi,” sio yenye vipingamizibali yanajumuishwa. Usambamba huu huu pia unapatikana katika Isa. 53:6 “wote” na 53:11,12 “wengi.” Neno “wengi” haliwezi kuwa na masharti kwa Mungu katika kutoa zawadi yake ya wokovu kwa wote (chaguo la Kelvin dhidi ya lisilochaguo).
Tazama IRABU TENDEWA. Vyote vinarejea katika kazi ya Mungu. Dhambi za wanadamu kwa mahusiano na tabia ya Mungu (kipimo cha uasi) na wanahalalishwa kwa uhusiano na tabia ya Mungu (zawadi ya neema yake)

**5:19 “kutotii kwa mtu mmoja…..kutii kwa mwingine”**Paulo alikuwa akitumia dhana ya kithiolojia ya ushirika wa Agano la Kale. Tendo la mtu mmoja linaathiri jamii yote (kama vile Akani katika Yoshua 7). Kutokutii kwa Adamu na Hawa kulileteleza hukumu ya Mungu kwa uumbaji wote (kama vile Mwa 3). Uumbaji wote umeathiriwa na matokeo ya uasi wa Adamu (kama vile 8:18-25). Ulimwengu sio mmoja. Wanadamu sio wamoja. Kifo kikawa ndio mwisho wa maisha yote duniani (kama vile Mwa 2:5). Huu sio ulimwengu ule alioukusudia uwe!

Katika maana hii ya pamoja, tendo moja la utii wa Yesu, Kalvari, lilileta matokeo ya (1) enzi mpya (2) watu wapya (3) Agano jipya. Aina ya uwasilishi wa thiolojia hii inaitwa taipolojia ya “Adamu- Kristo” (kama vile Flp. 2:6). Yesu ni Adamu wa pili. Ndiye mwanzo mpya wa mataifa yote yaliyoanguka.

◙**“Alifanywa kuwa wa haki”** Tazama Mada Maalum katika 1:17.

**5:20**

**NASB "na sheria ikaja ili makosa yaongezeke"**
**NKJV "hata hivyo sheria ikaingia iliuhalifu uongezeke"**
**NRSV "lakini sheria ikaja na matokeo na kasoro zikazidi"**
**TEV "sheria ikatungwa ili kuongeza matendo maovu"**
**NJB "sheria ilipokuja ilikuwa kuzidisha fursa ya kuanguka**"

Kusudi la sheria ilikuwa sio kuokoa watu bali kuonyesha hitaji na msaidizi kwa mwanadamu aliyaeanguka (kama vile Efe 2:1-3) na hivyo basi kuwaleta kwa Kristo (kama vile 3:20; 4:15; 7:5; Gal 3:19,23-26). Sheria ni nzuri lakini binadamu ni mwenye dhambi (kama vile Rum. 7).

◙**"Neema ikaongezeka zaidi"** Huu ulikuwa msukumo muhimu wa Paulo katika sehemu hii. Dhambi inatisha na inasambaa, lakini neema ni nyingi na huzidi madhara ya dhambi. Hii ilikuwa njia ya kuwapa matumaini waumini wa makanisa machanga ya karne ya kwanza. Walikuwa washindi katika Kristo (kama vile 5:9,11; 8:31-39; 1 Yn. 5:4). Hii siyo kibali cha kufanya dhambi zaidi. Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya maneno yaliungana naya *"Huper"* katika 1:30.Tazama Mada Maalum juu ya uhusiano wa neno "kuzidi" lilivyotumika katika mst. 15 na katika Rum 15:13.

**5:21** Yote mawili "dhambi" na "neema" yamefanana kuwa kama wafalme. Dhambi ilitawala kwa nguvu ya kifo cha ulimwengu wote (mst. 14, 17). Neema inatawala kupitia katika haki ya kazi ya Yesu Kristo aliyokwisha kuimaliza na kwa imani binafsi ya mwamini na ukubarifu wa kutubu kwenye injili.Kama watu wapya wa Mungu, kama mwili wa Kristo, wakristo pia watatawala na Christo (kama vile 5:17; 2 Tim. 2:12; Muh. 22:5). Hii inaweza kuonekana kama utawala wa dunia au milenia (kama vile Muh. 5:9-10; 20). Biblia pia inazungumza kwa ukweli ule ule kwa kutetea kuwa ufalme umetolewa kwa watakatifu (kama vile Mt. 5:3, 10; Lk. 12:32; Efe. 2:5-6). Tazama Mada Maalum: kutawaala katika ufalme wa Mungu katika 5:17,18.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Fasiri "haki" ya Mungu.
2. Ipi ni tofauti ya kithiolojia kati ya "mahala pa utakaso na umiliki wa moja kwa moja?"
3. Je tunaokolewa kwa neena au imani (kama vile Efe. 2:8-9)?
4. Kwa nini Wakristo wanateseka?
5. Je, <u>tumeokolewa</u>, <u>tunaendelea kuokolewa</u>, au <u>tutaokolewa</u>?
6. Sisi ni wenye dhambi kwa kuwa tunatenda dhambi au tunatenda dhambi kwa kuwa sisi ni wenye dhambi?
7. Ni vipi maneno haya "kuhalalishwa,", "kuokolewa" na "kupatanishwa" yanahusiana katika sura hii?
8. Kwa nini Mungu ananiwajibisha kwa dhambi iliyotendwa na mwingine aliyeishi maelfu ya miaka iliyopita (mist. 12-21)
9. Kwa nini kila mtu alikufa katika kipindi kati ya Adamu na Musa kama dhambi haikuhesabiwa katika kipindi hiki?
10. Je, maneno "wote" na "wengi"yanafanana? (mist. 18-19; Isa. 53:6, 11-12)

# WARUMI 6

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mfu katika dhambi, lakini mzima katika kristo | Mfu katika dhambi, mzima kwa Mungu | Kufa na kufufuka na Kristo | Mfu kwa dhambi lakini mzima katika Kristo | Ubatizo |
| 6:1-11 | 6:1-14 | 6:1-4 | 6:1-4 | 6:1-7 |
| | | 6:5-11 | 6:5-11 | |
| | | | | 6:8-11 |
| | | | | Utakatifu, sio Dhambi kuwa Bwana |
| 6:12-14 | | 6:12-14 | 6:12-14 | 6:12-14 |
| Watumwa wa haki | Kutoka utumwa Wa dhambi kuwa Utumwa wa Mungu | Utumwa aina Mbili | Watumwa wa haki | Mkristo ameondolewa Kutoka Utumwa wa Dhambi |
| 6:15-23 | 6:15-23 | 6:15-19 | 6:15-19 | 6:15:19 |
| | | | | Mshahara wa dhambi na Mshahara wa kusimama Imara |
| | | 6:20-25 | 6:20-23 | 6:20-23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura 6:1-8:39 zinaunda wazo moja (wazo la kiuandishi) ambalo linashugulika na uhusiano wa Mkristo na dhambi (yaani utakaso ). Hili ni suala nyeti sana kwa sababu injili inatokana na neema ya bure isiyostahiri toka kwa Mungu kupitia Kristo (3:21-5:21) kwa hiyo, vipi dhambi inamuathiri muumini? Sura ya sita 6

imetokana na maswali mawili yenye utata, mst 1 na 15. Msitari wa wa kwanza unahusiana na 5:20 wakati 15 inahusiana na 6:14.Wakwanza unahusiana na dhambi kama stadi ya maisha (NJEO YA WAKATI ULIOPO). Wa pili, unahusiana na matendo ya dhambi ya mtu binafsi. (NJEO YA WAKATI TIMILIFU). Ni wazi pia kwamba mistari ya 1-14 inahusika na uhuru wa muumini kutoka katika utawala wa dhambi, wakati mist ya 15-23 inashughulika na uhuru wa muumini wa kumtumikia Mungu, kama awali walivyotumikia dhambi kikamilifu, kwa moyo wao wote.

B. Utakaso ni yote mawili (Taz. Mada maalumu katika 6:4)
   1. Nafasi (iliyoingia kama uthibitisho kwenye wokovu, 3:21-5:21)
   2. Kuendelea kufanana na Kristo
      (a) 6:1-8:39 inaelezea ukweli huu kithiolojia.
      (b) 12:1-15:13 inaelezea kivitendo (Taz. Mada Maalumu katika 6:4)

C. Daima watoa maoni sharti watenganishe somo la uthibitisho na utakaso wa mahali ili kusaidia kuleta maana ya maneno haya kibiblia. Kusema kweli ni matendo yanayofuatana ya neema (ya mahali, 1wakor.1:30;6:11). Utendaji kazi wa yote ni sawa. Neema ya Mungu ilidhihirishwa katika maisha ya Yesu, kifo na ufufuo/kupaa mbinguni ambavyo vinapokelewa kwa imani (kama vile Efe.2:8-9).

D. Surah ii inafundisha ukomavu kamili (kutokuwa na dhambi kma vile Efe.2:8-9. Watoto katika Kristo. Sura ya 7 na 1 Yoh.1:8-2:1 inaonyesha ukweli wa waumini kuendelea kuishi katika maisha ya dhambi. Mgongano mkubwa juu ya maoni ya Paulo kuhusu msamaha (yaani uthibitisho kwa neema kupitia imani) ilihusiana na suala la maadili. Wayahudi walitaka kuhakikisha kuishi maisha ya Mungu, kwa kutaka waliobadilika waendane na sheria za Musa. Lazima ikubalike kuwa wengine walifanya hivyo na wakatumia maoni ya Paulo kama leseni ya kutenda dhambi (kama vile mst.1,15;IIPetr.3:15-16). Paulo aliamini kuwa , roho asiyeishi na kanuni za nje zingezaa wafuasi ambao wanafanana na Kristo kwa maisha ya Mungu.kusema kweli, hii ni tofauti na patano la kale (kama vile kumb.27-28) na patano jipya (kama vile Yer.31:31-34; Ezek.36:26-27).

E. Ubatizo ni kielelezo cha nje cha ukweli wa Roho kwa udhihilisho/utakaso. Katika warumi, mafundisho pacha ya utakaso wa mahali na utakaso wa mazoea (kufanana na Yesu) yote yanashinikiza. kuzikwa pamoja naye (mst.4) inenda sambamba na “kusurubishwa pamoja naye” (mst.6)

F. Miongozo ya kushinda majaribu na dhambi katika maisha ya Mkristo ni;-
   1. Kujua wewe ni nani katika Kristo. Kujua amekufanyia nini. Uko huru kutokana na dhambi! umeifia dhambi!
   2. Tabiri/hesabu nafasi yako katika kristo katika mazingira ya maisha yako ya kila siku.
   3. Hatuko peke yetu!. Lazima tumtumikie/tumtii Bwana wetu.Tunatumikia/tunatii mbali na shukrani na upendo kwa yule aliyetupenda kwanza na akajitoa maisha yake kwa ajili yetu.
   4. Maisha ya Mkristo ni maisha ya wasiwasi. Ni kama wokovu, ni zawadi toka kwa Mungu, katika Kristo. Anaianzisha na kuipa nguvu. Lazima tuikubali kwa toba na imani, tangu mwanzo wa siku zote.
   5. Usicheze na dhambi. Itambue kwa jinsi ilivyo. Igeukie mbali, ikimbie. Usijiweke katika maeneo ya majaribu.
   6. Dhambi kwa muumini kama ulevi uliopindukia uliomwathiri mtu (unaoweza kuvunjwa, lakini inahitaji uelewa wa injili, uwepo wa roho, muda,jitihada na uamuzi wa dhati.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:1-7**
**[1]Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? [2]hasa! Sisi tusioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? [3]Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? [4]Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. [5]Kwa maana kama tulivyounganika naya katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; [6]tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisurubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; [7]kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi.**

**6:1**
**NASB "Tuendelee ketenda dhambi ili kwamba neema iongezeke"**
**NKJV "Tuendelee kuwa katika dhambi ili neema iwe nyingi?"**
**NRSV "Kwamba twapaswa kuendelea kuishi katika dhambi hivyo kwamba neema ya Mungu iongezeke?"**
**TEV "Kwahiyo iwe kwamba yatupasa tubakie ndani ya dhambi ili kuifanya neema ipate kuongezeka kiwango"**
**NJB "Ni kweli tubaki katika dhambi ya kwamba kuifanya neema iwe na nafasi kubwa"**

Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO. Hasa inauliza tu swali, je! Wakristo "Washikamane" au "Wakumbatie" dhambi? Swali hili linarudi nyuma hadi kwenye 5:20. Paulo alitumia lugha ya kukemea ili kushughulika na matumizi mabaya ya neema .Neema ya Mungu na huruma hazimaanishi kutoa leseni ya maisha ya uasi (kama vile 1Yoh.3:6,9;5:18)

Injili ya Paulo ya wokovu wa bure kama zawadi ya neema ya Mungu kupitia kwa Kristo (kama vile 3:24; 5:15, 17; 6:23) ilizua maswali mengi kuhusu stadi ya maisha ya haki. Ni kwa vipi zawadi huru inaweza leta msimamo wa kimaadili? Udhihilisho na utakaso kamwe visitenganishwe (kama vile Mt.7:24-27; Luk.8:21; 11:28; Yoh. 13:17, Warumi 2:13; Yakobo 1:22-25; 2:14-26).

Katika kipengele hiki hebu ninukuu: F.F Bruce katika *Paulo*: *Apostle of the Heart Set Free*,

> "Ubatizo wa wakristo, uliundwa mpaka kati ya maisha yao ya zamani yasiyobadilika na maisha mapya katika Kristo. Uliweka kifo kwa mfumo wa maisha yao ya zamani hivyo kwamba kwa Mkristo aliyebatizwa, kuendelea kuwa kwenye dhambi ni upumbavu usio kifani, kama vile mtumwa aliyekombolewa kuendelea kuishi chini ya amri ya aliyekuwa Bwana wake (kama vile Warumi 6:1-4,15-23) au mjane kubakia akiwajibika kwa sheria za mume wake" (Uk. 281-82, kama vile Warumi 7:10-6).

Katika kitabu cha James S.stewart, *A Man in Christ*, anaandika:

> "The *locus classicus* Kwa upande huu wa wazo la mtume lingepatikana katika warumi 6. Pale Paulo, kwa shauku kubwa na nguvu, anajifikilia ndani ya Roho na nafisini mwake kuwa kuungana na Yesu katika kifo chake ina maana kwa muumini ni hatua ya kuvunja na kuachana kabisa na dhambi" (Uk 187-88).

**6:2 "Naomba isitokee/Isiwe"** Hii ni moja ya muundo adimu wa UCHAGUZI ambao ulikuwa ni DHAMIRA au NAMNA uliotumika kuakia heri au kuombea. Ilikuwa ni namna ya Paulo (nahau ya kiebrania) ya kumjibu mpinzani wa kinadharia. Ilionyesha jinsi Paulo alivyoshtuka na hofu kwa kutoamini hali ya wanadamu kutoelewa na kutukana neema (kama vile 3:4,6).

◙**"Sisi tuliokufa katika dhambi"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ikimaanisha kwamba tumekufa dhambi ya "HALI YA UMOJA" imetumika mara nyingi katika Sura hii. Ina maana kurejerea "dhambi ya asili" iliyorithiwa kutoka kwa Adamu (kama vile warumi 5:12-21; 1wakor.15:21-22) Paulo daima

anatumia dhana ya kifo kama njia mbadala ya kuonyesha uhusiano mpya nwa waumini na Yesu. Hawapo tena katika wazoefu wa dhambi.

◙**"Bado tunaishi ndani yake"** Hii hasa ina maana ya "mwendo." Stiari hii ilitumika kukandamiza stadi yetu ya maisha ya imani (kama vile Efe. 4:1;5:2,15) au stadi ya maisha ya dhambi (kama vile mst 4; Efe. 4:17). Waumini hawawezi kuwa na furaha katika dhambi.

**6:3-4 "Tumebatizwa…….tumezikwa"** Hizi zote ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Namna hii ya kisarufi inasistizia kitendo kilichokwisha fanyika toka kwa mtu wan je, hapa ambaye ni Roho, wako sambamba katika mazingira haya.

## MADA MAALUM: UBATIZO

I. Ubatizo katika maisha ya Kiyahudi

II. Ubatizo ulikuwa utaratibu wa kawaida miongoni mwa Wayahudi wa karne ya kwanza na ya pili.

1. maandalizi ya kuabudu hekaluni (yaani, utaratibu wa kujitakasa)
2. ubatizo wa kujibatiza mwenyewe kwa kubadili dini
   Ikiwa mtu aikuwa na hisori ya kuwa mtu wa Mataifa ilimlazimu kuwa mtoto kamili wa Israeli, huyu ilimpasa kutimiza majukumu matatu:
   a. tohara, ikiwa ni mwanamume
   b. kujibatiza mwenyewe kwa kuzama majini, katika uwepo wa mashahidi watatu
   c. dhabihu ndani ya Hekalu
3. Tendo la utakaso (kama vile Mambo ya Walawi 15)
   Makundi ya kimadhehebu ya karne ya kwanza ya ki- Palestina, kama vile Essene, kwa uwazi kabisa ubatizo lilikuwa jambo la kawaida, zoezi lililorudiwa rudiwa. Hata hivyo, kuipa kipaumbele dini ya Kiyahudi, Ubatizo wa Yohana wa toba ungeweza kuwa wa kumnyenyekeza mtoto wa asili kuyafanya Mataifa kuzikubali taratibu hizi.
   1. baadhi ya vigezo vya kitabu cha Agano la kale vinavyoweza kunukuliwa vinaweza kuonekana kupitia sikuu ya kutawazwa
   2. Kama taratibu zilivyofanywa na makuhani kwa ukawaida (kama vile Kutoka 19:10; Mambo ya Walawi 16)

   Lazima itambuliwe kwamba batizo nyingine zote katika karne ya kwanza ya utamaduni wa Kiyahudi zilikuwa ni za kujiendesha zenyewe. Wito pekee wa Yohana Mbatizaji kwa ajili ya ubatizo ndiyo uliomhusisha yeye kama mtathimini (kama vile Mt. 3:7-12) na mwendeshaji wa tendo hili la toba (kama vile Mt. 3:6).

III. Ubatizo ndani ya Kanisa

A. Sababu za Kithiolojia
   1. msamaha wa dhambi – ya Mitume 2:38; 22:16
   2. upokeaji wa Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 2:38 (Matendo ya Mitume 10:44-48)
   3. ushirika pamoja na Kristo – Gal. 3:26-27
   4. ushirika ndani ya kanisa – 1 Kor. 12:13
   5. dalili za kurudi kwa roho – 1 Pet. 3:20-21
   6. dalili za kifo cha kiroho na ufufuo – Rum. 6:1-5

B. Ubatizo ulikuwa fursa ya kanisa la kale kwa ajili ya ukiri wa umati wa watu (au ungamo). Huuu haukuwa/si kwa maana ya wokovu, bali tukio la ukili kwa maneno ya imani (yaani, bila shaka, "Yesu ni Bwana"). Kumbuka kanisa la kale halikuwa na majengo na hawa walikutana majumbani au walikutana katika maeneo ya maficho mara kwa mara kwa sababu ya kuteswa.

C. Watoa maoni wengi wamekuwa wakidai kuwa 1 Petro ni hotuba ya kiubatizo. Ijapokuwa hili linawezekana, huu si uchaguzi wa kipekee. Ni kweli kuwa Petro mara nyingi alitumia ubatizo kama tendo muhimu la imani

(kama vile Matendo ya Mitume 2:38, 41;10:47). Hata hivyo, hili lilikuwa/ ni tukio la kisakramenti, lakini tukio la imani, linaashiria mauti kuzikwa,na ufufuo kama mwamini atambuavyo kwa uzoefu wa mara kwa mara (kama vile Rum. 6:7-9; Kol. 2:12). Tendo ni la kiishara, si la kisakramenti; tendo ni tukio la ukiri, si kwa maana ya wokovu.

IV. Ubatizo na Toba katika Matendo ya Mitume 2:38

Curtis Vaughan, Kitabu cha Matendo ya Mitume kina tanbihi inayoshawishi katika ukr. 28 unahusiana na Matendo ya Mitume 2:38.

"Neno la Kiyunani la 'kubatizwa' ni nafsi ya tatu shurutishi; neno la 'kutubu,'ni nafsi ya pili shurutishi. Hii inabadilika moja kwa moja kutoka nafsi ya pili shurutishi hadi nafsi ya tatu ya chini ya moja kwa moja ya neno 'kubatizwa' linalomaanisha kwamba dai la msingi la Petro ni kwa ajili ya toba."

Hili linaufuata ule msisitizo wa Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:2) na Yesu (kama vile Mt. 4:17). Toba inaonekana kuwa ufunguzi wa kiroho na ubatizo uko nje ya sura ya madiliko hili la kiroho. Kitabu cha Agano Jipya hakifahamu lolote juu ya waamini wasiobatizwa! Kwa kanisa la kale ubatizo ulikuwa ungamo la imani ya wengi. Hili ni tukio la ungamo la imani ya walio wengi katika Kristo, si kwa maana ya wokovu! Inahitajika kukumbuka kwamba ubatizo hautajwi ndani ya hotuba ya pili ya Petro, ijapokuwa toba ipo (kama vile Matendo ya Mitume 3:19; Luka 24:17). Ubatizo ulikuwa mfano uliowekwa na Yesu (kama vile Mt. 3:13-18). Ubatizo uliamriwa na Yesu (kama vile Mt. 28:19). Swali la sasa la umuhimu wa ubatizo kwa ajili ya wokovu hauelezwi katika kitabu cha Agano Jipya; waamini wote wanatarajiwa kubatizwa. Hata hivyo, mtu lazima pia ajilinde dhidi ya sifa ya kisakramenti! Wokovu ni suala la imani, si sehemu ya haki, haki ya maneno, haki ya suala la utaratibu!

◙**"Katika Kristo Yesu"** Matumizi ya *eis* (ndani) inaendana na agizo kuu la Mathayo 28:19 ambapo waumini wapya wanabatizwa *eis* (kwa) jina la Baba na la Mwana na la Roho mtakatifu. KIVUMISHI pia kinaonyesha kuelezea muumini aliyebatizwa na Roho mtakatifu katika mwili wa Yesu katika 1 Kor.12:13. *Eis* katika mazingira haya linahusiana sawa na *en* (katika Kristo) kwenye mst.11, ambayo ni njia ya upendeleo wa Paulo katika kuelezea waumini. Ni MZUNGUKO WA MAHALI. Waumini wanaishi na kutembea na wamo ndani ya Kristo. Vihusishi hivi vinaonyesha hatua ya muungano, mzunguko huu wa ushirika,uhusiano wa mzabibu na tawi.Waumini wanabainiwa na kuungana na Kristo katika kifo chake.(kama vile 6;8:17), katika ufufuo wake ( kama vile mst. 5), katika utumishi wake wa utiifu kwa Mungu na katika ufalme wake.

◙ **"ndani ya kifo chake……. tumezikwa pamoja nae"** Ubatizo kwa kuzamishwa unadhihirisha kifo na kuzikwa (kama vile mst.5 na Kol.2:12). Yesu alitumia ubatizo kama mbadala wa kifo chake mwenyewe (kama vile Marko 10:38-39; Luk.12:50). Mkazo hapa sio imani ya ubatizo, Bali ni mahusiano mapya ya mkristo na kifo na maziko ya Yesu. Waumini wanatambulika na Yesu kwa ubatizo, tabia yake, sadaka yake na utume wake. Dhambi haina nguvu kwa waumini.

**6:4 "Tumezikwa naye kupitia ubatizo katika kifo"** Katika sura hii, kama ilivyo kawaida ya uandishi wa Paulo, anatumia *sun* (na) nyingi kwa muungano (mf.tatu katika Efe.2:5-6)

1. *Sun +thaptō* = kuzikwa naye, mst. 4; Wakol. 2:12; pia nukuu mst.8
2. *Sun +phuō* = *k*upandwa naye pamoja, mst. 5
3. *Sun + stauroō = kusulibishwa naye, mst. Wagalatia 2:20*
4. *Sun + zaō* = kuishi pamoja naye, mst.8; II Tim. 2: 11 ( pia kuna kufa naye na kutawala naye.

◙ **"kwa hiyo nasi pia tutatembea katika upya wa maisha"** Hii ni KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE UTEGEMEZI. Matarajio ya matokeo ya wokovu ni utakaso. Kwa kuwa waamini wamepokea neema ya Mungu kupita Kristo na Roho ameishi ndani yao, maisha yao lazima yawe tofauti. Miasha yetu mapya (*zoē*) hayatuletei wokovu, bali ni

matokeo ya wokovu ( mist. 16, 19, 8: 4, 13:13; 14:15; na Waef. 1:4 ; 2:8-9,10; Yak. 2: 14-26). Hii sio /ama swali, imani au kazi, lakini kuna mpangilio uliofuatana.

## MADA MAALUMU: UTAKASO KATIKA AGANO JIPYA

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kutomtia hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

| Mwitikio wa Awali | Ufanano na Kristo Endelevu |
|---|---|
| Matendo 26:18 | Warumi 6:19 |
| Warumi 15:16 | 2 Kor. 7:1 |
| 1 Wakorintho 1:2-3; 6:11 | Waefeso 1:4; 2:10 |
| 2 Wathesalonike 2:13 | 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2 |
| Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12 | 1 Timotheo 2:15 |
| 2 Petro 1:2 | 2 Timotheo 2:21 |
| | 1 Petro 1:15-16 |
| | Waebrania 12:14 |

◙ "**upya wa maisha"** Huu ni "upya" wa kiwango, na sio upya wa katika muda. Umetumika kwa njia nyingi katika Agano Jipya kuzungumzia badiliko kubwa analoleta Masiha. Ni enzi mpya. Isaya 40-66.

1. Agano jipya, Luka 22:20; 1 Kor. 11:25; 2 Kor. 3:6; Ebr. 8:8, 13; 9:15
2. amri mpya, Yohana 13:14; I Yohana 2:7,8; 2 Yn. mst. 5
3. Uumbaji mpya, II Kor. 5:17, Gal. 6:15
4. upya wa maisha,Rum.6:4
5. upya wa Roho ,Rum.7:6
6. mtu mpya, Efe.2:15;4:24
7. Mbingu mpya na dunia, 2 Pet. 3;13; Ufu.21:1 (kama vile Isa.66:22)
8. Jina jipya, Ufu.2:17; 3:12 (kama vile Isa. 62:2)
9. Wimbo mpya, Muh. 5:9; 14:3 (kama vile Isa 42:10)

◙ "**Kristo aliinuliwa"** katika mazingira haya, ukubarifu wa Baba, na kuidhinishwa kwa maneno na kazi ya mwanae yote hayo yanaelezwa katika matukio mawili makuu:

1. Kufufuka kwa Yesu kutoka katika wafu
2. Kupaa kwa Yesu mbinguni na kukaa mkono wa kulia wa Baba yake

Wote watatu katika utatu walihusika katika kumwinua Yesu kutoka katika ulimwengu wa wafu. Tazama nukuu kamili katika mst 9 na 8:11

◙ **"utukufu wa Baba"** kwa neno "utukufu" tazama mada maalumu katika 3:23. Kwa neno "Baba" tazama mada maalumu katika 1:7

**6:5: "kama"** Hii ni SENTESI NYUMBUFU DARAJA LA KWANZA ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa malengo yake ya kiuandishi. Paulo alichukulia kuwa viongozi wake walikuwa pia waumini.

◙ **"tumeungana naye"** Ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU ambao unaweza tafasiliwa "tumeungana na tutaendelea kuungana" au "tunapandwa naye na tutaendelea kupandwa naye". Ukweli huu kitheolojia unafananishwa na "kuunganishwa" katika Yohana 15. Kama waamini wanabainishwa na kifo cha Yesu (kama vile Gal 2:19-20; Kol 2:20; 3:3-5, kitheolojia sharti pia wabainishwe kwa kufufuka kwake (kama vile mst 10).

Maneno haya mbadala ya ubatizo kama kifo yalikusudia kuonyesha:

1. Tumekufa kwa maisha ya zamani, patano la kale
2. Tuko hai katika Roho, patano jipya

Ubatizo wa Kikristo, kwa hiyo, sio kama ule ubatizo wa Yohana mbatizaji, ambaye alikuwa mtume wa mwisho katika Agano la Kale. Ubatizo ulikuwa ni fursa ya mwanzo ya kanisa kwa muumini mpya kuonyesha imani yake hadharani. Kanuni ya ubatizo wa hapo mwanzo, uliosemwa kwa kurudiwa na waumini ulikuwa "naamini Yesu ni Bwana" (kama vile Rum 10:9-13). Tangazo hili katika hadhara, lilikuwa ni tendo rasmi la kitambiko kwa kile kilichotokea huko nyuma katika uzoefu wa maisha. Ubatizo haukuwa <u>chombo</u> cha kupata msamaha, wokovu au ujio wa Roho, bali ilikuwa tu <u>tukio</u> la hadhara la mtu kukiri imani yake (kama vile Mdo 2:28). Hata hivyo halikuwa uchaguzi ufanye au la. Yesu aliliamuru (Mdo. 28:19-20) na akaonyesha mfano (kama vile Mt 3; Marko 1; Luka 3) na ikawa ni sehemu ya mafundisho ya mitume na taratibu za matendo.

**6:6**
**NASB "kwa kujua hili, kwa nafsi zetu za kale ulisurubishwa naye"**
**NKJV "kwa kujua hili, kwamba mtu wetu wa kale ulisurubishwa naye"**
**NRSV "Tunajua kwamba, nafsi zetu za zamani zilisurubishwa naye"`**
**TEV "Na tunajua hili, utu wetu wa kale umeuawa pamoja na Kristo msalabani"**
**NJB "Lazima tutambue kuwa, nafsi zetu za mwanzo zimeangikwa naye"**

Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU likimaanisha utu wetu wa kale moja kwa moja umesurubishwa pamoja na Roho. IRABU TENDEWA inaonyesha uwakala wa Kiungu. Ukweli huu ni nyeti sana kwa maisha ya ushindi wa Mkisto. Waumini lazima watambue kuwa uhusiano wao mpya na dhambi (kama vile Gal 2:20; 6:14). Nafsi ya zamani ya mwanadamu iliyoanguka (asili ya Adamu) imekufa na Kristo (kama vile mst 7; Efe 4:22 na Kol 3:9). Kama waumini sasa tuna chaguo kuhusu dhambi kama Adamu alivyofanya mwanzo.

◙
**NASB, NKJV "Kwamba mwili wetu wa dhambi ungeweza kuachwa"**
**NRSV "Hivyo kwamba, mwili wa dhambi ungeweza kuharibiwa"**
**TEV "Ili kwamba, nguvu ya nafsi ya dhambi ingeharibiwa"**
**NJB "Kuharibu mwili wenye dhambi"**

Paulo alitumia neno "mwili" (*soma*) ikiwa na vifungu JINSI vingi:

1. Mwili (wa) dhambi, Rum 6:6
2. Mwili wa kifo hiki, Rum 7:24
3. Mwili wa nyama, Kol 2:11

Paulo anazungumuzia maisha ya kimwili ya enzi hii ya dhambi na uasi. Mwili mpya wa ufufuo wa Yesu, ni mwili wa enzi mpya ya haki (kama vile 2 Kor 5:17). Umbile sio tatizo (mwana falsafa wa Kiyunani) bali dhambi na uasi. Mwili sio mwovu. Ukristo unathibitisha imani katika mwili wa umilele (kama vile 1 Kor 15). Ingawa, mwili halisi ni uwanja wa vita vya majaribu na nafsi.

Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU YENYE UTEGEMEZI. Kifungu "kutupiliwa mbali" lina maana kwamba "kufanya kisitende kazi" "kufanywa kisiwe na uwezo" au "kufanywa kisizae" <u>sio</u> "kuharibiwa". Hili lilikuwa neno lililopendelewa sana na Paulo, alilotumia zaidi ya mara 25 (taz. Mada maalum: Batili na Utupu (*katargeō)* katika 3:3. Mwili wetu huu hauna upendeleo, lakini pia ni uwanja wa vita kwa mugongano wa kiroho unaoendelea (kama vile mst 12-13; 5:12-21; 12:1-2)

**6:7 "yeye aliyekufa, amewekwa huru kutokadhambini"** Ni KAULI TENDAJI YAWAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ENDELEVU na KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU ikiwa na maana kuwa "Yeye aliyekufa amekuwa na anaendelea kuwa huru toka dhambini". Kwa vile waumini ni uumbaji mpya katika Kristo, wamekuwa huru na wataendelea kuwa huru kutokana na utumwa wa dhambi uliorithiwa binafsi kutokana na anguko la Adamu (kama vile 7:1-6).

Neno la Kiyunani lililotafasiliwa hapa kama "kuwekwa huru" ni neno linalotafasiliwa katika sura ya ufunguzi kama "kudhihilishwa" (ASV). Katika mazingira haya "kuwekwa huru" (NKJV, NRSV) inaleta maana zaidi (ni sawa na matumizi yake katika Mdo. 13:39). Kumbuka, mazingira yanaamua maana ya neno, na sio kamusi au jinsi neno la awali lilivyofasiliwa kitaalamu. Maneno yana maana tu katika sentesi, na sentesi zina maana tu katika aya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:8-11**
**8 Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; 9 tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. 10 Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu. 11 Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi, na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.**

**6:8 "Kama"** Hii ni SENTESI DARAJA LA KWANZA YENYE MASHARTI ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kifasihi. Ubatizo wa muumini kimtazamo unatoa mfano wa kifo cha mtu na Kristo.

◙ "**Tutaishi pia na yeye"** katika mazingira haya yanadai mtazamo wa neno "hapa na sasa" (kama vile 1 Yn. 1:7) na sio muundo unaokuja mbeleni. Mst wa 5 unazungumzia ushiriki wa mauti na Kristo, wakati mst 8 unazungumzia ushiriki wa maisha yake. Huu ni mvutano asili ule ule katika dhana ya Biblia ya ufalme wa Mungu. Yote hapa na sasa, bado wakati ujao. Neema ya burelazima ilete kujizuiya mwenyewe, na sio ruhusa.

**6:9 "Akiwa ameinuliwa kutoka katika wafu"** Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA (angalia 6:4, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU). Agano Jipya linakazia kuwa nafsi hizi tatu za Utatu zilihusika kikamilifu
katika ufufuo wa Yesu.

1. Roho (kama vile Rum 8:11)
2. Mwana (kama vile Yn.2:19-22; 10:17-18)
3. Na mara nyingi Baba (kama vile Mdo. 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum 6:4,9)

Matendo ya Baba yalikuwa ya uthibitisho wa kukubalika kwa maisha ya Yesu, kifo na mafundisho. Hili lilikuwa jambo kubwa kabisa katika mafundisho ya awali ya mitume. Tazama mada maalumu: Mafundisho ya Kanisa la Kwanza "Kerygma" katika 1:2

◙
**NASB "Kifo sio tena mwamuzi juu yake"**
**NKJV "Kifo hakina himaya tena juu yake"**
**TEV "Kifo hakitatawala tena juu yake"**
**NJB "Kifo hakina nguvu juu yake tena"**

Kitenzi *kurieuō* kinatokana na neno *kurios* (yaani Bwana) likiwa na maana "mmiliki", "mwamuzi" "mume" au "Bwana". Yesu sasa ni Bwana juu ya kifo (kama vile Muh. 1:18). Yesu ndilo tunda la kwanza la ufufuo. Pamekuwepo watu:

1. Waliotwaliwa mbinguni wakiwa hai (yaani, imetafasiliwa, Enock na Eliya)

2. Waliorejeshwa katika uzima wa mwili (yaani, kupata fahamu upya)

Yesu pekee ndiye aliyefufuliwa katika mwili wa enzi mpya. Yesu ndiye wa kwanza kuvunja nguvu za mauti (kama vile 1Kor 15).

**6:10 "Kwa kifo alichokufa, alikufa kwa ajili ya dhambi"** Yesu aliishi katika ulimwengu wa dhambi, na ingawa yeye binafsi hakutenda dhambi, ulimwengu wenye dhambi ulimsurubisha msalabani (kama vile Ebr 10:10). Kifo mbadala alichokufa Yesu badala ya mwanadamu kilifuta mahitaji ya sheria na yote yanayoendana nayo juu ya watu (kama vile Gal 3:13; Kol 2:13-14)

◙ "**Mara moja kwa wote"** Katika mazingira haya, Paulo anasisitiza juu ya kusulubishwa kwa Yesu. Kifo chake cha mara moja tu kwa dhambi kimeathiri kifo cha wafuasi wake kwa dhambi. Kitabu cha Waebrania pia kinasisitizia hatma ya kifo cha mara moja cha dhabihu kwa watu wengine. Wokovu huu wa mara moja na msamaha umekamilishwa milele (kama vile "mara moja" [*ephapax]* 7:27; 9:12; 10:10 na "mara moja kwa wote" [*hapax]*, 6:4; 9:7,26,27,28; 10:2; 12:26,27). Huu ni urudiaji, utimizaji, uthibitisho wa dhabihu.

◙**"lakini maisha anayoyaishi, anamwishia Mungu"** Semi hizi mbili TIMILIFU katika mistari ya 10a zinasigishana na kauli mbili zile KAULI TENDAJI ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPO za mst 10b. Waumini walikufa na Kristo, waumini wanaishi kwa ajili ya Mungu, kupitia kwa Kristo (kama vile Gal. 2:19-20). Lengo la injili siyo tu msamaha (udhihilisho) bali, huduma kwa Mungu (utakaso). Waumini wanaokolewa ili wahudumu.

**6:11 "hata hivyo jifikirieni ninyi wenyewe kuwa mmekufa katika dhambi"** Ni KITENZI CHA KATI SHURUTISHI (chenye ushahidi). Hii ni amri ya mazoea, inayoendelea kwa waumini.Uelewa wa wakristo kuhusu kazi ya Kristo kwa niaba yao ni nyeti kwa maisha ya kila siku. Neno "fikiria" (kama vile 4:4, 9) lilikuwa ni neno la kuwajibisha lililokuwa linamaanisha "ongeza kwa uangalifu," na kisha tenda kwa uelewa huo. Mistari ya 1-11, inataarifu mtu nafasi yake katika Kristo (utakaso wa mahali), wakati 12-13 ilisisitiza kutembea ndani yake (utakaso unaoendelea). Tazama Mada Maalum mst. 4.

**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB** **"Kristo Yesu"**
**NKJV** **"Kristo Yesu, Bwana wetu"**

Soma fupi linapatikana katika MSS $P^{46}$, A,B,D,F,G. UBS$^4$ inatoa kadirio la alama A (hakika). Kifungu kilichopanuliwa ni cha awali (MSS $P^{94}$, C), lakini bila shaka kiliongezwa na wandishi kutoka mst.23. Kama ilivyo wingi wa ukubwa wa tofauti za maandiko, linaleta tofauti ndogo ya maana ya maandishi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6:12-14**

**[12]Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; [13]Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki. [14]kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamuwi chini ya sheria, bali chini ya neema.**

**6:12 "kwa hiyo, usiruhusu dhambi itawale katika mwili wako unaokufa"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, kikimaanisha kusitisha kitendo kilichoko kwenye mchakato. Neno "kutawala" linahusiana na 5:17-21 na 6:23. Paulo anafafanusha watu dhana kadhaa za kithiolojia.

1. kifo kilitawala kama mfalme (kama vile 5:14,17; 6:23).
2. neema ilitawala kama mfalme (kama vile 5:21)
3. dhambi ilitawala kama mfalme (kama vile 6:12,14).

Swali la msingi ni kwamba, nani anatawala katika maisha yako? Muumini ana uwezo katika Kristo kuchagua! Mkasa mkubwa kwa mtu binafsi, kanisa la mahali pale pale, na ufalme wa mbinguni ni pale ambapo waumini wanachagua nafsi zao na dhambi, hata pale wanapodai neema! Tazama Mada Maalum "kutawala katika Ufalme wa Mungu" katika 5:17 na 18.

**6:13 "usiendelee kutoa viungo vyako vya mwili katika dhambi"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, kikiwa na maana ya kuzuia kitendo ambacho tayari kilikuwa kwenye mchakato. Hii inaonesha umuhimu wa dhambi kuendelea kuwepo ndani ya maisha ya waumini (kama vile 7:1na kuendelea; Yohana 1:8-2:1). Lakini hitaji la dhambi limeondolewa katika uhusiano mpya wa waumini na Kristo, mist 1-11.

◙**"kama vyombo"** Neno (*hoplon*) linamaanisha "silaha za askari" (kama vile 13:12; Yohana 18:3; 1 Kor 6:7; 10:4). Miili yetu ni uwanja wa mapambano ya majaribu (mst. 12-13; 12:1-2; 1Kor 6:20, Flp. 1:20). Maisha yetu waziwazi yanatangaza injili.

◙**"lakini jiwasilisheni wenyewe kwa Mungu"** Hii ni KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE KUSHURUTISHA, ambayo ilikuwa wito kwa tendo la uamuzi. Waumini, fanyeni hivi kwa wokovu kwa imani, lakini sharti waendelee kufanya hivi kwa maisha yao yote.

Angalia usambamba wa mistari hii

1. KITENZI kile kile, na vyote ni vyenye KUSHURUTISHA.
2. Mgongano wa sitiari
   a. silaha ya wasio haki
   b. Silaha ya wenye haki
3. Waumini wanaweza kuiweka miili yao wenyewe katika dhambi ama kwa Mungu. Kumbuka, mstari huu unarejerea kwa waumini-uamuzi wao unaendelea; vita inaendelea (kama vile 6:12, 19; 1 Kor 6:18-19; Efe 6:10-18)!

**6:14 "na dhambi isijetawala juu yenu"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI UJAO (kama vile Zab. 19:13), likifanya kazi kama ya KUSHURUTISHA, "na dhambi isijetawala juu yenu. Dhambi siyo bwana wa waumini kwa sababu, siyo bwana juu ya Kristo (kama vile mst 9; Yoh 16:33).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:15-19**

**15 Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha! 16 hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. 17 Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; 18 na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki. 19 Nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu. Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa.**

**6:15** Swali hili la pili la kudhania (lugha ya kukemea) ni sawa na 6:1. Yote yanajibu maswali tofauti kuhusu uhusiano wa Mkristo na dhambi. Mstari 1 unashughulika na neema kutotumika kama leseni ya kufanya dhambi, wakati mst 15 unahusu, hitaji la mkristo kupinga au kukinza vitendo vya dhambi. Wakati huo huo muumini lazima amtumikie Mungu sasa kwa nia ile ile ambayo hapo mwanzo alitumikia dhambi (kama vile 6:14)

**NASB, NKJV,**
**TEV "ni lazima tutende dhambi"**
**NRSV "tutende dhambi"**
**NJB "kwamba tuko huru kutenda dhambi"**

Tafsiri za Williams na Phillips zote zinafasili hii KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE HALI YA UTEGEMEZI kama KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO ukifanana na mst. 1. Huu sio mtazamo mzuri. Tazama njia mbadala za tafsiri

1. KJV, ASV, NIV "je tutende dhambi?"
2. Tafsiri ya miaka mia "je, tutende tendo la dhambi?"
3. RSV "yatupasa kutenda dhambi?"

Swali hili linasisitiza katika Kiyunani na kutegemea jibu la "ndiyo". Hii ndiyo ilikuwa njia ya kukemea ya Paulo kuwasilisha ukweli. Aya hii inaelezea thiolojia batili! Paulo alijibu kwa namna yake ya kusema "haitakuwa". Injili ya Paulo ya msingi wa neema ya bure ya Mungu ilieleweka vibaya na kutukanwa na walimu wengi wa uongo.

**6:16** Swali linatarajia mwitikio wa "ndiyo". Binadamu wanahudumia kitu au mtu. Nani ambaye anatawala maisha yako, dhambi, au Mungu?. Yule mwanadamu anayemtii, inaonyesha ndiye anayemtumikia (kama vile Gal 6:7-8)

**6:17 "bali ashukuriwe Mungu"** Paulo daima alipasa sifa kwa Mungu. Maandiko yake yalikuwa na mtiririko kutoka katika maombi yake na maombi yake kutoka katika uelewa wake wa injili. Tazama Mada Maalum: Maombi ya Paulo, Sifa na Shukrani kwa Mungu katika 7:25.

◙**"ulikuwa…ukawa"** Hii ni NJEO ISIO TIMILIFU ya KITENZI "kuwa" ambayo ilielezea hali ya kuwa katika wakati uliopita (watumwa wa dhambi) ikifuatiwa na NJEO TIMILIFU ambayo inathibitisha kuwa hali ya uasi umekoma.

◙**"umekuwa mtiifu toka moyoni mwako kwa namna ya yale mafundisho"** Katika mazingira haya, hii ilimaanisha udhihilisho wao kwa neema kupitia imani, ambao ni lazima uongoze siku zote hali ya kufanana Kristo. Neno "Mafundisho" yalimaanisha mafundisho ya utume au injili.

◙**"moyo"** Tazama Mada Maalum: Moyo katika 1:24

**NASB "kwa namna ile ya mafundisho ambayo umeazimia"**
**NKJV "kwa namna ile ya imani ambayo uliokolewa"**
**NRSV, NIV, "kwa namna ile ya mafundisho ambayoa umeaminishwa"**
**TEV "ukweli uliopatikana katika mafundisho uliopokea"**
**NJB "kwa sehemu ya mafundisho uliyopewa"**

Wazo hili ni sambamba na 1Kor 15:1 na inarejerea kwenye ukweli wa injili kwamba waamini hawa wamesikia na kupokea. Injili ni

1. Mtu wa kumkaribisha
2. Ukweli kuhusu mtu kuamini
3. Maisha kama yale mtu anayoishi

◙ "**muundo"** Tazama mada maalum hapo chini.

## MADA MAALUMU: MUUNDO (*tupos*)

Neno *tupos* lina elimu-maana pana.

1. Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 645

a. Sampuli
b. mpango
c. Mtindo au namna ya kuandika
d. Amri ya serikali ama agizo litolewalo na mtawala
e. Sentensi ama uamuzi
f. Mfano wa mwili wa binadamu kama sadaka ya kuondoa nadhiri kwa Mungu anayeponya
g. Kitenzi kilichotumika kwa maana ya kuongeza agizo au mwongozo wa sheria

2. Louw and Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 2, uk. 249
    a. Kovu (kama vile Yohana 20:25)
    b. Sura (kama vile Matendo 7:43)
    c. Fanya kwa mfano (kama vile Ebr. 8:5)
    d. Mfano (kama vile 1 Kor. 10:6; Flp. 3:17)
    e. Umboasili (kama vile Rum. 5:14)
    f. Aina (kama vile Matendo 23:25)
    g. Maudhui (kama vile Matendo 23:25)
3. Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised,* p. 411
    a. Kipigo, chapa, alama (kama vile Yohana 20:25)
    b. Eleza kinaganaga
    c. Sanamu (kama vile Matendo 7:43)
    d. Kanuni, mpango (kama vile Rum. 6:17)
    e. Muundo, kusudi (kama vile Matendo 23:25)
    f. Umbo, enye kufanana na kitu kingine (kama vile 1 Kor. 10:6)
    g. Umbo tarajiwa, aina (kama vile Rum. 5:14; 1 Kor. 10:11)
    h. Sampuli mfano (kama vile Matendo 7:44; Ebr. 8:5)
    i. Mfano adilifu (kama vile. Flp. 3:17; 1 The. 1:7; 2 The. 3:9; 1 Tim. 4:12; 1 Pet. 5:3)

Kumbuka, msamiati hauweki maana; ni matumizi tu ya maneno kwenye sentensi/aya ndiyo yanaweka maana (yaani, muktadha). Kuwa mwangalifu kugawanya rasmi kundi la fafanuzi kwa neno na kulitumia kila mahali neno hilo linapotumika katika Biblia, muktadha huamua maana!

**6:18 "mlipokwisha kuwekwa huru toka dhambini"** Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU YA HALI YA KUENDELEA. Waumini wamewekwa huru na injili kwa uwakala wa Roho kupitia katika kazi ya Kristo. Waumini wameondolewa toka adhabu ya dhambi (udhihilisho) na utawala wa kikatili wa dhambi (utakaso, kama vile mist 7 na 22). Siku moja watakuwa huru kutoka katika uwepo wa dhambi (utukufu, kama vile 8:29-30).

◙**"mkawa watumwa wa haki"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, **"**mkawekwa kuwa watumwa wa haki." Tazama Mada Maalum mst. 7 na 22. Waumini wamewekwa huru kutoka katika dhambi ili wamtumikie Mungu (kama vie mist. 14,19, 22; 7:4; 8:2). Lengo la neema huru ni maisha ya kiungu. Udhihirisho kwa pamoja ni tamko la kisheria na msukumo kwa haki binafsi. Mungu anataka kutuokoa na kutubadilisha ili tuwafikie wengine. Neema haikomi kwa wokovu wa muumini binafsi (Mathayo 28:18-20; Luka 24:47; Matendo 1:8).

**6:19 "nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu"** Paulo anahutubia waumini wa Rumi. Je, anaelezea tatizo husika la mahali alilolisikia kuhusu (wivu miongoni mwa waumini wa Kiyahudi na waumini wa watu wa Mataifa) au anakazia ukweli kuhusu waumini wote?. Paulo alitumia fungu hili mapema katika Warumi 3:5 kama anavyofanya katika Wagalatia 3:15. Mstari wa 19 ni unaenda sambamba na mstari 16. Paulo anarudia mawazo ya kithiolojia ya kukazia.

Wengine wangalisema fungu hili lina maana ya kuwa Paulo alikuwa akiomba msamaha kwa kutumia sitiari ya utumwa. Hata hivyo, "kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu" halistahili tafsiri hii. Utumwa haukuangaliwa kama

kitu kibaya kwa jamii ya watu wa karne ya kwanza, hasa Rumi.Lilikuwa tu ni jambo kitamaduni kwa wakati huo. Theruthi mbili ya ulimwengu wa Rumi walikuwa watumwa.

◙**"mwili"** Tazama Mada Maaluma katika 1:3.

◙**"inatokea katika utakaso"** Hili ndilo lengo la udhihilisho (kama vile mst. 22). Agano Jipya lilitumia neno hili kwa maana mbili za kithiolojia.

1. Utakaso wa mahali, ambao ni zawadi ya Mungu ( dhana ya ushamirisho) iliyotolewa katika wokovu pamoja na udhihilisho kupitia katika imani ya Kristo (kama vile Mdo. 26:18; 1 Kor 1:2; 6:11; Efe 5:26-27; 1 The. 5:23; 2 The. 2:13; Ebr. 10:10; 13:12; 1 Pet 1:2).
2. Mwendelezo wa utakaso ambao pia ni kazi ya Mungu kupitia katika Roho Mtakatifu ambapo maisha ya muumini yanabadilishwa katika taswira na ukomavu kwa Kristo (dhana tegemezi, kama vile 2 Kor 7:1; 1 The. 4:3, 7; 1Tim 2:15; 2 Tim 2:21; Ebr 12:10, 14).

Tazama Mada Maalum Utakaso katika 6:4. Utakaso kwa pamoja ni zawadi na pia ni amri. Ni nafasi (msimamo) na ni shughuli (stadi ya kazi)! Ni kitu KINACHOONYESHA (maelezo) na KINASHURUTISHA (amri). Linatokea mwanzoni lakini halidumu hadi mwisho. (kama vile Flp. 1:6; 2:12-13:

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:20-23**
**[20]Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa huru mbali na haki. [21]Ni faida gani basi mliyopata siku zile kwa mambo hayo mnayoyatahayairikia sasa? Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni mauti. [22]Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, manayo faida yenu, ndiyo kutakaswa na mwisho wake ni uzima wa milele. [23]Kwa maana mshahara wa dhmbi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

**6:20-21** Hii kawaida inaongelea kinyume kwenye mistari ya 18 na 19. Waumini wanaweza tu kumtumikia bwana mmoja (kama vile Luka 16:13)

**6:22-23** Mistari hii inaunda mwendelezo wenye mantiki wa ujira unaolipwa kwa Yule unayemtumikia. Tunamshukuru Mungu kuwa mjadala huu wa dhambi na muumini unaishia kwa mtazamo wa neema! Kwanza, ni zawadi ya wokovu kupitia ushirikiano wetu na kisha zawadi ya maisha ya mkristo, pia kupitia katika ushirikianio wetu. Vyote hivi ni zawadi zinazopokelewa kupitia imani na toba

**6:22 "mnayo faida yenu, ndio kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele"** Neno "faida" haswa "tunda" limetumika katika mstari wa 21 kuzungumzia matokeo ya dhambi, lakini mstari 22 unazungumzia matokeo ya kumtumikia Mungu. Faida ya haraka ni muumini kufanana na Kristo. Hatima ya faida anayo yeye mwenyewe na kuma yeye milele (kama vile Yn. 3:2). Kama hakuna matokeo yoyote ya haraka (badiliko katika maisha, kama vile Yak 2) hatma ya matokeo yanapaswa kihalali kabisa kuulizwa (uzima wa milele, kama vile Mathayo 7). "Hakuna tunda, hakuna mzizi!"

**6:23** Huu ni muhtasari wa sura nzima. Paulo anaweka wazi uchaguzi. Uchaguzi ni wetu-dhambi na mauti au neema ya bure kupitia Kristo na uzima wa milele. Inafanana kabisa na "njia mbili" za fasihi ya hekima ya Agano la Kale (Kumb 30:1, 17; Zaburi 1; Mithali 4:10-19; Mathayo 7:13-14)

◙ **"mshahara wa dhambi"** Dhambi inafananishwa kama mtu (1) mmiliki wa mtumwa (2) jenerali wa jeshi, au (3) mfalme anayelipa ujira (kama vile 3:9; 5:21; 6:9,14,17).

◙**"zawadi ya bure ya Mungu ni uzima wa milele**" Neno hili lililotafsiriwa "zawadi ya bure" (*charisma*) lilikuwa ni kutoka asili ya neno neema (*charis,* kama vile 3:24; 5:15,16,17; Efe. 2:8-9) Tazama nukuu 3:24

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa vipi kazi njeme inavyohusiana na wokovu (kama vile Efe 2:8, 9, 10)?
2. Ni kwa vipi mwendelezo wa dhambi katika maisha ya muumini unavyohusiana na wokovu (kama vile Yohana 3:6, 9)?
3. Je, sura hii inafundisha "ukamilifu pasipo kutenda dhambi?
4. Ni kwa vipi sura ya 6 inahusiana na sura ya 5 na ya 7
5. Kwa nini ubatizo unajadiliwa hapa
6. Je wakristo wanadumisha asili yao ya zamani? Kwa nini?
7. Nini hatari ya vitendo vya NJEO YA WAKATI ULIOPO vinavyomiliki mst 1-14 na VITENDO VYA NJEO TIMILIFU katika 15

# WARUMI 7

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Ulinganifu kotokana Na ndoa | kuwekwa huru kutoka kwenye Sheria | Ulinganifu kutokana na ndoa | Uchambuzi kutokana na ndoa | Mkristo amewekwa huru kutoka utumwani kwenda Katika sheria |
| 7:1-6 | 7:1-6 | 7:1-3 | 7:1-6 | 7:1-6 |
| | | 7:4-6 | | |
| Tatizo la dhambi Iliyo ndani | Faida Ya dhambi katika Sheria | Sheria na dhambi | Sheria na dhambi | Kazi ya sheria |
| 7:7-12 | 7:7-12 | 7:7-12 | 7:7-11 | 7:7-8 |
| | | | | 7:9-11 |
| | Sheria haiwezi Kuokoa kutoka Dhambini | | 7:12-13 | 7:12-13 |
| 7:13-25 | 7:13-25 | 7:13 | | |
| | | Mgongano wa ndani | Mgongano ndani Ya mtu | jitihada za ndani |
| | | 7:14-20 | 7:14-20 | 7:14-20 |
| | | 7:21-25a | 7:21-25b | 7:21-23 |
| | | | | 7:24-25b |
| | | 7:25b | 7:25b | 7:25b |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI 1-6

A. Sura ya 7 yapaswa kutafsiriwa
   1. Kutokana na mwanga wa sura ya 6, hasa mist 12-14 (pia 3:20; 21-31; 4:13-16; 5:20)
   2. Lazima ihusishwe na mvutano katika kanisa la Rumi kati ya watu wa Mataifa wanaoamini na Wayahudi wanaoamini ambao inaonekana katika sura 9-11

   Chanzo kamili cha tatizo hakifahamiki; ingeweza kuwa
      a. Suala la kisheria kuhusiana na sheria ya Musa,
      b. Msisitizo wa kabila la Yuda, kuwa Musa kwanza, Kristo baadaye,
      c. Kutoelewana kuhusu injili inavyotumiwa kwa Wayahudi,
      d. Kutoelewana kuhusu uhusiano kati ya Agano la Kale na Agano Jipya,
      e. Wivu kanisani wa viongozi wa Wayahudi wanaoamini kwa kuwekewa badala yao uongozi wa watu wa mataifa wanaoamini wakati wa amri ya mtawala ambayo ilikataza mitambiko yote ya Wayahudi katika Roma. Wayahudi wengi walioamini wangeweza kuondoka pia.

B. Warumi 7:1-6 inaendeleza lugha ya kufanana na ile ya sura ya 6 kuhusu ushirikiano wa wakristo na maisha yake ya zamani. Sitiari zilizotumika ni:
   1. Kifo na kuondolewa katika utumwa na kwenda kwa Bwana mwingine (sura 6)
   2. Kifo na kuondolewa katika masharti ya mikataba ya ndoa (sura 7)

C. Sura za 6 na 7 kifasihi zinalandana. Sura ya 6 inashughulika na uhusiano wa muumini na "dhambi" na sura ya 7 inashughulika na uhusiano wa muumini na "sheria". Ulinganisho wa kifo kumweka huru mtumwa (6:12-23) ni sambamba na kifo kuweka huru mtu kutokana na mkataba wa ndoa (7:1-6)

| **Sura ya 6** | **Sura ya 7** |
|---|---|
| 6:1 "dhambi" | 7:1 "sheria" |
| 6:2 "alikufa kwa dhambi" | 7:4 "alikufa kwa sheria" |
| 6:4 "kwamba, lazima tutembee katika upya wa maisha | 7:6 "Kwamba lazima tutumikie katika upya wa Roho" |
| 6:7 "yule ambaye amekufa, amewekwa huru kutokana na dhambi" | 7:6 "tumewekwa huru kutokana na sheria kwa kufa kwa kile ambacho tulikuwa tumefungwa nacho" |
| 6:18 "kwa kuwe kwa kwetu huru kutoka dhambi | 7:3 "Huru na dhambi |

(imechukuliwa kutoka katika kitabu cha Anders Nygren's *commentary on Romans,* kilichotofasiriwa na Carl C. Rassmussen, uk 268)

D. Sheria na amri zake ilikuwa kunyongwa. Binadamu wote wana hatia chini ya sheria (kama vile Rum 6:14; 7:4; Gal 3:13, Efe 2:15; Kol. 2:14) sheria ya Musa ikawa laana.

E. Pamekuwa na nadharia kuu 4 katika kutafsiri sura ya 7
   1. Paulo anajizungumzia mwenyewe (Historia ya maisha ya mtu mwenyewe)
   2. Paulo anazungumza kama mwakilishi wa wanadamu wote (mwakilishi, Chrysostom)
   3. Paulo anazungumzi uzoefu wa Adamu (Theodore wa Mopsuetia)
   4. Paulo anazungumzia uzoefu wa Israeli.

F. Katika njia nyingi Warumi 7 inafanya kazi kama "Mwanzo 3". Inaonesha mvuto wa uasi hata kwa wale walio na ufahamu wa Mungu. Maarifa hayawezi kuwaweka huru wanadamu walioanguka bali neema ya

Mungu tu. Moyo mpya, fikra mpya na roho mpya, pekee vinaweza (Agano Jipya kama vile Yer 31:31-34; Eze 36:26-27). Na hatahivyo, kuna mapambano yanayoendelea (kama vile 6:12, 19, 1 Kor 6:10-19; Efe 6:10-18).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:1-3**
**1Ndugu zangu, hamjui, (maana nasema na hao waijuao sheria), ya kuwa torati humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai? 2Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile ya mume.3Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hatayeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine.**

**7:1 "(kwa vile anazungumza na wale wanaofahamu sheria)"** Hii ingeweza kumaanisha

1. Wayahudi waaminio tu
2. mgogoro kati ya Wayahudi waamini na watu wa mataifa katika kanisa la Rumi.
3. sheria kwa ujumla wake kama jamaa wa wanadamu wote (kama vile 2:14-15)
4. Kwa watu wa mataifa wapya waaminio katika kujifunza kuhusu imani yao mpya (katekismu, 6:17) kutoka katika Maandiko ya Agano la Kale.

◙**"sheria"** Hii ndiyo hoja nzito katika sura hii (kama vile mist. 1,2, 4, 5, 6 n.k). Hata hivyo, Paulo alitumia neno hili katika maana kadhaa tofauti (sheria asilia; sheria ya Musa, kanuni za jamii).Inaonekana kuwa, mjadala wa Paulo ulisababishwa na 6:14. Wasilisho lake liko sambamba na muundo wa sura ya 6. Angalia mtazamo halisi, C. sheria ya Musa na uhusiano wake kwa Agano Jipya katika Kristo pia inajadiliwa katika 3:21-31 na 4:13-16.

◙

**NASB "kwamba sheria ina haki juu ya mtu kadri anavyokuwa anaishi"**
**NKJV "kwamba sheria inatawala binadamu kadri navyokuwa anaishi"**
**NRSV "kwamba sheria inambana mtu tu, wakati wa maisha yake"**
**TEV "sheria inatawala mtu tu kadri anavyokuwa anaishi"**
**NJB "kwamba sheria inamuathiri mtu kwa wakati ule wa maisha yake"**

Hapa kifasihi ni kwamba "Bwana yuko juu" (*kurieuō*, kama vile 6:9, 14). Sheria ya Musa ilikuwa Baraka kubwa (kama vile Zab 19:119) na pia laana ya ajabu (kama vile Gal 3:13; Efe 2:13; Kol 2:14). Kwa kifo chake masharti ya sheria yakaisha. Hii ni sitiari ileile iliyotumika katika sura ya 6 kuhusu kifo cha muumini kwa dhambi.

**7:2 "kwa mwanamke aliyeolewa**" Huu ni ufafanuzi mkubwa wa Paulo katika mistari 1-6. Katika sura ya 6, alizungumzia kifo cha mtu kuwa ni mwisho wa masharti ya kuwa watumwa. Suala la kuzingatia hapa ni ndoa na masharti. Maelezo yalibadilishwa kwa sababu mwanamme ndiye aliyekufa ili mwanamke aolewe tena, wakati katika ulinganisho wa Paulo, ni muumini aliyekufa, na hivyo anakuwa hai kwa Mungu.

◙ **"anaachiliwa"** Hiki ni KITENZI kama ilivyo katika 6:6 ikiwa na maana, "kufanywa kutenda kazi," "kufanywa kutokuwa na kazi,"au "kuachwa". Katika 6:6 ilikuwa katika KAULI TENDEWA TIMILIFU, hapa iko katika KAULI TENDEWA YA WAKATI ULIOPITA, ikimaanisha ameachwa na anaendelea kuachwa. Tazama Mada Maalum katika 3:3.

**7:3 "ataitwa mwanamke mzinifu"** Maoni haya yanahusiana na hoja ya Wayahudi kati ya shule za uongozi wa kidini za Shammai na Hillel juu ya Kumb 24:1-4 hasa "baadhi ya mambo ya aibu." Shule ya Hillel kilikuwa kikundi cha wanaharakati ambacho kiliweza kuruhusu kuvunjika kwa ndoa kwa sababu yoyote ile. Shule ya Shammai ilikuwa ni kundi lisilopenda kubadili mambo yale ambayo yangaliruhusu taraka tu kwa habari za uzinifu au mambo mengine yasiofaa ya zinaa (kama vile Mt. 5:32; 19:9).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7: 4-6**
**[4]Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda. [5] Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata mkaizalia mauti mazao. [6] Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko.**

**7:4** "**ninyi pia mmeumbwa ili kufa"** Huu ndiyo msukumo mkuu katika haya hii (na sura ya 6). Ilihusiana na analojia katika sura ya 6 ya Wakristo wanaoifia dhambi kwa sababu "wamezikwa pamoja" (6:4) na "kusulibiwa pamoja"(6:6) na Kristo (kma vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20).Waamini ni viumbe vipya katika Kristo (tazama nukuu kamili katika 6:4) katika zama hizi mpya za Roho (kama vile 2 Kor. 5:17). Ubatizo uliweka mipaka kati ya zama za kale, mtu wa kale, na zama mpya, mtu mpya.

◙ "**kupitia mwili wa Kristo"** Hii hailejerei dhana ya kitheojia ya kanisa kama mwili wa Kristo (kama vile 2 Kor. 12:12, 27), bali katika mwili wa Kristo kama ilivyo katika 6:3-11 ambapo, wakati Yesu alipokufa, waamini, kwa namna ya utambulisho kupiti aubatizo, walikufa pamoja nae. Kifo Chake kilikuwa kifo chao (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20). Maisha ya ufufuo Wake yaliwaweka huru kumtumikia Mungu na wengine.

◙**"kwamba yatupasa kuzaa matunda kwa Mungu"**Hili pia lilikuwa sambamba na sura ya 6, hasa 6:22. Waamini sasa wako huru kupitia Kristo kujiungamanisha wao wenyewe kwa Kristo. Hii ni analojia ya ndoa endelevu. Kama Kristo alivyowafia waamini, sasa wanapaswa kuifia dhambi (2 Kor. 5:13-14; Gal. 2:20). Kama Kristo alivyopalizwa, nao, vilevile, wamepalizwa katika maisha mapya ya kiroho ya utumishi kwa Mungu (kama vile Rum. 6:22; Efe. 2: 5-6)na kila mmoja wao (kama vile 1 Yohana 3:16).

**7:5**
**NASB "wakati tulipokuwa mwilini"**
**NKJV "wakati ule tulipokuwa mwilini"**
**NRSV "Wakati tulipokuwa tukiishi mwilini"**
**TEV "wakati ule tuliishi kulingana na asili yetu ya ubinadamu"**
**NJB "Kabla ya kubadilika kwetu"**

Mstari huu ni tofauti na mst. wa 4. Mstari wa 4 uahusiana na uzoefu wa mwamini, kama ulivyo mst. 6. Mstari wa 5 unafafanua "matunda" ya maisha bila nguvu za Mungu (Gal. 5:18-24.)Sheria inawaonyesha waamini dhambi yao (mist. 7-9; Gal. 3: 23-25), lakini haiwezi kuwapa nguvu ya kuishinda. Katika mazingira fungu hili linagusia anguko la waamini, asili ya dhambi iliyorithiwa kutoka kwa Adamu (kama vile 6:19). Paulo anayatumia maneno haya *sarx* katika njia mbili tofauti (1) asili ya dhambi (mtu wa kale) na (2) umbo la nje (kama vile 1:3; 4:1; 9: 3,5). Hapa ni kinyume, lakini angalia Rum. 1:3; 4:1; 3:9; 3,5; Gal. 2:20. Mwili/umbo (*sarx/soma)* siyo ovu kwayo na juu yake yenyewe, bali ni, kama fikra (*nous)*,ni uwanja wa mapambano, sehemu ya makabiliano kati ya nguvu ya uovu ya zama hizi na Roho Mtakatifu. Paulo analitumia neno hili katika njia thabiti na tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania, siyo fasihi ya Kiyunani.Tazama Mada Maalumu Mwili (*sarx)* katika 1:3.

◙ **"ambayo ilitiwa nguvu na Sheria"**dhana hii ya uasi wa asili ya mwanadamu, ambao unaashiria shari kwa vipingamizi vyovyote vile, kunaonekana vema katika Mwanzo 3 na katika wanadamu wote. Sheria iliweka mipaka (kama vile mist. 7-8).
Mipaka hii ilikuwa kwa ajili ya ulinzi wa mwanadamu, lakini wanadamu waliichukulia kama minyororo na vizuizi. Dhambi, roho ya kuwa huru kutoka dhambini ilichochewa na Sheria ya Mungu. Tatizo halikuwa vizuizi (sheria kama vile mist. 12-13), lakini mwanadamu ajitawalaye na mapenzi yake mwenyewe.

◙ “**kuzaa matunda kwa kifo”** Ni tofauti kubwa kiasi gani kati ya

1. mst. 5- kuzaa matunda kwa Mungu
2. mst 6- kuzaa matunda kwa kifo.

Waumini wamekufa kwa kifo, dhambi, na sheria na sasa wanaishi kuzaa matunda kwa ufalme!Paulo anaweka wazi (au ni aina ya mafumbo bora, Tazama nukuu 8:2). Mtu ni moja ya makundi haya ya mwili. Adamu au Yesu (kama vile 5:12-21). Wale walio kwa Yesu wako huru, hawajafungwa, na ni wapya (kama vile Gal 2:19-20).Tembea ndani yake ,furahia ndani yake.

**7:6**“**lakini sasa**” Newman na Nida, *A Translator's Handbook on Paul's Letter to the Romans,* kina maoni yanayofurahisha sana.“Ni muhimu kutambua usambamba uliopo kati ya mistari ya 5 na 6 na wakati huo huo, uhusiano wao na kile kinachofuata. Mstari wa 5 unaelezea kipindi kabla ya uzoefu na wakristo, na una usambamba wake katika 7:7-25, mstari 6 unaelezea maisha ya sasa ya imani chini ya uongozi wa Roho wa Mungu, na una usambamba wake katika 8:1-11 (uk 130)

◙“**tumeachiliwa”** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Inatofautishwa na KAULI ELEKEZI YA KATI ISIO TIMILIFU ya mst 5. Waumini wamekuwa wanaendelea kushikwa na dhambi kama ilivyokuwa wazi katika sheria; lakini sasa wamewekwa huru na Roho kupitia habari njema ya injili. Neno hili pia limetumika kwa mwanamke ambaye mume wake amekufa katika mst. 2

◙“**kwa kufa kwetu kwa hilo ambalo kwalo tulikuwa tumefungwa**” Ni KAULI TENDAJI YA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ikifuatiwa na KAULI TENDWA ELEKEZI ISIO TIMILIFU. Mungu aliwaweka huru waumini kupitia kifo cha Kristo kutoka na

1. laana ya Agano la Kale
2. dhambi zao ndani ya nafsi wamekuwa wanaendelea kufungwa na uasi wao dhidi ya kusudio la wazi la utashi wa Mungu, asili iliyoanguka, dhambi binafsi, na majaribu ya nguvu (Efe. 2:2-3).

◙“**upya…uzamani”** Njia hii mpya ya kiroho inaonekana kumaanisha Patano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze 36:22-32). Neno la Kiyunani “mpya” *(kainos-kainotēs*) linatumiwa na Paulo kwa

1. upya wa maisha, Rum 6:4 (Tazama nukuu kamili katika 4:4)
2. upya wa roho, Rum 7:6
3. Patano Jipya, 1 Kor 11:2; 2 Kor 3:6.
4. uumbaji mpya, 2 Kor 5:17; Gal 6:15
5. mtu mpya, Efe 2:15; 4:24

Neno “zamani”linamaanisha sheria ya Musa iliyomaanisha “kuisha kabisa” Paulo anatofautisha Patano la Kale na Patano Jipya, kama anavyofanya mwandishi wa Waebrania (kama vile 8:7 na 13)

**NASB, NKJV** **“hivyo kwamba tunamtumikia katika upya wa roho”**
**NRSV** **“ya kwamba tu watumwa siyo chini ya sheria zilizoandikwa zamani, lakini katika maisha mapya ya Roho”**
**TEV** **“lakini kwa njia mpya ya Roho”**
**NJB** **“huru kutumika katika njia mpya ya Roho”**

Hii kifasihi “katika Upya wa Roho” hakuna uhakika kama hii ilimaanisha kuzaliwa upya kwa roho ya kibinadamu au Roho Mtakatifu. Tafsiri nyingi za Kiingereza zinaonyesha herufi kubwa ambayo inaonyesha Roho Mtakatifu ambaye anatajwa kwa kiasi kikubwa kwa mara ya kwanza katika Warumi 8 (mara 15). Neno “roho”, ingelimaanisha roho ya binadamu, iliyozaliwa na kupewa nguvu na injili na Roho katika Rum 1:4,9; 2:29; 7:6;8:15;11:8; 12:11; 1 Kor 2:11; 4:21; 5:3,4,5; 7:34; 14:15; 16,32; 16:18.

Katika maandiko ya Paulo, “mwili” na “roho” daima vinatofautishwa kwa njia mbili tofauti za kufikiri na kuishi (kama vile 7:14; 8:4; Gal 3:3; 5:16,17,25; 6:8). Maisha halisi yasiyo na Mungu maana yake ni “mwili”. (Tazama Mada Maalum katika 1:3, lakini maisha na Mungu ni “roho” au “Roho”. Roho Mtakatifu aishiye ndani (kama vile 8:9, 11) humbadilisha muumini kuwa kiumbe kipya katika Kristo (kwa nafasi na mazoea).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA JUU YA WARUMI 7:7-25

A. Warumi 7:7-25 inaelezea ukweli wa mwanadamu. Wanadamu, waliookolewa na waliopotea, wamekumbana na hali ya mazuri na mabaya katika ulimwengu wao na ndani ya mioyo yao na fikra zao. Swali ni kwamba, "ni kwa namna gani Paulo alikusudia habari hii ieleweke?" kwa mazingira haya, ni lazima ihusishwe na muktadha wa sura 1:18-6:23 na 8:1-39. Wengine wanaiona kuwa imezingatia sana juu ya wanadamu wote kwa hiyo, kuona uzoefu binafsi wa Paulo kama mfano hailisi. Tafsiri hii inaitwa "nadharia ya maisha ya mtu binafsi".

Paulo alitumia neno "mimi" bila kuwa na maana ya "ubinafsi". Matumizi haya ya kutojiangalia kama "mimi" binafsi yameweza pia kuchukuliwa kutoka katika viongozi wa dini ya Kiyahudi. Kama hii ni kweli, habari hii ingalimaanisha kuhama kwa mwanadamu kutoka "wema" kwa njia ya kuwekwa makosani hadi katika wokovu Sura 8 nadharia ya uwakilishi (yaani *Jerome Biblical Commentary* uk 312). Hata hivyo, wengine wameona mistari hii kama inahusiana na mapambano yasiyokoma ya waumini na asili ya mwanadamu aliyeanguka (yaani Augustine, Thomas Aquinas, Martin Luther, John Calvin, Karl Barth). Kilio cha uchungu moyoni katika mst. 24 unaonyesha mvutano wa ndani. KITENZI TIMILIFU na NJEO YA KITENZI KISICHOTIMILIFU vinatawala katika mist. ya 7-13 na wakati huo huo KITENZI CHA WAKATI ULIOPO na NJEO YA KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA vinatawala katika mistari ya 14-25. Hii inatoa imani kwa "nadharia ya mtu kuandika mwenyewe historia ya maisha yake," kwamba Paulo anaelezea uzoefu wake mwenyewe kutoka hali ya kutokujua, kwenda hali ya kubadilishwa , kwenda kuharalishwa na kuendelea katika hali hiyo lakini katika mapito ya njia ngumu ya kuelekea katika utakaso (cf. *autos, egō*, "mimi binafsi," cf. mst. 25).

Inawezekana kabisa maoni yote mawili ni kweli katika mist. 7-13 na 25b, Paulo anazungumzia historia ya maisha yake aliyoiandika mwenyewe; wakati katika mist. 14-25a, anazungumzia mapambano ya ndani na dhambi, kama mwakilishi wa wanadamu wote waliokombolewa. Hata hivyo inabidi ikumbukwe kuwa habari hii yote inabidi iangaliwe dhidi ya hatua ya Paulo kugeuka kama Myahudi mdini aliyejitoa kabla ya kuwa mpya. Uzoefu wa Paulo ulikuwa ni wa kipekee.

B. Sheria ni nzuri. Inatoka kwa Mungu, ilitumika na inaendea kutumika kwa lengo la Kimungu (kama vile 7:7, 12, 14, 22, 25; Mt 5:17-19). Haiwezi kuleta amani wala wokovu (kama vile Gal 3). James Stewart katika kitabu chake *A Man in Christ,* inaonesha mafumbo ya uandishi na fikra za Paulo.

"Ingeweza kwa kutegemea mtu aliyejiandaa kujenga mfumo wa wazo na imani ya kuweka imara maana za maneno aliyoyatumia. Ungetegemea alenge kwa uhakika/usahihi katika utaalam wa kuandika vifungu vya maneno kwa mawazo yake aliyoweka mbele. Ungedai kuwa, neno mara tu likisha tumika na mwandishi wako kwa maana fulani, lazima maana hiyo ionekane tangu mwanzo hadi mwisho. Lakini haya kwa Paulo ni kujifadhaisha. Uandishi mwingine wa fungu ni dhaifu, hauna nguvu. 'Sheria ni takatifu,' anaandika, 'ninafurahi katika sheria ya Mungu baada ya utu wa ndani' (kama vile Rum. 7:12-13). Lakini, ni wazi kuwa ni namna nyingine ya neno *nomos* inayomfanya aseme popote pale, 'Kristo ametukomboa kutoka katika laana ya sheria (kama vile Gal. 3:13)''' (uk.26)

C. Ushahidi wa maandiko unaoshughulika na swali "Je, Paulo anazungumzia mtu aliyeokolewa au asiyeokolewa katika mistari ya 14-25?" ni kama ifuatavyo

1. Mtu ambaye hajaokolewa
    a. Hii ilikuwa ni tafsiri ya viongozi wa zamani wa kanisa waliokuwa wakizungumza Kiyunani
    b. Mafungu yafuatayo yanaunga hoja mkono
        (1) "Mimi ni wa mwilini," mst.14
        (2) "naliuzwa utumwani mwa dhambi," mst. 14
        (3) "hakuna kizuri kisicho ndani yangu," mst. 18
        (4) "kunanifanya kuwa mfungwa wa sheria ya dhambi ambayo imo ndani ya wenzangu," mst 23
        (5) "mtu asiye na furaha kama nilivyo. Nani ataniondoa katika mwili huu wa kifo?" mst. 24

c. Ujumbe huu wa haraka uliomo katika sura ya 6 ni kwamba,tu huru kutoka katika utawala wa dhambi. Katika sura ya 8 unaanza na “kisha hapo”
d. kukosekana kwa rejea yoyote kwa Roho au Kristo hadi kufunga ujumbe huu, (mst. 25).

2. Mtu aliyeokolewa
   a. Hii ndiyo ilikuwa tafsiri ya Augustine, Calvin na utamaduni uliorekebishwa.
   b. Vifungu vifuatavyo vinaunga mkono hoja hii
      (1) “tunajua kuwa sheria ni ya kiroho,” mst. 14
      (2) “Nakubaliana na Sheria, kukiri kuwa ni nzuri,” mst. 16
      (3) “zuri ninalolitaka silitendi,” mst.19
      (4) “kwa furaha nakubaliana na sheria ya Mungu katika mtu wa ndani,” mst. 22.
   c. Sehemu kubwa ya Warumi inaiweka sura ya 7 katika sehemu inayoshughulikia utakaso.
   d. Badiliko la wazi la vitenzi kutoka kutokamilika na katika mistari 7-13 kwenda katika matumizi endelevu ya WAKATI ULIOPO katika mist 14-24 inaashiria sehemu mpya na tofauti kwa maisha ya Paulo (yaani badiliko)

D. Kadri muumini anavyopambana kuelekea kumfanana Yesu, ndivyo anavyokumbana na hali yake ya utendaji dhambi. Kisa hiki kinaendana sawa na mazingira na haiba ya Paulo (na kwa sababu hiyo, waumini wengi, kwa maoni tofauti wanamuona Gordon Fee, *Paul, The Spirit, and the People of God).*
Mstari kutoka katika Wimbo wa Kiutenzi uliotungwa na Henry Twells:

> “Na hakuna hata mmoja, O Bwana, ana pumziko la kweli,
> Kwa vile hakuna huru kwelikweli toka dhambini;
> Na wale wanaohangaika watamtumikia Bwana kwa dhati
> Watatambua wingi wa uovu wao ndani mwao.”

Nafikiri Paulo alikuwa akihangaika na mambo yake ya awali ya Kifarisayo, ambayo yalimpa namna yake ya kuwasilisha “sheria” na “dhambi, ” au “kifo.” Hata hivyo binafsi nabanwa na mahangaiko yangu kwa majaribu na dhambi baada ya wokovu.Ni hakika imepamba utafsiri wangu. Nafikiri Gordon Fee, *Paulo, the spirit, and the people of God,*” inatoa uzoefu na mtazamo mwingi chanya wa Mkristo. Jambo moja nafahamu mvutano au mgongano kati ya

1. enzi ya kale-enzi mpya
2. mtu wa kale - mtu mpya
3. sheria- roho

Vimeshughulikiwa katika Kristo! Ushindi ni wetu. Usitazame sura ya 7 bila kuangalia sura ya 6 na 8. Ushindi ni wetu katika Yeye.

E. *Sun* (KIHUSISHI katika 8:32) muungano wa maneno katika Warumi 8
1. mst, 16-*sun +* kushuhudia/ushuhuda
2. mst. 17-*sun+*kurithi
3. mst. 17-*sun+* kuteseka
4. mst. 17-*sun+* kutukuza
5. mst. 22-*sun+*kulia kwa uchungu
6. mst. 22-*sun+*maumivu ya kuzaa
7. mst. 26-*sun+* kushikilia
8. mst. 28-*sun+* kufanya kazi na/kushiriki
9. mst. 29-*sun+* kuendana na

Muungano huu wa maneno unaonyesha “ushirikiano wa pamoja” au “umoja na”

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:7-12**
**7Tusemeje, basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, usitamani. 8Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri, ikafanya ndani yangu kila namna ya kutamani. Kwa maana dhambi bila sheria imekufa. 9Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, dhambi ilihuika, nami nikafa. 10Nikaona ile amri iletayo uzima ya**

**kuwa kwangu mimi ililela mauti. [11]Kwa maana dhambi, kwa kupata nafasi kwa ile amri ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua. [12]Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema.**

**7:7 "tuseme nini basi"** Paulo anarudia kwenye matumizi ya maneno yake ya kukemea.

◙ **"je sheria ni dhambi**" Fumbo la ajabu la ufunuo ni kwamba Mungu alitumia utakatifu na uzuri wa sheria kama kioo kubaini dhambi ili kwamba kumleta mwanadamu aliyeanguka katika mahali pa toba na imani (kama vile mist. 12-13; wagalatia. 3). Pia cha ajabu, sheria imeendelea kufanya kazi katika utakaso lakini siyo uhalalisho (tazama Mada Maalum: Maoni ya Paulo ya sheria ya Musa katika 13:9.

◙**"kamwe hautakuwa"** Tabia ya Paulo ya kukataa utetezi wa uongo (kama vile mist 13; 3:4, 6,31; 6:2,15; 9:14; 11:1,11; Gal 2: 17; 3:21).

◙**"kinyume chake"** Mtindo wa kifasihi wa Paulo katika Warumi unatumia vinyume kuunda hoja zake, (kama vile 3:4,6,31; 6:2,15; 7:13; 9:14;11:1, 11; Gal. 3:21)

◙**"mimi"** Weka alama katika Biblia yako, ni mara ngapi viwakilishi hivi "mimi," "yangu" au inatokea sehemu ya habari hii ya mst. wa 7-25. Itakushangaza, wakati mwingine ni zaidi ya mara arobaini.

◙"**nisingalijua dhambi isipokuwa kwa kupitia sheria"**Hii ni mojawapo ya habari muhimu ambayo inabainisha dhana ya sheria ya Musa ikifanya kazi kama kioo cha kuona dhambi ya mtu (kama vile 3:20;4:65; 5:20; Gal 3:14-29, hasa mst. 24. Kuvunja sheria mara moja tu, ilikuwa ni kuvunja patano na hivyo, kukabili matokeo yake (kama vile mst. 10 na Yakobo 2:10)

◙**"isipokuwa kupitia katika Sheria"** Hii ni SENTENSI DARAJA LA PILI YENYE MASHARTI ambayo inaitwa "kinyume na ukweli" Paulo alitiwa katika hatia ya dhambi. Huu ndio mfano pekee wa kisarufi katika Warumi. Paulo anatumia katika Wagalatia 1:10; 3:21; vile vile 1 Kor 2:8; 5:10; 11:31, na 2 Kor 12:11.

◙"**USITAMANI"** Hii ni nukuu ya amri ya kumi (kama vile Kutoka 20:17; Kumb 5:21). Amri hii ya mwisho inaangalia tabia njema, ambayo kusema kweli ni ya muhimu mno kwa zote (kama vile Mt 5-7). Sheria daima inaitwa "amri"(kama vile mist 8, 9, 11, 12, 13). Neno "tamaa" lilimaanisha, kuwekwa juu ya moyo wa mtu au "shauku kubwa". Mungu amewapa wanadamu (waliopotea na waliokolewa) vitu vingi vizuri kupitia uumbaji wake, lakini wanadamu wanatamani kuchukua vitu vya Mungu zaidi ya vile walivyopewa kupita kiasi. "zaidi na zaidi kwangu kwa gharama yoyote" inakuwa ndiyo wito wao. Nafsi ni mtawala wa nguvu ya ajabu" Tazama Mada Maaalum: Nukuu kuhusu Kutoka 20:17 katika 13:8-9.

**7:8**
**NASB, NKJV "kuchukua fursa"**
**NRSV "kutwaa fursa"**
**TEV "kupata nafasi yake"**
**NJB "kutumia udhaifu wa"**

Hili lilikuwa neno la kijeshi lililotumika katika ngome ya mapambano (kama vile mist. 8 na 11). Imechukuliwa na kutumika katika mazingira haya (kama vile mist. 9, 11). Dhambi ilichukuliwa kama mapambano ya kijeshi (kama vile mst. 11) yaliyoongozwa na kiongozi wa kijeshi (kama vile mist. 11 na 17; 6:12; 14, 16).

◙**"kwamba mbali na sheria dhambi imekufa"** Dhambi ni uasi dhidi ya makusudio ya Mungu (kama vile Rum 4:15; 5:13; 1 Kor 15:56). Hakuna KITENZI katika kifungu hiki. Kimoja lazima kiwekwe. Kama mmoja akitoa NJEO YA WAKATI ULIOPO, inaashiria kuwa hii ni kanuni ya jumla. Kama mtu akitoa NJEO YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ilimaanisha maisha ya Paulo pekee.

**7:9 "niliwahi kuwa hai"** Hii ingemaanisha Paulo kama (1) mtoto enzi za walioishi bila hatia (yaani kabla ya *Bar mitzvah* au (2) kama Mfarisayo aliyejitoa kabla ya ukweli wa injili kuingia katika moyo wake (kama vile Mdo 23:1; Flp. 3:6; 1 Tim 1:3). Ya kwanza inawakilisha "nadharia ya mtu kujiandikia historia ya maisha binafsi" ya tafsiri ya sura ya 7, na ya pili "nadharia ya uwakilishi" ya tafsiri ya sura ya 7.

◙**"amri ilipokuja, dhambi ikawa hai nami nikafa**" Roho ya uasi ya mwanadamu, hutiwa nguvu kwa makatazo. "Yanayokataliwa"na sheria ya Mungu, huamsha kiburi binafsi cha mwanadamu aliyeanguka kufanya mambo, (kama vile Mwanzo 2:16-17, 3:1-6). Tazama jinsi dhambi inavyoendelea kujifanya kama mtu katika 5:21 na 7:8, 11, 17, 20.

**7:10 "amri, ambayo ingalitokea maishani, ikathibitisha matokeo ya kifo changu"** Hii pengine ni rejea kwa ahadi ya Walawi 18:5; Kumb 4:1 au bila shaka Warumi 2:13. Sheria ikaahidi kile ambacho haikuweza kutimiza, siyo kwamba ilikuwa na dhambi, bali kwamba, mwanadamu ni dhaifu na muasi. Sheria ikawa hukumu ya kifo (kama vile Gal 3:13; Efe 2:15; Kol.2:14)

**7:11 "aliyenilaghai na kupitia hilo akaniua"** Vyote viwilii ni VITENZI TENDAJI ELEKEZI VYA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Neno hili "laghai" linatumika kwa shetani (nyoka) kumdanganya Hawa katika maandiko ya kale ya mwaka 1970 katika Mwanzo 3:13. Paulo anatumia kitenzi hiki mara kadhaa Warumi 16:18;

1 Kor.3:18; 2 Ko.r 11:3; 2 The. 2:3; 1 Tim. 2:14). Tatizo la Adamu na Hawa lilikuwa pia "kutamani" (kama vile 2 Kor. 11:3; I Tim. 2:14). Adamu na Hawa wakafa kiroho kwa kutokutii amri ya Mungu (sasa inabainishwa katika sheria (kama vile 1 Kor 15:56) na vivyo alivyofanya Paulo, na vivyo wakafanya wanadamu wote (1:18-3:20).

**7:12** Huu ni wa uthibitisho wa Paulo wa uzuri wa sheria. Siyo tatizo. Hata hivyo miundo sambamba ya Paulo, iliyotumika "dhambi" katika sura ya 6 na "sheria" katika sura 7, itakuwa imeewaudhi waumini wa Kiyahudi (wadhaifu wa 14:1-15:13) katika kanisa la Rumi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:13**
**[13]Basi je! Ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu mimi? Hasha! Bali dhambi, ili ionekane ni dhambi hasa, ilifanya mauti ndani yangu kwa njia ya ile njema, kusudi kwa ile amri dhambi izidi kuwa mbaya mno.**

**7:13**
**NASB "dhambi ili ioneshwe kwamba ni dhambi, lazima iwe katika hali ya dhambi kabisa"**
**NKJV "dhambi ili ionekane kuwa ni dhambi, lazima iwe katika hali ya dhambikupita Kabisa"**
**NRSV "kuwa dhambi ionekane kuwa dhambi..ioneshe dhambi kuliko kipimo"**
**TEV "ili kwamba asili yake kama dhambi, lazima ibainishwe"**
**NJB "dhambi kujionyesha katika hali yake kama dhambi, ili kuwa na uwezo wa kudhihirisha nguvu yake ya kutenda dhambi"**

Asili ya uovu wa dhambi inaonekana wazi katika ukweli kuwa ilichukuwa kitu kama kizuri, safi, na cha Mungu kama sheria ya Musa (kama vile Zab. 19,119) na kigeuza kuwa kama chombo cha hatia na kifo (kama vile Efe. 2:15; Kol. 2:14). Mwanadamu aliyeanguka, amechukuwa kila zawadi nzuri Mungu aliyowapa, kupita kiasi alichostahili! Tazama *hina* (kusudi) mbili, vishazi vilivyotofasiriwa kama "ili kwamba," "kwa vile." VIHUSISHI vinaonesha kusudi la mwandishi.

◙"chenye dhambi kabisa" Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya muungano wa *Huper* katika 1:30. Dhambi imefananishwa na kitu ili kuonyesha asili ya uovu. Tazama Mada Maalum Uovu wa nafsi katika 16:20.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:14-20**
**[14]Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. [15]Maana sijui nifanyalo; kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda.**

**[16]Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri ile sheria ya kuwa ni njema. [17]Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. [18]Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati.[19] Kwa maana lile jema nilipendalo silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. [20]Basi kama lile nisilolitenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.**

**7:14** “sheria ni ya kiroho” Sheria ya Mungu ni nzuri. Sio tatizo (kama vile mist. 12 & 16b).

◙ **“mimi ni mwili”** Neno hili limetumiwa na Paulo katika (1) maana ya kawaida likimaanisha mwili wa mtu (kama vile 1:3; 2:28; 4:1; 9:3,5 na (2) maana hasi ikimaanisha asili ya anguko la mwanadamu katika Adamu (kama vile mst. 5) haueleweki vizuri inamaanisha nini hasa.

◙**“niliuzwa chini ya utumwa wa kutenda dhambi**” Hii ina maana ya KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU. Nilikuwa na ninaendelea kuuzwa chini ya utumwa wa dhambi. Dhambi tena imefanywa kuwa kama mtu, hapa kama mmiliki wa mtumwa. Wakala wa IRABU YA KUTENDWA hivyo haina uhakika. Ingeliweza kumaanisha shetani, dhambi, Paulo au Mungu.

Katika Agano la Kale, neno kubwa kwa Mungu kuwarudisha wanadamu kwake ni “fidia”au “ukombozi” (na visawe vyake). Awali neno hili lilimaanisha “kukirejeresha”(na visawe vyake. Tamaza Mada Maalum katika 3;24). Kinyume cha dhana ni kifugu kilichotumika hapa, “kuuzwa katika mikono ya..” (kama vile Amu. 4:2; 10:7; 1Sam. 12:9).

**7:15-24** Mtoto wa Mungu ana “asili ya Kiungu” (kama vile 2 Pet.1:4), lakini pia asili ya anguko! (kama vile Gal. 5:17). Kwa hakika dhambi imeharibiwa (kama vile Rum. 6:6), lakini pia uzoefu wa mwanadamu unafuata katika sura ya 7.Wayahudi wanasema kuwa katika kila moyo wa mtu kuna mbwa mweusi na mweupe.Yule anayelishwa zaidi, ndiye anayekuwa mkubwa zaidi.

Ninaposoma habari hii, kwa mazoea tu, nahisi maumivu ya Paulo anapoelezea mgongano wa kila siku wa asili zetu hizi mbili. Waumini wamewekwa huru kutoka katika asili iliyoanguka, lakini, Mungu anatusaidia, tunaendelea kujisalimisha katika amri yake. Daima inashangaza kwa ukweli kuwa vita kuu ya kiroho inaanza baada ya wokovu. Ukomavu ni ushirika wa kila siku wa upendo wa Mungu wa utatu na mgongano wa kila siku na maovu (kama vile 8:12,25,26; Gal. 5:16-18; Efe. 6:10-18; Kol. 3:5-10; Taz. J.D.G. Dunn, *Jesus and the Spirit*).

**7:16, 20 “kama”** zote ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambazo zinaonekana kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi kwa makusudi yake ya kiuandishi/kifasihi.

**7:18 “Najua kuwa hakuna kizuri kilichoko ndani yangu, yaani, mwilini mwangu’’** Paulo hatetei kuwa mwili tulionao ni mwovu, bali ulikuwa ni uwanja wa vita kati ya asili iliyoanguka na Roho wa Mungu. Wayunani walidai kuwa, mwili, vyote vilivyomo, vilikuwa viovu. Hii ilijengeka ndani ya imani mbili za mafundisho ya kipagani (kama vile Waefeso, Wakolosai, na I Yohana). Wayunani walikuwa wakilaumu, “umbile” kwa matatizo ya kiroho.Paulo haoneshi mgongano wa kiroho katika maneno haya. Alifanya dhambi kuwa mtu na Kutumia uasi wa mwanadamu dhidi ya sheria ya Mungu kama fursa kwa uvamizi wa maovu kwaasili ya mwanadamu. Neno “mwili” katika maandiko ya Paulo, yanaweza kumaanisha: (1) Mwili wa umbo ambao kimaoni hauna kitu (kama vile 1:3; 2:28; 4:1; 9:3,5) na (2) Asili ya dhambi iliyoanguka iliyorithiwa toka kwa Adam (kama vile mst .5).Tazama Mada Maalum “Mwili”(*sarx*) katika 1:3.

**7:20 “dhambi iishiyo ndani mwangu”**Inapendeza kuona kuwa kitabu cha Warumi kwa wazi kabisa kinaonyesha kuwa dhambi ya mwanadamu, lakini hakuna alipotajwa shetani hadi katika 16:20. Mwanadamu hawezi kumlaumu shetani kwa tatizo/kosa la dhambi. Tuna chaguo. Dhambi inafanywa kuwa mfalme, mtawala katili, Bwana wa watumwa.Inajaribu kutushawishi tusimtegemee Mungu, na tujitetee kwa gharama yoyote ile. Paulo kuifanya dhambi kama mtu aliunganisha chaguo la mwanadamu linaloakisi Mwa. 4:7.

Paulo anatumia neno “kuishi/kukaa” mara nyingi katika sura hii (kama vile mist. 17, 18, 20). Asili ya dhambi haiharibiwi au kuondolewa katika wokovu, bali ilifanywa kutokuwa na kazi. Kuendelea kutokuwa na nguvu yoyote

inategemea juu ya ushirikiano wetu na Roho aishiye ndani mwetu (kama vile 8, 9, 11). Mungu ametoa yale yote ya lazima kupambana na anayeitwa (fasihi) na wa nafsi (shetani na mapepo) uovu. Ni uwepo na nguvu ya Roho Mtakatifu. Kama tulivyokubali kupokea zawadi ya wokovu, kadhalika pia ni lazima tupokee zawadi ya Mungu ya matokeo ya Roho Mtakatifu. Wokovu na maisha ya Mkristo ni mchakato wa kila siku ambao unaanza na kuishia na maamuzi ya kila siku ya waumini. Mungu ametupatia vitu vyote tunavyotaka: vya Rohoni (Warumi 8), silaha ya kiroho (Efe. 6:11) Ufunuo, (Efe. 6:17) na ombi (Efe. 6:18).

Vita ni vikali (Warumi 7), lakini tunashinda vita (Warumi 8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 7:21-25**
**21 Basi nimeona shria hii, ya kuwa kwangu mimi nitaye kutenda lililo jema, lipo lililo 22 baya. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; 23 lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile shria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. 24 Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atayeniokoa na mwili huu wa mauti? 25 Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili sheria ya dhambi.**

**7:22 "sheria ya Mungu"** Kwa Wayahudi, hii alimaanisha sheria ya Musa. Kwa wasio Wayahudi, hii ilimanisha.

1. ushahidi wa asili (kama vile Rum. 1:19, 20; Zab. 19: 1,6)
2. dhamira zao za ndani (kama vile Rum. 2:14,15)
3. taratibu au kanuni za mira za kijamii

**NASB** **"mtu wa ndani"**
**NKJV** **"kufuatana na mtu aliye ndani"**
**NRSV, NJB** **"ndani yangu binafsi"**
**TEV** **"utu wangu wa ndani"**

Paulo anatofautisha mtu wa nje (umbile) na mtu wa ndani (Kiroho) katika Kor. 4:16. Katika mazingira haya, kifungu kinamaanisha ile sehemu ya Paulo au wanadamu waliookolewa wanaokubali mapenzi ya Mungu na sheria.

1. "sheria ni ya kiroho," 7:14
2. "ambacho ningependa nifanye," 7:15
3. "Nakubaliana na Sheria, na kukiri kuwa Sheria ni nzuri," 7:16
4. "uhitaji umo ndani mwangu," 7:18
5. "kizuri ninachokitaka," 7:19
6. "Ninatoa uovu ule ule ambao sikuutaka," 7:19
7. "Ninafanya kitu kile kile ambacho sikukitaka," 7:20
8. "yule ambaye alitaka kufanya kizuri," 7:21
9. "kwa furaha ninakubaliana na sheria ya Mungu,"7:22
10. "sheria ya fikra zangu," 7:23
11. "Mimi binfsi na fikra zangu ninatumikia sheria ya Mungu," 7:25

Sura 7 inaonyesha kuwa uelewa wa Mungu na neno lake pekee havitoshi. Waamini wanamhitaji Roho (sura 8)!

**7:23** Kuna tofauti halisi kati 6:2; 8:2 na7:23. Mstari huu kwa wazi unaonyesha matumizi ya Paulo ya sheria (*nomos*) kumaanisha. (1) sheria ya dhambi (kama vile mist. 21, 25) na (2). sheria ya Mungu (kama vile mist .22, 25). Ama katika mistari ya 4, 5,6,7,9 na 12, Paulo alitumia neno hili katika Agano la kale. Paulo hakuwa mwanathiolojia mwenye mpangilio. Alijishughulisha na dhana ya "sheria." Kwa maana moja ilikuwa ufunuo wa Mungu, zawadi ya ajabu kwa wanadamu, bado katika maana nyingine ilikuwa ni ile iliyo asilii ya dhambi na wazi wazi ikaweka mipaka ambayo mwanadamu aliyeanguka alishindwa kuitunza. Mipaka hii haikuwa tu, ufunuo wa Agano la kale (kama vile Zab. 19:7-14,119), bali miongozo yote ya kimaadili: ufunuo asilia,(kama vile Zab. 19:1-6, Rum. 1:18-3:31) au desturi na mila za kijamii. Wanadamu ni waasi ambao wanataka kutawala kabisa maisha yao;

**7:24** Je, Hii yaweza kuwa usemi kutoka kwa mtu aliyeokolewa? Wengine wanasema "hapana" kwa hiyo, sura hii inamaanisha mtu kimaadili, kidini na asiyeokolewa.Wengine wanasema ndiyo kwamba, inamaanisha mvutano wa injili, "walio, na wasio tayari" katika maisha ya waumini.Utimilifu wa hukumu ya kifo bado kabisa haijatimizwa.Muumini mkomavu anatambua kasoro hii vizuri kabisa.

**NASB "mwili wa mauti haya"**
**NKJV, NRSV "mwili huu wa mauti"**
**TEV "mwili huu unaonipeleka katika mauti"**
**NJB "mwili ukawa wa kufa"**

Umbo la mwili na fikra siyo viovu ndani na pia vyenyewe. Viliumbwa na Mungu viishi katika sayari hii, na kuwa na ushirika naye.Viliumbwa "vizuri sana" (kama vile Mwa. 1:31). Lakini, Mwanzo 3 ilibadili mwanadamu na sayari. Huu siyo ulimwengu Mungu alioukusudia uwe na sisi siyo wale watu Mungu aliokusudia tuwe. Dhambi imeathiri kabisa uumbaji. Dhambi imechukuwa kilichokuwa kizuri na kukigeuza kuwa kitovu cha maovu. Mwili na fikra zimekuwa uwanja wa vita vya majaribu na dhambi. Paulo anahisi vita kwa hakika. Anasubiria enzi mpya, mwili mpya, ushirika na Mungu (kama vile 8:23)

**7:25** Huu ni ufupisho na hatua kuelekea katika eneo la juu la Warumi 8. Hata katika sura ya 8 mvutano huu huu unaonekana katika mistari ya 5-11.

Swali kwa wafasili, linajitokeza kuwa Paulo anamzugumzia nani?

1. yeye binafsi na uzoefu wake ndani ya dini ya Kiyahudi
2. wakristo wote
3. Adamu kama mfano wa wanadamu
4. Israeli na uelewa wa Sheria, lakini bila kuitii

Binafsi, naunganisha # 1 (mist.7-13,25b) na # 2 (mist. 14-25a). Tazama, Mtazamo wa Ndani kwa Warumi 7:7, 25 maumivu na machungu ya sura ya 7 inaoanishwa na kupitwa juu ya sura ya 8.

◙ "Shukrani iwe kwa Mungu" Tazama Mada Maalumu ifuatayo:

## MADA MAALUM: SIFA ZA PAULO, MAOMBI, NA SHUKURANI KWA MUNGU

Paulo alikuwa ni mtu wa sifa. Alilifahamu Agano la Kale. Kila moja ya ile migawanyo minne (yaani., kitabu) ya mwisho wa Zaburi zenye nyimbo wa kumsifu Mungu (kama vile Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48). Watu wanao mjua Mungu humsifu na kumwinua mara zote.

1. Wakiwa wanaanza aya katika nyaraka zao
   a. Wakianza kwa Baraka au kwa salamu (kama vile Rum. 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2)
   b. Wakianza kwa dua (*eulogētos*, kama vile. 2 Kor. 1:3-4; Efe. 1:3-14)
2. Wakilipuka kwa shangwe fupi za sifa
   a. Rum. 1:25; 9:5.
   b. 2 Kor. 11:31
3. Nyimbo za Sifa (zikiainishwa kwa utumiaji wa[1] *doxa* {yaani., utukufu} na [2] "Milele na Milele")
   a. Rum. 11:36; 16:25-27
   b. Efe. 3:20-21
   c. Fil. 4:20
   d. 1 Tim. 1:17
   e. 2 Tim. 4:18
4. Shukrani (yaani., *eucharisteō*)
   a. Ufunguzi wa barua (kama vile. Rum. 1:8; 1 Kor. 1:4; 2 Kor. 1:11; Efe. 1:16; Fil. 1:3; Kol. 1:3,12; 1 The. 1:2; 2 The. 1:3; Filemoni 1:4; 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 1:3)

b. Wito wa kutoa shukrani (kama vile. Efe. 5:4,20; Fil. 4:6; Kol. 3:15,17; 4:2; 1 The. 5:18)

5. Wakilipuka kwa shangwe fupi za shukrani
   a. Rum. 6:17; 7:25
   b. 1 Kor. 15:57
   c. 2 Kor. 2:14; 8:16; 9:15
   d. 1 The. 2:13
   e. 2 The. 2:13
6. Wakihitimisha kwa dua
   a. Rum. 16:20,24
   b. 1 Kor. 16:23-24
   c. 2 Kor. 13:14
   d. Gal. 6:18
   e. Efe. 6:24

Paulo alimtambua Mungu wa Utatu kithiolojia na kiuzoefu. Katika uandishi wake alianza kwa maombi na sifa. Katikati ya uwasilishaji wake alilipuka kwa shangwe na shukrani. Katika hitimisho lake la waraka, siku zote alikumbuka kuomba, kusifu, na kumshukuru Mungu. Maandiko ya Paulo yana pumzi ya maombi, sifa na shukurani. Alimtambua Mungu, akajitambua mwenyewe, na kuitambua injili.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa vipi sura ya 6 inahusiana na ya 7?
2. Nini uhusiano wa sheria ya Agano Jipya na waamini wa Agano Jipya? (kama vile II Kor. 3:1, 11; Ebr. 8:7,13).
3. Ni vielelezo gani viwili, anavyovitumia Paulo katika sura ya 6 na 7 kuelezea uhusiano wetu na maisha yetu ya kale?
4. Ni vipi mkristo anahusishwa na sheria ya Musa?
5. Elezea kwa maneno yako mwenyewe tofauti ilioko kati ya nadharia za mtu kujiandikia historia ya maisha yake na ile ya uwakilishi katika kutafsiri Warumi 7:7-25.
6. Je, Warumi 7 ni maelezo kuhusu mtu aliyepotea, muumini mchanga au waumini wote?

# WARUMI 8

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI YA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Maisha Katika Roho | Kuwa huru kutoka Katika dhambi Iliyo ndani | Tendo la Mungu la Kuokoa | Maisha Katika Roho | Maisha Ya Roho |
| 8:1-11 | 8:1-11 | 8:1-4 | 8:1-8 | 8:1-11 |
| | | Maisha katika Mwili Na katika Roho | | |
| | | 8:5-8 | | |
| | | 8:9-11 | 8:9-11 | |
| | | Roho na kuasiri | | |
| 8:12-17 | 8:12-17 | 8:12-17 | 8:12-17 | 8:12-13 |
| | | | | Watoto wa Mungu |
| | | | | 8:14-17 |
| Utukufu Ujao Kuwepo | Kutoka katika mateso Kwenda utukufu | Tumaini la utimilifu | Utukufu Ujao | Utukufu kama Hatima Yetu |
| 8:18-25 | 8:18-30 | 8:18-25 | 8:18-25 | 8:18-25 |
| | | Udhaifu wa Kibinadamu Unashikiliwa | | |
| 8:26-30 | | 8:26-27 | 8:26-27 | 8:26-27 |
| Upendo wa Mungu | Upendo wa Mungu Wa milele | Kujiamini kwetu katika Pendo la Mungu | Upendo wa Mungu Katika Kristo | Wimbo wa Upendo Wa Mungu |
| 8:31-39 | 8:31-39 | 8:31-39 | 8:31-39 | 8:31-39 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura hii ni kilele cha hoja ya Paulo iliyoanza katika 1:18. Inaanza "hakuna laana" (msimamo wa kisheria) na unamalizia "hakuna utengano," (ushirika binafsi). Kithiolojia, inatoka kwenye uhalalisho kupitia utakaso hadi utukufu (kama vile mist 29-30)

B. Huu ni mwendelezo wa kithiolojia wa Paulo kuhusu Mungu kutoa roho yake kwa waumini (kama vile wasilisho la Yohana katika Yoh. 14:12-131; 16:7-16). Roho ni wakala wa KITENZI TENDEWA mst. 14 ambao unahusisha injili kuendelea kuimarika ndani ya binadamu walioanguka. Roho atafungamana nao na ndani yao, itaanza kumtengeneza Kristo. Sura ya 8 inatumia neno roho, *pneuma*, mara 21 wakati haimo kabisa katika sura ya 7 (hata sura 3-6 na inaonekana mara tatu katika sura 1-2 ni ngumu kuwa na uhakika wakati *pneuma* inapomaanisha roho ya mwanadamu au Roho Mtakatifu.

C. Katika maisha kuna mitazamo miwili (mitazamo binafsi ya ulimwengu), stadi mbili za maisha, vipaumbele viwili, njia mbili (njia pana na nyembamba) ambayo binadamu hufuata, hapa mwili au Roho. Moja inaenda mautini; na nyingine katika uzima. Hizi kiasili ilikuwa ikiitwa "njia mbili" za fasili ya hekima katika Agano la Kale (kama vile Zaburi 1 na Mithali 4:10-19). "Uzima wa milele", maisha ya Roho, ina tabia inayoonekana (yaani, baada ya mwili dhidi ya baada ya Roho).

   Tazama kutokuwepo kabisa kwa shetani katika mtazamo mzima wa kitheolojia (kama vile Rum. 1:8). Hasemwi kabisa katika Warumi hadi 16:20. Ni anguko la mwanadamu lenye asili ya Adamu lililoko katika mlengo. Hii ilikuwa njia ya Paulo kuondoa kisingizio cha mwanadamu aliyeanguka yaani - ("Shetani alinifanya nifanye hivyo") jaribu la nguvu ya giza kwa uasi wao dhidi ya Mungu. <u>Mwanadamu</u> anahusika mwenyewe.

D. Sura ni ngumu sana kuiandika kwa vile wazo limekuzwa kwa kuchanganya namna nyingi za ukweli pamoja katika mtindo wa kujirudia, bila kuwa na sehemu za mazingira hayo.

E. Mistari 12 -17 inamfahamisha muumini kuhusu uhakika wa imani thabiti.
   1. Ya kwanza ni badiliko la mtazamo wa kidunia na kukamilika kwa stadi ya maisha kupitia katika Roho
   2. Ya pili ni kwamba, hofu yetu ya Mungu imechukuliwa mbadala na maana ya upendo wa familia kwa Roho.
   3. Ya tatu ni uthibitisho wa ndani wa uwana kwa Roho mtakatifu aishie ndani.
   4. Ya nne ni kwamba uthibitisho huu ni zaidi ya ukweli katikati ya matatizo ya ulimwengu ulioanguka na mahangaiko.

F. Mistari 31-39 ni mtazamo wa kimahakama ambao ni mbinu halisi ya kiuandishi ya mtume wa Agano la kale. Mungu ndiye mtoa hukumu. Shetani ni mwendesha mashitaka , Yesu ni mwanasheria mtetezi, malaika ni wasikilizaji/watazamaji, imani ya wanadamu iko chini ya tuhuma ya shetani. (yaani Ayubu 1-2, Zakaria 3).
   1. Maneno ya kisheria
      a) Dhidi yetu (mist 31)
      b) Shauri (mst 33)
      c) Uthibitisho (mst 33)
      d) Hatiani (mst 34)
      e) Ombeeni (mst 34)
   2. Uendeshaji mashtaka "nani" (mistari 31 ,33, 34 [ mara tatu ],)

3. Kujitoa kwa Mungu katika kristo( mst 32,34b)
4. Hakuna utengano toka kwa Mungu.
   a) Mambo ya kidunia ( mst 35)
   b) Nukuu ya Agano la kale toka Zaburi 44: 22 (v. 36).
   c) Ushindi (mst 37,39)
   d) Mazingira ya nguvu za giza au wakala (mst 37-39).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 8:1-8**
**[1]Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. [2]Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. [3]Maana yale yasiyo wezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa mtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili, [4]ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusio enenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho. [5]Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. [6]kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. [7]kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. [8]wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.**

**8:1**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"Kwa hiyo yupo sasa"** |
| **KJV, NRSV** | **"yupo kwa hiyo sasa"** |
| **TEV** | **"yupo"** |
| **NJB** | **"Sababu, kwa hiyo"** |

Hii inahusisha kwa nyuma maandiko yaliyopita. Wengine wanaona inahusiana na 7:24-25. Lakini inakuwa ni vyema kurudi nyuma zaidi hadi 3:21-7:25.

◙**"hakuna"** "Hakuna" ni la kwanza katika sentensi ya Kiyunani. Linasisitiza, "hakuna hatia" kwa wale walio katika kristo. (kama vile mist 1-3) na wote wanaotembea katika Roho (kama vile 4-11) Hapa kuna pande mbili za patano jipya.

1. Ni kipawa cha bure katika kristo
2. Kuna stadi ya maisha, mwitikio wa patano unaohitajika.

Uhalalisho (kama vile 5:1-11) Kwa ujumla ni shabaha (ELEKEZI) na dhahania (SHURUTISHI) vyote ni hali na stadi ya maisha.

◙**"Hatia"** Neno *katakrima* halitumiki zaidi katika tafasiri za maandiko ya kale ya Kiyunani, lakini inaonyesha laana kwa kutoshiriki Katika Kumb. 27:26 (kama vile Kumb. 27:26 iliyonukuliwa katika Wagalatia. 3:10, ambalo ni sawa na "laana"). Hii ina maana, "adhabu kufuatia hukumu ya mahakama." Ni sheria, neno la kisheria kinyume na uhalalisho. Ni neno nadra katika maandiko ya Paulo (kama vile 5:16, 18) na halikutumika popote katika Agano jipya.

Dhana ya "laana" ilitokea kwa mara ya kwanza kwa Shetani akiwashitaki watu wa Mungu waliokiuka agano na baadaye watu wasio asili ya Waisraeli kama Ayubu. (kama vile Ayu. 1-2). Lakini sasa waumini wamekufa pamoja na kristo katika sheria (kama vile Warumi 6). Na kwa hiyo, sio sheria wala Shetani awezaye kulaumiwa. Tafsiri toka toleo la King James lililoongezwa katika mst 1. "atakayetembea si kwa ajili ya mwili bali Roho "fungu hili halionekani katika maandishi mengi ya zamani ya Kiyunani katika aya ya 1. Toleo la UBS[4] linatoa ondoleo la alama "A" (hakika). Inaonekana katika mst. 4. Kwa hakika sio sahihi kithiolojia katika mst.1, lakini inafaa kabisa katika mst 4. Mistari 1- 3 inashughulika na utakaso katika nafasi ya kristo (ELEKEZI) wakati mistari ya 4-11 inajihusisha na utakaso kwa mazoea (tazama mada maalumu katika 6:4) au kufanana na kiristo (SHURUTISHI, tazama mkuu katika

8:29).Tazama nukuu za awali katika ukurasa 289 katika kitabu cha *Romans verse by verse* cha William R. Newell, (Moody, 1938).

Toleo lililorekebishwa kiusahihi linaondoa neno "anayetembea si kwa mwili bali kwa Roho." Kwa vile tafsiri ya King James, zaidi ya miaka 300 iliyopita maandiko mengi mazuri, yaliyo sahihi kabisa maandishi ya kale ya Wayunani tuliyo nayo, yamepatikana, na watu wa Mungu wameenda zaidi bila kuyumba, na kazi ngumu, lakini yenye matunda ya kusahihisha yaliyojitokeza katika kunakili. Kwa vile, Kama wote tunavyofahamu, hatuna maandiko ya mwanzo/halisi ya mafundisho ya neno la Mungu. Mungu ameridhika kuzuia haya kutoka kwa viumbe walio dhaifu kwa maovu kama watoto wa Mungu.

Yatupasa kuhitimisha mstari wa kwanza kwa maneno, "katika Yesu kristo" kwa sababu nne (1) Ushahidi wa maadiko ya kiyunani kwa kiasi kikubwa yanapenda kuachwa kwa kishazi. "anayetembea,si kwa mwili, bali kwa Roho toka mst. 1, kwa vile ushahidi inahusisha maneno haya katika mst. 4. (2) Hata utambuzi wa kiroho pia unakubali, kwa vile utangulizi wa maneno haya toka mst.1, unafanya usalama wetu utegemee kutembea kwetu, na sio kutegemea Roho wa Mungu. Lakini wote katika Kristo ni salama kutoka katika laana. Kama inavyofundishwa wazi katika waraka wote. Vinginevyo, usalama wetu unategemea kutembea kwetu na sio nafasi yetu katika kristo. (3) Kishazi kwa uwazi kipo katika nafasi yake mwishoni mwa mstari wa 4, ambapo tabia za mwenendo wa muumini, na siyo usalama wake kutoka katika laana kumeelezwa. (4) Kwamba kishazi katika mwishoni mwa mstari 1, katika toleo la King James ni *ufafanuzi* (maelezo ya kukumbusha na baadhi ya wapiga chapa) inaonekana, sio tu ondoleo lake na maadiko makubwa, Aleph, A, B, C, D, F, G, A, D na machapisho ya zamani (tazama Olshausen, Meyer Alford, J. F na B., na mjadala mzuri wa Darby katika *Synopsis, in loc*); lakini pia inaonekana kutokana na usawa wa ufafanuzi huu kama nyongeza zilizo fanywa kupitia hofu za kisheria, zinazo patikana katika habari nyinginezo.

Kwamba Mungu alichagua kuwa na neno lake na kufasiliwa na bado mamlaka yanaonekana kutumika katika Agano jipya ya tafasiri ya kiyunani ya Agano la kale la Waebrania, wametumia muda wao wa maisha katika uchambuzi thabiti wa maandiko aliotuachia Mungu na ambao wametupa fasihi ya hakika ya ajabu tuliyo nayo. Lazima tutambue kabisa wanazuoni hawa,na daima wenye majivuno wa sasa (au, kwa siku za zamani, "Wanaharakati wa Juu"). Ambao wanathubutu kutuambia kile Mungu anachositahili kutuambia katika Biblia, kuliko katika hali ya kujishusha, kwa kujaribu kujua Mungu alichosema (uk. 289).

◙"**Kwa wale ambao wamo katika Kristo Yesu"** Aina hii ya fungu (yaani, KIELEZI CHA MAHALI) ya Paulo ni sawa na usemi wa kisasa "mahusiano binafsi." Paulo alijua, alipenda, alitumikia, na alifurahia katika Yesu. Injili ni ujumbe unaopaswa kuaminiwa na mtu wa kukalibishwa. Nguvu ya kuishi iliyotolewa kutoka katika uhusiano wake na Kristo aliyeinuka, ambaye walikutana njiani akielekea Damaskas (kama vile Matendo 9). Uzoefu wake na Kristo yalizidi thiolojia yake juu ya Yesu. Uzoefu wake uliotolewa usio katika siri za kitawa lakini katika huduma za kimisionari (Mdo. 28:18-20, Luka 24:47, Mdo. 1:8). Hali ya kumjua yeye, ni kumtumikia yeye. Ukomavu wa kikristo ni ujumbe, mtu, na stadi ya maisha. (tazama Nukuu katika 1:5).

**8:2 "Sheria ya Roho wa maisha . . . . sheria ya dhambi na ya kifo."** Hii ikimaanisha,

1. "Tofauti kati ya sheria ya dhambi, (kama vile Rum. 7:10,23,25) na sheria mpya ya Mungu (kama vile Rum. 7:6,22,25)
2. "Sheria ya upendo" (kama vile Yak. 1:25; 2:8,12) dhidi ya "Sheria ya Musa" (kama vile 7:6-12).
3. Enzi ya kale na enzi mpya
4. Agano la kale dhidi ya Agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34, Kitabu cha Agano Jipya cha Waebrania)

Mtindo huu wa kutofautisha vinakubaliana.

1. Sheria ya Roho wa uzima katika kristo dhidi ya sheria ya dhambi na mauti mst. 2
2. Kufatana na mwili dhidi ya kufatana na Roho mst. 4, &, 5.
3. Vitu vya mwili dhidi ya vitu vya Roho mst. 5.
4. Mawazo juu ya vitu vya mwili dhidi ya mawazo juu ya vitu vya Roho, mst. 5.
5. Mawazo juu ya mwili dhidi ya mawazo juu ya Roh, mst.6.
6. Vya mwili dhidi ya vya Roho. Mst.9.
7. Mwili uliokufa dhidi ya Roho inayoishi mst.10.
8. Lazima ufe dhidi ya kuishi mst.13.

9. Asiye roho wa utumwa dhidi ya Roho wa kurithi mst 15.

Usomaji wa Biblia wa NASB (uk.1645), una orodha ya kuvutia juu ya matumizi ya Paulo ya neno sheria" katika Warumi.

1. Mamlaka inayodhibiti, 8:2.
2. Sheria ya Mungu,2:17,20, 9:31;10:3-5
3. Torati , 3:21 b.
4. Agano la kale lote 3:19.
5. Kanuni 3:27.

◙

**NASB, NRSV,**
**NJB "amekuweka huru "**
**NKJV, TEV "alikwisha niweka huru"**

Mistari 2-3 ni ujumbe wa kithiolojia wa sura ya 6.

Kuna viwakilishi tofauti tofauti kadhaa vinavyotokea katika maandiko ya zamani ya Kiyunani.

1. "Mimi" inapatikana katika maandiko ya A, D, K & P.
2. "Wewe" inapatikana katika maandiko ya ℵ, B, F & G
3. "Sisi" inapatikana baadaye katika andiko la mwisho, Ψ

Waandishi wa UBS[4] wanakupa "wewe" (UMOJA) alama ya "B" (karibia kuwa hakika). UBS[3] iliipa alama "D" (ngumu kabisa). Utofautishi wa maandiko ulihusisha viwakilishi "sisi," "wewe" au "mimi/sisi" vinajirudia katika maandiko ya Paulo.

**8:3 "Kile sheria isingeweza kufanya"** Sheria ya Musa ni nzuri na takatifu, lakini ubinadamu ni dhaifu na utendaji dhambi (kama vile 7:12, 16). KITENZI hapa, KIVUMISHI *adunaton*, ambacho kinamaanisha "kutowezekana" (kama vile Mt. 19:26) Ebr. 6:4, 18;10:4; 11:6) lakini kinaweza kumaanisha, "pasipo nguvu" (kama vile Mdo. 14:8, Rum. 15:1). Sheria ilikuwa haina uwezo wa kuleta wokovu (kama vile Gal. 3:21). Kinyume chake, ilileta hatia, kifo na laana (kama vile Wagalatia 3).

◙ **"Dhaifu kama ilivyokuwa kupitia mwili."** Hii ndiyo hoja kuu ya Paulo katika sura ya 7. Sheria ya Mungu ni nzuri na takatifu, lakini wanadamu watenda dhambi, walioanguka, waasi hawawezi kutenda mahitaji yake. Paulo, tofauti na viongozi wa dini, alisisitiza matokeo ya Mwanzo 3. Viongozi wengi wa dini wanahamasisha maovu katika ulimwengu katika Mwanzo 3).

◙**"Mungu *alifanya* kwa kumtuma mwanaye pekee"** Kile ambacho binadamu aliyeanguka hangeweza kufanya, katika Agano la kale, Mungu alifanya katika Agano la Jipya (kama vile Yer. 31:31-34) Ezek.36:22-36) kupitia kwa Yesu (kama vile Isaya 53, Yohana 3:16). Badala ya mahitaji ya nje, Mungu alitoa Roho wa ndani, moyo mpya na fikra mpya. Patano jipya liko katika msingi wa toba na imani na kwa kazi ya kristo iliyomalizika, na sio kwa matendo ya wanadamu (kama vile Efe. 2, 8:9).Hata hivyo, mapatano yote mawili yalitarajia mfano mpya wa maisha ya kimungu (kama vile Efe. 1:4, 2:10).

◙**"Katika kufanana na mwili utendao dhambi"** Ukweli huu umesemwa katika Flp. 2:7-8,Yesu alikuwa na mwili wa kweli wa mwanadamu (lakini usio na asili ya dhambi).(kama vile Flp. 20:7-8, Ebr. 7:26) yeye yu nasi hakika. Alijaribiwa kwa njia zote kama sisi lakini bado hakuwa na dhambi (kama vile Waebrania 4:15). Anatutambua sisi, Anatuombea (kama vile 8:34; Ebr. 7:25; 9:24.

◙***"Kama toleo* kwa dhambi zetu"** Maneno yaliyosisitizwa yanajitokeza katika toleo la NJB na katika mwanzo wa toleo la NRSV. Dhana hii hii inasemwa katika 2 Kor. 5:21 na Pet. 2:24, Yesu alikuja kufa (Isa. 53:4-6, 10:12; Marko. 10:45).

◙**"Aliilaani dhambi katika mwili"** kifo cha Yesu kimwili kilibainishwa na kushughulikia tatizo la asili ya dhambi ya mwanadamu, na siyo matendo binafsi ya mwanadamu ( kama sheria ya Mungu ilivyofanya). Yalikuwa maisha yake, kifo chake, ufufuo wake, na kupaa kwake mbinguni kulikamilisha kusudi la Mungu la ukombozi wa milele (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29). Alituonesha pia kile binadamu wanaweza kuwa na wanapaswa kuwa (kama vile Yohana 13:15; Petro 2:21).

**8:4** Mstari huu yamkini unamaanisha patano jipya (kama vile Yn. 31:3:38 Ezek. 30:26-27). Inashughulika na maeneo mawili ya wokovu wetu.

1. Yesu alitimiza matakwa ya Agano la kale na kupitia imani katika yeye, haki hii inakwenda kwa waumini kama zawadi ya bure. Mbali na ufanisi wa mwanadamu; tunaiita hii kuwa ni uhalalisho au utakaso katika Kristo.
2. Mungu anawapa waumini moyo mpya, fikra mpya, na roho mpya. Sasa tunatembea katika Roho, na siyo katika mwili. Hii inaitwa "utakaso endelevu."

Ukristo ni patano jipya ambalo lina haki mbili (zawadi ya wokovu) na wajibu (kufanana na Kristo, kama vile 6:13). *Jarome Bible Commentary* (uk. 315) inafanya maoni sanifu ya kuvutia ambayo kwa WAKATI ULIOPO ENDELEVU na KIAMBATA MĒ vinaonyesha usemi wenye masharti ukimaanisha kuwa maisha kamilifu ya Mkristo hayatiririki tu kutokana na ubatizo. Sisi kama wanadamu tunao uchaguzi katika wokovu na uchaguzi katika kufanana na Kristo. Roho inaongoza na kutia moyo na wala hailazimishi kuendana nayo.

◙**"ambaye hatembei katika mwili, bali katika Roho?"** Utofauti kama huu unapatikana katika Gal. 5:16-25. Haki ya kisheria itakamilishwa na haki ya mtindo wa maisha. Moyo mpya na fikra ya Agano Jipya siyo msingii wa wokovu wetu, bali matokeo yake. Uzima wa milele una tabia inayo tazamika kama (Mt. 7)!

**8:5** Paulo anatofautisha maisha katika "mwili" na maisha katika "Roho" katika mst. 5-8 ("vitendo ya mwili" kama vile Gal. 5:19-21 na "tunda la Roho" kama vile 5:22-25). Tazama Nukuu kamili katika 8:2.

**8:6 "fikra zilizowekwa"** Wayahudi walitambua kuwa macho na masikio ni madirisha ya kuingia katika nafsi. Dhambi huanzia katika maisha ya kimawazo. Tunakuwa kama tulivyo kutokana na tunavyoishi (kama vile Rum 12:1-2, Flp 4:8). Paulo hakufuata kwa uhakika, mawazo ya kiasilia ya viongozi wa dini yaliyokuwa na "makusudi" mawili, (*yetzers*) katika binadamu. Kwa Paulo kusudio zuri halikuwa katika kiumbe kilichoanguka, bali katika badiliko. Kwa Paulo, ilikuwa Roho Mtakatifu aishie ndani, ambaye alianzisha mgongano wa ndani wa Kiroho, (kama vile Yoh. 16:7-14).

◙**"uzima"** Hii (*zoē*) ikimaanisha uzima wa milele, maisha mapya.

◙**"amani"** Neno hili awali lilimaanisha "kufungamanisha pamoja kile kilichovunjika" (kama vile Yn. 14:27; 16:33; Flp 4:7) Tazama Mada Maalum. Amani katika 5:1. Kuna njia tatu ambazo Agano Jipya linazungumzia Amani.

1. ukweli wa jambo wa amani yetu na Mungu kupiti kwa Kristo (kama vile Kol. 1:20).
2. Hisia zetu za kuwa sawa kwa Mungu (kama vile Yoh. 14:27; 16:33; Flp. 4:7)
3. Mungu, akiunganisha kuwa katika mwili mmoja kupitia Kristo, Wayahudi na Watu wa Mataifa (kama vile Efe. 2:14-17; Kol. 3:15)

**8:7-11** Paulo anamwelezea binadamu mbali na Mungu kwa njia kadhaa.

1. Uhasama juu ya Mungu, mst. 7
2. Isio na uelekeo na Mungu, mst. 7
3. kutokuwa na uwezo wa kumpendeza Mungu, mst. 8
4. Kiroho wamekufa ambapo kutasababisha kifo cha milele, mst. 10-11

Tazama usambamba katika Rum 5:6, 8 na 10.

**8:7**

**NASB, NRSV, "mawazo yaliyo katika mwili ni uhasama dhidi ya Mungu"**
**NKJV "mawazo ya kimwili ni uadui dhidi ya Mungu"**
**TEV "watu wakawa maadui wa Mungu"**
**NJB "hali ya kuvurugika kwa asili ya mwanadamu ni kinyume na Mungu''**

Tazama kuwa fungu hili ni sambamba na "fikra zilizowekwa juu ya mwili ni mauti" ya (kama vile mst.6) na "wale wanaotembea kutokana na mwili" ya mst. 5. Tazama pia kuwa anguko la asili ya mwanadamu ni suala la kifikra, mtazamo wa ulimwengu na matendo ya maisha. (kama vile 7:5). Tazama Mada Maalumu Mwili (*sarx*) katika 1:3.

◙**"kwa vile hapana uwezo hata kufanya hivyo"** mwanadamu aliyeanguka sio tu hachagui kumfuata Mungu bali, hawana uwezo wa kumfuata Mungu. Mwanadamu aliyeanguka, bila kusaidiwa na Roho Mtakatifu hawezi kukubali vitu vya kiroho (kama vile Isa. 53:6; 1 Pet. 2:24-25). Mungu lazima daima achukuwe hatua (kama vile Yn. 6:44,65). Hii haiondoi chaguzi za maagano, bali kwa wazi kabisa inatetea, kuwa wanadamu iwapo ni wapokeaji wala si waanzilishi

**8:8 "wale ambao wako katika mwili"** Paulo anatumia fungu hili katika njia mbili.
1. Mwili wa nyama (kama vile Rum 1:3; 2:28; 4:1; 9:3,5)
2. juhudi za mwanadamu kumweka mbali na Mungu (kama vile Rum 7:5; 8:4-5)

Hapa ni #2. Inamaanisha uasi, wanadamu wasio amini. Tazama Mada Maalum Mwili (*sarx*) katika 1:3.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 8:9-11**
**9 Lakini ikiwa Roho wa Mungu, anakaa ndani yenu, ninyi hamfuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo huyo si wake. 10 Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu I hai, kwa sababu ya haki. 11 Lakini, ikiwa roho wake yeye aliye mfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.**

**8:9 "kama"** kuna mfululizo wa SENTENSI ZENYE MASHARTI katika mst. 9:10; 11,13 (mara mbili), 17 (mara mbili). Zote ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambazo zinachukuliwa kuwa kweli kutokana na wazo la Mwandishi, au kwa kusudio lake la kiuandishi. Paulo alichukulia kuwa uandishi wake wote ulikuwa wa kikristo (kama vile mst. 9a).

◙**"Roho wa Kristo"** Watu ama wana Roho na au hawana Roho, kwa hiyo wamepotea kiroho. Tunapokea yote ya Roho Mtakatifu katika wokovu. Hatuhitaji sisi, bali yeye anatuhitaji!

Mafungu "Roho" ya 9a; "Roho wa Mungu"ya 9b na "Roho wa Kristo"ya 9c yote yanafanana.

## MADA MAALUMU: YESU NA ROHO

Kuna bubujiko kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan alisema jina zuri la Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine" (hata hivyo, tofauti yao, utu wa milele). Ufuatao ni mlinganisho wa mhutasari wa kazi na wadhifa wa Mwana na Roho.

1. Roho aitwaye "Roho wa Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. Wote wanaitwa kwa maneno sawa
   a. "kweli"
      1) Yesu (Yohana 14:6)
      2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
   b. "mwombezi"
      1) Yesu (1 Yohana 2:1)

2) Roho (Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7)
   c. "Mtakatifu"
      1) Yesu (Marko 1:24; Luka 1:35; Matendo 3:14; 4:27,30)
      2) Roho (Luka 1:35)
3. Wote hukaa ndani ya waamini
   a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17;Kol. 1:27)
   b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
   c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)
4. Kazi ya Roho ni kutoa ushuhuda juu ya Yesu (kama vile Yohana 15:29; 16:13-15)

**8:10 "kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA (ikiwa na KITENZI ELEKEZI "kuwa") Paulo anachukulia wasomaji wake yaaani kanisa katika Rumi kuwa
1. Kristo anakaa ndani mwao
2. Kuwa na Kristo miongoni mwao

◙**"Yesu yumo ndani mwenu"** Neno "mwenu" liko katika WINGI. Neno Kristo "lina maanisha Mwana/Roho aishiye ndani. (kama vile Yoh. 14:16-17; Kol. 1:27). Watu wana Mwana/Roho au wasio Wakristo (kama vile 1 Yoh. 5:12). Kwa Paulo, "katika Kristo" kithiolojia lina maana sawa na "katika Roho"

◙**"japo mwili umekufa kwa sababu ya dhambi"** Hata Wakristo watakufa kimwili kwa sababu ya dhambi ya Adamu, ulimwengu ulioanguka, na uasi binafsi (kama vile Mwanzo 5; Ebr. 9:27, Tazama Nukuu katika 8:13). Waumini wanaoishi katika enzi mpya ya Roho (kama vile Yoeli. 2:28-29; Mdo. 2:16). Na enzi ya kale ya dhambi na uasi (kama vile mst. 21, 35).

◙**"bado Roho yu hai kwa sababu ya haki"** Pamekuwepo kutokubaliana miongoni mwa Wakalimani na watoa maoni kwamba "Roho" inamaanisha roho wa mwanadamu (kama vile NASB, ASV, NIV, Williams, Biblia ya Yerusalem), au Roho Mtakatifu (kama vile KJV, TEV, REB, Karl Barth, C. K. Barrett, John Murray, Everett Harrison). Kwa mazingira haya, tunapanua zaidi kuelewa fungu hili fupi. Hata wale waliomwamini Yesu watakufa kwa vile wanaishi katika ulimwengu ulioanguka. Hata hivyo kwa sababu ya haki ambayo inakuja kupitia katika imani katika Yesu, tayari wana uzima wa milele (kama vile Efe. 2:4-6). Hii ni "tayari lakini bado" kwa hali ya Ufalme wa Mungu. Enzi ya Kale na enzi mpya vimeingiliana kwa wakati.

◙**"haki"** Katika mazingira haya ingeweza kumaanisha
1. haki ya kupewa, (uhalalisho na utakaso kwa nafsi) ukujiao kupitia imani katika Kristo (kama vile Rum. 4)
2. maisha mapya katika Roho (utakaso unaokuwa) ambao ndio ushahidi wa kuokolewa maisha. (Tazama Mada Maalum katika 1:17.

**8:11 "kama"** Tazama Nukuu katika mst.9.

◙**"Roho wake aliyemwinua Yesu kutoka katika wafu yu ndani yako"** Ni nafsi ipi ya utatu inayoishi ndani ya Waumini? Wakristo wengi wangejibu "Roho". Hii ni kweli kabisa, lakini kwa ukweli kabisa nafsi zote tatu zinaishi ndani ya muumini
1. Roho, Yoh. 14:16-17; Rum 8:11; 1 Kor 3:16; 6:19; 2 Tim 1:14
2. Wana, Mt. 28:20; Yoh. 14:29,23; 15:4-5; Rum 8:10; 2 Kor 13:5; Gal 2:20; Efe. 3:17; Kol 1:27
3. Baba, Yoh. 14:23; 2 Kor 6:16

Fungu hili ni fursa nzuri ya kuonyesha kwamba Agano Jipya daima linaunga mkono kazi ya ukombozi kwa nafsi zote tatu za utatu
1. Mungu Baba alimwinua Yesu (kama vile Mdo. 2:14; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum 6:4,9; 1 Kor 6:14; 2 Kor 4:14; Gal 1:1; Efe 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10)s
2. Mungu Mwana alijiinua mwenyewe (kama vile Yoh. 2:19-22; 10:17-18)

3. Mungu Roho alimuinua Yesu (kama vile Rum 8)

Msisitizo huu wa utatu unaweza kuonekana katika mist. 9-11.

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
   1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
   2. Yohana 14:26
B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
C. Paulo
   1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
   2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
   3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
   4. Gal. 4:4-6
   5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
   6. 1 The. 1:2-5
   7. 2 The. 2:13
   8. Tit. 3:4-6
D. Petro – 1 Pet. 1:2
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
   1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
   2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
   1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
   2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
   3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   4. Zakaria 3:1-2
B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Flp. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa

Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

◙ **Pia itaupa uzima mwili wako uliokufa** KITENZI hiki kinaonyesha KAULI TENDAJI ELEKEZI LA WAKATI UJAO ambalo ni kuelekea siku ya ufufuo. Ufufuo wa wote, Yesu na wafuasi wake ni mafundisho muhimu. (kama vile 1 Kor. 15:1ff, 2 Kor. 4: 14). Wakristo wanatetea kuwa, waaminio watakuwa na mwili wa umilele. (kama vile 1 Yoh. 3:2. Kama Yesu aliinuliwa na Roho (kama vile 1 Kor. 15:12-21), kadhalika wafuasi wake watainuliwa pia (kama vile mst.23).

◙
**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB,**
**REB, NET** **"kupitia katika Roho wake"**
**NRSV tanbihi** **"kwa mujibu wa Roho wake"**
**TEV** **"kwa uwepo wa Roho wake"**

Kuna utofauti wa maandiko katika namna ya fasihi ya fungu hili.

1. Uhusiano, MSS א, A, C, P.
2. Kuonesha nafsi MSS B,D F.G.

UBS[4] inaupa uhusiano huo "B" alama B (karibia uhakika).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:12-17**
**[12]Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili; [13]kwa maana kama mkiishi kwa kufuata mabo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi. [14]Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. [15]Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlimpokea roho ya kumfanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. [16]Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; [17]na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.**

**8:12 "kisha**" Paulo anaendelea kuonyesha umuhimu wa uwasilishi wake katika mst. 1- 11.

◙ **"Tupo chini ya shuruti.** Huu ni upande mwingine wa uhuru wa mkristo. (kama vile 14:1-15: 13).Hili ni hitimisho la mjadala juu ya utakaso. Katika mst. 1-11, ambayo ni hali ya kuonyesha mahali (ELEKEZI) na hali ya kuendelea (SHURUTISHI, Tazama mada maalumu katika 6:4). Bado inaonyesha kuwa waumini lazima wapambane na asili ya anguko la zamani (yaani 6:12,19; 7:7- 24, 1 Kor. 6:18-19; Efe. 6:10-19). Kuna uchaguzi ambao unabidi ufanyike (imani ya kwanza) na chaguzi zinazoendelea ili kufanyika (imani ya mtindo wa maisha).

**8:13 "kama"**kuna mfululizo wa SENTENSI ZENYE MASHARTI katika mst.9, 10,11 ,13 (mara mbili) na 17 (mara mbili). Zote ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambazo zinadhaniwa kuwa kweli kwa mujibu maoni ya mwandishi au kwa makusudi ya uadishi wake.Paulo alidhani kuwa wasomaji wake katika kanisa la Rumi walikuwa wakristo walioishi kwa Roho. Lakini palikuwa na mengineyo (ushirikiano wa wanadamu).

◙**"Unaishi kufuatana na mwili, lazima ufe"** VITENZI vyote katika mst. 13 viko katika WAKATI ULIOPO, ambavyo vinazungumzia tendo linaloendelea. Biblia inabainisha hatua tatu za kifo.

1. Kifo cha kiroho (kama vile Mwa. 2:17 ;3 :1 -7 ; Efe. 2:1).
2. Kifo cha mwili (kama vile Mwanzo 5).
3. Kifo cha milele (kama vile Ufu. 2:11; 20:6, 14: 21: 8).

Kinachozungumzwa katika habari hii ni kifo cha kiroho cha Adamu. (kama vile Mwa. 3:14-19), ambacho kiliibua kifo cha mwili wa wanadamu wote. (kama vile Mwanzo 5).

Dhambi ya Adamu ilileta kifo katika mazoea ya mwanadamu (kama vile 5:12 -21). Kila mmoja wetu amechagua kushiriki katika dhambi kwa dhamira yake. Kama utachagua kubaki ndani yake (dhambi) itatuua "milele" (kama

vile Ufu 20: 6, 14, “kifo cha pili.” Kama wakristo sharti tufe kwa utambulisho wa imani kwa kristo, kwa dhambi, nafsi na kuishi kwa Mungu (kama vile Warumi 6)

◙**“Kama kwa Roho tunaweka matendo ya mwili katika mauti, utaishi”**Uhakika wa wokovu wa waumini unadhihirishwa na mtindo wa maisha yao wenyewe. (vitabu vya Agano Jipya vya Amos na 1 Yohana). Waumini hawaishi maisha haya mapya kwa juhudi zao bali kwa uwakala wa Roho. (kama vile mst. 14). Hivyo ni sharti wajitoe siku zote kwa utawala wake. (kama vile Efe. 5:17- 18 :6 :10-18). Katika mazingira haya “matendo ya mwili yanaonekana kama mazingira ya zamani ya enzi ya dhambi (kama vile Gal 5 :19 -21). Hii sio kukataa kupokea hali ya mwili kuwepo katika umilele (kama vile 8:23), bali ni utofauti kati ya Roho aishie ndani (enzi mpya) na mwendelezo wa mapambano ya kiroho na dhambi (enzi ya kale).

◙**“Wote wale wanaoongozwa na Roho wa Mungu.”**Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU YA WAKATI ULIOPO, ambayo inaoonesha kuendelea kuongozwa na Roho aliye ndani.” Roho anatubembelezea kwa Kristo (Yn. 6:44- 65), na kisha kuunda kristo ndani yetu. (kama vile mst. 29-30). Kuna kitu katika ukristo zaidi ya uamuzi. Hasa hasa ni utume unaoendelea (kama vile Mt 28:19), ambao unaanza na uamuzi. (kama vile 10: 9 -13; Yoh. 1: 12; 3:16). Hii haina maana ya matukio muhimu, nyakati au makundi ya watu wanaohudumu, bali matendo ya kila siku. (Tazama mada maalumu, katika tofauti katika www.freebiblecommentary.org. Neno UMOJA lilitumika na Adamu, Israeli, mfalme wake, na Masiha. Hapa ana maanisha waumini wote (kama vile Gal. 4:6 -7). Katika mst. 14, neno la Kiyunani *huioi* (wana), limetumika, katika mst. 16 *tekna* (watoto). Yanatumika tofauti katika mazingira haya. Waumini si watumwa tena bali watu wa familia moja. (kama vile mst. 15- 17; Gal. 4:7).

**8:15 “Roho”** mstari huu kama wa 10 ni tata, unaweza kumaanisha, roho mpya ya mwanadamu kwa kristo, au Roho mtakatifu.Yote yanapatikana katika mst wa 16. Kuna maeneo kadha wa kadha katika maandiko ya Paulo ambapo mwendo huu wa kifasihi umetumika kuelezea ni kitu gani Roho mtakatifu anasababisha katika muumini.

1. Hapa “sio shauku ya utumwa” bali moyo wa kurithi mst wa 15.
2. “Moyo wa upendo na upole.” 1 Kor. 4: 21
3. “Moyo wa imani.” 2 Kor. 4: 13
4. “Moyo wa hekima na wa ufunuo.” Efe. 1: 17.
5. “Sio moyo wa uoga.” 2 Timotheo. 1: 7.

Kuna maeneo mbalimbali hasa katika 1 Wakorintho.ambapo Paulo anatumia *neno pneuma* kujisema yeye binafsi (kama vile 1 Kor. 2:11; 5: 3; 14; 7: 34; 16:8 na Kol. 2:5). Katika mazingira haya hakika mst. 10 na 15 inafaa hapa.

◙**“ya utumwa kuelekea kwenye uoga tena”** Tabia ya asili ya zamani ni uoga. Tabia ya asili mpya imeelezwa katika mstari 14- 17.

◙**“Kurithiwa kama wana”** Sheria ya warumi ilifanya suala la kurithi kuwa gumu sana, lakini lilipofanyika mara moja, likawa la kudumu. (kama vile Gal. 4:4 -6). Sitiari hii inaunga mkono ukweli wa kithiolojia wa usalama wa muumini (Tazama mada maalum katika 5:2). Mwana halali ana weza kuachwa, lakini sio mwana aliye rithiwa. Hii ilikuwa mojawapo ya sitiari pendwa ya Paulo kuelezea wokovu (kama vile mst. 15, 23). Yohana na Petro walitumia sitiari zingine za kawaida, “kuzaliwa upya” (kama vile Yn. 3: 3; 1 Petro. 1: 3, 23). Kwa nukuu zote kamili tazama, Gal. 4: 5 katika tofauti www. freebiblecommentary.org

◙**“Abba”** Neno la kiarama lililotumiwa na watoto kuwaita baba zao nyumbani (“baba au Papa”). Yesu na mitume wake walizungumza kiarama (kama vile Marko 5 :41 ;14 :36 ; 1 Kor. 16:22). Waumini wanaweza sasa kuja kwa Mungu mtakatifu kwa njia ya damu ya kristo, kupitia kwa Roho aishie ndani, katika imani dhabiti na kujiamini kawaida (kama vile Marko. 14: 36 ; Gal. 4: 6). Sio jambo la kushanga kuwa, wanadamu walioanguka wanaweza kumwita Mungu, Baba, na kwamba mtakatifu huyo wa milele angependezwa nalo! Tazama mada maalumu, Baba katika 1 :7.

**8: 16 "Roho, yeye pekee"** neno la kiyunani la Roho ni LISILO NA JINSI- kwa hiyo, KJV lilifasili kama "Roho pekee," lakini Roho ni mtu/ nafsi. Anaweza (kama vile Efe. 4: 30 kuhuzunika; 1 The. 5:19), kwa hiyo "Yeye binafsi," ni fasili nzuri zaidi. Tazama mada maalumu ubinafsi wa Roho katika 8:27.

◙**"Anashuhudia na roho zetu kuwa tu watoto wa Mungu"** Kama ilivyoonyeshwa katika mst. 13 kigezo kimoja cha mthibitisho wa imani ni kubadilika kwa muumini na mbadiliko wa maisha yao (kama vile Vitabu vya Agano jipya vya Amosi na 1 Yohana ). Kigezo kingine cha uthibitisho ni kuomba, Roho anayeishi ndani yao amechukuwa nafasi ya uoga kwa Mungu, kwa upendo wa familia. (kama vile 1 Yoh. 4: 17 -18).
Tazama fasili na alama za semi za RSV na NRSV "Tunapo lia ni Roho peke yake anaye shuhudia na roho zetu kuwa tu watoto wa Mungu." (kama vile Gal. 4 :6). Hii ina maana kuwa, uthibitisho unapokuja pale unapomwita Mungu, Baba kwa Roho. Ushuhuda wa ndani ya Roho hausikiki, bali ni kitendo.

1. Kosa juu ya dhambi.
2. Hamu ya kuwa kama kristo.
3. Hamu ya kuwa na familia ya Mungu.
4. Njaa kwa neno la Mungu.
5. Kujisikia kutoka kueneza injili.
6. Kujisikia kutaka kutoa kwa Mungu kama kristo.

Haya ni kama shauku za ndani zinazoonyesha mabadiliko ya kiimani.Uthibitisho wa wokovu umegeuzwa kuwa suala la kimathehebu.

1. Kithiolojia ya kikatoliki inapinga uwezo kama wa uthibitisho wa maisha kwa njia hii, bali wanaweka imani yao kwa mtu mmoja ambaye ni mmojawapo wa kanisa la "kweli."
2. John Calvin (mageuzi ya kijadi) alizingatia uthibitisho katika uchaguzi (kabla ya kufika mwisho), lakini mtu agejiweza kupata hakika hadi baada ya maisha haya siku ya hukumu.
3. John Wesley (utamaduni wa kimethodisti), walizingatia uthibitisho katika upendo halisi (kuishi juu na zaidi ya dhambi inayofahamika).
4. Wabaptisti wengi wamejaribu kuona uthibitisho katika ahadi za Biblia za Neema ya bure (lakini wakipuuza maonyo yote na ya kitabia).

Kuna hatari mbili zinazohusu utata wa kuwasilisha uthibitisho katika Agano jipya.

1. Kusisitiza kupita kiasi kuhusu "ukiokolewa tu, umeokolewa wakati wote"
2. Kusisitiza kupita kiasi kwa matendo ya binadamu kudumisha wokovu.

Waebrania 6 waziwazi inafundisha "ukisha kuwa nje, siku zote utakuwa nje."Juhudi za binadamu (kazi nzuri) hazimwokoi mwanadamu (kama vile Gal. 3: 1 -14). Lakini kazi nzuri ndilo lengo la maisha ya mkristo. (kama vile Efe. 2: 10). Ndio matokeo halisi ya kumpata Mungu na kuwa na Roho aishiye ndani. Ni ushahidi wa mtu kuhusu mabadiliko ya kweli. Uthibitisho hauna maana ya kurahisisha wito wa Mungu katika utakatifu. Kithiolojia, uthibitisho unatokana na tabia na matendo ya Mungu wa utatu.

1. Upendo na huruma ya baba.
2. Kazi ya sadaka ya mwana iliyotimilika.
3. kilio cha Roho kwa kristo na kumfanya kristo ndani ya muumini anaye tubu.

Ushuhuda wa wokovu huu ni badiliko la mtazamo wa ulimwengu; badiliko la moyo, badiliko la mtindo wa maisha, na badiliko la tumaini. Haiwezi kutokana na uamuzi wa hisia zilizopita, zisizo na ushahidi wa mtindo wa maisha. (yaani, tunda kama vile Mt 7: 15 -23; 13: 20- 22) Yoh. 15. Uthibitisho kama wokovu, kama maisha ya mkristo unaanza na kupokea huruma ya Mungu, na kuendeleza mapokeo haya kwa maisha yote. Ni badiliko, na kuendelea kubadilisha maisha kiimani.

◙**"shuhuda"** Hili neno *syn* ni neno lingine la kimuunganikano. Roho anashuhudia ndani ya roho ya muumini.Paulo anatumia miunganikano hii ya neno katika 2: 15; 8: 16 na 9: 1.

**8: 17 "kama"** Ni mfululizo wa SENTESI ZENYE MASHARTI katika mist 9,19,11,13 (mara mbili) na 17 (mara mbili). Zote ni SENTESI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambazo zina chukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa lengo la uandishi wake. Paulo alichukulia tu kwamba, wasomaji wake katika kanisa la

katoliki walikuwa wakristo. Katika mstari huu, kuna maneno matatu yaliyo ungana yakitumia neno *syn*, yanayomaanisha "muunganikano wa ushirikishi" na

1. Waumini wanagawana kwa urithi wa (mali mjane) na kristo.
2. Waumini wanagawana mateso na kristo
3. Waumini watagawana utukufu na kristo.

Kuna maneno zaidi yaliyo ungana katika mistari ya 22 (mara mbili), 26, 28. Efe. 2:5 -6 pia yana maneno matatu yenye neno *syn* yaliyoungana ambazo yakielezea maisha ya waumini katika kristo.

◙**"Warithi"** Hii ni jamii ya maneno mbadala kwa waumini (kama vile 4: 13; 14: 9: 8 ; Gal. 3: 29). Tazama mada maalumu ifuatayo.

## MADA MAALUM: URITHI WA MWAMINI (toka 1 Petro 1)

Katika Agano la Kale kila kabila isipokuwa la Walawi lilipokea urithi wa ardhi (kama vile Yoshua 14-22). Walawi, kama kabila la kikuhani, wahudumu wa hekaluni, na waalimu wa kanisa la mahali, walionekana kuwa na YHWH Mwenyewe kama mrithi wao (kama vile. Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Wimb. 3:24). Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walichukua haki na upendeleo wa Walawi na kuitumia kwa waamini. Hii ilikuwa ni njia yao ya kudai kuwa wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa Mungu na kwamba sasa waamini wote wameitwa kutumika kama makuhani mbele za Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), kama Agano la Kale linavyo watetea Waisrael wote(kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio juu ya mtu binafsi kama kuhani aliye na upendeleo Fulani, bali ni katika kweli kwamba waamini wote ni makuhani, wakihitaji ushirika wa mwenendo wa kitumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamekwisha pewa majukumu ya Agano la Kale ya kueneza injili ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Lk 24:46-47; Mdo 1:8; angalia Mda Maalum: Mpango wa YHWH wa ukombozi wa Milele).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwa sababu alikuwa ni wakala wa Baba kipindi cha uumbaji (kama vile. Yn 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wenza kwa vile Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24). Maandiko yanazungumza kuhusu kurithi kwa waamini (kama vile Mdo 20:32; 26:18; Efe. 1:4; Kol. 1:12; 3:24) vitu vingi kwa sababu ya mahusiano yao ya kifamilia na Yesu ambaye ndiye mrithi wa vitu vyote (kama vile Ebr. 1:2). Kwa hiyo, wao pia ni warithi wenza (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7) wa

1. Ufalme (kama vile Mt. 25:34, 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Efe. 5:5)
2. Maisha ya milele (kama vile Mt. 19:29; Ebr. 9:15)
3. Ahadi za Mungu (kama vile Ebr. 6:12)
4. Ulinzi wa Mungu wa ahadi zake (kama vile 1 Pet. 1:4-5)

◙**"Mrithi mwenza"** Hii ni muungano mwingine wa neno *sun*, Paulo, alitumia maneno haya kwa wingi katika sura ya 8 kusisitizia mgawano wa kifo na maisha ya kristo na waunimi.

1. Walithi-pamoja na mst. 17
2. Wateswa-pamoja na mst. 17.
3. Watukuka-pmoja na mst. 17

◙

**NASB, NKJV** **"kama tuna teswa kabisa naye"**
**NRSV** **"kama, kusema kweli, tunateseka naye"**
**TEV** **"endapo kama tunagawana mateso ya Yesu"**
**NJB** **"kugawana mateso yake"**

Mateso ni jambo la kawaida kwa waumini katika ulimwengu ulioanguka (kama vile Mt 5: 10- 12; Yoh. 15:18-21; 16: 1- 2; 17: 18. Mdo. 14: 22; Rum 5:3- 4; 8:17; 2 Kor 4: 16- 18; Flp. 1: 29; 1 The. 3: 3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1: 2-4; 1 Pet. 4: 12-19). Yesu aliweka utaratibu (kama vile Ebr. 5: 8. Sura zingine zote zinachukuwa dhima hii. Tazama mada maalum kwa nini waumini wanateseka! Katika 5:3.

◙**"Wakatukuka pamoja naye"** katika maandiko ya Yohana, popote Yesu alipozungumzia kifo chake, alikiita "kutakasika" Yesu alitakaswa kwa kuteseka kwake.Waumini kwa nafasi yao kwa kristo ama kwa mazoea, wanagawana matukio ya maisha ya Yesu (kama vile Warumi 6).

Tazama mada maalumu: kutawala katika ufalme wa Mungu katika 5:17-18.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:18 -25**
**[18]Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakofunuliwa kwetu. [19]Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingine kufunuliwa kwa wana wa Mungu. [20]Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili; si kwa hiari yake, ila kwa sababu yake yeye aliyevitiisha katika tumaini; [21]kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika huru wa utukufu wa watoto wa Mungu. [22]Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa. [23]Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu. [24]Kwa maana tulio okolewa kwa taraja; lakini kitu kilichotarajiwa kikionekana, hakuna taraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho? [25]Bali tukikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi.**

**8:18 "Fikiria"** Kihalisia hii ni "kuongeze juu ya." Ni KITENZI CHA KATI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO. Paulo anaendelea kufikiria athari za mateso ya kristo. Hii ilikuwa neno muhimu linalochangia katika kufikia kwa wangalifu hitimisho lililofanyiwa utafiti / uchunguzi. Hii ni dhima inayojirudia katika warumi (Taz. Nukuu katika 2:3). Waumini sharti waishi katika uelewa wa ukweli wa kiroho unao ufahamu.

◙**"Mateso"** Tunapata mawazo kadha ya mateso yaliyohusika katika kumtumikia kristo kutoka 1 Kor. 4: 9- 12; 2 Kor. 4: 7 – 12; 6: 4- 10; 11: 24- 27; Ebr. 11: 35- 38.

◙**"Kwa wakati uliopo"** Wayahudi waliamini kuwa, historia ya ulimwengu imegawanyika katika enzi mbili, Enzi iliyopo ya maovu, na enzi ijayo ya haki (kama vile 12: 32; Marko 10: 30). Agano la kale lilitegemea kuja kwa Masia, kutaunda enzi mpya ya haki, hata hivyo aina mbili za ujio wa Yesu, kwanza kama Mwokozi (katika sura ya binadamu) na pili kama Bwana (ujio wa pili) kulisababisha kuingiliana kwa enzi hizi mbili. Waumini wanaishi kwa wasiwasi kati ya enzi iliyoko tayari au na ile " iliyo bado," kwa ufalme wa Mungu. Tazama mada maalumu "Enzi hii na Enzi itakayo kuja" katika 12:2.

◙**"Wa thamani …. Utukufu"** Maneno yote mawili yana husiana na dhana ya "Uzito" katika Agano la kale. Kizito kilikuwa na thamani. "Thamani," lilikuwa neno la kibiashara kwa maana ya "kuwa na uzito sawa na." Neno la kiebrania –"utukufu" hutokana pia na thamani, kama dhahabu. Taz, nukuu kamili katika 3: 23.

Neno "Utakatifu" katika maandiko ya Paulo yalikuwa na maelezo ya mambo yajayo (kama vile 2 Kor. 4: 16-18). Kurudi kwa Yesu mwana, mwenye nguvu na mamlaka (kama vile Kol. 3: 4), Tazama mada maalum utukufu katika 3: 23

◙**"Hilo litabainishwa kwetu"** Hii ni IRABU TENDEWA (enye kushuhudia), ilimaanisha uwakala wa Mungu au Roho (kama vile mst. 20), waumini wanaishi katika maisha haya kwa imani siyo kwa kuona (kama vile mst 24, 1 Kor. 2: 9; 13:12; 2 Kor. 5: 7; Ebr. 11: 1).

Neno limetumika mara kadha katika Warumi na Paulo anasisitizia kuwa ukweli unatoka kwa Mungu si uvumbuzi wa mwanadamu.

1. Kitenzi.
    a. 1: 17 – Haki ya Mungu imebainishwa (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO).
    b. 1: 18 – Hasira ya Mungu imebainishwa (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO).
    c. 8: 18 - Utukufu ujao utabainishwa (KAULI TIMILIFU TENDEWA ISIO NA MWISHO).
2. NOMINO.

a. 2: 5- katika siku ya hasira, na ufufuo wa hukumu ya haki ya Mungu.
b. 8: 19- Uumbaji una subiri kwa hamu kwa wana wa Mungu.
c. 16 : 25- Kufuatana na ufufuo wa maajabu.

◙ **8:19 "Shauku ya uumbaji unaosubiliwa kwa hamu"** Uumbaji kimaumbile, unafananishwa na mtu aliyenyoosha shingo lake kutazama mbali. Uumbaji ulipata athari hasi wakati Adamu na Hawa walipoasi; (kama vile Mwa 3: 17 – 19). Uumbaji wote utumiaye utakombolewa (isipokuwa wakala wa uasi) malaika, wanadamu wasioamini, na eneo lao lililotengwa (kama vile Bruce corley na Curtis Vaughan Warumi – uk. 95 nukuu asili 46).
Kitenzi "subiri kwa hamu" KITENZI CHA KATI [chenye kushuhudia] ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO wakati uliopo kinaonekana mara tatu katika mazingira haya.

1. Mst. 19 - Uumbaji una subiri kwa hamu enzi mpya.
2. Mst. 23- Waumini wana subiri kwa hamu miili mipya.
3. Mst. 25 - Waumini wana subiri kwa tumaini, enzi mpya.

Paulo anatumia kitenzi hiki kwa imani ile katika 1 Kor. 1: 7; Gal. 5: 5; Flp. 3: 20. Ujio wa pili si tukio la kuogopa kwa waumini, bali muungano mpya wa familia.

## MADA MAALUM: MALI ASILI

I. Utangulizi
   A. Uumbaji wote ni tone au hatua kwa upendo wa Mungu unaomuunga mwanadamu.
   B. Inashirikisha anguko (kama vile Mwanzo. 3:17; 6:1 na kuendelea; Rum. 8:18-20). Pia inashirikisha ukombozi katika matukio ya siku za mwisho (kama vile Isa. 11:6-9; Rum. 8:20-22; Ufu. 21-22).
   C. Asili ya dhambi, anguko la mwanadamu lilichukua mazingira ya asili kwa ajili ya kuyaweka mbali. Ifuatayo ni nukuu kutoka *The Canon of Westminster* by Edward Carpenter. ". . . ulegevu wa mwanadamu katika muktadha wa kidunia, juu ya ulimwengu kumzunguka—yaani uumbaji wa Mungu—kushambuliwa kwa hewa inayochafuliwa; njia za maji zinazoharibiwa; udongo unaotiwa sumu; misitu inayokatwa na kuvunwa, inatengeneza na kusuka athari za muda mrefu za uharibifu. Kushambuliwa huku ni kipande cha chakula kisichoratibiwa. Hali ya kutojali inafanywa bila kuzingatia kujali mazingira na matokeo yake uwajibikaji mdogo kwa kizazi kimoja unapelekea kuaribika kwa kizazi kingine."
   D. Si tu kwamba tunavuna matokeo ya uchafuzi wa hali ya hewa kwenye sayari yetu, lakini vizazi vyetu vinavyofuata wanavuna matokeo mabaya zaidi yasiyoweza kurekebishika.

II. Vitu vya Kibiblia
   A. Agano la Kale
      1. Mwanzo 1-3
         a. Uumbaji ni mahali maalum palipoumbwa na Mungu kwa ajili ya kuwa na ushirika na mwanadamu (kama vile Mwanzo 1:1-25).
         b. Uumbaji ni mzuri (kama vile Mwanzo. 1:4,10,12,18,21,25), ndio, nzuri sana (kama vile Mwanzo. 1:31). Imekusudiwa kuwa ushuhuda kwa Mungu (kama vile Zaburi 19:1-14).
         c. Ubinadamu ni kusudi la kutiwa taji la uumbaji (kama vile Mwanzo 1:26-27).
         d. Ubinadamu umekusudiwa kufanyia kazi mamlaka (Kiebrania, "kuwa juu") kama mawakili wa Mungu (kama vile Mwanzo. 1:28-30; Zab. 8:3-8; Ebr. 2:6-8). Mungu anabaki na anaendelea kuwa Muumbaji/Mtoshelevu/ Mkombozi/Bwana wa uumbaji (kama vile Kut. 19:5; Ayubu 37-41; Zab.24:1-2; 95:3-5; 102:25; 115:15; 121:2; 124:8; 134:3; 146:6; Isa. 37:16).
         e. Uwakili wa kibinadamu wa uumbaji unaweza kuonekana. 2:15, "kuipalilia na kuutunza na kuulinda" (Kama vile Mambo ya Walawi. 25:23; I Nyakati. 29:14).
      2. Mungu anapenda uumbaji, hasa wanyama.
         a. Sheria ya Musa kwa ajili ya kutunza wanyama

b. YHWH anamuumba Leviathani kucheza ndani ya bahari (kama vile Zab. 104:26)
c. Mungu anajali wanyama (kama vile Yona 4:11)
d. uwepo wa asili ya matukio ya siku ya mwisho (kama vile Isa. 11:6-9; Ufu. 21-22)

3. Asili kwa sehemu fulani inamtukuza Mungu.
   a. Zab.19:1-6
   b. Zab. 29:1-9
   c. Ayubu 37-41
4. Asili ni namna ambayo Mungu anaonesha upendo wake na uthamini wake kwa Agano.
   a. Kumb. 27-28; I Wafalme 17
   b. kipindi chote cha manabii

B. Agano Jipya
   1. Mungu anaonekana kama muumbaji. Kuna muumbaji mmoja tu, Utatu Mtakatifu wa Mungu (Elohimu, Mwanzo. 1:1; Roho, Mwanzo. 1:2; na Yesu, Agano Jipya). Vingine vyote vinaumbwa
      a. Mdo.17:24
      b. Waebrania 11:3
      c. Ufunuo 4:11
   2. Yesu ni wakala wa uumbaji
      a. Yohana 1:3,10
      b. I Kor. 8:6
      c. Kol. 1:16
      d. Ebr. 1:2
   3. Yesu anazungumzia ujali wa Mungu kwa asili katika namna ya moja kwa moja katika mahubiri yake
      a. Mt. 6:26,28-30, ndege wa angani na majani ya kondeni
      b. Mt. 10:29, shorewanda
   4. Paulo anaelezea kwamba wanadamu ni kuwajibika kwa maarifa ya Mungu katika uumbaji (yaani ufunuo wa asili, kama vile Rum. 1:19-20; Ufu. 21-22).

III. Hitimisho
   A. Tunawajibika kwa utaratibu huu wa asili!
   B. Asili ya dhambi ubinadamu imeharibu karama ya Mungu ya asili kama wana walivyo na karama zingine zote za Mungu.
   C. Huu utaratibu wa kiasili ni wa Muda. Itaenda kupita (2 Pet. 3:7). Mungu anatembea katika ulimwengu wetu kwa mfululizo wa kihistoria. Dhambi itaendelea katika utaratibu wake, lakini Mungu ameamua mipaka yake. Uumbaji utakombolewa (kama vile Rum. 8:18-25).

◙**"Kwa kuweka wazi"** Hii ilimaanisha, "kufungua mapazia" ili kufungua au kufahamisha. Pia, ni kichwa cha habari cha kitabu cha mwisho cha Agano jipya, "Ufunuo." Ujio wa pili daima una maana ya Ufunuo au kuja. (kama vile 1 Kor. 1: 7- 8; 1 Pet. 17, 13).

◙**"Wana wa Mungu"** Huu ulikuwa usemi mbadala wa kawaida uliotumika kuelezea Wakristo (kama vile 8:14, 16). Inazungumzia Baba, Yesu kama mwana wa pekee. (kama vile Yoh. 1: 18; 3: 16, 18; Ebr. 1: 2; 3: 6 **;** 5: 8; 7:28; 1 Yoh. 4. 9).

Katika Agano la kale, Israeli ilikuwa mwana wa Mungu (kama vile Hos. 11: 1), lakini pia mfalme alikuwa mwan wa Mungu (kama 2 Samweli. 7). Dhana hii kwa mara ya kwanza ilitajwa katika Agano jipya katika Mathayo. 5: 9, (kama Yn. 1:12; 2 Kor. 6: 18; Gal. 3: 26, 1 Yoh. 3: 1, 10; Ufu. 21:7).

**8:20**
**NASB, NKJV,**

**NRSV "Kwa kuwa uumbaji ulifanywa kuwa bure"**
**TEV "kwa vile uumbaji ulilaaniwa kutokuwa na maana"**
**NJB "ilikuwa si kwa kosa lolote kwa upande wa uumbaji"**
**"kwamba alifanywa kutoweza kufikia lengo lake"**

Hii ingeweza kufasiliwa kuwa – bure-linatumika kwa maana tofauti tofauti katika maandiko ya kale- haina maana, haifai, miungu wa uongo na utupu. Umbaji wote ukakosa maana kwa lengo lililokusudiwa na Mung. (kama ile Mwa. 3: 17- 19; Isaya. 24:3- 8), lakini siku moja Mungu ataondoa laana ya anguko (kama vile Ufu. 22: 3). Huu sio ulimwengu Mungu aliokusudia uwe.

◙**"Lakini kwa sababu yake yeye ambaye aliikifanya kiwe, katika tumaini**" KITENZI kiko katika WAKATI TENDEWA TIMILIFU na moja kwa moja linamaanisha Mungu. (kama vile NASB, NKJV, TEV). Alisababisha, Uumbaji wake kuwa bure.

1. Kwa sababu ya uasi wa mwanadamu
2. Kwa jitihada ya kumgeuza mwanadamu kuwa kwake (kama vile Kumb. 27-29)

Madhumuni haya yasiokuwa na maana yatakuwa ya muda tu (kama vile Rum 11:11-32). Mwanadamu aliyeokolewa ana ahadi ya matarajio ya mbele (mwili na ulimwengu)

Mungu alitambua uasi wa Adamu. Aliruhusu utokee na kuchaguo kufanya kazi na mwanadamu aliyeanguka katika ulimwengu ulioanguka. Huu sio ulimwengu ule Mungu alikusudia uwe. Huu sio ule ulimwengu Siku moja utakaokuwa (kama vile 2 Pet 3:10; Ufu 21:1-3) Tazama Nukuu katika "tumaini" katika 5:2

**8:21 "uumbaji wenyewe pia utawekwa huru kutoka katika utumwa wake kwa rushwa"** Asili itakuwa sehemu ya milele (kama vile Isa 11:6-10). Mbingu zinarudi kuwa dunia iliyoumbwa upya (kama vile Mt 5:18; 24:35; 2 Pet. 3:10; Ufu 21:1). Mbeleni kunawezarudi kuwa Edeni yenye upeo wa furaha, ushirika kati ya Mungu na wanadamu, mtu na mtu, mwanadamu kwa wanyama, na mwanadamu kwa dunia! Biblia inaanza na Mungu, mwanadamu na wanyama (yaani Isa 11:6-9) kwa upendo na uelewano katika mazingira ya Bustani (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inamalizia kwa njia ile ile (kama vile Ufu 21-22)

◙**"rushwa"** Tazama Mada Maalum katika 1:3

◙**"ndani uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu"** Katika mst wa 14 waumini wanaitwa "Wana wa Mungu," na mst 16 "Watoto wa Mungu" na katika mst 17 "warithi wa Mungu." Katika mst 18 utukufu wa mambo yajayo ya Mungu unabainika kwa waumini. Sasa katika 19, uumbaji unasubiriwa kuwekwa wazi kwa wana wa Mungu kwa sababu utagawana utukufu wao (kama vile 21). Kurejeshwa huku kwa uumbaji hasa wanadamu kutaruhusu kusudi la awali la uumbaji kutimiazwa na wanadamu (uliofanya kwa sura yake) kwa upendo wake wa milele.

**8:22 "uumbaji wote unalalamika"** Hii ni muunganikano mojawapo ya maneno ya Paulo "kulalama pamoja na." atakuwa ametumia mengi kati ya hayo. Bila shaka alikuwa anasema kwa namna nyingine kwa Yer. 12:4, 11 (kama vile Kumb 27-29) ambapo nchi ya Israel inaomboleza kwa kwa ajili ya ukiwa uliousabishwa na dhambi ya mwanadamu.

Tazama kuwa, "kulalama" huku kumetajwa mara tatu katika mazingira hapa

1. Uumbaji unalalama (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) kwa ujio wa enzi mpya mist 22 (kama vile 19-21)
2. Waumini wanalalama kwa wokovu wao kamili (yaani, mwili mpya kama vile 2 Kor. 5:2;4), mst 23
3. Roho ambaye anajiweka katika nafasi ya tundu la kwanza la enzi mpya pia analalama (maombi kwa ajili ya, KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) waumini mst 26.

◙**"anateseka kwa maumivu ya kumzaa mwana"** Kwa mazingira ya Kiyahudi, dhana hii daima iliitwa "maumivu ya kuzaa mtoto katika enzi mpya" (kama vile Marko 13:8) machweo ya siku mpya ya haki haitakuwa bila matatizo. Haki ya kimaadili na kiroho ya sayari hii iliyooanguka itakuwa mbaya na mbaya zaidi (kama vile Mt 24:, Marko 13;

Lk. 21; 2 The. 2:1-12, na pia tazama lakiri saba, baragumu na bakuli za ufunuo 5-18). Hata hivyo maumivu kuzaa mtoto ni maumivu yenye tumaini na furaha katika uzao ujao, hivyo pia, enzi mpya.

**8:23 "sisi pekee…. sisi pekee….peke yetu"** VIWAKILISHI vinasisitiza na kurudiwa

◙**"matunda ya kwanza ya Roho"** Neno (*aparchē*) kithiolojia linafanana na "Lakiri ya Roho" katika IIKor 1:22; na "ombii la Roho" katika 2 Kor. 5:5 na Efe. 1:14 matunda ya kwanza katika Agano la Kale yalikuwa ahadi ya mavuno yajayo; yalifananishwa na umiliki wa Mungu wa mavuno yote (yaani Kumb. 26:1-11). Roho ndiyo matunda ya kwanza ya enzi mpya; kwa vile Yesu alikuwa tunda la kwanza la ufufuo (kama vile 1 Kor. 15:20). Waumini kama watoto wa Mungu, hata hivi sasa wanakutana na furaha ya mbinguni kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye anaishi nao ndani yao. Hii ndiyo "tayari" lakini "bado kidogo" mvutano wa miingiliano ya enzi mbili za Wayahudi. Waumini ni raia wa mbinguni na waishio duniani.

◙**"sisi wenyewe tunalalama miongoni mwetu"** Hii inaonyesha kuna mvutano wa mjadala kati ya "tayari" na "bado" kuhusu mwingiliano wa enzi mbili za Kiyahudi (Tazama Gordon Free na Doouglas Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth* kur. 144-148). Ufalme wa Mungu upo lakini haujakamilika. Waumini wana uzima wa kufufuka na lakini bado watakufa kimwili (2 Kor. 5:2-4). Tumekombolewa kutoka dhambini lakini bado tunasumbuka na dhambi (Rum 7; Efe. 6:18-18).

◙**"kusubiri kwa hamu urithi *wetu* kama wana"** Urithi ni usemi wa Paulo alioupendelea kama neno mbadala kwa "wokovu" (kama vile mst 15). Wokovu wa muumini ni mchakato unaoanza na uamuzi wa mwanzo wa toba na imani na unakuwa kumfanya mtu afanane na Kristo. Waumini hawataokolewa kikamilifu mpaka siku ya ufufuo (kama vile mst 30 na 1 Yn. 3:2). Neno "urithi" limeachwa katika maandiko ya Kiyunani (kama vile MSS $P^{46}$, D, F, G na baadhi ya machapisho ya Kitariano. Hata hivyo yamejumuishwa katika א, A, B, C na machapisho ya Zamani ya Kilatini, kama Vulgae, Kishamu, Kikoptiki, na chapisho la Amrmenian. $UBS^4$ inayapa alama ya "A" (kuwa hakika).

◙**"ukombozi wa miili yetu"** neno hili lina maana ya "kununua kitu ulichouzwa kwa kukirudisha kwako. Dhana hii ilitumiwa na Agano la Kale kuelezea hali ya mtu aliyekuwa huru toka utumwani na jamaa (*go'el*) lilikuja kutumiwa kama neno mbadala kwa ukombozi wa Mungu, kwa mwanadamu aliyetoka katika utumwa wa dhambi. Gharama iliyolipwa ilikuwa maisha yasiyo na dhambi ya Mwana aliyekuwa mwanadamu (Tazama Mada Maalum katika 3:4). Ukristo kama Uyuda, (kama vile Ayu. 14:14-15; 19:25-26, Dan. 12:2) inadai waumini watakuwa (japo siyo lazima) na (kama vile 1 Kor. 15:35-49 mwili wakibinadamu katika umilele. Mwili wa kiroho wa mwanadamu utaandaliwa kikamilifu kwa maisha ya enzi mpya, maisha ya upendo wa dhati na Mungu.

**8:24"katika tumaini tumeokolewa"**Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU ELEKEZI kama mstari wa 23 unavyozungumza kuhusu wokovu wetu ujao, mstari wa 24 unazungumza wokovu wetu wa nyuma kupitia wakala wa Roho. Agano Jipya lilitumia NJEO ZA VITENZI kadhaa kuelezea wokovu (Tazama Mada Mada Maalum katika 10:4)

1. WAKATI TIMILIFU Mdo. 15:11 (Rum 8:24; 2 Tim. 1:9; Tit. 3:5 na Rum. 13:11 inajumuisha WAKATI TIMILIFU na uwasilishaji wa WAKATI UJAO)
2. WAKATI ULIOPITA Efe. 2:5,8
3. WAKATI ILIOPO 1 Kor 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15; 1 Pet 3:21; 4:18
4. WAKATI UJAO (katika kitenzi au rejea ya mazingira), Rum 5:9,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28.

Kwa hiyo wokovu unanza na uamuzi wa awali wa imani kuendelea na mchakato wa imani katika mtindo wa maisha ambao siku moja utakamilishwa mbele ya maisha ya watu (kama vile 1 Yohana 3:2)

**8:25 "tumaini"** Tazama Mada Maalum chini.

## MADA MAALUM: TUMAINI (*elpis*, kwa Paulo)

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. Matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. Ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. Kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. Wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. Agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

◙**"saburi"** Neno *hupomonē* lilitumika pia katika 5:3 na 15:4-5. Wokovu wa waumini uko katika mchakato wa ukomavu, na iko siku moja utakamilika. Saburi (kama vile Ufu 2:8,11, 17, 26; 3:5,12, 2, 21; 21:7 ni hitaji la msimamo wa kibiblia, husisitiza juu ya "wokovu wa awali." Ukweli mwingi wa kibiblia (yaani Fasihi ya Mashariki, Tazama Mada Maalum katika 3:27) inaelezwa katika utofauti tu wa matamshi.

## MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahusuyo uhakika
    a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
    b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
    c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu
    a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)

b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5
- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8

- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote vya nyakati:
- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:26-27**
**26Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. 27Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.**

**8:26 "kwa njia ile ile"** Hii inaunganisha kikundi cha Kiroho cha maombi "kinacholia na kutumaini" kilichotajwa katika mistari ya 18-25

◙**"pia Roho hutusaidia"** Ni KITENZI CHA KATI [chenye kushuhudia] ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO. KITENZI kina muungano wa maneno mawili, *syn* (kama vile mst 28) na *anti*. Inafasiliwa vizuri zaidi kama "shikilia" neno hili linapatikana hapa na katika Luka 10:40 tu. Mungu wa utatu wote ni kwa ajili ya waumini. Baba alimtuma Mwanaye aje afe kwa niaba ya mwanadamu, na hivi sasa anatuombea pia (kama vile 34; Ebr. 7:25; 9:24; 1 Yoh 2:1). Roho anamleta mwanadamu aliyeanguka kwa Kristo na kumfanya Roho kuwa ndani yao (kama vile Yn. 16:8-15). Hata hivyo, KITENZI "kusaidia" kilichomaanisha "kumshikilia mtu" ikibainisha kuwa muumini ana sehemu yake ya kusaidia Roho katika (maombi yake).

◙**"udhaifu"** NOMINO hii imetumiwa na Paulo kwa maana kadhaa wa kadhaa (BAGD, uk 115).
1. udhaifu wa mwili au maradhi, 2 Kor. 11:30; 12:5,9,10; Gal 4:13; ITim 5:23
2. hali ya mwanadamu, 1 Kor 15:43; 2 Kor 13:4
3. mtazamo wa
   a. uwoga, 1 Kor 2:3
   b. maamuzi Rum 6:19
   c. kutokuwa na maono ya kidini 8:26

KITENZI kinatumiwa kwa njia ileile
1. udhaifu wa mwili, (Flp 2:26-27; 2 Tim 4:20
2. hali ya mwanadamu, Rum 8:3; 2 Kor 11:21, (tazama Mt 8:17; nukuu ya Isa 53:4
3. mtazamo wa
   a. udhaifu wa kidini au kimaadili, Rum 14:2; 1 Kor 8:11-12
   b. udhaifu katika imani, Rum 4:19; 14:1
   c. moyo ulikata tamaa na uwoga, 2 Kor 11:29

Kumbuka muundo waweza kudadili maana kufuatana na vigezo vya maneno. Misamiati inawezesha tu vidokezo na matumizi.

◙**" Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua"** Waumini wanalia kwa uchungu kwa anguko lao. Roho naye analia kwa uchungu katika kuwaombea. Roho kwa wale waliokombolewa anawaombea. Na Yesu katika mkono wa kulia wa Mungu pia anawaombea (kama vile mist 27,34; Ebr. 7:25; 9:24; 1 Yn. 2:1). Maombi haya yanampa muumini nguvu ya kuomba (kama vile mst. 15; Gal 4:6). Habari hii kwa mazingira yake haimaanishi kipawa cha roho wa kunena kwa lugha, bali maombezi ya Roho kwa Baba kwa niaba ya waumini.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"kwa ndani sana kuliko maneno"** |
| **NKJV** | **"ambayo hayawezi kutamkwa"** |
| **TEV** | **"maneno ambayo hayawezi kueza"** |

**NJB** **"ambayo hayawezi kuwekwa katika maneno"**

Neno hili ni neno la kawaida katika "kuzungumza" lugha (kama vile 1 Kor 13:1) ENYE HALI YA UFALAGHA. Linapatikana tu hapa na katika Agano Jipya. Neno la namna nyingine limetumika katika injili ya Marko kwa mababu / watu wasioweza kama (kama vile 7:37; 9: 17, 25).

◙**"Kuombea"** Tazama mada maalum: Matumizi ya Paulo ya maneno ya *Huper* yaliyo unganishwa katika 1:30.

**8: 27 "yeye atafutaye moyo"** Hii ilikuwa dhima iliyorudiwa katika Agano la kale (kama vile 1 Sam 2:7; 16: 7; IFalm 8: 39; 1 Nyak. 28:9; 1 Kor. 6:30; Zab. 9:7; 44:21; Mith. 15:11; 20:27; 21:2; Yer. 11:20; 17:9-10; 20:12; Luk. 16:15; Mdo. 1:24; 15:8). Mungu kweli anatujua na bado anatupenda (kama vile Zab 139).

◙**"anawaombea watakatifu"** kazi ya Roho ilikuwa imewekwa bayana katika Yohana 16:2-15. Mojawapo ilikuwa maombezi. Neno "watakatifu" ilikuwa daima katika (Efe. 4:21) wingi, isipokuwa pale pia ilipomaanisha wauimini wote. Wakristo ni mojawapo ya wanafamilia ya Mungu. Mwili wa Kristo, hekalu jipya lililojengwa kutokana na waumini binafsi. Huu ndiyo ulinganifu wa kithiolojia uliotakiwa kwa ubinafsi (Marekani). Tazama Mada Maaalum: Watakatifu katika 1:7

## MADA MAALUMU: HULKA YA ROHO

Kwenye Agano la Kale "Roho wa Mungu" (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa "ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Matendo 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu:Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:28-30**
**28 Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi lake. 29 Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishe na mfano wa mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. 30 Na wale aliowachagua tangu asili hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza**.

**8:28 "Na tunajua"** KITENZI hiki (*oida*) kinatokea mara nne katika andiko hili

1. waumini wanajua kuwa uumbaji wote unalia kwa uchungu (mst. 22)
2. waumini wote hawajui namna ya kuomba (mst. 26)
3. Baba anajua mioyo ya wanadamu na fikra za roho (mst. 27)
4. waumini wanajua kuwa vitu vyote vinafanya kazi kwa kusudi jema (mst. 28)

◙
**NASB, TCNT "Mungu anasababisha vitu vyote"**
**NKJV, NRSV,**
**NET "vitu vyote"**
**TEV, NIV "katika mambo yote Mungu hufanya kazi"**

Swali la kimaandiko ni mara ngapi neno "*Theos*" (au "*Theon*") linatokea katika mstari huu?

Hakuna utofauti wa kimaandiko unaohusiana na fungu "kwa kweli wanaompenda Mungu" lakini kuna utofauti unaohusiana na fungu "vitu vyote vinafanya kazi kwa nia njema"

1. Machapisho mengine "*ho Theos*" baada ya KITENZI P[46], A, B, 81, na machapisho kadhaa kadhaa ya Kihabeshi na Koptiki.
2. Machapisho mengi yanaacha, ℵ, C, D, F, G na machapisho ya Vulgate, Peshitta na Armenian. UBS[4] inatoa alama kwa kuliacha kwa kiwango cha "B" (karibia sawa).

Toleo la NASB linajumuisha kukazia hoja ya tendo la imani. Inawezekana kutoka katika mazingira kuwa uwakala wa Roho uondolewa (kama vile mst. 27; NEB, REB).

◙**"kufanya kazi pamoja kwa lengo zuri"** Hii KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Hili ni neno lingine lenye maneno yaliyoungana yenye neno *syn* (kama vile mst 26). Kwa hiyo kwa lugha rahisi "vitu vyote vinavyoendelea kufanya kazi kwa ushirikiano kwa lengo zuri" hii ni dhana ngumu kwa ulimwengu wenye maovu na mateso (vitabu viwili vinavyoweza kusaidia katika somo hili ni *The Goodness of God* na Wenham na Hannah Whithall Smith, *The Christian's Secret of a Happy Life*). Neno "zuri" hapa limefasiriwa katika mst. 29 kama "kufanana na sura ya Mwanaye" "kufanana na Kristo" siyo, mali kujulikana au afya ni mpango usiobadilika wa Mungu kwa kila muumini .

◙**"na wale wampendao Mungu, kwa wale walioitwa kwa kusudi lake"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Haya ni masharti mawili yanayoendelea kumruhusu muumini kuona maisha bila kujali mazingira katika hali chanya (kama vile mst. 15). Angalia tena swala la maagano pacha ya uhuru wa mwanadamu ("upendo") na Ukuu wa Mungu ("anaitwa").

Neno "kusudi" kwa kuungama na mipango ya milele ya Mungu linapatikana katika Rum. 9: 11; Efe. 1: 11; 3:11na 2 Tim. 1:9. Mungu ana mpango wa ukombozi wa milele kwa wanadamu walioanguka. Tazama mada maalum. "Upendeleo wa injili ya Baba katika 1: 5.

**8:29-30** VITENZI katika mistali hii yote ni KAULI TENDAJI ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Vinaunda mnyororo toka kabla hadi muda wa mwisho. Mungu anatujua na bado yu kwa ajili yetu na anatutaka tuwe naye. Hili ni andiko jumuishi na sio binafsi. Tendo la mwisho la utukufu bado linakuja. Lakini katika mazingira haya linaelezwa kana kwamba ni tukio lililokamilika.

**8:29 "Alijua kabla"** Paulo alitumia neno hili mara mbili hapa na katika 11:2. Katika 11: 2 ilimaanisha upendo wa agano la Mungu kwa Israeli kabla ya wakati. Kumbuka kuwa, neno "kujua" katika Kiebrania lilihusishwa na agano

binafsi, na sio mambo kuhusu mtu (kama vile Mwa. 4: 1; Yer. 1: 5). Hapa linajumuishwa katika mfululizo wa matukio. (kama vile mist. 29-30). Neno linaunganishwa na dhana kuwa vyote vitendekavyo vilishapingwa na Mungu, hakuna wa kuvibatilisha. Hata hivyo,inapaswa kusemwa kwamba uelewa wa Mungu kabla sio msingi wa uchaguzi kwa sababu, kama hilo lingekuwa hivyo, basi uchaguzi ungezingatia kukubaliwa kwa baadaye kwa binadamu aliyeanguka, ambalo lingelikuwa ni utendaji wa mwanadamu. Neno hili pia lilipatikana katika Mt. 26: 5; 1 Pet. 1:2, 20 na 2 Pet. 3: 17.

◙**"Lilikwisha kupangwa na Mungu**" Neno "kujua kabla" (*proginōskō*) au "kupanga kabla" (*proorizō*) yote ni maneno yaliyo ungana yenye kihusishi "kabla" *(pr*o) na kwa hiyo, sharti lifasiliwe "kujua kabla" "kuweka mipaka kabla" au "weka alama kabla."

Habari inayo fasili kuhusu kupangwa au kujua kabla katika Agano jipya ni Rum.8: 28- 30; Efe. 1: 3- 14 na Rum. 9. Maandiko waziwazi yanasisitiza kuwa Mungu ni mkuu. Ni yeye atawalaye vitu vyote, vikiwemo historia ya mtu, Kuna hivi sasa, imani ya mpango wa ukombozi unaotayarishwa kwa wakati. Hata hivyo mpango huu sio hivihivi au ubaguzi; Sio tu kwa Ukuu wa Mungu au ufahamu wake kabla, bali ni wa tabia yake isiyobadilika ya huruma na Neema isiyostahili. Lazima tuwe waangalifu kwa ubinafsi wetu wa Magharibi (Kimarekani) au shauku yetu ya kiinjili inayopaka rangi ukweli huu wa ajabu.

Lazima pia tujilinde dhidi ya kutenganishwa katika migongano ya kihistori, kithiolojia baina ya Agostino na Pelegius au Calvinism na Arminianism.

Yale Yaliyoamuliwa kabla sio mafundisho yaliyomaanisha kupunguza upendo wa Mungu, huruma au neema wala si kuondoa vingine kutoka katika injili. Inakusudiwa kuimalisha waumini na kuwaundia mtazamo wao wa kidunia. Mungu ni kwa ajili ya watu wote, (kama vile Yoh. 3: 16; 1 Tim. 2: 4, 2 Pet. 3: 9). Mungu ni mtawala wa vitu vyote. Ni nani au nini kitatutenganisha naye? (kama vile Rum. 8: 31- 39). Dhana ya Mungu kuwa kila kitu kimepangwa na Mungu kabla, unaunda moja ya njia mbili za kuutazama ulimwengu, Mungu aliona historia yote kuwa ipo. Binadamu anabanwa na wakati. Mitazamo yetu na fikra zetu ni fupi. Hakuna mgongano kati ya Ukuu wa Mungu na hiari ya mwanadamu. Ni muundo wa patano kwa pande mbili. Huu ni mfumo mwingine wa ukweli wa Biblia uliotolewa katika mvutano wa pande mbili za kiasili. (Tazama mada maalumu fasihi ya mashariki katika 3: 27).Imani za kibiblia daima zinawasilishwa katika mitizamo tofauti.

Daima zinatokea kama fumbo. Ukweli ni mlinganyo kati ya jozi mbili zinazoonekana kukinzana. Hatuwezi kuondoa mvutano kwa kuchukuwa aina moja tu ya ukweli. Hatuwezi kutenganisha ukweli wowote wa kibiblia kuwa katika mfumo wa kithiolojia usiyohusiana kabisa na muundo maalum. Ni muhimu pia kuongeza kuwa lengo la uchaguzi sio tu mbinguni tunapo kufa, bali kufanana na kristo sasa. (kama vile Efe. 1: 4; 2: 10). Tulichaguliwa kuwa "watakatifu na bila lawama." Mungu anachagua kutubadilisha iliwengine waone badiliko na kuitikia kwake kristo kwa imani. Kuamini kuwa Mungu amepanga kila kitu tangu awali, sio maslahi binafsi bali wajibu wa patano.

◙**"Kumfanana yeye kwa mfano wa mwanaye."** Huu ndio ukweli mkubwa wa habari hii. Hili ndilo lengo la ukristo (kama vile 8: 9; 2 Kor. 3: 118; Gal. 4: 19; Efe. 1: 4; 2:10; 4: 13; 1 The. 3:13, 4: 3; 1 Pet. 1:15). Utakatifu ndilo mapenzi ya Mungu kwa kila muumini. Uchaguzi wa Mungu ni kufanana na Yesu (kama vile Efe. 1: 4) na sio msimamo maalum. Sura ya Mungu, waliopewa wanadamu katika uumbaji, (kama vile Mwa. 1: 26, 5: 1, 3; 9:6) ndio unabidi kurejeshwa (kama vile Kol. 3: 10). Tazama nukuu katika 8:21na mada maalum. Kuitwa katika 1: 6.

◙**"Kwamba, sharti awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa kaka zake"** Katika Zab. 89: 27 "mzaliwa wa kwanza" ni wadhifa wa masiha. Katika Agano la kale, mzaliwa wa kwanza wa kiume, alikuwa na umaarufu na maslahi. Neno lilitumiwa katika Kol. 1: 15 kuonesha umaarufu wa Yesu katika uumbaji na katika Kol. 1: 18 na Ufu. 1: 5 kuonyesha umaarufu wa Yesu katika ufufuo. Katika mazingira haya, waumini kupitia kwake, huletwa katika umaarufu wake. Neno hili halina maana hali ya Yesu kuwa kama mwanadamu, lakini kwake kama kichwa cha taifa jipya (kama vile 5:12- 21); wa kwanza katika mfuatano wa imani yetu, njia ya Baraka ya Baba kwa imani ya familia. Tazama Mada Maalumu ifuatayo:

## MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA

Neno hili "mzaliwa wa kwanza" (*prōtotokos*) limetumika katika Biblia kwa maana tofauti mbali mbali.

1. Mazingira yake ya nyuma yanrejelea kwa
   a. Mzaliwa wa kwanza anamhusu YHWH (BDB 114, KB 131, kama vile Kut. 13:2,12; 22:29; 34:19; Hes. 3:13)
   b. Ukaribu uliokuwepo kabla wa mzaliwa wa kwanza wa kiume katika familia (kama vile. Kumb. 21:17; Zab. 89:27; Lk. 2:7; Rum. 8:29; Ebr. 11:28)
2. Matumizi yake katika Kol. 1:15 yanazungumza juu ya Yesu kama mzaliwa wa kwanza wa uumbaji ambacho kinawezekana katika kidokezo cha Agano la Kale Mit. 8:22-31, au wakala wa Mungu wa uumbaji (kama vile Yn 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:15-16; Ebr. 1:2)
3. Matumizi yake katika Kol. 1:15,18; 1 Kor. 15:20,23; Uf. 1:5 inarejelea kwa Yesu kama mzaliwa wa kwanza toka katika wafu
4. Ni wasifu wa Agano la Kale uliotumika kwa Masihi (kama vile Zab. 89:27; Ebr. 1:6; 12:23); ni wasifu unaojumuisha dhana mbali mbali za Yesu kama kitovu na mmiliki wa mambo yote.

**8:30 "kutukuzwa"** Mungu daima anaelezwa katika biblia kwa neno "utakatifu" neno lilitokana na neno la msingi la kibiashara lililomaanisha "uzito" na kwa maana hiyo thamani, kama dhahabu. Tazama Mada Maalum katika 3:23. Kithiolojia, Mungu anaokoa mwanadamu aliyeanguka kupitia hatua mfuatano zilizoorodheshwa katika mistari ya 29-30. Hatua ya mwisho ni "kufanywa kuwa mtakatifu" (kutakaswa) hii itakuwa ndio wokovu kamili wa muumini. Itatokea siku ya ufufuo wakati wa wanapewa miili yao mipya ya kiroho. (kama vile 1 Kor 15:50-51) na wameungana kikamilifu na Mungu wa Utatu na wao kwa wao (kama vile 1 The. 4:13-18; 1 Yn. 3:2) daima, mchakato uliotajwa katika mistari ya 29-30 unawekwa katika kundi la kithiolojia.

1. Uhalalisho mist. 29-30 ni kuweka huru kutoka katika adhabu ya dhambi (urithi, warithi mist 16-17)
2. Kutukuza (yaani "kuwa sawa na taswira ya Mwanaye"), mst. 29 kuwekwa huru kutoka katika mabavu ya dhambi (kuishi kama Kristo)
3. Kutakasa kuwekwa huru kulitoka na dhambi (yaani, mbinguni).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:31-39**
**31 Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? 32 Yeye asiye mwachilia
Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja
naye? 33 Ni nani atayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. 34 Ni nani
atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu,
naye yuko mkono yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea. 35 Ni nani atayetutenga na
upendo wa Kristo? Je! ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? 36 Kama
ilivyoandikwa, ya kwamba, kwa ajili yako tunauwawa mchana kutwa, tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa
kuchinjwa. 37 Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. 38 Kwa
maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamalaka,
wala yaliyopo, wala yatakayo kuwapo, wala wenye uwezo, 39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe
kinginecho chote hakiataweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

**8:31 "tuseme nini basi kwa vitu hivi"** Hili lilikuwa fungu la Paulo alilolipenda likionyesha tabia yake ya makemeo aliyoiwasilisha (kama vile 3:5; 4:1; 6:1; 7:7; 9:14,30) suala hili linahusiana na ukweli uliotolewa wakati uliotangulia. Haijulikani linaelezea kiasi gani huko nyuma. Lingeweza kurejea katika 3:21-31 au 8:1 au 8:18. Kwa sababu ya matumizi ya neno"kwa hiyo" katika 8:1 na muundo, 8:18 bila shaka ni ubunifu mzuri.

◙**"kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inakadiriwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa lengo lake la uandishi. la kushangaza, katikati ya jitihada zetu zote za kupambana na dhambi, Mungu yu pamoja nasi sote.

◙**"nani yu kinyume na sisi "** KIWAKILISHI "nani" kinarudiwa katika mist 33;34;35. Inamaanisha shetani (ambaye hajatamkwa kwa jina hadi 16-20). Aya hii toka 31-39 inatumia fasihi ya imani ya Agano la Kale la Manabii, shauri la miaka (kama vile Mika 1:6). YHWH anapeleka watu wake mahakamani kwa uzinifu wa kiroho. Ni fikra potofu katika Isa 50:8-9.

Tazama maneno ya kisheria dhidi ya mst. 31 "tozo," mst. 33 "kuhalalisha," mst. 33 "kulaani," mst. 34 "kuombea," mst. 34. Mungu ndiye mwamuzi. Kristo ni mwanasheria mtetezi, shetani ni mwendesha mashtaka (lakini yu kimya). Malaika wanajaa ndani ya mahakama kama watazamaji 1 Kor 4:9; Efe 2:7; 3:10)

**8:32 "yeye ambaye hakuokoa maisha ya mwanaye"** Mungu Baba amewapa wanadamu walioanguka yote yaliyo mazuri kwake. Hatawaonyesha waumini sasa hata kuwapungukia (kama vile Yn. 3:16; Rum 5:8). Ni kiasi gani dhana ya Mungu wa agano la kale na Yesu mpendwa imekosea! Zawadi ya mwisho inaoneka katika maneno ya Mungu kwa Ibrahimu katika Mwa. 22:12,16. Viongozi wa dini walitumia habari hii ya Agano la Kale kuunga mkono imani ya toba kama mbadala kwa mbegu ya Ibrahimu.

◙**"lakini alitolewa kwa ajili yetu sote"** Neno "wote" katika andiko hili ni muhimu sana. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu (kama vile Lk. 2:10-11; Yoh 3:16; 4:42; 11:51; 1 Tim 4:10; 1 Yn. 2:2; 4:14). Inaonyesha uainishi wa adamu kwenda kwa Kristo katika 5:12-21. Kifo cha Yesu kilitatua tatizo la dhambi. Na sasa ni tatizo "kuamini na kupokea.

◙**"tupe bure vitu vyote"** KITENZI hiki kinatokana na msingi wa neno la Kiyunani vitu vyote vikimaanisha mst. 17. Tazama Nukuu lkatika 3:24.

**8:33-34 "toza… halalisha….tia hatiani….ombea"** Maneno haya yote ni ya kisheria. Mistari ya 31-39 ni picha ya kimahakama ya mbinguni. Huu unaweza kuwa ni msemo mbadala kwa Isaya 50:8-9

**8:33 "chaguo la Mungu"** Yesu ni chaguo la Mungu kwa wanadamu wote. Habari iliyowazi na iliyoelezwa kikamilifu kuhusu ukweli huu uliopo katika Agano Jipya ni katika Efe 1:3-4 na Rum 9:14-26. Baba alimchagua Yesu kuwachagua wanadamu wote. Yesu ni "ndiyo" ya Mungu "hapana" ya mwanadamu aliyeanguka!

## MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAJAALIWA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile Warumi 10:11, 13).

Umuhimu wa huu mvutano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelel!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja (fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu

2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihilisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhimu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kithiolojia ya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maneno na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

**8:34** Mstari huu unaorodhesha sababu kuu kwa nini hakuna laana ( kama vile mst.1)
1. Alikufa
2. Aliinuliwa
3. Ameketi mkono wa kuume wa Mungu
4. Anawaombea waumini

Kifo cha Yesu kililipa adhabu/ gharama ya dhambi zetu. (kama vile Marko. 10: 45; 2 Kor. 5: 21). Ufufuo wa Yesu unaonyesha. Baba kupokea maombi ya mwanaye na kutoa matumaini. (Tunda la kwanza kwa wele waliolala) mbele ya hukumu na kifo. Utakaso wa Yesu katika mkono wa kuume wa Baba na maombi kwa waumini, inawapa ujasiri wa kupigana vita takatifu ya imani.

◙**"Mkono wa kuume wa Mungu."** Hili ni neno mbadala linaloelezea imani ya kuabudu vitu/ wanyama kama Mungu. (Tazama mada maalum katika 1: 18). Mungu hana mwili wa kuonekana wala kushikika. Yeye ni "roho." Neno hili mbadala linazungumzia nafasi ya mamlaka, nguvu, na umaarufu wake wa hali ya juu. Paulo hatumii usemi huu mara kwa mara (Efe. 1: 20; Kol. 3: 1). Paulo anaweza kuwa alikuwa ananukuu sheria ya zamani ya kikristo katika mst. 34 (kama vile Flp. 2: 6 na kuendelea; 1 Tim. 3:16).

◙**"Anatuombea"** Yesu anaendelea na kazi ya Mungu. Yesu anatuombea (kama vile Ebr. 4: 4-16; 7:25; 9: 24; 1 Yoh. 2: 1) kama afanyavyo Roho (mist. 26- 27). Hii inatokana na neno *paraclete*, ambalo limetumika kwa Roho katika Yoh. 14: 16 na kwa mwana katika 1 Yoh. 2: 1. Huu ni usemi mbadala wa wimbo wa mtumishi anayeteseka (kama vile Isa. 53: 12).

◙**"Upendo wa Kristo"** Hii ni mojawapo ya SENTESI TEGEMEZI au UMILIKISHI WA JINSI enye asili ya kulenga mhusika au lengo kwa mwingine. Hii ama inaweza kuwa (1)Upendo wa kristo kwa waumini au (2) Upendo wa Wakristo kwa Yesu. Namba 1 inafaa kabisa katika mazingira haya (na 2 Kor. 5: 14) kwa sababu upendo wa waumini kwa kristo huja na kuondoka, lakini upendo wa kristo kwetu ni wa kweli na imara.
Kuna maandiko ya kiyunani yenye utofauti kufuatana na fungu hili.
1. Andiko moja la kale la kiyunani lina "upendo wa Mungu" (kama vile ms ℵ).
2. Andiko moja la kale la kiyunani linayaunganisha pamoja "upendo wa Mungu katika kristo" (kama vile MS B)
3. Waandishi wa UBS[4] wanatoa alama A kwa "Upendo wa kristo (Hakika inaonekana katika MSS C, D, F,G, na machapisho mengi ya zamani ya kilatini, na Vulgate na Peshitta.

◙**"Patakuwa na dhiki kuu, mafadhaiko au mateso"** Wakristo watakuwa na matatizo katika ulimwengu huu, lakini hakuna hata moja au nguvu za Shetani zitaweza kuwatenganisha na Mungu.Tazama mada maalum ( " Matatizo."

**8: 36** Hii ni nukuu kuto katika Zab. 44:22. Katika Zaburi hii, Mungu anaitwa kuja kuwaokowa watu wake wanaoumia.

**8: 37**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"Lakini katika mambo haya yote tutashinda kwa kishindo"** |
| **NKJV** | **"Bado, katika mambo yote haya sisitu zaidi ya washindi."** |
| **NRSV** | **"Hapana, katika mambo yote haya tu zaidi ya washindi."** |
| **TEV** | **"Hapana, katika mambo yote haya, tuna ushindi kamili kupitia Yeye.** |
| **NJB** | **"Haya ni majaribu ambayo kwa kupitia humo tunashinda."** |

Hii ilikuwa njia madhubuti ya kuelezea "kushinda." Paulo atakuwa amelitumia neno hili kwa namna nyingine. (*huper + nikaõ*). Huu ni mchanganyiko wa ajabu wa maneno mbadala "kumshinda kondoo". Waumini ni washindi kupitia Kristo (kama vile Yoh. 16: 33; 1 Yoh. 2: 13- 14; 4: 4; 5: 4). Tazama mada maalum "matumizi" ya Paulo ya muunganiko wa *Huper* katika 1:30.

◙**"Kupitia kwake, yeye aliyetupenda?** KIWAKILISHI kinaweza kumaanisha Baba au Mwana.

**8:38 Nina shawishika** Hili ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU inayomaanisha "Nimeshawishika na nitaendelea kushawishika".

◙**"Malaika"** Viongozi wa dini walifikili kuwa, malaika walikuwa na wivu kwa upendo wa Mungu na kuwajali wanadamu, na kwa hiyo, walikuwa maadui kwao. Walimu wa uongo walidai kuwa, wokovu ulikuwepo tu kwa njia ya neno la siri kupitia katika mazingira ya malaika katili (kama vile Wakolosai na Waefeso).

George Eldon Ladd ana ufupisho mzuri wa maneno yaliyotumiwa na Paulo kwa malaika katika kitabu chake "*A theology of the New Testament."*

"Paulo anaelezea sio tu malaika wazuri na wabaya bali pia Shetani na majini. Anatumia kundi lingine la maneno kuonyesha wasifu wa Roho za malaika. Misamiati hii ni kama ifuatavyo:
'Utawala' [*arche*] 1 Kor 15:24; Efe 1:21; Kol 2:10
'Watawala' [*archai* RSV, "falme"], Efe. 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15; Rum. 8:38
'Mamlaka' [*exousia*], 1 Kor 15:24; Efe. 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15; Rum. 8:38
'Mamlaka' [*exousiai*; RSV, "mamlaka"], Efe 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15
'Nguvu'[*dynamis*], 1 Kor 15:24; Efe 1:2
'Nguvu' [*dynamis*], Rum 8:38
'Kiti cha Enzi' [*thronoi*], Kol 1:16
'Ubwana' [*kyriotes*; RSV, "ushirika"], Efe 1:21
'Ubwana' [*kyretetes*], Kol 1:16
'Watawala wa ulimwengu wa giza hili,' Efe 6:12
'Roho (uhifadhi) za uongo katika mbingu,' Efe 6:12
'Mamlaka ya giza' Kol 1:13
'Kila jina litakalo litakaloitwa,' Efe 1:21
'Viumbe vya mbinguni, duniani na chini ya ardhi,' Flp 2:10" (uk 401)

Hakuna taarifa ya Biblia ya moja kwa moja kuhusu namna malaika walioanguka wa Agano la Kale wanavyohusiana na majini wa Agano Jipya, wengi wanadhani wanafanana. Katika fasili ya uharibifu wa Kiyunani, hata hivyo majini ni roho manephili wa Mwanzo 6 waliokuwa nusu malaika na nusu wanadamu. Miili yao iliharibiwa katika mafuriko, kwa hiyo yanatafuta pa kukaa. Hizi ni hisia tu, biblia hujibu maswali yetu yote kuhusu asili. lengo lake ni ukombozi wa mwanadamu, na siyo matamanio yao.

◙**"mamlaka….nguvu"** Hii inarejea (1) nguvu za wakati huu za kimalaika au kimajini (Efe 2:2; 6:12; 1 Kor 15:24; Kol 1:16) au (2) bila shaka muundo usio binafsi wa anguko la ulimwengu (dini, serikali, elimu, tiba n.k) ambayo inamruhusu mwanadamu aliyeanguka kutomtegea Mungu (kama vile Hendrckus Berkhoff, *Principalities and Power*). Tazama nukuu katika 13:1

## MADA MAALUMU: *ARCHĒ*

Neno la Kiyunani *archē* linamaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.

1. mwanzo wa mpangilio ulioumbwa (kama vile. Yohana 1:1; Ebr. 1:10)
2. mwanzoni mwa injili (kama vile Mk. 1:1; Flp. 4:15; 2 The. 2:13; Ebr. 2:3; 1 Yohana 1:1)
3. mwanzo wa jicho la kwanza la ushahidi (kama vile Luka 1:2)
4. mwanzo wa dhambi (miujiza, kama vile Yohana 2:11)
5. mwanzo wa mafundisho (kama vile Ebr. 5:12)
6. mwanzo wa udhihirisho uliojikita katika kweli ya Injili (kama vile. Ebr. 3:14)
7. mwanzo, Kol. 1:18; Ufu. 3:14

Ilikuja kutumika juu ya "utawala" au "mamlaka"

1. juu ya wanadamu rasmi watawalao
   a. Luka 12:11
   b. Luka 20:20
   c. Warumi 13:3; Tito 3:1
2. juu ya mpangilio wa mamlaka
   a. Warumi 8:38
   b. 1 Kor. 15:24
   c. Efe. 1:21; 3:10; 6:12
   d. Kol. 1:16; 2:10,15
   e. Yuda 1:6

**8:39 "urefu, wala kina"** Maneno haya yalitumika kutenga na njia ya nyota, zilizoaminiwa kuwa miungu walioongoza maisha ya watu (elimu juu ya nyota) baadaye yakawa maneno ya kitaalamu katika maarifa ya karne ya pili kwa neno *eons* au ngazi za kimalaika kati ya miungu watakatifu na wasio watakatifu watendao dhambi

◙**"Kitu kingine kilichoumbwa"** Hili ni neno la kifasihi"kiumbe wa aina nyingine" (*heteros*). Mazingira yanadai kuwa hii ni rejea zaidi kwa mamlaka ya malaika tofauti kati ya KIHUSISHI cha Kiyunani *heteros*, kingine cha aina tofauti na *allos*, kingine cha aina moja, zilianza kutoka katika Koine ya Wayunani, lakini hapa mazingira bado yanaonyesha utofauti.

◙**"siyo…wala…kitakachoweza kututenga na upendo wa Mungu"** Ni usemi wa uhakika kiasi. Sura inaanza kwa kusema hakuna hatia na kumalizia na hakuna utengano. Hakuna awezaye kuchukua wokovu wa muumini. Hivyo, mtu yampasa kukubali mwanzo (kama vile 3:21-31) na kuendelea (kama vile sura ya nne 4-8). Roho ni kielezo lakini kuna masharti ya kukubali patano. Toba na imani vinahitajika (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21), kama ilivyo utii na pambano!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni vipi sura ya 8 inahusiana na sura ya 7?

2. Kama hakuna laana, dhambi inaathiri nini maisha ya muumini?
3. Je, Roho na Yesu hukaa ndani ya muumini (mst. 9)
4. Ni vipi asili iliathiriwa na dhambi ya mwanadamu (mist.19-22)? Asili itakuwa mbali na mbingu (kama vile Isa 11:6-10)?
5. Roho atuombeaje (mist 26-27)? Hii ina maana "kunena kwa lugha"
6. Ni vipi biblia inasema vitu vyote vinafanywa kwa uzuri kama katika dunia ya uovu (mst. 28)? Fafanua "uzuri" (mst.29)
7. Kwa nini utakaso umeachwa katika mlolongo wa matukio ya kithiolojia katika mst.30?
8. Kwa nini mistari 13-39 inasema kuwa na sura ya kimahakama?
9. Orodhesha vitu vinne katika mst. 34 vinavyotetea kuhusu Yesu.

# WARUMI 9

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Uchaguzi wa Mungu | Israeli kumkataa Kristo | Tatizo la Israeli Kutoamini | Mungu na watu wake | Maslahi ya Israeli |
| 9:1-5 | 9:1-5 | 9:1-5 | 9:1-5 | 9:1-5 |
| | Kukataa kwa Israel na kusudi la Mungu | Ahadiya Mungu kwa Israeli haijashindwa | | Mungu ametunza ahadi yake |
| 9:6-13 | 9:6-13 | 9:6-13 | 9:6-13 | 9:6-13 |
| | | | 9:10-13 | |
| | Kukataa kwa Israeli na haki ya Mungu | Haki ya Mungu kuchagua | | Mungu hana upendeleo |
| 9:14-18 | 9:14-29 | 9:14-18 | 9:14-18 | 9:14-18 |
| Ghadhabu ya Mungu na huruma | | | Hasira ya Mungu na huruma | |
| 9:19-29 | | 9:19-26 | 9:19-21 | 9:19-21 |
| | | | 9:22-29 | 9:22-24 |
| | | | | Wote waliambiwa katika Agano la Kale |
| | | | | 9:25-29 |
| | | 9:27-29 | | |
| Israeli na injili | Hali ya sasa ya Israeli | Haki ya kweli ni kwa imani | Israeli na Injili | |
| 9:30-10:4 | 9:30-33 | 9:30-10:4 | 9:30-10-4 | 9:30-33 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. viii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya  ya tatu

4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

A. Pamekuwa na njia mbili za kuelewa uhusiano wa fasihi hii na sura 1- 8.
   1. Ni mada tofauti kabisa, iliyotengwa kithiolojia.
      a. Kunautofauti mkubwa na uhaba wa muungano wenye mantiki kati ya 8:39 na 9:1.
      b. Inahusiana moja kwa moja na mvutano wa kihistoria katika kanisa la Roma kati ya Wayahudi walioamini na watu wa mataifa walioamini. Ilikuwa pengine panahusishwa na kukua kwa uongozi wa watu wa Mataifa wa Kanisa.
      c. Palikuwa na kutoelewa kuhusu mahubiri ya Paulo kuhusu Israeli (na Sheria) na utume wake kwa watu wa Mataifa (kupewa neema bure), kwa hiyo, anashughulika na mada hii katika sehemu hii.
   2. Ni kilele na hitimisho lenye mantiki la uwasilisho wa injili ya Paulo.
      a. Paulo anahitimisha sura ya 8 kwa ahadi ya "hakuna utengano na upendo wa Mungu." Vipi kuhusu kutoamini kwa watu wa agano?
      b. Warumi 9 – 11 inajibu fumbo la injili kuhusu kutoamini kwa Israeli!
      c. Paulo amekuwa akielezea suala hili hili katika barua yake yote (kama vile 1:3, 16; 3:21, 31 na 4:1na kuendelea).
      d. Paulo anadai kuwa Mungu ni mkweli kwa neno lake. Vipi kuhusu neno lake la Agano la Kale kwa Israeli? Je ahadi zake zote ni bure na tupu?

B. Kuna njia kadhaa zinazoweza kudokeza kifungu hiki cha fasihi
   1. kwa matumizi ya Paulo ya lugha yanayoonesha kama mpingaji(mkemeaji).
      a. 9:6
      b. 9:14
      c. 9:19
      d. 9:30
      e. 11:1
      f. 11:11
   2. Warumi 9 -11 inaunda fungu la kifasihi(mgawanyiko wa sura na mistari si kazi iliyovuviwa na iliongezwa baadaye). Ni lazima itafasiriwe yote kwapamoja kama ilivyo kamilifu. Ingawa, kuna migawanyo mikubwa mitatu ya somo.
      a. 9: 1 -29 (ikiangalia juu ya ukuu wa Mungu)
      b. 9:30 – 10:21(ikiangalia uwajibikaji wa mwanadamu)
      c. 11: 1 – 32 (kujumuishwa kwa Mungu, milele, kusudi la ukombozi)
   3. kwa mada kuu: mchanaganuo mzuri wa sehemu hii ya Warumi unapatikana katika mgawanyo wa aya za NKJV uliofanywa na wachapishaji wa Thomas Nelson
      a. Israeli kumkataa Kristo, 9:1-5
      b. Israeli kukataa kusudio la Mungu, 9:6-13
      c. Israeli kukataa haki ya Mungu, 9:14-29
      d. Hali ya sasa ya Israeli, 9:30-33
      e. Israeli na injili, 10:1-13
      f. Israeli kukataa injili, 10:14-21
      g. Kukataa kwa Israeli si kwa ujumla, 11:1-10
      h. Kukataa kwa Israeli siyo mwisho, 11:11-36

C. Kipengele hiki ni kama zaidi ya kilio kutoka katika moyo kama wasilisho kutoka katika fikra (kidokezo chenye mantiki) hisia yake inakumbusha mojawapo ya mambo mazito ya Mungu kuhusu Israel iliyoasi katika Hosea 11:1-4,8-9.Kwa namna mbalimbali maumivu na uzuri wa Sheria katika sura ya 7 viko sambamba katika sura ya 9-10. Kwa hali zote roho ya Paulo iliumia juuya ugumu wa sheria toka kwa Mungu ambayo ilileta kifo badala ya uzima!

D. Matumizi ya Paulo ya zaidi ya nukuu 25 za Agano la Kale katika sura ya 9-11ikionyesha nia yake ya kufafanua fumbo la Israeli kutoka vyanzo vya Agano la Kale,kama alivyofanya katika Sura ya 4, na siyo tu uzoefu wa sasa. Wengi wao wa uzao wa Abrahamu umemkataa Mungu, hata wakati uliopita (kama vile Matendo 7; Nehemia 9)

E. Andiko hili, kama Waefeso 1:3-14, linashughulika na makusudi ya Mungu kwa ukombozi wa wanadamu wote.Mwanzoni inaonekana kuelezea Mungu katika kuchagua baadhi ya watu na kukataa watu wengine (supralapsarian Calvinism), hata hivyo,ninafikiri mtazamo siyo watu binafsi, bali kuhusu mpango wa Mungu wa milele wa ukombozi (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; na 13:29, Tazama Mada Maalum katika 8:28)

*Jorome Biblical Commentary,juzuu ya 2*, "Agano Jipya''iliyohaririwa na Joseph A. Fitzmyer and Raymond E. Brown, inasema:

''Tangu mwanzo ni muhimu kutambua kuwa mtazamo wa Paulo ni wa ujumuisho; yeyehajadili uwajibikaji wa watu binafsi. Kama inaonekana kuleta swali la imani kuwa, Mungu alijua kabla. Hii haihusiani na mtu kujua utukufu wa Mungu kabla (uk. 318).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA SURA YA 9

A. Ni badiliko kubwa kiasi gani la mwenendo kati ya sura ya 8 na sura ya 9.
B. Kipengele cha kifasihi ( 9- 11) kinashughulika kithiolojia na:-
    1. Msingi wa wokovu
    2. Kusudi la uchaguzi wa Mungu
    3. Ukosefu wa imani kwa waisraeli wasioamini dhidi ya imani ya YHWH.
    4. Jumuisho la wanadamu wote katika ukombozi wa Yesu.
C. Sura ya 9 ni mojawapo ya kurasa zenye uzitosana katika Agano Jipya kuhusu Ukuu wa Mungu (yaani mtu mwingine Efe. 1: 3 -14) wakati sura ya 10 inasema wazi na kwa kurudia nia huru ya mwanadamu (kama vile "kila mmoja" mst. 4; "yeyote yule" mist. 11, 13; "wote" mst. 12 [mara mbili]). Paulo hakujaribu hata kupatanisha mvutano huu wa kithiolojia. wote wanasema kweli! Maandiko mengi ya kibiblia yametayarishwa katika hali ya kimafumbo au mafungu ya kiuhakiki.Mifumo mingi ya kithiolojia ni ya kimantiki, bali kuthibitisha kimaandiko ni kigezo kimoja tu cha ukweli wa kibiblia. Wote akina-Augustino na ki-Kalvin dhidi ya akina- Pelagiani naArminiani wana viashirio vya ukweli na makosa. Mvutano wa kibiblia kati ya imani, bila shaka ni mfumo wa kithiolojia ulio hakikiwa kimaandiko, uliotulia, usio na upande ambao unaipeleka biblia kwenye hali ngumu isiyokubalika au kutafsirika. Tazama Mada Maaalum Tafsiri ya mashariki katika 3:27.
D. 9:30-33 ni ufupisho wa sura ya 9 na dhima ya sura ya 10.
E. Angalia, ni mara ngapi Paulo anatumia maandiko ya Agano la Kale katika hoja zake. Hii inaweka mashaka ya awali ya uongozi wa Wayahudi katika Warumi.
    1. mst. 7 – Mwa. 21:12

2. mst. 9 – Mwa. 18:10,14
3. mst. 12-Mwa. 25:32
4. mst. 13 –Mal. 1:2-3
5. mst. 15 –Kut. 33:19
6. mst. 17 - Kut. 9:16
7. mst. 25 –Hos. 2:23
8. mst. 26 – Hos. 1:10
9. mst. 27 – Isa. 10:22
10. mst. 28 – Isa. 10:23
11. mst. 29 – Isa. 1:9
12. mst. 33 – Isa. 28:16 na 8:14

Kuna nukuu nyingine zaidi za Agano la Kale katika sura ya 19 na 11!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9:1-5**
**[1]Nasema kweli katika Kristo, sisemi uongo, dhamira yangu ikinishuhudia katika Roho Mtakatifu, [2]Ya kwamba nina huzuni nyingi na maumivu yasiyokoma moyoni mwangu. [3]Kwa maana ningeweza kuomba mimi mwenyewe niharimishwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu kwa jinsi ya mwili; [4]ambao ni Waisraeli, wenye kule kufanywa wana, na ule utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Mungu, na ahadi zake; [5]ambao mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili. Ndiye aliye juu ya mambo yote, Mungu, mwenye kuhimidiwa milele. Amina.**

**9:1-2** Mistari ya kwanza na 2 inaunda sentensi moja kwa Kiyunani. Paulo anatoa sababu kadhaa (kanisa katika Roma) ambazo wangejua kuwa alikuwa anaelezea ukweli.

1. muungano wake na Kristo mst. 1
2. hali yake tambuzi iliyoongozwa na Roho mst. 1
3. hisia zake za dhati kwa Waisrael mst. 2

**9:1 "Ninasema ukweli katika Kristo, sisemi uongo"** Paulo mara kadhaa amenena aina hii ya usemi wake wa tabia ya ukweli (kama vile 2 Kor. 11:10; Gal. 1:20; 1 Tim. 2:7) au usemi wa aina hiyo hiyo kuhusu Mungu kama shahidi, (kama vile Rum. 1:9; 2 Kor. 1:23; 11:31; Flp. 1:8; 1 The. 2:5,10). Ilikuwa ni namna yake ya kutetea ukweli wa mafundisho yake na mahubiri. Uzoefu akiwa njiani kwenda Damaska ulibadili kila kitu!

◙ **"dhamiri yangu"** Hii inamaanisha hali ya utambuzi kimaono unaoongozwa na Roho wa Mungu aliompa muumini. Kwa namna moja tu, hiki ni chanzo muhimu cha mamlaka kwa waumini. Ni neno la Mungu, linaloeleweka na kutumiwa na Roho wa Mungu kwa mawazo yetu (kama vile 1 Tim. 1:5,19). Tatizo linakuja wakati waumini na hasa wasioamini wanapoendelea kukataa neno na Roho; sasa inakuwa rahisi kukadiria dhambi ya mtu husika (kama vile 1 Tim. 4:2). Dhamiri yetu inaweza dhibitiwa kiasili au kwa kujizoeza.

## MADA MAALUM: DHAMIRI

Paulo anatumia neno "dhamiri" mara kadhaa katika barua za Wakorintho (kama vile 4:4; 8:7,10,12; 10:25,27,28,29; 2 Kor. 1:12; 4:2; 5:11). Inarejeresha ile hisia adilifu ya ndani ya lipi sawa au si sawa (kama vile Mdo. 23:1). Dhamiri yetu inaweza kuathiriwa na maisha yetu ya nyuma, uchaguzi wetu dhaifu au Roho ya Mungu. Si mwongozo usio na dosari, bali inaamua mipaka ya imani ya mtu binafsi. Kwa hiyo, kuipinga dhamiri

hata kama iko katika makosa au udhaifu, ni tatizo kubwa la imani.
Dhamiri ya Waumini, inahitaji kutengenenezwa kila mara kwa neno la Mungu na la Roho wa Mungu (kama vile 1 Tim. 3:9). Mungu atahukumu waumini kwa uelewa walio nao (dhaifu au imara) lakini sisi sote tunabidi kuwa wazi kwa Biblia na Roho wa Mungu zaidi na kukua katika maarifa ya Bwana Yesu Kristo. Tazama nukuu kamili juu ya “dhamiri” katika 2 Kor. 10:25. Tazama Mada Maalum: Udhaifu

◙
**NASB, NKJV “kunishuhudia katika Roho Mtakatifu”**
**NRSV “kuithibitisha kwa Roho Mtakatifu”**
**TEV “kutawaliwa na Roho Mtakatifu”**
**NJB “katika Muungano naRoho Mtakatifu anayenifikiria”**

Paulo aliamini kuwaalikuwa na wito maalum na mamlaka toka kwa Kristo (kama vile Mdo. 9: 1- 22; Gal. 1: 1) NENO (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, kama vile 2:15) ni muungano na neno *sun* (la kawaida sana kwa Paulo). Alishawishika na uelewa wake mpya ulikuwa juu ya

1. ufunuo wa Kristo
    a. barabarani kwenda Damaska
    b. Kufundishwa Uarabuni (Nebetean)
2. ushahidi wa ndani wa Roho

Alikuwa mtume na alizungumza kwa mamlaka ya Kimungu (kama vile 1 Kor. 7:25,40). Alishiriki majonzi ya Mungu juu ya wasioamini na taifa la Israeli (kama mst. 2). Walikuwa na faida nyingi sana (kama vile mist. 4-5).

**9:3**
**NASB, NKJV**
**NRSV “Kwa vile nilitamani…..”**
**TEV “Kwa ajili yao ningetamani”**
**NJB “Ningalipendelea……”**

Paulo alifikiriasana kwa ajili ya watu wake, Israel, kuwa kama utengano wake ungeathiri kujumuishwa kwao, angekuwa tayari, mst. 3. Mstari huu una maana ya nguvu na msisitizo wa muundo fasaha (KITENZI CHA KATI ELEKEZI KISICHOTIMILIFU) ikiwa na yote *autos* na *egō*, na KITENZIJINA CHA WAKATI ULIOPO). Uzito na ugumu wa ombi hili ni sawa kabisa na maombezi ya ndani ya Musa kwa Waisraeli watenda dhambi katika Kutoka 32:30-35.Hii inaeleweka vizuri zaidi kama usemi wa kutamani, usiyo kweli. Inafanana namatumizi ya NJEO ISIYO TIMILIFU katika Gal. 4:20.Tazama Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUMU: MAOMBI YA KUSIHI

I. Utangulizi
  A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
    1. Maombi binafsi, Mk 1:35; Luk 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
    2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk 11:17; Luk 19:46
    3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luk 11:2-4
  B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
  C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
  D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
  E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza

kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.

F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
   1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
   2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
   3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
   4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
   5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba

G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

II. Taarifa za Kibiblia

A. Agano la Kale
   1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
      a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22ff
      b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
         1) Kutoka 5:22-23
         2) Kutoka 32:9-14,31-35
         3) Kutoka 33:12-16
         4) Kutoka 34:9
         5) Kumbu. 9:18,25-29
      c. Samweli akiiombea Israeli
         1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
         2) 1 Samweli 12:16-23
         3) 1 Samweli 15:11
      d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
   2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
   3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
      a. Zaburi 66:18
      b. Mithali 28:9
      c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya
   1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho
      a. Yesu
         1) Warumi 8:34
         2) Waebrania 7:25
         3) 1 Yohana 2:1
      b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
   2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi
      a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
         1) Warumi 9:1ff
         2) Warumi 10:1
      b. Akiliombea kanisa
         1) Warumi 1:9
         2) Waefeso 1:16
         3) Wafilipi 1:3-4,9
         4) Wakolosai 1:3,9
         5) 1 Wathesalonike 1:2-3
         6) 2 Wathesalonike 1:11
         7) 2 Timotheo 1:3
         8) Filemon, uk. 4

c. Paulo analiomba kanisa limwombee
    1) Warumi 15:30
    2) 2 Wakorinthp 1:11
    3) Waefeso 6:19
    4) Wakolosai 4:3
    5) 1 Wathesalonike 5:25
    6) 2 Wathesalonike 3:1

3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi
    a. Kuombeana wao kwa wao
        1) Waefeso 6:18
        2) 1 Timotheo 2:1
        3) Yakobo 5:16
    b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
        1) Adui zetu, Mt. 5:44
        2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
        3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
        4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
        5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa

A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
    1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
    2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
    3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Yuda 20
    4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

B. Visababishi
    1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
    2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
    3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
    4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

C. Mitazamo mingine
    a. Usitahimilivu
    b. Luka 18:1-8
    c. Wakolosai 4:2
    1. Endelea kuomba
        a. Mathayo 7:7-8
        b. Luka 11:5-13
        c. Yakobo 1:5
    2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
    3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo
        a. Zaburi 66:18
        b. Mithali 28:9
        c. Isaya 59:1-2
        d. Isaya 64:7

IV. Hitimisho la kithiolojia

A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

◙

**NASB "walilaaniwa, *walitengwa* toka kwa Kristo"**
**NKJV "walilaaniwa toka kwa Kristo"**
**NRSV "walilaaniwa na kuondolewa kwa Kristo"**
**TEV "walikuwa chini ya laana ya Mungu na wakatengwa kutoka kwa Kristo"**
**NJB "kwa hiari walitiwa hatiani na kuondolewa kwa Kristo"**

Maana ya asili ya neno "mtakatifu" ni kutengwa pembeni kwa Mungu kwa matumizi Yake. Dhana sawia inahusishwa na maneno "Laana." (*anathema,* kama vile 1 Kor. 12: 3; 16: 22; Gal. 1: 8, 9). Kitu fulani au mtu fulani anatengwa kwa ajili ya Mungu.

Unaweza kuwa uzoefu chanya (kama vile Walawi 27: 28; Luka. 21: 5) au uzoefu hasi (kama vile Yosh. 6- 7; Rum. 9: 3), kutegemeana na habari husika.

## MADA MAALUM: LAANA (*anathema*)

I. AGANO LA KALE

Kuna maneno mbalimbali kwa ajili ya neno "laana." *Herem* (BDB 356, KB 353) yaliyotumika kwa kitu Fulani kilichotolewa kwa Mungu (kama vile toleo la LXX linakitafasiri kama *anathema,* BAGD 54, Law. 27:28). Mara nyingi lilitumika kuangamiza vitu kwa sababu ni vitakatifu mno kwa mwanadamu kuvitumia (kama vile Kumb. 7:26; Yos. 6:17-18; 17:12). Lilikuwa ni neno lililotumika kwenye dhana ya "vita vitakatifu." Mungu alimwambia Yoshua kuwaangamiza Wakanani. Yeriko ilikuwa fursa ya kwanza, "matunda ya kwanza" ya maangamizo matakatifu.

II. AGANO JIPYA

Katika Agano Jipya neno *anathema* na miundo yake yenye kuhusiana ilitumika katika maana tofauti mbalimbali:

A. kama zawadi au matoleo kwa Mungu (kama vile Luka 21:5)
B. kama kiapo cha kifo (kama vile Mdo. 23:14)
C. kulaani na kuapa (kama vile Marko 14:71)
D. kanuni ya laana inayohusiana na Yesu (kama vile 1 Kor. 12:3)
E. kumtoa mtu fulani au kitu Fulani kwenye hukumu au maangamizo kwa Mungu (kama vile Rum. 9:3; 1 Kor. 16:22; Gal. 1:8-9)

Namba D hapo juu ni yenye mkanganyiko. Nimejumuisha hoja zangu toka 1 Kor. 12:3:

> "Yesu kushitakiwa" ni maelezo yenye kushtua. Kwa nini mtu yeyote angaliweza (isipokuwa mila za Kiyahudi) ambaye anadai kuzungumza kwa ajili ya Mungu aliseme hili? Neno (yaani., *anathema*) lenyewe lina mazingira ya Agano la Kale (yaani., Kiebrania, *herem*). Linahusiana na dhana ya vita takatifu, ambapo mji ulitolewa kwa Mungu na, kwa hiyo, ukawa mtakatifu. Hii inamaanisha kuwa kila kitu ndani yake chenye kupumua, mwanadamu au mnyama, kinapaswa kufa (kama vile Yosh. 6:17; 7:12). Nadharia ya jinsi neno hili lilivyotumika huko Korintho ni:
>
> 1. kuwa lina mazingira ya Kiyahudi yanayohusiana na kiapo cha kwenye Sinagogi (kama vile Mdo. 26:11, yaani., baadaye, kanuni za laana za dini ya Kiyahudi zilitumika kuuondoa Ukristo toka kwenye Sinagogi). Ili kubaki mwanachama ilibidi mtu amukatae Yesu au kumulaani Yesu wa Nazareti.
> 2. kuwa lina mazingira ya Kirumi yenye kuhusiana na kumwabudu mfalme mkuu ambapo Kaisari angeitwa "Bwana"
> 3. kuwa lina mazingira ya ibada za kipagani ambapo laana ziliitishwa juu ya watu kwa kutumia jina la mungu. Hili baadaye lingeweza kutafasiriwa, "Yesu na akulaani

______" (kama vile 1 Kor. 16:22).

4. Kuwa mtu Fulani ahusianaye na kifungu kwenye dhana na kithiolojia ya Yesu kutoa laana ya Agano la Kale kwa ajili yetu (kama vile Kumb. 21:23; Gal. 3:13).
5. Uchunguzi wa hivi karibuni toka huko Korintho (kama vile tanbihi #1 uk. 164 katika nyaraka za Bruce Winter's *After Paul Left Corinth*) bamba za laana zimepatikana juu ya mji wa kale ulijengwa juu ya kilima huko Korintho. Wanazuoni wa Kibiblia wamedhani kuwa KITENZI chenye kuhusiana na "ni " yapaswa kuwekwa kwenye kifungu, "Yesu anashitakiwa," lakini huu ushahidi wa elimukale kwa uwazi yanaonyesha kuwa hizi laana za kipindi cha Warumi cha karne ya kwanza Toka Korintho zinapungukiwa KITENZI (kama zifanyavyo baadhi ya laana katika toleo la LXX la Kumb. 22:15-20), kama ilivyo 1 Kor. 12:3. Kuna ushahidi zaidi wa elimukale kuwa Wakristo wa karne ya kwanza ya Warumi huko Korintho walitumia kanuni ya laana kwenye utaratibu wa maziko (yaani., kipindi cha Byzantine, zilizopatikana kwenye makaburi ya Wakristo (J. H. Kent, The Inscriptions, 1926-50. Princeton: American School of Classical Studies, 1966, vol. 8:3, no. 644).

Baadhi ya vipengele vya kanisa huko Korintho walikuwa wakirudia kwenye laana za kipagani kwa jina la Yesu dhidi ya washirika wengine wa kanisa. Sio tu kwenye tatizo la utumiaji, bali pia kwenye muonekano wa chuki. Huu ni mfano mwingine wa mvutano ndani ya kanisa. Paulo aliwahitaji kulijenga kanisa, kuliimarisha kanisa, walitaka kulaani kulaani sehemu ya kanisa!

◙ **"ukoo wangu kulingana na mwili"** Tazama Mada Maalum katika 1:3.

**9:4-5** Mfuatano huu wa MAFUNGU NOMINO zinaelezea undani wa faida ya Israeli. Kutoamini kwao kulikuwa suala la kulaumiwa katika faida hizi. Nani kapewa kingi, kingi kinatakiwa (kama vile Luka. 12:48)!

**9:4 "Waisraeli"** Hili lilikuwa jina la agano katika Agano Jipya kwa uzao wa Abrahamu. Baada ya kikwazo kikubwa na Mungu, jina la Yakobo lilibadilishwa kuwa Israeli (Mwa. 32:28). Likawa ni jina la jumla la Taifa la Wayahudi.

Asili yake inaweza kuwa "*El* (Mungu) stahimili" na kwa uamuzi wake, siyo kwa hila za Yakobo.

## MADA MAALUM: ISRAELI (Jina)

I. Kwa mshangao maana ya jina haijulikani (BDB 975, KB 442).
   A. *El* Kug'ag'ania
   B. Mwache *El* ag'ag'ane (KAULI AMRISHI)
   C. *El* Hulinda
   D. *Mwache El* na apambane
   E. *El* Achuchumilie
   F. Yule apambanaye na Mungu (neno la mzaha la Mwa. 32:28)
   G. Mwenye Kutegemewa (IDB, juzuu ya 2, uk. 765)
   H. Aliye fanikiwa
   I. Furaha

II. Matumizi katika Agano la Kale
   A. Jina la Yakobo (mbadilishaji, mshika kisigino, BDB 784, KB 872, kama vile Mwa. 25:26) linabadilishwa baada ya kushindana mweleka na mtu katika mto Yaboki (kama vile Mwa. 32:22-32; Kut. 32:13). Mara nyingi maana ya majina ya Kiebrania ayanatamkika kama lahaja, si kwa asili zake (kama vile Mwa. 32:28). "Israeli" likawa jina lake la kupewa (kama vile, Mwa. 35:10).
   B. Hili lilikuja kutumika kama jina la jumla kwa wana wote kumi na wawili wa Yakobo (mf. Mwa.

32:32; 49:16; Kut. 1:7; 4:22; 28:11; Kumb. 3:18; 10:6).

C. Hili lilikuja kubeba wadhifa wa taifa lililoundwa kwa makabila kumi na mawili kabla ya kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile Mwa. 47:27; Kut. 4:22; 5:2) na baadaye (kama vile Kut. 1:1; 18:6; 33:10).

D. Baada ya muungano wa utawala wa kifalme wa Sauli, Daudi, na Suleimani chini ya waliyatenga makabila Rehoboamu (kama vile 1 Fal. 12).
   1. tofauti inaanza hata kabla ya utenganishaji wa kiutawala (mf. II Sam. 3:10; 5:5; 20:1; 24:9; 1 Fal. 1:35; 4:20)
   2. hili linabeba wadhifa wa makabila ya kaskazini hadi kufikia kuanguka kwa Samaria hadi Ashuru katika 722 K.K. (kama vile 2 Wafalme 17).

E. Hili linatumika kumaanisha Yuda katika maeneo machache (mf. Isaya 1; Mika 1:15-16).

F. Baada ya kupelekwa utumwani Ashuru na Babeli kwa mara nyingiine jina hili lilikuwa jina la ujumla kwa vizazi vya Yakobo vilivyoishi katika Palestina (mf. Isa. 17:7,9; Yer. 2:4; 50:17,19).

G. Hili lilitumika jumuisho la muundo wa kuwatofautisha makuhani (kama vile 1 Nya. 9:2; Ezra 10:25; Neh. 11:3).

◙ **"nani wanahusika na urithi kama wana"** Katika Agano la Kale WINGI wa "wana" kawaida lilimaanisha malaika (kama vile Ayubu 1:6; 2:1; 38:7; Kumb. 3:25; Zab. 29:1; 89:6-7), wakati katika hali ya UMOJA lilimaanisha

1. Wafalme wa Israeli (kama vile 2 Sam 7:14)
2. Taifa (kama vile Kut. 4:22,23; Kumb. 14:1; Hosea 11:1)
3. Masihi (Zab. 2:7)
4. Inaweza kuhusu wanadamu (kama vile Kumb. 32:5; Zab. 73:15; Ezek. 2:1; Hosea 1:10; Kut. 6:2 nitata; linaweza pia kumaanisha chochote). Katika Agano Jipya lilimaanisha pia yeyote katika familia ya Mungu.

Neno kubwa la Paulo katika wokovu lilikuwa ni "kuasili" (kama vile Rum. 8:5,23; Gal. 4:5; Efe. 1:5). Wakati Petro na Yohana walitumia "kuzaliwa upya" yote ni maneno yaliyozoeleka. Siyo ya Kiyahudi balini ya Kiroma. Kuasili ulikuwa ni mchakato wa kisheria uliokuwa mgumu na uliochukua muda chini ya sheria za Rumi. Mara mtu akishaasiliwa, huchukuliwa kama ni mtu mpya, ambaye kisheria hawezi milikiwa au kuuwawa na baba aliyemwasili.

◙ **"utukufu"** Mzizi wa neno hili kwa Kiebrania ni "kuwa kizito" ambacho ilikuwa neno mbadala kwa kitu kilichokuwa cha thamani. Hapa ina maana ya

1. Mungu kujidhihirisha Mwenyewe katika mlima Sinai (kama vile Kut. 19:18-19)
2. Wingu la utukufu *Shekinah* lililoongoza Waisraeli katika kipindi cha safari ndefu jangwaani (kama vile Kut. 40:34-38)YHWH kipekee alijidhihirisha mwenyewe kwa Israeli. Uwepo wa YHWH ulitambulika kama utukufu Wake (kama vile 1 Fal. 8:10-11; Eze. 1:28). Tazama Mada Maalum katika 3:23.

◙ **"maagano"** Katika maandiko ya Kiyunani ya zama hizo $P^{46}$, B, F na G, neno la UMOJA "agano" linatumika. Hata hivyo neno hili katika WINGI linatumika katika MSS א, C, na maneno mengine ya zamani ya Kilatini, Vulgate, na Koptiki. $UBS^4$ inatoa alama B katika WINGI (karibia hakika). Hata hivyo katika WINGI hautumiki katika Agano la Kale. Kuna maagano kadhaa maalum katika Agano la Kale: Adamu, Nuhu, Abrahamu, Musa na Daudi. Kwa vile kuletwa kwa sheria kumetajwa mbeleni, hii bila shaka inalenga Agano la Abrahamu ambalo ndilo Paulo aliloona kama la msingi (kama vile 4:1-25; Gal. 3:16-17) na lilirudiwa mara kadhaa (yaani, Mwanzo 12,15,17) na kwa kila Kiongozi wa juu wa dini.

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni "kukata"ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano (kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji. Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abraham (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya" (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi)

◙ **"utoaji waSheria na huduma katika nyumba ya Mungu"**Hii inamaanisha:

1. Musa anapokea sheria katika mlima Sinai (Kutoka. 19- 20)
2. kibanda cha kusalia katika Kipindi cha Kusafiri Nyikani (kama vile Kutoka. 25- 40 na Walawi).

◙ **"ahadi"** Mungu ameweka wazi mipango Yake ijayo (kama vile 1:2; Mdo. 13: 32; Tit. 1:2; Ebr. 1:1) kupitia katika Agano la Kale. Kwa vile "maagano"yalikwisha tajwa awali,"ahadi" bila shaka zinamaanisha kwa Masia (kama vile mst. 5, kwa mfano, Mwanzo. 3: 15; 49:10; Kumb. 18: 15, 18- 19; 2 Sam. 7; Zab. 16: 10; 118: 22; Isa.7: 14; 9: 6; 11: 1- 5; Dan. 7: 13, 27; Mika 5: 2-5a; Zek. 2: 6- 13; 6: 12- 13; 9: 9; 11: 12). Ahadi (maagano) hizi zote ni zile za masharti na zisizo za masharti. Hazikuwa za masharti kwa upande wa utendaji wa Mungu (kama vile Mwa. 15:12-22), lakini zilikuwa na masharti kwa imani na utii wa mwanadamu (kama vile Mwa. 15: 6 na Warumi. 4). Ni Waisraeli tu waliokuwa na ufunuo wa Mungu kabla ya ujio wa Kristo (isipokuwa kwa Ayubu, Yethro).

**9: 5 "mababa"**Hii ilihusu Abrahamu, Isaka na Yakobo na viongozi wakubwa wa dini wa mwanzo. 12- 50 (kama vile Rum. 11: 28; Kumb. 7: 8; 10: 15).

◙ **"ni kutokana na aliyeKristo kulingana na mwili"** Hii inamaanisha ukoo wa kimaumbile wa Masia (kama vile 1: 3; Tazama mada maalum "Masihi" katika. 1: 4), Aliyepakwa Mafuta, mtumishi maalum aliyechaguliwa na Mungu ambaye angekamilisha ahadi na mipango ya Mungu, (kama vile 10: 6).

Neno "Kristo" nitafasiri ya kiebrania "Aliyepakwa Mafuta."Katika Agano la Kale, makundi matatu ya viongozi walipakwa mafuta maalum matakatifu.

1. wafalme wa Israeli
2. viongozi wakuu wa dini waIsraeli.
3. manabiikatika Israeli.

Ilikuwa ni alama ya Mungu ya uchaguzi na kuwaandaa kwa ajili ya huduma Yake. Yesu alikamilisha kazi hiyokwa wote hawa watatu (kama vile Ebr. 1:2- 3). Alikuwa ni ufunuo kamili wa Mungu kwa sababu alikuwa mfano wa Mungu (kama vile Isa. 7:14; 9: 6; Mika 5: 2- 5a, Kol. 1:13- 20).

Kwa "mwili", Tazama Mada Maalumkatika 1: 3.

◙

**NASB "Kristo, kwa kutokana na mwili, aliye juu ya yote, Mungu alimbariki milele"**
**NKJV "Kristo alikuja, aliye juu ya wote, aliye barikiwa milele na Mungu"**
**NRSV "Anakuja Masihi, aliye juu ya wote, Mungu alimbariki milele"**
**TEV "na Kristo kama mwanadamu, akiwa mmoja wao wa mwanadamu, Mungu atawalaye vyote atukuzwe Milele"**
**NJB "Alikuja Kristo, aliye juu ya wote, Mungu milele amebarikiwa"**

Kisarufi, hii ingeweza kumaanisha kumsifu Baba (TEV, kufuatana na mila za Kiyahudi), lakini mazingira yanapendelea uthibitisho wa Paulo kwa uungu wa Yesu (haifuatani na kielelezo cha Wayahudi cha kumsifu YHWH katika LXX tazama J. Murray, II, uk. 245- 248). Japo Paulo hatumii neno *Theos* kwa Yesu mara nyingi, lakini hulitumia (kama vile Matendo. 20: 28; 2 The.7:12; Tito. 2:13; Flp. 2:6). Mapadri wote wa makanisa ya kale walitafsiri andiko hili kama kumaanisha Yesu. Bruce Metzger, *ATextual Commentary on the Greek New Testament*, uk. 520- 522, kinaonesha kuwa chaguzi tofauti zinahusishwa na palipo na alama na funga semi zilipo. Maandiko ya zamani hayakuwa na:

1. matumizi ya herufi kubwa
2. alama za kufunga na kufungua semi
3. mgawanyiko wa aya
4. hata tu nafasi kati ya maneno

◙ **"nani aliyeko juu ya wote"** Hii pia ingeweza kuwa ni fungu la kumwelezea Mungu Baba au Yesu Mwana. Iinaakisi usemi wa Yesu wa Mat. 28: 19 na Paulo katika Kol.1:15- 20. Fungu hili zuri lilionyesha kimo cha ujinga cha Waisraeli kumkataa Yesu wa Nazareti.

◙ **"milele"**Hii kwa lugha rahisi ni fungu la nahau ya Kiyunani "katika enzi" (kama vile Luka. 1:33; Rum. 1:25; 11:36; Wagal. 1: 5; 1 Tim. 1:17). Hayani miongoni mwa mafungu kadhaa yanayoweza kushabihiana. (1) "katika enzi" (kama vile Mt. 21:19 [Marko 11: 14]; Lk. 1: 55; Yn. 6: 5, 58; 8: 35; 12:34;13: 8;14: 16; 2 Kor. 9: 9)au (2) "wakati wa nyakati" (kama vile Efe. 3: 21). Haionekani kuwapo na utofati kati ya nahau hizi "milele."Neno "nyakati" linaweza kuwa katika hali ya WINGI katika kuonesha sura au namna ya kitu katika muundo wa kisarufi wa viongozi wa kidini wa enzi hizo ulioitwa "wingi wa ukuu wa enzi" au inaweza kumaanisha dhana ya kadhaawakadha ya"nyakati" katika maana ya Wayahudi ya "enzi zilizokuwa bila makosa" "enzi za ukaidi" "enzi ya kuja" au "enzi ya haki."

◙ **"Amina"** Tazama mada maalum katika 1:25.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9: 6- 13**
**6Si kama kwamba neno la Mungu limetanguka. Maana hawawi wote Waisraeli walio wa uzao wa Israeli. 7Wala hawawi wote wana kwa kuwa wazao wa Ibrahimu, bali, Katika Isaka wazao wako wataitwa, 8yaani, si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao. 9Kwa maana neno la ahadi ni hili, Panapo wakati huu nitakuja, na Sara atakuwa na mwana.10Wala si hivyo tu, lakini Rebeka naye, akiisha kuchukua mimba kwa mume mmoja, naye ni Isaka baba yetu,11(kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia yake aitaye), 12aliambiwa hivi, Mkubwa atamtumikia mdogo. 13Kama ilivyoandikwa, Nimempenda Yakobo bali Esau nimemchukia.**

**9: 6 "neno la Mungu**" katika maandiko haya, fungu hili linamaanisha ahadi za mapatano ya Agano la Kale. Ahadi za Munguni hakika (kama vile Nah.23:19; Yosh. 21: 45; 23:14; 2 Fal. 10:10; Isa. 40: 8; 55:11; 59:21).

◙
**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB "ameshindwa"**
**NKJV "hajaleta athari yoyote"**

Neno hili (*ekpiptō*) lilitumika katika maandiko ya kale mara kadhaa kwa kitu (kama vile Isa. 6:13) au mtu fulani (kama vile Isa. 14:12) anayeanguka. Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA ambayo inamaanisha hali ya kuwa na matokeo ya kudumu (lakini linapingwa). Tazama nukuu hapo juu kwa uhakika wa neno la Mungu.

◙
**NASB "Maana hawawi wote Waisraeli walio wa uzao wa Israeli"**
**NKJV "Kwa vile siyo wote Waisraeli ni Waisraeli"**
**NRSV "Kwa kuwa sio Waisraeli wote kweli ni wa Israeli "**
**TEV "Kwa kuwa sio watu wote waIsraeli ni watu wa Mungu"**
**NJB "Sio wotewanaotokana na Israeli ni Waisraeli**."

Maana ya usemi huu wa fumbo unazungukia maana mbali mbali tofauti za kibiblia kwa neno "Israeli."
1. Israeli, ikimaanisha uzao wa Yakobo (kama vile Mwa.32:22- 32).
2. Israeli, ikimaanisha watu waliochaguliwa na Mungu (kama vile TEV).
3. Israeli ya kiroho, Israeli ikimaanisha kanisa, (kama vile Gal. 6:16; Pet. 2: 8, 9; Ufu. 1: 6 dhidi ya Israeli asili (kama vile mist. 3- 6).

Baadhi tu ya watoto wa Abrahamu walikuwa watoto wa ahadi (kama vile mst.7). Hata Wayahudi hawakuwa sahihi na Mungu kufuatana tu na koo zao (kama vile mst.7), lakini katika imani zao (kama vile 2:28- 29; 4:1ff; Yohana 8:31- 59; Gal. 3:7- 9; 4:23).Ilikuwa ni waumini masalia (tazama Mada Maalumu katika 9: 27- 28). Ambao walipokea ahadi za Mungu na walitembea ndani yake kwa imani (kama vile 9:27; 11: 5). Mst. 6 unaanza mfululizo wa dhana ya upinzani (kama vile 9:14, 19, 30; 11:1). Hii inaendeleza muundo wa Paulo wa makemeo, inawasilisha ukweli kwa namna ya upinzani, (yaani Mal. 1: 2,6,7 [mara mbili], 12, 13; 2:14, 17 [mara mbili]; 3: 7,13,14).

**9: 7** Nusu ya pili ya mstari huu ni nukuu kutoka Mwa. 21:12d. Sio watoto wote wa Ibrahimu walikuwa watoto wa ahadi ya agano la Mungu (kama vile Mwa. 12: 1- 3; 15: 1- 11; 17: 1- 21; 18:1- 15; Gal. 4: 23). Hii inaonyesha utofauti kati ya Ishimaeli na Isaka katika mist. ya 8-9, na Yakobo na Esau katika mist. 10- 11.

**9: 8** Hapa, Paulo anatumia neno "mwili" kumaanisha uzao wa taifa (kama vile 1: 3; 4: 1; 9: 3, 5, tazama Mada Maaluma katika 1: 3). Anatofautisha watoto asilia wa Abrahamu (Wayahudi wa 9:3) na watoto wa kiroho (watoto wa ahadi) wa Abrahamu (wale watakao mwamini Masiha aliyeahidiwa na Mungu kwa imani, kama vile 2:28- 29). Hii <u>siyo</u> tofauti ile katika 8: 4- 11, wanadamu walioanguka dhidi ya wale waliokombolewa.

**9: 9** Hii ni nukuu kutoka Mwanzo. 18:10, 14.Mtoto wa ahadi ("uzao") atakuja kutoka kwa Sara kwa utashi wa Mungu. Hii hatimaye itakamilishwa kwa kuzaliwa Masiha. Isaka alikuwa utimilifu maalum wa ahadi ya Mungu kwa Abrahamu katika Mwa. 12: 1- 3 miaka 13 kabla.

**9: 10** Wake za Abrahamu, Isaka na Yakobo walikuwa tasa; hawakuweza kupata mimba. Kutoweza kwao kupata mtoto ilikuwa mojawapo ya njia za Mungu kuonyesha kuwa Alikuwa ana uwezo wa kutawala ahadi zake za patano, uzao wa Masia. Njia nyingine ilikuwa kwamba uzao wa kweli wa Masiha hauwezi kuendelea kupitia kwa mwana mkubwa wa watawala wa kidini, (ambaye kijadi alitarajiwa). Kubwa ni uchaguzi wa Mungu (kama vile mist.11- 12).

**9: 11- 12** Mist. ya 11- 12 ni sentensi moja katika Kiyunani.Maelezo haya yamechukuliwa kutoka.Mwa. 25: 19- 34. Mfano huu unatumika kuthibitisha kuwa chaguo la Mungu (kama vile mst.16), siyo (1) Uzao wa mwanadamu au (2) mafanikio ya binadamu au ufanisi (kama vile mst. 16). Hii ni namna mpya ya utendaji wa injili, patano jipya (kama vile Yer. 31: 31- 34; Hezekia. 36: 22- 36). Hata hivyo lazima ikumbukwe kuwa, uchaguzi wa Mungu haukukusudiwa kutenga, bali kujumuisha! Masia alikuja kutoka katika uzao uliochaguliwa, lakini Atakuja kwa wote (nani anaitenda imani, kama vile 2: 28- 29; 4: 3, 22- 25; sura ya 10).

**9: 11 "kusudio"** Hili ni neno lililounga kwa maneno *pro* ukiongeza *tithēmi,* lililo na maana zifuatazo.
1. katika Warumi. 3:25
   a. imeweka wazi
   b. zawadi ya kutuliza
2. kupanga kabla ya
   a. wa Paulo, Rum. 1:13
   b. wa Mungu, Efe. 1: 9

NOMINO (*prosthesis*), imetumika katika andiko hili kumaanisha "kutayarisha kabla"
1. Ilitumika kwa mikate katika hekalu, Mt. 12: 4; Marko; 2: 26; Lk. 6: 4
2. Ilitumika kwa kilichofikiriwa kabla chenye kusudio la wokovu wa Mungu, Rum. 8:28; 9: 11; Efe. 1: 5, 11; 3: 10; 2 Tim. 1: 9; 3: 10.

Paulo anatumia maneno kadhaa yaliyoungana yenye KIHUSISHI *pro* (kabla) katika sura ya 8 na 9 ya Warumi na Waefeso 1 (vinaonesha shughuli za Mungu zilizopangwa)
1. *Proginōskō*(alijua kabla), Rum. 8:29
2. *Proorizō* (kusanifu kabla), Rum. 8: 29 (Efe. 1:5; 11), 30 (Efe. 1: 9).

3. *Prothesis* (kusudi lililowekwa kabla), Rum.9:11
4. *Proetoimazō*(kusudi lililowekwa kabla), Rum. 9:23
5. *Prolegō*(lililosemwa kabla), Efe. 9:29
6. *Proelpizō* (lililotumainiwa kabla), Efe. 1:12)

**9: 12** Hii ni nukuu kutoka katika unabii wa Mwa. 25:23iliyohusishwa na Esau na Yakobo. Hii inaonyesha kuwa Rebeka na Yakobo walifanya hivyo kutokana na unabii na siyo kwa faida yao binafsi, kwa kumuandaa Isaka kwa Baraka.

**9:13 "Lakini Esau nimemchukia"** Hii ni nukuu kutoka katika Mal. 1:2-3. "Chukia" ni nahau ya kiebrania ya ulinganifu. Itatoa sauti kali kwa kiingereza, lakini linganisha na Mwa. 29:31- 33, Kumb. 21:15; Mt. 10:37- 38, Luk. 14:26; na Yn. 12:25. Maneno ya kibinadamu"Upendo" na "chuki" unahusiana si kwa mihemko ya Mungu kwa haya, bali kwa kujitoa kwake kwa uzao wa Masihi na ahadi. Yakobo alikuwa mwana wa ahadi kutokana na unabii wa Mwa. 25: 23. Esau, katika Malaki. 1: 2- 3, ikimaanisha Taifa la Edomu (uzao wa Esau).

## MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UUNGU

IV. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
   E. Viungo vya mwili
      11. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
      12. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
      13. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
      14. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
      15. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
      16. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
      17. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
      18. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
      19. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
      20. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   F. Matendo ya mwili (angalia mifano)
      7. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
      8. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
      9. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
      10. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
      11. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
      12. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
   G. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
      5. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
      6. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
      7. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
      8. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
   H. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
      5. Baba
         d. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
         e. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
         f. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17

6. Mzazi – Hosea 11:1-4
7. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
8. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

V. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

E. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!

F. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)

G. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)

H. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

VI. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible,* ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika The International Standard Bible Encyclopaedia, kurasa za. 152-154

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9: 14- 18**
**14 Tuseme nini basi? Kuna udhalimu kwa Mungu? Hasha! 15 Maana amwambia Musa, Nitamrehemu yeye nimrehemuye, nitamhurumia yeye nimuhurumiaye. 16 Basi, kama ni hivyo, si katika uwezo wa yule atakaye, wala yule apigaye mbio; bali wa Yule arehemuye, yaani, Mungu. 17 Kwa maana maandiko yasema juu ya Farao, ya kwamba, Nilikusimamisha kwa kusudi hili, ili nionyeshe nguvu zangu kwako, jina langu likatangazwe katika nchi yote. 18 Basi, kama ni hivyo, atakaye kumrehemu humrehemu, na atakaye kumfanya mgumu humfanye mgumu.**

**9: 14 "Tunasema nini basi"** Paulo daima alitumia lugha hii ya kukemea (kama vile 3: 5; 4: 1; 6: 1; 7: 7; 8: 31; 9: 14, 19, 30)

◙ **"Kuna udhalimu kwa Mungu?"**Kwa mtizamo wa kisarufi, jibu la "hapana." Mungu atawajibishaje wanadamu kama ukuu wa Mungu ndicho kigezo cha uamuzi (kama vile mst. 19)? Hii ndiyo ajabu ya uchaguzi. Msisitizo mkubwa katika eneo hili ni kwamba Mungu yu huru kufanya chochote anacho hiari kwa wanadamu. (Wanadamu walioasi), hata hivyo ukuu wa Mungu unaelezwa katika hali ya uhuru na (Tazama nukuu katika mst. 15), siyo mamlaka. Lazima pia isemwe kuwa, uchaguzi wa msingi wa Mungu hauzingatii juu ya uelewa wa matendo yajayo ya wanadamu. Kama haya yalikuwa kweli basi maamuzi na matendo na ufanisi wa mtu vingekuwa ndiyo msingi wa uchaguzi wa Mungu (kama vile mst. 16; I Pet. 1: 2). Kufuatia hili kuna mtazamo wa asili wa Kiyahudi na ufanisi wa haki (kama vile Kumb. 27- 28; Ayubu na Zaburi. 73). Lakini, Mungu anachagua kuwabariki wasiostahili kupitia imani (sio Matendo kama vile 5: 8). Mungu anajua mambo yote lakini amechagua kupunguza uchaguzi wake. (1) Katika huruma na (2) katika ahadi. Kuna itikio la lazima la mwanadamu, lakini inafatia na hatimaye kuthibitisha uchaguzi thabiti wa Mungu wa kubadili maisha.

◙ **"Hasha "**Huu ni mara chache kuona MUUNDO WA KIUCHAGUZI aliotumia Paulo daima kwa msisitizo wa kukemea kwa kawaida maswali ya kipinzani (kama vile 3:4, 31; 6: 2, 15; 7: 7, 13; 11: 1, 11 pia 1 Kor. 6: 15; Gal. 2: 17; 3: 21; 6: 14). Bila shaka ni nahau ya Kiibrania.

**9: 15**Hii ni nukuu kutoka katika kitabu cha Kutoka. 33:19. Mungu yu huru kutenda kufuatana na kusudi lake la wokovu, hata Musa hakufanikisha baraka za Mungu (kama vile Kutoka 33:20). Aliuawa (kama vile Kut. 2: 11- 15). Cha msingi hapa ni kuwa na chaguzi zake uko katika huruma (kama vile mist.16, 18- 23; 11: 30,31, 32).

**9: 15-16 "huruma"** Neno hili la Kiyunani (*eleos,* kama vile mist. 15,16,18, 23;11: 30, 31, 32) linatumika katika maandiko ya kale (LXX) kutafasiri neno maalum la Kiibrania h*esed* (kumbuka waandishi wa Agano Jipya walikuwa waebrania wenye fikra kubwa walioandika kwa Kiyunani cha mitaani),kilichomaanisha "uaminifu thabiti wa patano." Huruma na uchaguzi wa Mungu upo katika wingi, shirikishi (Wayahudi [Isaka], sio Waarabu [Ismaili]; Israeli [Yakobo], siyo Edomu [Esau],bali wayahudi walioamini na watu wa mataifa walioamini, (kama vile mst. 24), kadhalika na watu binafsi.Ukweli huu, ni moja ya nia katika kufungua muujiza wa imani ya yale yaliyowekwa na Mungu kabla ndiyo yanayotendeka (ukombozi wa ulimwengu).Ufunguo mwingine katika mazingira ya sura 9-11 ni tabia ya Mungu isiyobadilika -huruma (kama vile 9: 15, 16, 18, 23; 11: 30; 30,31,32), na siyo matendo ya mwanadamu. Huruma kupitia katika uchaguzi hatimaye utawafikia wote wanaomwamini Kristo. Kile kinacho fungua mlango wa imani kwa wote (kama vile 5: 18- 19).

## MADA MAALUMU: WEMA/HURUMA (*hesed*)

Neno hili (BDB 338 I, KB 336 II) lina maeneo mapana ya maana.

A. Lilitumika katika kuwaunganisha wanadamu
   1. Wema kwa wenzetu (mf. 1 Sam. 20:14; 2 Sam. 16:17; 2 Nya. 24:22; Ayubu 6:14; Zab. 141:5; Mit. 19:22; 20:6)
   2. wema kwa maskini na wahitaji (mf. Mika 6:8)
   3. upendo wa Israeli kumuelekea HWH (kama vile. Yer. 2:2; Hos. 6:4,6)
   4. uzuri wa maua ya kondeni (kama vile. Isa. 40:6)

B. Lilitumika katika uungaishaji na Mungu
   1. uaminifu wa agano na upendo
      a. "ukombozi kutoka katika maadui na taabu" (mf. Mwa. 19:19; 39:21; Kut. 15:13; Zab. 31:16; 32:10; 33:18,22; 36:7,10; 42:8; 44:26; 66:20; 85:7; 90:14; 94:18; 107:8,15,21,31; 109:21-22; 143:8,12; Yer. 31:3; Ezr. 7:28; 9:9)
      b. "katika ulinzi wa maisha kutokka katika kifo" (mf. Ayubu 10:12; Zab. 6:4-5; 86:13)
      c. "katika wepesi wa maisha ya kiroho" (mf. Zab. 119:41,76,88,124,149,159)
      d. "katika ukombozi wa kutoka dhambini" (kama vile. Zab. 25:7; 51:1; 130:7-8)
      e. "katika kutunza maagano" (mf., Kum. 7:9,12; 2 Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4; Mik. 7:20)
   2. kuzielezea sifa za Mungu (mf. Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona 4:2; Mika 7:20)
   3. wema wa Mungu
      a. "utele" (mf. Hes.14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:5; 103:8; 145:8; Yoeli 2:13; Yer. 4:2)
      b. "ukuu katika kiwango chake" (mf. Kut. 20:6; Kum. 5:10; 7:9)
      c. "umilele" (mf. 1 Nya. 16:34,41; 2 Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136:1-26; 138:8; Yer. 33:11)
      d. nguvu zilizo sawa (mf. Zab. 59:17)
      e. ilihusiana na nguvu za Mungu (mf. Zab. 62:11c-12a)
   4. matendo ya wema (mf. 2 Nya. 6:42; Zab. 89:2; Isa. 55:3; 63:7; Omb. 3:22)

Neno hili linatafsiriwa kwa njia mbalimbali katika tafsiri za Kiingereza. Nafikiri maelezo bora yaliyo katiaka ufupisho yangelikuwa "hakuna kamba iliyounganisha utii wa agano la Kimungu" neno hili ni sambamba na neno la Agano Jipya "upendo" (agapaō). Munguni mwaminifu na mwenye upendo kwa sababu ya Yeye alivyo!!

**9: 17- 18** Mst 17 ni nukuu pana yenye nguvu kutoka katika kitabu cha Kutoka. 9:16; mst. 18 ni hitimisho lililochukuliwa kutoka katika nukuu. Farao inasemekana aliufanya moyo wake kuwa mgumu, katika Kutoka. 8: 15; 19:32; 9: 34. Mungu inasemekana alimfanya awe na moyo mgumu katika Kutoka. 4: 21; 7: 3; 9: 12; 10: 20, 27; 11:

10. Mfano huu unatumika kuonesha Ukuu wa Mungu (kama vile mst. 18), Farao anawajibika kwa uchaguzi wake. Mungu anatumia ukorofi, majivuno na tabia yake hiyo kukamilisha nia Yake kwa Waisraeli. (kama vile mst. 18).

Pia angalia kusudi la matendo ya Mungu kwa Farao yalilenga ukombozi uliokusudiwa; Yalikusudia.

1. Kuonyesha nguvu ya Mungu (dhidi ya asili ya Wamisri na miungu ya wanyama kama mwanzo 1 inavyofanya kwa miungu ya Babiloni)
2. Kumdhihirisha Mungu kwa Misri, na matokeo yake, dunia yote (kama vile mst. 17)

Mawazo ya Magharibi (Marekani) yanakuza mtu binafsi, lakini mawazo ya mashariki yanatazama mahitaji ya pamoja kwa wote. Mungu alimtumia Farao kujidhihirisha kwa ulimwengu wenye shida. Atafanya vivyo hivyo kwa Waisrael wasioamini (kama vile sura ya 11). Katika mazingira haya, haki ya mmoja, inaishia katika mahitaji ya wote. Kumbuka pia mifano jumuishi katika Agano la Kale kwa

1. Watoto asili wa Ayubu kufa kwa sababu ya mjadala wa Mungu na shetani (kama vile Ayubu 1-2).
2. Askari wa Israel kufa kwa sababu ya dhambi ya Akani (kama vile Yoshua 7).
3. Mtoto wa kwanza wa Daudi na Bathsheba kufa kwa sababu ya dhambi ya Daudi (kama vile 2 Sam 12:15).

Sote tumeathiriwa na chaguzi za wengine. Hali hii jumuishi inaweza kuonekana katika Agano Jipya, katika Rum 5:12-21.

◙ **"kwa vile maandiko yanasema"** hali ya kuyafanya maandiko kuwa kama mtu ni njia ya kuonyesha uhai na umuhimu wake (kama vile 10:6-8). Paulo anazifanya dhambi na kifo kama vile ni watu Rum 6-7)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9:19-26**
**[19]Basi, utaniambia, Mbona angali akilaumu? Kwa maana ni nani ashindanaye na kusudi lake? [20] La! Sivyo, Ee binadamu; wewe u nani umjibuye Mungu? Je! Kitu kilichoumbwa kimwambiye yeye aliyekiumba, Kwani kuniumba hivi? [21]Au mfinyazi je! Hana amri juu ya udongo, kwa fungu moja la udongo kuumba chombo kimoja kiwe cha heshima, na kimoja kiwe hakina heshima? [22]Ni nini basi, ikiwa Mungu kwa kutaka kuonyesha ghadhabu yake, na kuudhihirisha uweza wake, kwa uvumilivu mwingi alichukuliana na vile vyombo vya ghadhabu vilivyofanywa tayari kwa uharibifu; [23]tena, ili audhihirishe wingi wa utukufu wake katika vile vyombo vya rehema, alivyovitengeneza tangu zamani vipate utukufu; [24]ndio sisi aliotuita, si watu wa Wayahudi tu, ila na watu wa mataifa pia? [25]Ni kama vile alivyosema katika Hosea, Nitawaita watu wangu wale wasiokuwa watu wangu, na mpenzi wangu yeye asiyekuwa mpenzi wangu. [26]Tena itakuwa mahali pale walipoambiwa, Ninyi si watu wangu, Hapo wataitwa wana wa Mungu aliye hai.**

◙ **9:19 "Mbona angali akilaumu"**ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU, ambayo inasisitizia hoja iliyokamilishwa lakini yenye matokeo yanayoendelea (kama vile 2 Nyak. 20:6; Ayu 9:12; Zab 135:6; Kumb 4:35). Lugha ya kukemea inaendelea. Kimantiki, kufuatia lugha ya kukemea ya Paulo ndiyo njia bora ya kubaini na kuelewa wazo la Paulo. Tazama utangulizi wa sura B., 1. Matakwa ya Mungu yanahitaji kuonekana katika ngazi mbili. Ya kwanza ni mpango wake wa ukombozi kwa wanadamu wote walioanguka (kama vile Mwa. 3:15). Mipango hii haiathiriwi na uchaguzi binafsi wa mtu. Lakini katika ngazi ya pili, Mungu anachagua kutumia wanadamu kama vyombo (kama vile Kut. 3:7-9 na 10). Watu wanachaguliwa kukamilisha mipango yake (yote chanya, Musa, na hasi, Farao).

◙ **9:20-21** Hii hali ya kufikirika inatoka katika Isaya 29:16; 45:9-13; 64:8 na Yer. 18:1-12. Neno mbadala la YHWH kama mfinyanzi lilitumika daima kwa Mungu kama Muumba, kwa vile mwanadamu anatokana na udongo, (kama vile Mwa. 2:7). Paulo akapeleka hoja yake ya ukuu wa Muumba kwa njia ya maswali matatu zaidi-mawili ya kwanza katika mstari wa 20 na la tatu katika mstari wa 21. Swali la mwisho linarudi kwa ulinganifu wa uchaguzi chanya wa Mungu kwa Musa, na uchaguzi hasi kwa Farao. Tofauti hizi mbili zinaonekana katika

1. Isaka – Ishmaeli, mist. 8-9
2. Yakobo – Esau katika mist. 10-12
3. Taifa la Israeli na taifa la Edomu katika mst. 13.

Ulinganifu huu huu umeendelezwa kuonyesha hali ya wakati ule wa Paulo juu yaWayahudi wanao amini na wasio amini. Uchaguzi chanya wa Mungu hatimaye unaelezwa katika hitimisho la watu wa mataifa wanaoamini (mist. 24-29, 30-33)!
Mfano wa kisarufi unatarajia

1. jibu la "hapana" kila swali la mst. 20
2. jibu la "ndiyo" katika swali katika mst. 21

**9:22 "kama"**hii ni sehemu ya SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA inayodhaaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi, lakini bila hitimisho la kisarufi. Mistari ya 22-24 ni sentensi moja katika Kiyunani. Mstari 22, unaelezea tabia ya Mungu ya ukombozi. Mungu ni Mungu wa haki. Atawaajibisha wanadamu kwa matendo yao. Lakini pia ni Mungu wa huruma. Wanadamu wote wanastahili kifo (kama vile 1:18—3:21). Haki siyo habari njema! tabia ya Mungu kimsingi ni huruma, siyo hasira (kama vile Kumb. 5:9-10; 7:9; Hos. 11:8-9). Uchaguzi wake ni kwa ajili ya ukombozi (kama vile Eze. 36:22-33). Ni Mvumilivu kwa wanadamu watenda dhambi (kama vile Eze. 18). Wakati mwingine hutumia uovukwa kusudi lake la ukombozi (mfano, shetani, Farao, wachawi wa Endor, Ashuru, Nebukadneza, Koreshi, na katika sura ya 11, Israeli isioamini)!

◙
**NASB "tayari kuonyesha ghadhabu yake"**
**NKJV "akitaka kuonyesha ghadhabu yake"**
**NRSV "akitamani kuonyesha ghadhabu yake"**
**TEV "alitaka kuonyesha hasira yake"**
**NJB "yu tayari kuonyesha hasira yake"**

Mungu anaonyesha ghadhabu yake kutambulisha nguvu zake (kama vile mst. 22) na utajiri wa utukufu wake (kama vile mst. 23). Matendo ya Mungu siku zote yana makusudi ya ukombozi (isipokuwa *Gehenna*, ambayo ni hatua ya mwisho ya utenganisho wa kutoamini na dhambi).

◙ **"vyombo vya ghadhabu"** Neno hili linaendeleza maneno mbadala ya Paulo juu ya mwili wa mwanadamu kutoka mist. 20 na 21. Inaonyesha waziwazi juu ya wanadamu wasioamini ambao Mungu anawatumia kuendeleza mipango yake ya ukombozi.

◙
**NASB, NKJV "kuandaliwa"**
**NRSV "wametengenezwa"**
**TEV "wanakosa tumaini"**
**NJB "wamesanifiwa"**

Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA. Neno hili linatumika katika maandiko yaliyokuwa kwenye mafunjo (Moulton na Milligan) ya kitu kilichotayarishwa kwa kusudi kamili. Waasi wasioamini kutakuwepo na siku yao ya haki na matokeo yanayoambatana nayo. Hata hivyo, Mungu anachagua kutumia wasioamini ili kukamilisha kusudi lake pana la ukombozi. M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu ya 2 inasema "halikuunganishwa na Mungu kwa uharibifu, bali kwa maana ya KISIFA, *tayari, komaa*, kwa kuharibiwa, kutendewa, kukionyesha hali ya sasa iliyotayarishwa kabla, ila kwa kutoonyesha kidokezo chochote kuhusu namna kilivyotengenezwa (uk. 716).

◙ **"uharibifu"** Tazama Mada Maalum katika 3:3

**9:23 "kuufanya utajiri wa utukufu wake kujulikana katika vyombo vya huruma"** Fungu hili linaonyesha kusudi la Mungu la milele, (yaani huruma). KITENZI ni KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE UTEGEMEZI. Mungu alifanya utajiri Wake kujulikana katika kumtuma Yesu!

Paulo daima anamaanisha utajiri wa

1. Wema wake na uvumilivu na ustahimilivu, Rum. 2:4
2. Utukufu wake kwa vyombo vya huruma, Rum. 9:23
3. Neema Yake, Efe.1:7
4. Utukufu wa urithi Wake, Efe.1:18
5. Neema Yake katika wema kwetu katika Kristo, Efe. 2:7
6. Kristo kwa watu wa mataifa, Efe. 3:8
7. Utukufu Wake, Efe. 3:16
8. Utukufu wake wa muujiza huu miongoni mwa watu wa mataifa ambao ni Kristo ndani yako,matumaini ya utukufu, Kol. 1:27

◙ **"Alichoandaa kabla ya yote kwa ajili ya utukufu"** Ukweli huo huo umesemwa katika Rum. 8: 29- 30 na Efe. 1: 4, 11. Sura hii ndiyo inaeleza kwa uthabiti mkubwa juu ya Ukuu wa Mungu katika Agano Jipya. Hapataweza kuwa na ubishi kuwa Mungu ndiye mwenye dhamana yote ya uumbaji na ukombozi. Ukweli huu mkubwa usipunguzwe walakurahisishwa. Hata hivyo ni lazima uwekwe sawa na uchaguzi wa Mungu wa patano kama njia ya kuhusisha na uumbaji wa mwanadamu uliofanywa kwa mfano Wake. Ni kweli kabisa kuwa baadhi ya mapatano katika Agano la Kale kama vile Mwa..9: 8- 17 na 5:12- 21, hayana masharti na hayahusishwi kabisa na itikio la mwanadamu, lakini mapatano mengine yanayo masharti kwa itikio la mwanadamu (yaani; Edeni, Nuhu, Musa, Daudi). Mungu ana mpango wa ukombozi kwa uumbaji wake,hakuna mwanadamu atakaye athiri mpango huu.Mungu amechagua kuwaruhusu watu jinsi ya kushiriki katika mpango Wake.

Fursa hii ya ushiriki ni mvutano wa kithiolojia kati ya ukuu (Rum 9) na matakwa huru ya mwanadamu (Warumi. 10). Si sahihi kuchagua msisitizo mmoja wa kibiblia na kuacha mwingine. Kuna mvutano katika mafundisho kwa sababu watu wa mashariki wanatoa ukweli katika sera za rafudhi ya lugha yao au mvutano wa pande mbili. Mafundisho lazima yachukuliwe kwa uhusiano na mafundisho mengine. Ukweli ni muungano utokanao na ukweli zingine.

Kwa hakika kuna muujiza hapa!Paulo hakuonyesha mantiki katika hitimisho lake kuhusu waumini waliojiandaa (*kataptizō*) kwa ghadhabu (mst. 22)na waumini waliojiandaa (*proetoimazō*) kwa utukufu (mst. 23) je uchaguzi wa Mungu ndiyo kigezo pekee au ni uchaguzi wa Mungu uliozingatia huruma kwa wote, lakini wengine wanakataa zawadi Yake? Je hali ya uanadamu una nafasi yoyote katika maisha yao yajayo (kama vile 9:30-10:21)? Kuna kutia chumvi katika pande zote mbili (Augustine – Pelagius). Kwangu mimi, dhana ya patano inawaunganisha wote wawili na msisitizo juu ya Mungu. Ubinadamu, unaweza tu kuitikia maamuzi ya Mungu (mf.Yoh. 6:44, 65).

Lakini kwangu mimi tabia ya Mungu sio kwamba haibadili, bali ni wa huruma. Anaufikia uumbaji wake wote wenye utambuzi, ulio katika mfano wake (kama vile Mwa. 1:26, 27). Nashughulika na sehemu hii ya andiko. Ni nzito mno bali inaonyesha ukweli ulivyo. Mtazamo wake ni kutokuamini kwa Wayahudi, ambako kunapelekea kujumuisha watu wa mataifa. (sura ya 11)!Lakini siyo andiko pekee juu ya tabia ya Mungu!

◙**"utukufu"** Tazama nukuu maalum katika 3:23

**9:24** Mstari huu unaonyesha kuwa lengo la ahadi ya Mungu ni pana kuliko ya Israeli. Mungu ameonyesha huruma kwa wanadamu kutokana na uchaguzi Wake. Ahadi ya Mwanzo 3:15inahusika na wanadamu wote (kwa sababu hakuna Wayahudi hadi sura 12). Wito wa Abrahamu ulihusika na wanadamu wote Mwanzo 12:3, wito wa Israeli kama ufalme wamakuhani ulihusisha wanadamu wote (kama vile Kut. 19:5-6). Huu ni muujiza wa Mungu

uliofichwa, lakini sasa uko bayana (kama vile Efe 2:11-3:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11).Hoja ya Paulo katika mst. 24 utafafanuliwa na mfululizo wa nukuu za Agano la Kale (mist. 25-29)

1. mst. 25, Hosea 2:23
2. mst. 26, Hosea 1:10b
3. mst. 27, Isaya 10:22 na/ au Hosea 1:10a
4. mst. 28, Isaya 10:23
5. mst. 29, Isaya 1:9

**9:25-26** Katika eneo hili habari hii inatoka katika maandiko ya kale (ya tafasiri za kiyunani) ya Hosea 2:23 (na marekebisho machache) na 1:10, ambao unarejea makabila kumi ya kaskazini, lakini hapa Paulo anamaanisha watu wa mataifa. Huu ni mfano mzuri wa Agano Jipya kwa matumizi ya waandishi kwa Agano la Kale. Walioona kanisa kama ni ukamilisho wa ahadi ya Mungu kwa Waisraeli (kama vile 2 Kor.6:16; Tit. 2:14; 1 Pet. 2:5-9).Kwa eneo hili, habari katika Hosea inaonyesha Israeli isiyo na imani. Kama Mungu angerejesha yale Makabila Kumi ya Kaskazini yaabuduyo miungu, Paulo aliona hili kama ni ushahidi wa pendo na msamaha wa Mungu ambaye siku moja ungeweza hata kujumuisha hawa wapagani ( watu wa Mataifa).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9:27-29**
**27 Isaya naye atoa sauti yake juu ya Israeli, kusema, HESABU YA WANA WA ISRAELI IJAPOKUWA NI KAMA MCHANGA WA BAHARI, NI MABAKI YAO TU WATAKAOOKOLEWA. 28 KWA MAANA BWANA ATALITEKELEZA NENO LAKE JUU YA NCHI, AKILIMALIZA NA KULIKATA. 29 Tena kama Isaya alivyotangulia kunena, KAMA BWANA WA MAJESHI ASINGALITUACHIA UZAO, TUNGALIKUWA KAMA SODOMA, TUNGALIFANANISHWA NA GOMORA.**

**9:27**
**NASB,**
**NKJV,**
**NRSV, NJB "japo"**
**TEV "hata kama"**

Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA TATU (*ean* kikiongeza DHMIRA YA UTEGEMEZI), ambayo inaonyesha tendo lenye umuhimu.

**9:27-28** Hii ni nukuu dhaifu kutoka katika maandiko ya kale ya tafasiri ya Kiyunani katika Isaya 10:22-23. Andiko lililoongezwa fungu la kuhitimisha kutoka katika maandiko ya kale ya tafasiri za Kiyunani katika Isaya 10:23.Lakini haimo katika maandiko ya zamani ya Kiyunani $P^{46}$, א, A na B, inaonyesha kuwa nyongeza ya baadaye iliyofanywa na wachapishaji. $UBS^4$ inatoa alama kwa kuachwa kwake kama "hakika"

**9:27 "KAMA MCHANGA WA BAHARI"**Hii ni sehemu mbadala ya lugha isiyonyooka ya ahadi ya Mungu kwa Abrahamu (kama vile Mwa.15:5; 22:17; 26:4).

◙ **"NI MABAKI YAO TU YATAKAYOOKOLEWA"** Neno "masalia" linatumiwa mara kwa mara na Manabii wa Agano la Kale kumaanisha Waisraeli wale waliochukuliwa katika utumwa, lakini wangerejeshwa nyumbani katika nchi iliyoahidiwa na Mungu. Kwa matumizi ya Paulo ya neno hili inamaanisha wale wayahudi waliokuwa na uhusiano wa kiimani na Mungu na/ au wale waliosikia neno la Mungu na wakaitikia kwa imani katika Kristo.Hata hivyo ndani ya Israeli ya agano, utengano wa kiroho ulitokea, ni baadhi tu waliokuwa na haki na Mungu. Uchaguzi wa Israeli haukutenga hitaji la mwitikio wa imani ya mtu (kama vile Isa. 1:16-20).

Paulo anatumia fungu la Agano la Kale ambalo zamani lilimaanisha Waisraeli waliochukuliwa utumwani, wachache wao wakarudi Palestina, kumaanisha wale waliosikia injili (neno), lakini sehemu (idadi) kubwa hawakuamini na kumpokea Kristo. Ni asilimia ndogo tu ya waliosikia wa karne ya kwanza (Wayahudi na watu wa mataifa) waliokubali ujumbe wa injili. Paulo anawaita wale waliokubali kuwa ni "masalia."

## MADA MAALUM: MABAKI (BDB 984, KB 1375), NAMNA TATU

Dhana ya Agano la Kale ya kifungu cha "mabaki matakatifu" ni kigezo cha sasacha Manabii (hasa manabii wa karne ya nane na Yeremia). Neno hili linatumika katika maana tatu:

1. wale waliomudu kuishi ndani ya uhamisho (yaani Ezra 9:8,14-15; Neh. 1:2-3; Isa. 10:20-23; 17:4-6; 37:4,31-32; 46:3; Yer. 23:3; 31:7-8; 42:15,19; 44:12,14,28; Mika 2:12; 5:7-8; 7:18; Hag. 1:12-14; 2:2; Zak. 8:6,11-12)
2. wale waliobaki kuwa waaminifu kwa YHWH (yaani, Isa. 4:1-5; 11:11,16; 28:5; Yoeli 2:32; Amosi 5:14-15)
3. wale walio sehemu ya matengenezo mapya ya siku za mwisho na uumbaji mpya (yaani, Amosi 9:11-15; Zek. 8:6)

Ule mfano wa udongo katika Marko 4:1-20 na Mt. 13:1-23, ambao unanukuu Isa. 6:9-10, ni mfano mzuri wa namna Agano Jipya linavyolielewa neno hili (pia nukuu Rum. 9:6 katika kuirejelea Israeli ya siku za Paulo).
Haya "mabaki" ya Agano Jipya yameundwa na Wayahudi waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:27-29) na Mataifa waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:24-26). Makundi yote yanazungumziwa katika Rum. 9:30-35; 11:11-24,25-32. Kuamini juu ya Israeli si suala la rangi (yaani, Rum. 9:6; 2:18-19), bali kuliamini kundi la wafuasi waaminifu wa mambo mapya wa Mungu, ufunuo kamili katika Yesu. Kulizungumza hili kunaonekana kuwa ni kuyakataa maandiko ya Agano la Kale (yaani, Yer. 31:7-9; Mika 5:7-8) kuhusu taifa la Israeli kuwa mabaki. Tafadhari tazama katika Mada Maalumu yangu: Kwa nini Ahadi za Agano la Agano la Kale Zinaonekana kuwa Tofauti Sana na Ahadi za Agano Jipya? Injili hubadilisha kila kitu!

**9:28**
**NASB "akilimaliza na kulikata"**
**NKJV "maliza… fupisha"**
**NRSV "kwa haraka na kwa uamuzi"**
**TEV "kwa haraka na kutekeleza wajibu wake kikamilifu"**
**NJB "bila kusitasita au kuchelewa"**
**REB "itakuwa kwa ufupisho na mwisho"**
**NIV "kwa mwendokasi na umaliziaji"**
**NET "kwa kumalizia na kwa haraka"**

Maneno mawili ya Kiyunani yanahusisha neno cheza, (muungano wa maneno wenye *sun* ambao ni wa kawaida kwa Paulo).

1. *Suntelōn,* KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO *ya*
   a. *sun*
   b. *teleō*ambalo kimsingi linamaanisha"kukamilisha" au "kuimarishwa kabisa" (kama vile Marko 13:4; Lk. 4:2,13; Mdo. 21:27; Ebr. 8:8)
2. *suntemnōn* KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ya
   a. *sun*
   b. *temnō*

ambalo kimsingi linamaanisha "kupunguza" au "kutekeleza haraka" (linapatikana hapa tu lakini maana yake inapatikana na pia katika Mdo. 24:4). Pale amabapo michezo hiyo ya sauti inatumika, ni eneo husika tu, na siyo asili ya neno au usambamba ulio na msaada. Mungu ana kusudi na mpango wa wokovu kwa watu wake wa kweli

na hukumu Yake kwa wengine wote! Mstari huu ni mgumu kutafsiri kwa hiyo maelezo mengine kadhaa ya yanayofuatia yaliyojaribu kuongezea mafungu, kufafanua walichofikiria kilimaanisha. UBS[4] inatoa alama "A" (uhakika) kwa andiko hili fupi.

**9:29** Hii ni nukuu kutoka katika maandiko ya kale ya tafasiri za Kiyunani katika Isaya 1:9, ambayo inafuata hali ya dhambi ya taifa la Israeli.

◙ **"BWANA WA SABATO"** Hili lilikuwa jina la YHWH katika Agano la Kale, kwa kawaida lilitafsiriwa kama "Bwana Wa hifadhi" (kama vile Yakobo 5:4). Kutegemeana na eneo husika katika sura, inamaanisha Mungu katika mtazamo wa kijeshi "nahodha wa jeshi la mbinguni" (kama vile Yoshua 5:13-15) au, katika mtazamo wa kiutawala kwa kawaida katika imani ya Kibabeli kwamba kuna Mungu zaidi ya mmoja, wakihusisha miili ya mbinguni "Bwana wa miili ya mbinguni." Nyota ni jeshi la Bwana, haiwezi kudhibiti au kubadili matukio (kama vile Mwa. 1:16; Zab. 8:3; 147:4; Isa 40:26).

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El* (BDB 42, KB 48)
   1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra),akaitwa "baba wa miungu" na "bwana wa mbinguni"
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana BDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe" BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
      d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
      e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46
   4. *El* inalinganishwa na
      a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
      b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
      c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
      d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
      e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
      f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
      g. "maarifa" katika I Sam. 2:3
      h. "kimbilio langu" katika II Sam. 22:33
      i. "mlipa kisasi wangu" katika II Sam. 22:48
      j. "mtakatifu" katika Isa. 5:16
      k. "muweza" katika Isa. 10:21
      l. "wokovu wangu" katika Isa. 12:2
      m. "mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
      n. "anayepatiliza: katika Yer. 51:56
   5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)

1. Maana yake ya msingi ni "juu," "aliyetukuzwa," au "kuinuliwa" (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
   18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
   a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
   b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
   c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
   d. *El* - Hes. 24:16
   e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya "Mungu aliye Juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
   a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
   b. Balaamu, Hes. 24:15
   c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
   d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104).
   Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
   a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
   b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.
   c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)
1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
   a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
   b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).

Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.

2. Katika Mwanzo 4:26 inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
    a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
    b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
    c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
    d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
    e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
    f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
    g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
    h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
        (1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
        (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
        (3) *Yo* (majina mfano Joeli)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
    a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwanzo. 22:14
    b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Kutoka. 15:26
    c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651, Kutoka. 17:15
    d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA),Kut. 31:13
    e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
    f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
    g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu,BDB 217 & 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
    h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
    i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa,BDB 217 & 1027), Ezek. 48:35

**NASB "isipokuwa…kama atakuwa ametuachia vizazi vijavyo"**
**NKJV "isipokuwa… kama atakuwa ametuachia uzao"**

**NRSV "hakutuachia waliopona"**
**TEV "hakutuachia uzao kadhaa"**
**NJB "hakutuachia wachachewaliopona"**

Maandiko ya Kiebrania ya Isaya 1:9 yana "masalia" lakini maandiko ya kale ya tafasiri ya Kiyunani ilikalimani neno hilo kuwa "uzao" (NKJV). Hukumu ya Mungu kwa Waisraeli daima iliacha (1) masalia yalioamini au (2) uzao wa Masiha, Mungu aliacha wachache wawafikie wengi

◙ **"Sodoma….Gomora"** Mst. wa 28 unahusiana na hukumu ya Mungu. Mistari yake hasa inataja miji miwili ya wapagani, iliyoharibiwa na Mungu katika Mwanzo 19:24-26, lakini wakawa na mbinu katika hukumu ya Mungu (kama vile Kumb. 29:34; Isa 13:19; Yer. 20:16; 49:18; 50:40; Amo. 4:11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 9:30-33**
**30Tuseme nini, basi? Ya kwamba watu wa Mataifa, wasiofuata haki, walipata haki; lakini ni ile haki iliyo ya imani; 31bali Israeli wakiifuata sheria ya haki hawakuifikilia ile sheria. 32Kwa sababu gani? Kwa sababu hawakuifuata kwa njia ya imani, bali kana kwamba kwa njia ya matendo. Wakajikwaa juu ya lile jiwe likwazalo,33 kama ilivyoandikwa, Tazama, naweka katika Sayuni jiwe likwazalo, na mwamba uangushao; Na kila amwaminiye hatatahayarika.**

**9:30-31** Hili ni hitimisho la kushangaza la kusudi la uchaguzi wa Mungu, mistari ya 30-33 ni ufupisho wa sura ya 9 na utangulizi wa sura ya 10. Watu wa mataifa walioamini walifanywa kuwa na haki na Mungu, lakini siyo Wayahudi wote (kama vile mst. 6).

Mungu anashughulika na wanadamu wote kwa njia ya patano. Mungu daima anachukua hatua na kuweka masharti. Watu lazima wayakubali kwa toba na imani, utii na mapatano, ili kufanikisha wanadamu wote waliotumikia.

1. Kwa ukuu wa Mungu
2. Kwa huruma ya Mungu kupitia katika imani kwa kazi ya masiha iliyotimilika.
3. Kwa tendo la imani binafsi?

Kwa "jihihada" tazama nukuu katika sura ya 14:19

**9:30 "Haki"**Kwa kundi hili la maneno, tazama mada maalum katika 1:17 NOMINO imetumika mara tatu katika mst. 30na mara moja katika mst. 31. "haki" ya imani inatofautishwa na "haki"ya sheria. Tena tofauti kati ya agano la Kale na agano Jipya. Matatizo ya agano la Kale, yanafungua mlango wa injili kwa ulimwengu wote katika sura ya 11.

**9:32 "Kwa kazi"**andiko lililopokelewaliliongeza "kwa sheria"hii ilikuwa nyongeza ya baadaye iliyofanywa na mchapishaji. Paulo, mara nyingi alitumia fungu hilo "kazi za sheria" (kama vile 3:20,28; Gal 2:16;3:2,5,10). Hata hivyo, maandiko ya kale ya Wayunani $P^{46}$, $א^{*}$, A,B, F na G yanaacha neno hili katika mstari. $UBS^{4}$, inatoa alama B kwa andiko hili fupi (linakaribia "hakika").

Kielelezo kwa haki ya Mungu siyo utendaji wa mwanadamu bali, tabia na zawadi ya Mungu kupitia Kristo. Haki ni jambo lisilowezekana kutekelezeka kwa kwa wanadamu walioanguka, bali ni zawadi inayotolewa bure kupitia katika imani kwa Kristo (kama vile 3:21-31). Hata hivyo lazima ipokelwe (kama vile mst. 33, Yonaha 1:12; 3:16; Rum. 4:1ff; 10:9-13; Efe 2:8-9). Huu ni ukweli ambao Myahudi mwaminifu mwenye dini na mwadilifu (na watu wa sheria) anaukosa!

George Eldon Ladd katika kitabu chake *A Theology of the New Testament,*yaani (Thiolojia ya Agano Jipya) anaonyesha hoja ya msingi:

"Mafundisho ya Paulo kuhusu sheria daima yanafuatwa kutokana na mtazamo wa uzoefu wa kihistoria ama wa Paulo mwenyewe, kama mwalimu wa dini ya Wayahudi au hasa ya myahudi wa karne ya kwanza chini ya sheria.

Hata hivyo, wazo la Paulo lazima litazamwe kuwa sio ombi la msamaha wa historia binafsi ya kiroho ama maelezo ya tabia ya kisheria ya utawala wa Farao wa karne ya kwanza bali ni tafasiri ya kithiolojia iliyofanywa na mkristo wa fikra kubwa, mwenye haki za namna mbili "sheria na imani," (uk. 495).

**9:33** Hii imechukuliwa kutoka katika Isa. 28:16 ikiunganishwa na 8: 14.

"Tazama, naweka jiwe katika Sayuni," 28: 16a
"jiwe la kujikwaa na mwamba wa kujikwaa," 8:14b
"yeye aaminiye hatafanya haraka." 28:16b

Kwa kuiunganisha mistari hii kwa njia hii, (mbinu ya walimu wa sheria za Kiyahudi), anabadilisha maana ya Isa. 28:16 kutoka chanya kuwa hasi. Paulo anatumia mbinu katika Agano la Kale kwa makusudi yake.

1. Anachagua ni ukalimani upi (LXX, MT, au wa kwake pekee).
2. Anabadilisha rejea (kutoka watu waliochukuliwa utumwani, na watu wa mataifa).
3. Anaunganisha maandiko.
4. Anabadilisha nyadhifa na VIWAKILISHI, ambapo inaashiria YHWH kuwa Yesu

◙ **"Na kila amwaminiye hatatahayarika"** Hii ni kutoka kwa Isa. 28:16b. Pia imenukuliwa kutoka katika Warumi 10:11 na ni sawa na Yoeli. 2:32, imenukuliwa katika Warumi. 10:13. Kielelezo kwa wokovu ni (1) kitu (jiwe la pembeni) na (2) mapokeo ya mtu binafsi (imani katika Yeye).Tazama mada maalum Amini katika 4: 5.

◙ **"JIWE"** Hii awali ilikuwa jina la Mungu (kama vile 18: 1-2, 31, 46; Kumb. 32: 18; 1 Sam. 2: 2; Zab. 28: 1; 31: 3; 42: 9; 71: 3; 78: 35), badaye likawa jina la masiha (kama vile Mwa. 49: 24; Zab. 118: 22; Isa. 8: 14; 28: 16; Dan. 2: 34-35; 44- 45; Mt. 21: 42- 44). Kitu muhimu cha ahadi ya patano la Mungu (Masihi) hakikueleweka, kilikataliwa (kama vile 1 Kor. 1: 23).

Wayahudi hawakuelewa, sio tu kusudi la Masihi, bali hitaji muhimu la patano la Mungu. Kristo alikuja kwa Wayahudi akawa sababisho la kikwazo (kama vile Isa. 8:14; Lk. 2: 34) lakini kwa waumini, Wayahudi na watu wa mataifa akawa ndiye jiwe la msingi (kama vile Isa. 28:16; 1 Pet. 2: 6- 10).

## MADA MAALUM: "JIWE" (BDB 6, KB 7) na "JIWE KUU LA PEMBENI" (BDB 819, KB 944)

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
   B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
   C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
   D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
      1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwa linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa" jiwe kuu la pembeni"
      2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
      3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya

A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)
B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)
C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo
D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

III. Kauli za Kithiolojia

A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!
B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.
C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).
D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).
E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni vipi sura ya 9 (wazo la awali) inahusiana na sura ya 10 (utashi huru wa wanadamu)?
2. Ni Ipi dhima kuu katika sura ya 9:1-29?
3. Je, Mungu amevunja ahadi yake juu ya Israeli?
4. Orodhesha faida ambazo taifa la Israeli lilizifaidi (9:4-5)
5. Je, Wayahudi wote walikuwa sahihi na Mungu? Kwa nini ndiyo au hapana (9:6)?
6. Kama mtu atalazimika kutenda mapenzi ya Mungu, je kimaadili anawajibika?
7. Vipi “huruma” ni kielelezo kwa wazo lililotangulia la Mungu (kama vile 15, 16, 18, 23; 11:30-32)?

# WARUMI 10

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **USB[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Israeli Na injili | Israeli inahitaji injili | Haki ya kweli ni kwa njia ya imani | Israeli na injili | Israeli inashindwa kuona kuwa Mungu ndiye anayetufanya |
| watakatifu | | | | |
| 9:5-13 | | 9:30-10:4 | 9:30-10:4 | |
| | 10:1-13 | | | 10:1-4 |
| Wokovu kwa wote | | | Wokovu ni kwa Wote | Ushuhuda wa Musa |
| 10:5-13 | | 10:6-13 | 10:5-13 | 10:5-13 |
| | Israeli inakataa Injili | Israeli inawajibika kwa kushindwa kwake | | Israeli haina cha kujitetea |
| 10:14-21 | 10:14-21 | 10:14-17 | 10:14-17 | 10:14-15 |
| | | | | 10:16-17 |
| | | 10:18-21 | 10:18-21 | 10:18-21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura ya 10 inaangalia zaidi fursa ya mwitikio wa Israeli toka kwa YHWH kwa zawadi ya neema ya ukombozi katika Kristo. Sura ya 9 inajadili uchaguzi wa Mungu wa Wayahudi kwa lengo la kuchagua ulimwengu (kama vile Mwa.3:15; 12:3; Kut. 19:5-6), lakini Wayahudi walikataa kukumbatia chaguo lake (yaani utii wa patano, kama vile Kumb. 27-29).

B. Paulo anaendelea kutumia Agano la Kale kufanya shauri lake kwa ajili ya injili (tazama Uambuzi wa Kimuktadha E wa sura ya 9). Hii ndiyo sifa ya mahubiri ya kitume ya Matendo, ambayo yanajulikana kama *kerygma* (yaani, yale yaliyotangazwa). Tazama Mada Maalum: *Kerygma* katika 1:2.

C. Ukweli halisi wa 9:30-10:4 ni
   1. Watu wa Mataifa wana haki kwa Mungu kupitia imani katika Kristo
   2. Wayahudi hawana haki kwa Mungu kutokana na kukosa imani kwa Kristo
   3. Sheria haikuweza kutoa haki. Ilikuwa ni zawadi ya Mungu kupitia kwa Kristo, na isingelipatikana kwa juhudi za kibinadamu (kama vile 3:21-31)

D. Bruce Corley na Curtis Vaughan katika kitabu chao,*A study Guide Commentary, Romans*, kilichochapishwa na Zondervan, uk. 115-116, kina vidokezo vyenye msaada kuhusu dhambi za Wayahudi .
   1. majivuno ya kidini, 10:2a
   2. upofu wa kiroho, 10:2b, 3a
   3. haki binafsi 10:3b
   4. kiburi kisicho na manufaa 10:4a

   Napenda pia hitimisho la maoni yao mwisho wa sura za 9 kuhusu sura ya 10, "Uchaguzi unatokea katika kuhubiri msalaba (kama vile 1 The. 1:4-10), inaeleza jinsi kinga halisi ya ukuu wa Mungu (9:6-29) inaweza kufuatwa na habari kuu ya Kimisionari katika nyaraka za Paulo (10:1-21). Wajibu mkubwa wa kufundisha injili ni maarifa ambayo kwa kufanywa hivyo, Mungu ni mwaminifu akitekeleza kusudi lake la kuchagua kwa imani katika Kristo (uk. 114)

E. Kama ilivyo katika sura ya 9, sura 10 ina nukuu nyingi za Agano la Kale
   1. mst. 5 – Law. 18:5
   2. mst. 6 – Kumb. 30:12 na kugusiwa katika utangulizi wa Kumb. 9:4
   3. mst. 7 – Kumb. 30:13 na kugusiwa katika Zab. 107:26
   4. mst. 8 – Kumb. 30:14
   5. mst. 11– Isa. 28:16
   6. mst. 13 – Yoeli 2:32
   7. mst. 15 – Isa. 52:7 au Nahumu 1:15
   8. mst. 16 – Isa. 53:1
   9. mst. 18 – Zab. 19:4
   10. mst. 19 – Kumb. 32:21
   11. mst. 20 – Isa. 65:1
   12. mst. 21 – Isa. 65:2

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:1-4**
**[1]Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimuombayo Mungu ni kwa ajili yao, ili waokolewe. [2]Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. [3]Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu. [4]Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki.**

**10:1 "Ndugu zangu"** Neno hili daima lilitumiwa na Paulo katika utangulizi wa somo jipya (kama vile 1:13; 7:1,4; 8:12).

◙ **"nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimuombayo Mungu ni kwa ajili yao"** Paulo aliamini Wayahudi wangeweza kuokolewa, na kwamba ombi lake kwao lilikuwa jambo la pekee. Hapa ni mahali pa ajabu pa kukutania wazo la Mungu lililowekwa kwanza tangu awali. Tazama Mada Maalum: Maombi ya Utetezi katika 9:3. Kuna utofauti katika maandiko ya Kiyunani ya neno "kwa ajili yao" andiko lililopokelewa linaweka neno mbadala

"kwa ajili ya Waisreli." Hata hivyo, ushahidi wa maandiko unapendelea "kwa ajili yao." (MSS P[46],א*, B, C, D*, F, G). UBS[4] inatoa alama "A" (hakika) katika tathmini.

**10:2 "wana juhudi kwa ajili ya Mungu"** Uaminifu na shauku pekee havitoshi (kama vile mist. 3-4) Paulo alijua hili fika (kama vile Mdo. 9:1; Gal. 1:14; Flp. 3:6)!

**10:2-3 "lakini sio katika maarifa. Kwa maana wakiwa hawajui haki ya Mungu"** Neno "kujua" (mst. 2 *epinginōskō*) linaweza kufanya kazi mara mbili.

1. Wayahudi hawakujua injili ya bure (maana ya Kiyunani ya neno "kujua")
2. Wayahudi hawakuwa na ushirika wa imani pamoja na Mungu (maana ya Kiebrania "kujua" kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5)

Wayahudi hawakujuwa hitaji la uwajibikaji wao kwa Mungu (mistari ya 16,18,19), lakini walibadilisha utendaji kazi wa binadamu na imani, ambao uliwapelekea kuwa na kiburi, majivuno na kutojumuishwa kwao (mst. 3a)!

## MADA MAALUM: KUJUA (kama ilivyoelezewa toka Kumbukumbu la Torati kama)

Neno la Kiebrania "kujua"(BDB 393) lina maana kadhaa (mazingira ya kimaana) katika shina la neno *Qal*.

1. Kuelewa mema na mabaya - Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yohana 4:11
2. Kujua kwa kuelewa - Kumb. 9:2,3,6; 18:21
3. Kujua kupitia mazoea - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Yos. 23:14
4. kufikiri - Kumb. 4:39; 11:2; 29:16
5. kujua kibinafsi
   a. Mtu - Mwa. 29:5; Kut. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9, Yer. 1:5
   b. Mungu -Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
   c. YHWH - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
   d. kizinaa - Mwa. 4:1,17,25; 24:16; 38:26
6. ujuzi wa kujifunza - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. kuwa mwenye hekima - Kumb. 29:4; Mit. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. maarifa ya Mungu
   a. kwa Musa - Kumb. 34:10
   b. kwa Israeli- Kumb. 31:21

Kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya kibiblia ni ushirika wa ndani, wa kila siku, unaokua pamoja na Mungu (angalia Mada Maalum: *Koinōnia*). Sio sheria pekee au maisha ya kiadilifu pekee. Ni imani binafsi ya kiushirika. Hii ndio sababu Paulo alitumia nyumba ya mshirika katika Efe.5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa.

**10:3 "haki ya Mungu"** Katika maandiko sura ya 9-11 fungu hili lilimaanisha kweli ya Mungu iliyosimama (Rom 4) naye, kwa msingi wa

1. huruma Yake
2. kazi liyotimizwa na Kristo
3. kilio cha Roho Mtakatifu
4. kutubu kwa mwanadamu mwenye dhambi, mwitikio wa imani na kuendelea kutii na ustahimilivu.

Ni rahisi mtu kuelewa jinsi Wayahudi walivyoshindwa kuelewa haki ya Mungu. Agano la Kale lilisisitiza utii wa sheria (kama vile Kumb. 4:28-6:3,17,24-25). Walichoshindwa kuelewani uwiano wa toba na imani (kama vile Kumb.5:29-30; 6:5). Kumbukumbu la Torati linatetea waziwazi kuwa Mungu alitenda kwa niaba ya Israeli, siyo kwa haki waliokuwa nayo, bali kwa tabia yake Mungu (kama vile .9:6,7,13,24,27;10:12-22; Eze.36:22-38). Hata Wakanaani hawakunyang'anywa kwa ajili ya haki ya Israeli, lakini ni kutokana na dhambi yao (kama vile 9:4-6; Mwa.15:16). Tazama Mada Maalum katika 1:17.

◙ **"hawakujitia chini ya haki ya Mungu"** KITENZI hiki kinaashiria KAULI TENDEWA TIMILIFU ELEKEZI, lakini kinatafasiliwa kama IRABU YA TENDWA (kama vile TEV). Kazi ya IRABU YA KATI inachukuwa nafasi ya IRABU TENDEWA katika lugha ya koine ya Kiyunani. Mazingira ndiyo kigezo cha kuamua.

Kwa kifasihi, "salimisha" ambalo ni neno la kijeshi katika mlolongo wa amri. Wayahudi wanajaribu kupata haki ya Mungu, bali ilikuwa ni zawadi (kama vile 3:24; 5:15; 6-23; Efe. 2:8-9). Paulo aliona ukweli huo njiani akienda Dameski.

## MADA MAALUM: KUJITOA *(HUPOTASSŌ)*

Tafasiri hii ya mandiko ya kale yanatumia neno hili kwa maneno 10 tofauti ya Kiebrania. Maana yake halisi kufuatana na Agano la kale ilikuwa "kuamuru" " amri iliyo sawa" neno hili limechukuliwa kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya miaka ya 70.

1. Mungu anaamuru (kama vile Law. 10:1; Yn. 2:1; 4: 6-8)
2. Musa anaamuru (kama vile Kut. 36:6; Kumb. 27:1)
3. Amri za wafalme (kama vile 2 Nya. 31: 13)

Katika Agano jipya, maana hii inaendelea hadi katika Mdo. 10:48, ambapo Mtume anaamuru. Hata hivyo, mitazamo mipya imeibuka katika Agano Jipya.

1. Suala la hiari linaibuliwa (mara nyingi IRABU YA KATI)
2. Tendo la mtu pekee kujizuia linaweza kuonekana kwa Yesu kutii kwa Baba (Luk. 2: 51)
3. Waumini wanatii katika sura ya kijadi ili kwamba injili isiathiriwe sana.
   a. Waumini wengine (kama vile Efe.5:21)
   b. Wake za wanaoamini (kama vile Kol. 3:18; Efe. 5:22- 24; Tit.2:5; 1Petr.3:1.
   c. Waumini katika serikali za kipagani (kama vile Rum. 13:1-7; 1Pet. 2: 13).

Waumini wanatenda kutokana na msukumo wa upendo, kwa Mungu, kwa Kristo, na kwa Ufalme, kwa faida ya wengine. Kama *agapaō* (upendo), kanisaliliingiza neno hili kwa maana mpya iliyohusiana na mahitaji ya Ufalme na ya wengine. Neno hili tena linachukuliwa kama uzuri wa kutokuwa mbinafsi, usiohitaji amri, bali kwa ushirika mpya wa kujitoa kwa Mungu na Masihi Wake. Waumini wanatii na kukubali kwa manufaa ya wote na Baraka za familia ya Mungu.

**10: 4**
**NASB, NKJV,**
**NRSV "kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria"**
**TEV "kwa vile Kristo amesababisha mwisho wa sheria"**
**NJB "lakini sasa, sheria imefika mwisho kutokana na ujio wa Yesu"**

Usemi huu uko pamoja na Mt.5:17- 48. Kusudi, lengo au mwisho (*telos*) ya Sheria haukuwa wokovu, bali kutia hatiani na lengo hilo bado linaendelea (kama vile Gal.3: 24- 25). Andiko la Agano Jipya kuhusu somo hilini Gal.3:1-29 na kitabu cha Waebrania.

Wakati wa kujadili suala hili, mazingira yake ni nyeti. Paulo anatumia Agano la Kale katika njia kadhaa tofauti. Wakati tunajadili maisha ya Mkristo, Agano la Kale ni ufunuo wa Mungu (kama vile 15:4; 1 Kor 10:6,11), Lakini wakati wa kujadili wokovu, ni utupu na limeondolewa (kama vile Ebr. 8:13). Hii ndiyo maana, ni neno mbadala kwa enzi yakale. Injili ya imani katika Yesu ni enzi mpya ya Roho. Wakati wa sheria umekwisha! Tazama Mada Maalum: Maoni ya Paulo kwa Sheria ya Musa katika 13:9.

◙
**NASB, NKJV "ili kila anayeamini ahesabiwe haki"**
**NRSV "hivyo kwamba, patakuwa na haki kwa kila anayeamini"**
**TEV "hivyo kwamba kila aaminiye anajiweka sawa na Mungu"**
**NJB "hivyo kwamba, wote walio na imani watahesabiwa haki"**

Sura ya 9-11 ni lazima kutafsiriwa pamoja. Msisitizo juu ya ukuu wa Mungu unaelezwa kwa nguvu sana katika Sura ya 9 unapaswa kuchukuliwa kwa uangalifu mkubwa na wito kwa wote kuamini katika sura ya 10 (kama vile mist. 4,9,11, 13; 3:22; 4:11-16).

Ujumla wa pendo la Mungu na kusudi la ukombozi limeelezwa katika Mwa. 3:15 na kwa nguvu kabisa kuonekana katika Mwa. 12:3 na Kut. 19:5-6. Manabii wakati wote walizungumzia upendo wa Mungu kwa wote, na mpango wake wa kuwaunganisha wanadamu wote. Ukweli kwamba kuna Mungu mmoja tu na kuwa aliwaumba wanadamu wote kwa mfano wake inamfanya kuwaalika wote katika ukombozi huu. Ajabu ni kwamba, hakuna hata mmoja atakayekubali bila uwakala wa Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Ndipo swali linakuja, "je Mungu anawavuta wote katika wokovu?" Jibu linapaswa kuwa "ndiyo!" (kama vile Yn. 3:16; 4:42; 1 Yn. 2:2; 4:14; 1 Tim 2:4; 2 Pet 3:9).

Fumbo la kutisha la dhambi, kuanguka, na shetani ni kuwa baadhi wanasema "hapana." Paulo alipohubiri, Wayahudi wengine walikubali, wengine walikataa; wengine wa Mataifa walikubali, wenginewalikataa! Neno "amini" (*pisteuō*) limetafasiliwa katika maneno matatu ya Kiingereza "amini, imani, na tumaini."Ni NJEO YA WAKATI ULIOPO, unaozungumzia imani endelevu. Siyo tu kuthibitisha ukweli, (Thiolojia, maelezo ya kina ya historia, habari ya injili) ambavyo vinapokea kipawa cha neema ya Mungu kupitia kwa Kristo. Agano Jipya ni Patano; Mungu huweka hoja na kuandaa mapokeo ya lazima, lakini mtu sharti akubali katika imani ya awali na toba, na kuendelea katika imani na toba. Utii na mapambano ni masuala nyeti. Kumfanana Kristo na huduma ndiyo lengo!

## MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI VILIVYOTUMIKA)

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

**WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI TIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI TIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

**WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

**WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

**WOKOVU KAMA UKAMILISHO UJAO (WAKATI UJAO katika NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13
- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13),lakini hili <u>lazima</u> liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1 Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu.Hili linaweza kuelezwa kama

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:5-13**
**[5]Kwa maana Musa aliandika juu ya haki itokayo kwa sheria, ya kuwa, Mtu afanyaye hiyo ataishi kwa hiyo. [6]Bali ile haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi, Usiseme moyoni mwako, Ni nani atakayepanda kwenda mbinguni?' (yaani, ni kumleta Kristo chini), [7]au, Ni nani atakayeshuka kwenda kuzimu? (yaani, ni kumleta Kristo juu, kutoka kwa wafu.) [8]Lakini yanenaje, Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo. [9]Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. [10]Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. [11]Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatayaharika. [12]Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye Yule ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao; [13]kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.**

**10:5** Mstari huu ni kidokezo toka Walawi 18:5. Ahadi yake ni ya hakika. Kama mtu angetunza Sheria, angelikubalika kwa Mungu (kama vile Lk.10:28; Gal 3:12). Tatizo ni kuwa Rom.3:9,10-18,19,23; 5:18;11:32 inasema ukweli. Wote wametenda dhambi. Nafsi inayotenda dhambi itakufa (kama vile Mwa. 2:17; Kumb. 30:18; Eze. 18:4,20). Njia hii ya zamani ya patano imefungwa. Imekuwa ni hukumu ya kifo, laana, (kama vile 7:10; Gal 3:13; Kol. 2:14).

**10:6-8** Hili ni dokezo katika Kumb.30:11-14 katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ya miaka ya 70, ambalo Paulo alililirekebisha kwa malengo yake. Andiko hili awali lilisema na Musa akimaanisha Sheria (hasa katika mazingira yaliyolenga upendo na tohara ya moyo, kama vile Kumb.30:6,16,20), lakini hapa inamaanisha Yesu kuwa kama mwanadamu, kifo, na ufufuo (kama vile mst. 9; Efe. 4:9-10). Hoja ya Paulo ni kwamba, wokovu u tayari kwa Yesu, Masihi, kupitia katika imani, (kama vile Kumb.30:15-20). Ni urahisi, unapatikana, ni kwa wote, kitu ambacho kilikuwa tofauti kabisa na Sheria ya Musa.

**10:6"Bali ile haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi"** Paulo awali alijifanya kuwa "dhambi," "neema," na "Mafundisho" na sasa anajifanya kuwa "haki kwa imani." Inazungumza katika nukuu za Agano la Kale katika mist. 6,7 na 8.

◙ **"MOYO"** Moyo unasimama badala wa kioo cha nafsi. Tazama Mada Maalum katika 1:24.

◙ **"KUPAA…..KUSHUKA"** Wanadamu hawalazimiki kwenda kumtafuta Kristo; Mungu ametumia Kristo wazi kwa wote. Kutafutwa na wanadamu siyo lazima.

**10:8 "LILE NENO LI KARIBU NAWE"** Hii ni nukuu kutoka katika Kumb.30:14. Katika Kumb.30:11 ni msisitizo kuwa nia ya YHWH kwa watu Wake, Israeli ilikuwa inapatikana (kama vile mist. 12-13). Paulo anatumia aya (mist. 11-14) kusisitiza uwepo wa mara moja wa injili!

**10:9 "kama"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA TATU ikimaanisha tendo linalosubiria mbele.Mstariwa 9 ndiyo maudhui (*hoti*) ya ujumbe wa imani.

◙ **"ukimkiri"** Hili ni neno lililoungana *humologeō* hasa ni "kusema" na "lile lile" na lilimaanisha "kukubaliana na mtu waziwazi" (sema kwa sauti ili wengine wasikie). Uwazi wa weledi wa imani katika Kristo ni muhimu sana (kama vile Mt. 10:32; Lk.12:8; Yn.9:22; 12:42; 1 Tim 6:12; 1 Yn.2:23; 4:15). Weledi wa wazi katika kanisa la kwanza ilikuwa ubatizo. Mtarajiwa anatangaza imani yake kwa Kristo katika kanuni isemayo "namwamini Yesu ni Bwana." Tazama Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama Mada Maalumu: Toba

[Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kithiolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoeō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 and Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

◙

**NASB** **"Yesu ni Bwana"**
**NKJV** **"Bwana Yesu"**
**NRSV, TEV**
**NJB** **"Yesu ni Bwana**"

Haya yalikuwa maudhui ya kithiolojia ya fani ya imani na liturgia ya ubatizo wa kanisa la kwanza. Matumizi ya "Bwana "yanathibitisha uungu wa Yesu (kam vile Yoeli.2:32; Mdo 2:32-33,36; 10:36; 1 Kor 12:3; 2 Kor 4:5; Flp. 2:11; Kol. 2:6), wakati jina alilopewa "Yesu" linathibitisha uanadamu wake kihistoria (kama vile 1 Yn-.4:1-3). Uthibitisho pia unafanya kazi kama wito wa uanafunzi/kumfanana Kristo.Matumizi ya neno "Bwana" yalihusiana na mbadala wa viongozi wa dini wa YHWH na *Adon*wakati wa kusoma Maandiko. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 9:29. Hili inathibitishwa na nukuu kutoka Yoeli 2:32 ambayo iko katika mst 13.Yesu anapewa vyeo kadhaa vyenye nguvu

1. Yesu ni Masihi/Kristo – Mdo. 5:42; 9:22; 17:3; 18:5,28; 1 Kor 1:23
2. Yesu ni Mwana wa Mungu – Mt. 4:3, 6; Mdo. 9:20; 13:33; Rum. 1:4
3. Yesu ni Bwana – tazama juu

## MADA MAALUMU: JINA LA BWANA (AGANO JIPYA)

Hii ilikuwa aya ya kawaida kwenye Agano Jipya kwa ajili ya uwepo binafsi na nguvu ya tendaji ya nafsi tatu za Mungu kanisani. Haikuwa kanuni ya kichawi, bali kupeleka hitaji kwa tabia ya Mungu kama inavyoonekana

ndani ya Yesu. Mara nyingi aya hii humhusisha Yesu kama Bwana (kama vile Wafilipi 2:11)

1. Katika ukiri wa imani ya mtu kwa Yesu (kama vile Warumi 10:9-13; Mdo. 2:21, 30; 8:12 16:10, 48; 19:5; 22:16; 1 Wakorintho 1:13, 15, Yakobo 2:7)
2. Kwenye kukemea pepo (kama vile Mt. 7:22 Marko 9:38; Luka 9:49; 10:17 ; Mdo. 19:13
3. Kwenye uponyaji (kama vile Mdo. 3:6, 16:4 10:9 34; Yakobo 5:14)
4. Kwenye tendo la kufanya huduma (kama vile Mathayo 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. Kwenye wakati wa nidhamu kanisani (kama vile Mathayo 18:15-20)
6. Wakati wa kuwahubilia mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo. 9:15 15:17 Warumi 1:5)
7. Kwenye maombi (kama vile Yohana 14:13-14 15:7, 16, 16:23 1 Wakorintho 1:2)
8. Njia ya kuhusisha Ukristo (kama vile Matendo 26:9; 1 Wakorintho 1:10; 2 Tim 2:19, Yakobo 2:7; 1 Pet. 4:14)

Lolote tulifanyalo kama watangazaji, wachungaji au wahubiri watoa misaada, waponyaji watoa mapepo n.k tufanye katika tabia yake, uweza, utoaji wake kwa jina lake (yaani, Wafilipi 2:9-10)!

◙ **"kuamini moyoni mwako"** Fungu hili ni sambamba na kuungama, hivyo kuleta mitazamo pacha ya imani. Neno la kibiblia "kuamini"(*pistis*, tazama mada maalum katika 4:3 na 4:5) lilihusisha

1. Ukweli wa mtu binafsi (Waebrania)
2. Maudhui ya kisomi (Kiyunani)
3. Mwendelezo wa kujitoa kwa hiari (kama vile Kumb. 30: 20)

Neno "moyo" lilitumika katika Agano la Kale kwa maana ya mtu kamili. Paulo anataja "mdomo" na "moyo" katika andiko hili kwa sababu ya nukuu yake kutoka katika Kumb. 30:14 iliyonukuliwa katika mst.8. Hii haikumaanisha kuanzisha kanuni ngumu na ya haraka ambayo kwayo mtu lazima aombe kwa sauti kubwa/kupayuka ili aokolewe.

◙ **"kwamba Mungu Alimfufua toka katika wafu"**Ukristo unasimama au kuanguka kwenye ukweli wa kaburi tupu (kama vile 4:24; 8:11; 1 Kor. 15). Ni kweli thabiti katika mahubiri ya kitume (*kerygma*, Tazama mada maalum katika 1:2) ya matendo (yaani 2:31- 32; 3:15; 4:10; 5:30; 10: 40; 13:30, 37).
Kwa Baba kumfufua Mwana ni uthibitisho wa kupokea mausha nyan Yesu, mafundisho na sadaka kwake. Agano Jipya linatetea kuwa nafsi zote zaUtatu zilihusika katika ufufuo wa Yesu.

1. Baba Mdo. 2:24; 3: 15; 4: 10; 5: 30; 10: 40; 13: 30, 33, 34, 37; 17: 31; Rum. 6: 4,9; 8:11; 10: 9; 1 Kor. 6: 14; 2 Kor. 4: 14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The.1:10
2. Roho, Rum. 8: 11
3. Mwana- Yoh. 2: 19- 22; 10: 17- 18

**10:10 "hata kupata haki"** Lengo la Mungu kwa kila muumini sio tu mbinguni siku moja, balikumfanana Kristo sasa! Habari nyingine yenye uzito kuhusu neno la Mungu kuwepo kabla, katika Efe. 1:3- 14, kwa nguvu kabisa, linaunga mkono ukweli huo katika mst. 4. Waumini walichaguliwa kuwa watakatifu na wasio laumiwa! Uchaguzi sio tu mafundisho balini mtindo wa maisha (kama vile Kumb. 30:15- 20).

Mst wa 10 unaakisi namna mbili za msisitizo wa kujitolea sana (kama vile Mt. 28: 19- 20), Wokovu (kufanya wanafunzi) na haki (kuwafundisha yale yote niliyowamuru ninyi). Usawa huu unapatikana pia katika Efe. 2: 8- 9 (wokovu wa bure kwa neema ya Mungu kupitia katika Kristo) na wito kwa "kazi njema" katika Efe. 2:10, watu katika mfano wake siku zote imekuwa shauku ya Mungu.

**10: 11** Hii ni nukuu kutoka katika Isa. 28:16 ambayo kwayo Paulo aliongeza neno "yeyote Yule." Katika Isaya hii ilimaanisha imani katika Masihi, jiwe kuu la pembeni la Mungu (kama vile 9:32- 33).Kwa vile Warumi 9 inakuza ukuu wa Mungu, sura ya 10 inakuza mahitaji ya watu binafsi, yeyote na wote kumkubali Kristo. Zawadi ya wote inayoonekana wazi katika "kila mtu" katikamst wa 4 na "yeyote yule" katika mist ya 11, 13 na "wote" katika mst 12 (mara mbili)! Huu niuwiano wa kithiolojia kwa neno lililochaguliwa (kilichowekwa na Mungu kabla) na kusisitizwa katika sura ya 9.

◙ **"kila amwaminiye"** Ni kitendo TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIHUSISHI *epi* (kama vile 4:24; 9:33; 1 Tim.1:16).Kuamini sio tu ni mwitikio wa awali, bali mahitaji ya wokovu yanayoendelea! Sio tu ni thiolojia sahihi (ukweli wa injili) ambao unaokoa, bali uhusiano binafsi (injili ya mtu), inayotoa mtindo wa maisha wa kiungu (kuishi katika injili). Chukua tahadhari kwa kuamini kirahisi ambako kunatenganisha ukweli kutoka katika maisha, uhalalisho kutoka katika utakaso. Imani inayookoa ni imani inayodumu na kubadilisha! Maisha ya milele yana tabia zinazojionesha! (Tazama mada maalum, Kuamini katika 4: 5.

◙

**NASB, TEV "hatatahayarika"**
**NKJV, NRSV "hataaibishwa"**
**NJB "hatakuwa na sababu ya kuabika"**

Wale walio na imani ("wanaoamini") katika Kristo hawatatishika. Hii ni nukuu kutoka katika Isaya 28:16, ambao ulikuwa mst muhimu katika uwasilisho wa Paulo katika 9:33.

**10: 12 "Kwa maana hakuna tofati kati ya Myahudi na Myunani"** Hii ndiyo imani kubwa katika agano jipya (kam vile Rom. 3:22,29; Gal. 3:28; Efe. 2:11-3: 13; Kol. 3:11). Mungu mmoja alikomboa uumbaji wake uliopotea kupitia katika matendo yake. Anatamani wanadamu wote, walioumbwa kwa mfano wake waje kwake nakuwa kama yeye! Wote wanaweza kuja kwake!

Asili ya jumla ya injili ("wote" imetumika mara mbili katika mst. wa 12) iko katika sehemu mbili.

1. Hakuna tofauti kati ya Wayahudi na watu wa mataifa; wote wamepotea (kama vile 3: 9, 19, 22- 23; 11: 32)
2. Hakuna tofauti kati ya Wayahudi na watu wa mataifa, wote wanaweza kuokolewa.

Injili inaondoa mipaka yote ya kibinadamu (kama vile Yoeli. 2: 28- 29; 1 Kor. 12: 13; Gal. 3: 28; Kol. 3: 11), angalau katika eneo la wokovu.

◙ **"Kujawa katika utajiri"** Paulo anapowaza juu ya neema ya Mungu kwa Kristo, anatumia neno "utajiri" daima (kama vile 2: 4; 9:23; 11:12 [mara mbili], 33; 1 Kor.1:5; 2 Kor. 8:9; Efe.1: 7, 18; 2:7; 3:8, 16; Flp. 4:19; Kol. 1:27; 2: 2).

**10: 13** Hii nukuu maarufukutoka katika Yoeli. 2:32 ina msisitizo mpya waaina mbili katika matumizi ya Paulo.

1. Katika Yoeli,jina la YHWH lilitumika. Paulo katika Warumi na Petro katika Matendo. 2:21 walitumia jina mbadala la Yesu (pia angalia Yn. 12: 41 na Isa. 6: 9- 10; Flp. 2: 9 na Isa. 45: 22- 25; Rum. 9: 33 na Isa**.** 8:13- 14).
2. Katika Yoeli "kuokolewa" lilimaanisha kukombolewa kimwili toka katika tatizo, katika Warumi lilimaanisha kusamehewa kiroho na wokovu wa milele.

Dhana ya Agano la Kale ya "kuitwa jina" lilimaanisha kukiri imani wazi katika mkao wa ibada. Dhana hii inaonekana katika Mdo.7: 59; 9:14, 21; 22:16; 1 Kor. 1:2; 2 Tim. 2:22.Tazama mada maalum. Iliyoitiwa katika 1: 6.

**ANDIKO LA NASB ( LILILOBORESHWA) 10: 14- 15**
**[14]Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo muhubiri? [15]Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, "NI MIZURI KAMA NINI MIGUU YAO WAHUBIRIO HABARI YA MEMA"!**

**10: 14-15** Kuna mfululizo wa maswali yakifuatiwa na nukuu za Agano la Kale ambazo zinafanya hoja kuwa Israeli haijawahi kukubali/kuitikia ujumbe au wajumbe wa YHWH (kama vile Neh.9, Mdo. 7). Mungu anatuma wajumbe wake (manabii mitume, wahubiri, walimu, wainjilisti).Wajumbe hawa ni Baraka za Mungu kwa ulimwengu wenye shida. Kwa vile Mungu kwa neema anawatuma wajumbe wa injiliwasikilize yawapasa kuitikia kikamilifu ujumbe wake. Pauloaliweka pamoja wazo hili kwa nukuu toka katika Isa.52: 7. Paulo anapanua mst huu wa Agano la Kale kumaanisha wahubiri wa injili. Huduma ya imani, inamambo kadhaa yafuatayo: (1) ujumbe wa kuamini (2) mtu wa kupokelewa; (3) toba ya awali inayoendelea na kupokelewa kwa imani; (4) maisha ya utii na; (5) usitahimilivu (Tazama nukuu katika 1: 5).

**10: 15** Hii ni nukuu kutoka katika Isa.52:70. Ni majukumu makubwa ya Warumi.Wokovu unakuja kwa kusikia injili, na kupokea injili. Wahubiri wanatumwa ili "wote" wapate kuokolewa!

Baadhi ya maandiko ya kale ya Wayunani (yaani MSS $\aleph^2$, D, F, G, na machapisho mengi), yanaongeza fungu kutoka maandiko ya kale ya tafasiri ya Kiyunani ya Isa. 52:7. UBS[4] inatoa alama fupi "A" (hakika).

◙

**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB** **"Ni mizuri kama nini miguu yao"**
**TEV** **"Ni ujio wa ajabu kiasi gani"**
**NET** **"Ni uwasili mwafaka kiasi gani"**
**NET Tanbihi** **"kuja katika wakati sahihi au fursa sahihi"**

Neno "uzuri" limetumika kwa lugha mbadala. Hapa lina maana "wakati/muda" sio mwonekano.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10: 16- 17**
**[16]Lakini si wote walioitii ile habari njema, Kwa maana Isaya asema, Bwana, ni nani aliyeziamini habari zetu? [17]Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.**

**10:16** Tena Paulo anatumia maneno ya kinabii katika Agano la Kale, ambayo awali yalimaanisha ujumbe wa YHWH kwa Israeli, kumaanisha, injili ya Yesu Masihi. Kwa vile Wayahudi wa Agano la Kale walikataa ujumbe wa Mungu, kwa hivyo, Wayahudi wa siku za Paulo waliukataa pia. Hii imenukuliwa kutoka katika Isa. 53:1, lakini pia kithiolojia inahusishwa na Israeli kukataa ujumbe wa Mungu katika Isa. 6:9-13.

**10:17** Injili ni ujumbe wa mwanzo kabisa (kama vile Gal. 3:2). Lakini ujumbe uliotangazwa unakuwa neno binafsi, "Neno la Kristo lililopokelewa"(kama vile Kol. 3:15- 16).

◙ **"Neno la Kristo"** Kwa sababu ya muundo wenyewe, hii lazima inamaanisha ujumbe kuhusu Kristo uliyehubiriwa. Mahubiri ya injili ni njia ya Mungu kupeleka zawadi yake ya Kristo kwa ulimwengu. Kunautofauti katika maandiko ya kale ya Kiyunani katika hoja hii.

1. MSS $P^{46}$,$\aleph$*,B,C,D* yana "neno la Kristo"
2. MSS $\aleph^C$, A, $D^C$, K, P yana "neno la Mungu"

La kwanza si la kawaida sana (kama vile Kol. 3:16) na kwahiyo bila shaka ni asili (hii ni moja wapo ya neno muhimu katika ukosoaji wa kimaandishi). UBS[4] inatoa alama ya "A" (hakika).Hapa ndipo pia eneo pekee linajitokeza katika Agano Jipya. La pili, "neno la Mungu," linajitokeza mara kadhaa (kama vile Lk. 3:2; Yoh. 3:34; Efe. 6: 17; Ebr. 6: 5 na 11: 3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10: 18- 21**
**[18]Lakini nasema, Je! Wao hawakusikia? Naam, wamesikia, Sauti yao imeenea duniani mwote, Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu. [19]Lakini nasema, Je! Waisraeli hawakufahamu? Kwanza Musa anena, Nitawatia wivu kwa watu ambao si taifa, Kwa taifa lisilo nafahamu nitawaghadhabisha. [20]Na Isaya anao ujasiri mwingi, asema, Nalipatikana nao wasionitafuta. Nalidhihirika kwao wasioniulizia. [21]Lakini kwa Israeli asema, Mchana kutwa naliwanyooshea mikono watu wasiotii na ukaidi.**

**10:18** Mstari huu unasisitiza kuwa, Wayahudi wengi walikuwa wamesikia ujumbe na kwamba walipaswa kuwajibika kwa kuukataa (msisitizo wa UKANUSHAJI HASI MARA MBILI wa msemo wa Kiyunani, swali linatarajia jibu "hapana").Tatizo halikuwa ujinga bali, kutoamini kwa kukusudia!

Paulo ananukuu Zab. 19:4. Katika Zaburi hii mistari ya 1- 6 inamaanisha ufunuo wa asili, ambao Mungu anazungumza kupitia katika uumbaji (kama vile Rum. 1:2). Paulo anabadilisha

1. Ushahidi wa wote ("katika dunia yote" na"miisho ya ulimwengu").

2. Njia ya kupitisha ujumbe kutoka katika sauti ya utulivu ya muumbaji hadi kwa wahubiri wa injili (manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu kama vile Efe. 4:11), ambayo inamaanisha ufunuo maalum (kama vile Zab. 19: 8-14)

Wazo kuu ni kwamba ujumbe wa injili umekwenda na kuufikia ulimwengu uliojulikana nyakati za Paulo (Warumi wenye asili ya Kiyunani). Paulo anatumia kauli za viongozi wa dini, naanabadilisha muundo waasili wa Agano la Kale kwa makusudi yake ya kithiolojia, au ubishi. Lazima pia ielezwe wazi kuwa, matumizi ya Paulo ya Agano la Kale kama mitume wengine yalikuwa ya kipekee yakiongozwa na Roho Mtakatifu (kama vile 2 Pet. 1: 20 – 21). Waumini wa leo, chini ya mwangaza wa Roho, hawawezi kuzalisha, njia ya tafsiri za waandishi wa Agano Jipya.

## MADA MAALUMU: NURU

Mungu ametenda hapo mwanzo ilikujidhihirisha wazi kwa wanadamu. Kithiolojia, huu unaitwa ufunuo. Alichagua watu kadhaa kuweka kumbukumbu na kueleza ufunuo wake huu. Katika thiolojia, huu unaitwa uvuvio. Ametuma Roho kusaidia wasomaji kuelewa neno lake. Katika thiolojia, huu unaitwa mwangaza.Tatizo linatokea pale tunapobisha kuwa Roho anahusika katika kuelewa neno la Mungu- Sasa, kwa nini panakuwa na tafsiri nyingine kiasi hicho? Sehemu ya tatizo ipo kwa uelewa wa nyuma wa wasomaji au uzoefu binafsi. Daima hoja binafsi inaelezwa kwa kutumia Biblia katika uthibitisho wa kimaandishi au mtindo wa kuhakiki. Daima thiolojia inachagua maneno ya kusoma BibliaI ikiruhusu kusoma maneno kadha na kwa njia zilizopendekezwa. Mwangaza hauwezi kulinganishwa na uvuvio ingawa sehemu zote mbili Roho mtakatifu anahusika.

Njia rahisi ya kusoma ni kujaribu kufafanua wazo kuu katika aya, na siyo kutafsiri kila neno kwa kina katika maandiko. Ni wazo la juu tu ambalo linapeleka ukweli hasili wa mwandishi wa kwanza. Kudokezea kitabu au sehemu ya kifasihi inasaidia kufuatilia kusudio la mwandishi wa awali aliyevuviwa. Hakuna mfasili aliyevuviwa.

Hatuwezi kuzalisha njia ya tafasiri ya mwandishi wa Kibiblia. Tunaweza na lazima tujaribu kuelewa walichokuwa wakisema enzi za nyakati zao na kuwakilisha ukweli huo nyakati zetu.Kuna sehemu za Biblia ambazo ni tata au zimefichika (hadi wakati/kipindi kingine). Daima patakuwapo kutokukubaliana katika baadhi ya maandiko na masomo lakini lazima tuseme wazi kweli halisi na kuruhusu uhuru wa tafsiri binafsi ndani ya mipaka ya kusudio la mwandishi wa mwanzo. Wafasiri lazima watembee ndani ya mwanga walio nao, na siku zote wakiwa tayari kwa mwanga zaidi kutoka katika Biblia na Roho. Mungu atatuhukumu kutokana na kiwango cha uelewa wetu na jinsi tulivyoishi katika uelewa huu.

**10: 19- 20** Wayahudi walikuwa tayari na ujumbe (mist.18na 19 ambayo ni maswali yanayotarajia jibu “hapana”), hata kutoka kwa Musa.Wayahudi walisikia na walikuwa na uwezo wa kuelewa ujumbe jumuhishi wa imani ya kwamba, watu wote wana haki na Mungu. Katika mistari hii, Mungu alizungumza na watu wake wa agano kuhusu kuwajumuisha watu wa mataifa.Hii inafanyika kwa njia ya nukuu kutoka Kumb.32: 21 katika mst. wa 19 na Isa. 65: 1- 2 Katika mist ya 20- 21.Ujumbe huu wa kushtua wa kujumuisha watu wa mataifa, ulikuwa na lengo la kuamsha (kwa njia ya wivu), Wayahudi katika imani (kama vile 11: 11, 14).

**10: 21** Usemi huu ni nukuu kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani katika Isa. 65: 2 kuhusu watu wa patano kukataa YHWH (kama vile Isa. 65: 1- 7). Mungu amekuwa mwaminifu; Israeli imekuwa hainauaminifu. Kutokuwa kwao na uaminifu kulipelekea hukumu ya muda kwa taifa kadhalika na watu binafsi kwa siku za nyuma, lakini kukataa kwao haki ya Mungu kupitia katika imani kwa Kristo kutasababisha hukumu ya milele!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Mst. 4 una maana gani? Je, “Kristo ameondoa sheria?”
2. Orodhesha mambo yanayohusika katika imani katika 10: 9- 10.
3. Kwa nini Paulo daima ananukuu kutoka katika Agano la Kale? Kimsingi hii linahusishaje kanisa la Rumi la watu wa mataifa?
4. Ni kwa namnagani mist ya 11- 13 inahusiana na sura ya 9?
5. Ni kwa vipi mist ya 14- 15 inahusika na umisionari wa ulimwengu?
6. Ni vipi hiari ya mtu inaoneshwa kuwa sehemu ya wokovu wa mtu katika sura ya 10?

# WARUMI 11

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS$^4$** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Masalia ya Israeli | Kukataliwa kwa Israeli si kwa wote | Kukataliwa kwa Israeli siyo mwisho | Huruma ya Mungu kwa Israeli | Masalia ya Israel |
| 11:1-10 | 11:1-10 | 11:1-10 | 11:1-6 | 11:1-6 |
| | | | 11:7-10 | 11:7-10 |
| Wokovu wa watu wa Mtaifa | Kukataliwa kwa Israeli siyo mwisho | | | Wayahudi kurejeshwa siku za mbeleni |
| 11:11-12 | 11:11-36 | 11:11-12 | 11:11-12 | 11:11-12 |
| | | | Wokovu wa watu wa Mataifa | |
| 11: 13- 16 | | 11: 13- 16 | 11: 13- 15 | 11: 13- 15 |
| | | | | Wayahudi bado ni wabarikiwa |
| | | sitiari ya mti wa mzaituni | 11: 16- 18 | 11: 16- 24 |
| 11:17-24 | | 11:17-24 | | |
| | | | 11:19-24 | |
| Kurejeshwa kwa Israel | | Waisrael wote wataokolewa | Huruma ya Mungu kwa wote | Kubadilishwa kwa Wayahudi |
| 11: 25- 32 | | 11: 25- 32 | 11: 25- 32 | 11: 25-29 |
| | | | | 11: 30 – 32 |
| | | | Sifa kwa Bwana | Utenzi kwa huruma yake Mungu na hekima |
| 11: 33 – 36 | | 11: 33- 36 | 11: 33- 36 | 11: 33- 36 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.

Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

A. Sura ya 11 inaendeleza uhusiano wa fumbo kati ya uchaguzi na injili. Uchaguzi wa Agano la Kale ulikuwa kwa huduma, wakati uchaguzi wa Agano Jipya ni kwa ajili ya wokovu (chunguza uhusiano wake!). Kimantiki, waumini wanaitwa wote familia ya Mungu (Agano Jipya) na watumishi (Agano la Kale). Uchaguzi ni wa yote mawili, ushiriki au ubinafsi, chanya au hasi (Yakobo/Israeli- Esau/Edomu; Musa/Farao). Hatimaye, mvutano sio tu kati ya ukuu wa Mungu na utashi huru wa mwanadamu,bali ni tabia kamilifu ya Mungu. Sura ya 9- 11 inasisitiza tena na tena huruma ya Mungu na uasi wa mwanadamu aliyeanguka. Mungu ni mwaminifu, mwanadamu sio mwaminifu.

   Uchaguzi sio mafundisho ya kubagua baadhi ya wengine, bali ni msingi wa matumaini, usalama, na kujiamini ni kwa wale walio itikia (1) ahadi na (2) Mwana wa Mungu mpatanishi wa agano.

B. Katika sura ya 9, Paulo alitetea ukuu na uhuru wa Mungu. Hata katika mahusiano ya agano, Mungu yu huru. Katika sura ya 10 Paulo anaeleza kuwa Wayahudi walikuwa huru kupokea au kukataa ahadi za Mungu na maagano. Kwa kuwa walithibitisha kutokuwa waaminifu na wakazikataa ahadi za Mungu na agano, kwa maana moja walikataliwa na Mungu.Hata hivyo katika sura ya 11, Paulo atathibitisha uaminifu wa Mungu hata mbele ya uso wa Waisrael waliokosa imani (kama vile Kumb. 8).

C. Enzi za kale, kama ilivyo sasa, Salia la Uyahudi liliamini na kutekeleza imani katika Masihi wa Mungu. Paulo binafsi alikuwa mfano wa hili. Kukataa kwa baadhi ya Wayahudi wasio amini, iliruhusu kujumuishwa kwa watu wa Mataifa wanaoamini. Kujumuishwa kwa watu wa Mataifa kutaleta matokeo ya (1) watu kamili wa Mungu au (2) namba kamili ya watu waliochaguliwa na Mungu Wayahudi na watu wa Mataifa.Huku kujumuisha watu wa Mataifa, kutahamasisha Israeli kumwamini Yesu Masihi wa Mungu.

D. Kama ilivyo sura ya 9 na 10, Paulo anatumia nukuu kadhaa za Agano la Kale katika sura ya 11
   1. mst. 3- 1 Fal. 19: 14
   2. mst. 4 - 1Fal. 19: 18
   3. mst. 8 - Isa. 29:10 na Kumb. 29: 4
   4. mst. 9- Zab. 69: 22
   5. mst. 10 - Zab.69: 23
   6. mst. 26- Isa.59: 20- 21
   7. mst. 27- Isa. 27: 9
   8. mst. 34- Isa. 40: 13- 14
   9. mst 35- Ayubu. 35: 7; 41: 11

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11: 1-6**
**1 Basi, nauliza, je! Mungu aliwasukumia mbali watu wake? Hasha! Kwa kuwa mimi nami ni Mwisraeli, mmoja**
**wa wazao wa Ibrahimu, mtu wa kabila ya Benyamini. 2 Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua**
**tokea awali. Au hamjui yale yaliyonenwa na maandiko juu ya elia? jinsi anavyowashitaki waisraeli mbele za**
**mungu, 3 bwana, wamewaua manabii wako, wamezibomoa madhabahu zako, nami nimesalia peke yangu, nao**
**wanitafuta roho yangu. 4 Lakini ile jawabu ya Mungu yamwambiaje? NIMEJISAZIA WATU ELFU saba wasiopiga**

**goti mbele ya baali. [5]Basi ni vivi hivi wakati huu wa sasa, yako mabaki waliochaguliwa kwa neema. [6]Lakini ikiwa ni kwa neema, haiwi kwa matendo tena, au hapo neema isingekuwa neema.**

**11: 1 "je! Mungu aliwasukumia mbali watu wake" S**wali hili linategemea jibu la "hapana."Paulo anajibu swali hili katika mist 1b- 10. Sehemu hii lazima ihusiane na hoja iliyopita ya Paulo. Sura ya 9-11 inaunda kipengele cha kifasihi, hoja inayoendelea.
Neno lililo kalimaniwa "kukataa" ni (KITENZI CHA KATI CHA WAKATI USIO TIMILIFU [chenye ushahidi] KINACHOONYESHA) kimsingi inamaanisha "kukataa" au "kutupilia mbali".kimetumika katika

1. Mdo. 7: 39- Israeli nyikani kukataa uongozi wa Musa.
2. Mdo. 13: 46-Wayahudi wa masinagogi katika pisidia ya Antiokia kukataa mahubiri ya Paulo ya injili.
3. 1 Tim. 1: 19- Baadhi ya waumini wa kanisa katika Efeso kukataa na kuacha imani yao ( yaani Himenayo na Iskanda).

YHWH hakuitupa Israeli! Ni Israeli ndio ilimtupilia mbali, kwa kuendelea na kutotii kwao, kuabudu sanamu na sasa kujihalalishia haki kisheria.
Inapendeza kuona kuwa maandiko ya awali ya Kiyunani ya kwenye mafunjo $P^{46}$na machapisho ya F na G yana urithi mbadala ya "watu" ambayo yanaweza kuwa yametoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya miaka ya 70 Zab. 94:14. $UBS^4$ inatoa alama ya "A" (yenye hakika) kwa watu.

◙ **"Hasha"**Hii ni namna ya tabia ya Paulo ya kukataa maswali ya hisia za anayepinga (lugha ya shutuma kama vile 3: 4, 6, 31; 6: 2, 15; 7: 7, 13; 9: 14; 11: 1, 11).

◙ **"mimi name ni mwisraeli"** Paulo anatumia nafsi yake mwenyewe kuthibitisha uwepo wa salia la myahudi anayeamini. Kwa kuona matokeo ya historia ya Wayahudi wa Paulo. Tazama Flp. 3: 5.

◙ **"Mungu hajawasukumia mbali watu wake"** Hili linaweza kuwa ni usemi uliojitokeza katika Zab. 94: 14 (kama vile Kumb. 31: 6; 1 Sam. 12: 22; 1 Flp. 6: 13; Omb. 3: 31- 32). Ni jibu maalum kwa swali la mst. 1.

◙ **"Aliowajua tokea awali"** Hii ni wazi inamaanisha uchaguzi wa Mungu wa Israeli. Tazama nukuu katika 8: 29. Inairejesha hoja hii kwenye sura ya 9, kama ilivyo katika mist. ya 4-6. Kiini hakikuwa utendaji wa kazi nzuri wa Israeli, bali uchaguzi wa Mungu. Mungu ni mwaminifu kwa ahadi zake kwa sababu ya jinsi alivyo, na sio kwa utendaji wa Israeli (kama vile Eze. 36: 22- 32).

◙ **"Maandiko ya Mungu yanasema"** Hii ni rejea kwa maelezo kuhusu safari ya Eliya kutoka Beersheba katika 1Fal. 19: 10, iliyonukuliwa katika mst wa 3.

**11: 4 "NIMEJISAZIA kwa ajili yangu WATU ELFU SABA" "**kwa ajili yangu" haiko katika maandiko ya kale ya Kiebrania kwenye 1Fal. 19: 18 (Paulo hajanukuu toka katika tafasiri za maandiko ya kale ya Kiyunani ya 70), lakini inaongezwa na Paulo kusisitiza chaguo la Mungu. Salia ambalo ni aminifu la 1 Fal. 19: 18 linatazamwa kutoka katika chaguo la Mungu, na siyo kukataa kwao kwa ibada ya Baali.
Hoja anayoitengeneza Paulo ni kuwa, palikuwa na kundi dogo la waumini hata katika hali ya kutokuwa na imani, na kuabudu miungu kwa Israeli katika siku za Eliya. Katika siku za Paulo, palikuwa pia na salia lililoamini la watu wa Uyahudi (Tazama Mada Maalumu katika 9: 27- 28). Katika kila enzi, Wayahudi wamepokea kwa imani. Paulo anatetea kuwa Wayahudi hawa walioamini wanapata nguvu kwa huruma na neema ya Mungu (mist 5-6).

◙ **"Kwa Baali"** Hiki ni KIBAINISHI JINSIA YA KIKE chenye NOMINO YA JINSIA YA KIUME. Hii ilikuwa ni kwa sababu Wayahudi mara kwa mara waliweka silabi kutoka kwa neno ya jinsia ya kike ya Waebrania "aibu" (*bosheth*) katika konsonanti za majina ya miungu ya wapagani kuonesha kama kituko, kitu cha kufurahisha.

**11: 5- 6** Hii ni mist ya msingi. Inaunganisha matendo ya nyuma ya Mungu katika Agano la Kale na mazingira/hali za sasa. Kiungo ndiyo uchaguzi wa Mungu kwa huruma (kama vile 9:15,16,18; 11:30,31,32). Neema ya Mungu ni kipaumbele, lakini imani ya mwanadamu ni lazima (kama vile Marko. 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21), hata hivyo, haitegemei kabisa utendaji bora wa mwanadamu (kama vile Efe. 2:8-9; 2Tim.1:9; Tito 3:5). Ukweli huu ni muhimu katika utetezi wa Paulo katika sura yote ya 9- 11.

**11: 6 "Kama"** HiI ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi lake la kifasihi. Wokovu ni kwa neema ya Mungu (Tazama nukuu 3:24; kama vile 6:23; Efe. 2:8-9).

KJV inaongeza fungu la kuhitimisha katika mst. 6, "lakini kama itakuwa ni kazi, bali si tena neema, vinginevyo, kazi si kazi tena." Fungu hili halimo katika maandiko mengine ya kale ya wayunani $P^{46}$,$\aleph^*$, A, C, D, G au P na machapisho ya zamani ya kilatini, lakini mafungu mawili ya maandiko yanaonekana katika $\aleph^c$ na B.$UBS^4$ inatoa alama ya "A" (yenye uhakika) kwa kuacha fungu hilo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11: 7-10**
**[7]Imekuwaje basi? Kitu kile ambacho Israeli alikuwa akikitafuta hakukipata; lakini wale waliochaguliwa walikipata; na wengine walitiwa uzito. [8]Kama ilivyoandikwa, Mungu aliwapa roho ya usingizi, macho hata wasione, na masikio hata wasisikie, hata siku hii ya leo. [9]Na Daudi alisema, meza yao na iwe tanzi na mtego, Na kitu cha kuwakwaza, na malipo kwao; [10]Macho yao yatiwe giza ili wasione, Ukawainamishe mgongo wao siku zote.**

**11: 7 "Israeli inachokitafuta, haijakipata"**Hii inachukuwa nafasi ya kwanza katika sentensi ya kiyunani kusisitiza wazo la Paulo. Wayahudi wengi walikuwa wakitafuta kuwa na haki na Mungu, na walifanya hili katika utendaji wa mitambiko ya kidini, maslahi ya kitaifa, na juhudi binafsi. Walikosa lengo lao! Hakuna mwili utakaotukuka mbele ya Mungu (kama vile 1 Kor. 1: 29; Efe. 2: 9).

◙
**NASB "lakini wale waliochaguliwa, waliipata"**
**NKJV "lakini waliochaguliwa wameipata"**
**NRSV "waliochaguliwa waliipata"**
**TEV "lilikuwa kundi dogo tu, ambalo Mungu alilichagua naliliipata"**
**NJB "lakini ni wale wachache tu waliochaguliwa"**

Hii ndiyo dhana ya Agano la Kale ya"masalia" (Tazama Mada Maalum katika 9: 27- 28) hapa akimaanisha 7,000 katika 1 Fal. 19: 18. Kiini hapa sio juhudi ya Binadamu, taifa au udini (mst. 6), bali neema ya Mungu katika uchaguzi (Efe. 1: 3- 14).

◙**"Waliobaki walitiwa uzito"** Inamaanisha kuwa Mungu aliwapumbaza (kama vile 8- 10). Wakala wa kuwapumbaza alikuwa shetani "kupumbazwa" huku (*pōroō*), ni neno la kitabibu kwa maana ya upofu (kama vile Rum. 11:25; 2 Kor. 3:14; Efe. 4:18). Neno hili hili linatumiwa kwa mitume katika Marko 6: 52. Ni neno tofauti na lile la Kiyunani kutoka 9:18 (*sklērunō*) ambalo ni kinyume cha huruma (kama vile Ebr. 3: 8, 15; 4: 7).

Mstari huu uko wazi kabisa, ni ufupisho wa 11:1-6. Baadhi ya waliyochaguliwa waliamini, baadhi ya wale wasiochaguliwa wakafanywa mioyo yao kuwa migumu. Hata hivyo mstari huu haukuandikwa kutenganishwa kama nahau ya kithiolojia. Ilikuwa ni sehemu ya hoja ya kithiolojia isiyobadilika.Kuna mvutano kati ya ukweli ulioelezwa wazi kabisa katika mstari huu na mwaliko wa wote, katika sura ya 10 Kuna muujiza hapa lakini jibu sio kukanusha au kupunguza ncha za kikwazo au ncha za muujiza.

**11:8-10** Mistari hii ni nukuu kutoka katika Isa. 29: 10 (mst wa 8a), kumb. 29: 4 (mst. 8b, lakini sio kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani) na Zabu. 69: 22-23 (mst. 9- 10). Ni hakika vinaakisi wito na ujumbe wa Isaya kwa Israeli iliyoasi katika 6: 9- 13. Isaya angeweza kutoa neno la Mungu, lakini watu wa Mungu wasingeweza kulipokea. Paulo anatoa uthibitisho katika Agano la Kale wa msimamo wa Mungu kama alivyofanya katika 9:13,15, 17.

**11: 8**
**NASB, NKJV "Mungu aliwapa roho ya usingizi"**
**NRSV, NJB "Mungu aliwapa roho wa unyonge"**
**TEV "Mungu alifanya fikra zao na mioyo yao kuwa ya kuzubaa"**

Neno hili la Kiyunani (*katanuxis*), lililotumika hapa tu katika Agano Jipya, linatumika kama kun'gatwa na mdudu hali inayosababisha kuzubaa kwa fahamu kwa kuingiza msisimko mkubwa.

**11:10 "MACHO YAO YATIWE GIZA ILI WASIONE"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISH YA WAKATI USIO TIMILIFU ikifuatiwa na KAULI TENDAJI USHURUTISHI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Huu ni muujiza wa ukuu wa Mungu na umuhimu wa mwanadamu kujongea. Mungu ndio chanzo cha kila kitu, mwanzilishi wa vitu vyote, na bado kwa hiari ya ukuu wake alitamka kwa wanadamu huyo, uumbaji wake, waukubali bila masharti. Wale wasioweza kumpokea kwa imani, watafanywa kuwa na mioyo migumu (yaani chaguo lao, limehitimishwa), katika kuamini kwao. Katika mazingira haya, Paulo anatetea hoja yake ya mpango wa milele wa Mungu wa kuwakomboa watoto wote wa Adam. Wayahudi wasioamini watafungua mlango wa imani kwa watu wa mataifa na kupitia katika wivu watarudisha Taifa la Israeli! Ni mpango jumuishi (kama vile 2:11-3:13) na siyo wa utenganishi! Kufanywa mioyo yao kuwa migumu kunaokoa mavuno makubwa (mfano Farao).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11:11-16**
**[11]Basi nasema, je! Wamejikwaa hata waanguke kabisa? Hasha! Lakini kwa kosa lao wokovu umewafikia mataifa, ili wao wenyewe watiwe wivu. [12]Basi ikiwa kosa lao limekuwa utajiri wa ulimwengu, na upungufu wao umekuwa utajiri wa mataifa, je! Si zaidi sana utimilifu wao?[13] Lakini nasema na ninyi, mlio watu wa mataifa. Basi, kwa kadri nilivyo mtume wa watu wa mataifa, naitukuza huduma iliyo yangu, [14]nipate kuwatia wivu walio damu moja na mimi na kuwaokoa baadhi yao. [15]Maana ikiwa kutupwa kwao kumeleta upanisho kwa ulimwengu, je! Kukubaliwa kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa? [16]Tena malimbuko yakiwa matakatifu, kadhalika na donge lote, na shina likiwa takatifu, matawi nayo kadhalika.**

**11:11 "Basi nasema"** Hili ni fungu lilelile lisilo hitaji jibu kama katika 11: 1. Linaendeleza hoja ya kithiolojia ya Paulo katika njia nyingine tofauti. Katika mist. 1-10 siyo Israeli yote imekataliwa na Mungu; katika mst. 11- 24 kukataliwa kwa Israeli siyo kwa kudumu; kuna makusudi yake. Ingawaje watu wa Mataifa wamejumuishwa.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"hawakujikwaa ili waanguke, ndiyo"** |
| **NKJV, NRSV** | **"walijikwaa ili waanguke"** |
| **TEV** | **"wayahudi walipojikwaa, walianguka katika uharibifu wao"** |
| **NJB** | **"wayahudi wameanguka milele, au wamejikwaa** |

Swali hili linategemea jibu la "Hapana"kutokuamini kwa Waisraeli sio hali ya kudumu.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa ajili ya makosa yao"** |
| **NJKV** | **"kupitia anguka lao"** |
| **NRSV** | **"kupitia kujikwaa kwao"** |
| **TEV** | **"kwa sababu walitenda dhambi"** |
| **NJB** | **"Anguko lao"** |

Katika mazingira haya, hii inamaanisha Wayahudi kukataa Yesu kama Masihi (kama vile mst. 12)

◙ **"Wokovu umekuja kwa watu wa Mataifa"** Ni usemi uliokuwa wa kushitua kiasi gani kwa Wayahudi wa Karne ya kwanza? (kama vile mst. 12; Mdo. 13:46; 18:6; 22:21; 28: 28.

◙ **"kuwafanya wawe na wivu"** Neno "wivu" linatokea katika 10:19 na 11:14. Mpango wa Mungu wa kujumuisha watu wa Mataifa ulikuwa na makusudi mawili.

1. Ukombozi wa Mungu wa watu wote**.**
2. Mpango wa Mungu wa kurejesha mabaki ya Waisrael waliotubu katika imani binafsi.

Binafsi nashangaa kama #2 unahusu

1. Uamusho wa Wayahudi muda wa mwisho (kama vile Zek. 12: 10)

2. Waumini wa kiyahudi wa karne ya kwanza na kila karne
3. Masinagogi ya kisasa ya Masihi yangeweza kuwa ni ahadi ya utimilifu.

**11: 12-14** Mistari hii ilikuwa katika mifuatano wa SENTENSI kumi SHURUTISHI ambazo zinahusiana na kutokuamini kwa Wayahudi dhidi ya imani ya watu wa Mataifa. Mist. ya 12,14,15,16,17,18,21,24 ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ambazo zinachukuliwa kuwa zakweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa lengo lake kifasihi, wakati mist. ya 22 na 23 ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA TATU ambazo zinaonyesha uwepo wa tendo linalo subiria wakati ujao.

**11: 12**
**NASB** **"Ni kiasi gani zaidi, utimilifu wao utakuwa"**
**NJKV** **"Ni kwa kiasi gani zaidi wingi wao"**
**NRSV** **"Ni kwa kiasi gani zaidi, kujumuishwa kwa kutamaanisha"**
**TEV** **"Ni ukubwa kiasi gani Baraka zao zitakuwa wakati idadi kamili ya wayahudi wote inajumuishwa"**
**NJB** **"Kisha fikiri nikwa kiasi gani zaidi itanufaika kutokana na kubadilishwa kwao wote"**

Dhumuni katika utafsiri ni maana ya neno "kwa ujazo wao." Je linahusiana na
1. Kuokolewa kwa wayahudi, mist. 14b, 26a, au (2) idadi ya mwisho ya waliochaguliwa ya Wayahudi na watu wa Mataifa wanaoamini

**11:13 "nasema na ninyi mlio watu wa Mataifa"** Sura 9-11inaundwa na sehemu ya fasihi ambayo ilijibu swali, "kwa nini Masihi wa wayahudi amekataliwa na wayahudi?" Hata hivyo swali linabaki kuwa, kwa nini Paulo alisikia uhitaji katika waraka huu, kwa wakati huu katika kuwakilisha kwake, ashughulikie swali hili?

Mistari ya 13- 24, 25c inaonekana kutafakari tatizo katika kanisa huko Rumi kati ya wayahudi wabaguzi na watu wa Mataifa. Hata kama ingekuwa kati ya watu wa Mataifa wanaoamini na wayahudi wanaoamini au watu wa Mataifa wanaoamini na Wayahudi wasioamini (masinagogi) kuna mashaka.

◙ **"Mimi ni mtume wa watu wa Mataifa"** Paulo alijisikia mtu wa pekee kuitwa mhudumu wa watu wa Mataifa (kama vile Mdo. 9: 15; 22: 21; 26: 17; Rum. 1:5; 15: 16; Gal. 1: 16; 2: 7,9; 1 Tim. 2: 7; 2Tim. 4: 17).

◙
**NASB, NKJV** **"Ninakuza huduma yangu"**
**NRSV** **"Ninaitukuza huduma yangu"**
**TEV** **"Nitajivunia kazi yangu"**
**NJB** **"Na ninajivunia kutumwa"**

Neno "kukuza" laweweza kumaanisha (1) shukrani (2) majivuno katika (3) kufanya jambo kubwa. Hii pia inaweza kuakisi tatizo kubwa ndani ya kanisa la Rumi! Paulo (1) anafurahia kuhudumia watu wa Mataifa (2)aliona kuwa huduma yake iliwafanya Wayahudi wasioamini kuwa na wivu,ambapo ingepelekea kuwapa wokovu (kama vile mist 11,14,na 9: 1- 3).

**11: 14 "kuwaokoa baadhi yao"** Huu ni wito wa kiinjili wa Paulo. Alijua baadhi wataitikia mahubiri ya injili (kama vile 1 Kor. 1: 21), na wengine hawataitikia (kama vile 1 Kor. 9:22). Huu ni muujiza wa uchaguzi (Agano la Kale na Agano Jipya).

**11:15** Kukataa (neno tofauti mbali na mst 1) kwa Israeli iliyochaguliwa katika Agano la Kale, ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa ukombozi wa wanadamu wote (*kosmos*). Haki binafsi ya Wayahudi, majigambo ya Taifa, hali za sheria, wazi wazi ilizidisha hali ya kuhitaji imani (kama vile 9: 30- 33). Imani katika YHWH na Masihi Wake ni kielelezo cha msimamo sahihi, na sio utendaji wa kidini wa mwanadamu. Lakini kumbuka, kukataa kwa Israeli kulikuwa na kusudio la ukombozi wa wanadamu wote. Hakuna nafasi kwa majivuno ya mwanadamu awe myahudi au mtu wa Mataifa. Huu kwa ujumla ni ujumbe ambao kanisa la Warumi lilihitaji kuusikia!

◙ **"Upatanisho wa ulimwengu wote"** Hii kithiolojia ni sambamba na "Hakika ya Mungu." Muungano wa neno unatokana na *kata* pamoja na *alassō* (kubadili, kutamka au kubadilisha). Inamaanisha kubadilishana kati ya uhasama na amani, hivyo kurejesha upendeleo (kama vile Rum.5:11; 11:15; 2 Kor.5:18,19). Mungu anatafuta kurejesha ushirika wa Edeni. Dhambi ilivunja ushirika huo. Lakini Kristo amerejesha mfano wa Mungu kwa wanadamu walioanguka kwa ajili ya wote wanaotekeleza imani. Wamepatanishwa na kupokelewa (usambamba wa mst 15).Mwanadamu hangeweza kurejesha uhusiano huu bali Mungu anaweza na alifanya.

◙ **"Lakini si uhai baada ya kufa"** Mazingira yanaashiria taifa la Israeli, kwa hivyo.

1. Je, fungu hili linamaanisha kurudishwa kwa taifa la Israeli.
2. Je, fungu hili linamaanisha "jumla/idadi yote" ya wayahudi na watu wa Mataifa (yaani, Israeli ya kiroho, kama vile 9:6; 11:25-26)
3. Je, fungu hili linamaanisha (kama vile 6:13) enzi mpya, maisha ya ufufuo?

Naipenda #3. Kwa sababu zangu tazama "Utangulizi muhimu wa makala," kuhusu maoni yangu juu ya ufunuo, katika www.freebiblecommentary.org.

**11: 16 "tena malimbuko yakiwa matakatifu"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtIzamo wa mwandishi au kusudio lake la kifasihi. Ni neno lililokwisha semwa katika Ebr. 15: 17- 21. Ni neno mbadala ambalo ni sawa na dhana ya Agano la Kale ya matunda ya kwanza (fungu la kumi) ambayo alikuwa anapewa Mungu kuonyesha kuwa mavuno yote yalikuwa mali yake.

Waumini wa zamani wa masalia ya kiyahudi bado walikuwa na athari kwa taifa zima (kama vile Mwa. 18: 27- 33; 2 Nya 7: 14). Neno mbadala kwa neno "sehemu ya kwanza" ni sambamba na neno "chanzo" (kama vile Yer.16-17), yote yakimaanisha Yule mwaminifu wa Israeli, hasa wazee walio heshimika (mfano "chanzo" kwenye mistari ya 16-17) ya Agano la Kale (kama vile mst. 28).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11: 17- 24**

**17 Lakini iwapo matawi mengine yamekatwa, na wewe mzeituni mwitu ulipandikizwa kati yao, ukawa mshirika wa shina la mzeituni na unono wake, 18 usijisifu juu ya matawi yale; au ikiwa wajisifu, si wewe ulichukuaye shina, bali ni shina *likuchukualo* wewe. 19 Basi utasema, Matawi yale yalikatwa kusudi ili nipandikizwe mimi. 20 Vema. Yalikatwa kwa kutokuamini kwao; na wewe wasimama kwa imani yako. Usijivune, bali uogope. 21 Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaachia matawi ya asili, wala hatakuachia wewe. 22 Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukukaa katika wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali. 23 Na hao pia, wasipokaa katika kutokuamini kwao, watapandikizwa; kwa kuwa Mungu aweza kuwapandikiza tena. 24 Kwa maana ikiwa wewe ulikatwa ukatolewa katika mzeituni, ulio mzeituni mwitu kwa asili yake, kisha ukapandikizwa, kinyume cha asili, katika mzeituni ulio mwema; si zaidi sana wale walio wa asili kuweza kupandikizwa katika mzeituni wao wenyewe.**

**11: 17- 24** Kwa mshangao "wewe" katika aya hii iko katika UMOJA (HALI YA UWINGI unatokea katika mst 25). Hii ina maana gani?

1. Mtu wa mataifa mmoja kama alama ya watu wa mataifa wote.
2. Tatizo katika kanisa la Roma kati ya uongozi wa wayahudi na ule wa watu wa mataifa, hivyo basi, ikimaanisha viongozi katika uongozi wa sasa wa watu wa mataifa (kama vile mist. 18 – 20).

**11: 17 "kama"** Tazama nukuu katika 11: 12- 24

◙ **"Matawi yalikatwa"** Hii ilimaanisha Waisraeli wasioamini (kama vile mst 18, 19 "matawi asilia" mst 21).

◙ **"Mzeituni pori"**Hii ilimaanisha watu wa Mataifa walioamini wanaokubali mahubiri ya injili

◙ **"Kupandikizwa"** Paulo anaendeleza neno la taaluma ya kilimo lilioanza katika mstari wa 16. Kupandikizwa kwa matawi ya mzeituni pori katika mzeituni wa asili kulisaidia kuboresha mavuno (kama vile mst. 24).

◙ **"Mzizi ulionona"** Msemo asilia wa neno "asili ya unene" (UBS[4] inatoa alama "B" [karibia sawa]), unapatikana katika MSS א*, B,C. Kuna maarifa mengine mengi katika maandiko ya utamaduni wa kiyunani ambayo yanajaribu kunyoosha maana hii. (Bruce Matziger*A*, *Textual Commentary on the Greek New Testament*,uk. 526).

◙**"Mti wa mzeituni"** Hii ni alama ya Taifa la Israeli (kama vile mst.24; Zab. 52:8; 128:3; Yer. 11:16; Hos. 14:6). Hili ni neno la pili mbadala la Paulo katika Agano la Kale linaloelezea uhusiano kati ya Wayahudi na watu wa Mataifa.

**11: 18 "Usijisifu juu ya matawi yale"** Hii ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, yenye KIAMBATA HASI ambacho kwa kawaida kinamaanisha kuzuia kitendo kilicho tayari katika mchakato. Mstari huu ukiunganisha na mist 13,20,25 inaonyesha kuwa, palikuwepo na tatizo katika kanisa la Roma kati ya Wayahudi wanaoamini na watu wa Mataifa.

**11: 19 – 20** Mstari wa 19 ni maneno mengine ya kukemea (anayedhaniwa kuwa mpinzani). Paulo anaelezea kwa nini Wayahudi walikataliwa, ilikuwa ni kwa sababu ya kutoamini kwao, na siyo kwamba watu wa Mataifa walikuwa wanapendwa zaidi! Watu wa Mataifa walijumuishwa tu kwa sababu ya upendo wa Mungu (kama vile Mwa. 3: 15) na imani yao! Wangeweza pia kusababisha wayahudi kurudi kwa Mungu kwa ajili ya wivu (kama vile mst 11, 14).

**11: 20**
**NASB "Lakini unasimama kwa imani yako"**
**NKJV "Na unasimama kwa imani"**
**NRSV "Lakini unasimama tu kwa kupitia katika imani"**
**TEV "Wakati unabaki pale ulipo kwa vile unaamini"**
**NJB "Kama bado uko imara, ni shukrani tu kwa imani yako"**

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Hata hivyo, imo katika muktadha wa SENTENSI ZENYE MASHARTI. Kusimama kwetu mbele ya Mungu ni kwa imani na kutaendelea kuwa kwa imani. Kama imani yetu itakwisha, kusimama kwetu nako kutakwisha. Wokovu ni: (1) mwitikio wa awali wa imani (2) hali ya kuwa katika imani (3) ni mchakato endelevu wa imani (4) hatimaye hitimisho la wokovu. Uwe mwangalifu kwa tabia ya thiolojia inayoangalia moja ya kweli hizi za biblia (Tazama mada maalum vitenzi vya nyakati vya kiyunani vilivyo tumika kwa wokovu katika 10: 4. Mungu ndiye mwandishi, mwanzilishi, mdumishaji, na mhitimishaji wa wokovu, lakini katika mtindo wa agano. Amechaguwa kuwa mwanadamu mwenye dhambi lazima akubali na aendelee kukubali kwa njia ya toba, na imani katika kila hatua ya mchakato. Anategemea utii, kufanana na kristo, na usitahimilivu!

◙
**NASB "Usiwe mjivuni bali uwe na hofu"**
**NKJV "Usijikweze bali kuwa na hofu"**
**NRSV "Kwa hiyo usiwe wa kujivuna, bali simama kwa heshima"**
**TEV "Lakini usiwena majivuno kwa kitu bali uwe na hofu"**
**NJB "Kuliko kukufanya kuwa na majivuno, heri kukufanya kuwa na uoga"**

Kauli zote hizi ni ZENYE MASHARTI ZA WAKATI ULIOPO, ya kwanza ina KIAMBATA HASI ambacho kwa kawaida, kinamaanisha kusimamisha kitendo ambacho kipo katika mchakato. Kinadhihirisha tatizo katika kanisa la Rumi. Sababu ya kuogopa imeelezwa katika mst. wa 21.

**11: 21 "Wala hatakuachia wewe"** Kama Israeli ilivyoasi na kwenda mbali usoni pa YHWH kwa majivuno ya kutoamini na kuachwa, vivyo ndivyo kanisa litaachwa kama litaacha imani katika Kristo kwa majivuno ya haki binafsi. lmani ya kwanza sharti ifuatwe na imani ya mtindo wa maisha (kama vile Mt. 13:1-23; Marko. 4:1-12; Lk. 8:4-10). Majivuno lazima yaendelee kupingwa, tuko kama tulivyo kwa neema ya Mungu na tu ndugu na wengine wote ambao pia wanamwamini Kristo.

## MADA MAALUMU: UKANAJI WA IMANI (*APHISTĒMI*)

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" and *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kithiolojia):

1. kuondoa kimwili
   a. kutoka Hekaluni, Luka 2:37
   b. kutoka katika nyumba, Marko 13:34
   c. kutoka kwa mtu, Marko12:12; 14:50; Matendo 5:38
   d. kutoka katika vitu vyote, Mt. 19:27,29
2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37
3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29
4. kuondoa kisheria (tarakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX ) na Agano Jipya, Mat. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Cor. 7:11
5. kuondao deni, Mt. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mat. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mt. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipya, Mt. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiondoa toka kwenye
   a. Sheria, Mat. 23:23; Matendo 21:21
   b. imani, Ezek. 20:8 (LXX ); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipya wasingalifikiri kuyahusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusishwa miongoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

I. Agano la Kale
   A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
   B. Kora, Namba 16
   C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4
   D. Sauli, 1 Samueli 11-31
   E. Manabii wa uongo (mifano)
      1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (nji za kumtambau nabii wa uongo)
      2. Yeremia 28
      3. Ezekieli 13:1-7
   F. Manabii wa uongo
      1. Ezekieli 13:17
      2. Nehemia 6:14
   G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
      1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
      2. Ezekieli 22:23-31
      3. Mika 3:5-12

II. Agano Jipya

A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi."Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya

vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mt. 24:24; Marko 13:22;
Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo 13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12).

Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).

B. Imani Thabiti
  1. Yuda, Yohana 17:1
  2. Simoni mchawi, Matendo 8
  3. Wale waliozungumziwa katika Mat. 7:13-2
  4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
  5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59
  6. Alexanda na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
  7. Wale wa 1 Tim. 6:21
  8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
  9. Dema, 2 Tim. 4:10
  10. Walimu wa uongo, 2 Petro 2:19-22; Yuda 1:12-19
  11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19

C. mani isiyo kuwa na matunda
  1. 1 Wakorintho 3:10-15
  2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injlili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvn, Arminian, n.k.) unaamuru mwitikio wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki,mchungaji), si za kibiblia (tazama Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama,"na "Itisha"?). Wengine walio miongoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa miongoni mwa watu wa Mungu (m.f. Rum. 9:6).

**11: 22 "Wema na ukali wa Mungu"** Njia za Mungu siku zote zinaonekana kuwa mafumbo kwa wanadamu walioanguka (kama vile Isa. 55: 8- 11). Kuna matokeo mabaya kwa chaguzi zetu. Uchaguzi wa Mungu haukatazi uajibikaji wa mwanadamu. Uchaguzi wa taifa la Israeli haukumuhakikishia kila mtu kupata wokovu.

◙ **"Kama utaendelea katika wema wake"** Hii ni SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA TATU yenye KAULI TEGEMEZI YA UTEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO. Muundo huu ulimaanisha kuwa, kudumu kwa watu wa mataifa walioamini ni sharti (huu ni upande usiopendeza wa ukuu wa Mungu wa Warumi. 9); lazima tuwe waangalifu kudumisha imani yetu (kama vile Flp. 2: 12- 13). Hii inamaanisha usitahimilivu wa kundi na mtu binafsi (kama vile Gal. 6:9; Ufu. 2:7, 17; 3:6, 13, 22). Huu ni muujiza na mvutano wa ushirika na ubinafsi katika Biblia. Kuna ahadi zote mbili (kutokana na tabia ya Mungu), na patano la masharti (kutokana na kuitikia/mapokeo ya mwanadamu) Tazama Mada Maalum: Hitaji la Ustahimilivu katika 8: 25.

**11:23** Mstari huu unafuata mpangilio wa kifasihi na kithiolojia wa mst. wa 22. Kama Wayahudi watatubu na kuamini watajumuishwa. Kama watu wa Mataifa wataacha kuamini, watakataliwa (kama vile mst 20). Imani ya awali katika Kristo na kuendelea kuamini katika yeye ni muhimu kwa wote.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11: 25- 32**

**25 Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msiijue siri hii ili msijione kuwa wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli mpaka utimilifu wa Mataifa uwasili. 26 Hivyo Israeli wote wataokoka; kama**

**ilivyoandikwa. MWOKOZI ATAKUJA KUTOKA SAYUNI; ATAMTENGA YAKOBO NA MAASIA YAKE. [27]NA HILI NDILO AGANO LANGU NAO, NITAKAPOWAONDOLEA DHAMBI ZAO. [28]Basi kwa habari ya Injili wamekuwa adui kwa ajili yenu; kwa habari ya kule kuchaguliwa wamekuwa wapenzi kwa ajili ya baba zetu; [29]kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake. [30]Kwa maana kama ninyi zamani mlivyomuasi Mungu, lakini sasa mmepata rehema kwa kuasi kwao; [31]kadhalika na hao wameasi sasa, ili kwa kupata rehema kwenu wao nao wapate rehema. [32]Maana Mungu amewafunga wote pamoja katika kuasi ili awarehemu wote.**

**11: 25 "kwa maana, ndugu zangu, sipendi msijue siri hii."**Hii ni namna ya nahau za Paulo (kama vile 1:13; 1 Kor. 10:1; 12: 1; 2 Kor. 1:8; 1 The. 4:13). Kawaida inaanzisha mjadala muhimu. Inafanya kazi kama herufi ya mwanzo ya jina Yesu "Amina, Amina" Paulo mara nyingi anaitumia kuashiria mada mpya.

◙

**NASB, NKJV,**
**NRSV "muujiza"**
**TEV "siri ya ukweli"**
**NJB "sababu iliyofichika kwa yote haya"**

## MADA MAALUM: SIRI

A. Katika vidokezo vya injili "siri" unatumika kwenye mitizamo ya kiroho iliyokusanywa toka kwenye mifano ya Yesu.
   1. Marko 4:11
   2. Mathayo 13:11
   3. Luka 8:10
B. Paulo anaitumia kwa namna tofauti mbalimbali.
   1. Kusita kwa Israeli kuwaruhusu watu wa mataifa ili kujumuishwa. Uvamizi huu wa watu wa mataifa utatenda kazi kama chombo kwa ajili ya Wayahudi kumkubali Kristo Yule wa unabii (kama vile Rum. 11:25-32).
   2. Injili ilijulikana kwa mataifa, ikisema kuwa wote wamejumuishwa katika Kristo na kupitia Kristo (kama vile Rum. 16:25-27; Kol. 2:2).
   3. Miili mipya ya waamini kwenye ujio wa mara ya pili (kama vile 1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).
   4. Kuhitimisha mambo yote katika Kristo (kama vile Efe. 1:8-11).
   5. Wamataifa na Wayahudi kama warithi wenza (kama vile Efe. 2:11-3:13).
   6. Ushirika wa ndani kati ya Kristo na kanisa ulioelezewa kwa namna ya maneno ya ndoa (kama vile Efe. 5:22-33).
   7. Wamataifa wakajumuishwa ndani ya watu wa agano na Roho wa Kristo kuishi ndani yao ili kuleta ukomavu unaomfanana Kristo, yaani, kurejesha taswira ya Mungu iliyoharibika ndani ya mwanadamu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 6:5,11-13; 8:21; 9:6; Kol. 1:26-28).
   8. Mpinga Kristo wa siku ya mwisho (kama vile 2 The. 2:1-11).
   9. Wimbo wa kanisa la mwanzo kuhusu muujiza wa injili unaopatikana katika 1 Tim. 3:16.
C. Katika ufunuo wa Yohana unatumika kumaanisha alama za Yohana za matukio ya siku ya mwisho.
   1. 1:20
   2. 10:7
   3. 17:5,6
D. Hizi ni kweli ambazo mwanadamu hawezi kuzigundua; lazima zifunuliwe na Mungu. Hii mitizamo ni ya muhimu kwa ajili ya uelewa wa kweli wa mpango wa Mungu wa milele kwa ajili ya ukombozi wa watu wote (kama vile Mwa. 3:15). Angalia MADA MAALUM: MPANGO WA YHWH WA UKOMBOZI WA MILELE.

◙ **"Hebu uwe na hekima katika makadirio yako"** Hapa kuna kidokezo kingine cha mvutano katika makanisa ya Rumi (kama vile mst. 18).

◙

**NASB "kwamba kushupaza moyo kiasi kumeonekana kwa Israeli"**
**NKJV "kwamba kushupaza moyo kidogo kumetokea kwa Israeli"**
**NRSV "kushupazwa moyo kumetokea katika sehemu ya Israeli"**
**TEV "kwamba ukaidi wa watu wa Israeli sio wakudumu"**
**NJB "sehemu moja ya israeli imetiwa upofu"**

Usemi huu lazima uhusishwe na sura yote ya 11. Pamekuwa na pataendelea kuwepo baadhi ya wayahudi wanaoamini. Sehemu hii ya upofu ulisababishwa na Mungu (mst. 8- 10) kwa sababu ya wayahudi kukataa Yesu, unaoana vizuri na mpango wa Mungu wa kuwakomboa wanadamu wote. Mungu aliahidi wokovu kwa wote (kama vile Mwa. 3:15). Yeye alimchagua Ibrahimu ili kuwafikia wote (kama vile Mwa. 12:3). Aliichagua Israeli kuwafikia wote (kama vile Kut. 19:5-6, Tazama mada maalumu katika 8: 28). Israeli ilishindwa katika juhudi za mkakati wake kupitia majivuno, kutokuwa na uaminifu na kutoamini.

Mungu alitaka kuufikia ulimwengu wa watu wa Mataifa kupitia katika baraka zake kwa Israeli (kama vile Kumb. 27-29). Israeli haikuweza kutunza agano kwa hiyo hukumu ya Mungu ya muda ikawaangukia. Sasa Mungu ameichukua hukumu hii na kuitumia kutimiza kusudi lake la awali la kuwakomboa wanadamu kupitia imani (mst. 30-31; Eze. 36:22-38).

◙ **"Hadi ukamilifu wa watu wa Mataifa utakapotimia"** Neno hilihili *(pleroma*) limetumika katika mst. 12 kwa wayahudi. Misitari yote miwili inazungumzia ufahamu na uchaguzi wa Mungu wa kujua kabla. Neno "hadi" linazungumzia ukomo wa muda kwa hawa watu wa Mataifa (kama vile Lk. 21-24).

**11: 26 "Israeli yote itaokolewa"** kuna tafsiri mbili zinazowezekana.

1. Hii inamaanisha taifa la Israeli - sio kila Myahudi mmoja mmoja lakini kwa wingi wao katika hatua fulani.
2. Inamaanisha pia Israeli ya Kiroho, kanisa.

Paulo alitumia dhana hii katika Rum.2: 28- 29; Gal. 6: 16; 1 Pet.2: 5,9; Ufu. 1: 6. "Sehemu yote ya Wayahudi" katika mst 12 na "sehemu yote ya watu wa Mataifa"katika mst 25 yana uhusiano uliosambamba. "Wote" kwa maana ya uchaguzi wa Mungu, na sio wote kwa maana ya kila mmoja. Mti wa mzeituni wa ahadi siku moja utakuja kutimia.

Baadhi ya watoa maoni wanasema kuwa, hii inamaanisha taifa la Israeli <u>pekee</u> kwa sababu ya

1. Mazingira ya sura ya 9-11
2. Nukuu za Agano la Kale katika mst. 26-27
3. Maelezo ya wazi katika mst. wa 28.

Mungu bado ana upendo na shauku ya kuokolewa kwa mbegu ya uzao asilia wa Ibrahimu! Lazima waje kupitia katika imani kwa Kristo (Zek. 12:10). Swali ni kama wale wayahudi "walioshupazwa mioyo yao"watakuwa na nafasi ya muda wa mwisho wa kukubali haliwezi kujibiwa kutoka katika maandiko haya au mengine.Kama wamarekani tulivyo tamadunishwa kuhoji maswali, lakini Biblia imeweka wazi kwa watu wote. Maswali yote kama haya lazima yaachiwe Mungu. Atakuwa wa haki kwa uumbaji wake ambao anaupenda!

◙ **"Kama ilivyoandikwa"** Hii inarejea katika nukuu mbili kutoka katika maandiko ya kale ya tafasiri za Kiyunani ya Isa. 59: 20- 21 (mst. 26) na 27: 9 (mst. 27). Mbinu ya wokovu lazima iwe katika imani kwa Yesu Masihi.Hakuna mpango B, ni mpango wa A tu. Kuna njia moja tu ya kuokolewa,(kama vile Yn. 10: 7-18; 11: 25-29; 14: 6).

**11: 27** Isa. 27: 9, ambayo inanukuliwa katika mst. 27, inaunganisha kurejeshwa kwa Israeli katika nchi ya ahadi (mst 1- 11) ukiwa na ukaribisho kwa adui wa kitamaduni (mataifa ya watu wa mataifa) kujumuishwa (mist. 12-13). Kama kurejeshwa huku ni kwa kawaida, kwa hiyo karne hii itatimiza unabii huu. Kama nimwonekano, basi agano jipya ambao ni muujiza wa injili, ambao wayahudi na watu wa mataifa wameunganishwa kwa imani katika Masihi wa Mungu litakuwa ndiyo lengo (kama vile Efe. 2: 11- 13). Ni vigumu kuamua. Baadhi ya unabii wa Agano la Kale unatumika kwa kanisa la agano jipya. Lakini bado Mungu yu mwaminifu kwa ahadi zake, hata pale ambapo wanadamu hawako tayari (kama vile Eze. 36: 22- 36).

**11: 28** Mstari huu unaakisi maswala pacha ya uchaguzi

1. Katika Agano la Kale, uchaguzi ulikuwa kwa ajili yahuduma, Mungu alichagua vyombo vya binadamu kwa lengo la kumkomboa mwanadamu.
2. Uchanguzi katika Agano Jipya unaunganishwa na injili na wokovu wa milele, wokovu huu wa wanadamu wote waliotengenezwa kwa mfano wake limekuwa daima ndilo lengo lake (kama vile Mwa. 3: 15)

Mungu ni mwaminifu kwa ahadi zake. Hii ni kweli kwa waumini wa Agano la Kale na watakatifu wa Agano Jipya. Kiini niuaminifu wa Munguna siyo wa mwanadamu, huruma ya Mungu, na siyo utendaji wa mwanadamu. Uchaguzi ni kwa kusudi la kubariki na siyo la kubagua!

◙ **"Ni wapendwa kwa ajili ya Baba zao"** Hii ni ahadi toka Kut. 20: 5- 6 na Kumb. 5: 9- 10 na 7: 9. Familia zinabarikiwa kutokana na imani ya vizazi vilivyopita. Israeli ilibarikiwa kutokana na wazee wa umri walioheshimika (kama vile Kumb. 4: 37; 7: 8; 10: 15). Kwamba Masihi angekuja kutoka Yuda ambayo ilikuwa pia ni ahadi kwa Daudi (kama vile 2 Sam. 7). Hata hivyo lazima isemwe kwamba, hata "wenye imani" hawakuweza kutunza sheria kikamilifu (kama vile Ezek. 36: 22- 36).Imani – imani binafsi, imani ya familia, lakini siyo imani kamilifu-inakubalika na Mungu na inaendelezwa kwa hakika kupitia familia (kama vile 1 Kor. 7: 8- 16)

**11:29**

**NASB, NKJV,**

**NRSV "kwa vile zawadi na wito wa Mungu haubatilishwi"**

**TEV "kwa vile Mungu habadili mawazo yake kuhusu nani Wa kumchagua na kumbariki"**

**NJB "Mungu harudishi vipawa vyake au kubatilisha uchaguzi wake"**

Hii haimanishi zawadi za kiroho kwa watu binafsi (kama vile 1 Kor. 12), lakini kwa ahadi za Mungu za wokovu katika Agano la Kale na Agano Jipya. Uchaguzi una uwezo.uaminifu wa Mungu ni tumaini la Taifa la Israeli (kama vile Mal. 3: 6) na Israeli ya kiroho!

**11: 30-32** Mistari hii ni ufupisho wa mipango na makusudi ya Mungu.

1. Siku zote zinalenga huruma yake (Tazama maelezo katika 9: 15- 16. Sio uamuzi wa ovyo ovyo. Neno "huruma" limetumiwa mara nne kwa upana wa mazingira haya (kama vile 9: 15, 16, 18, 23)
2. Mungu amehukumu wanadamu wote. Wayahudi na watu Mataifa wote ni watenda dhambi (kama vile 3: 9, 19, 23; 5: 11).
3. Mungu ametumia mahitaji ya mwanadamu na uwezo wao duni kama fursa ya kuonyesha huruma kwa wanadamu wote (kama vile mst 22). Tena katika mazingira hayo ya neno"wote" lazima inaonekana katika mwanga wa mistari 12 na 25-26. Siyo wanadamu wote watapokea vipawa vya Mungu, lakini wote wamejumuishwa katika mtizamo wa ukombozi (kama vile 5: 12-21; Yoh. 3:16).
   Mungu wangu, na iwe hivyo!

**11:30 na 31 "lakini sasa"** Hii kwa nguvu zote inaonyesha kubadilika kiroho katika taifa la waisraeli kwa imani katika Kristo (kama vile Zek. 12: 10). Kama watu wa mataifa,"kutoamini"kumeshindwa na huruma ya Mungu, vivyo hivyo kwa "kutoamini" kwa wayahudi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11: 33-36**

**33 Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! 34 maana ni nani aliyeijua nia ya bwana? au ni nani aliyekuwa mshauri wake ? 35 au ni nani aliyempa yeye kitu kwanza, naye atalipwa tena? 36 Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu *una* yeye milele. Amina.**

**11:33-36** Hii ni mojawapo ya namna za ajabu za kumsifu Mungu zilizofanywa na Paulo bila kufikiria. Paulo anazidiwa na njia za Mungu: uaminifu wa agano, jumuisho la agano, utimilifu wa agano.

**11: 33 “utajiri”** Hii ni nahau alioipenda Paulo (kama vile 2: 4; 9: 23; 10: 12; 11: 12, 33; Efe. 1: 7, 8; 2: 7; 3: 8, 16; Flp. 4:19; Kol. 1: 27). Msukumo wa injili na tumaini la mwanadamu ni tabia na mpango wa Mungu wa wingi wa huruma yake (kama vile Isa. 55: 1 -7).

◙ **“Hukumu zake hazitafutwi wala njia zake hazielezeki”** Hii ni namna sahihi ya kumsifu Mungu katika ukweli wa sura ya 9- 11 (kama vile Isa. 55: 8-11)

**11: 34** Hii ni nukuu kutoka katika maandiko ya kale ya tafasiri ya Kiyunani katika Isa. 40: 13-14, ambapo Mungu anawarudisha watu wake toka utumwani. Katika 1 Kor. 2: 16, Paulo ananukuu habari hii lakini anakithamanisha cheo cha neno “Bwana” kwa Yesu.

**11: 35** Hii ni nukuu dhaifu kutoka katika Ayubu. 35: 7 au 41: 11.

**11: 36 “Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake”** Mafungu haya yanamaanisha Mungu Baba katika muktadha huu (kaka vile 1 Kor.11: 12), lakini yanafanana kabisa na jumbe zingine za Agano jipya ambazo zinamaanisha Mungu Mwana (kama vile 1 Kor. 8: 6; Kol. 1: 16; Ebr. 2: 10). Paulo anakazia kuwa, vitu vyote hutoka kwa Mungu na vitarudi kwa Mungu.

◙ **“Utukufu *una* yeye milele”** Hii ni namna ya Baraka za Agano Jipya juu ya Uungu. Ilimaanisha

1. Wakati mwingine kwa Baba (kama vile 16: 27; Efe. 3: 21; Flp. 4: 20; 1 Pet. 4: 11; 5: 11;Yuda 25; Ufu. 5: 13; 7: 12)
2. Wakati mwingine kwa mwana (kama vile 1 Tim. 1: 17; 2 Tim. 4: 18; 2 Pet. 3: 18; Ufu. 1: 16). Tazama nukuu kamili katika 3: 23.

◙ **“Amina”** Tazama mada maalum katika 1: 25.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa vipi Israeli ilikosa njia ya Mungu ya wokovu?
2. Paulo anatoa sababu gani mbili kuu kuthibitisha kuwa, Mungu hajaikataa Israeli?
3. Kwa nini Mungu alifanya mioyo ya Israeli kuwa migumu? Kwa namna gani?
4. Inamaanisha nini kwa dhana ya Wayahudi ya neno “masalia” (mst 2- 5)?
5. Fasili neno “muujiza” katika Agano Jipya
6. 11: 26 inamaanisha nini? Kwa nini? Inahusianaje na 9:6
7. Ni onyo gani Paulo analitoa kwa watu wa Mataifa wanaoamini (mist. 17-24)

# WARUMI 12

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Maisha Mapya katika Kristo | Maisha ya kujidhabihu kwa Mungu | Maisha ya Kujiweka wakfu | Maisha katika huduma ya Mungu | Ibada ya Kiroho |
| 12:1-2 | 12:1-8 | 12:1-2 | 12:1-2 | 12:1-2 |
| | | | | Unyenyekevu Wema |
| 12:3-8 | | 12:3-8 | 12:3-8 | 12:3-13 |
| Sheria za Maisha Ya Mkristo | Kuishi kama Mkristo | Ushawishi | | |
| 12:9-21 | 12:9-21 | 12:9-13 | 12:9-13 | Unyenyekevu kwa Kila mtu Wakiwemo Maadui |
| | | 12:14-21 | 12:14-6 | 12:14-21 |
| | | | 12:17-21 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA MISTARI 1-8

A. Hii inaanza na sehemu ya vitendo vya Warumi (12:11-15-3). Barua za Paulo zilikuwa hati za wakati tu, kwa hiyo zina sehemu za imani na matumizi. Paulo aliandika kuhusu tatizo au mgogoro katika eneo. Kwa vile Warumi 1-8 ni ufupisho wa kiimani na ajabu, sehemu yake ya kimaandishi na vitendo ina nguvu sawa.

B. Theolojia bila matumizi ya mtindo wa maisha sio ya Mungu (kama vile Mt 7:24-27; Yoh.13:17; Rum.2:13; Yak. 1:22, 25; 2:14-26) Paulo waziwazi anfundisha wokovu wa bure kwa neema ya Mungu kupitia imani katika Yesu, lakini zawadi hii ya bure inakusudiwa kufanya mabadiliko makubwa ya maisha yetu! Wokovu

ni bure, lakini lazima ufuatiwe na kufanana kwa dhati na Kristo! Hatuthubutu katu kutenganisha uhalalisho kutoka katika utakaso.

C. Mistari ya 1-2 inaunda utangulizi kwa sehemu nzima ya vitendo. Ni msingi wa maisha yanayoongozwa na Roho (yaani, sura ya 8).

D. Mistari ya 3-8 inajadili hali ya kuzawadiwa kiroho. Kujitoa kwetu kikamilifu kwa Kristo lazima ulenge katika huduma kwa Mungu (kama vile Kumb. 6:4-5; Mt. 22:27) na kwa wengine (kama vile Uf.19:18; Mt. 19:19). Zawadi hizi zinasisitiza umoja wetu katika Kristo na kutofautiana kwetu katika hali ya zawadi (kama vile Efe. 4:1-10). Waliokombolewa lazima wapambane kuupata umoja na sio kufanana. Tumeimarishwa na Mungu kuhudumiana (kama vile 1Kor. 12:7, 11; Efe. 4:11-13)!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:1-2**
**1Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. 2Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.**

◙ **"Kwa hiyo"** Paulo alitumia neno hili katika hatua muhimu ya kutoka wazo moja kwenda lingine wakati wa kuuwasilisha ukweli wa injili katika kitabu cha Warumi.

1. katika 5:1 na kuendelea ni jumuisho la "uhalalisho kwa imani"
2. katika 8:1 na kuendelea ni jumuisho la uhusiano wa waumini' na dhambi, iliyoitwa utakaso
3. 12:1 na kuendelea inahusianisha na kitendo cha utekelezaji wa uhalalisho na utakaso katika maisha ya kila siku ya waumini'

**12:1**
**NASB "Nawasihi"**
**NKJV "Namtakeni".**
**NRSV, TEV "Nawaombeni"**
**NJB "Ninaomba**

Usemi huo ni rahisi na ni mgumu. Ni wito wa kuishi vizuri. Paulo siku zote alilitumia neno hili (kama vile 12:1; 15:30; 16:17; 1 Kor.1:10; 4:16; 16: 15; 2 Kor.2:8; 5:20; 6;1; 10:1; 12:8; Efe.4:1; Flp. 4:2; The. 4:10; Tim. 1:3; Flp. Mist. 9-10).

◙ **"ndugu"** Daima Paulo alitumia neno hili katika kuanza somo jipya.

◙ **"kwa huruma zake Mungu"** katika maandiko ya kale ya miaka ya 70 hii inaelezea asili ya upendo wa YHWH (kama vile Kut.34:16) hii inamaanisha maendeleo ya imani ya sura ya 1-11. Kuna msisitizo wa wazi katika warumi juu ya "huruma" (*oikieir o* na *elee o*) ya Mungu katika kushughulika na mwanadamu aliyeanguka (kama vile 9:15,16, 18, 23; 11:30, 31, 32; 12:8; 15:9). Kwa kuwa neema na huruma vinatolewa bure, waumini lazima waishi maisha ya kimungu (kama vile Efe. 1:4; 2:10) kutokana na sio ubora wa utendaji (kama vile Efe. 2:8-9). Maisha mapya (yaani Kol. 3:9;10, 12) inakusudiwa kugeuza wengine kuwa na imani kwa Kristo!

◙ **"itoeni"** Hii ni KAULI TIMILIFU ISIYO NA UKOMO Hii ilikuwa moja ya maneno ya sadaka yaliyo tumika katika mazingira haya. Sadaka mst. 1; takatifu mst. 1, kupokelewa, mst. 1. Dhana hii inaelezwa katika 6:13, 16, 19. Wanadamu watajitoa kwa Mungu au kawa shetani. Kwa vile Kristo alijitoa kipekee kutimiza haja ya Babaye, hata kifo katika msalaba, wafuasi wake lazima pia waige maisha yake yasiyo ya ubinafsi (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yn. 3:16).

◙ **"miili yenu"** Ukristo ni tofauti kutoka falsafa halisi ya Kiyunanai, iliyofikilia kuwa mwili wa ulioumbwa ni mwovu. Ni neno la majaribu lakini kati kimaadili. Neno "mwili" inaonekana kuendana na "fikra" katika mst. 2. Waumini inawapasa kujitoa kikamilifu kwa Mungu (kama vile Kumb. 6:5; 1Kor. 6:20) kama mwanzo walivyokuwa wamejitoa kwa dhambi (kama vile Warumi. 6).

◙**"iliyo hai"** Hii ilikuwa tofauti kabisa na sadaka mfu za Wayahudi au mahekalu ya wapagani (kama vile 6:13; Gal. 2:20).

Lazima pia itofautishwe na kusulibiwa (tendo la kikatili kwa mwili kwa lengo la kidini). Sio kulengwa kwa mwili, adhabu au utaua bali maisha kamili ya huduma na upendo wa kufanana na Kristo.

◙ **"sadaka takatifu"** neno "takatifu" lina maana ya "kutengwa kwa ajili ya huduma ya Mungu". Mtazamo wa neno hili katika mazingira haya ni kwa ajili ya kuwakifishwa waumini na upatikanaji wao kwa Mungu kwa ajili ya kusudi lake.

## MADA MAALUMU: TAKATIFU

I. Agano la Kale (likielezwa kwa zaidi kutoka Isaya)
   A. Asili ya neno *kadosh* (BDB 872, KB 1072) halina uhakika, pengine ni Ki-kanaani (yaani, lugha Magharibi mwa Syria). Inawezekana kwamba sehemu ya mzizi wa neno (yaani, *kd*) unamaanisha "kugawanya."

      Hiki ni chanzo cha ufafanuzi unaofahamika wa neno "tengwa (kutoka kwenye utamaduni wa ki-Kanaani, kama vile Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19) kwa matumizi ya Mungu."
   B. Inahusiana na uwepo wa Mungu ndani ya vitu, mahali, wakati, na watu. Halitumiki katika kitabu cha Mwanzo, bali linakuwa la kawaida katika vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu.
   C. Katika fasihi ya Kinabii (hasa Isaya na Hosea) hali ya kibinadamu ilikuwepo hapo awali, lakini haikuhimizwa kwa ajili ya kutenda kazi (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu). Inakuwa njia ya kueleza asili ya Mungu.(kama vile Isa. 6:3). Mungu ni Mtakatifu. Jina Lake linalowakilisha sifa yake ni takatifu. Watu wake ndio wanaopaswa kuifunua sifa Yake kwa ulimwengu unaohitaji utakatifu (ikiwa watalitii agano katika imani).
      1. KIVUMISHI, BDB 872 קדוֹשׁ, "takatifu," "tukufu" linatumika juu ya
         a. Mungu, Isa. 5:16; 6:3 (mata tatu); tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu
         b. Jina Lake, Isa. 40:25; 49:7; 57:15
         c. kukaa Kwake ndani, Isa. 57:15
         d. Sabato, Isa. 58:13
      2. KITENZI, BDB 872 קדשׁ, "kutengwa mbali," "wekwa wakfu"
         a. sifa ya Mungu, Isa. 5:16; 29:23
         b. Mungu, Isa. 8:13; 65:5
         c. malaika wa Mungu, Isa. 13:3
         d. jina la Mungu, Isa. 29:23
         e. sherehe za kidini, Isa. 30:29
         f. wanadamu walioweka wakfu, Isa. 66:17
      3. NOMINO, BDB 871 קדשׁ, "utengwaji," "uwekwaji wakfu"
         a. uzao mtakatifu, Isa. 6:13
         b. mlima mtakatifu, Isa. 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
         c. kutengwa, Isa. 23:18
         d. njia ya utakatifu, Isa. 35:8
         e. mahali patakatifu, Isa. 43:28; 62:9; 64:11
         f. mji mtakatifu, Isa. 48:2; 52:1
         g. aliye Mtakatifu, Isa. 49:7 (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu)
         h. mkono mtakatifu, Isa. 52:10
         i. siku takatifu, Isa. 58:13

j. watu watakatifu, Isa. 62:12
k. Roha Mtakatifu, 63:10,11
l. Kiti cha enzi cha Mungu, Isa. 63:15
m. sehemu takatifu, Isa. 63:18
n. miji mitakatifu, Isa. 64:10

D. Huruma ya Mungu na upendo havitenganishwi kutoka katika dhana ya theojia ya maagano,haki, na sifa ya muhimu. Humu ndani pana mvutano wa Mungu dhidi ya utu ulioanguka, usio mtakatifu ,wenye kuasi. Kuna mada inayotia shauku sana kuhusiana na mahuhusiano kati ya Mungu kama "mwenye huruma" na Mungu kama "mtakatifu" katika kitabu cha Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 112-113.

II. Agano Jipya

A. Waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Luka) walikuwa Waebrania wenye fikra pana, lakini waliandika katika lugha ya kawaida ya Koine. Kanisa la Agano Jipya lilitumia fasiri ya Kiyunani kufasiri kitabu cha Agano la Kale. Ilikuwa ni tafasili ya Kiyunani ya Agano la Kale, sio fasihi ya Kiyunani cha daraja la juu, fikra, au dini, iliyodhibiti misamiati yao.

B. Yesu ni mtakatifu kwa kuwa Yeye ni wa Mungu na ni sawa na Mungu (kama vile Luka 1:35; 4:34; Matendo 3:14; 4:27,30; Ufu. 3:7). Yeye ni Mtakatifu na Mwenye Haki (kama vile Matendo 3:14; 22:14). Yesu ni mtakatifu kwa sababu hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).

C. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu (kama vile Yohana 17:11; 1 Pet. 1:156-16; Ufu. 4:8; 6:10), watoto Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Mat. 5:48; 1 Pet. 1:16). Kwa kuwa Yesu ni mtakatifu, wafuasi Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Wakristo wameokolewa ili kutumika katika ufanano wa Kristo (wenye utakatifu)

◙**"ya kumpendeza Mungu"** Hii inamaanisha kutoa kwa usawa katika Agano la Kale (kama vile) Hii ni sawa na dhana ya kutokuwa na lawama, linapotumika kwa watu (kama vile Mwa. 6:9; 17:1; Kumb. 18:13; Ayubu 1:1.

◙

**NASB "hii ndiyo ibada yenu ya kuabudu"**
**NKJV "hii ndio ibada yenu"**
**NRSV "ipi ni ibada yako ya kiroho"**
**TEV "hii ndiyo njia yenu halisi ya kumwabudu"**
**NJB "kwa njia ipasayo ya wanadamu"**

Neno hili [*logikos*] limetokana na *logizomai*, likimaanisha "kufikiria" (kama vile Marko 11:31; 1 Kor 13:11; Flp. 4:8). Katika mazingira haya ingemaanisha usawa au chenye maana sawa. Lakini neno pia lilitumika kwa maana ya "kiroho" kama ilivyo katika 1 Pet. 2:2. Umuhimu unaonekana kuwa ni utambuzi wa kujitoa kwa ukweli wa nafsi na ya mtu mwenyewe dhidi ya wafu au kafara ya mitambiko ya wafu na wanyama. Mungu anataka maisha yetu katika upendo na sio kufuata taratibu zilizo rasmi ambazo hazina matokeo yo yote katika maisha ya kila siku.

**12:2 "wala msifuatishe"** Ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (au KAULI TIMILIFU YA KATI) Yenye KISHIRIKISHI HASI ambacho kinamaanisha kusitisha kitendo ambacho kinaendelea. Kuna tofauti na mstari wa 2 unaofanana na ule katika Wafilipi 2:6-8, kati ya badiliko la umbo la nje (*schema*, 2:8) na kutobadilika kwa ndani. (*Morphe* 2:6-7). Waumini wanashauliwa kutoendelea kuwa kama kubadilika kwa mfumo wa ulimwengu ulioanguka (enzi Za kale Za uasi), ambao hata leo bado umemeguka, bali kubadilishwa kikweli kuwa kama Kristo (enzi mpya ya Roho).

◙ **"namna ya dunia hii"** Hii kwa lugha rahisi ni "enzi". Wayahudi waliona enzi mbili (kama vile Mt. 28:20; Ebr.1:3; 1 Yn. 2:15-17). Waumini wanaishi katika wakati uliojaa mvutano, ambao enzi hizi kwa mshangao zinaingiliana. Kwa sababu ya aina mbili za ujio wa Kristo, waumini wanaishi katika mvutano wa "tayari na bado" wa Ufalme wa Mungu kama vile sawa na badaye

## MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

| **Yesu** | **Paulo** | **Webrania (Paulo)** |
|---|---|---|
| Mt. 12:32; 13:22,39 | Warumi 12:2 | Ebr.1:2; 6:5; 11:3 |
| Marko 10:30 | 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18 | |
| Luka 16:8; 18:30; 20:34-35 | 2 Kor. 4:4 | |
| | Wagalatia 1:4 | |
| | Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12 | |
| | 1 Timotheo 6:17 | |
| | 2 Timotheo 4:10 | |
| | Tito 2:12 | |

Katika theolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

◙ **"mgeuzwe"** Waumini lazima wabadilishwe (kama vile 6:4; 7:6; 2Kor. 5:17; Gal. 6:15; Efe. 4; 22-24; Kol. 3:10), na sio tu kufahamishwa! Muundo wa kisarufi wa neno hili laweza kuwa KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO "kuendelea kujibadilisha ninyi wenyewe" au NI HALI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO "kuendelea kubadilishwa" Hii pia ni sawa na "kujifananisha" kiumbe katika mst. 2a. Kwa utofautisho huo huo, linganisha Ezekiell 18:31 (kujitoa kwa mwanadamu na kitendo) na Ezekiel 36:26-27 (zawadi ya Mungu) vyote viwili vinatakiwa!.

Namna hii ya neno kwa "badilishwa" linatumiwa juu ya Yesu katika kugeuka sura (kama vile Mt. 17:2), ambapo maana Yake halisi ilifunuliwa. Uwepo wake huu wa imani (kama vile 2 Pet. 1:3-4) ni kubadilishwa katika kila muumini (kama vile 2 Kor. 3:18; Efe. 4:13).

◙ **"kwa kufanywa upya nia zenu"** Hili linatokana na asili ya neno Kiyunani kuwa"mpya" kwa ubora (*kainos*) na siyo "mpya" kwa wakati (*kronos*). Kwa Wayahudi, milango ya fahamu ya kuona na kusikia ilikuwa madilisha ya nafsi. Mtu anachofikiria ndicho huwa. Baada ya wokovu kwa ajili ya roho aishie ndani, waumini wana mtazama mpya (kama vile Efe.4:13, 23; Tito. 3:5). Mtazamo huu mpya wa ulimwengu wa Biblia, pamoja na Roho aliye ndani, ndivyo vinavyobadili fikra na mtindo wa maisha wa waumini. Waumini wanaangalia ukweli katika njia tofauti kabisa kwa sababu mawazo yao yamepata nguvu kutokana na Roho. Fikra iliyokombolewa kwa kuongozwa na Roho, inaleta matokeo mapya katika mtindo wa maisha. Hiki ndicho Agano Jipya lilichoahidi (kama vile Yer.31:31-34).

## MADA MAALUM: KUFANYA UPYA (*anakainōsis*)

Neno hili la Kiyunani katika muonekano wake tofauti (*anakainoō, anakainizō*) lina maana mbili za msingi

1. "Kukifanya kitu kuwa kipya na cha tofauti (yaani., bora)"-Rum. 12:2; Kol.3:10
2. "Kufanya badiliko toka kwenye hali ya nyuma iliyokuwa ikipendelewa"-2 Kor. 4:16; Ebr. 6:4-6

(limechukuliwa toka kwa Louw and Nida's *Greek-English Lexicon,* juzuu. 1, kur. 157, 594)
Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, anasema kuwa neno hili (yaani., *anakkainōsis*) haliwezi kupatikana katika fasihi za Kiyunani mapema zaidi kuliko Paulo. Huenda Paulo amelitunga neno hili mwenyewe (uk. 34).

Frank Stagg, *New Testament Theology,* ana hoja ya kufurahisha.

"kuzaliwa upya na kufanywa upya kunamhusu Mungu mwenyewe. *Anakainōsis*, neno kwa ajili ya "kufanywa upya," ni nomino ya kitendo, na linatumika katika Agano Jipya, likiwa na miundo wa kitenzi, ikielezea hali ya mwendelezo wa kufanyika upya, kama ilivyo katika Warumi 12:2, ' ….' na 2 Wakorintho 4:16, '….' Wakolosai 3:10 inamwelezea 'mtu mpya' kama 'yule aliyefanywa upya kwa mpangilio kutokana na taswira ya yule aliye muumba.' Kwa maana hiyo ni 'mtu mpya,' 'maisha mapya' 'kuzaliwa upya' au 'kufanywa upya' hata hivyo usanifishwaji, unaangaliwa kwenye kitendo cha awali na kitendo endelevu cha Mungu kama mtoaji na mwezeshaji wa maisha ya milele" (uk. 118).

◙**"mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu"** Huu ni WAKATI ULIOPO UNAOENDELEA. Neno (*dokimazō)* linatumika kumaanisha "kujaribu kwa uthibitisho" Tazama Mada Maalumu katika 2:18. Nia ya Mungu ni kuwa wote waokolewe kupitia Kristo (kama vile Yoh. 6:39-40), na kisha kuishi maisha sawa na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19, Efe. 1:4; 4:13, 15; 5:17-18). Uthibitisho wa Kristo (tazama Mada Maalumu katika 5:2) imejikita katika

1. Ahadi za Mungu anaye aminika
2. Roho Mtakatifu aishie ndani (kama vile Rum. 8:14-16)
3. Maisha ya muumini yaliyobadilika (kama vile Yakobo. Na I Yohana) "Hakuna tunda hakuna mzizi" (kama vile Mt.13:1-9 19:23)

◙ **"yapi mapenzi ya Mungu ni"** Tazama Mada Maalumu ifuatayo.

## MADA MAALUM: MAPENZI (*thelēma*) YA MUNGU

"Mapenzi" ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

INJILI YA YOHANA

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wale wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama vile Yn. 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibiwa kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vileYn. 9:31 na Yn 5:14)

VODOKEZO VYA INJILI

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile. Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)
- Sio mapenzi ya Mungu kwa yeyote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile. Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanywa kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (kama vile 1The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyekea kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (kama vile 1Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)

waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibiwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

◙ **"yaliyo mema, yakumpendeza na makamilifu"** Haya yanawakilisha mapenzi ya Mungu kwa waumini baada ya wokovu (kama vile Flp.4:4-9). Lengo la Mungu kwa kila muumini ni ukomavu wa kumfanana Kristo sasa (kama vile Mt.5:48)

◙ **"Kamilifu"** Neno hili lina maana ya "kukomaa, tayari kabisa kukamilisha kazi aliyopewa," "kukua" au "kukamilika" Haimaanishi kutokuwepo "dhambi." Ilitumika kwa

1. Mikono na miguu iliyovunjika lakini sasa imepona na imerudi hali ya kawaida ya kufanya kazi.
2. Nyavu zilizochanika, lakini sasa zimeshonwa tena na zinatumika kunasa samaki.
3. Vifaranga ambavyo sasa vimekua na viko tayari kupelekwa sokoni kuuzwa.
4. Meli iliyotayarishwa kwa ajili ya safari.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:3-8**
**3Kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu asinie makuu kupita ilivyompasa kunai; bali awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani. 4kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; 5Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. 6Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadri ya neema miliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadri ya imani; 7ikiwa huduma, tutoe katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; 8mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimamia kwa bidii mwenye kurehemu, kwa furaha.**

**12:3** Mistari ya 1-2 inasisitiza haja ya kuwa na “fikra mpya.” Katika mstari wa 3. Kuna mchezo wa njia nne, kuhusu neno “fikiri.” Katika maandiko ya *The Zondervan Study Guide Commentary*, *Romans*, Bruce Corley na Curtis Vaughan wanafanya uchunguzi huu.
“Kuwaza kulikozidi, kuwaza sahihi, kuwaza kwa kusudio,…kuwaza kwa busara” (uk. 138).Ubainishaji huu unasaidia. Mstari huu, kama 11:13-24, unaweza kuakisi

1. Mvutano katika kanisa la Roma kati ya Wayahudi walioamini na watu wa Mataifa walioamini.
2. Ukweli kwamba, Paulo aliandika kuhusu Waroma akiwa Korintho (katika safari yake ya mwisho ya tatu ya Kimisionari), ambapo alikutana na waumini wakorofi, na wajivuni.

◙ **“Kwa neema niliyopewa”** Hii ni SENTESI TIMILIFU YA KUTENDEWA. Neema ilitoka kwa Mungu katika siku zilizopita, tukio lililokamilika (yaani, walipokutana njiani akielekea Dameski). Katika mazingira haya “neema” ilihusishwa na zawadi za kiroho (kama vile 15:15; 1 Kor. 3:10; 15:10; Gal. 2:9; Efe. 3:7-8). Siyo zawadi ya haki (kama vile Warumi. 4). Hii ilimaanisha kubadilika kwa Paulo na wito kuwa mtume kwa watu wa Mataifa (kama vile Mdo. 9:15; Rum. 1:1, 5; Gal. 1:15-16; 2:7-8, Efe. 3:1-2,8; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 4:17)

◙ **“Namwambia kila mmoja aliyeko kwenu”** Onyo la mstari wa tatu ni kwa wakristo wote, na si tu viongozi.

◙ **“msinie makuu kupita ilivyowapasa”** Tazama Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya maneno yaliyounga (Huper) katika 1:30.

◙ **“Kama Mungu alivyomgawia kila mtu”** Hii ni KAULI TENDEWA YENYE KUALIFU. Waumini hawachagui karama zao za kiroho (kama vile 1 Kor. 7:17; 12:11; Efe. 4:7). Wanapewa na Roho wakati wa wokovu kwa lengo zuri kwa wote (kama vile 1 Kor. 12:7). Karama za Roho siyo beji za utendaji ambazo zinampandisha mtu cheo, bali ni kuhusiana na mtumishi ili kila muumini aweze kutumika katika mwili wa Kristo, ambao ni Kanisa.

◙ **“Kiasi cha imani”**Hii ilimaanisha uwezo wa mtu kufanya kazi kikamilifu katika karama zao za kiroho walizopewa (kama vile mstari wa 6). Kuwa na afya, karama ya kiroho lazima zitumike kwa njia ya tunda la Roho (kama vilemstari wa 9-12; Gal. 5:22-23). Karama ni huduma za Yesu zilizogawiwa miongoni mwa wafuasi wake; wakati tunda ni fikra ya Kristo, vyote ni muhimu kwa utendaji sahihi wa huduma.

**12:4** Hii ni stiari ya kawaida katika maandiko ya Paulo. Kutegemeana kwa mwili wa mwanadamu kunaelezea karama za Kanisa (kama vile 1 Kor. 12:12-27; Efe. 1:23, 4:4, 12, 16, 5:30; Kol. 1:18,24, 2:19). Ukristo ni ushirika na ni wa mtu binafsi!

**12:5 “sisi tulio wengi, tu mwili mmoja katika Kristo”** Mstari huu, unasisitiza umoja wa waumini na mtu mmoja mmoja. Huu ni mvutano wa zawadi za kiroho ndani ya Kanisa. Sura ya upendo ya 1 Wakorintho 13 inajadili mvutano wa zawadi moja moja (kama vile 1 Kor. 12 na 14). Wakristo hawako katika mashindano, bali katika tume kuu ya ushirikiano!

**12:6-8** Mistari hii inaunda sentensi moja katika Kiyunani yenye KUTENDEWA lakini bila KITENZI kikuu. Kwa hiyo, inakalimaniwa kama NAFSI YA TATU YENYE SHURUTI, “hebu tutumie.

**12:6 “Vipawa..neema”** Maneno “vipawa” (*charismata*) na “neema” (*charis*) yana asili moja ya neno la Kiyunani, linalomaanisha ‘kupewa bure.” Tazama nukuu katika 3:24. Karama za Roho zimeorodheshwa katika 1Wakorintho 12; Warumi 12; Waefeso 4 na 1 Petro 4. Orodha na mpangilio wake haubainishwi, kwa hiyo lazima ziwe zinawakilisha na siyo zote kabisa. Biblia haiwaelezi waumini namna ya kutambua karama zao za kiroho. Wazo moja zuri sana la busara, lisilo la kibiblia katika swala hili, linapatikana katika kanuni zilizomo katika kijitabu, cha ‘Inter Varsity Press’ kilichoandikwa na Paulo mdogo kiitwacho ‘*Affirming the Will of God*.’ Miongozo hii ya kuyajua mapenzi ya Mungu inafanya kazi katika kujua neno la mtu katika utendaji thabiti. Sambamba na hayo, kujua kuwa waumini wamezawadiwa ni muhimu zaidi kuliko kujua namna gani wamezawadiwa, au ni zawadi ipi hasa wamepewa.

◙ **"kama"** Hii ni neno *eite* (kama vile mistari ya 6,7 [mara mbili], 8), ambalo linakalimaniwa kuwa " kama…kama" au "endapo…endapo" katika maana yake. Inafatiwa na bila KITENZI katika mstari huu (kama vile 1 Kor. 3:22; 8:5; 2 Kor 5:10), lakini daima inafuatiliwa na KITENDO ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO (kama vile 1 Kor 12:26; 2 Kor 1:6) na, kwa hiyo ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukulia uwepo wa karama hizi za kiroho.

◙ **"Unabii"** Huu hauhusiani na unabii katika AGANO LA KALE kama ujumbe (uliovuviwa) kutoka kwa Mungu. Katika AGANO LA KALE, manabii waliandika mafundisho ya Mungu (uvuvio), katika AGANO JIPYA ni tendo la kutangaza ukweli wa Mungu. Inaweza pia kuhusisha utabiri (kama vile Mdo. 11:27-28; 21:10-11). Mtazamo siyo maudhui mapya, bali ni kueleza ujumbe wa injili na jinsi unavyotumiwa sasa. Kuna udhaifu katika neno. Linaweza kutumika Kama tendo lililotendwa na waumini. (kama vile 1 Kor. 12:28; 14:29; Efe. 4:11). Udhaifu huu huu, unaweza pia kuonekana katika barua za Paulo kwa Wakorintho, zilizoandikwa karibia kipindi hicho hicho (1 Kor. 12:10, 12; 13:8; 14:1, 5,29,39).

## MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO JIPYA

I. Sio sawa na Unabii wa Agano la Kale (BDB 611, KB 661; tazama Mada Maalumu: Unabii [Agano la Kale]), ambao una vidokezo vya upokeaji wa sheria za Kiyahudi na kunukuu mafunuo yaliyovuviwa toka kwa YHWH (kama vile Matendo 3:18, 21; Rum. 16:26). Ni manabii tu waliweza kuandika maandiko.
   A. Musa aliitwa nabii (kama vile kumb. 18:15-21)
   B. Vitabu vya historia (Yoshua – Wafalme [isipokuwa Ruthu]) waliitwa "manabii wa mwanzo" (kama vile Matendo. 3:24)
   C. Manabii wanachukua nafasi ya makuhani wakuu kama chanzo cha habari kutoka kwa Mungu. (kama vile Isaya –Malaki)
   D. Mgawanyo wa pili wa kanuni za kanisa la Kiebrania ni "Manabii" (kama vile Mt. 5:17; 22:40; Luka 16:16; 24:25, 27; Rum. 3:21).

II. Katika Agano Jipya dhana ya unabii imetumika katika njia kadhaa tofauti tofauti.
   A. Kuwarejea manabii wa Agano la Kale na jumbe zao zilizovuviwa (kama vile Mt. 2:23; 5:12 11:13; 13:14; Rum. 1:2).
   B. Kuurejea ujumbe kwa mtu mmoja badala ya kikundi kichoungana (yaani, manabii wa Agano la Kale kimsingi waliongelea juu ya Israeli).
   C. Kuwarejea wote wawili Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:9; 14:5; 21:26 Luka 1:76) na Yesu kama mpiga mbiu wa ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 13:57; 21:11, 46; Luka 4:24; 7:16; 13:33; 24:19). Yesu pia alidai kuwa mkuu kuliko manabii (kama vile Mt. 11:9; 12:41; Luka 7:26).
   D. Manabii wengine katika Agano Jipya
      1. Maisha ya awali ya Yesu kama ilivyoandikwa katika injili ya Luka (yaani., kumbu kumbu za Maria)
         a. Elizabethi (kama vile Luka 1:41-42)
         b. Zakaria (kama vile Luka 1:67-79)
         c. Simoni (kama vile Luka 2:25-35)
         d. Ana (kama vile Luka 2:36)
      2. Ubashiri wa kejeli (kama vile. Kayafa, Yohana 11:51)
   E. Inarejea juu ya mtu anayeitangaza injili (ikijumuishwa kwenye orodha ya kipawa cha utangazaji katika 1 Kor. 12:28-29; Efe. 14:11)
   F. Ikirejea juu ya vipawa vinavyoendelea kanisani (kama vile Mt. 23:34; Matendo 13:1; 15:32; Rum. 12:6; 1 Kor. 12:10, 28-29; 13:2; Efe. 4:11) wakati mwingine hii inaweza kumaanisha kwa wanawake (kama vile Luka 2:36; Matendo 2:17; 21:9; 1 Kor. 14:4-5).
   G. Ikirejea kwa sehemu mafunuo ya kitabu cha ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 22:7, 10, 18,19)

III. Manabii wa Agano Jipya

A. Hawatoi ufunuo uliovuviwa kwa maana sawa kama manabii wa Agano la Kale waliofanya (yaani mafundisho ya Biblia). Usemi huu unawezekana kwa sababu ya Matumizi ya kifungu cha neno "Imani" (yaani., kwa maana ya injili iliyokamilika) iliyotumika katika Matendo 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3, 20.
Dhana hii iko wazi kutokana na fungu kamili la maneno lililotumika katika Yuda 3, "imani ya mara moja pasipo kujirudia imekabidhiwa kwa watakatifu." Imani ya "jumla pasipo kujirudia" inarejerea kwenye ukweli, mafundisho, dhana, maoni ya dunia juu ya mafundisho ya ukristo. Msisitizo huu unaotolewa mara moja tu ni msingi wa Kibiblia kwa ajili ya kuzuia uvuvio ulio wa kithiolojia wa maandiko ya Agano Jipya na pasipo kuruhusu maandiko mengine kufikirika kimafunuo (angalia Mada Maalumu: Uvuvio). Kuna maeneo mengi yenye utata, yasiojulikana katika agano jipya (Tazama Mada Maalumu: Fasihi za mashariki [mafumbo ya Kibiblia]), lakini waamini wanathibitisha kwa imani kuwa kila kitu "kinachohitajika" kwa ajili ya imani na utendaji inajumuishwa ikiwa na utosherevu wenye uwazi wa kutosha katika Agano Jipya. Dhana hii inaelezwa kama "ufunuo pembe tatu."
   1. Mungu amejidhihirisha mwenyewe katika historia kwa muda muafaka (UFUNUO)
   2. Amechagua baadhi ya waandishi wa kibinadamu kuweka kumbu kumbu na kuelezea matendo yake (UVUVIO).
   3. Alimtoa Roho Wake ili kufungua mawazo na mioyo ya watu wapate kuyaelewa maandishi haya, si kwa ubora tu bali kwa utoshelevu wa wokovu na maisha ya Mkristo yenye kufaa (NURU, tazama Mada Maalumu: nuru). Hoja iliyopo hapa ni kuwa uvuvio umewekewa ukomo kwa waandishi wa neno la Mungu. Hakuna maandiko mengine, maono au mafunuo yenye mamlaka. Sheria za kanisa zimefungwa. Tuna ukweli wote tunaouhitaji ili kuitikia vizuri kwa Mungu. Ukweli huu unaonekana vizuri katika makubariano ya waandishi wa Kibiblia dhidi ya waumini watiifu wa ki-Mungu wasiokubali. Hakuna mwandishi au mnenaji wa kisasa aliye na kiwango cha uongozi wa ki-Uungu kama ambao waandishi wa neno la Mungu waliokuwa nacho.

B. Kwa namna nyingine manabii wa Agano Jipya ni sawa na wale wa Agano la Kale.
   1. Utabiri wa matukio yajayo (kama vile Paulo, Matendo 27:22; Agabo, Matendo 11:27-28; 21:10-11; manabii wengine wasiotajwa Matendo 20:23).
   1. Kutangaza hukumu (kama vile Paulo, Matendo 13:11; 28, 25-28)
   2. Dalili za matendo ambayo dhahili yanaonyesha matukio (kama vile Agabo Matendo 21:11).

C. Mara zote wananena kweli ya injili, wakati mwingine kwa njia ya utabiri (kama vile Matendo 11:27-28; 20-23; 21:10-11) Lakini kimsingi huu sio mtazamo wenyewe. Unenaji wa unabii katika Wakorinto wa 1 kimsingi unaibainisha injili (kama vile 1 Kor. 14:24,39).

D. Ni Roho wa wakati ule ule akimaanisha kudhihirika wakati ule ule na utumiaji wa kiutendaji wa kweli ya Mungu kwa kila hali, tamaduni mpya au kipindi cha muda (kama vile 1 Kor. 14:3).

E. Walikuwa imara katika makanisa ya mwanzo ya Paulo (kama vile 1 Kor. 11:4-5; 12:28, 29;13:2, 8, 8,9; 14:1 3,4,5,6,22,24,29,31,32,37,39; Efe. 2:20; 3:5; 4:11; 1 The. 5:20) na wametajwa katika *Didache* (iliyoandikwa katika karne ya mwisho au karne ya pili tarehe haijulikani) na wakati wa mienendo ya Kikristo ya karne ya pili na tatu katika Afrika ya kaskazini.

IV. Je karama za Agano Jipya zimekoma?

A. Swali ni gumu kulijibu. Linasaidia kufafanua jambo kwa kuelezea kusudi la karama. Je wanamaanisha kuthibitisha mafundisho ya awali ya kuhubiri injili au ni njia endelevu ya kanisa kujihudumia lenyewe kwenye ulimwengu ulipotea?

B. Je mmoja aweza kuangalia kwenye historia ya kanisa kujibu maswali au Agano Jipya lenyewe? Hakuna kiashirio chochote kinachoonyesha katika Agano Jipya kuwa karama za

rohoni zilikuwa za muda tu. Wale wote wanaojaribu kutumia 1 Kor 13:8-13 kuelezea habari hii wanatukanisha kusudi la mwandishi wa aya hii, ambayo inadokeza kuwa kila kitu kitatoweka isipokuwa upendo.

C. Nathubutu kusema kuwa tangu Agano Jipya, si historia ya kanisa, ndiyo yenye mamlaka, waamini wanapaswa kuthibitisha kuwa karama zinaendelea. Hata hivyo ninaamini kuwa mila zinaathiri tafsiri za maandiko. Baadhi ya maandiko yalioko wazi hayatumiki tena (yaani busu takatifu, Baibui, makanisa kukutana nyumbani n.k). kama mila zinaathiri maandiko, hivyo kwa vipi zisiathiri historia ya kanisa?

D. Hili ni swali ambalo haliwezi kujibiwa. Baadhi ya waumini wanatetea kuwepo na“ukoma” na wengine watetea “kusiwepo na ukomo”. Katika eneo hili, kama ilivyo kwa mambo mengi yaliyo fasiliwa, moyo wa mwamini unabaki kuwa ndo kiini. Agano jipya ni tata na la kitamaduni zaidi. Ugumu unaweza kuamua ni maandiko yapi yanaathiliwa na mila/historia na yapi yanaathiriwa kwa wakati wote na yapi kwa mila (kama vile Fee na Stuart, *How to read the Bible for all its Worth,* kur. 14-19 na 69-77 hapa ndipo pale mjadala wa uhuru na kuwajibika, unaopatikana katika Warumi 14:1-15, 13 na Kor. 8-10 unapokuwa wenye umuhimu mkubwa. Namna tunavyojibu swali ni muhimu katika njia mbili.

1. Kila mwamini anapaswa kutembea katika imani yake kwa mwanga walio nao. Mungu anaona mioyo yetu na nia.
2. Kila mwamini yampasa aruhusu waamini wengine kutembea katika uelewa wa imani. Lazima pawepo na uvumilivu ndani ya mipaka ya kibiblia. Mungu anatutaka tupendane kama anavyotupenda.

E. Kwa kuhitimisha suala hili, Ukristo ni maisha ya imani na upendo, na sio tu thiolojia kamili. Uhusiano wetu na Yeye unaosababisha kuwepo na uhusiano na wengine ni muhimu zaidi kuliko habari au imani kamili.

◙ **“kwa Kadri ya imani”** Hii inahusiana moja kwa moja na mstari wa 3, “Kwa vile Mungu amegawa kwa kila mtu kipimo cha imani” (kama vile Efe. 4:7). Inahusiana pia kwa kiasi kikubwa na jinsi waumini wanavyotumia karama zao. Hii inategemeana na tabia, msukumo na juhudi za waumini katika kutenda kila moja na huduma yake aliyopewa na Mungu, ambayo kimsingi ni tunda la Roho, kama yalivyoorodheshwa katika Gal. 2:22-23.

**12:7**
**NASB** **“ikiwa huduma”**
**NKJV, NRSV** **“au huduma, hebu tuitumie katika huduma zetu”**
**TEV** **“kama ni kuhudumu, yatupasa tuhudumu”**
**NJB** **“kama utawala, basi itumie kwa utawala”**

Ukalimani wa kisasa unatofautiana kwa sababu hakuna neno maalumu la kiingereza lenye kulingana na neno hili la Kiyunani (*diakonia*). Linaweza kumaanisha (1) huduma kwa vitendo au (2) utawala (kama vile Mdo. 6:1; 1Kor. 12:5,28).T*he analytical Greek Lexicon Revised By Harold Moulton)* iliyotafasiriwa na Harold K Moulton, inafasiri neno hili kama “kazi, huduma, au ofisi” katika Rum. 12:7; 1 Kor.12:5; Kol.4:17; 2 Tim. 4:5 (uk, 92). Mtazamo wa mazingira haya ni kwa jinsi gani ya kuwasaidia waumini wengine.

◙ **“waalimu…ufundishaji”** Kipaji hiki (*didaskō*) kimeorodheshwa katika 1 Kor. 12:28 na 14:26. Inahusiana na manabii katika Mdo. 13:1 na wachungaji katika Efe. 4:11. Kanisa la kwanza liliona haya kama watu waliopata vipaji wakifanya kazi kwa kuvioanisha. Mahubiri, utabiri, kutoa injili; na kufundisha, vyote vinatangaza injili lakini kwa msisitizo tofauti na mbinu tofauti.

**12:8 “mwenye kukirimu…akirimu”** Neno hili (*parakaleō*) linahusiana na kufundisha (kama vile 1 Tim. 4:13). Bila shaka ni ujuzi ambao unatumika kuonyesha ukweli kwa maisha. Kisha pia ungehusiana na Efe. 4:15, 16 “kusema ukweli katika upendo…mwili ukijijenga wenyewe katika upendo.

◙**"yeye atoaye kwa ukarimu"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUM: WEMA/UAMINIFU (*haplotēs*)**

Neno hili (*haplotēs*) lina vidokezo viwili, "wema" au "uaminifu." Ni sitiari iliyohusiana na maono. Katika Agano la Kale jicho lilitumika kama sitiari kwa ajili ya kusudi katika njia mbili.

1. Jicho baya (bahili, kama vile Kumb. 15:9 na Mith. 23:6; 28:22)
2. Jicho jema (wema, kama vile Mith. 22:9)

Yesu alifuatisha matumizi haya (kama vile Mt. 6:22-23; 20:15).
Paulo alilitumia neno hili kwa maana mbili.

1. "urahisi, uaminifu, usafi" (kama vile 2 Kor. 1:12; 11:3; Efe. 6:5; Kol. 3:22)
2. "ukarimu" (kama vile Rum. 12:8; 2 Kor. 8:2; 9:11,13)

◙**"mwenye kusimamia kwa bidii"** Hii inamaanisha uongozi wa kikristo aidha pale alipo au katika ziara.

◙**"mwenye kurehemu kwa furaha"** Hii inamaanisha kuwasaidia wagonjwa na wahitaji. Haipaswi kuwepo tofauti kati ya mafundisho ya imani na masuala ya kijamii kwa jamii ya wanaoamini. Ni pande mbili za sarafu. "Hakuna injili ya kijamii." Ni injili tu!

## MASWALI YA MJADALA KWA MISTARI 1-8

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni nini kinachohusika katika kuwasilisha mwili wako kama sadaka iliyo hai (mstari 1)?
2. Je, kila muumini anacho kipaji cha kiroho (mistari ya 3-8; 1 Kor. 12:7)? Kama ndivyo, je anachukua kile wanachotaka?
3. Nini lengo la kipaji cha kiroho?
4. Je, kuna orodha ndefu ya vipaji vya kiroho?
5. Mtu anatambuaje kipawa chake?

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI 9-21

A. Sehemu hii ingestahili kupewa kichwa cha habari "Mwongozo wa Kikristo, kwa mahusiano baina ya watu." Huu ni mjadala wa upendo kwa vitendo (kama vile Mt. 5-7; 1 Kor. 13 na 1 Yoh. 3:18; 4:7-21).

B. Sura ya 12 ya Warumi inafanana kimaudhui na muundo na 1 Wakorintho 12-13. Mara tu baada ya mjadala wa vipaji vya kiroho, linafuata onyo kuhusu majivuno na msisitizo katika mtindo wa maisha na mapenzi kwa vitendo.

C. Mazingira haya yanashughulika na
   1. Uhusiano wetu na Wakristo wengine (kama vile 12:9-13). Hii pia imejadiliwa kwa kina katika 14:1-15:13 na katika 1 Kor. 8:11 na kuendelea; 10:23-33)
   2. Uhusiano wetu na wasio waamini au hata inawezekana na wakristo wengine ambao miongoni mwao wana migogoro (kama vile 12:14-21). Sehemu hii inaonekana kuakisi mahubiri ya Yesu katika mlima (kama vile Mt. 5-7).
   3. Mgawanyo huu katika habari hii kwa kiasi fulani siyo halisi (batili) kwa sababu, maneno haya (mahusiano) yanaingiliana.

D. Habari hii imetawaliwa na amri zinazo endelea za mitindo ya maisha (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, kama vile mst 4[mara tatu], 16, 20 [mara mbili] 21[mara mbili] na kwa KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO- uliotumika kwa namna ya amri mara kumi na saba). Wokovu ni zawadi au kipaji cha bure cha neema ya Mungu kupitia kazi iliyokamilishwa ya Kristo na kilio cha Roho; lakini mara tu kikipelekana, na gharama ya kila kitu katika maisha! Kumwita Yesu "Bwana" sio neno mbadala (kama vile Lk. 6: 46)

E. Sura hii pia ina KAULI ZINAZOENDELEA ZA WAKATI ULIOPO zilizotumika kwa hali ya KUSHURUTISHA zikiwa na KIAMBATA HASI ambacho kina maanisha kusitisha kitendo ambacho tayari kinaendelea. Mist. ya 14, 16 (mara mbili), 17, 19 na 21. Wakristo walikuwa tayari wanaishi nje ya mipaka. Kwa maana moja, dhambi inaweza kufasiliwa kama kuchukuwa vipaji vya Mungu nje ya mipaka ulipotakiwa kuishi.

F. Ukristo sharti uwe "wazi" fika wazi, mikono wazi, mioyo wazi na milango wazi (ukarimu) kama vile Yakobo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:9-13**
**9mwingine imani katika Roho yeye Yule; na mwingi karama za uponyaji katika Roho Yule mmoja; 10 na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua Roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; 11lakini kazi hizo zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye Yule, akimugawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye. 12Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, na navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo. 13Kwa maana katika Roho mmoja sisisote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.**

**12:9 "pendo na lisiwe na unafiki"** Katika maandiko ya Kiyunani, hapakuwa na kiungo cha maneno yanayounganisha (*asyndeton*) katika mazingira haya ambalo lilikuwa siyo jambo la kawaida kwa Wayunani wa Koine. Inaweza kuakisi namna fasaha ya Kiebrania nyuma ya ibada ya kubarikiwa kwa Kristo ya Mathayo 5. Namna hii ya fasihi ingeweza kusisitiza kila moja ya fungu hili kama ukweli uliosimama pekee.

"Unafiki" lilikuwa ni neno la kisanii lililomaanisha "kusema nyuma ya pazia." Upendo hauwezi kuwa mchezo wa kuigiza au kughushi (kama vile 2 Kor. 6:6). Upendo ndiyo sifa/tabia ya waumini (kama vile Yoh. 13:34-35; 15:12,17; 1 Yn. 3:11,18; 4:7-21) kwa sababu ndiyo tabia ya Mungu.

◙ **"lichukieni lililo ovu"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO uliotumika kama KUSHURUTISHA. Waumini wanahitaji kushangazwa na kuchukizwa na maovu (kama vile 1 The. 5:21-22). Daima tunashangazwa na matokeo ambayo yana athari ya moja kwa moja kwa maisha <u>yetu</u>.

◙
**NASB, NKJV "kumbatieni lililo jema"**
**NRSV "zingatieni jema"**
**TEV "shikilieni kilicho chema"**
**NJB "zingatieni kwa kilicho chema"**

Hiki ni KITENZI TENDEWA CHA WAKATI ULIOPO (lakini umetumika katika maana ya KATI) na limetumika namna ya KUSHURUTISHA "iliyounganishwa kwenye" (kama vile Maandiko ya kale ya Mwa. 2:24; Mt. 8:29 na pia Flp. 4:8; 1 The. 5:21-22). Tazama umuhimu wa maarifa na kupambana!

**12:10**
**NASB, NKJV "jitoeni ninyi kwa ninyi kwa pendo la kindugu"**
**NKJV "kwa upendo wa udugu, pendaneni ninyi kwa ninyi"**

**NRSV** **"pendaneni kwa pendo la udugu"**
**TEV** **"Pendaneni kwa dhati kama Wakristo"**
**NJB** **"Pendaneni kadri muwezavyo kama ndugu wapaswavyo"**

Hili lilikuwa neno lililoungana la Kiyunani (*phileo + storge*) likiunganisha "upendo wa kindugu na upendo wa kifamilia", na linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Wakristo ni familia moja. Tunaamriwa kupendana (kama vile 1 The.4:9).

Hili ni la kwanza katika mfululizo wa VIPINDI yaliyowekwa ya kwanza katika sentensi za Kiyunani kwa kusisitiza.

◙
**NASB** **"Pendaneni kwa heshima"**
**NKJV** **"kwa heshima pendaneni"**
**NRSV** **"kila mmoja amfikirie mwenzake kwa heshima"**
**TEV** **"kuwa na shauku ya kuonyesha heshima kwa mwenzako"**
**NJB** **"kuwa na heshima ya dhati kwa mwenzako"**

Hiki ni KITENZI CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO (tetezi) ENDELEVU. Kimetumika kwa maana ya KUSHURUTISHA. Waumini lazima watendee wenzao wa agano kama wa maana zaidi kuliko wao wenyewe (kama vile Efe. 4:2; Flp. 2:3).

**12:11**
**NASB** **"kwa bidii, si walegevu"**
**NKJV** **"msilegee katika bidii"**
**NRSV** **"msilegee katika moyo"**
**TEV** **"fanya kazi kwa bidii, usiwe mvivu"**
**NJB** **"mkiwa na juhudi kumtumikia Bwana"**

Upendo wa kweli huzaa nguvu/nishati (kama vile Gal. 6:9).

◙
**NASB, NKJV** **"mkiwa na juhudi katika roho"**
**NRSV** **"muwe wachangamfu katika roho"**
**TEV** **"mkiwa na moyo wa kujitoa"**
**NJB** **"mkiwa na dhamira kubwa katika roho"**

Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kiliochotumika kwa namna ya KUSHURUTISHA. Kwa lugha rahisi "kuchemsha." Hii ingeweza kumaanisha kuamsha upya roho ya mwanadamu au Roho Mtakatifu aishie ndani (RSV, kama vile Mdo. 18:25; Ufu. 3:15-16).

◙**"mkimtumikia Bwana"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO chenye namna ya KUSHURUTISHA. Kuna utofauti wa kimaandishi hapa. Baadhi ya familia za kimagharibi za maandishi ya Kiyunani (MSS D*[,3], F, na G) yaliyosomwa "kwa wakati" (*kairos*) badala ya "katika Bwana" (*kurios*). Utofauti ungesisitiza kumtumikia Bwana na kanisa lake kadri fursa zinavyojitokeza (kama vile Yoh. 9:4; Efe. 5:16). Kwa namna moja au nyingine, mkanganyiko ulitokea kwa sababu *kurios* haikueleweka au ilisomwa kwa makosa. Maandiko sahihi na ya zamani ya Wayunani $P^{46}$, א, A, na B yana "kumtumikia Bwana." $UBS^4$ inaipa "Bwana" kama "hakika"alama (A).

**12:12 "mkifurahi katika tumaini"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika katika hali ya KUSHURUTISHA.
Neno "matumaini" lilitumiwa daima kwa kuunganika na Ujio wa Pili (kama vile 5:2; 8:24; 15:13; 1 The. 5:8). Haina maana ya Kingereza kutumaini kitu, bali katika maana ya Agano Jipya ya tukio Fulani, lakini ikiendelea na suala kubwa la muda. Tazama nukuu kamili katika 4:18 na 5:2.

◙**"mkisitahimili"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika kwa namna ya KUSHURUTISHA. Neno lina maana "kutenda kwa juhudi, kujitolea au hiari, mwendo usiobadilika"

◙ **"katika dhiki kuu"** Kama katika 5:3,5 "tumaini" liliunganishwa na dhiki (*thlipsis*). Hii ni kawaida kwa wafuasi wa Kristo katika ulimwengu ulioanguka (kama vile Mt.5:10-12; Yoh. 16:1-3; 17:14; Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; 2 Kor. 4:16-18; 6:3-10; 11:23-30; Flp. 1:29; 1 The. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yak. 1:2-4; 1 Pet. 4:12-16). Hatupaswi kuitafuta, wala kuikataa! Tazama Mada Maalum: Dhiki katika 5:3.

◙ **"mkidumu katika kusali"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO. Lilitumika kwa namna ya KUSHURUTISHA. Maombi ni nidhamu ya kiroho na kipawa kinachotambua mkono wa utendaji/uumbaji wa Mungu katika historia. Waumini wanaweza kumwathiri mpendwa Baba wa Mbinguni. Mungu amechagua kujishughulisha tu, na maombi kwa watoto wake (kama vile Mdo. 1:14; 2:42; 6:4; Efe. 6:18-19; Kol. 4:2). Hii inafanya maombi kuwa ni wajibu. Tazama *Three Crucial Questions about Spiritual Warfare* kilichoandikwa na Clinton Arnold, uk. 43-44, 187-188.

**12:13**
**NASB, NRSV "mkisaidia katika mahitaji ya watakatifu"**
**NKJV "mkichangia katika mahitaji ya watakatifu"**
**TEV "mkigawana vilivyo vyenu na wahitaji katika Kristo"**
**NJB "wasaidieni watu wa Mungu katika mahitaji"**

Kitenzi cha Kiyunani *koinōneō* kinamaanisha "ushirika pamoja na." Neno hili lina maana nyingi kwa Paulo. Inajumuisha undugu katika Injili na mahitaji ya mwili (kama vile Gal. 6:6). Inatumia hata na kugawa mateso ya Kristo (kama vile Flp. 3:8-10; 1 Pet. 4:13) na ya Paulo (kama vile Flp. 4:14). Kuunganishwa na Kristo kulimaanisha, kuunganishwa na watu wake katika ngazi zote! Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika 1:7. Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika kwa maana ya K. (kama vile Mit. 3:27; Gal. 6:10). Waumini wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kwamba wapate ziada kwa wengine katika jina la Yesu (kama vile 2 Kor. 8:11-12; Efe. 4:28)

## MADA MAALUM: *KOINŌNIA* (USHIRIKA)

Neno "ushirika" (*koinōnia*) unamaanisha

1. Ushirika wa karibu na mtu
   a. na Mwana (kama vile 1 Kor 1:9; 1 Yohana 1:6)
   b. na Roho (kama vile. 2 Kor. 13:14; Flp. 2:1)
   c. na Baba na Mwana (kama vile. 1 Yohana 1:3)
   d. na ndugu wa agano wa kiume/kike (kama vile. Matendo 2:42; 2 Kor. 8:23; Gal. 2:9; Filemoni mst. 17; 1 Yohana 1:3,7)
   e. usio na uovu (kama vile. 2 Kor. 6:14)
2. ushirika wa karibu na vitu ama makundi
   a. na injili (kama vile Flp. 1:5; Filemoni mst. 6)
   b. na damu ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:16)
   c. usio na giza (kama vile 2 Kor. 6:14)
   d. na mateso (kama vile 2 Kor. 1:7; Flp. 3:10; 4:14; 1 Pet. 4:13)
3. Zawadi ama changizo zilizotolewa kwa mtindo wa ukarimu (kama vile Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 8:4; 9:13; Flp. 4:15; Ebr. 13:16)
4. Kipawa cha Mungu cha neema, kupitia Kristo kinachorejesha ushirika wa mwanadamu na yeye na ndugu zake wa kiume na kike

Hii inatangaza uhusiano wa ulalo (mwanadamu kwa mwanadamu) ambao unaletwa kwa uhusiano wa kweli (mwanadamu na muumbaji). Pia unasisitiza hitaji na furaha ya jumuiya ya Kikristo (yaani, Ebr. 10:25).

◙ **"mkifuata ukarimu"** Huki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO KIliochotumika kwa namna ya KUSHURUTISHA. Kwa lugha rahisi ni "kuendeleza wema" (tazama nukuu katika 14:19, kama vile 1 Tim. 3:2; Tito 1:8; Ebr. 13:2; 1 Pet. 4:9). Huduma hii ilikuwa muhimu sana katika kanisa la kwanza kwa sababu ya sifa mbaya ya maovu ya "nyumba za wageni." Hii kimsingi ilimaanisha kuwapa nyumba (makazi) na kuwalisha wahudumu wa ki-Kristo walioendesha huduma za kiziara toka sehemu moja kwenda nyingine.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 12:14-21**

**14Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali vingi. 15Mguu ukisema, kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Sisi wa mwili kwa sababu hiyo? 16Na sikio likisema, kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? 17Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? 18 Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. 19Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? 20Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja. 21Na jicho haliwezi kuuambia mkono, sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu,sina haja na ninyi.**

**12:14 "wabarikini wanaowaudhi"** Hiki ni KITENZI TENDAJI SHURUTISHI CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika mara mbili katika mstari huu. Tunapata neno la kingereza "neno la kusifu" kutokana na neno, "bariki" (kama vile Mt. 5:44; Lk. 6:28; 1 Kor. 4:12; Yak. 3:9-12; 1 Pet. 3;9). Katika $P^{46}$ (The Chester Beatty Papyri) na maandiko B (Vaticanus), neno "wewe" limeachwa, ili kufanya maelezo kuwa jumuishi zaidi au, kwa maelezo mengine kuwa maelezo ya jumla zaidi. Kwa neno "shitaki" tazama nukuu katika 14:9.

◙**"wala musilaani"** Hiki ni KITENZI CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO (tetezi) CHENYE KUSHURUTISHA kilicho na KIAMBATA HASI ambacho kinamaanisha kusitisha tendo lililoendelea katika mchakato. Hii inamaanisha kuitwa jina la Mungu katika maombi kwa kulipiza kisasi (sawa na laana ya 1 Kor. 12:3). Hii haimaanishi kukosa utii kwa Mungu (kama vile Efe. 4:29; 1 Pet. 3:9).

**12:15 "furahini pamoja na wafurahiao, lieni pamoja na waliao"** Hivi VITENZIJINA VYA WAKATI ULIOPO viwili vinatumika katika namna ya KUSHURUTISHA. Wakristo ni familia. Waumini hawako katika mashindano, lakini wanapaswa kutendeana katika upendo, kwa sababu ya mazingira katika mistari ya 14-21, pengine inawezekana hii inaashiria mwitikio wa waumini kwa jamii isiyoamini kwa kutumia fursa za kitamaduni au mazingira ya namna hiyo katika kubainisha fursa za kiinjili.

**12:16**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi"** |
| **NRSV** | **"ishini kwa kupatana vema ninyi kwa ninyi"** |
| **TEV** | **"msinie yaliyo makuu"** |
| **NJB** | **"Mtendeeni kila mmoja kwa wema ulio sawa"** |

Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika KUSHURUTISHA (kama vile 15:5; 2 Kor. 13:11; Flp. 2:2). Mstari wa 16 waweza kutazamwa katika uhusiano na mgogoro kati ya

1. Wayahudi wanaoamini na watu wa Mataifa wanaoamini katika Kanisa la Warumi (kama vile 11:13-24)
2. Mgogoro mkongwe kati ya tabaka za kiuchumi
3. Vipaji vinavyotofautiana
4. Tamaduni za kizazi na mtu anavyopendelea

◙**"msinie yaliyo makuu, bali mkubali kushughulishwa na mambo manyonge"** Hiki ni KITENZI TENDAJI SHURUTISHI CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA HASI, kinachomanisha kusisitiza tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Neno "duni" linaweza kuwa JINSIA YA KIUME au TASA. Kama ni TASA basi tafsiri inapaswa kusomeka hivi "pokea/kubali wajibu wa hali ya chini", kama ni JINSIA YA KIUME,"shirikiana na maskini au watu wanyonge."

◙**"msiwe watu wa kujivunia akili katika makadirio yenu"** Hiki ni KITENZI CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO (tetezi) CHENYE KUSHURUTISHA kikiwa na KIAMBATA HASI, kwa kawaida kilimaanisha kusitisha tendo tayari linaloendelea katika mchakato (kama vile Mith. 3:7; Isa. 5:21; 1 Kor. 10:12; Gal. 6:3). Waumini wasifanye kuwa wa hali ya juu au wa maana, miongoni mwao, au wakorofi wenye kudharau jamii isiyoamini.

◙**"msimlipe mtu ovu kwa ovu"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO chenye KIAMBATA HASI, kuonyesha kusitisha tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Ni juu ya Mungu peke yake kuweka mambo yaendelee sawa na siyo waumini (kama vile Mith. 20:22; 24:29; Mt. 5:38-48; Lk. 6:27; 1The. 5:15; 1 Pet. 3:9)

◙**"angaliyeni yaliyo mema machoni pa watu wote".** Hiki ni KITENZI CHA KATI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO kilichotumika KUSHURUTISHA (kama vile 2 Kor. 8:21; 1 The. 5:22; na 1Tim. 3:7). Hili linaweza kuwa limesemwa kabla katika Mithali 3:4 katika maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX). Waumini wanaishi kwa jicho la kuwashawishi wale wasioamini ili waaminio tusifanye cho chote kile kinachoweza kuwakwaza au kuwabigudhi (kama vile 1 Kor. 9:19-23). Hata katika kuhoji makosa ya mtu kwa kina sharti ifanyike kwa upendo.

**12:18** "**Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae na amani na watu wote"**Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA inayochukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudio lake la kiuandishi/kifasihi. Ikifuatiwa na sura inayofuata na KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO, kilichotumika KUSHURUTISHA. Huu sio siku zote kuwa ni uchunguzi wa muumini, bali ufasaha unaoonyesha siku zote inawezekana (kama vile Marko 9:50, 2 Kor. 13:11, 1 The. 5:13).

**12:19 "Msijilipize kisasi"** Hiki ni KITENZI TENDAJI ENDELEVU CHA WAKATI ULIOPO chenye KIAMBATA HASI kilichotumika KUSHURUTISHA ambacho kinamaanisha kusitisha tendo linaloendelea tayari katika mchakato. Mungu ataonyesha jambo hilo siku moja (kama vile Law. 19:18, Kumb. 32:35, Ebr.10:30).

◙ **"Maana imeandikwa"** Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU ELEKEZI ikiwa katika hali ya kinahau yenye kueleza mafundisho yaliyovuviwa. Nahau hii ya uvuvio ni sambamba na "kama Bwana asemavyo" (kama vile 1 Kor. 14:21, 2 Kor. 6:17). Hii ni nukuu kutoka Kumb. 32:35.

◙ **12:20 "Lakini adui yako"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU mbayo inaonesha tegemeo la tendo la wakati ujao. Maadui watakuja!

◙ **"mpalie makaa ya moto kichwani pake"** Huu ni usemi uliokwisha semwa katika Mith. 25: 21-22.Na dharia za tafsiri ni:

1. Hii ilikuwa nahau ya kitamaduni/asili inawezekana kutoka misri iliyomaanisha neema ndiyo njia pekee ya kugeuza adui kuwa rafiki. Bado ni mwitikio wa Mkristo kwa uovu uliojijenga (kama vile Mt. 5: 44).
2. "makaa yanayo waka" inaonekana inawakilisha aibu kwa matendo ya mtu yasiyo sitahili, ambayo kwa wazi kabisa yamebainishwa na upendo na msamaha wa mwenzake/mtu. (kama vile Ambrosiaster, Augustine na Jerome).
3. Orgen na Chrysostom walisema, hii inamaanisha wema wa Mkristo, ambao unasababisha Mungu kutoa hukumu hata mbaya zaidi kwa wasiotubu. (kama vile the *Jerome Biblical Commentary*, juzuu. 2, uk wa 326).

Nadharia zote hapo juu ni kwamba kielelezo halisi ni ufupisho wa maelezo ya Paulo katika mst wa 21

**12:21 "Usishindwe na uovu, bali uushinde uovu kwa wema"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO na KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Mwitikio wetu kwa kutendewa mabaya utaamua na kuonyesha/ akisi, kiwango chetu cha amani na raha iliyo ndani mwetu. Machungu ni saratani ya roho. Waumini yawapasa wayatoe kwa Mungu.

◙ **"Uovu"** Hii ama ni JINSI YA KIUME na hivyo inamaanisha mwenye uovu.(tazama Mada Maalumu katika 16:20), au ingemaanisha TASA hivyo kumaanisha uovu kwa ujumla (kama vile 12:9; 1The. 5:21-22). Huu ndio upana na

maana nyingi zilizo za kawaida katika Agano Jipya. (kama vile Mt 5:37, 6:13, 13:19,28 Yn. 17:15, 2 The. 3:3, 1 Yoh 2:13-14, 3:12, 5:18-19).
Lazima ikumbukwe kuwa, lengo la hii mienendo mipya na vitendo ni uenezaji wa injili.

## MASWALI YA MJADALA KWA MISTARI YA 9-21

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini katika mistari ya 9-21 kuna KAULI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO nyingi zenye VIAMBATA HASI?
2. Orodhesha amri zote kwenye mistari katika safu zinazojitegemea. Ni orodha nzuri, yenye mambo ama ya kuvutia, magumu au ya kushangaza ambayo nitendo, kufanana na Yesu kwa kila siku kunavyofanyika.
3. Kwa nini ni vigumu sana kutambua mistari gani inamaanisha ni vipi Wakristo wanawatendea waumini wengine na ipi inamaanisha wawatendeavyo wasioamini?

# WARUMI 13

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Utii wa sheria za serikali | Kutii serikali za raia | Mkristo na dola | Wajibu kwa mamlaka | Utii kwa mamlaka |
| 13:1-7 | 13:1-7 | 13:1-7 | 13:1-5 | 13:1-7 |
| | | | 13:1-7 | |
| Upendo wa kindugu | Mpende jirani yako | Upendo unatekeleza sheria | Wajibu wa kila mmoja kwa mwingine | Upendo na vita |
| 13:8-10 | 13:8-10 | 13:8-10 | 13:8-10 | 13:8-10 |
| Kukaribia kwa siku ya Kristo | Jiwekekwa Kristo | Kukaribia kwa ujio wa pili wa Kristo | | Wana wa Nuru |
| 13:11-14 | 13:11-14 | 13:11-14 | 13:11-14 | 13:11-13 |
| | | | 13:11-14 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA 1-7

A. Kwa vile sura ya 12 ilishughurika kimsingi naMkristo na waamini wakependwa (mst. 9- 13) na wengine katika jamii (mst. 14- 21) sura 13: 1- 7 inashughulika kimsingi na Mkristo na serikali ya wananchi.
Haya hivyo, hakuna mazingira ya mgawanyiko katika masomo haya. Paulo aliyaona masomo haya kama ainamoja. Hakuna kitakatifu na mgawanyo wa kawaida wa sehemu mbili. Maisha yote ni mali ya Mungu. Waumini ni wachungaji, katika kila eneo. Kiungo kati ya sura hizi mbili kinaweza kuonekana katika 12: 18.

B. Uelewa wa waamini wa nafasi ya serikali ya wananchi umetofautiana.Katika Agano la Kale, serikali ilianzia katika ukoo wa Kaini (kama vile Mwa. 4: 16- 22). Mnara wa Babeli (kama vile Mwa. 11) unahusiana na jaribio la mwanadamu la kuwa na utawala wa utofauti na Mungu. Ukoo katika Israeli ulikusudiwa kuwa utawala wa Mungu kupitia sheria ya imani na kupitia utaratibu chini ya mchungaji (Mfalme), lakini haikufanikiwa kutokana na dhambi ya mwanadamu. Mjadara wa Yesu kuhusu nafasi sahihi ya serikali katika Mt. 22: 21 na Mark 12: 17

ni muhimili/nguzo. Inashangaza kuona kuwa, Paulo hatamkichochote kuhusu maneno ya Yesu katika eneo hili (ingawa mist. 1- 7 na 11 inaonekana kushabihiana na Mt. 22: 15-22 na 39). Kuna majibu sahihi ya serikali kwa ulimwengu ulioanguka uliotolewa na Mungu. Daima mitume walilazimika kushughulika na namna ya kuhusisha raia na dini katika mamlaka.

Inaonekana kuwa ni kazi chanya na hasi kutegemeana na matendo ya mamlaka za watu. Paulo alilindwa na pia alishtakiwana serikali. Hata hivyo katika ufunuo, anaisema serikali kama Kahaba Mkuu. (Ufu. 17)!

Lazima tuisaidie serikali, labda kama itavuruga dhamira zetu zinazoongozwa na Roho au Sheria za kiraia inauwezekano wa vurugu (kama vile 2 The. 2: 6- 7).

C. Somo hili pia linashughulikiwa katika Tito. 3: 1 na 1 Pet. 2: 13- 17.

D. Dini ya Kiyahudi ilikuwa halali kisheria chini ya serikali ya Roma ya karne ya kwanza. Ukristo ulionekana kama sehemu ndani yake kwa miaka mingi (kama vile Matendo. 18: 12- 16). Hii iliweza kupata ulinzi wa serikali kwa misafara ya kimisionari katika miaka ya mwanzo. Kusudio moja la matendo lilikuwa kuonesha kuwa, ukristo haukuwa kipingamizi cha kisiasakwa Roma. Roma ilihakikisha amani ya kimataifa na utulivu *(paxRomana)* kutokana na hilo injili ikaenea (kama vile 1 Tim. 2: 1- 2).

E. Habari hii ipo zaidi kutokana na uzoefu binafsi wa Paulo kuhusu mamlaka hizi. Na inawezekana pia kwamba, sehemu hii ilijumuisha/ilihusishwa kwa sababu
   1. Ya mivutano ndani ya kanisa la Roma kuhusiana na amri za serikali (mf., kuzuia mitambiko ya wayahudi). Hii iliweza kuwa ilisababisha baadhi ya wayahudi kuuhama mji (mf., Aquila na Priscilla, kama vile Matendo. 18: 2).Kwa kutokuwepo kwao, uongozi wa watu wa mataifa ukaendelea.
   2. Ya mivutano katika Roma iliyosababishwa na mafundisho ya injili katika maeneo makubwa ya kiyahudi katika Roma. Mwana historia Suetonius, *Life of Claudius* 25. 2*,*una kumbukumbu kuwa mfalme aliwafukuza Wayahudi kutoka katika mji katika 49 B.K kwasababu ya uasi na fujo nyingi za mara kwa mara zilizosababishwa na "Chrestus." Hii inaweza kuwa ni tofauti ya silabi katika kilatini kwa neno Kristo (Christos).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13: 1-7**
**1 Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu. 2 Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. 3 Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi, wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake; 4 kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure; kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu. 5 Kwa hiyo ni lazima kutii, si kwa sababu ya ile ghadhabu tu, ila kwa sababu ya dhamiri. 6 Kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi kwa kuwa wao ni wahudumu wa Mungu wakidumu katika kazi iyo hiyo. 7 Wapeni wote haki zao; mtu wa kodi, kodi; mtu wa ushuru, ushuru; astahiliye hofu, hofu; astahiliye heshima, heshima.**

**13:1 "Kila mtu aitii"** Hii ni (1) KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikimaanisha, "endelea kujitoa"au (2) KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, "jitoe mwenyewe" (kama vile Tito. 3: 1; 1 Pet. 2: 13). "Kutii" lilikuwa neno la kijeshi liliotumika kuelezea mlolongo wa amri.

Paulo anahutubia waamini wote. Paulo anawasihi kuwa, waamini lazima watiishiane kati yao wenyewe (ama vile Efe. 5: 21).

Katika siku zetu neno kutii linaonekana kama neno hasi. Ni neno linalotoa picha ya unyenyekevu na athari ya uelewa wa ulimwengu wa Mungu na nafasi yetu humo. Yesu ilisemekana alikuwa mtiifu kwa (1) wazazi wake wa

duniani; (kama vile Luka 2:51) na (2) Baba yake wa mbinguni (kama vile 1 Kor.15:28). Yeye ni kiongozi wetu katika eneo hili (tazama mada maalumu: Utii katika 10:3.

◙"**mamlaka iliyo kuu**" Ingawa Paulo alitumia neno hili (*exousia*) katika mazingira mengine ilimaanisha nguvu za kimalaika, hasa kimsingi kimapepo (kama vile 8:38; Kol. 1:16; 2:10, 15; Efe. 1:21; 3:10; 6:12), Hapa mazingira yanahusu mamlaka za kiraia (wananchi) (kama vile 1Kor. 2:6, 8; Tito 3:1; 1 Pet. 2:13). Biblia inaonekana kusema kuwa, pana mamlaka za kimalaika nyuma ya serikali za wanadamu (Danieli 10 na Kumb. 32:8, "wakati yeye aliye juu" alipoyagawa mataifa, alipowatenganisha wana wa Adamu, aliweka mipaka ya mataifa kufuatana na idadi ya malaika wa Mungu. Tazama Oscar Cullman, *Christ and Time* and Hendrikus Berkhof*, Christ and the Powers).* Lakini bado mamlaka zinazotawala zinafanya kazi chini ya Mungu (kama vile mist. ya 1b, 4a, na 6). Tazama Mada Maalumu ifuatayo.

## MADA MAALUM: MAMLAKA (*EXOUSIA*)

I. Matumizi ya Luka – Inatia shauku kuyachunguza matumizi ya Luka ya neno *exousia* (mamlaka, uweza, au haki ya kisheria).
   1. Katika Luka 4:6 Shetani anadai kuwa na uwezo wa kumpa Yesu mamlaka.
   2. Katika Luka 4:32,36 watu wa Kiyahudi walistaajabishwa namna Yesu alivyofundisha, kwa kutumia mamlaka yake binafsi.
   3. Katika Luka 9:1 Aliwapa uweza na mamlaka Mitume Wamke.
   4. Katika Luka 10:19 Aliwapa mamlaka wamisionari wake sabini.
   5. Katka Luka 20:2,8 kiini cha swali la mamlaka ya Yesu kinaulizwa.
   6. Katika Luka 22:53 uovu umeruhusu mamlaka ya kushtumu na kumuua Yesu.

   Ijapokuwa si katika Luka, utangulizi wa injili ya Mathayo kuhusu Agizo Kuu (Mt. 28:18), "nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,"huu ni usemi wa mamlaka yaYesu unaoshangaza.
   Yesu alidai kuwa na mamlaka kwa sababu
   1. maneno ya Mungu yaliyonenwa kwake katika
      a. ubatizo wake (Luka 3:21-22)
      b. kubadilika kwake (Luka 9:35)
   2. utimilifu wa unabii wa Agano la Kale
      a. kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10)
      b. uzao wa Yese (kama vile 2 Samueli 7)
      c. kuzaliwa kwake katika Bethlehemu (kama vile Mika 5:2)
      d. kuzaliwa kwake wakati wa dora ya nne (Rumi) ya Danieli 2
      e. alivyowasaidia maskini, vipofu, wahitaji (Isaya)
   3. kupunga kwake pepo kulifunua uweza wake na mamlaka juu ya Shetani na ufalme wake.
   4. kuwaansha waliolala mauti kulionyesha uweza wake juu ya maisha ya kimwili na mauti.
   5. miujiza yake yote aliufunua uweza wake na mamlaka mpangilio, utofauti, na muonekano.
      a. Asili
      b. Ulishaji
      c. Uponyaji
      d. kumbukumbu za kiakili
      e. uvuaji wa samaki

II. Matumizi ya Paulo ya neno "mamlaka" yalihusiana na wanawake wa ki-Kristo.
   Suala hili la mamlaka pia limejadilikwa katika 1 Wakorintho 11 katika uhusianao wa wanawake kufunika vichwa. Ufuatao ni muundo wa maelezo yangu yalioypo hapa.

**1 Kor. 11:10 "Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani"** Matumizi ya mamlaka katika 1 Wakorintho yanaweza kueleweka katika njia kadhaa. Jambo la msingi (katika muktadha huu) ni "mamlaka" (exousia) gani yanayozungumziwa. Kwanza, lazima ieleweke kwamba neno exousia mara nyingi

lilihusiana na neno dunamis (uweza). Otto Betz ina makala yenye kuvutia kuhusu neno exousia katika New International Dictionary of New Testament Theology, juzuu 2, kr. 606-611. Hapa kuna mifano mitano.

"Sifa zake za Agano la Kale kwamba maneno *exousia* na *dunamis* yote yalihusikana na kazi ya Kristo, matukio ya mpangilio mpya wa nguvu ya umbile la kiulimwengu na kuwawezesha waamini" (uk. 609).

"Hili neno exousia kwa waamini. Mamlaka ya muumini wa ki- Kristo inapatikana katika utawala wa Kristo na kuzivunja nguvu zote. Hili linamaanisha vyote uhuru na huduma" (uk. 611).

"Huyu yuko huru kwa kila kitu (1 Kor. 6:12; 10:23 *exestin*); dai hili, ambalo lilikuwepo tangu awali kupitia kwa wanaushawishi wa kimathehebu huko Korintho, lilipendelewa na Paulo ambaye alilithibitisha kwa usahii kabisat" (uk. 611).

"Katika utendaji, hata hiovyo, uhuru huu usiozuiliwa kinadharia unaongozwa kwa kwa fikra za kile chenye kuwasaidia Wakristo wengine na kusanyiko kama kama kitu kamili cha mtazamo wa ukweli kwamba ukombozi kamili bado unakuja (1 Kor. 6:12; 10:23)" (uk. 611).

"'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*] kwangu mimi,' lakini si mambo yote yenye kusaidia. 'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*],' lakini si mambo yote yenye kujenga. Mtu asiyatafute yaliyo mema tu, bali mema kwa ajili ya jirani yake" (1 Kor. 10:23 na kuendelea). Nukuu iliyo ndani ya nukuuu hizi bila shaka ndio wito wa wa wanasheria huko Korintho. Paulo anawakabili kwa kuukubali ukweli wao, lakini kwa kuonyesha kwamba si ukweli kamili" (uk. 611).

Mara nyingi Paulo anatumia maneno haya mawili ndani ya barua zake kwa kanisa la Korintho.

1. *exousia*, 1 Kor. 7:37; 9:4,5,6,12 (mara mbili),18; 11:10; 2 Kor. 13:10
2. *dunamis*, 1 Kor. 1:18; 2:4,5; 4:19,20; 5:4; 15:24,43; 2 Kor. 4:7; 6:7; 8:3 (mara mbili); 12:9; 13:4 (mara mbili)

Haki na uweza yalikuwa mambo makuu kwa wate wanasheria na wanahaki. Paulo anajaribu kutembea katika mstari uliyonyooka katika ya kingo zote. Katika muktadha huu wanawake wa ki-Kristo wanasisitizwa kuyakubali maagizo ya Mungu ya uumbaji yaliyotolewa (yaani, Kristo-mwanadamu-mwanamke) kwa makusudi ya ufalme wa baadaye. Paulo anaeleza juu ya makubaliano halisi (kama vile Mwa. 1:26-27; 2:18) katika mistari ya 1 Kor. 11:11-12. Hili ni la hatari kithiolojia

1. kutenga mstari mmoja katika muktadha huu
2. kutumia mabadiliko ya mawasiliano ya madhehebu ya kifumo katika suala hili la mahusiano ya wanaume na wanawake/waume kwa wake wa karne ya kwanza kwa kila utamaduni katka kila karne
3. kuukosa ulinganifu wa Paulo baina ya uhuru wa Mkristo na agano la wajibu wa ushirika wa Mkristo.

Wanawake wa ki-Kristo walipata wapi uhuru wa kushiriki kama viongozi katika ibada za kusanyiko (yaani, kanisa la nyumbani)? Hakika si kutoka katika sinagogi. Ni mwelekeo gani wa kiutamaduni utokanao na jamii ya Kirumi ya karne ya kwanza? kwa hakika hililinawezekana na katika mtazamo wangu hili linasaidia kueleza juu ya mitazamo yangu ya sura hii. Hata hivyo, pia inawezwekamna kwamba nguvu ya injili, ujrejesho wa "sura na mfano wa Mungu" halisi uliopotea katika Anguko, hiki ndicho chanzo. Kuna kiwango cha ubora mpya wenye kuogopesha katika maeneo yote ya maisha ya mwanadamu na jamii. Lakini usawa huu unaweza kurudishwa ndani ya bima kwa ajili ya matumizi mabaya binafsi. Upanuzi huu usiofaa ndiyo Paulo anaoujelezae.

F. F. Bruce, Answers to Questions, kwa ujkweli amenisaidia kufikiri kupitia mambo mbalimbali ya kimkanganyiko yalihusu mapokeo ya kanisa la Ukristo wa sasa wa magharibi. Kama ulivyo ufafanuzi wa maandiko matakatifu mara nyingi nimekuwa nikifikiria kwamba wanawake kujifunika ilimaanisha kuonyesha karama ya Mungu (au usawa wa pade mbili wa Mwa. 1:26,27), si mamlaka wa mume wake. Hata hivyo, Nisingeipata tafsri hii miongoni wa vyanzo vya kibiblia nivitumiavyo, hivyo, nilisita kuliweka hili katika maoni au kulihubiri/kulifundisha. Bado nakumbuka msisimko na uhuru niliokuwa nikiusikia wakati F. F. Bruce alipofikiria

kitu kile kile (tazama Answers to Questions, uk. 95). Nafikiri waamini wote wanaitwa, kwa wakati wote, wamekirimiwa kuwa watumishi wa Kristo (kama vile Efe. 4:11-12)!

## MADA MAALUMU: SERIKALI YA KIBINADAMU

I. UTANGULIZI
  A. Ufafanuzi – serikali ni utaratibu wa kibinadamu wenyewe wa kutoa na kulinda kwa maana ya mahitaji (yaani, Mwanzo 4 na 11). Binadamu ni jamii ya viumbe hata kabla ya anguko (kama vile Mwa. 2:18).Familia, makabila, mataifa hutupatia jamii.
  B. Kusudi – Mungu anapendelea kuwa utaratibu wafaaa kwenye utawala huria.
    1. Sheria za Musa, hasa amri kumi za Mungu, ni mapenzi ya Mungu kwa wanadamu katika jamii. Inaleta ulinganifu wa ibada na Maisha.
    2. Hakuna mfumo wa muundo wa serikari unatetewa katika maandiko, ingawa Serikali ya kale ya makasisi wa Israeli ni mfumo tarajiwa wa huko mbinguni. Sio demokrasia wala ubepari ni ukweli wa kibiblia. Wakristo wanapaswa kutenda ipasavyo kwenye mfumo wa serikali yeyote walioikuta. Kusudi la mkristo ni uinjilisti na huduma, sio mapinduzi. Serikali zote ni za mpito
  C. Asili ya serikali ya mwandamu

    1. Romani katholiki wanadai kwamba serikali ya mwanadamu ni hitaji la asili. Aristotle anaonekana kwanza kudai wazo hili. Anasema, “mwanadamu ni mnyama wa kisiasa” na kwa hili alimaanisha kwamba serikali “ipo kwa ajili ya msaada wa maisha mazuri.
    2. Mprotestanti, hasa Martin Luther, anadai kuwa serikali ya mwanadamu ni ya asili toka kwenye anguko. Anaiita “ufalme wa Mungu wa mkono wa Kushoto.” Alisema kuwa “Njia ya Mungu ya kutawala wanadamu wabaya ni kuweka watu wabaya katika utawala.”
    3. Karl Marx anadai kuwa Serikali ndiyo njia ambayo wasomi wachache wanawaweka watu wengi chini ya utawala. Kwa yeye, serikali na dini huwa na jukumu sawa

NYENZO ZA KIBIBLIA
  A. Agano la Kale
    1. Israeli ni mfumo ambao utatumika mbinguni. Katika Israeli ya kale YHWH alikuwa mfalme. Serikali ya makasisi ni neno linalotumika kuelezea utawala wa Mungu wa moja kwa moja (kama vile 1 Sam. 1. 8:4-9).
    2. Utawala wa Mungu katika serikali ya mwanadamu unaweza kuonekana wazi katika kuteuwa kwake.
      a. wafalme wote, Dan. 2:21; 4:17,24-25
      b. Uongozi wa Musa, Dan. 2:44-45
      c. Nebuchadnezar (Babeli mpya), Yer. 27:6; Dan. 5:28
      d. Koreshi II (Uajemi), 2 Kor. 36:22; Ezra 1:1; Isa. 44:28; 45:1
    3. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa watiifu na wenye adabu hata kuvamia na kumiliki serikali…
      a. Danieli 1-4, Nebuchadnezar (Babeli mpya)
      b. Danieli 5, Belshazzar (Babeli mpya)
      c. Danieli 6, Dario (Uajemi)
      d. Ezra na Nehemia (Uajemi)
    4. Kurudishwa kwa Yuda kulikuwa ni kuomba kwa Koreshi na kutawala na uzao wake..
      a. Ezra 6:10; 7:23
      b. Wayahudi walipaswa kuomba kwa mamlaka ya kiraia, Mihnah, Avot. 3:2
  B. Agano Jipya
    1. Yesu alionyesha heshima kwa serikali ya kibinadamu.

a. Mathayo 17:24-27, Yeye alilipa kodi ya hekalu (dini na utawala wa kiraia ulikuwa na maaana ya kuwa mmoja,kama ile. Petro 2. 2:17)
b. Mathayo 22:15-22; Marko 12:13-17; Luka 20:20-26, Alitetea nafasi ya kodi ya kirumi na hivyo mamlaka ya kiraia ya kirujmi.
c. Yohana 19:11, Mungu aliruhusu utawala wa kiraia kufanya kazi.

2. Maneno ya Paulo yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Warumi 13:1-5, waaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa kuwa walianzishwa na Mungu
   b. Warumi 13:6-7, waaminio lazima kulipa kodi na kuheshimu utawala wa kiraia.
   c. Timotheo 1. 2:1-3, waaminio lazima kuomba kwa utawala wa kiraia.
   d. Tito 3:1, waaminio lazima kunyenyekea kwa utawala wa kiraia.
3. Maneno ya Petro yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Matendo 4:1-31; 5:29, Petro na Yohana kabla ya wakuu wa sinagogi (hii inaonyesha kuendelea mbele kibiblia kwa kutokutii kwa raia)
   b. Petro 2. 2:13-17, waaaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa mazuri ya jamii na kwa uinjilisti.
4. Maneno ya Yohana yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Ufunuo 17,uzizi wa Babeli unawakilisha serikali ya wanadamu iliyoandaliwa na kufanya kazi mbali na Mungu.
   b. Ufunuo 18, uzinzi wa Babeli umeharibiwa.

. HITIMISHO

A. Serikali ya mwanadamu (katika ulimwengu ulioanguka) imewekwa na Mungu. Hii sio "haki ya kiungu ya wafalme," bali kazi ya kiungu ya Serikali (yaani, amri sio machafuko). Hakuna mfumo wa mtu unaotetewa juu ya mwingine.
B. Ni wajibu wa dini kwa waaminio kutii na kuomba kwa mamlaka ya kiraia.
C. Ni sawa kwa waaminio kuunga mkono serikali ya wanadamu kwa kodo na mtazamo wa heshima.
D. Serikali ya mwanadamu ni kwa lengo la utaratibu wa kiraia. Wao ni watumishi wa Mungu kwa kazi hii.
E. Serikali ya mwanadamu sio mwisho. Ina kikomo katika mamlaka yake.Waaminio lazima kutenda kwa sababu ya dhamiri zao kwa kukataa mamlaka ya kiraia wakati inapita mipaka yake iliyowekwa na Mungu. Kama Augustino alionyesha katika *The City of God*, sisi ni raia wa falme mbili, moja ya muda na moja ya milele (kama vile. Wafil. 3:20). Tua wajibu kwa wote, lakini ufalme wa Mungu ni mwisho! Kuna yote mwelekeo wa kibinafsi na ushirika katika wajibu wetu kwa Mungu.
F. Tunapaswa kuwatia moyo waminio katika mfumo wa kidemokrasia kushiriki kikamilifu katika mchakato wa serikali na kuutekeleza, wakati ikiwezekana, mafundisho ya maandiko.
G. Mabadiliko ya kijamii lazima kuendelezwa na ubadilishaji wa mtu binafsi. Hakuna tawi halisi la theolojia linalojishughulisha na kifo, hukumu, pepo na jehanam la kudumu katika serikali. Serikali zote za mwanadamu, ingawa lazima na kutumiwa na Mungu, ni maonyesho ya dhambi ya shirika la mwanadamu mbali na Mungu. Dhana hii inaelezewa katika matumizi ya Johannine ya neno "ulimwengu (yaani, Yohana 1. 2:15-17).

◙

**NASB "vyote vilivyopo vimewekwa na Mungu"**
**NKJV "na ile iliyopo imeamriwa na Mungu"**
**NRSV "nao wenye mamlaka wamewekwa na Mungu"**
**TEV "vimewekwa pale na Mungu"**
**NJB "vimeteuliwa na Mungu"**

Hiki ni KITENZI TENDEWA TIMILIFU ENDELEVU CHENYE MAFUMBO. Fasihi yake inakazia uwepo wa Mungu nyuma ya kila mamlaka za wanadamu (kama vile Yohana 19:11; Dan. 2:21; 4:17). Hii haimaanishi "haki ya kiungu

ya wafalme" bali matakwa ya Mungu kwa ajili ya amri. Hii haimaanishi aina Fulani ya serikali, bali serikali yenyewe. Amri ya utawala kwa watu ni bora zaidi kuliko vurugu/ghasia (kama vile mst. 6).

**13:2 "amwasiye mwenye mamlaka"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hii inamaanisha tabia binafsi ya uasi dhidi ya amri na taratibu zilizowekwa kwa maneno rahisi "kuiweka nafsi ya mtu katika upinzani (kama vile Mdo. 18:6; Yakobo. 5:6). Katika Marko. 12:17, Yesu alitamka wazi mipaka ya serikali na kanisa. Katika Matendo 5:25-32 tunaona kinachotokea serikali zinapovuka mipaka yao.

◙**"hushindana…hushindana"** Hii inaonyesha KAULI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZIna KAULI TENDAJI TIMILIFU ENDELEVU. Haya yanazungumzia uasi uliopo au unaoanzishwa. Mungu ameweka amri katika ulimwengu huu ulioanguka (kama vile mist. 4,6). Kupinga amri ni kumpinga Mungu. Labda kama mamlaka za watu zimevuka mipaka uliopewa na Mungu. Ukweli wa swala la kiroho ni kutii au kunyenyekea kwa mamlaka. Anguko la mwanadamu linahitaji utawala binafsi!

◙"**watajipatia hukumu"** KJV inatafasiri "hukumu" kama "laana" Neno hili limeimarika katika maana yake ya kupeleleza tangu miaka ya 161 B.K. NKJV inakalimani neno hili kama "hukumu." Katika mazingira haya neno hili lingemaanisha (1) Hukumu ya Mungu" au (2) Adhabu ya raia/watu (kama vile mst. 4). Watu hawa wanajipa hukumu wenyewe kwa tabia na matendo yao dhidi ya mamlaka (kama vile Yohana. 3: 17- 21).

**13: 3** Tazama maoni yaliyo sambamba katika 1 Pet. 2: 14.

◙ **"wenye mamlaka"** Tazama Mada Maalumu: *Archē* katika 8: 38.

◙ **"mamlaka"** Tazama Mada Maalumu katika 13: 1.

**13: 4 "kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema"** Mamlaka za serikali zinatenda dhidi ya watenda maovu miongoni mwa raia, wakati ambapo muumini amebanwa katika mahusiano yake binafsi, (kama vile 12: 17-19). Martini Lutha, alisema "Njia ya Mungu ya kuwadhibiti watu wabaya ni kuwaweka wabaya hao katika udhibiti."

◙ **"kama"**Hii ni SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA TATU inayomaanisha uwezekano wa tendo lijalo.

◙

**NASB "kwa vile haikutoa upanga bila sababu"**
**NKJV "kwa maana hauchukui upanga bure"**
**NRSV "maana anao kweli uwezo wa kukuadhibu"**
**TEV "nguvu yao ya kuadhibu ni ya kweli"**
**NJB "siyo bure kuwa alama yao ya mamlaka ni upanga"**

Neno "upanga"(*machair*a) linamaanisha aina ya upanga mdogo wa warumi uliyotumika kwa adhabu kubwa (kama vile Mdo. 12: 2; Rum. 8: 35). Habari hii na Matendo 25: 11 inalifanya Agano Jipya kupata msingi kwa adhabu kubwa, wakati Mwa. 9: 6 waziwazi kinasema mtazamo wa Agano la kale, Uoga ni kitendo madhubuti cha kuzuia vurugu!

◙ **"kwa vile ni mtumishi wa Mungu, mlipizi wa visasi"** Neno kwa mlipizi wa visasi (*ekdikos*) limetumika mara kadhaa katika Agano la kale. Linatumika hata katika sehemu ya kwanza ya Walawi. 19: 18. Katika Agano la Kale kama mtu alimwua mwenzake hata kwa bahati mbaya, familiya ya mtu Yule walikuwa na haki ya kufanya ulipizi wa kisasi wa "jicho kwa jicho" (mlipizi kisasi wa damu). Paulo anaonekana kuhusisha desturi ya Agano la kale na mamlaka ya serikali ya kiraia. Katika 1The. 4: 6, Mungu anasemwa kuwa "mlipizi wa kisasi" inayofuata Rum. 12: 19, wote hawa wawili wanamaanisha Kumb. 32: 35 (kama vile Ebr. 10: 30).

**13:5 "ni lazima kutii"** kuna sababu mbili zinazosemwa (1) kuepuka adhabu, au ya Mungu au ya Mamlaka ya serikali za Raia na (2) kwa dhamira ya waumini.

◙ **“kwasababu ya dhamira”** hakuna neno lenye kufanana katika Agano la Kale kwa neno “dhamira” labda kama neno la Kiebrania “titi” litamaanisha ufahamu wa nafsi na shabaha zake. Awali, neno hili la Kiyunani lilimaanisha dhamira kwa kulihusisha na milango ya fahamu ya ndani (kama vile Rum. 2: 15). Paulo anatumia neno hili mara mbili katika majaribio yake katika matendo (yaani 23: 1na 24: 16). Lilimaanisha uelewa wake kuwa hakuweza kuvunja wajibu wowote wa kidini dhidi ya Mungu (kama vile 1 Kor. 4: 4).

Dhamira, ni kukuwa kwa uelewa wa waumini wa matendo yao na sababu katika:

1. Maono ya ulimwengu ya kibiblia
2. Roho aishie ndani
3. Uelewa wa mtindo wa maisha unaozingatia neno la Mungu

Inawezena tu kutokana na mapokeo binafsi ya injili.

**13:6“kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi”** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ingawa kwa muundo, lingeweza kuwa KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile JB). Huu ni mfano mojawapowa wajibu wa mkristokwa mamlaka za serikali za Raia haswa kwa sababumamlaka za serikali ni watumishi wa Mungu (kama vile mst. 1- 2).

**13:7**

**NASB “Watuimizie wote, kwa kile wanacho stahili: kodi; …; ushuru...; hofu……heshima**

**NKJV “Wapeni wote haki zao; kodi…; kodi…; ushuru…; hofu…; heshima”**

**NRSV “Mpeni kila mtu haki yake; -ushuru…;kodi…; heshima…; heshima”**

**TEV “Lipa basi, unachodaiwa, walipe kodi yako binafsi, kodi ya mali zako, na onyesha utii na heshima kwa wote**

**NJB “Lipa kila mtumishi wa serikali alicho na haki kuuliza, kama ni kodi ya kichwa au kupitia katika vitu na toa heshima kwao "**

Hii inaweza kumaanisha makundi mawili tofauti ya mamlaka za raia (kama vile RSV), lakini hasa pengine kilicho maanishwa ni kuwa, wakristo yapasa walipe kodi zote na kuheshimu mamlaka za raia kwa sababu zinafanya kazi kama watumishi wa Mungu (kama vile mist. 1, 4 [mara mbili], 6;Mt. 22: 15- 22).

Maneno mawili, “kodi” na “ushuru” yanatumika hapa kama maneno yaliyosawa (japo TEV inaonyesha utofauti). Kama yatachambuliwa kufuatana na asili yao (maana asilia), ya kwanza inamaanisha kodi inayolipwa na taifa lililoshindwa vita (kama vile Luka. 20: 22) na ya pili, kodi ya kichwa (kama vile Mt. 17: 25; 22: 17, 19).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA WARUMI 13:8–14

A. Inawezekana kuielewa mst. 1-7 kama andiko la pekee linapojitosheleza. Hata hivyo somo la “uajibikaji” katika mst. 7 unaonekana kuendelezwa katika maana tofauti, katika mst 8. Waumini wana wajibu kwa dola waamini pia wanawajibika kwa wanadamu wengine.

B. Mistari 8- 10 Inawazo linaloungana kama ilivyo mst. 11- 14. inaendeleza mjadala kutoka sura ya 12 ya wajibu wa mkristo wa kuwapenda wengine.

C. Matumizi ya Paulo ya amri kumi za Mungu ya Agano la Kale kama muongozo wa kimaadili kwa waamini wa Agano Jipya linaonyesha uhusiano endelevu wa Agano laKale katika maeneo ya kuishi kiungu (utakaso), na sio wokovu (uhalalisho kama vile Wagalatia. 3). Inaonekana kuwa Paulo ameunganisha vyanzo kadhaa kuunda mwongozo wa kimaadili:

   1. maneno ya Yesu
   2. mwongozo wa Roho
   3. Agano la Kale
   4. mafunzo kwa viongozi wa dini
   5. ufahamu wake wa watu wenye fikra kubwa wa Kiyunani (Wavumilivu).

Hii ikabainisha "sheria ya upendo" upendo wa Mungu, upendo kwa wanadamu, huduma kwa Mungu, huduma kwa wanadamu.

D. Mistari ya 11- 14 inaonyesha mambo ya wakati ujao (nyakati za mwisho). Utofauti wa giza na nuru ilikuwa sifa ya fasihi ya Kiyahudi, ikiwemo Magombo ya Bahari ya Chumvi. Ni neno la kawaida pia katika maandiko ya Yohana na Paulo. Muvutano wa neno "Tayari" dhidi ya neno "Bado" wa maisha ya mkristo ni kichochezi cha maisha ya Kimungu. "Enzi mpya" (ufalme wa Mungu) umezinduliwa na mara tu utakamilishwa. Habari hii ni sawa kabisa na 1 The. 5: 1- 11)

E. Mistari ya 13- 14 ilikuwa na athari ya badiliko la maisha kwa Agustino katika nyakati za miaka 386. Baada ya kristo B.K. Anasema, katika maandiko yake ya *Confessions* 8: 29, "Nisinge soma zaidi, wala kuwa na hitaji, la ghafla mwisho wa sentensi hii, mwangaza angavu ulifulika moyo wangu na giza langu lote la mashaka lililoweka.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13: 8-10**
**[8]Msiwiwe na kitu chochote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. [9]Maana kule kusema, usizini, usiue, usiibe, usitamani; na ikiwepo amri nyingine yo yote, inajumulishwa katika neno hili, ya kwamba, mpende jirani yako kama nafsi yako. [10]Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu *wa* sheria.**

**13:8"Msiwiwe na mtu chochote"**Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASIambacho kwa kawaida kinamaanisha kusitisha tendo ambalo liko tayari linaendelea katika mchakato, fungu hilila kusisitiza lina HASI mbili. Hii inaweza kuwa inahusishwa na masuala ya kodi (mist. ya 6- 7). Deni la kifedha daima ni mihemuko na ukame wa kiroho. Kuweni waangalifuna mambo ya ulimwengu. Inawaondolea waumini uwezo wao wa kusaidia visabbishivya Mkristo na misaada binafsi. Hata hivyo mstari huu hauwezi kutumika kama andiko hakiki kwa "yule asiye na mkopo" Biblia inapaswa kutafsiriwa kulingana na nuru yake yenyewe. "Sio gazeti la asubuhi la Kimarekani! Mistari ya 8- 10 inasisitiza kipaumbele cha kupendana sisi kwa sisi (1) kama ndugu wa agano (Mt. 22: 39- 40; Yohana. 13: 34- 35) na (2) kama sisi sote wanadamu (kama vile Mt. 5: 42; Gal. 6: 10).

NIDTT, juzuu.1,uk.668, unafanya uchunguzi ya kuwa KITENZI"wiwa" lina maana mbili.

1. katika injili, limetumika kama "deni"
2. katika barua za Paulo, limetumika kama uajibikaji

Katika andiko hili, Paulo anaonekana kuunganisha vidokezo hizi.

◙ **"isipokuwa kupendana"** Hili ni wazo muhimu la mistari 8-10 (kama vile Yoh. 13:34;15:12; Rum. 12:10; 1 Kor 13; Flp. 2: 3- 4; 1 The. 4: 9; Ebr. 13: 1; 2 Pet. 1: 7; 1 Yoh. 3: 11; 4: 7, 11- 12).

◙ **"kwa maana ampendaye mwenzake"** KITENZI hiki ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO.Hii haimaanishi kutenga au matendo ya upendo wa muda fulani, bali mtindo wa maisha kama pendo la Kristo.

Neno "jirani" kwa lugha rahisi ni "mwingine wa aina tofauti" (*heteros*), japo tofauti kati ya *heteros* na *alls* (lingine la aina hiyo) yalikuwa yanarahisishwa katika lugha ya Wayunani wa Koine. Katika mazingira haya neno hili linaweza kumaanisha kwa mmojawapo wa jirani, katika upana wa neno, kwa mwamini au asiye (Lk. 12:14-21; 10:25-37). Ingawa nukuu toka katika kitabu cha Walawi 19:18 inarejelea agano lingine pacha (Mwisraeli mwenza) Wakristo sharti wapendane kama ndugu na ndugu wa thamaniwaliopotea (kama vile Gal. 6:10). Ukiristo ni familia. Kila mmoja anaishi na anatenda kwa ustawi na ukuwaji wa wote (kama vile 1 Kor. 12: 7)

◙
**NASB, NKJV,**
**NRSV** **"ametimizaSheria"**
**TEV** **"ni utimilifu waSheria"**

**NJB** **"ametekeleza wajibu**"

KITENZI hiki cha kawaida cha Kiyunani (*pleroō*) kinaweza kutafasiliwa katika njia tofauti. Ni KITENZI TENDAJI TIMILIFU CHENYE KUELEKEZA, ambacho kinaweza kutafasiliwa kama "kimekuwapo na kinaendelea kutimizwa." Robrt Hanna, *A Grammatical Aid to the Greek New Testament,* kinanukuu A.T. Robertson anaita "utimilifu usioaminika" (likimaanisha ukweli wa jadi, uliofahamika vizuri na watumiaji wa neno") uk. 28 na limerudiwa katika mst. 10 (kama vile Gal. 5: 14; 6: 2).

**13:9** Ni jambo la kawaida kwa Paulo kutumia sheria ya Musa (Kutoka. 20: 13- 17 au Kumb. 5: 17- 21 na Walawi. 19: 18) katika kuwahamasisha waumini wa agano jipya. Katika Efe. 6: 2- 3, Paulo pia alitumia moja wapo ya amri kumi za Mungu kama njia ya kuwahamasisha wakristo (kama vile 1 Tim. 1: 9- 10). Andiko hili la Agano la kale halikuwa njia ya wokovu, lakini badoni njia ya kudhihirisha nia/ kusudi la Mungu la jinsi gani wanadamu inawabidi kumtendea Mungu na wao kwa wao (kama vile Rum. 15: 4; 1 Kor. 10: 6, 11).

Inawezekana kunukuu kutoka katika Agano la kale, ilikuwa ni njia ya Paulo kuhusisha wote wawili, waumini wa kiyahudi na waumini wa watu wa mataifa katika kanisa la Roma. Matumizi haya ya neno "kutimizwa" pia lilihusishwa na mjadara wa Yesu juu ya sheria katika Mt. 5: 17.

Yamkini, hii inamaanisha sheria kwa jumla, taratibu za jamii, na sio sheria ya Musa haswa (kama vile JB). Hata hivyo, ukwelinikwamba, Paulo, ananukuu kutoka katika Agano la kale, katika mst. wa 9, inaonesha kulejea katika sheria ya Musa. Angalia ni upendo tu, na siyo utunzaji wakanuni za wanadamu, ambayo hasa na kwa ukweli unaweza kutimiza sheria. Tazama Mada Maalumu ifuatayo hapa chini

Law. 19: 18 inatumika katika njia mbili muhimu

1. Yesu anaitumia kwa pamoja na neno *shema* (yaani Kumb. 6: 4- 6) kama majumuisho ya sheria yote (kama vile Mt. 22: 37- 40; Marko 12: 29- 31; Lk. 10: 27).
2. Kwa Paulo inafanya kazi kama majumuisho ya sehemu ya pili ya amri za Mungu (yaani uhusiano wa mtu binafsi na washirika wa agano (kama vile Gal. 5: 14), kufuatia maoni ya Yesu katika Mt. 7: 12 na Lk. 6: 31).

## MADA MAALUMU: MTAZAMO WA PAULO KUIHUSU SHERIA YA MUSA

Ni nzuri na inatoka kwa Mungu (kama vile Rum. 7:12, 16).

A. Si njia ya kuielekea haki na ukubalifu wa Mungu (inaweza hata kuwa laana, kama vile Gal. 3). Tazama Mada Maalumu: Sheria ya Musa na Mkristo.
B. Bado ni mapenzi ya Mungu kwa waaminio kwa sababu ni ufunuo wa Mungu Mwenyewe (mara nyingi Paulo amelinukuu Agano la Kale kuwasadikisha na /au kuwatia moyo waaminio).
C. Waamini wanafahamishwa naAgano la Kale (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 10:6,11), lakini hawaokolewi na Agano la Kale (kama vile Matendo 15; Warumi 4; Wagalatia 3; Waebrania). Inafanya kazi ndani ya utakaso lakini si uthibitisho.
D. Inafanya kazi ndani ya agano jipya ili:
   1. kuonyesha dhambi (kama vile Gal. 3:15-29)
   2. kuwaongoza wanadamu ndani ya jamii waliokombolewa
   3. kumfahamisha Mkristo maamuzi ya kimaadili

Ni mpangilio maalumu unaomulika kithiolojia uliohusiana na Sheria, kutoka katika hali ya kulaaniwa (kama vile Gal. 3:10-13) na badala yake kuwepo baraka za kudumu, jambo ambalo linasababisha tatizo katika kujaribu kuuelewa mtazamo wa Paulo kuihusu Sheria ya Musa. Mwanadamu aliye ndani ya Kristo, James Stewart analionyesha fumbo la fikra na maadiko ya Paulo:

"Kwa kawaida ungetarajia kuwepo kwa mwanadamu anayejiendesha mwenyewe ili kuunda mfumo wa fikra na mafundisho yaliyoimarishwa na kama kitu kisichobadilishwa kama alivyotumia maneno yenye manufaa. Ungetarajia yeye kuulenga usahihi katika kutumia maneno yalioziongoza fikra zake. Ungedai kwamba neno, linapotumiwa na mwandishi wetu katika maana mahususi, linapaswa kuibeba maana hiyo kotekote. Lakini kwa kuangalia muundo huu yakupasa kutomtia moyo Paulo. Matumizi mengi ya maneno yake ni marahisi, si magumu. . . anaandika 'Basi torati ni njema', 'Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani' (kama

vile Rum. 7:12,22) lakini ni dhahiri kwamba kipengele kingine cha *nomos* ndicho kinachomfanya kuzungumza hali hii pengine, 'Kristo alitukomboa katika laana ya torati' (kama vile Gal. 3:13)" (uk. 26).

## MADA MAALUM: TAMBUZI ZA KUTOKA 20:12-17 (AMRI KUMI)

## KUTOKA 20:13, MUUAJI (BDB 953, KB 1283)

I. MUKTADHA

A. Inahitajika kukumbukwa kwamba hata amri zinazooonekana kuwa na asili ya kijamii ni za kidini hasa. Ukuu wa Mungu juu ya uumbaji na ukombozi umefichwa ndani ya amri hizi. Amri ya usiue, katika tazamio sahihi, neno kuhusu sura ya Mungu katika kila mwanadamu na kujali kwa Mungu na uhusika kwa ajili ya maisha ya mwanadamu.

B. Inahitajika kukumbukwa kwamba kila amri inaikisi yajamii imani. Hili zuio linazungumzia juu ya kuuondoa uhai wa mtu katika hali ya jinai la la msingi na kiuhalisia linaweka msukumo wa maisha ya jamii iaminio. Vidokezo vyake ni vipana kama ulivyo ubinadamu!

II. USOMAJI WA NENO WA MANENO MUHIMU

A. "Mauaji"
   1. Hili ni neno adimu (*rasah,* BDB 953, KB 1283) lenye kumaanisha kuuondoa uhai, lililotumika mara 46 atika Agano Jipya. Kuna maneno mengine ya Kiebrania yanayokinzana yaliyotumika mara mara mia moja.

   2. Hili neno (*rasah*) linaonekana kuwa na maana halisi iliyowekewa mipaka na yenye kunuliwa.
      a. Kiuhalisia hili linahusiana na kuundoa uhai wa mwenza wa agano katika sheria, kwa njia iliyokusudiwa, mara nyingi inahusiana na "mkombozi wa udugu wa damu" au "*go'el.*" Matumizi haya yalihusisha mauaji ya kukusudia lakini katika maana ya Tkulipa kisasi kisheria (kama vile Hes. 35:30-34; Law. 24:13-23).Katika ukweli LexTalionis, ya "jicho kwa jicho," (kama vile Mwa. 9:5-6) ilikuwa njia ya kuzuia kisasi. Baadaye, miji ya wakimbizi (Kumb. 4:41; Yosh. 20:3) ilihimarishwa ili kwamba wenza wa agano waliouawa kwa bahati mbaya au walimwua mwanajamii kwa hamaki waweze kuiepuka ghadhabu ya mhanga wa familia.
      b. Baadaye hili neno lilikuja kurejelea juu ya shauku au mtazamo ulio nyuma ya kuuondoa uhai. Hii dhana ya "kudhamiria" inakuwa kuu zaidi! (kama vile Kut. 21:12-14; Hes. 35:11,22; Kumb. 28:24).
      c. Tofauti hii inakuwa ya muhimu sana katika amri hii. Katika muktadha hii inaonekana kuwarejelea wengine tu walio ndani ya jamiii ya agano. Hii inaonekana kuhusiana na mkombozi wa kidugu, ua kisasi cha damu. Hata hivyo, hili neno linatumika katika vifungu vinavyofuatia vyenye kuziakisi Amri Kumi za Mungu, Hosea 4:2 na Yeremia 7:9, Kumrejerea muuaji. Neno hili linahusiana na sheria tu lakini kwa kuielekea shauku. Hii inapanuka kuanzia kwa jirani hadi kwa rafiki.

   3. Neno hili kwa namna fulani linahusiana na mambo yetu ya sasa yahusuyo maadili ya adhabu za kifedha au vita. Wayahudi walikuwa na tatizo la utekelezaji wa kijamii au vita takatifu (au,

wa ajili hiyo, vita isiyo takatifu).

4. Tafsiri iliyo njema ya utamaduni wetu wa sasa ingekuwa "mauaji ya kudhamiria."

## III. TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ya sita, ya saba, na amri ya nane zimeundwa na maneno mawili tu ya Kiebrania. Haya ni mafupi sana na yanaenda moja kwa moja katika hoja.

B. Maisha, kama yalivyo maisha yote, yanahusiana na Mungu. Ni kwa namna gani tunavyowachukulia wengine kunaziakisi fikra zetu kuhusu Mungu.

## IV. UFANANO WA AGANO JIPYA

A. Yesu
1. Upanuzi wa amri hii (kama vile Mt. 5:21-26) unatupa ubobezi sahihi wa mjadala wetu wa sasa kuhusu namna ya kulitumia andiko hili katika siku zetu.
2. Kwa uwazi Yesu alizichukua Amri Kumi za Mungu kutoka katika uhalisia wa matendo na kuziweka katika uhalisia wa shauku. Tupo kama tunavyofikiri! "Awazavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Maisha ya fikra yanahusiana sana na ni muhimu kuliko namna ambavyo huwa tunayachukulia.

B. Yohana
1. 1 Yohana 3:15, hii dhana ya chuki yenye kufanana inafikiriwa kama mauaji inaelezwa.
2. Maneno ya Kiyunani yaliyotumika katika Mathayo 5:21 na kuendelea na 1 Yohana 3:15 ni tofauti lakini maana zake kimsingi ni zile zile.
3. Kitambue kipengele yakini kilicho katika 1 Yohana 4:19-21.

## V. KWELI ZITUMIKAZO

A. Ingawa mauaji yasiyokusudiwa yanaweza kumwepusha mlipa kisasi kwa kukimbilia katika mji wa wakimbizi (kama vile Hesabu 35; Yoshua 20), yampasa huyu kulipa fidia ya kifungo katika mji huo hadi mauti yatakapomkuta Kuhani Mkuu. Matokeo ya tendo lake bado yanabaki pale pale!

B. Ingawa mstari huu hausiani moja kwa moja na tukio kujiua, kama ilivyo ajali huenda tukio hili haliwezi kufikirika kamwe, bado andiko linatoa msingi wa kiroho kuhusu utakaso wa maisha ya mwanadamu na ukuu wa Mungu na makusudi maisha ya mwanadamu kuwa katika sura yake. Andiko hili linazungumza neno lenye nguvu juu ya maisha yetu katika mstari huu!

C. Hata hivyo, andiko hili, halizungumzii juu ya neno la udanganyifu kwa swali letu la sasa la: (1) adhabu ya kifedha au (2) vita. Kwa Israeli, haya hayakuwa mambo maovu kwao. Waisraeli walihusishwa katika matendo yote haya. Bado, bado kanuni ya umuhimu wa maisha ya kufanywa katika sura ya Mungu na chini ya utawala wake ni kweli muhimu katika eneo hili.

D. Andiko hili haliuzungumzii juu ya uhitaji wa neno linalohusu utu na utakaso wa maisha ya mwandamu! Sisi tulio katika jamii iaminiyo tu watumishi, si kwa matendo yetu tu, bali kwa jamii yetu. Zawadi ya maisha ni vyote binafsi na ushirika. Tunawajibika kimwili, kijamii, na matumizi ya kisaikolojia ya miili yetu kama tulivyo kimwili, kisiasa, na kisaikolojia kuwahusu wengine katika jamii yetu. Hasa hili ni la kweli katika utamaduni kama wetu ambapo tunaruhusiwa kuzungumzia hili na, ambapo, hubadili mfumo. Sisi ni walinzi wa ndugu zetu!

## KUTOKA 20:14, UZINZI (BDB 610, KB 658)

I. MUKTADHA

A. Ni dhahiri kwamba amri zinahusiana na heshima ya mtu kwa Mungu ambayo inaonekana katika heshima kwa maisha ya jirani, mke, na mali (kama vile Yer. 5:8). Hili lilithibitishwa na mpangilio tofauti wa amri hizi katika Agano la Kale la Kiebrania.

B. Ufanano wa Kumbukumbu la Torati unaonyesha usahihi wa hii kweli ya kale kwa utamaduni wetu.

C. Kama kuwaheshimu wazazi kulivyoonekana kuwa msingi wa jamii imara, hivyo hivyo, hii ni amri.

D. Amri hii pia inadokeza umiliki wa Mungu na utawala wa tendo la ndoa na maisha ya familia.

II. USOMAJI WA NENO

A. Neno kuu katika andiko hili ni "uzinzi." Ni muhimu kwamba mtu huilielewa neno hili katika mwangaza wa utamaduni wa kale wa Kiebrania.
   1. Neno hili ni tofauti na muktadha unaotokana na Agano la Kale "uasherati" uasherati unahusiana na mtu kuwa na mahusiano ya kiuzinifu huku akiwa katika ndoa. Hili neno “uasherati" linadokeza sehemu zote zlizomo katika ndoa (kama vile Zab. 29:3; 31:3). Tofauti inapotea katika maneno ya Kiyunani ya Agano Jipya.
   2. Huenda hili linaeleza sababu ya msisitizo juu ya maelezo ya ndoa kwa sababu hili linahusiana na umuhimu wa haki za kurithi ambazo zilijumuishwa katika ahadi ya Mungu ya "nchi." Kila miaka 50 (Jubilee) ardhi zote zilitakiwa kurudishwa kwa makabila asilia (ama vile Law. 25:8-17).
   3. Kiutamaduni uasherati ulishutumiwa kabla ya utungaji wa sheria ya Musa (kama vile Mwa. 12:10 na kuendelea; 26:7 na kuendelea; 39:9).
   4. Uasherati ulionekana kama dhambi dhidi ya:
      a. Jirani – Kutoka 20:14; Kumbukumbu la Torati 5:18
      b. Ndoa – Mambo ya Walawi 18:20
      c. Mungu – Mwanzo 20:1-13; 26:7-11
   5. Hii ilkuwa na adhabu ya kifo kwa pande zote mbili:
      a. Mambo ya Walawi 20:10
      b. Kumbukumbu la Torati 22:22-24
      c. Ezekieli 16:40 (tiyari)
      d. Angalizo kali zinazopatikana katika Mithali 1-9

III. UHUSIANO WAKE NA AGANO JIPYA

A. Yesu alitumia Mambo ya Walawi 19:18 kama muhtasari wa Ufunuo wa zamani (kama vile Luka 10:27). Hii inathibitisha kwamba Amri Kumi zinahusiana na kuwatendea kwetu wengine.

B. Yesu anaweda zidisho la amri katika Mathayo 5:28. Anaweka mkazo katika kusudio badala ya kitendo. Wayahudi waliona akili kama kilalio cha nafsi. Kile mtu alichofikiria ndicho kile kilichokuwa (Mith. 23:7). Hii inafanya maneno Kumi yanayokaribia kuwa ngumu kuyatimiza—hili ndilo kusudi! (kama vile Gal. 2:15-3:29).

IV. UTEKELEZAJI WA KISASA

A. Ndoa inawezekana kuwa masimulizi mazuri zaidi ya kisasa ya imani ya muda mrefu ya kujizatiti katika jina la Mungu. Ni nafasi yetu nzuri zaidi kuelewa uhalisia wa dhana za agano la Agano la

Kale (Mal. 2:14). Heshima yetu kwa wenza wetu katika sehemu zote ikijumuisha jinsi ya kujamiiana kibinadamu, kunatusaidia kuelewa dhumuni la mstari huu.

B. Kusimama kwa ndoa na uaminifu, kama heshima kwa wazazi ni nguzo kuu ya nguvu ya kijamii na kuishi muda mrefu.

C. Inahitajika kusisitizwa kwamba kujamiiana kibinadamu ni zawadi kutoka kwa Mungu (kama vile Mwa. 1:27,28; 9:1,7). Lilikuwa ni wazo lake na mapenzi kwa ubinadamu. Miongozo haikusudiwi kukandamiza uhuru wa mwanadamu au furaha bali kutoa baadhi ya miongozo ya kiungu kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka. Mipaka inafunuliwa kwa ajili ya faida zetu za muda mrefu na furaha. Ingawa mwanadamu ametumia vibaya kujamiiana kama walivyofanyia karama zote za Mungu, bado ni msukumo wa nguvu ndani ya mwanadamu ambao lazima uwe chini ya uangalizi wa Mungu na mwongozo.

D. Kujamiiana lazima kulindwa ili kwamba uungu wa nafsi ya mwanadamu (mwanamke au mwanaume) kuheshimiwe kwasababu wameumbwa kwa sura ya Mungu (Mwa. 1:27). Kuanguka kwetu kunalenga kwenye "mimi" ni wazi sana katika eneo hili.

## KUTOKA 20:15, KUIBA (BDB 170, KB 198)

I. TAARIFA ZA JUMLA

A. Kama ilivyo miongozo mingine katika Amri kumi, imani yetu, upendo na heshima kwa Mungu lazima kuonekane katika vipengele vya uungu na maisha yetu ya kawaida ya kila siku. Ni hasira kwa Mungu kujidai kumjua Yeye alafu kumpunja na kumnyonya mwenza wetu wa kiagano (kama vile 1 Yohana 2:7-11; 4:20-21).

B. Amri yake imekusudiwa kusaidia kuweka ushirika wa jamii ya agano. Ubora wa ushirika huu wa kiroho utavuta ulimwengu uliochanganyikiwa kwa Mungu wetu ambalo ndilo kusudi la Maandiko.

C. Kama ilivyo kwa amri zingine zilivyojikita katika umiliki wa Mungu wa maisha yote, ndivyo ilivyo na hili pia! Sisi tu mawakili, sio wamiliki. Msukumo wetu ulioanguka juu ya umiliki wa mali bila gharama uko nyuma ya onyo na katazo hili (kama vile Zab. 50:10-12).

II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

A. Hii ni amri ya tatu katika nusu ya pili ya Amri Kumi ambayo inatengenezwa kwa maneno maweli tu.

B. Kilichofanya upigaji wa marufuku hakipo. Hii mara nyingi inasaidiwa na:
   1. Muktadha wa amri mbili zilizotangulia zinazohusiana na makosa makubwa.
   2. Uwepo wa vifungu vya habari vinavyofanana vyote ikiwa ni haraka (Kut. 21:16) vyenye kujitenga (Kumb. 24:7). Pia angalia Mwanzo 37.

C. Hatahivyo, kifupi pia kinalindwa
   1. imeandikwa kwa uvuvio
   2. inatanua upana wa ujumuishi
   3. Pia kuna kifungu kinachofanana katika muktadha wa ghafla ambacho kinahusiana na kuiba—Kutoka 22:1 na kuendelea (sio kutekwa).
   4. Yesu kwa dhahiri ananukuu kifungu hiki katika rejea ya kuiba (kama vile Mt. 19:18).

D. Wizi pia unashughulikiwa katika Vifungu vingine vya Sheria za Kale lakini siku zote adhabu ni mauti, kukatwa, au kurejesha mara 30.

E. Kuna baadhi ya vifungu vya muhimu ambavyo vinaweka maana na kuelezea kweli hii:
   1. Mambo ya Walawi 19:1-18—"Utakuwa mtakatifu kwa kuwa Mimi Bwana Mungu wako ni Mtakatifu"
      a. Mtindo wetu wa maisha lazima uaksi tabia za familia ya Baba yetu na Mungu wetu

(kama vile Mambo ya Walawi 19:18).

b. Imani yetu lazima iathiri maisha yetu kwa namna zote mbili matendo yetu chanya na makatazo hasi kwa vyote misukumo sahihi iliyo na taarifa njema (kama vile Law. 19:17).

c. Huruma kwa waliokataliwa na wahitaji, Law. 19:9-10, 13, ni muhimu kama kuwakataa jirani zeu katika kuwahudumia, mstari wa 11.

2. Amosi 8:4-7 – Mungu anachukia unyonywaji!
3. Mika 6:6-8 – Mungu anataka maazimio sahihi katika matendo yetu yote. Kwanini hatuibi hilo nalo ni jambo!
4. Kutoka 22:1 na kuendelea – Mara kwa mara ukweli unaokosekana katika mijadala yetu ya kisasa ya wizi ni urejeshwaji! Dhambi siku zote inagharama!

III. UTEKELEZAJI WA KWELI

A. Joy Davidman, C. S. mke wa Lewis, ameandika kitabu kizuri sana juu ya Amri Kumi. Anatafsiri "Usijaribu kupata kitu fulani bila gharama." Huu uhakika unapanua uwanja zadi ya umiliki wa mali. Pia anasema kwamba "mali huwa si dhambi wala haki iliyokataliwa bali ni mkopo, kuaminiwa na Mungu."
B. Kuiba kama dhambi zingine za moyo ulioanguka inashughulikia na moyo mpya (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:26; Efe. 4:28). Inafurahisha namna asili ya zamani ya "kuchukua" zamu katika sili mpya ya "ubia"!
C. Heshima yetu kwa Mungu inaonekana kwa wazi katika heshima yetu kwa wabia wenzetu wa kiagano! Kweli hii inatabiri Amri kumi.
D. Watu walioanguka huiba kwa namna nyingi!

## MASWALI YA MJADALA

1. Ni kwa namna gani mtu mwizi wa kisasa anaiba?
2. Je urejeshwaji unahusiana vipi na toba?
3. Mstari huu ni kwa namna gani unahusiana na mtazamo wa Kibeberu wa mali?

## KUTOKA 20:17, TAMAA (BDB 326, KB 328)

I. UTANGULIZI

A. Inawezekana kuona uhusiano kati ya Amri tano za mwisho kama ifuatavyo:
   1. Namba 6, 7, na 8 inakataza majeraha ya ndugu wa kiagano katika matendo ya wazi.
   2. Namba 9 inakataa majeraha ya ndugu wa kiagano katika lugha.
   3. Namba 10 inakataza majeraha ya ndugu wa kiagano katika mawazo.
B. Ni kweli kwamba tendo la tamaa linamsumbua mtu anayewakwa na tamaa, na sio tama bal jirani. Hatahivyo, inawezekana kwamba amri hii inatarajia kwamba mawazo yataendelea katika matendo.
C. Wengi wanaona amri hii kama dhana ya kipekee inayopatikana tu katika Vifungu vya Sheria ya kale ya Israeli na ambayo haipo katika vifungu vya sheria zingine vya Mashariki ya Karibu ya Kale. Dhana hii mpya ingekuwa katazo la mawazo. Ni kweli kwamba Israel walichukulia mawazo maisha ya wazo kuwa asili ya matendo machafu (kama vile Mith. 23:7; Yak. 1:14-15). Bado mstari huu unaonekana kuhusiana na mawazo ambayo yanaababisha matendo.
Vifungu kadhaa vinatumia neno "tamaa" katika muunganiko na matendo yenye matokeo (kama vile Kumb. 7:25; Yos. 7:21; Mika 2:2).

D. Ikiwa ni kweli kwamba msisitizo unawekwa juu ya kile kinachoorodheshwa kwanza na mwisho, umuhimu wa kweli wa amri hii inaonekana. Kumwabudu Mungu bila kuacha kunaanza kwanza lakini mitazamo yetu na misukumo kuelekea vitu vya ulimwengu huu unaathiri kujitoa kwetu kwa Mungu. Msisitizo huu pacha pia unaonekana katika mahubiri ya Mlimani ya Yesu, Mt. 6:33 —"Bali utafuteni kwanza ufalme na Haki Yake: na mengine (kama vile mistari ya 19-32) mtazidishiwa."

## II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

A. Kutoka 20:17 na Kumb. 5:21, ingawa kimsingi ni yale yale yana tofauti za muhimu:
1. Mke anajumuishwa kwa dhana pana ya "nyumba" au mali ya mtu katika Kut. 20, wakati anawekwa katika kipaumbele kinachoonekana tofauti na sehemu katika Kumb. 5.
2. Kifungu katika Kut. 20 kina neno la Kiebrania "tamaa" ambayo inamaanisha "kutamani kupata," lakini katika Kumb. 5 kuna neno la pili, "shauku" (BDB 16, KB 20), na pia "tamaa." "Tamaa" inazungumzia shauku ambayo imeunganishwa na kitendo cha kupata kitu kilichokusudiwa na shauku "shauku" inaonekana kulenga katika mtazamo pekee.
3. Pia Kut. 20, imeandikwa kwa wana wa Israeli wakati wa kuzagaa kwao jangwani, hapatajwi "shamba" katika orodha za mali, wakati Kumb. 5 inataja upya amri zile zile kwa jamii iliyothabiti katika Nchi ya Ahadi.

B. Neno "tamaa" ni neno la kati kati. Linaweza kurejerea kuwa na shauku ya vitu vyema (kama vile Zab. 19:10; 1 Kor. 12:31).

C. Shauku mbaya ni mzizi wa anguko la shetani, Adamu na Hawa na sisi wengineo wote. Paulo anaweka msisitizo mihangaiko yake ya kushughulikia tama katika Warumi 7:7-8. Kutamani kimsingi ni hali ya kutoridhika na kupoteza tumaini katika kujali kwa Mungu na Utoshelevu.

D. Vifungu vya Agano Jipya kadhaa vinahusiana na tamaa:
1. Tatizo la mwanadamu ni kutoridhika na uchu (kama vile Luka 12:15; 1 Tim. 6:8-10).
2. Kutamani kunajumuishwa katika orodha za Yesu za dhambi zinazotia unajisi (kama vile Marko 7:17-23; 1 Kor. 5:10; Efe. 5:5; Kol. 3:5).

## III. UTEKELEZAJI WA KWELI

A. Majibu ya uchu wa tamaa na kutoridhika ni:
1. Upendo – Rum. 13:8-10
2. Kuridhika – Ebr. 13:5; Flp. 4:11-13 (na kushirikishana, Flp. 4:14)

B. Amri inasema "acha" lakini Kristo anatupa namna ya kuacha! Katika Yeye tunaweza kuyatawala mawazo yetu kwa viwango fulani.

C. Mungu anajua mioyo yetu na akili zetu
1. 1 Nyak. 28:9
2. Mith. 20:27
3. Zab. 139:1,23
4. Yer. 17:10
5. Warumi 8:27
6. Ufunuo 2:23

D. Vitu sio viovu bali vinakuwa vinapokuwa kipaumbele. Vitu si kilele au vya kudumu milele; watu walioumbwa kwa sura ya Mungu ndio! Tamaa huathiri Jamii ya kiagano katika njia za ulaghai na uharibifu!

## IV. MAELEZO YA NYONGEZA KUTOKA KUMBU KUMBU LA TORATI 5:21:

Kumb. 5:21, "hutatamani. . .hutamtamani," kunatumika VITENZI viwili ambavyo vinafanana :

A. "tamaa" – BDB 326, KB 325, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ikimaanisha "shauku kuu" kwa vitu vinavyoshikika, ambavyo inaweza kuwa hasi au chanya. Katika muktadha huu inaweza kusimamiwa, shauku ya kibinafsi ambayo anakuwa nayo ndugu wa agano.

B. "shauku" – BDB 16, KB 20, *Hipthpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ikimanisha "shauku" (kama vile Kumb. 14:26) au "tamaa" (mara kwa mara ina muktadha wa kingono 5:21) kwa ajili ya zaidi na zaidi kwa ajili yangu kwa gharama yoyote (mfano Hes. 11:4; Zab. 106:14; Mith. 13:4; 21:26; 23:3,6; 24:1).

Hii inafanana na tazamo wa ndani wa mtu na misukumo. Ni maelezo ya mwisho kwa amri zingine zote. Hii ni amri pekee ambayo inashughulika na kwanini, sio namna gani. Hii hapa haisemi tu "usifanye" bali "usifikirie hili." Yesu alifundisha kwamba si tu kwamba tusiue, bali pia tusichukie au kuonesha mtazamo ambao unaweza kupelekea katika mauaji. Yesu alichukua amri hii ya mwisho na kuinua zilizobaki kwa kiwango cha makusudio ya ndani na mtazamo kama juu ya matendo yetu ya nje (kama vile Mt. 5:17-48). Kuna tofauti zote katika ulimwengu kwa mtu ambaye haibi kwasababu haimpendezi Mungu na mtu ambaye haibi kwasababu anaogopa kukamatwa. Mmoja anatendea kazi kanuni za Kikristo na mwingine anatendea kazi matakwa yake mwenyewe.

## MASWALI YA MJADALA

1. Kuwakwa na tamaa ni nini?
2. Mtu wa nyakati hizi anatamanije?
3. Je mawazo yetu ni dhambi?
4. Kwanini mawazo yetu ni muhimu sana katika maisha ya Mkristo?
5. Kwanini Amri katika Kut. 20:17 kwa namna fulani ni tofauti na zile katika Kumbu Kumbu la Torati 5:21?

◙**"katika neno hili"** Hii ni rejea kwa amri kumi. Mpangiliao wa kuorodhosha sehemu ya pili ya amri ya kumi inayofuata maandiko B, ya Kiyunani yaliyoitwa "Vaticanus". Ni tofauti kidogo na maandiko ya Waebrania ya kitabu cha Kutoka. 20 na Kumbukumbu 5. Sehemu ya pili ya washirika wa agano ilyoshughulika na Amri za Munguna mahusiano yaWaisraeli waokwa wao kufuatana na uhusiano wao na YHWH.

◙**"na ikiwapo amri nyingine yo yote"**. Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudi lake la uandishi/kifasihi. Kuna amri zingine. Usemi Ulimaanisha. "Kama kuna amri nyingine yoyote ile tofauti na amri za Mungu". Kwa maneno mengine, hii inajumuisha sheria zote za Musa au inawezekana "sheria" zote kwa ujumla.

Kuna utofauti kidogo katika maandiko ya asili ya Kiyunani ya kwamba ni nyingi kiasi gani na kwa utaratibu gani amri hizi zimeorodheshwa. Wayuda wana aina moja ya kuandika nambari; Wakatoliki na Waprotestanti pia wana namna tofauti ya kuandika nambari. Maana ya kifungu hiki haikuathiriwa na utofauti huu, ambavyo ni kweli kwa kadri ya utofauti kadha wa kadha katika maandiko mengi mbalimbali.

◙ **"yamejumuishwa katika neno hili"** Hii ni nukuu kutoka katika Law. 19:18.Ilinukuliwa mara kadhaa katika injili (kama vile Mt. 5:43; 19:19;22:39; Marko 12:31 na Luka 10:27). Yesu anaiita amri kuu ya pili au amri ya kwanza kabisa. Vile vile Ilinukuliwa kutoka katika Gal. 5:14 na Yakobo 2:8. Mtu anapompenda Mungu anapenda pia yale ayapendayo Mungu" (yaani wanadamu walioumbwa kwa mfano wake kama vile Mwa. 1:26-27).

◙ **"MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO"** Waamini sharti wajipende wenyewe kama Mungu awapendavyo kabla hawajawapenda na kuwapokea wengine. Upendo wa dhati wa mtu mwenyewe sio uovu. Ukweli haswa wa sehemu hii unaelezewa wazi – wapende wengine (kama vile mst. 10). Wale ambao wameguswa na utoaji binafsi wa Mungu, upendo wa kujitoa sadaka kuwa utawapenda wengine kama wewe unavyojipenda (kama vile 1 Yohana

3:16). Hii nikiini cha ufanano na Kristo (sura ya Mungu iliyorejeshwa). Uwepo wa aina hii ya upendo hakuna uhitaji wa "sheria."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13: 11-14**
**11*Naam*, tukijua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini. 12Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia; basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. 13Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. 14Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa*zake.***

**13: 11**
**NASB "*fanya* hiki"**
**NKJV "na *fanya* hiki"**
**NRSV "Aidha hiki"**
**TEV "lazima ufanye hiki"**
**NJB "Aidha"**

Hii ni njia ya kuunganisha kile kinachofuata (mist. 11- 14) na kile kilichotangulia (mst. 9- 10). Kuweni watendaji wa neno, na sio wasikilizaji (kama vile Yakobo 1: 22, 23, 25)! Upendo lazima uwekwe katika matendo.

◙ **"tukiujua wakati"** Hii ni KAULI TENDAJI TIMILIFU ENDELEVU. Neno hili kwa wakati (*kairos*) lilitumika kwa maana ya kipindi cha muda maalum, na siyo wakati tu unaofuatana kwa utaratibu wa kawaida (*chromos*). Waaminilazima waishi katika: (1) kurudi mara ya pilikwa Kristo wakati wowote (2) kumekucha kwa enzi mpya.

◙ **"kwamba saa ya kuamka"** Sitiari hii, "wakati"(lilitumika mara kwa mara katika injili ya Yohana), linamaanisha wakati maalumu (sawa na *kairos*) katika mpango wa Mungu wa ukombozi (kama vile 3: 26; 1 Kor. 7: 29; 10: 11; Yakobo 5: 8; 1 Pet. 4: 7; 2 Pet. 3: 9- 13; 1 Yohana 2: 18; Ufu. 1: 3; 22: 10). Linatumika pote wakati wa kusulubiwa kwa Yesu na kurudi kwake.

◙ **"usingizi"** Neno hili linatumika kamastiari ya uadilifu na uzembe wa kiroho, (kama vile Efe. 5: 8- 14; 1 The. 5: 6). Maneno pekee yana maana maalumu katika mazingira maalum. Kuwa mwangalifu wa fasili isiyo nyumbulika. Maneno yoteyana uwezekano wa maana kadhaa (eneo lenye maana za maneno).

◙ "**kwa maana sasa, wokovu wetu u karibu"** Wokovu ndiyo uamuzi wa awali na mchakato (taz.Mada Maalum katika 10: 14). Wokovu hauwezi kukamilika mpaka waaminio wapate miili mipya (kama vile 1 Yohana 3: 2; 1 The. 4: 13- 18; Ebr. 9: 28; 1 Pet. 1: 5). Kithiolojia hii inaitwa "utukufu" (Rum. 8: 30).Ni tumaini la kila kizazi cha Wakristo kutegemea Bwana kurudi katika muda/kipindi cha maisha yake. (kama vile Luka. 21: 28). Paulo hakuwa wa tofauti (kama vile 1 The. 4: 15).

◙**"kuliko tulipoanza kuamini"** Ukristo unaanza na uamuzi (uhalalisho wa papo hapo na utakaso), na lazima utokee mtindo wa maisha ya kiungu (utakaso endelevu, tazama Mada Maalum katika 6: 4) na unaishia katika kufanana na Kristo (utukufu). Yapasa mtu kupokea zawadi ya Mungu katika Kristo (kama vile Yohana 1: 12; 3: 16; Rum. 10: 9- 13). Uamuzi huu wa awali sio mwisho, bali ni mwanzo.

**13:12 "usiku umeendelea sana"** Hii inamaanisha enzi ya sasa ya maovu ambao umeharibiwa (kama vile 1 Kor. 7: 29- 31; 10: 11; Yakobo 5: 8, Efe.5:8, 14; 1 Yohana 4: 7; 2 Yohana 2: 17- 18; Ufu. 1: 3; 22: 10). Tazama Mada Maalum katika 12: 2, Paulo, na hasa Yohana wanatumia tofauti kati ya giza na nuru, kutofautisha, kama ilivyo fanyika katika Magombo ya Bahari ya Chumvi.

◙"**mchana umekaribia"** Hiini KAULI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI. Hizi ni siku za mwisho (kama vile Flp. 4: 5; Yakobo 5: 9). Tumekuwa katika siku za mwisho tangu wakati Yesu alipokuja duniani kama mwanadamu. Watadumu hadi kurudi kwake katika utukufu. Waamini wote tangu karne ya kwanza wameshangazwa kwa kuchelewa kurudi kwa Kristo. Hata hivo, enzi mpya imepambazuka katika Kristo.

Nukuu hii juu ya kukaribia kurudi kwa yesu inachukuliwa kutoka. "Utangulizi wa Msingi" kwa fasiri juu ya Ufunuo.Tazama wavuti katika www.freebiblecommentary.org.

**"MVUTANO WA SITA** (kurudi haraka kwa Kristo dhidi ya kuchelewa kwake *Parousia)*. Waamini wengi wamefundishwa kuwa Yesu atarudi karibuni, ghafula, na bila kutarajiwa (kama vile Mt. 10: 23, 24; 27, 34, 44, Mark. 9: 1; 13: 30). Lakini kizazi cha waumini watalajiao kimekuwa kimepotoka! Kurudi haraka (moja kwa moja) kwa Yesu ni tumaini lenye nguvu lililoahidiwa kwa kila kizazi, lakini ni kwa yule mmoja (na huyo mmoja aliyeteswa). Waamini lazima waishi kana kwamba anakuja kesho, lakini panga na kutekeleza agizo kuu (kama vile Mt. 28: 19- 20) kama akichelewa.

Baadhi ya vifungu katika Injili (kama vile Marko. 13: 10; Luka. 17: 2; 18: 8 na 1 The. na 2 vimezingatia kuchelewa kwa Ujio wa Pili (*Parousia*). Kuna matukio ya kihistoria ambayo lazima yatokee kwanza:

1. kuenezwa injili ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24: 15; Marko. 13: 10.
2. ufunuo wa "mtu mwenye Dhambi" (kama vile Mt. 24: 15; 2 The. 2; Ufu. 13).
3. dhiki kuu (kama vile Mt. 24: 21, 24; Ufu. 13)

Kuna makusudi tata (kama vile Mt. 24: 42- 51, Marko 13: 32- 36)! Ishi Kila siku kana kwamba ndiyo mwisho lakini panga na kujifunza kwa huduma ijayo!"

◙ **"tuyavue…kuzivaa"** Hizi ni KAULI YA KATI TEGEMEZI, ambayo inatoa taarifa ya dharura.Ishara ni "wewe mwenyewe kukaa pembeni…. vaa mara moja yote au kata shauri. Wote Mungu na mwanadamu wako imara katika uhalalisho (toba na imani) na utakaso (maisha ya kiungu). Stiari hii ya kuvishana ni neno la kawaida sana katika maandiko ya Paulo. Waamini yawapasa waondoe nguo zao za kulalia na kuvaa belamu za kivita (kama vile Efe. 4: 22-25; Kol. 3: 10, 12, 14). Sisi ni askari wa Kikristo tunaojiandaa kwa vita ya kila siku ya kiroho (kama vile Efe. 6: 10- 18). Tazama nukuu katika NIDNTT, juzuu ya 1, k k. 315- 316.

◙ **"silaha za nuru"** Yumkini hiki ni kidokezo katika Isa. 59: 17. Waamini sharti waamue kuvaa ngao na silaha za haki (kama vile 2 Kor. 6: 7; 10: 4; Efe. 6: 11, 13; 1 The. 5: 8). Silaha za Munguzinapatikana kwa waaminio lakini inawapasa:

1. kutambua mahitaji yao
2. kutambua utoaji wa Mungu
3. binafsi na kwa maksudi kuzitekeleza katika maisha yao ya kila siku

Binafsi na kwa makusudi kutekeleza katika mawazo na maisha yao ya kila siku. Kuna vita ya kiroho ya kila siku wa kujitoa, utawapenda wengine kwa namna ilele (kama vile 1 Yoh. 3:16). Hiki ndicho kiini cha kufunana na Kristo (kurejeshwa kwa mfano wa Mungu) katika kuwepo kwa aina hii ya upendo hakuna haja ya "sheria"

Hata hivyo, enzi mpya katika Kristo imewaangazia. Taarifa hii ya kukaribia kurudi kwa Yesu imechukuliwa kutoka katika "*Crucia*

4. Tazama Clinton F. Arnold, *Three CrucialQuestions about Spiritual Warfare*.

**13: 13 "na tuenende kwa adabu"** Hii ni KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE UTEGEMEZI, kihalisia, kihalisia "tembea." Hii ilikuwa nahau ya Kiebrania katika mtindo wa maisha (kama vile Efe. 4: 1, 17; 5: 2, 15). Paulo aliitumia zaidi ya mara 33.

Orodha ya dhambi katika mstari huu umeundwa kwa jozi tatu za maneno mawili. Maneno yana maana zinazoingiliana.Inawezekana yakawa na maana sawa. Tazama Mada Maalum: Uovu na Wema katika 1: 28- 32. Maneno haya yanaweza kuhusiana namvutano kati ya Wayahudi waaminio na Watu wa Mataifa katika kanisa la Kirumi. Waumini wapya wa Watu wa Mataifa wanaweza kuwa wanaendeleza (1) baadhi ya tabia zao za kipagani za kuabudu (2) wakitenda kwa majivuno dhidi ya viongozi wa Wayahudi walioamini waliokuwa wakirudi kutoka walikokimbilia kwa sababu ya amri ya Nero aliyepiga marufuku ibada za Kiyahudi katika Roma.

◙ **"si kwa ulafi na ulevi"**Hii ina maanisha matendo ya zinaa iliyounganishwa na mitambiko ya dini ya kipagani na ulevi. Katika orodha ya dhambi za mwili kwenye Gal. 5: 21, maneno haya pia yameorodheshwa sambamba.

◙ **"si kwa ufisadi na uasherati"**Jozi hii inaingiliana na ya kwanza. Neno la pili linatumika kwa mapana katika Agano jipya (kama vile Marko 7: 22; 2 Kor. 12: 21; Gal. 5: 19; Efe. 4:19; 1 Pet. 4: 3; 2 Pet. 2: 7). Kama jozi ya kwanza inazingatia kwenye ulevi, jozi hii inazingatia matendo ya zinaa, hata matamanio yasiodhibitiwa.

◙ **"si kwa ugomvi na wivu"** Maneno haya yanazungumzia magomvi baina ya watu (kama vile Gal. 5: 20). Hii inaweza kuwa imetokana na mwenendo usiofaa wa jozi mbili za kwanza. Kama haya yatasemwa kwa Wakristo (kama vile 1 Kor. 3: 3; Kol. 3: 8), yanaakisi hadi matendo ya dini za kipagani ambayo lazima yaachwe katika maisha ya wakristo. Hata hivyo, katika mazingira haya mstari huu ni kinyume na waumini, Kwa maana hiyo, inapaswa kuwa onyo.

**13:14"Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo"** Neno stiari linahusishwa na vazi takatifu la Mfalme Yesu sasa anawekwa juu ya mabega ya waumini (utakaso wa nafasi).Baadhi ya wasomi wanaona tukio hili kama uongo katika vazi la ubatizo. Sitiari hii ya vazi linatajwa kwa mara ya kwanza katika mst.wa 12. Ni njia ya kuonesha nafasi mpya ya muumini katika Kristo.Pia ilisisitiza ukweli kuwa waamini lazima watekeleze uchaguzi wa mitindo yao mipya ya maisha (utakaso endelevu) kwa sababu ya nafasi yao mpya katika Kristo (kama vile Efe. 4: 22; 24; Kol.3: 8).Katika Gal. 3: 27 ukweli huu unaelezwa kama usemi wa ukweli (ONYESHI); hapa inaelezwa kama SHURUTISHI (KAULI SHURUTISHI YA KATI) amri.

Mvutano huu kati ya usemi wa KITENZI ELEKEZI na SHURUTISHI ni mvutano kati ya nafasi yetu katika Kristo na jitihada zetu za kupata nafasi hiyo (Tazama Mada Maalum katika 6: 4). Sisi ni "watakatifu" (mtakatifu) wakati wa wokovu, lakini tumeonywa kuwa "watakatifu." Hili ni fumbo la kibiblia la wokovu kamili na huru katika Kristo na wito wa parapanda ilikufanana na Kristo.

◙ **"msiuangalie mwili"** Hii ni KITENZI SHURUTISHI CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO chenye KIAMBATA HASI. Namna hii ya ufasihikwa kawaida inamaanisha kusitisha tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Inaonekana kuwa baadhi ya

Wakristo katika Roma walikuwa wakiishi maisha yasiyo adilifu. Hii ingalikuwa ni kuchukua toka katika taratibu zao za kipagani za kuabudu.

Ni vigumu kueleza mafundisho ya Agano Jipya kuhusu Ukristo wa kimwili. Waandishi wa Agano Jipya wanaiweka hali ya wanadamu wazi. Mkristo wa kimwili ni kinyume katika semi. Kwa maendelezo haya, lakini bado niukweli wa maisha ya "utayari" au "yasiyo tayari." Paulo aliwaweka wanadamu katika makundi matatu (1 Kor. 2: 14- 3:1)

1. watu wa asili (wanadamu walio potea), 2: 14
2. watu wa kiroho (wanadanu waliokolewa), 3: 1
3. watu wa mwili (Wakristo wa Kimwili au Wakristo wachanga), 3: 1

◙ **"mwili hata kuwashatamaazake"**Paulo alijua vizuri kabisa hatari inayoendelea ya anguko la asili ya Adamu (kama vile Rum. 7; Efe. 2: 3), lakini Yesu anatupa nguvu na hamu ya kuishi kwa ajili ya Mungu (kama vile Warumi. 6). Ni Pambano linaloendelea (kama vile 8: 5- 7; 1 Yoh. 3: 6- 9). Tazama Mada Maalumu: Mwili (*sarx)* katika 1: 3.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana**.**

1. Kwa nini usemi wa Paulo kuhusu serikali yalikuwa makali sana kwa Wakristo wa mwanzo?
2. Je, yawapasa Wakristo kutii kila aina ya serikali?
3. Je, yawapasa Wakristo kutii kila hitaji la kisheria la serikali?
4. Je, mstari wa 1 unafundisha haki ya kiimani ya wafalme?

5. Je, Paulo anavunja msimamo mpya kithiolojia? au kunamaneno yaliyotendeka nyuma ya Yesu ya namna hii Katika Mt. 22: 21?
6. Je, ukaidiwa raia, unahalalishwa kwa Wakristo (Mdo. 5: 25- 32)?
7. Mstari wa 4 unahusianaje na suala la adhabu kubwa?
8. Je dhamiri ya Mkristo kila marani sahihi (kama vile 5)?
9. Kwa kuzingatia mstari wa 8, je, waumini wasipatevibali?
10. Je, mstari wa 8, unazungumzia upendo wetu kwa Wakristo wengine au kwa watu wote?
11. Kwa nini Paulo anatumia Amri za Mungukama kivutio kwa waamini wa Agano Jipya?
12. Kwa nini Paulo angeorodhesha adhabu hizi za kutisha kwa kuhusisha waamini?
13. Nikwa namna gani mtu “amvae Bwana Yesu Kristo?”

# WARUMI 14

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Usimhukumu ndugu Yako | Sheria ya uhuru | Upendo unaheshimu hisia za wengine | Usihukumu wengine | Misaada kwa wanaojali |
| 14: 1- 12 | 14: 1- 13 | 14: 1- 4 | 14: 1- 4 | 14: 1- 12 |
| | | 14: 5- 6 | 14: 5- 12 | |
| | | 14: 7- 9 | | |
| | | 14: 10- 12 | | |
| Usimkwaze ndugu yako | Sheria ya upendo | | Usiwafanye wengine waanguke | |
| 14:13-23 | | 14:13-23 | 14:13-18 | 14:13-21 |
| | 14:13-23 | | | |
| | | | 14:19-23 | |
| | | | | (14:22-15:6) |
| | | | | 14:22-23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA MISTARI 1-12

A. Sura hii inajaribu kusawazisha utata ulioko katika uhuru wa mkristo na uwajibikaji. Kipengele hiki kinapitia 15: 13.

B. Tatizo lililo jitokeza katika sura hii lilikuwa bila shaka ni mvutano kati ya waumini wa watu wa mataifa na waumini wa Kiyahudi katika kanisa la Roma (au bila shaka uzoefu wa Paulo wa sasa katika Korintho). Kabla ya kubadilika, wayahudi walijitahidi kufuata sheria na wapagani wakaendeleaza tabia zisizo ridhisha jamii.

Kumbuka sura hii inazungumzia wafuasi waaminifu wa Yesu. Sura hii haizungumzii waumini wa dunia (1 Kor. 3: 1). Sababu kubwa kabisa inazungumzia makundi yote mawili. Kuna hatari ya kujikita pande zote. Mjadala huu sio kibali cha kukosoa sheria iliyoaminiwa au uhuru wa kupokea maoni. Kumbuka kuwa Paulo aliandika Warumi akiwa Korinto. Tatizo ni kwamba palikuwa na kikundi fulani cha imani, lakini hapa kuna waumini wa aina mbali mbali

C. Waumini lazima wawe waangalifu kutofanya thiolojia zao au imani za desturi na mila zao kwa waumini wengine (kama vile 2 Kor.10: 12). Waumini wote sharti watembee katika mwanga walionao, lakini kwa kuelewa kuwa thiolojia yao, sio tu thiolojia ya Mungu. Waumini wote bado wanathiriwa na dhambi. Lazima tuwahimize, tuwashawishi na kufudishana kutoka katika mafundisho, sababu na uzoefu lakini siku zote katika upendo. Kadri mtu anavyojua, ndivyo kadri anavyojua kwamba hajui (kama vile 1 Kor.13: 12)!

D. Tabia ya mtu na sababu mbele ya Mungu ni kitu muhimu katika kutathimini matendo ya waumini wengine. wakristo watasimama mbele ya Mungu kuhukumiwa kuhusu namana walivyo tendeana (kama vile mistari 10, 12 na 2 Kor.5: 10).

E. Martin Luther- alisema, “Mkristo ni Bwana aliye huru kuliko wote, asiyewajibika kwa yeyote, mkristo ni mtumishi mwenye wajibu kuliko yeyote, anayewajibika kwa wote. Ukweli wa Biblia daima umeelezwa katika hali ya mvutano kimafumbo.

F. Somo hili gumu lakini nyeti sana linashughulikiwa katika andiko zima la Warumi. 14: 1- 15: 13 na pia katika 1 Kor. 8- 10 na Kol. 2: 8- 23. Kitabu kinachonisaidia katika eneo hili ni Gordon fee & Douglas Stuart *“How to read the Bible for all its worth*- kur.- 75- 86” (Namna ya kusoma Biblia kwa ubora wake/thamani yake yote- uk 75- 86)

G. Hata hivyo panahitajika kusemwa kuwa wingi kwa waumini watiifu Sio kitu kibaya. Kila muumini ana ukamilifu na udhaifu wake. Kila mmoja yampasa atembee katika mwanga alionao, siku zote akiwa wazi kwa Roho na Biblia kwa mwanga zaidi. Katika kipindi hiki cha kuangalia kupitia katika kioo pasipo na mwanga (1 Kor. 13: 8- 13), yampasa mtu atembee katika upendo (mst. 15), na amani (mist. 17, 19) kwa kuimarishana.

H. Sifa za “imara” na “dhaifu” ambazo Paulo anazitoa kwa makundi haya zinatusababishia chuki. Hili lilikuwa kusudi la Paulo. Makudi yote yalikuwa waumini watiifu. Sisi haitubidi kujaribu kuunda wakristo wengine ndani yetu. Kila mmoja ana mkubali mwenzake katika Kristo.

I. Mjadala mzima ungeweza kufupishwa kama ifuatavyo:
   1. Kila mmoja kumkubali mwenzake kwa sababu Mungu anatukubali katika Kristo (kama vile 14: 1, 3; 15: 7);
   2. Mtu asimuhukumu mwenzake kwa sababu Kristo ndiye Bwana na hakimu wetu wa pekee (kama vile 14: 3-12).
   3. Upendo ni kitu cha maana zaidi kuliko uhuru (kama vile 14:13-23).
   4. Fuata mfumo wa Kristo na toa haki kwa wengine kwa wema na kuwaimarisha (kama vile 15: 1-13)**.**

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 14: 1-4**
**[1]Yeye aliye dhaifu wa imani, mkaribisheni, walakini msimuhukumu mawazo yake. [2]Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu hula mboga. [3]Yeye alaye asimdharau huyu asiyekula, wala yeye asiyekula asimhukumu huyo alaye; kwa maana Mungu amemkubali. [4]Wewe u nani unayemhukumu mtumishi wa mwingine? Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka. Naam, atasimamishwa, kwa kuwaBwana aweza kumsimamisha.**

**14: 1**
**NASB "Sasa kubali"**
**NKJV "Pokea**
**NRSV, TEV "Karibu"**
**NJB "Mkaribishe**"

Hiki ni KITENZI SHURUTISHI CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO. Hii ni amri inayoendelea yenye msisitizo katika somo. KIWAKILISHI "wewe"kiko katika KITENZI cha kiyunani, lakini kinatumika katika kiingereza kumaanisha Wakristo"imara" (kama vile 15: 1). Hii inamaanisha makundi mawili katika kanisa la Rumi. Hili lingaliweza kuhusishwa na: (1) mvutano kati ya wayahudi waaminio na watu wa mataifa waaminio (kama vile 15: 7- 21) au (2) kutofautiana kwa aina za nafsi (watu).
Mazingira haya yanahusu waumini wakweli, watiifu; baadhi yao "imara" na wengine"dhaifu" katika imani zao. Imani inatumika hapa katika uelewa wa injili na matokeo yake mapya na kuhusishwa kuwaweka huru.

◙
**NASB, NKJV "yuye aliye dhaifu wa imani"**
**NRSV, TEV "wale walio dhaifu wa imani"**
**NJB "kama imani ya mtu sio thabiti"**

Usemi huu umesisitizwa kwa kuwekwa mbele (yaani kuwekwa wa kwanza katika andiko la kiyunani) kwa maneno rahisi, ni dhaifu katika imani." NJEO YA WAKATI ULIOPO unazingatia ukweli kwamba ni sifa/tabia ya mtindo wa maisha. Hii inamaanisha mtazamo wa fikra kisheria. Muumini makini wa Kikristo anaelezewa katika sura hii kwa njia tatu:
1. Kukataza vyakula (kama vile 14: 2, 6, 21)
2. Mkazo juu ya siku maalum (kama vile 14: 5, 6)
3. Kukataza pombe (kama vile 14: 17, 21)

Mtu wa aina hii alitajwa katika Rum. 15: 1 na 1 Kor.8: 9- 13; 9: 22. Kuwa mwangalifu usijiweke haraka katika kundi la mkristo imara au dhaifu.
Daima waumini ni dhaifu katika eneo moja na imara katika eneo lingine. Tabia ya Paulo kwa masuala haya ni tofauti kabisa katika Gal. 4:9- 10 na Kol. 2:16- 23). Maandiko haya yanaashiria tabia na mafundisho ya waalimu wa uongo. Katika Warumi, hawa ni waumini watiifu ambao wana dhamira makini.
Watoa maoni wengi wanafikiri kuwa wadhaifu katika imani inamaanisha waumini wa Kiyahudi (yaani wasaliti), na msisitizo wao wa kuendelea kuwa watiifu kwa sheria ya Musa kama ilivyofahamika katika mila na desturi za viongozi wa kidini (yaani Talmud). Hili kwa hakika linaingiliana na #1 na #2 katika aya ya 1 lakini sivyo katika #3. Kwa sababu hii nafikiri ni aina nyingine ya tabia ambayo itafaa zaidi katika mazingira haya. Inaweza kumaanisha waumini wa Kiyahudi au watu wa Mataifa ambao mila na desturi zao za nyuma zilikuwa na nguvu za kuyumbisha.

## MADA MAALUM: UDHAIFU

Hapa kunatofauti. Waalimu wa uongo wanajivuna kwa sifa na mitindo yao ya kulaghai, lakini Paulo anajua thamani ya "udhaifu"(*astheneō*). Tazama ni mara ngapi maneno haya (au ya namna tofauti), yametumika katika 1Wakorintho na 2 Wakorintho.

| **majivuno** | **<u>Udhaifu</u>** |
|---|---|
| 1kor. 1: 29, 31 | 1kor. 1: 25, 27 |
| 3: 21 | 2: 3 |
| 4: 7 | 4: 10 |
| 5: 6 | 8: 7, 9, 10, 11, 12 |
| 9: 15, 16 | 9: 22 |
| 2kor. 1: 12, 14 | 11: 30 |
| 5: 12 (x2) | 12: 22 |

| | |
|---|---|
| 7: 4, 14 (x2) | 15: 43 |
| 8: 24 | 2kor. 10: 10 |
| 9: 2, 3 | 11: 21, 29, 30 |
| 10: 8, 13, 15, 16, 17 | 12: 5, 9, 10 (x2) |
| 11: 12, 16, 17, 18, 30 | 13: 3; 4 (x2), 9 |
| 12: 1, 5, 6, 9 | |

Paulo anatumia dhana ya udhaifu katika njia mbalimbali.

1. Udhaifu wa Mungu, 1 Kor. 1: 25
2. Dhaifu katika ulimwengu, 1 Kor. 1: 27
3. Udhaifu wa Paulo na uoga, 1 Kor. 2: 3; 9: 22; 2 Kor. 11: 29, 30; 12: 5.
4. Paulo na kikosi chake cha ujumbe, 1 kor. 4: 10; 2 Kor. 11: 21
5. Muumini dhaifu (kama vile Rum. 14: 1- 15: 13); 1 Kor. 8: 7, 9, 10, 11, 12; 9: 22.
6. Maradhi ya mwili 1 Kor.11: 30.
7. Sehemu ya mwili wa binadamu, 1 Kor.12: 22
8. Umbile la mwili, 1 Kor.15: 43
9. Uwepo wa Paulo kimwili – au ujuzi wake wa maneno ya ulaghai 2 Kor.10: 10
10. Udhaifu wa Paulo ulikuza nguvu ya Mungu 2 Kor. 12: 9, 10; 13: 4, 9
11. Ujumbe wa kristo kupitia kwa Paulo, 2 Kor. 13: 3
12. Umbile la mwili wa Kristo, 2 Kor. 13: 4.

◙

**NASB** **"lakini sio kwa kusudi la kupitisha hukumu juu maoni yake"**
**NKJV** **"lakini sio kubishana juu ya vitu vyenye mashaka"**
**NRSV** **"lakini sio kwa sababu ya kugombana juu maoni**
**TEV** **"lakini msibishane na wao kuhusu maoni yao binafsi"**
**NJB** **"bila kuanzisha ubishi"**

Waumini sharti wawakubali waumini wengine ambao kwa namna moja au nyingine hawakubaliani kuwabadilisha. Hii inataka uhuru wa dhamira kama msingi wa ushirika, na sio usawa uliosababishwa. Waumini wote wamo katika mchakato. Lazima waipe Roho muda wa kufanya kazi na kumuumba kila mmoja katika ukomavu, lakini hata pia katika ukomavu wote hawatakubaliana

**14:2** mlo unaozungumziwa katika mstari huu ni kwa makusudi ya kidini, sio afya. Tatizo hili la chakula liliibuka kutoka vyanzo viwili bila shaka: (1) Sheria ya chakula ya Wayahudi (kama vile Walawi. 11) au (2) Nyama ilitolewa kafara kwa miungu ya wapagani (kama vile 1 Kor. 8- 10). Yesu alishundisha waziwazi kuwa chakula sicho kinachomtia mtu unajisi (kama vile Mt. 15: 10- 20; Marko 7: 14- 23). Ukweli huu umefafanuliwa na maoni ya Petro kuhusu Cornelius katika Mdo. 10.

**14:3 "Yule alaye asimdharau huyu asiye kula"** "usimdharau yeye asiye kula" ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ya neno *ezoutheneō* ikiwa na KIAMBATA HASI ambacho kwa kawaida kinaonesha kusitishwa kwa tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato.
"Usidharau" kwa lugha rahisi ni "kufanya kikose uzito", "ukorofi," au "kukosa thamani." (kama vile 14: 10; Luk. 18: 9; 1 Kor.6: 4; 16:11; 2 Kor. 10: 10, Gal. 4: 14; 1 The. 5: 20). Waumini lazima wajilinde dhidi ya kujiona kuwa wao ni wa maana/bora wenye haki kuliko wenzao. Mwenye nguvu katika imani amsidharau au kumshutumu mdhaifu wa imani.

◙ **"asimhukumu"** Hiki ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO Yenye KIAMBATA HASI Kinachonesha kusitisha tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Wadhaifu katika imani wasipitishe hukumu kwa matendo ya ndungu (kaka/dada) zao wasiokubaliana nao.

◙ **"Kwa maana Mungu amemkubali"** – Hiki ni KAULI TIMILIFU YA KATI ELEKEZI. Neno hili linakalimaniwa kama "kupokea" katika mst 1. Msngi wa waumini kukubali mwenzake ni kwamba Mungu kupitia kwa Kristo (15: 7) amewakubali. Katika mazingira haya mst 3 unazungumzia juu ya wale walio wangarifu zaidi, wakristo walio dhaifu katika imani.

**14: 4 "wewe u nani?"** -Huu ni mkazo katika kiyunani kumaanisha kaka/dada dhaifu.

◙**"Mtumishi"** Hili ni neno *oiketēs*, lililoundwa kutoka kwa neno *oikos*, likimaanisha "nyumba", kwa hiyo huyu ni mtumwa wa nyumbani, au mtumishi (kama vile Luk. 16: 13; Mdo. 10: 7; Rum. 14: 4; 1 Pet. 2: 18). Linatumika katika maana hii katika maandiko ya kale ya Kiyunani (kama vile 9:25; 27:37; 44:16,33; 50:18). Halitumiki kama neno linalo tawala au kuzidi kwa mtumwa au mtumishi katika Agano Jipya ambalo ni *doulos*; lingeweza pia kuashilia watumishi wa nyumbani au watumwa.

Hoja ya Paulo hapa ni kwamba kila muumini ni mtumwa/mtumishi wa Kristo. Ni "Bwana" wao na ni yeye, yeye pekee atawaongoza na kuwawajibisha kwa matendo na mienendo yao (kama vile 2 Kor. 5: 10)

◙ **"Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka"** Katika mazingira haya, Paulo anawazungumzia wenye umakini zaidi/wanaojali zaidi, lakini usemi wenyewe unamaanisha makundi yote mawili. Waumini wangekuwa bora zaidi kama wangeondoa vibanzi katika macho yao wenyewe (kama vile Mt. 7: 1- 15).

◙ **"Naam, atasimamishwa, kwa Bwana wake mwenyewe aweza kumusimamisha"**Hii ilikuwa ahadi ya ajabu (kama vile 5:1-2; Yuda 24-25). Inajumuisha pia ushilikiano baina ya waumini (kama vile 1 Kor.15: 1-2). Tazama mada maalum: simama katika 5:2.

Kuna utofauti hapa katika maandiko ya wayahudi. NKJV, yakifuata maandiko ya kiyunani D, F, G, O48 na O150, sawa na sawa na tafasiri ya Biblia ya Kiratini yana "Mungu" (*theos*), hata hivyo, MSS $P^{46}$, ℵ, A, B, C, P yana "Bwana" (*kurios*). $UBS^4$ inatoa alama A (hakika) kwa "Bwana".

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14: 5-9**
**5Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku; mwingine aona siku zote kuwa sawasawa. Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe. 6Yeye aadhimishaye siku, huiadhimisha kwa Bwana; naye alaye, hula kwa Bwana kwa maana amshukuru Mungu; tena asiyekula, hali kwa Bwana, naye pia amshukuru Mungu.**
**7Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake. 8Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, au kama tukifa, twafa kwa Bwana. Basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana. 9Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sabau hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia.**

**14:5 "Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku"** watu wengine bado wanawazia kalenda kufuatana na dini (kama vile Gal. 4: 10; Kol. 2: 16- 17). Siku zote ni siku za Mungu, kwa usawa. Hakuna siku maalumu. Hakuna siku za kawaida na za kuabudiwa. Zote ni za kuabudiwa!

◙**"Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hii ndiyo nguzo ya imani katika eneo hili. Ushawishi binafsi wa muumini ndio kipaumbele kwa matendo (kama vile mst 23), lakini sio kwa waumini wengine wote. Mungu haishi ndani ya sanduku langu la thiolojia. Thiolojia yangu sio lazima iwe ni ya Mungu.

**14:6"Kwa ajili ya Bwana"** Kifungu hiki WAKATI kimetumika mara tatu katika mst. 6 na mara 2 katika mst wa 8. Uchaguzi wote wa mtindo wa maisha wa muumini mtiifu unahitaji kufanywa kwa "ajili ya Bwana" (kama vile Efe. 6: 7 na Kol. 3: 23), na sio tu kwa mapenzi ya mtu mwenyewe apendacho kufanya , au matakwa ya dhehebu, utamaduni wa familia, au maoni.

**14:7"Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake"** Hakuna mkristo aliyeko kisiwani. Wakristo wanaishi kwanza na hasa kwa kristo (kama vile mst 8). Matendo ya muumini yanaathiri watu wengine. Ni sehemu kubwa ya familia ya kiroho. Kwa hiyo, lazima wapunguze mipaka ya uhuru wao kwa upendo (kama vile

1 Kor. 10: 24, 27- 33). Lazima waruhusu wengine wakue katika uhuru binafsi. Taratibu za sheria zinaleta haki ya usawa kwa mtu lakini ambayo siyo ya Mungu. Maneno makali ya Yesu na laana yalielekezwa kwa mafarisayo wa haki binafsi.

**14:8"kama ………kama"** Hizi ni SENTESI MBILI ZENYE MASHARTI DARAJA LA TATU zikimaanisha uwezekano wa matendo yajayo. Waumini wana mtumikia Bwana katika njia zozote zile zinazowezekana (kama vile Efe. 6: 7; Kol. 3: 23)!

**14:9"Bwana walio kufa na walio hai"** Huu ni mpangilio wa maneno usio wa kawaida. Mpangilio wake unaoweza kuakisi kifo cha Yesu na ufufuo. Yeye sasa ni mkuu wa Nyanja zote.

Ukweli huu unafanya sababu ya kithiolojia kwa nini wakristo wanaishi sio kwa ajili yao wenyewe, lakini pia kwa ajili ya waumini wengine. Siyo kwa ajili yao wenyewe, wamenunuliwa kwa gharama. Ni watumishi wa Yesu, aliye kufa kwa ajili ya dhambi zao kwamba wasiwe watumwa wa dhambi tena, bali kwa Mungu (kama vile Warumi). Waumini sharti waige maisha ya Yesu ya huduma ya upendo kwa kufa kwa ajili ya matakwa yao wenyewe (kama vile 2 Kor. 5: 14- 15; Gal. 2:20; 1 Yoh. 3:16).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14: 10-12**
**10 Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. 11 Kwa kuwa imeandikwa, Kama niishivyo, anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu, Na kila ulimi utamkiri Mungu. 12 Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.**

**14: 10 "Lakini wewe"** Hili limewekwa mbele kwa ajili kusisitiza.

◙ Maswali mawili ya mst. 10 yanaangazia mist ya 1- 12. Makundi mawili yaliyomaanishwa katika mst 3 yanatofautishwa tena. Kundi moja "lina hukumu" kundi lingine "linaonesha kudharau." Tabia zote mbili sio sahihi kwa "watumwa"! Bwana wao Yesu Kristo ndiye pekee mwenye haki yao "kukosoa" au "kudharau jambo/mtu." Kwa waumini kuwa kama waamuzi: (1) kunachukuwa nafasi ya Mungu na (1) Ni cha kwanza, na hakikukamilika.

◙ **"sote tutasimama mbele ya kiti cha Hukumu ya Mungu"** Usemi huu tena unaelezwa katika 2 Kor. 5: 10. Waumini wataeleza kwa Bwana vipi walivyo watendea wenzao. Yesu atasimama kama Hakimu/mwamzi wa Mungu (kama vile Mt. 25: 31- 46).

NKJV ina "Kiti cha Hukumu ya Kristo" maandiko ya kiyunani yanayounga mkono KJV, ndio wasahilishaji wa mwanzo wa maandiko haya ya kiyunani $\aleph^2$, na $C^2$. *Theos* imo katika MISS, ℵ, B, C, D, F, na G. Waandishi wa habari bila shaka walibadili maandiko ya kiyunani na kufanana na 2 Kor. 5: 10. Inawezekana pia kuwa waandishi hawa wa nakala walibadili mstari huu kupinga wazo la awali la Kristo lililoitwa "Urithi" kuna kasoro kadhaa za kimaandishi yaliyoonekana kuwa yaliweza kufanyika kufanya maandiko kuwa ya imani kamili (kama vile Bart D. Ehrman's *Othodox corruption of scripture"*- kilicho chapishwa na Oxford University Press 1993), uk 9091. UBS[4] inatoa alama 'B' kwa *Theos* (kukaribia uhakika).

**14:11"Kwa vile imeandikwa"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Hii ilikuwa nahau ya waebrania iliyotumiwa kuelezea nukuu zilizovuviwa za Agano la kale. Hii pia ilikwisha gusiwa katika Isa. 45: 23, ambayo pia imenukuliwa kutoka katika Flp. 2: 10- 11.

◙**"Kama ninavyo ishi"** Hiki ni kanuni ya kiapo ambacho ni neno la mchezo katika jina la patano kwa Mungu, YHWH, ambalo ni namna ya KITENZI cha Waebrania, "kuwa" (kama vile Kut. 3: 14). Ni yeye aishie milele, Mungu wa pekee na aishie. Kwa hiyo, anaapa kwa maisha yake mwenyewe.
Tazama mada maalum majina ya Miungu katika 9: 29

**14:12"Hivyo basi, kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu"** Wakristo watahukumiwa yatakayoshughulikiwa. Baadhi ya maandiko ya zamani ya Wayunani, acha "kwa Mungu." Bila shaka ingeweza

kuwa imetokana na tofauti katika mst 10. UBS[4] inaonesha kugusiwa kwake, (yaani MSS ℵ, A, C, D), ambayo imepewa alama C (vigumu katika kuamua).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WARUMI 14: 13-23

A. Somo kuhusu ni vipi wakristo watendeane lilianza katika mst 1-12. Linazingatia ukweli kuwa, wanapaswa kuwapokea kikamilifu wakristo wa aina zote kwa sababu kristo ambaye ndiye Bwana wao wa pekee na mwamuzi anapokea makundi yote kikamilifu. Daima vitu vya kiroho ambayo ni ya muhimu katika kundi moja kwa sababu ya historia yao, aina ya nafsi yake, wazazi wake, mahitaji binafsi, uzoefu wake, n. k. Siyo vya muhimu kwa Mungu.

B. Sehemu hii ya pili ya mjadala wa uhuru wa mkristo na wajibu wake unakuza somo kutoka katika mitizamo tofauti. Katika mstari hii ni upendo wa muumini kwa Mungu katika kristo ambao ulimhamasisha mkristo huyo kuwapenda wakristo wenzake. Kwa kuwa Yesu alizika chini uhai wake kwa waumini, nao kadhalika sharti wafanye vile kwa kuweka chini uhuru wao kwa ajili ya wenzao (yaani waumini wengine) ambao yeye aliwafia. (kama vile 2 Kor.5:13-14; 1 Yoh.3:16). Msisitizo huu katika upendo kama sababu muhimu ya maisha ya mkristo inaonekana pia katika 13:8-10 katika uhusiano wa muumini na wasio waumini.

C. Ukweli kwamba vitu katika ulimwengu huu ni safi ni vigumu sana kwa baadhi ya wakristo wengine kukubaliana nao. Daima hata waumini hulaumu dhambi kwa "vitu," badala ya wao wenyewe (yaa ni-mapepo). Paulo anaweka wazi kuwa vitu vyote ni safi (kama vile 14: 14, 20; 1 Kor. 6: 12; 10: 25-26; 1 Tim. 4: 4; Tito 1: 15). Maneno yake yanafuata mafundisho ya Yesu kuhusu vyakula katika Marko. 7: 18- 25. Vyakula safi na visivyo safi vimetumika kama kielelezo kwa Petro kwa ajili ya ukubalifu wa Mungu kwa Cornelius katika Mdo. 10: 15.

D. Sehemu hii kimsingi inazungumzia "Ndugu mwenye nguvu zaidi." Paulo anakili nusu- ukweli wa usemi kuwa "vitu vyote ni safi" ila anaongezea kuwa vitu vyote havijengi wala kuboresha familia ya Mungu (kama vile 1 Kor. 6: 12; 10: 23). Uhuru wa ndugu mwenye nguvu unaweza kuharibu kabisa wakristo wengine. Waumini ni wachungaji wa waumini wenzao kupitia kwa kristo, kwa ajili ya Kristo.

E. Inafurahisha kuwa Paulo hasemi wala kuonesha kuwa "ndugu aliye mdhaifu" yuko katika mchakato wa kiroho ambao hatimaye utamfikisha kwa "ndugu mwenye nguvu" mjadala wote huu hauzungumzii kukua katika neema bali kipaumbele cha upendo baina ya wakristo wasioelewana. Kuingizwa kwa waumini katika moja wapo ya makundi haya mawili umezingatia zaidi katika aina ya nafsi, mafunzo ya kidini, na uzoefu binafsi kuliko "usahihi" au "kosa." Wajibu wa muumini siyo kubadilisha wengine bali kupenda na kuheshimu makundi mengine. Ni suala la moyo, siyo fikra. Mungu anapenda, anapokea na alimtoa mwanaye kwa wanadamu wote kwa makundi yote.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14: 13-23**
**13Basi tusizidi kuhukumiana, bali afadhali toeni hukumu hii, mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha**
**kumwangusha. 14Najua, tena nimehakikishwa, sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kicho najisi kwa**
**asili yake; lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi. 15Na ndugu yako**
**akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimuharibu**
**mtu Yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. 16Basi, huo wema wenu usitajwe kwa ubaya. 17Maana ufalme**
**wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika roho Mtakatifu. 18Kwa kuwa yeye**
**amtumikiaye Kristo mambo hayo humpendeza Mungu, tena hukubaliwa na wanadamu. 19Basi kama ni**
**hivyo, na tufuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana. 20Kwa ajili ya chakula ushiaribu kazi**
**ya Mungu. Kweli, vyote ni safi; bali ni vibaya kwa mtu alaye na kujikwaza. 21Ni vyema kutokula nyama wala**
**kunywa divai wala kutenda neno lo lote ambalo kwa hilo ndugu yako hukwazwa. 22Ile imani uliyonayo uwe**

**nayo nafsini mwako mbele za Mungu. Heri mtu Yule asiyejihukumu nafsi yake katika neno lile analolikubali. [23]Lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia, kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi.**

**14:13"basi tusizidi kuhukumiana"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI. Kinaonesha kusitisha tendo linaloendelea katika mchakato. Hili sio onyo bali katazo. Hii ni sawa na mst 16. Neno "hukumu" limeisha tumiwa na Paulo mara 5. Katika mst. 1- 12 na sasa mara 4 zaidi katika mist. 13- 23.

## MADA MAALUM: KUHUKUMU (JE! YAWAPASA WAKRISTO KUHUKUMIANA?)

Hukumu ni hakika (kama vile Mt. 12:36; Ebr. 9:27; 10:27; 2 Pet. 2:4,9; 3:7).

A. Yeye anayehukumu ni
  1. Mungu (kama vile Rum. 2:2-3; 14:10,12; 1 Pet. 1:17; 2:23; Ufu. 20:11-15)
  2. Kristo (kama vile Yohana 9:39; Mt. 16:27; 25:31-46; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
  3. Baba kupitia Mwana (kama vile Yohana 5:22-27; Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

Hukumu sio somo zuri, lakini ni maudhui ya sasa katika Biblia. Imejikita katika misingi au miamba za kweli kibiblia.

1. Huu ni ulimwengu wa kimaadili ulioumbwa na Mungu mwadilifu (tunavuna tunachopanda, kama vile Gal. 6:7).
2. Uanadamu umeanguka; tumeasi.
3. Huu si ulimwengu ambao Mungu alikusudia uwepo.
4. Uumbwaji wote unaojielewa (malaika na wanadamu) tutatoa hesabu kwa muumbaji wao kwa zawadi ya uzima. Sisi ni mawakili.
5. Milele itaamuliwa kwa kudumu na matendo yetu na chaguzi tulizozifanya katika haya maisha.

B. Je Wakristo wahukumiane wao kwa wao? Jambo hili lazima lishughulikiwe katika namna mbili.
  1. waamini wanaonywa wasije wakahukumiana wao kwa wao (kama vile Mt. 7:1-5; Luka 6:37,42; Rum. 2:1-11; Yakobo 4:11-12)
  2. waamini waanaonywa kuwatathmini viongozi wao (kama vile Mt. 7:6,15-16; 1 Kor. 14:29; 1 The. 5:21; 1 Tim. 3:1-13; na 1 Yohana 4:1-6)

Baadhi ya vigezo kwa ajili ya tathmini sahihi inaweza kusaidia

1. tathmini lazima iwe kwa kusudi la kukiri (kama vile 1 Yohana 4:1 – "jaribu" ikiwa na mtizamo wa kuthibitisha; angalia Mada Maalum: Kujaribiwa [*peirazō* na *dokimazō*])
2. tathmini lazima ifanyike katika upole na unyenyekevu (kama vile Gal. 6:1)
3. tathmini lazima iweke shabaha kwenye upendeleo wa mambo ya kibinafsi (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33)

Tathmini lazima itambue wale viongozi walio na "sio weza kuvumilia kukosolewa" kutoka ndani ya kanisa au katika jamii (kama vile 1 Timotheo 3).

◙ **"Usitie kitu cha kukwaza ndugu au cha kumwangusha"** Ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI inayoashiria kusitisha tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Ukweli huu huu umesemwa tena katika mstari 21 na 1 Kor. 8: 9.

Neno "kukwaza" lilimaanisha kitu kilichoko njiani kinacho mfanya mtu kujikwaa. Neno "jiwe la kujikwaa" kwa lugha rahisi ni linaelezea tendo la mtego uliowekewa chambo kumnasa.

Kuna suala la ushirikiano katika ukristo. Sisi ni walinzi wa waumini wenzetu, watu wa kuwatia moyo, na rafiki. Imani ni familia!

**14:14**
**NASB "Najua, tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu"**
**NKJV "Ninajua, tena ninashawishika na Bwana Yesu"**
**NRSV "Ninajua na ninashawishika ndani ya Bwana Yesu"**
**TEV "Muungano wangu na Bwana Yesu, unanifanya kuwa na hakika"**
**NJB "Sasa nina tambua kwa hakika,bila shaka na ninasema kwa Bwana Yesu"**

Ni KAULI TENDAJI TIMILIFU ya neno *oida*, iliyotumika katika maana ya WAKATI ULIOPO pamoja na KAULI TENDEWA TIMILIFU YENYE KUARIFU. Kwa lugha rahisi, ina maanisha- "Ninaendelea kujua, na nimekuwa nikijua na naendelea kushawishika."

Haya ni maelezo ya ukweli yanayorudiwa katika mstari ya 5b na 22- 23. Uelewa wa waumini wa vitu vya kiroho unatokana na uhusiano wao na Yesu kupitia Roho mtakatifu. Lazima waishi katika mwanga tulionao.

◙ **"Hakuna kilicho najisi kwa ajili yake"** Ukweli huu huu umefafanuliwa katika Mdo. 10: 9-16. Vitu sio viovu bali watu ndio waovu. Hakuna katika uumbaji ambacho ni kiovu ndani na chenyewe (kama vile mst. 20; Marko 7: 18-23; 1 Kor. 10: 25- 26; 1 Tim. 4: 4 na Tito 1: 15)!

◙ **"lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi"** Hii ilimaanisha ni najisi kwa maana ya kidini. Waumini wanapaswa kutathmini matendo yao kwa dhamira zao (kama vile mst. 5, 22- 23). Hata kama waelewa katika suala fulani au tendo wanapaswa kutembea katika mwanga walio nao mbele ya Mungu. Wanapaswa pia kutowahukumu waumini wengine kwa mwanga walio nao na hasa katika maeneo yasiyo na mipaka (kama vile 14: 1, 3,4,10, 13).

**14:15"Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa kweli, kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi lake la kiwandishi. Upendo, siohaki, wajibu, sio uhuru vinaamua aina ya mtindo wa maisha yetu. Hii ama inahusiana na (1) Sheria za wayahudi kuhusu chakula (kama vile Law. 11) au (2) nyama iliyotolewa kafara kwa miungu (kama vile 1 Kor. 8: 10). Mistari 20 unaelezea ukweli huu kwa wazi kabisa. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake.

◙**"umeacha kwenda katika upendo"** Hii daima inaitwa "Sheria ya uhuru" (kama vile Yak. 1: 25; 3: 12); "Sheria takatifu" (kama vile Yak. 2: 8), a "Sheria ya Kristo" (kama vile Gal. 6: 2). Kuna wajibu na miongozo ya Agano Jipya!

◙
**NASB, NKJV "Usimharibu kwa chakula chako yule ambaye Kristo alimfia kwa ajili yake"**
**NRSV "Usiruhusu unachokula kisababishe madhara kwa mtu ambaye kwaye Kristo alikufa"**
**TEV "Usiruhusu chakukula unachokula kiharibu mtu ambaye kwaye, kwa ajili yake, alikufa"**
**NJB "Wewe kwa hakika, huna uhuru wa kula unachotaka, kama hivyo inamaanisha kuanguka kwa mtu ambaye kwaye Kristo alikufa"**

Ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI ambayo kwa kawaida inaonesha, kusitisha kitendo ambacho tayari kinaendelea katika mchakato. Huu ni usemi mzito sana. Uhuru wa baadhi ya wakristo usisababishe kuharibiwa kwa wakristo wengine. Hii haimaanishi kupoteza wokovu, bali upotevu wa amani thabiti na huduma madhubuti. Tazama F.F Bruce, *Answer to quastion*- uk. 88- 89.

Neno "kuharibu" ni neno la Kiyunani *lupeō* ambalo linamaanisha "kusababisha huzuni, fadhaiko, au maumivu" (sawa katika maandiko ya kale ya miaka ya 70). Paulo anatumia neno hili zaidi katika 2Wakorinto (kama vile 2:2,4,5;6:10;7:8,9,11). Kuharibu ni ngumu sana katika ukalimani. Hii haina maana ya upotevu wa wokovu, bali ni kutiwa hatiani kwa Roho mtakatifu katika kuvuruga hatia binafsi ya mtu. Kuna matendo ya muumini hayatokani na imani, basi, hayo ni dhambi (kama vile mst. 23)

**14: 16**
**NASB "Basi, huo wema wenu usitajwe kwa ubaya"**

**NKJV, NRSV** **"mazuri yenu yasitajwe kwa mabaya"**
**TEV** **"Usiruhusu unacho kiona kwako kuwa kizuri, kitajwe kwa ubaya"**
**NJB** **"Usikubali kuafikiana na mtu kuhusu maisha yako**"

Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI kilichomaanisha kusitisha tendo ambalo tayari linaendelea katika mchakato. Uhuru unaweza kirahisi tu kugeuka kuwa tija. Neno hili "kitu kizuri" katika mstari huu kunamaanisha matendo ya muumini mwenye nguvu. Kama mkristo mzuri anatenda kwa uhuru alionao kwa namna ambayo waumini dhaifu wanapata athari hasi na kuharibiwa kiroho, "kitu kizuri" kina kuwa na fursa kuwa kitu kiovu.

Mstari huu unaonekana kubadili mtazamo kutoka jinsi gani wakristo wanatendeana na kurudi pengine kwa wasio waumini (kama vile mstari wa 18b). KITENZI kinatokana na neno "kuchukiza" (linasemwa) ambalo kwa kawaida linatumika kwa wasioamini.

**14:17"Ufalme wa mbinguni"** Haya ni matumizi pekee ya usemi huu katika Warumi. Ni mada inayojitokeza sana juu ya Yesu. Ni ukweli hapa na sasa, vile vile na katika utimilifu ujao (kama vile Mt. 6: 10). Kwa ujumla Maisha ya mwili wa Yesu yanathamani kubwa kuliko uhuru wa maisha ya mtu. Tazama Mada Maalum ifuatayo:

## MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masihi akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Bethlehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi ("Agano Jipya," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luka 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Marko 9:1; Luka 21:31; 22:16, 18).

Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, "ufalme wa Mungu." Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mt.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani., Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). Katika injili ya Yohana "uzima wa milele" ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)! Waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu "uliotayari" dhidi ya "ule ambao bado" (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

◙**"bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu"** Ni roho ndiye atoae sifa hizi kwa kila muumini na jamii yote inayoamini. Hizi ndizo sifa za familia ya Mungu za nje na za ndani. Neno "haki" linatumiwa hapa na Paulo kwa maana ya pekee. Tazama mada maalum katika 1: 17; kwa maana yake ya kawaida ni haki ya kupewa. Tamko halali

(kisheria) la Mungu kwa msamaha wa muumini na kusimama kwake katika Kristo (kama vile 3: 21- 31: 4). Utu wa dhambi hauchukuliwi tu kama haki, bali utakuwa nao. Ni kipaji na kusudi la HALI YA KUONYESHA na KUSHURUTISHA kwa tendo la imani na maisha ya imani. Tazama Mada Maalum katika 6: 4.

**14:18** Waumini kupunguza uhuru wao kwa ajili ya waumini dhaifu ni huduma kwa kristo mwenyewe. Hakuna njia thabiti ya kuthibitisha upendo wetu kwa Yesu bali kwa njia ya kuwapenda, kuwajali na kuwalinda wale ambao aliwafia.

◙**"tena hukubaliwa na wanadamu"** Hii ina weza kuwa ni njia ya kutetea kuwa, upendo wa Yesu kati ya mtu na mwingine unaweza kufungua milango kwa huduma ya kiroho na ushahidi kwa jamii isiyoamini (kama vile mst. 16; 2 Kor. 8: 21; 1 Petro 2: 12). Jinsi tunavyowatendea wenzetu katika jamii yenye kuamini ni ushahidi tosha, ama chanya au hasi.

**14:19 "Hebu twenende"** Neno hili *diokō,* nahau ya kawaida ya Agano la kale katika maandiko ya kale ya Kiyunani, na pia la kawaida katika maandiko ya Paulo, lilimaanisha "fuatilia kwa nia," au "tenda kwa moyo ili kupata" Paulo anatumia neno hili katika Rum.9: 30- 31; 12: 13, na hapa katika maana ya kufuatilia lakini kwa moyo kwa wale wanao watia hatiani waumini (kama vile 1 Kor. 4: 12, hata yeye mwenyewe, 15: 9; 2 Kor. 4: 9; Gal. 1: 13, 23; Efe. 3: 6).

Hii ama ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO(MSS ℵ, A, B, F, G, L, & P), au KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO (MSS C, D) inayotumika kwa maana ya KUSHURUTISHA (MSSC, D). UBS[4] inaweka UTEGEMEZI katika andiko lake, lakini kwa kuipa alama ya 'D' (kwa shida kabisa). Tazama mambo ambayo wakristo wanapaswa kufanya:

1. Wema 12: 13
2. Mambo yanayoleta amani, na kujengana baina yao. 14: 19
3. Upendo 1 Kor. 14: 1
4. Kufanana na kristo Flp. 3: 12, 14.
5. Kilicho kizuri kati ya mtu na mtu na kwa watu wote
6. Haki, kuishi kwa namna ya Mungu, upendo na amani, na wote wamuitao Bwana kutoka katika mioyo iliyo safi (2 Tim. 2: 22).

◙ **"mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana"** Hili lapaswa kuwa ndilo lengo la muumini kati ya vyote (kama vile Zab. 34: 14; Ebr. 12: 14). Uhuru wa mtu mwenyewe na uelewa wake wa thiolojia sharti utengeneze uimara na kukua kwa mwili wa kristo (kama vile 15: 2; 1 Kor. 6: 12; 14: 26; Efe. 4: 12). Tazama mada maalum kuboresha 15: 2).

**14:20"Usiharibu kazi ya Mungu"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI. Kwa kawaida kinachomaanisha kusitisha tendo linaloendelea katika mchakato. Hiki ni KITENZI KILICHO UNGANA chenye nguvu (*kata +huo*). Kimetumika tu mara tatu katika maandiko ya Paulo (kama vile 2 Kor. 5: 1 kwa mauti na Gal. 2: 18 kwa maana hii hapa, kuharibu). Kuna mchezo kati ya "kujenga" katika mst. 19 na neno hili, ambalo kwa lugha rahisi "kuharibu". Yote yameundwa kama mbadala.

Nini maana ya "kazi ya Mungu" katika mazingira haya. Haitamaanisha ukomavu, bali matendo ya Roho katika maisha ya "waumini dhaifu". Hakuna hata sehemu moja katika mazingira haya au 1 Kor. 8- 10 ambayo Paulo anasema kundi moja sharti lisaidiye lingine kutoka hali ya mfanano au kubadilika!

◙ **"Vitu vyote hakika ni safi"** Tazama nukuu katika mst. 14.

◙

**NASB "bali ni vibaya kwa mtu alaye na kujikwaza"**
**NKJV "Lakini ni vibaya kwa mtu anayekula kwa kujikwaza"**
**NRSV "Lakini ni vibaya kuwafanya wengine wakwazike kwa kile ulacho"**
**TEV "Lakini ni vibaya kula kitu kitakacho sababisha mtu mwingine aanguke dhambini"**
**NJB "Lakini ni vibaya kama ukila kitu kikamsababisha mtu ajikwae"**

Huu ni ukweli halisi wa sura hii (kama vile 1 Kor. 10: 25-26: Tito 1: 15. Hii inamaanisha nyama iliyotolewa kafara (kama vile 1 Kor. 8: 10) nyama sio nzuri au mbaya, lakini kama muumini dhaifu, anayefikiri kuwa si sawa kula, anamwona mkristo mwingine anaila naye pia akala, basi nyama hiyo inakuwa najisi kwa kuwa inaharibu dhamira yake ya mapenzi kwa Mungu. Aina mbali mbali za ukalimani wa kiingereza unahusisha usemi huu na "ndugu" mwenye nguvu, kwamba, kwa kula kwake hiyo nyama muumini dhaifu ataathiriwa. Ukalimani wa kutoka kwenye Biblia mpya ya Marekani (New American Bible) unatoa wazo jingine linalohusisha usemi huu na "ndugu dhaifu. "Lakini ni kosa kwa mtu kumpa chakula ambacho kinakwaza dhamira yake." Katika mazingira haya usemi wa kwanza unaonekana kufaa lakini maana yake nyingine zinaweza kuwa zinalenga na zina maana zote mbili Kama ilivyo katika mistari ya 22-23.

**14:21** Hili ni neno kwa "ndugu mwenye nguvu." Huu ndio msingi pekee katika Biblia kwa dhana ya kithiolojia ya kuacha kabisa baadhi ya vyakula au vinywaji. Wakristo imara yawapasa kupunguza uhuru wao kwa ndugu zao wakristo (kaka/dada) na watafutaji wa kweli (watu waliopotea). Kupunguza kwa mambo haya, kwa mtu binafsi kumo katika desturi zetu, maneno yetu ya kuishi kijografia, na madhehebu yetu.
Hivi viwili ni VITENZI TENDAJI TIMILIFU VYA WAKATI ENDELEVU vyenye VIAMBATA HASI vikimaanisha kuwa "kamwe usianzishe tendo" wengine wametafsiri hizi TIMILIFU kuwa zinahusika tu katika matukio kadhaa (kama vile 1 Kor. 8- 10). Bila shaka, kula na kunywa hariwezi kukatazwa.

**14:22**

**NASB** **"Ile imani uliyo nayo uwe nayo nafsini mwako mbele za Mungu. Heri mtu yule asiyejihukumu nafsi yake katika neno lile analolikubali"**

**NKJV** **"Unayo imani? Kuwa nayo mbele za Mungu. Heri mtu yule asiyejihukumu nafsi yake katika neno lile analolikubali"**

**NRSV** **"Imani uliyo nayo, uwe nayo nafsini mwako mbele ya Mungu. Heri wale wasio na sababu ya kujihukumu wenyewe katika neno lile alilolikubali"**

**TEV** **"Tunza kile unachokiamini kaqtika jambo hili, kwa hiyo, kati yako na Mungu. Heri wale wasio hukumiwa wafanyapo maamuzi ya kweli"**

**NJB** **"Shikilia imani yako, kati yako na Mungu.mfikirie mtu yule awezae kufanya maamuzi yake bila kwenda kinyume na dhamira yake"**

Huku ni kuimarishwa tena kwa muumini kuwa lazima waishi katika dhamira yao inayoongozwa na Roho mtakatifu na ufahamu kutoka katika Biblia, (kama vile mst. 5). Sharti watembee katika mwanga walio nao, lakini wakifanya hivyo bila kukwaza imani ya waumini wenzao.Mstari wa 22 unahusiana na "ndugu mwenye nguvu" wakati mstari wa 23 unahusiana na "ndugu aliye dhaifu" Mstari 22 unaanza na utofauti wa kimaandishi. Linaweza kuwa swali (NKJV) au maelezo (NASB**,** NRSV, TEV na JB).

◙ **"Ushahidi"** Tazama mada maalum katika 2: 18.

◙ **"Lakini aliye na shaka"** Hiki ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hii inamaanisha mkristo aliye makini kupindukia wa mst 3.

◙ **"Ametiwa hatiani"** Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU YENYE KUELEKEZA toka neno *kata + krinō* likimaanisha

1. Kutiwa katika makosa kwa kutofautiana (kama vile Harold K. Moulton, *The analytical Greek Lexicon Revised,* uk. 216).
2. Siyo kutiwa hatiani, bali kupata adhabu baada ya hukumu (kama vile Rum. 5: 16, 18, 8: 1 [kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament,* uk. 328]).

Hapa ana maanisha kuikosea dhamira ya mtu na maumivu yatokanayo husiana na kumtia hatiani, Roho mtakatifu.

◙ **"Kama akila"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU.

◙ **"Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi"** Katika maana pana ya kibiblia, dhambi ni uasi wa dhamira zetu, na sio uasi wa Sheria. Yatupasa tutembee katika mwanga tulio nao, na siku zote tukiwa tayari kwa kupokea nuru zaidi toka katika biblia na Roho. Uelewa wa waumini wenye mapenzi ya Mungu (maana ya "imani" katika mazingira haya) lazima yaamue matendo yao. Inawezekana kwa waumini wakomavu kuwa na maoni tofauti kwa maswala mbali mbali ya kibiblia na yote yawe kwa mapenzi ya ya Mungu.

◙ Baadhi ya maandiko ya kiyunani yana sifa za 16: 25- 27 katika sura ya kufungia ya 14. Mengine yanayo yote katika sehemu zote mbili. Andiko moja la Mafunjo $P^{46}$ kuna sehemu sita mbali mbali za kumsifu Mungu katika maandiko ya asili ya Warumi. Kwa mjadala kamili Tazama Sana, *ATextual Commentary of the Greek New Testament* by Bruce M. Metzber*,* kilicho andikwa na United Bible Societies, uk. 533- 536. Hapa chini kuna ufupisho wa Nadharia zinazohusika.

1. Origen alisema upotofu wa awali katika Rumi, Marcion, yaliondoa sura mbili za mwisho za Warumi. Hii ingeweza kueleza katika sura ya 14.
2. Wasomi wengine wanawazia kuwa Paulo aliandika aina moja ya warumi ili kuipeleka Rumi, sura ya 1-14, na baadaye akaona vema kupeleka waraka kama ulu ule kule Efeso, sura ya 1-16. Orodha ndefu ya salamu binafsi (sura 16) inaakisi Efeso na sio Rumi.
3. Salamu katika sura ya 16 zilikuwa ni kwa ajili ya waumini njiani kwenda Roma kwa sababu Aquila na Priscilla wako Efeso na haijulikani kama wangerudi Roma.
4. Kumsifu Mungu hakukuwa halisi na kuliongezewa na wandishi kwa makusudi ya Liturujia katika ibada ya wazi.

M. R. Vincent, *Word Studies,* juzuu la 2, linafurahisha.

Kinyume na nadharia hizi kuna kweli zinazopingana na nyaraka zenye kujulikana za MSS ya Paulo (karibia mia tatu), yote ya MSS yaliyowekwa pamoja, zikijumuishwa zote za muhimu unazipa sura hizi kupokelewa kwa utaratibu na mfululizo, isipokuwa zile za kumsifu Mungu (uk. 750).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

1. Elezea maana ya ndugu "aliye dhaifu." Je, Paulo ana maana hawajakomaa?
2. Ni vipi uhuru wa mkristo unahusiana na wajubu wa mkristo?
3. Je, kila kitu katika asili yake ni "safi"au kiko kati uzuri au uchafu (mst. 14, 20)?
4. Kwa nini suala la chakula lilikuwa muhimu sana katika Korintho (kama vile 1 Kor. 8, 10), kumbuka Paulo aliandika Warumi akiwa Korintho?
5. Eleza uhusiano uliopo kati ya maarifa, uhuru na upendo katika sura hii.
6. Ni msingi gani tuuzingatie kuhusu udugu katika kanisa?
7. Ni msingi gani tuzingatie katika uchaguzi na matendo ya mtu?
8. Ni vipi matendo yetu yanaaathiri wengine. Hii inatutaka tufanye nini?
9. Ni kwa namna gani tunaweza kupima maadili mema ya mkristo?
10. Je, inawezekana mkristo mkomavu kutokubaliana na wote wakapokelewa na Mungu?

# WARUMI 15

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Waridhishe jamaa zako isiwe wewe tu | ukichukuliana Mizigo ya wengine | mwenye nguvu atachukuliana na aliye dhaifu | Waridhishe na wengine isiwe wewe tu | (14:22-15:6) |
| 15:1-6 | 15:1-6 | 15:1-6 | 15:1-6 | |
| Injili ya watu wa mataifa na na Wayahudi | Mtukuzeni Mungu pamoja | | Injili kwa watu wa Mataifa | |
| 15:7-13 | 15:7-13 | 15:7-13 | 15:7-12 | 15:7-12 |
| | | | 15:13 | 15:13 |
| Agizo la Paulo Katika Wito | Toka Yerusalemu mpaka Iliriko | Muhtasari binafsi | sababu ya Paulo ya kuandika kwa ujasiri | Huduma ya Paulo |
| 15:14-21 | 15:14-21 | 15:14-21 | 15:14-21 | 15:14-16 |
| | | | | 15:17-21 |
| Mpango wa Paulo wa Kuizuru Rumi | Mpango wa Kuzuru Rumi | | Mpango wa Paulo Kuizuru Romi | Mpango wa Paulo |
| 15:22-29 | 15:22-33 | 15:22-29 | 15:22-29 | 15:22-26 |
| | | | | 15:27-29 |
| 15:30-33 | | 15:30-33 | 15:30-33 | 15:30-33 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 1-13

A. Mjadala kuhusu uhuru wa Mkristo na wajibu wake unaendelea katika 15:1-13 kutoka sura ya 14.

B. Hoja nzima katika 14:1-15:13 ingeweza kufupishwa kama ifuatavyo
   1. Pokeaneni ninyi kwa ninyi kwa sababu Mungu anatupokea katika Kristo (kama vile 14:1,3; 15:7)
   2. Mtu asimhukumu mwenzake kwa sababu Kristo ni Bwana wetu sisi sote na Mwamuzi (kama vile 14:3-12)
   3. Upendo ni muhimu sana kuliko uhuru binafsi wa mtu (kama vile 14:13-23)
   4. Mfuateni mfano wa Kristo na weka wazi haki zako kwa ajili ya kuwajenga wenzako na yote yaliyo mema (kama vile 15:1-13).

C. 15:5-6 inaakisi Nyanja tatu za kusudi la hoja hii ya 14:1-15:13
   1. Ishi kwa upendo na mwenzako
   2. Ishi kufuatana na mfano wa Kristo
   3. Kwa mioyo iliyo pamoja, na midomo, sifuni Mungu kwa pamoja

D. Mvutano huu huu kati ya uhuru binafsi na wajibu wa pamoja unashughulikiwa katika 1 Kor. 8-10.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 15:1-6**
**1Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendekeza wenyewe.2Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema, akajengwe. 3Kwa maana Kristo naye hakujipendekeza mwenyewe; bali kama ilivyoandikwa, Malaumu yao waliokulaumu wewe yalinipata mimi. 4Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa sabauri na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini. 5Na Mungu mwenye saburi na faraja awajalie kunia mamoja ninyi kwa ninyi, kwa mfano wa Kristo Yesu; 6ili kwa moyo mmoja na kwa kinywa kimoja mpate kumtukuza Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.**

**15:1**
**NASB** **"Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu"**
**NKAJV** **"Sisi pia tulio na nguvu yatupasa kubebaana na walio dhaifu"**
**NRSV** **"Sisi tulio na nguvu lazima tuchukuliane na wadhaifu wanaoshindwa"**
**TEV** **"Sisi tulio na nguvu katika imani yatupasa tubebeane mizigo na walio wadhaifu"**
**NJB** **"Sisi tulio na nguv tuna wajibu wa kuchukuliana na mashaka ya walio dhaifu"**

Hivi ni vitenzi viwili ENDELEVU VYA WAKATI ULIOPO vilivyotumika kwa namna ya KUSHURUTISHA. Kutaja wenye nguvu/imara na wanyonge/dhaifu inaonyesha kuwa sura ya 15 iliendeleza mjadala ulioanza katika 14:1. Inaonekana kuakisi mvutano ndani ya kanisa la Warumi, na makanisa yote, kwa namna Wakristo wanavyoishi maisha yao katika
1. maeneo mapana ya kibiblia
2. mahitaji ya Agano la Kale
3. mapambano kwa masuala ya kimila yasiyo adilifu

Kitabu kizuri kilicho nisaidia katika eneo hili ni kile kilichoandikwa na Gordon Fee, *Gospel and Spirit*. Kwa wasomaji wa kisasa wa Kingereza, kutambua mitazamo hii miwili, "nguvu/imara" na "dhaifu/nyonge" ni kuathiri makundi.Hili halikuwa kundi la Paulo. Kundi la nguvu/imara lilimaanisha wale waliokwisha wekwa huru kutokana na kanuni, au maisha ya kikristo yaendanayo na matambiko. Mahusiano yao na Mungu hayakutegemea kabisa utendaji wa majukumu/kazi, au kuepuka baadhi ya desturi za kidini. Kikundi kingine kilikuwa ni waumini ambao ni, Mkristo kamili, aliyekubalika kikamilifu, na aliyejito. Hata hivyo walizifanya imani zao kupitia mawazo ya kidini ya uzoefu wao. Waumini wa Kiyahudi walikusudia kung'ang'ania matendo ya mapatano ya zamani ya Wayuda. Wapagani waliobadilika walitaka kuendelea kulinda baadhi ya matendo na mawazo yao ya dini zao za kipagani. Lakini angalia kuwa, Paulo hakukubali fikra hizi za dhambi miongoni mwa waumini. Ni kwa wakati tu walipoasi

dhamira zao ndipo ikawa dhambi (kama vile mstari wa 23). Neno *adunatos*, "bila nguvu" (kama vile Mdo. 14:8) linaunganishwa na neno *astheneō* (kama vile 14:1,21; 1 Kor. 8:7,10,11,12; 9:22), ambalo pia linamaanisha "bila nguvu."

Andiko hili linamaanisha kuwa, Wakristo wasiovumilia wakristo wenzao kwa huruma tu, bali kwa "kuwatendea kwa upendo" na "kufanya kazi na wenzake." Neno "kubeba" lilitumika pia kwa Yesu' "kubeba msalaba" katika Yoh. 19:17 na Luk. 14:27. Paulo alijua mvutano ambao ungetokea kwa watu wa dini. Alifundishwa chini ya Gamalieli, aliyekuwa mwalimu, kiongozi wa dini katika shule huru ya Hillelo.

◙**"wala haitupasi kujipendeza wenyewe"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, ambacho kwa kawaida kinamaanisha kusitisha tendo ambalo tayari limo katika mchakato. Ubinafsi ni ishara tosha ya kutokukomaa. Kwa kufuata mfano wa Kristo (kama vile mstari wa 3; Flp. 2:1-11) ni ishara ya ukomavu. Tena, ni wale wenye nguvu waliokuwa wanazungumziwa (kama vile 14:1,14,16,21,27). Hii haimaanishi walikuwa wote na wajibu katika kuhahakisha uwepo wa undugu. Wanyonge pia wanazungumziwa katika 14:3, 20, 23; 15:5-6,7.

**15:2"kila mmoja wetu ampendeze jirani yake"** Huyu ni "jirani" aliyesemwa kwa maana ya Mkristo mwenzake. Hii haina maana ya maelewano binafsi katika migogoro, bali kwamba, mtu hapaswi kuweka matakwa au maoni yake shagalabagala. Umoja na kukua kwa mwili wa Kristo, siyo uhuru binafsi, unalingana (kama vile 1 Kor.9:19-23; 10:24-33; Efe. 4:1-16).

◙
**NASB** **"kwa ajili ya kuwaadilisha"**
**NKJV** **"kuwaongoza katika uadilifu"**
**NRSV** **"kwa lengo zuri la kuwajenga jirani"**
**TEV** **"ili kuwajenga sawa katika imani"**
**NJB** **"wasaidie wawe Wakristo imara"**

Hii ndiyo dhima kuu ya sura ya 14 (kama vile 14:16,19). Hii pia ni moja ya majaribio makubwa ya vipawa vya roho vinavyopatikana katika 1 Kor.10:23; 12:7; 14:26; Efe. 4:29. Katika mazingira haya inamaanisha muumini imara kupunguza uhuru wake kwa upendo kwa lengo la kuwasaidia wenzake Wakristo kukua katika imani. Joseph A. Fitzmyer na Raymond E. Brown, ed, *The Jerome Biblical Commentary*, vol. 2, kuna maoni ya kuvutia katika mstari huu.

> "Usemi huu daima umechukuliwa kumaanisha "kumjenga" (jirani), ukiwa na maana ya maendeleo binafsi ya jirani Mkristo. "Lakini kwa kufikiria kuwa Paulo alitumia neno mbadala la kujenga katika barua zake kwa maana ya ushirika/muungano, usemi huu bila mashaka una maana kijamii, washirika, na pia (kama vile 1 Kor. 14:12; Efe. 4:12; Rum. 14:19)" (uk. 328)

## MADA MAALUM: KUADILISHA

Neno hili *oikodomeō* na muundo wa maneno yake mengine yanatumiwa mara kwa mara na Paulo. Kidhahiri lilimaanisha "kujenga nyumba" (kama vile Mt. 7:24), lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa:

1. Mwili wa Kristo, kanisa, 1 Kor. 3:9; Efe. 2:21; 4:16
2. Kujenga
   a. ndugu wadhaifu, Rum. 15:1
   b. majirani, Rum. 15:2
   c. ninyi kwa ninyi, Efe. 4:29; 1 Wathesalonike 5:11
   d. watakatifu kwa ajili ya huduma, Efe. 4:11
3. tunajenga au kuonya kwa
   a. upendo, 1 Kor. 8:1; Efe. 4:16
   b. kuweka mipaka juu ya uhuru binafsi, 1 Kor. 10:23-24
   c. kukwepa kudhaniwa, 1 Tim. 1:4

d. kuweka mipaka ya wazungumzaji katika huduma za kuabudu (waimbaji, walimu, manabii, wanenaji kwa lugha, na wakalimani), 1 Kor. 14:3-4,12

4. vitu vyote sharti vionywe
   a. mamlaka ya Paulo, 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10
   b. kauli za kimutahsari katika Rum. 14:19 na 1 Kor. 14:26

**15:3 "kwa maana Kristo naye"** Kristo ndiye kielelezo chetu na mfano. Ukweli huu unasisitizwa katika mstari wa 5; Flp. 2:1-11; 1 Pet. 2:21; 1 Yoh.3:16.

◙**"imeandikwa"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, ambayo ni nahau kwa mafundisho ya Agano la Kale. Hii ni nukuu kutoka katika Zab. 69:9. Kwa kurejea katika mfano wa Kristo (haukumridhisha, kama vile Flp. 2:5-8) na nyongeza ya nukuu ya Agano la Kale, Paulo anatumia vyanzo viwili muhimu vya mamlaka katika Kanisa la mwanzo (kama vile Newman na Nida, *A Translator's Handbook on Paul letter to the Romans*, uk. 271). Mfano wa Kristo wa kutokuwa na choyo katika kubeba dhambi za ulimwengu wote (kama vile 1 Yn.. 3:16).

Paulo anaonekana kuunganisha
1. Yesu kubeba aibu kama Masihi
2. Paulo kubeba aibu ya Injili

Kuna gharama ya kulipa kwa kumtumikia Mungu katika ulimwengu ulioanguka.
1. Yesu aliyekataliwa na kusulubiwa
2. Paulo anaelezea kukataliwa na kusulubishwa kwake katika 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:23-33. Paulo pia hatimaye alikatwa kichwa.

**15:4 "Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi"** Agano la Kale liliandikwa kwa waumini wa Agano Jipya pia (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 9:10; 10:6,11). Inafaa kwa waumini wa agano jipya (kama vile 2 Tim. 2:15; 3:16-17). Kuna mwendelezo, lakini pia utenganisho kati ya Agano la Kale na A gano Jipya.

◙**"ili kwa saburi na faraja ya maandiko"**Tazama jinsi ukweli wa Neno la Mungu na mwitikio wa mitindo ya maisha ya waumini yalivyounganishwa. Imani na matendo yameunganishwa pamoja (kama vile mstari wa 5). Matokeo yake ni kujiamini katika maisha, katika kifo, na katika matumaini ya ahadi ya kurudi kwa Kristo.

◙**"tupate kuwa na tumaini"** Hiki ni KITENZI TENDAJI TEGEMEZI CHA WAKATI ULIOPO, kikiashiria tumaini letu kutegemea matendo yaliyotajwa awali katika mstari wa 4. Katika Agano Jipya, "tumaini" daima linamaanisha Ujio wa Pili, wakati wokovu wetu utakamilishwa (kama vile Rum. 8:30; 1 Yoh. 3:2). Neno hili la Kiyunani, halionyeshi kutokuwepo na uhakika kama ilivyo katika neno la Kingereza. Ujio wa Pili ni tukio la hakika, lisilokuwa na hakika ya muda.

Paulo anatumia neno hili mara kadhaa katika njia tofauti lakini zinazohusiana. Daima inahusishwa na utimilifu wa imani ya mwumini. Hii inaweza kuelezwa kama utukufu, maisha ya milele, wokovu hatimaye, Ujio wa Pili na kadhalika. Utimilifu ni hakika, lakini wakati ni suala lijalo lisilojulikana. Daima linahusishwa na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Sehemu ya orodha ya baadhi ya matumizi ya maneno ya Paulo ni:
1. Ujio wa Pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tito 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1
3. Imani katika Injili, Kol. 1:23
4. Wokovu hatimaye, Kol. 1:5; 1The. 4:13; 5:8
5. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2; 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
6. Uhakikisho wa wokovu, 1 The. 5:8
7. Uzima wa milele, Tito 1:2; 3:7
8. Ukombozi wa viumbe vyote, Rum. 8:20
9. Imani, Rum. 8:23-25, 15:4
10. Jina la Mungu, Rum. 15:13

11. Matamanio ya Paulo kwa waumini, 2 Kor. 1:7

**15:5 "na Mungu mwenye…….awajalie"** Hii ni kati ya KAULI TENDAJI YA HIARI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU chache yenye kuonyesha, kutakia, au ombi. Ombi la Paulo, mistari ya 5-6, lilikuwa na rufaa mbili.

1. Kuwa katika fikra (kama vile 12:16; 2 Kor. 13:11; Flp. 2:2)
2. Kuwa katika sauti moja ya kusifia (kama vile mistari ya 6,7,9)

◙**"Mungu mwenye saburi na faraja"** Haya ndiyo maelezo thabiti ya jina la Mungu (kama vile 15:13; 1 Kor. 1:3). Tabia hii ya Mungu inakuja kupitia mafundisho (kama vile mstari wa 4). Tazama Mada Maalumu: Haja ya Kupambana katika 8:25.

**15:6 "Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo"** Hili ni jina kamili la Uungu katika Agano Jipya (kama vile 2 Kor. 1:3; Efe. 1:3; Kol. 1:3; 1 Pet. 1:3; tazama jina sawia katika 1:7). Huyu siyo Mungu wa umuhimu kithiolojia, bali wa ufufuo. Tazama majina mawili ya Mungu katika maombi ya Paulo ya mistari 5-6.

1. Mungu wa usitahimilivu na kutia moyo
2. Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo

Angalia Mada Maalumu: Ustahimilivu katika 8:25 na Baba katika 1:7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 15:7-13**
**7Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe. 8Kwa maana nasema, ya kwamba Kristo amefanyika mhudumu wa agano la kutahiriwa kwa ajili ya kweli ya Mungu, kusudi azithibitishe ahadi walizopewa baba zetu; 9tena ili Mataifa wamtukuze Mungu kwa ajili ya rehema zake; kama ilivyoandikwa, Kwa hiyo nitakushukuru kati ya mataifa. Nami nitaliimbia jina lako. 10Na tena anena, Furahini, Mataifa, pamoja na watu wake. 11Na tena, Enyi Mataifa yote, msifuni Bwana; Enyi watu wote, mhimidini. 12Na tena Isaya anena, Litakuwako shina la Yese, Naye aondokeaye kuwatawala Mataifa; Ndiye Mataifa watakayemtumaini. 13Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu**

**15:7**

| | |
|---|---|
| **NASB, TEV** | **"kubalianeni ninyi kwa ninyi"** |
| **NKJV** | **"pokeaneni ninyi kwa ninyi"** |
| **NRSV** | **"karibishaneni ninyi kwa ninyi"** |
| **NJB** | **"tendeaneni ninyi kwa ninyi katika njia ya udugu"** |

Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Waumini lazima waendelee kila mmoja kumkubali mwenzake, kwa vile Kristo aliwapokea. Ukweli huu unapatikana katika14:1. Hata hivyo, hii inaleta mfululizo wa hatari kuhusu Mungu kuwakubali na kuwapokea watu wa Mataifa (kama vile mistari ya 9-12). Hii inaweza kuwa imeonyesha mvutano ndani ya Kanisa la Roma.

Ukristo unajionyesha kwa tabia ya muumini kutoa kwa mwenzake (kama vile 1:12; 12:5,10,16; 13:8; 14:13,19; 15:5,7,14; 16:16).

◙**"kama naye Kristo alivyotukaribisha"** Hiki ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU, hapa kuna sababu na msukumo wa matendo ya waumini kwa wenzao (kama vile 14:3). Katika sura ya 14 shabaha ilikuwa kwa

1. Kristo kama Bwana na Mwamuzi, mistari ya 1-12
2. Kristo kama mfano wetu wa kutoa upendo, mstari wa 13-23

Kristo alitukubali, ni lazima tuwakubali wengine!

◙**"kwa ajili ya utukufu wa Mungu"** Tazama dokezo katika 3:23.

**15:8 "Kristo amekuwa mtumishi kwa ajili ya tohara"** Yesu ni utimilifu wa Mungu wa utekelezaji wa unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 10:6; 15:24). Hii inaweza kuelekezwa kwa mvutano katika Kanisa la Roma kati ya WayahudI wanaoamini na watu wa mataifa wanaoamini.

**NASB** **"kwa niaba ya ukweli wa Mungu, ili kuthibitisha ahadi zilizotolewa kwa baba zetu"**
**NKJV** **"kwa ajili ya ukweli wa Mungu, kuthibitisha ahadi zilizofanywa kwa baba zetu"**
**NRSV** **"kwa niaba ya ukweli wa Mungu, ili kwamba, kuthibitisha ahadi zilizotolewa kwa uongozi wa juu wa dini"**
**TEV** **"kwa niaba ya Wayahudi, kuonyesha kuwa Mungu ni mwaminifu, kufanya ahadi zake kwa waliotangulia kuwa za kweli"**
**NJB** **"hivyo kwamba Mungu angeweza kwa imani kutekeleza ahadi zake zilizofanywa kwa uongozi wa juu wa dini"**

Hii bila shaka inahusishwa na ahadi za Mungu za patano katika Agano la Kale kwa Israeli (kama vile 4:16). Hata hivyo, ingeweza kumaanisha ahadi ya Mungu kuwakomboa wanadamu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Isa. 2:2-4; 56:7; 66:18-24). Siri ya Injili ni kuwa, mpango wa Mungu siku zote ulikuwa ni kuunganisha Wayahudi na watu wa Mataifa kupitia katika Kristo (kama vile Efe. 2:11—3:13).

Ujumbe wa Agano Jipya ni utekelezaji wa matumaini wa Agano la Kale, hakuna kitu kipya kabisa. Mkakati mkubwa wa Kristo ulikuwa: (1) kutekelezea Israeli tumaini lake lililoahidiwa na (2) kufungua mlango kwa Mataifa (kama vile Rum. 3:29-30; 9:30 10:11-12,16-20; 11:25,32; 16:25; Efe. 2:11-3:21). Kwa Israeli ilikuwa imeshindwa katika mkakati wake wa kumdhihirisha Mungu na kuwavuta watu wa Mataifa katika imani, Yesu anaiwezesha Israeli mpya ya kiroho (kama vile9:6; Wagal. 6:16) kukamilisha kazi ya ulimwengu (kama vile Mt. 28:19-20; Luk. 24:47; Yoh. 3:16; Mdo. 1:8).

◙**"thibitisha"** Tazama Mada Maalumu katika 4:16.

**15:9-12** Huu ni mfululizo wa nukuu za Agano la Kale kuonyesha kuwa watu wa Mataifa wamekuwa siku zote sehemu ya mpango wa Mungu (tazama Mada Maalumu: *Bob's Evangelical Biases* katika 1:5, kama vile 10:16-20). Huu ni mfululizo wa nukuu za Agano la Kale kutoka

1. Mstari wa 9 – Zab. 18:49 au 2 Sam. 22:50
2. Mstari wa 10 – Kumb. 32:43
3. Mstari wa 11 – Zab. 117:1
4. Mstari wa 12 –Isa. 11:1,10

Tazama, kuna nukuu kutoka kila sehemu ya kanuni ya Kiebrania: Sheria, Manabii, na Maandiko.

**15:9 "kumtukuza Mungu kwa rehema zake"** Huruma ya Mungu ni ufunguo wa kithiolojia kwa yaliyokuwa yafanyike kwa Waroma (kaa vile 9:15,16,18,23) na jumuisho la watu wa Mataifa (kama vile 11:30,31,32; 15:9). Ni huruma ya Mungu ambayo iliokoa Israeli. Ni huruma ya Mungu ambayo inaokoa watu wa Mataifa wanaoamini. Mbinu siyo utendaji wa mwanadamu (kama vile Warumi 9), bali tabia ya Mungu ya neema isiyobadilika (kama vile Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8,4; Yoeli 2:13) na ahadi ya Masihi (kama vile Isa. 11:1,10).
Inapendeza kuwa watu wa Mataifa "wanamtukuza" Mungu kwa

1. kutubu/kusifu
2. kuimba

Muumini anapomwimbia Mungu, ni kwamba anatubu! Nyimbo za Mungu kama amri/imani ni njia madhubuti ya kumwomba Mungu msamaha (kama vile 10:9-13).

**15:13 "Na Mungu wa tumaini"** Huu ulikuwa namna ya kumsifu Mungu wakati wa kufunga maandiko yaliyoanza katika sura ya 14:1. Na hili lilikuwa jina lingine la Ajabu la Uungu-Mungu wa tumaini.

**15:13 "Akujaze furaha yote na amani"** Hii ni KAULI TENDAJI YA HIARI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU kuonyesha ombi la Paulo kwa waumini wa Roma. Angalia uwepo wa "wote" (kama vile 5:1-2; 14:17).

◙
**NASB, NKJV,**
**NRSV "katika kuamini"**
**TEV "kwa njia ya imani katika yeye"**
**NJB "katika imani yako"**

Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hii inaelezea kujiamini katika ustahimilivu kwa njia ya imani isiyokoma katika Kristo, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, aliyeko katika furaha na amani binafsi ya mtu. Imani katika Kristo siyo tu mwitikio wa kwanza, bali ni itikio la mtindo wa maisha.

◙**"hivyo kwamba ujazwe katika tumaini"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ya *perisseuō,* ambacho kimsingi kinamaanisha "juu zaidi ya vyote." Kwa "tumaini" tazama nukuu katika 15:4.

## MADA MAALUM: UTELE *(PERISEUŌ)*

Neno hili linatumiwa mara nyingi na Paulo. Hili linadokeza kile chenye kujaa hadi pomoni (yaani, maana chanya).

1. Kweli ya Mungu yenye kuzidisha utukufu wake, Rum. 3:7
2. Kipawa cha bure katika neema ile ya mwanadamu mmoja, Yesu Kristo, kilichozidi, Rum. 5:15
3. Waamini wazidi sana katika tumaini, Rum. 15:13
4. Waamini hawasifiwi mbele za Mungu kwa kula au kwa kutokula vyakula fulani, 1 Kor. 8:8 (kama vile Mko 7:15,17-23)
5. Waamini wazidi katika kulijenga kanisa, 1 Kor. 14:12
6. Waamini wazidi kutenda kazi ya Bwana, 1 Kor. 15:58
7. Waamini wanazidi kuyashiriki mateso ya Kristo na wanazidi katika kuipokea faraja ya Kristo, 2 Kor. 1:5
8. Huduma ya haki ina utukufu unaozidi, 2 Kor. 3:9
9. Shukrani ya waamini yapaswa kuzidi ili Mungu atukuzwe, 2 Kor. 4:15
10. Wingi wa furaha ya mwamini, 2 Kor. 8:2
11. Waamini wana wingi katika mambo yote (imani, usemi, elimu, na bidii yote, na upendo), pia katika neema kwa ajili ya kanisa la Yeresalemu, 2 Kor. 8:7
12. Wingi wa neema zote kwa waamini, 2 Kor. 9:8
13. Wingi wa shukrani za mwamini kwa Mungu, 2 Kor. 9:12
14. Utajiri wa neema ya Mungu unazidishwa kwa mwamini, Efe. 1:8
15. Pendo la waamini lizidi kuwa jingi sana, Efe. 1:9
16. Fahari ya waamini kuwa na Paulo katika Kristo, Flp. 1:26
17. Kuwa na wingi, Flp. 4:12,18
18. Waamini wakizidi katika shukrani, Kol. 2:7
19. Waamini wanaongezewa na kuzidishiwa katika upendo wao kwa wao, 1 The. 3:12
20. Kuzidi kuenenda katika kumpendeza Mungu, 1 The. 4:1
21. Kuzidi katika pendo na waaini wengine, 1 The. 4:10

Uelewa wa Paulo kuhusu neema ya Mungu katika Kristo ulikuwa "juu ya na zidi wastani," hivyo sana, unahitajika kwa waamini kuenenda katika juu ya na "zidisha wastani" neema na pendo katika maisha ya kila siku!

◙**"kwa nguvu ya Roho Mtakatifu"** Roho Mtakatifu ni Mtu wa utatu aliye imara katika Enzi hii. Hakuna chenye thamani ya kudumu au athari inayoweza kutokea bila yeye (kama vile 15:19; 1 Kor. 2:4; 1 The. 1:5). Tazama Mada Maalumu katika 8:9 na 8:11.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Upi ndiyo ukweli halisi wa Warumi 14:1-15:13?
2. Kwa nini Paulo ananukuu habari za Agano la Kale katika mistari ya 9-12? Ni ukweli upi halisi (mkuu) wanaoufundisha?

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 14-33

A. Kwa namna yeyote ile, hitimisho la barua hii ni sawa na ufunguaji wake, 1:8-15
   1. Inasifiwa imani
   2. Inalinda Mtume Paulo wa Injili kwa watu wa Mataifa (kama vile 1:13,14)
   3. Inatetea nia ya Paulo ya kuwatembelea (kama vile 1:10,13)
   4. Inaelezea nia ya Paulo kuwa, wangemsaidia katika safari yake ya kwenda katika mikoa mingine ambayo ilikuwa bado haijapata kufikiwa na Injili (Hispania, kama vile 1:13)

B. Tena, pana kidokezo cha mkutano katika Kanisa la Roma kati ya Wayahudi wanaoamini na watu wa Mataifa wanaoamini, ambao ulikuwa umeisha dokezwa/kuelezwa katika barua yote, na hasa sura za 9-11, 14:1-15:13.

C. Pia kuna kidokezo kuhusu mvutano katika Kanisa la mwanzo kuhusu msimamo wa Paulo juu ya Utume. Inaonekana anajitetea katika mistari 15-19; 1:2,5.

D. Andiko hili la kifasihi lina maana mbili.
   1. Huduma ya Paulo ya kiroho, iliyokuwa ya Kiinjili, kiutume, na iliyoelekezwa zaidi kwa watu wa Mataifa (kama vile mistari 14-21)
   2. Mipango ya Paulo ya safari kukamilisha kusudi hili, inaweza kumpitisha katika Roma (kama vile mistari 22-33).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 15:14-21**
**[14]Ndugu zangu, nimehakikishwa mimi mwenyewe kwa habari zenu ya kuwa ninyi nanyi mmejaa wema,**
**mmejazwa elimu yote, tena mwaweza kuonyana. [15]Lakini nawaandikia, kwa ujasiri zaidi katika sehemu za**
**waraka huu, kama kwamba kuwakumbusha, kwa neema ile niliyopewa na Mungu, [16]ili niwe mhudumu wa**
**Kristo Yesu kati ya watu wa Mataifa, niifanye Injili ya Mungu kazi ya ukuhani, kusudi Mataifa wawe sadaka**
**yenye kibali, ukiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu. [17]Basi, nina sababu ya kuona fahari katika Kristo Yesu**
**mbele za Mungu. [18]Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, Mataifa wapate kutii.**
**Kwa neno au kwa tendo, [19]kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu; hata ikawa**
**tangu Yerusalemu, na kando kando yake, mpaka Illyricum nimekwisha kuihubiri Injili ya Kristo kwa utimilifu;**
**[20]kadhalika nikijitahidi kuihubiri Injili, nisihubiri hapo ambapo jina la Kristo limekwisha kutajwa, nisije**
**nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine; [21]bali kama ilivyoandikwa, Wale wasiohubiriwa habari zake**
**wataona, na wale wasiojasikia watafahamu.**

**15:14**
**NASB** **"Ndugu zangu, nimehakikishwa mimi mwenyewe"**
**NKJV** **"kuhusu mimi mwenyewe nimehakikishwa ndugu zangu"**
**NRSV** **"Mimi mwenyewe najihakikisha kuhusu ninyi, kaka na dada zangu**
**TEV** **"Rafiki zangu, mwenyewe najihakikisha kuhusu ninyi"**
**NJB** **"Siyo kwa vile nina mashaka kuwahusu ninyi, ndugu zangu,**
**"Niko kinyume na mashaka yeyote juu yenu**"

Neno "mimi" (*autoegō*) linakaziwa sana katika Kiyunani. Paulo kwa hakika analisaidia Kanisa hili ("anashawishika," inaonyesha KAULI TENDEWA TIMILIFU ELEKEZI).

Paulo anatetea vitu vitatu kuhusu Wakristo wa Roma katika mstari wa 14.

1. Wamejaa wema (kuonyesha KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO)
2. Wamejaa maarifa (KAULI TENDEWA TIMILIFU INAYOENDELEA)
3. Wana uwezo wa kuinuana wao kwa wao KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO

Mstari huu unaashiria kuwa, Paulo, hakuleta habari mpya kwao, bali anaelezea na kufafanua habari njema ambayo tayari walikuwa wamekwisha isikia na kuipokea/kuikubali (kama vile mstari wa 15).

◙**"ninyi nanyi mmejaa wema"** Kama ilivyo "mimi mwenyewe" inasisitiza katika fungu la kwanza, "ninyi wenyewe" inasisitiza hapa. Neno "kujaa" (*mestos*) linamaanisha "liojaa" au "tele." Paulo alitumia neno hili mara mbili tu, nyakati zote mbili katika Rum.(1:29; 15:14).

Neno "kujazwa" (*plēroō*) ni KAULI TENDEWA TIMILIFU INAYOENDELEA. Paulo alitumia neno hili daima katika Warumi (kama vile 1:29; 8:4; 13:8; 15:13,14,19). Pia anatumia NOMINO *plērōma* daima katika Warumi (kama vile 11:12,25; 13:10; 15:29), lakini siyo KISIFA katika maandiko yake yo yote yale.

Ilikuwa ni nia ya Paulo kuwa, Injili kamili huwajaa kikamilifu waumini na kufurika katika upendo na huduma.Waumini wana kila kitu wanachotaka katika Kristo. Wanahitaji tu kukubali na kupokea kikamilifu uthibitisho huu.

◙**"mmejaa wema, mmejaa elimu yote"** Kuna njia mbili za kuelewa maneno haya: (1) kwamba yanahusiana kimazingira na maandiko yaliyotangulia ya 14:1-15:13-upendo wa mwamini kati yake na mwenzake katikati ya mfarakano au utofauti kati ya Wakristo katika sehemu mbalimbali za biblia. Hii inathibitishwa kwa matumizi ya kiujumla ya neno "wema/uzuri" katika 14:16; 15:2 na hapa au (2) kwamba ina uhusiano na injili nzima ya imani na matendo, wenye imani kamili/halisi.

◙**"tena mwaweza kuonyana"** Kanisa limekusudiwa na Mungu kuwatia moyo na kuwashauri wengine (kama vile 1 Kor. 12:7; Kol. 3:16; 1 The. 5:14; 2 The. 3:15). Tumeokolewa ili tutumikie, tumtumikie Mungu kwa kutumikiana! Tunaishi kwa afya na kukua kwa mwili.

**15:15"Lakini nawaandikia, kwa ujasiri zaidi"** Paulo aliandika barua yake kwa Warumi kutoka Korintho. Alishauriwa na mmojawapo wa kikundi pinzani katika kanisa hilo kwa kuwa mkali katika barua yake, lakini dhaifu kimwili. KITENZI cha neno "ujasiri" inapatikana katika 2 Kor. 10:2,12; 11:21. Hali ya Paulo ya ukali ilitokana na kubadilika, wito, na ufahamu wa Injili.

◙**"kwa sababu ya neema niliyopewa toka kwa Mungu"** Paulo anamaanisha neema ya Mungu (kama vile 1:5; 12:3; 1 Kor. 3:10; 15:10; Gal. 2:9; na Efe. 3:7-8) iliyomwiita, iliyomwokoa, iliyomzawadia, na iliyomtuma kwa Mataifa (kama vile 11:13; 15:16). Ni njia ya kutetea utume wake na mamlaka (kama vile 1:1,5).

**15:16 "Mhudumu…ahudumiae…niifanyie…kukubalika"** Mistari ya 16 na 17 ina maneno machache kimahubiri na mafungu. "Mtawala" linatumika kwa huduma ya kikuhani katika mstari wa 27. Linatumika kwa huduma ya Kristo katika Ebr. 8:2. Paulo alijiona kama kuhani (kama vile Flp. 2:17) akiwatoa watu wa Mataifa kwa Mungu, ambayo ni kazi ya Israeli (kama vile Kut. 19:5-6; Isa. 66:20). Kanisa limepewa kazi hii ya Kiinjili (kama vile Mt. 28:18-20; Luk. 24:47; Mdo. 1:8). Kanisa linaitwa kwa maneno ya kikuhani katika Agano la Kale katika 1 Pet. 2:5,9 na Ufu. 1:6.

◙**"injili ya Mungu"** Siyo tu injili ya Yesu (kama vile Marko. 1:1; Rum. 1:16; 15:19; 1 Kor. 9:12, 18; 2 Kor. 2:12; 4:4; 9:13; 10:14; Gal. 1:7, n.k.), lakini pia kiusahihi zaidi inaweza kuitwa "injili ya Mungu" (kama vile Marko 1:14; Rum. 15:16; 2 Kor. 11:7; 1 The. 2:2,8,9; 1 Pet. 4:17). Ni upeo wa moyo wa Mungu ulioahidiwa katika Mwa.3:15; 12:3; Kut. 19:5-6 na uliyotabiriwa mara nyingi katika Isaya (yaani, Isa. 2:2-4; 51:4,5).

◙**"kutakaswa na Roho Mtakatifu"** Hii ni KAULI TENDEWA TIMILIFU INAYOENDELEA inayomaanisha, "ametakaswa na ataendelea kutakaswa kwa Roho Mtakatifu." Hii pia inaweza kuakisi mvutano kati ya Wayahudi waumini na Mataifa waumini katika kanisa la Roma. Paulo alisema wazi kuwa, mataifa (watu wa Mataifa) watakuwa na wataendelea kupokelewa kikamilifu na kuwekwa wakfu na Roho Mtakatifu (kama vile 1 Kor. 6:11).

**15:17-19** Angalia tendo la kuunganishwa na Utatu wa Mungu: kwa Mungu (kama vile mstari wa 17); katika Kristo (kama vile mstari wa 17); na katika nguvu ya Roho (kama vile mstari wa 19). Tazama pia watu watatu wa Mungu katika mstari wa 30. Ingawa neno "Utatu" siyo kibiblia, dhana ni (kama vile Mt. 3:16-17; 28:19; Mdo. 2:33-34; Rum. 8:9-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21; 13:14; Efe. 1:3-14; 4:4-6; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2). Tazama Mada Maalumu: Utatu katika 8:11.

**15:18-19** Paulo aliorodhesha njia tofauti ambazo huduma yake ya watu wa Mataifa ilivyofanikiwa (1) kwa neno; (2) kwa matendo; (3) katika ishara; (4) katika maajabu; na (5) yote katika uweza wa Roho.

Kipengele kimoja tu katika tofauti ya maandiko kuhusiana na namba 5, "Roho" (yaani, MS B): baadhi ya maandiko ya Kiyunani yanaongeza "Roho Mtakatifu" (yaani, MSS A, D*), baadhi yana "Roho wa Mungu" (yaani, MSS P[46], א, D[1]). Kama ilivyo katika tofauti hizi nyingi, nyongeza hii, au ufafanuzi usiovuviwa, hautaathiri ukweli wa habari. Kwa kawaida ulikuwa ni kujaribu kusawazisha mpangilio wa maneno wa Agano Jipya na wapiga chapa zamani walionakiri maandiko. UBS[4] inatoa alama "C" kwa "Roho wa Mungu" (vigumu kuamua).

**15:18 "mataifa wapate kulitii"** Lengo la Mungu siku zote limekuwa watu wanaoakisi tabia Yake. Injili ya Yesu inarejesha mfano wa Mungu uliopotea katika anguko la Mwanzo. 3. Undugu au uhusiano wa ndani pamoja na Mungu unathibitishwa na tabia ya ki-Mungu. Lengo la Ukristo ni uhusiano na Mungu na kumfanana Kristo, sasa!

◙**"kwa neno au kwa matendo"** Hii inamaanisha huduma ya Paulo, na siyo utii wa Wakristo wa Roma. Bila shaka inaungamanishwa na nguvu ya Roho katika mstari wa 19.

**15:19 "kwa nguvu na ishara na maajabu"** Maneno haya mawili, yanajitokeza mara nyingi katika Matendo ya Mitume (kama vile 14:8-10; 16:16-18, 25-26; 20:9-12; 28:8-9), yanafafanua nguvu ya Mungu inayotenda kazi kupitia injili (kama vile 1 Kor. 12:12) yanaonekana kufanana. Sawa na kinachomaanisha-miujiza au kubadilika-ni hakika. Hapa tena, hili linaweza kuwa kidokezo kwa mvutano juu ya utume wa Paulo. Kama Mungu alivyothibitisha kazi ya Kumi na Wawili katika Yerusalemu, pia alithibitisha kazi ya Paulo miongoni mwa watu wa Mataifa kwa njia ya ishara zinazoonekana.

◙**"nimekwisha kuihubiri Injili ya Kristo kwa utimilifu"** Hiki ni kitendo cha KAULI TENDAJI TIMILIFU YA WAKATI UNAOENDELEA ya *plēroō* (kama vile mstari wa 14). Hii inaashiria kuwa Paulo aliamini alikwishamaliza kazi yake ya kuhubiri katika Mediterania ya magharibi (kama vile mstari wa 23).

◙**"hadi huko Iliriko"** Jimbo hili la Roma, ambalo pia lilijulikana kama Dalmatia, lililokuwa upande wa mashariki wa bahari ya Adriati, kaskazini magharibi mwa Rasi ya Grecia (Makedonia). Matendo hayakuonyesha kumbukumbu yo yote ya Paulo kufundisha huko, lakini, yanamweka katika eneo hilo (kama vile 20:1-2). "hadi" ingemaanisha "katika mpaka wa" au "katika mkoa wa."

**15:20"kadhalika nikijitahidi kuihubiri Injili, nisihubiri hapo ambapo jina la Kristo limekwisha kutajwa"** Hili lilikuwa lengo kuu la kimisionari Paulo alilokuwa nalo muda wote (kama vile 1 Kor. 3:10; 2 Kor. 10:15-16). Alitaka kuwafikia wapagani ambao walikuwa hawajawahi kusikia na kupokea injili. Kwa kawaida alichukua eneo kubwa, lililolengwa la miji ya himaya ya Roma, hivyo kwamba kanisa lililoanzishwa lingeweza kutoa injili na kufundisha maeneo yaliyowazunguka.

**15:21** Hii ni nukuu kutoka katika tafasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale katika Isa. 52:15 ambayo inanena juu ya usikivu wa watu wa Mataifa kuhusu Mungu. Paulo alichagua unabii huu kama mkakati wake wa kimisionari.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 15:22-29**
**[22]Ndio sababu nalizuiwa mara nyingi nisije kwenu. [22]Lakini sasa, kwa kuwa sina wasaa tena pande hizi, tena tangu miaka mingi nina shauku kuja kwenu; [24]wakati wo wote nitakaosafiri kwenda Spania [nitakuja kwenu]. Kwa maana natarajia kuwaona ninyi katika kusafiri kwangu, na kusafirishwa nanyi, moyo wangu ushibe kwenu kidogo. [25]Ila sasa ninakwenda Yerusalemu, nikiwahudumu watakatifu; [26]maana imewapendeza watu wa Makedonia na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya wtakatifu huko Yerusalemu walio maskini. [27]Naam, imewapendeza, tena wamekuwa wadeni wao. Kwa maana ikiwa Mataifa wameyashiriki mambo yao ya roho,**

**imewabidi kuwahudumu kwa mambo yao ya mwili. [28]Basi mkiisha kuimaliza kazi hiyo, na kuwatilia muhuri tunda hilo, nitapitia kwenu, kwenda Spania. [29]Nami najua ya kuwa nikija kwenu nitakuja kwa utimilifu wa Baraka ya Kristo.**

**15:22 "Kwa sababu hii"** Sababu hii imeelezwa katika mstari wa 20.

◙**"Ndiyo sababu nalizuiwa mara nyingi"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI ISIYO TIMILIFU. Alizuiliwa tena na tena (kama vile 1:13). Wakala hakuelezwa.Inawezekana ikawa Mungu, Shetani, watu waovu, au fursa nyinginezo za injili. Kumbuka, Paulo aliwaandikia Warumi wakati akiwa Korintho. Akiwa Korintho, wapinzani wake Paulo walimshambulia kwa sababu alikuwa hajaweza kutekeleza mpango wake wa kusafiri. Paulo kwa hakika aliathiriwa na mashambulizi kutoka ndani ya kanisa la Korintho. Anaweza kuwa amesema mpango wake wa safari ulikuwa unavurugwa mara kwa mara.

**15:23 "Lakini sasa, kwa kuwa sina wasaa tena pande hizi"** Mstari huu unapaswa kuchukuliwa katika maana ya kijiografia ya maeneo ya Asia Ndogo au eneo la Mediterania ya Mashariki. Paulo alikuwa hajamhubiria mtu ye yote, po pote katika eneo hili, bali kwa baadhi tu.

◙**"tena tangu miaka mingi nina shauku kuja kwenu"** Paulo daima amekuwa nia yake ya kutembelea Roma (kama vile 1:10-15; Mdo. 19:21; 23:11). Kuna kasoro ya kimaandishi katika maandiko ya Kiyunani katika eneo hili ambalo halikuorodheshwa katika nukuu za msingi za UBS[4]. Maandiko ya zamani ya Kiyunani MSS P[46], א, A, D, F, G & L yana (*polus*) "nyingi" ambayo imetumika katika mstari wa 22, lakini MSS B, C & P yana (*ikanos*) "chache au kadhaa." Bila shaka waandishi wa baadaye, waliudhika na uandishi wa Paulo uliotiwa chumvi.

**15:24 "kila niendapo Hispania"** Paulo alitaka kwenda katika jimbo la magharibi la himaya ya Roma (kama vile 2 Kor. 10:16). Aliachiliwa kutoka kifungo cha Roma baada ya kufungwa kwa Matendo na kwenda katika safari ya nne ya kimisionari. Habari za Wachungaji 9, 1 Timotheo, 2 Timotheo, na Tito) ziliandikwa katika safari hii ya nne. Bila shaka kuna rejea kwa hili katika 2 Tim. 4:10 ambapo maandiko ya kale ya Kiyunani, א, C na ukalimani wa biblia wa maandiko ya Kilatini na Koptiki una "*Gaule.*" Clement wa Roma (kama vile Kol. 5:7), walioandika kabla ya mwisho wa karne ya kwanza, katika "Barua yake kwa Wakorintho," 5:7, pia inatetea kuwa Paulo alisafiri katika "mipaka" ya Magharibi.

◙**"katika kusafiri kwangu, na kusafirishwa nanyi"** Usemi huu ukawa ni nahau ya kitaalamu katika kanisa ili kuwasaidia wamisionari waliokuwa wakisafiri bila makazi maalum, kufika katika vituo vyao (kama vile Mdo. 15:3; 1 Kor. 16:6, 11; 2 Kor. 1:16; Tito 3:13; 3 Yn. 6). Roma haikuwa na uwezo wa kuchanga katika mfuko wa maafa kwa kanisa la Yerusalemu, lakini walikuwa wa msaada kifedha kwa safari za kimisionari za Paulo kwenda magharibi.

**15:25 "nikiwahudumia watakatifu"**Neno hili daima linatumika kwa kuunganisha na kukusanya fedha (kama vile mstari wa 31; 1 Kor. 16:15; 2 Kor. 8:4; 9:1). Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika 1:7.

**15:26 "kufanya changizo kwa ajili ya watakatifu huko Yerusalemu walio maskini"** Paulo amekuwa akipokea makusanyo haya (Angalia Mada Maalum: *Koinōnia* katika 12:13) kwa miaka kadhaa kutoka (1) Galatia na Asia Ndogo (kama vile 1 Kor. 16:1-4), na (2) Makedonia na Achaia (kama vile 2 Kor. 8-9). Alipata wazo kutoka katika kanisa la Antiokia (kama vile Mdo. 11:30; 12:25). Ilikusudiwa kuunganisha matawi haya mawili ya kanisa la mwanzo-Wayahudi na watu wa Mataifa. Makanisa ya watu wa Mataifa yanafafanuliwa kama "yaliyofurahisha" kufanya (kama vile mistari ya 26 na 27). Tazama Mada Maalum chini/ifuatayo.

## MADA MAALUM: NJAA

I. Utangulizi
   A. Njaa ni kitu kilichopo daima kinachokumbushia hali mbaya ya wanadamu na uumbaji wake.
   B. Njaa ni kigezo kimoja cha tatizo la maovu na mateso. Kinachosababishwa moja kwa moja na wanadamu, siyo Mungu. Ingawa Mungu alitumia Baraka za kilimo au laana/balaa, kama njia

kuzawadia, au kuadhibu watu wake wa patano (Kumb. 27-28), hii haijawa hivyo kwa waumini kwa ujumla (Mt. 5:45). Njaa ni mfano mmoja zaidi wa mchoyo, mlafi, matini ya mawanadamu ya vitu. Tatizo la njaa siyo tu la chakula, bali ni kichocheo na kipaumbele.

C. Njaa ni fursa kwa mwanadamu aliyekombolewa kuakisi upendo wa Mungu.Mapambano ya waumini kwa mahitaji ya vitu katika kanisa na katika ulimwengu inatuonyesha sisi tuko vipi hasa.

II. Matini ya Kibiblia

A. Agano la Kale
1. Musa
   a. Mojawapo ya aina tatu za fungu la kumi katika Israeli ya zamani ilikuwa watu maskini/fukara (Kumb. 14:28-29)
   b. Sheria ilitamka haki ya maskini kula (Kut. 23:11; Law. 19:10; 23:22; Kumb. 24:19-22)
   c. Sheria iliweka wazi sadaka maalumu zisizo ghali kwa maskini (Law. 14:21)
   d. Israeli ilipaswa kuwa na tabia ya huruma ya kuwasaidia na kuwapokea maskini na wahitaji (Kumb. 15:7-11, kama vile Ayu. 29:16; 30:25; 31:16-23)
2. Fasihi ya hekima
   a. Palikuwa na Baraka maalum zilizowekwa kwa ajili ya wale waliosaidia maskini na wahitaji (Zab. 41:4)
   b. Kuwasaidia maskini ilikuwa kumsaidia Mungu (Mith. 14:31; 17:5; 19:17)
3. Manabii
   a. Mungu alidai kuabudiwa katika njia ya haki ya jamii na msaada kwa wahitaji (Isa. 58:6-7; Mik. 6:8)
   b. Ishara moja ya ujumbe wa Mungu ulikuwa kwamba ilitangazwa kwa maskini na wahitaji (Isa. 61:1-2)
   c. Manabii wa Mungu walipinga unyonyaji wa jamii (Amo. 2:6-8; 5:10-13; Mika)

B. Agano Jipya
1. Injili
   a. Msaada kwa maskini umeaswa (Marko. 10:21; Luk. 3:11)
   b. Hukumu inatokana na upendo wetu wa kijamii kwa watu wengine katika jina la Yesu (Mt. 25:31-46)
   c. Marko. 14:7 imeeleweka vibaya sana inaposema kuwa hii inaakisi Yesu kutojali watu maskini. Mstari huu unakusudia kusisitiza upekee wake na siyo kupuuza maskini.
   d. Isaya 61:1-2 inaakisi kuwa wanaopokea ujumbe wa Mungu watatenganishwa kijamii (Luka. 4:18; 7:22; 14:21)
2. Paulo
   a. Paulo alijifunza kutoka Antioch ya Syria dhana ya upendo maalum uliotolewa kwa maskini wa kanisa la Yerusalemu (Rum. 15:26; 1Kor. 16:1; 2Kor. 8:4,6,19; Gal. 2)
   b. Paulo anasisitiza neema, imani na kazi (Efe. 2:8-10)
3. Yakobo (Fasihi ya hekima za Agano Jipya)
   a. Imani katika Mungu kupitia Kristo pasipo kujali jamii ni ugonjwa (Yak. 2:14-17)
   b. Hata anasema kuwa, imani bila kazi imekufa!
4. Yohana
   a. Kitabu cha 1Yohana kinatetea kuwa uthibitisho wa mkristo uko katika msingi wa kubadilika maisha ya imani na huduma (1Yoh. 3:17-18).

III. Hitimisho

A. Masononeko ya mwanadamu na mahitaji yanahusiana na dhambi ya mwanadamu. Kuna masuala kadhaa ya njaa:
1. Tabia ya upumbavu (Mith. 19:15)
2. Adhabu ya Mungu (Kumb. 27-28)
3. Kuhusiana na huduma ya kiroho (2Kor. 11:27)
4. Mazingira ya kijadi (ulaji, kupata mimba, n.k)

5. Mazingira ya vitu (njaa, mafuriko, mvua ya m awe, n.k)

B. Mungu kweli huwajali watu. Anawapenda wale wenye njaa katika njia ya pekee!

C. Kanisa katika matendo ni jibu la Mungu kwa mwanadamu mhitaji (kimwili na kiroho)

1. Matendo ya moja kwa moja ya mwili
2. Matendo ya ushirika na kanisa
3. Ushirikiano wa kisiasa kwa mabadiliko

D. Ni lazima tutathimini kwa makini tamaduni zetu na vipaumbele binafsi katika nuru ya maandiko (2Kor 8-9)

E. Tunahitaji macho yetu, mioyo, na mikono ifunguke kwa watu walio na uhitaji majumbani kwetu na hata ng'ambo, kanisani na duniani.

F. Msaada ni lazima uendane na sisi tulio katika Kristo katika mwanga wa agizo kuu.

**15:27 "kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudi la uandishi wake. Kama watu wa Mataifa watagawana Baraka za kiroho za Wayahudi (kama vile Rum. 10-11) yawapasa wasaidie katika mahitaji ya kimwili katika kanisa mama la Yerusalemu.

**15:28**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"nikishamaliza hili, na kuwatilia muhuri ya tunda hilo"** |
| **NKJV** | **"nikisha kutenda hili, na kuwatilia muhuri tunda hili"** |
| **NRSV** | **"nikishamaliza hili, na kuwakabidhi kile nilichokusanya"** |
| **TEV** | **"nikishamaliza kazi hii, na kuwapeni pesa niliyokusanya"** |
| **NJB** | **"kwa hiyo, nimefanya hiki na kukabidhi rasmi kilichokusanywa"** |

Hii ni KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPITA INAYOENDELEA na KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU INAYOENDELEA. Hii kwa maneno rahisi, inagusia utaratibu wa kawaida wa kuweka nakili juu ya mzigo kuhakikisha usalama wa kilichomo ndani. Hii inaweza kuwa njia ya Paulo kutetea kuwa, fedha yote aliyopewa itatumwa na kupokelewa. Kuthibitisha hili, alichukua pia wawakilishi kutoka katika makanisa yaliyochangia (kama vile Mdo. 20:4).

Kwa neno "nakili" tazama Mada Maalum katika 4:11

**15:29** Tazama neno *plērōma/ plērōma*, limetumika tena. Tazama nukuu katika mstari wa 14.

◙**"wa Baraka ya Kristo"** Fungu hili linarejea Baraka ambazo mahubiri/mafundisho ya injili yanaleta. Haimaanishi maombi katika mazingira haya. Baadhi ya maandiko ya zamani ya Wayunani yalijaribu kufafanua uelewa huu kwa kuongeza kifungu, "Baraka za injili ya Kristo" (MS A[2], NKJV). Maandiko mafupi yanapatikana katika MSS א[*], A, B, C, D, F,G,P. UBS[4] unatoa alama "A" (hakika).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 15:30-33**
**[30]Ndugu zangu, nawasihi kwa Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa upendo wa Roho, nitajitahidi pamoja nanyi katika maombi yenu kwa ajili yangu mbele za Mungu; [31]kwamba niokolewe na wale wasioamini katika Uyahudi, na tene huduma yangu niliyonayo huko Yerusalemu ikubalike kwa Watakatifu; [32]nipate kufika kwenu kwa furaha, kama apendavyo Mungu, nikapate kupumzika pamoja nanyi. [33]Mungu wa amani na awe pamoja nanyi nyote, Amina.**

**15:30 "jitahidini.....pamoja nami"** Haya ni maneno mazito ya Kiyunani. La kwanza pia linatumika katika 12:1. La pili linatumika kwa mapambano ya Yesu katika Gethsemane. Paulo alitambua hitaji kubwa la ombi kwa ajili yake mwenyewe na kikundi chake cha huduma ya injili (kama vile 2 Kor. 1:11; Efe 6:18-20; Kol. 4:3; 1 The. 5:25; 2 The. 3:1). Uzoefu wake katika Yerusalemu ulionyesha kuwepo ugumu (kama vile mstari wa 31). Aliwasili katika Roma lakini siyo kwa namna aliyoona. Tazama Mada Maalumu: Maombezi/kuombea watu katika 9:3.

**15:30-33** Maombi ya Paulo yanaelezea mambo matatu.

1. Kwamba angeondolewa kutoka kwa maadui wake katika Yuda (kama vile Mdo. 20:22-23)
2. Kuwa vipaji kutoka katika kanisa la watu wa Mataifa lingepokelewa sawa na kanisa katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 15:1na kuendelea; 21:17 na kuendelea)
3. Kwamba angeweza kutembelea Roma, akiwa njiani akielekea Hispania

**15:30 "kujitahidi pamoja naye"** Neno hili limetumika hapa tu katika Agano Jipya. Ni muungano wa *sun* (pamoja na) na *agōnizomai* (kupambana, kupigana, kujitahidi, kwa makini, kama vile 1 Kor. 9:25; Kol. 1:29; 4:12; 1 Tim. 4:10; 6:12). Neno la nguvu lisiloonyesha mwisho linahitaji kanisa la Roma kupambana kwa hasira na Paulo katika maombi kuhusu kupokelewa kwa sadaka za watu wa Mataifa na kanisa mama la Yerusalemu.

**15:31 "na wale wasioamini"** Hii inamaanisha upinzani wa Wayahudi au watu wa uzao wa Yuda, lakini siyo kanisa kwa ujumla 9, kama vile 11:30,31).

**15:32** Maombi ya Paulo yanaishia na maombi makubwa mawili zaidi: (1) angeweza kuwatembelea kwa furaha na (2) angeweza kuwa na muda wa kupumzika nao (KAULI TEGEMEZI YA KATI [yenye ushahidi] ya *sunanapauomai*, hapa tu katika Agano Jipya, bali limetumika katika Isa. 11:6. Paulo alinukuu Isa. 11:1, 10 katika mstari wa 12). Paulo anahitaji muda tulivu wa pumziko na kurejesha afya yake miongoni mwa waumini wakomavu (kama vile 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:23-33)! Hakuipata hata hivyo. Kukamatwa, kushtakiwa na kukaa miaka mingi jela, ni mambo yanayokuwa yakimsubiria huko Palestina.

Mstari huu una tofauti nyingi za kimaandishi.

**15:33 "Mungu wa amani"** Hili ni jina la ajabu kwa Mungu (kama vile 16:20; 2 Kor. 13:11; Flp. 4:9; 1 The. 5:23; 2 The. 3:16; Ebr. 13:20).

◙**"Amina"** Tazama Mada Maalum katika 1:25.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni vipi Agano la Kale linawafaidisha waumini wa Agano Jipya? (mstari wa 4-5; 1 Kor. 10:6,11)
2. Kwa nini Paulo ananukuu Agano la Kale katika mistari ya 9-12? Kweli ipi kubwa wanayoifundisha?
3. Ni wapi katika sehemu hii ya Warumi ambapo mvutano kuhusu utume wa Paulo unajitokeza?
4. Ni wapi katika sehemu hii ya Warumi mvutano kati ya Wayahudi na watu wa Mataifa unajitokeza?
5. Nini ilikuwa sababu ya Paulo ya kuyapa makanisa ya watu wa Mataifa sadaka kwa kanisa la Yerusalemu? (mstari wa 15-28)
6. Ni nini ilikuwa lengo la Paulo la Umisionari? Kwa nini alitaka kwenda Hispania?
7. Kwa namna gani na sababu gani Paulo anaelezea kazi yake sawa na ile ya kuhani (mstari wa 16) kuhusiana na Israeli kama Ufalme wa Makuhani (Kut. 19:5-6) au kwa kanisa (1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6)?
8. Je, Mungu alijibu maombi ya Paulo katika mistari ya 30-33?

# WARUMI 16

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Salamu binafsi | Dada Fibi Anapendekezwa | Salamu | Salamu binafsi | Salamu na heri |
| 16:1-2 | 16:1-2 | 16:1-2 | 16:1-2 | 16:1-2 |
| | Salamu kwa watakatifu wa Rumi | | | |
| 16:3-16 | 16:3-16 | 16:3-16 | 16:3-5a | 16:3-5a |
| | | | 16:5b-7 | 16:5b-16 |
| | | | 16:8-11 | |
| | | | 16:12-15 | |
| | | | 16:16 | |
| | Epuka watu Wanaowagawa | | Maelekezo ya mwisho | Onyo na taarifa ya mwanzo |
| 16:17-20 | 16:17-20 | 16:17-20 | 16:17-20a | 16:17-20 |
| | | | 16:20b-21 | |
| | Salamu toka kwa marafiki wa Paulo | | | Salamu za mwisho na Taarifa ya pili |
| 16:21-23 | 16:21-24 | 16:21 | | 16:21-23 |
| | | 16:22 | 16:22 | |
| | | 16:23 | 16:23 | |
| Wimbo wa Kumsifu Mungu | Dua | | Majumuisho ya Maombi ya sifa | Wimbo wa Kumsifu Mungu |
| 16:25-27 | 16:25-27 | 16:25-27 | 16:25-26 | 16:25-27 |
| | | | 16:27 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa viii)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 1-27

A. Angalia kuwa wanawake wote katika sehemu hii ya kufungia walikuwa watumishi wenza na Paulo katika injili (kama vile Flp. 4:3): Fibi katika mstari wa 1; Priska katika mstari wa 3; Maria katika mstari wa 6; Yunia (au Junias-kama alikuwa mwanamume) katika mstari wa 7; Trifaina na Trifosa katika mstari wa 12; Persis katika mstari wa 12; "mama yake" katika mstari wa 13; Yulia katika mstari wa 15; na "dada yake" katika mstari wa 15. Kuwa mwangalifu na hali ya kubadilika katika eneo la wanawake katika huduma. Waumini wote wana vipawa (kama vile 1 Kor. 12:7, 11), watoa huduma wakati wote (kama vile Efe. 4:12).

   Katika orodha hii tuna shemasi mwanamke Fibi na mtarajiwa mwanamke mtume, Yunia (kama vile Yoeli. 2:28; Mdo. 2:16-21). Ni vigumu kujua jinsi ya kukabili suala hili kibiblia kwa sababu ya taarifa zinazoonekana kupingana za Paulo kama vile 1 Kor. 11:4-5, ukilinganisha na 14:34.

B. Angalia uwezekano wa historia ya makabila kwa majina haya
   1. Wayahudi wanaoamini: Akila, Prisca, Androniko, Yunia, Maria [baadhi ya MSS yana Mariam];
   2. Majina ya koo bora za Roma: Prisca, Ampliato, Apele, Narkiso, Yulia, Flegoni;
   3. Majina ya koo bora za Kiyahudi: Aristobulo, Herodioni.

C. Mistari ya 1-16 ni salamu binafsi za Paulo wakati mistari ya 17-20 ni maonyo yake ya kufungia dhidi ya walimu waongo. Katika mistari ya 21-23 kikosi cha ujumbe kinatuma salamu kutoka Korintho.

D. Mjadala katika sura ya 16 katika *Tyndale New Testament commentary* iliyoandikwa na F. F. Bruce ni ya msaada mkubwa. Kama utapendelea kusoma majina haya kwa undani, yanayopatikana katika sura hii, soma kurasa za 266-284.

E. Kuna mashaka pahali ambapo barua inafungia. Kufunga kunaonekana mara kadhaa katika sura za 14, 15 (MS $P^{46}$) na 16, katika maandiko ya zamani ya Kiyunani. Hata hivyo ufungaji wa kitamaduni wa 16:25-27 unaonekena katika MSS $P^{61}$, א, B,C na D vile vile na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Clement wa Roma (95 B.K).

   Mstari wa 24 hauonekani katika maandiko ya kale ya Wayunani, $P^{46}$,$P^{61}$, א, A, B, C, wala tafasiri ya biblia ya Kilatini au maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen wa Iskandria. Kwa mjadala kamili wa kutofautiana, tazama Bruce M. Metzger*, A Textual Commentary on the Greek New Testament*, uk.533-536.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 16:1-2**
**[1]Namkabidhi kwenu Fibi, ndugu yetu, aliye mhudumu wa kanisa lililoko Kenkrea; [2]kwamba mmpokee katika Bwana, kama iwapasavyo watakatifu, mkamsaidie katika neno lo lote atakalohitaji kwenu; kwa sababu yeye naye amekuwa msaidizi wa watu wengi, akinisaidia mimi pia.**

**16:1"Ninamkabidhi kwenu"** Mistari ya 1-2 inatumika kama barua ya kumpendekeza shemasi Fibi. Bila shaka alichukua barua ya Paulo hadi Roma. Kuna mifano kadhaa ya barua kama hizi za utambulisho au za mapendekezo katika Agano Jipya (kama vile Mdo. 18:27; 1 Kor. 16:3; 2 Kor. 3:1; 8:18-24; na Flp. 2:19-30).

◙**"Fibi"** Jina lake lilimaanisha "kung'aa" au "kumeremeta."

◙
**NASB, NKJV "aliye mhudumu wa kanisa"**
**NRSV "shemasi wa kanisa"**
**TEV "ahudumiaye kanisa"**
**NJB "shemasi mwanamke wa kanisa"**

Hili neno *diakonos* ni neno lenye HALI YA KUSHUTUMU YENYE UMOJA KATIKA TABIA YA KIKE. Ni neno la Kiyunani kwa maana ya mtumishi. Linatumika (1) kwa Kristo katika 15:8; Marko 10:45; (2) kwa Paulo katika Efe. 3:7; Kol. 1:23,25; na (3) kwa mashemasi katika Flp. 1:1; 1Tim. 3:11.

Kuna ushahidi katika Agano Jipya na maandiko ya kwanza ya kanisa baada ya kuandikwa Biblia, kwa ajili ya ofisi ya mashemasi wa kike. Mfano mwingine wa mwanamke katika huduma ya kanisa ya eneo hilo katika Agano Jipya ni "orodha ya wajane" wa watumishi/wahudumu (kama vile 1 Tim. 3:11; 5:3-16). RSV iliyokuzwa na tafsiri za Wafilipi zina "mashemasi" katika 16:1. NASB na NIV zinazo mwanzoni kabisa. NEB ina "nani anashikilia ofisi." Waumini wote wameitwa, wana vipawa, wahudumu wa muda wote (kama vile Efe. 4:12). Wenginehupewa majukumu ya uongozi. Asili zetu sharti zifungue njia kwa mafundisho ya Mungu! Mashemasi hawa wa kiume na kike wa kwanza, walikuwa watumishi sio maofisa. M.R. Vincent, *World Studies*, juzuu ya 2. Uk. 752 na 1196, inasema kuwa Katiba za Utume, zikianzia kutoka karne ya pili mwishoni au mwanzoni mwa karne ya tatu, zinaonyesha utenganisho wa shughuli/wajibu wa uongozi wa wanawake na wasaidizi wa kanisani.

1. Mashemasi wanawake
2. Wajane (kama vile 1 Tim. 3:11; 5:9-10)
3. Mabikira (kama vile Mdo. 21:9 na bila shaka 1 Kor. 7:34)

Shughuli na wajibu huu unajumuisha

1. Kutunza wagonjwa
2. Kutunza wale walio na shida ya viungo/walemavu
3. Kuwatembelea walio kifungoni kwa imani
4. Kufundisha waumini wapya
5. Kusaidia katika ubatizo wa wanawake
6. Baadhi wakiwasimamia wanajumuiya wa kike wa kanisa

## MADA MAALUMU: WANAWAKE KATIKA BIBLIA

I. Agano la Kale
   A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
      1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
      2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
      3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
      4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
   B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
      1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
      2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
      3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
      4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
      5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
      6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
      7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
      8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1

Mambo ya Nyakati 25:5-6).

9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)

C. Wanawake katika dhima ya uongozi
   1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
   2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya Vibanda(Kutoka 35:25-26)

3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vileWaamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipya
   A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).
   B. Wanawake katika dhima ya uongozi
      1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
      2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
      3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
      4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
      5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
      6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
      7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
      8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
      9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?
   A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?
      1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
      2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti nay a kihistoria yaliyovuviwa.
         a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
         b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
         c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
            1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
            2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
            3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
            4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
            5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
            6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
      3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .
   B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa

akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi
   1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
   2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
   3. *Hard Sayings of the Bible by* Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667*)*

◙**"kanisa"** Tazama Mada Maalum hapa chini

## MADA MAALUM: KANISA (*ekklesia*)

Neno hili la Kiyunana, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya"na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (*Qahal,* BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30),na matumizi ya kidini. kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisrael wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH

Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia, Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israel kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

◙**"Kenkrea"**Hii ilikuwa mojawapo ya bandari mbili za Korintho. Hii ilikuja upande wa mashariki (kama vile Mdo. 18:18)

**16:2 "kwamba umpokee katika Bwana kwa namna inayostahili"** Hii ni KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU CHA KATI cha *prosdechomai*, ambacho kinamanisha kuwa "kumpokea kwa mapenzi kama mgeni" (kama vile Flp. 2:29). Paulo alimwamini mgeni huyo na kulitaka kanisa kumpokea na kumsaidia kwa niaba yake. Ukweli kwamba alihitaji kusema hili, inajionyesha katika mazingira ya tamaduni.

◙**"watakatifu"** Neno hili linamaanisha "mtakatifu" Inaeleza siyo tu nafasi ya Wakristo katika Yesu lakini pia kwa tumaini la maisha yao ya Kiungu, ikiendelea kuonyesha nafasi zao mpya za utakatifu katika Kristo. Neno "mtakatifu" daima lipo katika wingu isipokuwa mara moja tu katika Wafilipi (4:21) na hata hapo kuna maana ya ushirika. Kuwa mkristo ni kuwa sehemu ya jamii inayoamini familia, mwili. Kanisa la sasa la magharibi, limedhoofisha suala hili la ushirika wa imani ya Biblia! Tazama Mada Maalum: Watakatifu katika 1:7.

◙**" mkamsaidie katika neno lo lote atakalohitaji kwenu"**Hapa kuna vitenzi viwili TEGEMEZI, cha kwanza *paristēmi* (KAULI TENDAJI TIMILIFU), kikimaanisha "kuwa tayari kwa ajili ya kusaidia." cha pili, *chrēzō* (KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO), kikimaanisha "kusaidia kila kinachohitajika" (kama vile 2 Kor. 3:1).

Hii ilikuwa na maana kutoa msaada wa vitu kwa wahudumu waliokuwa wakitoa sehemu moja kwenda nyingine bila makazi maalum kwa ajili ya kueneza injili. Hili ndilo lilikuwa kusudi la mapendekezo ya nyaraka zake.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"amekuwa wa msaada kwa watu wengi"** |
| **NRSV** | **"amekuwa msaada kwa wengi"** |
| **TEV** | **"kwa vile yeye mwenyewe amekuwa rafiki kwa watu wengi"** |
| **NJB** | **"amekuwa mwangalizi mkubwa kwa watu wengi"** |

Neno hili *proistatis* limepatikana tu katika Agano Jipya. Lingeweza kuwa linamaanisha msaada wa vitu au wa fedha. Neno hili mwanzo lilimaanisha kiongozi mwenye mali (tajiri). Kwa vile Fibi alikuwa akisafiri kwenda Roma (kama vile mstari wa 1) na aliwasaidia wengi (kama vile mstari wa 2), hii kihistoria ingeweza kuwa kweli.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:3-16**
**[3]Nisalimieni Prika na Akila, watenda kazi pamoja name katika Kristo Yesu; [4]waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote**

**pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao. [5]Nisalimieni Epainero, mpenzi wangu, aliye malimbuko ya Asia kwa Kristo. [6]Nisalimieni Mariamu, aliyejitaabisha sana kwa ajili yenu. [7]Nisalimieni Androniko na Yunia, jamaa zangu, waliofungwa pamoja nami, ambao ni maarufu miongoni mwa mitume; nao walikuwa katika Kristo kabla yangu. [8]Nisalimieni Ampliato, mpenzi wangu katika Bwana. [9]Nisalimieni Urbano, mtenda kazi pamoja nami katika Kristo, na Stakisi, mpenzi wangu. [10]Nisalimieni Apele, mwenye kukubaliwa katika Kristo. Nisalimieni watu wa nyumbani mwa Aristobulo. [11]Nisalimieni Herodioni, jamaa yangu. Nisalimieni watu wa nyumbni mwa Narkiso, walio katika Bwana. [12]Nisalimieni Trifaina na Trifosa, wenye bidii katika Bwana, Nisalimieni Persisi, mpenzi aliyejitahidi sana katika Bwana. [13]Nisalimieni Rufo, mteule katika Bwana, na mamaye, aliye mama yangu pia. [14]Nisalimieni Asinkristo, Flegoni, Herme, Patroba, Herma, na ndugu walio pamoja nao. [15]Nisalimieni Filologo na Yulia, Nerea na dada yake na Olimpa, na watakatifu wote walio pamoja nao. [16]Salimieni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.**

**16:3 "Prika na Akila"** Luka alimwita "Priscilla." Siku zote anaitwa kwa jina la mumewe, ambavyo kwa utamaduni wao haikuwa kawaida (kama vile Mdo. 18:18, 26; 1 Kor. 16:19; 2 Tim. 4:19). Bila shaka alikuwa wa kutokea katika ngazi ya heshima ya Warumi, au ambaye ni wa juu kati ya wawili hao. Wote Paulo na hawa wawili walikuwa watengeneza Mahema au wanafanya kazi za ngozi. Paulo anawaita "wafanyakazi wenzake katika Yesu Kristo." Bila shaka alijua uimara na udhaifu wa kanisa hili kutoka kwa watu hawa wawili.

**16:4 "waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa"** Hii ni nahau kutokana na maneno "shoka la mtoa hukumu" Biblia inanyamaza kuhusu Paulo alichomaanisha kwa maneno haya.

◙**"ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote pia"** Hii ilikuwa shukrani kubwa kwa urafiki na msaada madhubuti kwa watu hawa wawili. Na hata anapanua huduma yao kwa "makanisa yote ya watu wa Mataifa" Ni uthibitisho kiasi gani na utoaji shukrani? Ingeweza kumaanisha kuwatia moyo na kutaarifu huduma kwa Apollo (kama vile Mdo. 18:24-28)

**16:5"kanisa"** Hii inamaanisha watu, siyo jengo. Neno hili linamaanisha "walioitwa" Katika Agano la Kale la Kiyunani, tafasiri ya maandiko ya kale, neno hili lilitumiwa kukalimani neno la Kiebrania la *qahal*, lililomaanisha "kusanyiko au mkutano wa watu."Kanisa la kwanza walijiona wao kama ni warithi wa asilia na watekelezaji wa Agano la Kale kuhusu "kusanyiko la Israeli" na siyo lile kundi lisilokuwa na sifa, lililojitenga. Tazama Mada Maalum katika 16:1.

◙**"aliyemo nyumbani mwao"**Kanisa la kwanza walikutanika ndani ya kaya/nyumba. (kama vile 16:23; matendo 12:12; 1 Kor 16:19; Kol 4:15; Filemoni 2). Majengo ya Kanisa hayakuonekana hadi karne ya tatu baada ya Kristo

◙"**Epaineto"** Jina la huyu mtu lilimaanisha "kusifiwa".

◙"**aliye wa kwanza kama limbuko"** Hili nalo lilisemwa katika nyumba ya Stefano katika 1 Kor. 16:15.

◙"**Kutoka Asia"** Hii inamaanisha jimbo la Roma lililounda moja ya tatu ya sehemu ya mashariki ya Uturuki ya sasa.

**16:6**"**Mariamu, aliyejitaabisha sana kwa ajili yenu**" Hakuna kinachofahamika kuhusu mtu huyu. Inawezekana akawa ni Mmishionari kutoka katika kanisa la Roma. Waumini wengi wa Mungu ambao ni wa ajabu, hawajulikani kwetu, lakini wanajulikana sana kwa Mungu.

**16:7"waliofungwa pamoja nami** " Wasomi wa sasa hawana hakika kwamba kifungo hiki kinamaanisha nini. Paulo aliteseka sana kwa imani yake. (kama vile 2 Kor. 4:8-11; 6:4-10; 11:25-28). Alikuwa kifungoni huko Filipi, Kaisaria, Roma na bila shaka sehemu zingine pia (kama vile Waefeso, 1 Kor. 15:32; 2 Kor. 1:8)

◙"**Yunia**"Jina hili linaweza kuwa ni la kiume au la kike; ambalo linaweza kutambuliwa kwa alama za matamshi ya maneno. Kuna utofauti katika maandiko ya kiyunani, "*Lounian*"linapatikana katika MSS א, A,B,C,D,F,G & P,lakini bila alama ya matamshi ya eneo. Neno linalotamkwa namna ya mwanamke linapatikana katika MSS $B^2$,$D^2$, na 0150. Maandishi ya zamani ya mafunjo $p^{46}$na ukalimani mwingine wa baadhi ya tafasiri ya biblia ya Kilatini na

Koptiki, vile vile na maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Jerome, zina "*loulian*" ambalo ni la KIKE. Wasomi wengine wanaamini kuwa hili ni kosa tu la uandishi (makarani).Namna hii ya JINSIA YA KIKE haionekani katika 16:15. Inawezekana kuna watu wawili waliotajwa katika mstari wa 7 walikuwa

1. Waumini wawili wa Kiyahudi waliofungwa pamoja na Paulo
2. Kaka na dada
3. Mme na mke

Kama ni JINSIA YA KIKE na kama maneno "mitume" lilimaanisha matumizi mapana ya neno hili zaidi ya "Kumi na Wawili," Basi huyu alikuwa mtume mwanamke. Inapendeza kuona kuwa silabi za "Junias" haijapata kupatikana po pote katika fasihi ya Warumi au maandishi yalioandikwa juu ya vitu, lakini jina Yunias lilikuwa la kawaida sana. Lilikuwa ni jia la familia ya Kirumi, kwa habari zaidi juu ya wanawake katika huduma tazama *Women leaders and the church,* na Linda L. Belleville, ukurasa 188 maneno ya kutangulia 42.

◙

**NASB** **"ambao ni maarufu miongoni mwa mitume"**
**NKJV** **"ambao ni wa kutambuliwa miongoni mwa mitume"**
**NRSV** **"ni maarufu miongoni mwa mitume"**
**TEV** **"wajulikanao sana miongoni mwa mitume"**
**NJB** **"kati ya wale mitume maarufu"**

Hii inamaanisha wale kumi na wawili, kama ndivyo hawa walikuwa wamefahamika zaidi kwao au kwa kundi kubwa la wahudumu waliojulikana kama "mitume" (kama vile Mdo. 14:4, 14; 18:5; 1 Kor. 4:9; Gal. 1:19; Efe. 2:25; 1The.2:6). Mazingira yanaashiria matumizi haya mapana katika Efe. 4:11, lakini KIFUNGU KILICHO WAZI kinamaanisha wale kumi na mbili. Tazama Mada Maalum: Kupelekwa (*Apostello*) katika 1:1.

◙**"nao walikuwa katika Kristo kabla yangu"** Hii bila shaka inamaanisha walikuwa wameokolewa na wakawa wakitenda kazi katika huduma ya Kristo kabla ya uzoefu wa Paulo katika njia ya kuelekea Damaski.

**16:8-16** Majina katika sehemu hii hayajulikani kwa wasomi. Ni wapenzi wa Mungu na Paulo, lakini majina yao na huduma haviko katika kumbukumbu katika Agano Jipya au fasihi ya kwanza ya Kikristo. Kinachoonekana ni mchanganyiko wa (1) majina ya watumwa wa kawaida; (2) Waroma bora; na (3) majina ya familia za Kiyahudi. Kuna wanaume na wanawake. Kuna watu huru, tajiri na wasio na wahubiri wasio na makazi maalumu. Kuna wageni toka Uajemi. Vikwazo vyote viko katika kanisa la Yesu Kristo (kama vile 3:22; 10:12; Yoeli. 2:28-32 [Mdo. 2:14-21]; 1 Kor. 12:11; Gal. 3:28; Kol. 3:11)!

**16:8 "Ampliato"** Jina hili, kama Priska na Yunia, lilikuwa jina mashuhuri la familia ya Roma.

◙**"mpendwa wangu katika Bwana"** Neno "mpenzi/mpendwa" linatumiwa na Mungu Baba kwa Yesu mwana katika Mt. 3:17 na 17:5, ambalo linaweza kuwa jina kutoka katika Nyimbo za utumishi za Isaya (kama vile Mt. 12:18, ikinukuu Isa. 42:1). Hivyo Paulo analitumia kuzungumza na waumini (kama vile 1:7; 16:8,9; 1Kor. 4:14,17; 15:58; Efe. 6:21; Flp. 2:12; Kol. 4:7,9,14; 1 Tim. 6:2; Filemoni mstari wa 16).

**16:9 "Urbano"** Jina hili linamaanisha "aishie mjini" au "mzaliwa wa mjini."

◙**"katika Kristo"** Huu ni usemi uliorudiwa pamoja na "katika Bwana," katika sura nzima. Wakristo watumishi hawa, wote walikuwa sehemu ya familia moja, Mkombozi mmoja.

◙**"Stakisi"** Hili ni jina adimu linalomaanisha "sikio" (la mbegu). Wataalamu wa mambo ya kale wamegundua jina hili kutokana na familia ya Kaisari.

**16:10 "mwenye kukubaliwa katika Kristo"** Usemi wa kinahau unamaanisha Yule ambaye amepita katika majaribio na akabakia mwaminifu. Tazama Mada Maalum katika 2:18.

◙**"wale wa nyumbani mwake"** Wasomi wengine wanatabiri kuwa usemi huu unamaanisha watumwa katika shughuli za nyumbani mwa Aristobula na siyo wana familia. Ukweli huu pia upo katika mstari wa 11, "wale wa nyumba ya Narkiso."

◙**"wa Aristobulo"** Baadhi ya wasomi wanatabiri kuwa huyu alikuwa kaka yake na Herode Agrippa 1(ambaye katika Mdo. 12 alisababisha kifo cha mtume Yakobo). Kama ndivyo, inaonyesha jinsi Injili ilivyoanza kupenyeza katika familia tukufu ya Idumean.

**16:11 "wa Herodi"** Huyu inawezekana alikuwa mtumwa katika familia ya Herode.

◙**"wale wa nyumba mwa Narkiso"** Hii inaweza kuwa inamaanisha mtumishi aliyejulikana sana wa mfalme Claudia. Kama ndivyo, inaonyesha jinsi ambavyo Injili ilikwisha anza kupenyeza katika utukufu wa Warumi.

**16:12 "Trifaina"** Jina hili linamaanisha kitu "kitafunio"

◙**"Trifosa"** Jina hili linamaanisha "laini." Bila shaka walikuwa wadada au mapacha.

◙**"walifanya kazi kwa bidii"**Neno hili lina kidokezo cha kazi "kwa kiwango cha kuchoka."

◙**"Persisi"** Hii inamaanisha "mwanamke wa Uajemi.

**16:13 "Rufo"** Neno hili linamaanisha "mwekundu" au "mwenye kichwa chekundu." Hapa kuna Yule anayejulikana sana Rufo katika Roma (kama vile Marko. 15:21). Pengine anaweza kutambuliwa pamoja na mtu huyu, si hakika lakini inawezekana sana.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"mtu mteule katika Bwana"** |
| **NKJV, NRSV** | **"mteule wa Bwana"** |
| **TEV** | **"Yule mtumishi hodari katika huduma ya Bwana"** |
| **NJB** | **"mtumishi wa Bwana aliyechaguliwa"** |

Hii kwa lugha rahisi anaitwa "mteule." Hapa neno halihusiani tu na mwito wa Bwana, bali pia kwa huduma ya mtindo wake wa maisha. Mama yake pia alimtenda Paulo kwa mapenzi makubwa.

**16:14 "Herme"** Hili ni jina la mungu wa bahati. Lilikuwa ni jina la kawaida la mtumwa katika karne ya kwanza ya ulimwengu wa Roma ya Uyunani.

**16:15 "watakatifu wote"** Tazama Mada Maalum: katika 1:7.

**16:16 "busu takatifu"** Hakuna ushahidi uliopo wa awali kuwa nani alimbusu nani, au lini au wapi. Katika Sinagogi ambamo mfumo wake wa salamu uliendelea kanisani, wanaume waliwabusu wanaume wenzao katika mashavu, na wanawake waliwabusu wanawake wenzao (kama vile 1 Kor. 16:20; 2 Kor. 13:12; 1 The. 5:26; 1 Pet. 5:14). Tendo hili la kusalimiana likawa tatizo ndani ya kanisa kwa sababu halikueleweka kwa wasio waamini na kwa hiyo liliachwa katika baadhi ya makanisa, ingawa Justin Martyr analitaja katika karne ya pili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 16:17-20**
**17Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. 18Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu. 19Maana utii wenu umewafikilia watu wote; basi, nafurahi kwa ajili yenu, lakini nataka ninyi kuwa wenye hekima katika mambo mema, na wajinga katika mambo mabaya. 20Naye Mungu wa amani atamseta shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. [Amina.]**

**16:17** Onyo hili linaonekana kuingia katika mazingira haya bila kutarajiwa. Hata hivyo, Paulo atakuwa amelihusisha kama kutofautisha na wahudumu wa Mungu waliokuwa wakitembea kueneza Injili. Kuna orodha katika mistari ya 17-18 kuhusu walichokuwa wanafanya walimu hawa wa uongo.

1. Wakisababisha mgawanyiko
2. Waliweka vikwazo katika njia ya muumini
3. Walifundisha kwa kupinga maagizo yaliyokuwa yametolewa na kanisa
4. Walihudumia kwa misingi ya ulafi wao wa kula
5. Walikuwa wanadanganya mioyo ya watu wasioweza kuhisi, kwa maneno laini ya udanganyifu

Orodha hii haihusiki na waumini imara na wanyonge wa 14:1-15:13.

◙**"jitenge nao"** Hili ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hii ni dhima inayojirudia (kama vile Gal. 1:8-9; 2 The. 3:6,14; 2 Yoh. 10).

**16:18**
**NASB, NRSV**
**TEV "bali matumbo yao wenyewe"**
**NKJV "matumbo yao wenyewe"**
**NJB "ulafi wao wenyewe"**

Kwa lugha rahisi "matumbo" (kama vile Flp. 3:19; Tito 1:12). Walimu wa uongo wakageuza kila kitu kwa mahitaji yao.

◙**"kwa maneno laini ya ulaghai"** Walimu wa uongo wanaonekana kuwa na mvuto, na wana hulka zinazobadilika (kama vile Kol. 2:4). Ni makini mno katika kuwasilisha hoja zao. Kuwa mwangalifu! Baadhi ya mbinu za kibiblia za kutambua walimu wa uongo zinapatikana katika Kumb. 13:1-5; 18:22; Mt. 7; Flp. 3:2-3, 18-19; 1 Yoh. 4:1-3).

◙**"waidanganya mioyo ya watu wanyofu"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO kinachoonyesha uongo unaoendelea. Angalau waumini wapya au wajinga waliathiriwa ("wasio na uzoefu wa maovu").

**16:19 "Maana utii wenu umewafikilia watu wote"** Hii inarejewa katika 1:8. Hii ni mojawapo ya ukuzaji wa habari wa Paulo.

◙**"kuwa wenye hekima….. katika mambo mema**, **na wajinga katika mambo mabaya"** Usemi huu unaakisi mafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 10:16; Luk. 10:3).

**16:20 "Mungu wa amani"** Hili ni jina la ajabu la la Mungu (kama vile 15:33; 2 Kor.13:16; Flp.4:9; 1The.5:23 na Ebr. 13:20).

◙**"karibuni atamseta Shetani chini ya miguu yako"** Haya yaliwahi kusemwa katika Mwa. 3:15. Uhusiano wa muumini na Masihi unampa ushindi pia (kama vile 1 Yoh. 5:18-20). Hii ni ahadi ya heshima na uwajibikaji. Katika mazingira haya, shetani anajionyesha kuwa mkanganyiko na mgawanyiko uliosababishwa na walimu wa uongo, ambao unasababisha kanisa lipoteze msimamo wake juu ya wajibu lililopewa. Nyuma ya walimu wa uongo kuna mapepo! Injili, hata hivyo inafukuza giza na maovu kwa wale wanaoyakumbatia na kuishi nayo. Kwa kitabu kizuri kuhusu somo hili tazama *Three Crucial Questions about Spiritual Warfare*, kilichoandikwa na Clinton E. Arnold.

## MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI

I. Somo kuhusu shetani ni gumu sana
1. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT,* kur. 300-306).
2. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa)

katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Uajemi).

3. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

   Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (lama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake (tazama Mada Maalumu: Lusifa),kusudi lake,lakini amebainisha kushindwa kwake!

II. Shetani katika agano la kale

Katika Agano la kale neno "Shetani" (BDB 966, KB 1317) au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

1. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29
2. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)
    1. Malaika wa Bwana – Hes. 22:22-23
    2. Shetani – 1 Nya. 21:1; Ayubu 1-2; Zak. 3:1
3. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile.Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. Sot 9b na Sanh. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani,)katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu (kama vile. Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6, 8, 24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babiloni na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile Ezek. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

III. Shetani katika agano jipya

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile.Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroaster).

1. *Ahura Mazda,* baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema
2. *Angra Mainyu,*baadaye aliitwa *Ahriman*,roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyoelezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi wawezakuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile. Ufu. 20:10)!

◙**"neema ya Bwana wetu Yesu iwe nasi sote"**Hii ni namna ya kuhitimisha kwa Paulo (kama vile 1 Kor. 16:23; 2 Kor. 13:14; Gal. 6:18; Flp. 4:23; Kol. 4:18; 1 The. 5:28, 2 The. 3:18 na pia katika Ufu. 22:21). Hii ilikuwa bila shaka imeandikwa kwa mkono wake mwenyewe. Ilikuwa ni namna yake ya kuhakiki barua zake (kama vile 2 The. 3:17; 1 Kor. 16:21; Kol. 4:18).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:21**
**21 Timotheo, mtenda kazi pamoja name, awasalimu, na Lukio, na Yasoni, na Sosipatro, jamaa zangu.**

**16:21-23** Mistari hii ni baada ya uandishi. Wafanyakazi wenza na Paulo katika Korintho walituma salamu.

**16:21 "Lucius"** Huyu angeweza kuwa
1. Luka tabibu (kama vile Kol. 4:14), au bila shaka nahau kwa "mtu aliyesoma sana."
2. Lucius wa Kirene (kama vile Mdo. 13:1)
3. Mkristo asiyejulikana

◙**"Yasoni"** Huyu bila shaka ni Jason ambaye Paulo aliishi kwake katika Thesalonike (kama vile Mdo. 17:5-9).

◙**"Sospatra"** Mtu huyu bila shaka ni Sospiter wa Beroya katika Mdo. 20:4.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 16:22**
**22 Mimi Tertio, niliyeandika waraka huu, nawasalimu katika Bwana.**

**16:22 "Mimi, Tertio, ambaye ninaandika barua hii"** Paulo alitumia neno *(amanuensis*) kuandika barua yake (kama vile 1 Kor. 16:21; Gal. 6:11; Kol. 4:18; 2 The. 3:17). Nafikiri Paulo alikuwa haoni vizuri na hakuweza kuandika herufi ndogo, maandiko sahihi yaliyotakiwa kutunza nafasi katika karatasi ya mafunjo au magombo ya ngozi (kama vile Gal. 6:18)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 16:23-24**
**[23]Gayo, mwenyeji wangu na wa Kanisa lote pia awasalimu. Erasto, wakili wa mji, awasalimu, na Kwarto ndugu yetu. [24][Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi nyote. Amina.]**

**16:23 "Gayo"** Huyu angeweza kuwa ni
1. Gayo Tito Yusta wa Mdo. 18:7
2. Gayo wa Derbe (kama vile Mdo. 19:29; 20:4; 1 Kor. 1:14)
3. Gayo wa III Yohana mstari wa 1

◙**"mwenyeji wangu na kanisa lote"** Huu ni ukarimu unaohitajika kanisani. Waumini wenye rasilimali waliwaruhusu wahudumu wa Kikiristo wanaosafiri kupanga na kulala katika nyumba zao za wageni. Wengine kama huyu bwana, pia walifungua miji yao kuwa mahali pa kukutania kwa matukio yaliyohitaji kukutana. Makanisa ya nyumbani yalikuwa kawaida kwa zaidi ya mamia ya miaka.

◙**"Erasto, mhazini wa mji"** Pia anatajwa katika Mdo. 19:22; 2 Tim. 4:20. Alikuwa na wahudumu waliokuwa wakisafiri waliounganishwa na Paulo.

◙**"Kwarto"** Jina hili Kilatini linamaanisha "wa nne." Bila shaka alikuwa kaka yake na Tito, ambaye katika Kilatini inamaanisha "wa tatu" (kama vile mstari wa 22).

**16:24** Mstari huu haumo katika maandiko ya kale ya Kiyunani, P[46,61], אָ, A, B, C na 0150. Unapatikana katika maandiko mengine ya Kiyunani baada ya 16:23 na mengine baada ya 16:27. Bila shaka siyo ya kwanza kwa Paulo. Yameondolewa katika ukalimani wa NASB, NRSV, TEV na NJB. UBS[4] yanatathiminisha uondolewaji wake kama alama "Fulani" (A). Ni jaribio la kuitimisha barua na inahusiana na tatizo la kufunga nyimbo za sifa zikiwa karibu na mwisho wa sura ya 14, 15 na 16 katika maandiko mbalimbali ya zamani ya Kiyunani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 16:25-27**
**[25]Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, [26]ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii Imani. [27]Ndiye Mungu mwenye hekima peke yake. Utukufu una yeye kwa Yesu Kristo, milele na milele. Amina.**

**16:25-27** Hii ni sentensi moja kwa Kiyunani. Ushuhuda huu unaweza kupatikana katika maandiko ya zamani ya Kiyunani, yote katika mwisho wa sura ya 14 na 15. Mazingira haya ni marejeo ya dhana kuu za kitabu, bila shaka kikiwa kimeandikwa na Paulo kwa mikono yake mwenyewe. Wengine wanaamini kuwa nyimbo hizi za sifa zinaweza kuwa,
1. barua iliyoambatanishwa na barua inayozunguka ya Efeso
2. kwa wale waliokuwa njiani kwenda Roma kwa sababu
   a. Paulo hakuwahi kutembelea Roma, lakini bado anawasiliana watu ishirini na sita
   b. Sura ya 16 ndimo kwa mara ya kwanza kumetajwa walimu wa uongo
   c. Sifa hizi zinaonekana katika maandiko ya zamani ya Kiyunani katika sehemu mbalimbali tofauti

Inawezekana pia kuwa Paulo alifanya nakala mbili, sura za 1-14 kwenda Roma, sura za 1-16 kwenda Efeso. Kwa kawaida hoja hizi zinajibiwa na
1. Ukweli kwamba wengi wa hawa Wakristo, hawa wafanyakazi wa mwanzo walisafiri
2. Ukweli kwamba hakuna andiko la Kirumi lisilo na sura ya 16
3. Uwezekano kuwa walimu wa uongo wametajwa katika 14:1-15:13

**16:25 "kwake yeye aliye na uweza"** Hili ni jina lingine la ajabu kwa Mungu lililotumika mara tatu katika Agano Jipya (kama vile Efe. 3:20; Yuda 24).
Tazama jinsi Mungu anavyopata waumini.
1. Uwasilisho wa Injili wa Paulo

2. Mahubiri kuhusu Yesu Kristo
3. Kubainisha mpango wa Mungu wa wokovu wa milele, ambao ulikuwa umewekwa kama siri

Waumini wanawezeshwa kwa ufahamu wa injili. Injili hii sasa imefanywa wazi kwa wote!

◙**"mwujiza"**Mungu ana kusudi la kuunganisha wokovu wa wanadamu ambao ulikuwepo hata kabla ya anguko (kama vile Mwa. 3). Vidokezo vya mpango huu vinabainishwa katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 3:15, 12:3; Kut. 19:5-6; na habari za ulimwengu katika manabii). Hata hivyo suala hili zima halikuwa wazi (kama vile 1 Kor. 2:6-8). Kutokana na ujio wa Yesu na Roho inaanza kuwa wazi zaidi. Paulo alitumia neno "siri" kuelezea mpango kamili wa ukombozi (kama vile 1 Kor. 4:1; Efe. 2:11-3:13; 6:19; Kol. 4:3; 1 Tim. 1:9). Hata hivyo analitumia katika maana kadhaa tofauti tofauti.

1. Kufungwa kwa muda kwa Israeli ili kuruhusu watu wa Mataifa kujumuishwa. Kuingia huko kwa watu wa Mataifa kutafanya kazi kama namna ya Wayahudi kumpokea Yesu kama Kristo wa unabii (kama vile Rum. 11:25-32).
2. Injili ilifanywa kujulikana kwa Mataifa ambamo yote yalijumuishwa katika Kristo na kupitia kwa Kristo (kama vile Rum. 16:25-27; Kol. 2:2).
3. Miili mipya ya waumini katika ujio wa pili (kama vile 1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).
4. Majumuisho ya vitu vyote katika Kristo (kama vile Efe. 1:8-11).
5. Watu wa Mataifa Wayahudi kama ndugu warithi (kama vile Efe. 2:11-3:13).
6. Hatima ya uhusiano kati ya Kristo na kanisa unaelezwa katika mazingira ya ndoa (kama vile Efe. 5:22-33).
7. Watu wa Mataifa wanajumuishwa katika watu wa agano na ndani mwao kuishi Roho wa Kristo ili kuzaa ukomavu wa kufanana na Kristo, yaani kurejesha mfano wa Mungu uliochafuliwa katika anguko la mwanadamu (kama ville Mwa. 6:5, 11-13; 8:21; Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6; Kol. 1:26-28).
8. Mpinga Kristo wa nyakati za mwisho (kama vile 2 The. 2:1-11).
9. Muhtasari wa kanisa la kwanza kuhusu siri unapatikana katika 1 Tim. 1:16.

**16:26 "sasa amejidhihirisha"** Siri hii au mpango huu wa Mungu, sasa umejidhihirisha wazi kwa wanadamu wote. Ni injili ya Yesu Kristo (kama vile Efe. 2:11-3:13).

◙**"na kwa maandiko"** Mungu ameweka wazi siri hii katika mtu na kazi ya Yesu. Hii ilikwisha semwa mapema siku za mwanzo na manabii wa Agano la Kale. Kuanzishwa kwa kanisa la Agano Jipya lililoundwa na Wayahudi waaminio na watu wa Mataifa ulikuwa siku zote ni mpango wa Mungu (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34).

◙**"Mungu wa milele"** Tazama Mada Maalum chini.

## MADA MAALUM: UMILELE (*aiōnios)*

Robert B. Girdlestone, katika kitabu chake *Synonyms of the Old Testament*, ana maoni ya kushangaza juu ya neno "umilele":

> "Kivumishi *aiōnios* kimetumika zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya. Kwa kuzungumzia uzima wa milele, ambao unachukuliwa kwa sehemu kama zawadi tuliyonayo sasa, kwa sehemu kma ahadi kwa ajili ya ubaadaye. Pia inafanya kazi kwa uwepo wa Mungu usio na ukomo katika Rum. 16.26; kwa thamani ya ondoleo la dhambi lisilokuwa na ukomo la Kristo katika Ebr. 9.12; 13.20; na nyakati zilizopita katika Rum. 16.25; 2 Tim. 1.9; Tito 1.2.
>
> Neno hili linatumika kurejerea moto wa milele, Mt. 18.8; 25.41; Yuda 1:7; adhabu ya milele, Mt. 25.46; hukumu ya milele au shutuma, Marko 3.29; Ebr. 6.2; uharibifu wa milele, 2 The. 1:9. Neno katika vifungu hivi inamaanisha hitimisho na kwa dhahiri ikiashiria kwamba wakati hukumu hizi zikitolewa, muda zaidi zwa uangalizi, mabadiliko au nafasi ya kurudisha nafasi ya mtu ya kwanza, vitakuwa vimekwisha ondoka kikamilifu na milele. Tunaelewa kidogo juu ya wakati wa baadaye, kuhusu mahusiano ya maisha ya mwanadamu na maisha mengine. Ikiwa upande mmoja, sio sawa kuongeza neno la Mungu, upande mwingine lazima tusiondoe; na ikiwa tutayumba yumba katika fundisho la

adhabu ya milele kama inavyowekwa katika maandiko, lazima tukubaliane kusubiri tukishikiria injili ya upendo wa Mungu katika Kristo wakati tukitambua kwamba kuna historia isiyojulikana ambayo hatuna uwezo wa kuielewa" (kur. 318-319).

◙**"limefanywa kufahamika kwa Mataifa yote"**Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Liliwekwa la mwisho katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya kusisitiza. Mungu ameweka wazi zawadi ya injili kwa ulimwengu wote, ambalo ndilo limekuwa kusudi lake (kama vile Mwa. 3:15).

◙
**NASB** **"kuelekea katika utii wa imani"**
**NKJV** **"kwa ajili ya utii kwa imani"**
**NRSV** **"kuleta utii wa imani"**
**TEV** **"kuelekea kwa utii wa imani"**
**NJB** **"kuwaleta katika utii wa upendo"**

Kuna njia tofauti za kuelewa usemi huo; unaweza kumaanisha
1. Imani katika Kristo
2. Kuamini katika Kristo
3. Utii kwa injili, mwanzo na kuendelea

Utii (kama vile 1:5) unapaswa kuunganishwa kithiolojia na dhana ya toba na imani (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21).

**16:27 "Mungu pekee wa hekima"** Hii ilikwisha dokezwa kwa maana ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalum katika 3:30, kama vile Kumb. 6:4-5). Ukristo una Mungu mmoja tu, kama ilivyo imani ya Yuda, hata hivyo, uungu kamili wa Yesu, na nafsi kamili, Roho, vinatusukuma katika "utatu," Utatu (tazama Mada Maalum katika 8:11).

◙**"uwe utukufu milele"** Tazama nukuu katika 3:23.

◙**"Amina"** Tazama Mada Maalum katika 1:25.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.
1. Paulo alijuaje watu wote hawa katika kanisa la mwanzo, wakati hajawahi kwenda huko?
2. Kuna ushahidi wowote wa kibiblia kwa wanawake mashemasi? (kama vile 16:1; 1 Tim. 3:11; 5:3-16)
3. Kuna ashiria nini kwa wanawake wengi kuorodheshwa katika sura hii?
4. Elezea njia na ujumbe wa walimu wa uongo (mistari ya 17-18).

# TAFSIRI SAHIHI ZA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 B.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-B.K 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)

2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (kama vile 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (kama vile Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale….wata...”(Mt 5:4-9).

II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).

B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna <u>pekee</u> ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.

C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.

D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo. 8:20 na 1Thes 3:11

E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.

F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.

G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.

B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;

1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI "kuwa" au "kufaa"
2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, "aina gani?" mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza "ya/za"
3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza "kutoka".
4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ya".
5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na"
6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno "kwa" au "enye"
7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali "kwa umbali gani" au "kwa namna gani"
8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.

B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament

1. Viunganishi vya wakati
   (a) *epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- "lini"
   (b) *heōs- "*wakati"
   (c) *hotan, epan (*TEGEMEZI)- "kila, wakati wowote"
   (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- "mpaka"
      a. *priv (*kitenzijina)- "kabla"
      b. *hōs*- "tangu", "lini", "kama".
2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs*- "ya kwamba", "kuwa"
      2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- "kuwa"

3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”

b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)

(1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”

(2) *hiva(*TEGEMEZI)- “ya kwamba”

(3) *ara*- “kwa kiasi hicho”

c. Chanzo au sababu

1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”

2) *dioti, hotiy- “*kwa sababu ya”

3) *epei, epeidē, hōs*- “tangu”

4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”

d. Maamuzi

(1) *ara, poinun, hōste*- “kwa hiyo”

(2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”

(3) *oun- “*kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”

(4) *tinoun*- “kufuatana na”

e. –a kinyume au tofauti

(1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”

(2) *de- “*lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”

(3) *kai- “lakini”*

(4) *mentoi, oun- “ingawa”*

(5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)

(6) *oun- “ingawa”*

f. Ulinganifu

(1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)

(2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*

(3) *hasos(*katika Kiebrania)

(4) *ē- “kuliko”*

g. Enye mlolongo au mtiririko

(1) *de- “*na”, “sasa”

(2) *kai- “*na”

(3) *tei*- “na”

(4) *hina, oun- “*kile”

(5) *oun- “*kasha”(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo

a. *alla- “*kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”

b. *ara- “*hakika”, agharabu”, “kweli”

c. *gar- “*lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”

d. *de- “*hakika”

e. *ean- “*hata”

f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”

g. *mentoi- “*hakika”

h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.

B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno "kama." Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa "tangu"(kama vile Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(kama vile Mt 12:27)

C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa "inayopingana na ukweli". Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
   1. "kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng'ang'ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
   2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
   3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)

D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi "hiki". Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16

E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: "msijiwekee hazina yenu duniani…………"(Mt 6:19); "msisumbukie maisha yenu………." ( Mt 6:25); "wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi……."(Rum 6:13); "wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na "tena msilewe kwa mvinyo…………………"(Ef 5:18)

B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa "udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo" baadhi ya mifano: "msidhani ya kuwa…….."(Mt 5:17); "msisumbuke………"(Mt 6:31); "msiuonee haya……….."(2Tim 1:8)

C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. "kamwe, katu" au "kwa hali yeyote ile". Baadhi ya mifano: "kamwe, hataonja mauti………"(Yoh 8:51); "hakika, kamwe……….."(1Kor 8:13)

XI

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno "wale, Yule,ile" kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya "muonyeshwaji", ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
   1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
   2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
   3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: "Mungu ni Roho" Yoh 4:24, "Mungu ni nuru" 1Yoh 1:5; "Mungu ni upendo" 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO
         (2) KIVUMISHI
         (3) KIRAI HUSISHI
   3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
      a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
      b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
      c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na

1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe…….”(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
   a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
   b. Yohana 14:1 (maada mpya)
   c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
   d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifiwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
   a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
   b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)
   c. Maumbo ya hotuba
      (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      (4) Kejeli (Gal 5:12)
      (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
         (a) “kanisa”
            i. “kanisa” (Efe 3:21)
            ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
            iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
         (b) “huru “
            i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)
            ii. “uhuru” (Gal 5:1)
            iii. “huru” (Gal 5:1)
   d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)
      (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      (4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
   a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
   b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
   1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.

2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)

   Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
   a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
   b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
   a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
      (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
         (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
         (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
   b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
      (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
   c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''

(2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), "Ataona …… ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki."

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili B.K., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya"Maandishi ya Kialekzandria."
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alekzandrianus, kijulikanacho kama "A" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alekzandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama "B" au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya "Maandishi ya Kialekzandria."
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama "C" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama "D" au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama "Maandishi ya Magharibi." Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale "Bezae" ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

(2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
(3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
(4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya

d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
(1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea
1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
(1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
(2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)
1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
*a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).

*b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda (Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.”Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…”

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# UFAFANUZI/FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (kama vile Rum.1:4).Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!
Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.**Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.**Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.**Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo yanahusiana na wanadamu (kama vile Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (kama vile Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inaahidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1) katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi "ulinzi wa kisheria." Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kififikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno "dhanio." Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli pasipo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K. walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama "D." Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa "uundaji wa maandiko"ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.**Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.**Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.**Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (kama vile Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu k.k.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.**Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-----------mapenzi huru, ulinzi-----------ustahimilivu, imani----------kazi; uwamuzi--------ufuasi; uhuru wa Mkristo---------uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.**Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali. Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini

wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa  na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth,* uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na  kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika*)* kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (kama vile 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (kama vile 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons)*; au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "ilikuwa ni vizuri sana" au "umeniua".  Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na "misamiati ya kiuchunguzi" ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno "MS" (umoja) au "MSS" (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane B.K maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano " birika linachemka" ki uhalisia inamaanisha "maji yaliyeko kwenye birika yanachemka".

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 B.K Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa "kiutendaji" pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum. 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum. 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa "dunia ya zamani" kati ya wanasayansi wa Kikristo (kama vile maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu, hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha "mama wa Mungu" alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo**. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa "neon kwa neon" ambapo neon la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye "fasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi "mlinganyo wa nguvu" ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 k.k). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 b.k muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoelezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3) Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 k.k (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu k.k (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne b.k Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "*eleph*" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (kama vile Zab. 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa "taaluma ya mabadiliko ya hali" (k.v. Zab. 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna (Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuwandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa "uhakiki wa asili ya neno".

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 B.K. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema "andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 B.K.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya "ufundishaji". Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne B.K. Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa "B".

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa "kawaida"wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 B.K.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno "picha ya ulimwengu" inarejerea "kwa namna gani" juu ya uumbaji wakati "mtizamo wa kidunia" unahusiana na "nani." Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezewa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania "kuwa" ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani "Adonai" likimaanisha "Bwana". Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

# KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine". Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa

kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

> "Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo."